# HABARI KUBWA

## Mtazamo mpya kuhusu Quran

Mwandishi

Dkt. Muhammad Abdallah Daraaz, Allah amrehemu

Mwaandaaji na kueleza vyanzo vya hadithi zake ni

*Abdulhamid Al-Dukhaakhiniyyu*

Matini Chanzi ilichapwa na: Daaru Twayyibah kwa uchapaji na usambazaji

Kimetafsiriwa na: Omari Juma Mangilile

Tafsiri imepitiwa na: Shaibu Swalehe Saidi

# HABARI KUBWA

## MTAZAMO MPYA KUHUSU QURAN


MWANDISHI

DKT. MUHAMMAD ABDALLAH DARAAZ, ALLAH AMREHEMU


MWAANDAAJI NA KUELEZA VYANZO VYA HADITHI ZAKE NI

*ABDULHAMID AL-DUKHAAKHINIYYU*


MATINI CHANZI ILICHAPWA NA: DAARU TWAYYIBAH KWA UCHAPAJI NA USAMBAZAJI

KIMETAFSIRIWA NA: OMARI JUMA MANGILILE

TAFSIRI IMEPITIWA NA: SHAIBU SWALEHE SAIDI

*Haki zote zimehifadhiwa*

Chapa ya kwanza ya Matini Chanzi

Iliyoandaliwa na kuelezewa vyanzo vya hadithi zake

1417 HD. – 1997 AD.

Chapa ya pili

1431 HD. – 2000 AD.

**Daaru Twayyibah kwa uchapaji na usambazaji**

Ufalme wa Saudi Arabia – Riyadh – Assuwaydiyyu – Mtaa wa: Assuwaydiyyu Al-aam – magharibi mwa njia ya chini. S. L. P 7612 – Kodi ya posta 11472 – Simu: 4253737 – Faksi: 4258277

## UTANGULIZI

Shukrani zote ni za Allah, tunamshukuru, tunamtaka msaada na kumuomba msamaha. Na tunajikinga kwa Allah kutokana na shari za nafsi zetu na matendo yetu maovu. Yule atakayeongozwa na Allah, basi hana wa kumpoteza. Na yule atakayepotea, hana wa kumwongoza. Na ninashuhudia[1] ya kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, ni mmoja, hana mshirika. Na ninashuhudia ya kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake.

﴿**Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waisalmu kamili.** ﴾ Aali Imran 102.

﴿**Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi (asili) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana. Na (mwatazame) jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu (anayaona kila mnayoyafanya)**﴾ **.** An-Nisaa 1.

﴿ **Enyi mlioamini! Muogopeni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na Atakusameheni madhambi yeni. Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.**﴾ Ah-Ahzab 70 – 71. Ama baada ya hayo[2]:

---

([1]) Sheikh Albani Allah amuhifadhi, ameitaja kauli kutoka kwa Ibnu Al-Qayyimu Allah amrehemu, katika kitabu Tahadhibu Assunani (3/54) isemayo: Sheikh Al-Islaam Ibnu Taymiya amesema: (Kwa vile ilivyokuwa neno la shahada (kuingia Uislamu), kwa hali yoyote ile, haliwezi kubebwa na mtu mwingine kwa niaba ya mtu mwingine na wala halikubali kutamkwa kwa niaba ya mwingine. Kwa ajili hiyo ameitamka hiyo shahada kwa muundo wa umoja. Na kwa vile kuomba msaada, kujikinga na kuomba msamaha yote haya yanakubalika kutamkwa kwa niaba ya mwingine, kwa hiyo mtu anaweza kumuombea msamaha mtu mwingine, na kumuombea kwa Allah apate msaada wake, na kumuombea kwa Allah amkinge, kwa ajili hiyo ndio akayatamka maneno haya kwa muundo wa wingi – tunakuomba, nk.) Hotuba ya Haja Uk 10 , 11.

([2]) Hii ndio hotuba ya Haja, hotuba ambayo, Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akianza hotuba zake kwa hotuba hii. Na alikuwa akiwafundisha maswahaba zake hotoba hii. Na inapendeza kusomwa mwanzoni mwa kila hotuba kuanzia hotuba ya idi, Ijumaa, ndoa, darsa au mhadhara. Na hotuba hii inakuja kwa njia nyingi zilizo katika Sahih na sunani. Albani amezikusanya zote katika risala yake iitwayo (Hotuba ya Haja).

- Kila sifa njema ni za Allah aliyempeleka Mtume wake Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. Katika wakati ambao wanadamu wote walikuwa wameporomoka katika mashimo ya upotevu. Kwa hakika wanadamu wote wa wakati huo walikuwa wanahitaji sana kumpata mtu wa kuwaongoza katika njia iliyonyooka. Na kuwalingania waingie katika dini madhubuti. Na kuwatoa katika kiza na kuwapeleka katika nuru. Na kuwatoa kutoka katika kuabudu matwaghuti waelekee katika kumwabudu Allah peke yake, ambaye ni Mtukufu na Muweza.

- Waarabu walikuwa wakiabudu masanamu, kuwazika hai mabinti, kudhulumiana wao kwa wao, kuibadilisha dini ya Ibrahimu, na kutoa kauli zisizo za ujuzi kumhusu Allah.
- Wafursi (Wairani wa kale) walikuwa na itikadi ya miungu miwili: mungu wa kiza na mungu wa nuru. Kuwaingilia mama zao na mabinti zao. Na kufanyana watumwa wao kwa wao.
- Na Wayunani (Wagiriki) walikuwa wanaabudu masanamu. Na miungu ya batili inayogombana yenyewe kwa yenyewe. Na kujishughulisha na mambo ya muhali na kujiweka mbali na nuru ya ufunuo na uongofu wa mitume.
- Na waturuki walikuwa wanaharibu miji na kuwaadhibu waja.
- Na wahindi walikuwa wanaabudu ng`ombe. Na kusujudia mawe na miti.
- Warumi walikuwa wakiabudu nguvu ya ushenzi na kutumia mabavu na matamanio maovu yenye kuwaudhi watu wengine chini ya gamba laini la ukristo uliopotoshwa.
- Na Wayahudi walikuwa wakipinga na kukanusha, na wakiwa na dini kutatanisha, na kuchanganya uongo na uzushi kwa Allah.
- Na Wakristo walikuwa katika kauli ya Utatu, na kuabudu msalaba na picha (sanamu) za watakatifu na vitu vitakatifu.

Na hivyo hivyo yalikuwa makundi, nyumati na dini nyingine katika dunia yote.

Hii ni picha ya kusikitisha, kufedhehesha na ovu kwa huyu mwanadamu mwenye kupotea na kupasuka pasuka baada ya kukengeuka na kuiacha njia ya Allah na mwongozo wa ufunuo na nuru ya Utume.

- Allah akampeleka Mtume wake Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. na akateremsha Quran Tukufu ikiwa ni muujiza unaoendelea kubakia mpaka siku ya kiyama. Ikishuhudia kuwa Mtume amepewa

ujumbe.. na umma utaongoka kama utashikamana nayo. Kwa hakika Allah amekiteremsha kitabu chake vifungu vifungu kulingana na matukio na hatua waliyopitia nyota wema miongoni mwa Maswahaba waliokuwa kando ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake. ﴿**… Kama hivi (unavyoona tumeiteremsha kidogo kidogo kwa mpango mzuri) ili tuuthubutishe, (tuutilie nguvu) moyo wako (kwa hizo aya mpya zinazoteremka wakati baada ya wakati), na tumeipanga kwa uzuri.** ﴾ Al-Furqan 32.

Na kizazi cha kwanza miongoni mwa maswahaba kililelewa kwa Quran. Na kizazi hiki shupavu ndicho kilichobadilisha sura ya dunia yote katika kipindi kifupi cha chini ya miongo miwili. Na kwao ndipo kilipokuwa kile kinachojulikana tangu kuanza kwa umma wa Kiislamu, kupanda kwake na kuwa juu ya nyumati za dunia, za mashariki na magharibi, kwa upande wa kidini na kidunia na katika kila sekta.

- Na sifa njema ni za Allah aliyeitukuza dini yake, na kuifanya kuzishinda dini nyingine zote japo makafiri wanachukia. Na amempa ushindi mja wake na Mtume wake Muhammad rehema na amani ziwe juu yake dhidi ya wapinzani wake miongoni mwa washirikina na wafedhuli miongoni mwa maadui wa Allah na maadui wa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuchukuliwa na Allah hadi pale jicho lake lilipopata kitulizo kwa watu wengi kuingia katika dini ya Allah wakiwa makundi kwa makundi.
- Na sifa njema ni za Allah aliyekilinda kitabu chake kisipotee hadi kikatufikia kikiwa salama usalimini, hakina ziada, upungufu, kupotoshwa wala kubadilishwa. Na hii ni kinyume na yale yaliyotokea katika vitabu vilivyopita, vilivoteremshwa kwa nyumati nyingine. Na Allah mtukufu aliyetukuka ametusimbulia neema hizo kwa kusema: ﴿**Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Qrani); na hakika sisi ndio tutakaoyalinda.** ﴾ Al-Hijr 9. Allah ameifanya Quran ni yenye kubakia licha kurefuka kwa zama na kutofautiana kwa maeneo.
- Na sifa njema ni za Allah aliyekifanya kitabu hiki Kitukufu kuwa katiba ya umma huu. Na atakayefuata mwongozo wake atafuzu duniani na kufaulu huko Akhera. Na atakayekipuuza, basi Allah atamjaalia mtu huyo kuwa na maisha magumu duniani na siku ya

kiama atamfufua akiwa kipofu. Kisha atapewa adhabu ya jehanam, ambayo ni kali mno na ya yenye kubakia milele.

- Na sifa njema ni za Allah aliyeifanya Quran kuwa kipasuo cha nishati za ubunifu katika mioyo ya waislamu. Na pale waislamu wa mwanzo walipokielekea kitabu cha Mola wao, wakakisoma, kujifundisha na kuzilea nafsi zao na watu wao kwa mujibu wake. Na wakiwafundisha watoto wao na watumwa wao waliowaachia huru. Wanakifanyia kazi na kukitekeleza. Na kwa mwongozo wake walijenga mambo ya maisha yao miongoni mwa mambo ya kielimu na kazi na wito wa kulingania kuja katika sheria, siasa, uchumi na jihadi katika njia ya Allah huku wakibeba ujumbe wao kwa ulimwengu wote… Basi miongoni mwa matunda ya huku kuielekea Quran, yalikuwa ni haya: Allah aliwafungulia elimu ya dini yao – kiasi ambacho, kwa sababu ya Quran zilitokeza elimu zote za lugha, usuli (misingi), fiqihi (sheria za kidini), mawaidha, upokezi… mpaka mwisho - pia Allah aliwafungulia elimu za mazingira (dunia) zenye manufaa. Elimu za Kiislamu pale ziliposhamiri katika umma huu uliobora, hazikuleta matunda katika maarifa ya kinadharia tu, bali pia zilileta matunda katika maarifa ya kimalezi ya hakika, yaliyobadilisha uso wote wa dunia hii. Sio haya tu, bali pia ziliziandaa akili za umma huu ili ziwe akili zenye nguvu zaidi kielimu zilizowahi kudhihiri duniani… Akili za kufuata njia ya kisayansi iliyojipanga vizuri. Imepangwa na aya za Quran Tukufu. Na kuandaliwa ili zitoke na kwenda katika upeo wote wa ustaarabu wa kweli… Ustaarabu ambao unakusanya kwa pamoja baina ya mwongozo wa ufunuo na maono ya kidunia. Ustaraabu unaomwandaa mwanadamu ili afaulu duniani na kufanikiwa ahera. Ustaarabu unaojengwa juu ya: ﴿**… Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera, na utulinde na adhabu ya moto'.** ﴾ Al-Baqarah 201. Maendeleo yanayojipambanua kwa ukati na kati na kuzingatia roho na mwili kwa pamoja, akili na hisia kwa pamoja… Hayo sio maendeleo mabaya yaliyoharibiwa[1]. Yale maendeleo yasiyotazama chochote isipokuwa matamanio na starehe za kihisia za dunia hii tu. Maendeleo hayo yanathamini muonekano wa nje wa mwanadamu, tumbo lake na tupu (uchi) yake tu, na kupuuzia roho yake, hisia yake, misingi na malengo yake mazuri yaliyo matukufu,

[1] Mfano wa maendeleo ya Kimagharibi yanayowayawaya na kutahayari. Ambao ni urithi wa ustaarabu wa Kirumi wa kishenzi na ambao umeshatoweka.

ambayo kwa ajili ya hayo ndio ameumbwa na Allah na kupewa cheo cha kuisimamia dunia (ukhalifa) na kuhakikisha hayo yanatimia. Malengo yenyewe ni kumwabudu Allah Mtukufu.

- Na katika utimilifu wa neema za Allah kwa umma huu, ni pale alipoifanya muujiza wa Mtume wa umma huu kuwa muujiza ya kubakia milele. Zindiku, muujiza wenyewe ni Quran Tukufu. Qurana ambayo maajabu yake hayatoweki wala faida zake haziishi… Na Allah Mtukufu Aliyetukuka amekifanya kitabu hiki na kukifanyia kazi kuwa ndio utajo (ukumbusho) mkuu wa umma huu. ﴿**Bila shaka tumekuteremshieni Kitabu ambacho muna ndani mauidha kwenu. Je! Hamfahamu?** ﴾ Katika kitabu hiki kuna utajo na ukumbusho wetu … kuna utukufu wetu… kuna nguvu zetu duniani na ahera. Na Quran hii ndio utajo wetu baina ya nyumati zote. Kama tutakiacha na kukipotezea na kukipa mgongo… tunapotea na kudhalilika… na nyumati zote za dunia hii zitatushughulikia… kama inavyotokea sasa hivi. Tunayaona na kuyaishi, bali pia sote tunasagwa chini. Kitabu hiki sio kitabu cha kusomwa kwa kutabaruku tu! Wala hakiwekwi kama pambo tu! Na sio kitabu cha kupambwa na kuchovwa dhahabu na kutundikwa ukutani au kuwekwa katika magari ili kuondoa mikosi… Bali chenyewe ni kitabu cha uhai… kitabu cha utukufu… Kwa hakika kitabu hiki ni: ufunuo wa Mola… katiba ya Mwenyezi Mungu… ni mwongozo na rehema… ni ponyo la vifua (mioyo)… Hiki ni kitabu kilichosifiwa na Mola wetu ya kwamba chenyewe ni ﴿**… (Hiki ni) Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatowe watu katika giza uwapeleke katika nuru, kwa idhini ya Mola wao, uwafikishe katika njia ya yule Mwenye kushinda Mwenye kusifiwa (Naye ni Mwenyezi Mungu.** ﴾. Ibrahimu 1.
- Na Quran hii tukufu inakutaka wewe usimame na nafsi yako – ndugu yangu Muislamu – ili uutafakari uhakika wake. Na hiki kitabu cha (Habari Kubwa) – ambacho kipo mbele yako – cha mtunzi wake Dr. Muhammad Abdullah Daraazu Allah amrehemu. Kitabu hiki ni miongoni mwa maandishi bora kabisa yaliyoandikwa katika zama zetu za sasa. Kinamfungua macho na kumkumbusha muislamu wa kisasa juu ya uhakika wa Quran Tukufu – akiwa katika mihangaiko yake na kujishughulisha kwake na dunia. Kitabu hiki kinageuza mtazamo wako utazame pande nyingi ambazo inawezekana zimekupita kimaono na kihisia. Hata kama hazijakupita katika moyo

wako na kuwa unazisadikisha na kuziamini. Pia kinakukumbusha mambo ambayo muislamu anayahitaji kuwa macho nayo ili daima moyo wake ubakie ukiwa umefungamana na maneno ya Mola wake… kwa Quran Tukufu.

- Kwa hakika Allah – kwa ukarimu wake na neeza zake – ameweka wepesi – kukubaliana na warithi wa mtunzi, Allah amrehemu. Na kwa upekee kabisa Balozi Mustafa Daraazu Allah amlipe malipo mema. Kukubaliana juu ya kukiandaa kitabu hiki kwa ajili ya kukichapa kulingana na umuhimu wake na nafasi yake.

  Kwa hakika nimekitoa kikiwa na maelezo mafupi juu ya mtunzi wake – Allah amrehemu – kisha nikafuatisha kwa kutoa neno fupi lenye kichwa cha habari: (katika kitabu hiki). Kisha (Kubainisha kazi yangu katika kukitoa kitabu hiki kizuri).

**WASIFU WA PROFESA / MUHAMMAD ABDULLAH DARAAZU – ALLAH AMREHEMU.**

- Amezaliwa katika kijiji cha Mahallah Diyaayu mkoani Kafri Sheik, mwaka 1312 HD. – 1894 AD.
- Alikulia katika nyumba yenye elimu kubwa na kutengenekewa. Kwani baba yake Sheikh Abdullah Daraazu – alikuwa naye ni sheikh na mwanazuoni wa Dumiyaatwi – yeye ndiye mwenye sherehe ya Al-Muwaafaqaati ya Asshaatwibiyyi.
- Aliihifadhi Quran Tukufu yote akiwa na miaka kumi.
- Tangu utotoni alijulikana kwa utambuzi, uerevu na kuongoza masomoni.
- Alienda Alexandria mwanzoni mwa mwaka 1905 AD. Na kujiunga na chuo cha kidini. Akapata cheti cha elimu ya sekondari kidato cha sita mwaka 1912 AD.
- Akapata cheti cha Kimataifa cha Annidhaamiyya mwaka 1916.
- Alipata kazi ya uwalimu punde tu baada ya kuhitimu mafunzo ya kutoka katika chuo cha kidini. Akajifunza Kifaransa katika shule ya Allayliyya. Hadi akawa mtu wa kwanza katika waliofaulu katika shahada ya kitengo cha juu katika shule hiyo mwaka 1919 AD.
- Alichaguliwa kufundisha kitengo cha Kiarabu cha Azhar Sharifu mwaka 1928 AD. Kisha kitengo cha Attakhaswuswi mwaka 1929 AD. Kisha kitengo cha misingi ya dini cha Azhar mwaka 1930 AD. Kisha katika kitengo cha Attakhaswuswi.
- Aliandika kitabu (Almukhtaaru) alipokuwa anafundisha somo la Tafsiri (Tafasili ya Quran) na Hadithi katika kitengo cha Misingi ya Dini mwaka 1932 AD.
- Alianza kuandika tafiti kuhusu Quran Tukufu – aliouwasilisha kwa jina la: Katika Tafsiri – na utafiti huu ndio mwanzo wa kitabu hiki cha (Habari Kubwa).
- Alitekeleza faradhi ya Hija mwaka 1355 HD. – 1936 AD.
- Alichaguliwa kuwa mwakilishi wa Azhar kwenda Ufaransa ili akajiunge na chuo kikuu cha Sorbonne mjini Paris. Hivyo akapitisha muda mwingi akiwa nje ya Misri, muda ulio baina ya Machi 1937 AD. – mpaka Machi 1948 AD.
- Alipata digrii kutoka chuo cha Sorbonne mwaka 1940 AD.
- Mtunzi alitumia muda wa miaka sita (1941 AD. – 1947 AD.) kuandaa risala mbili za kupata udaktari wa falsafa kwa lugha ya Kifaransa. Nazo

ni (Mlango wa Kuingia katika Quran) na (Desturi / Katiba ya tabia njema katika Quran). Risala hii ilijadiliwa mbele ya tume iliyoundwa na wakuu wa kistashriqiina, na miongoni mwao ni: Massignon – Levi Provencal na wenginewe. Na mtunzi akapewa cheti cha udaktari wa falsafa kwa kiwango cha juu kabisa mnamo 15 / 12 / 1947 AD.

- Baada ya kurejea kwake nchini Misri Machi 1948 AD alitakiwa afundishe historia ya dini mbalimbali katika chuo kikuu cha Cairo.
- Alipata kuwa mwanachama wa jopo la wanazuoni wakuu wa Misri mwaka 1949 AD.
- Akapewa kazi ya kufundisha tafsiri katika kitengo cha Daaru Al-Uluumi na kufundisha Falsafa ya Tabia katika kitengo cha Attakhaswuswi katika chuo kikuu cha Al-Azhar.
- Alijulikana kwa tabia njema katika mazungumzo yake, upole na unyenyekevu. Ijapokuwa alikuwa jasiri, mgumu mwenye kusimamia haki. Na pale alipopewa nafasi ya kuwa Sheikh Al-Azhar Asshariifu mwaka 1953 AD. Alikataa kwa sababu ya pingu / vizuizi vilivyokuwa vimeambatanishwa na ofa hiyo. Alifanya hivyo kwa kuienzi dini ya Allah na kwa ajili ya nia yake safi kwa itikadi yake.
- Allah amrehemu, alikuwa anasoma sudusi (moja ya sita) ya Quran kila siku. Alidumisha suala hili hata pale alipokuwa Ufaransa wakati wa vita.
- Allah amrehemu, alifariki nchini Pakistani alipokuwa anahudhuria mkutano wa Kiislamu, Januari 1958 AD.

  Kwa kufariki kwake, ulimwengu wa Kiislamu ulipoteza mtu wa kupigiwa mfano wa mwanazuoni wa Ki-Azhari mwenye uchungu na dini yake. Mwenye kulinda heshima yake. Mlinganiaji kuelekea kwa Mola wake kwa hekima na mawaidha mazuri. Allah amrehemu na amsamehe.

**Kazi (Vitabu vya) Daktari Muhammad Abdullah Daraazu:**

- Al-Mukhtaaru.
- Mlango wa Kuingilia Katika Quran (Kwa Kifaransa – kimefasiriwa kwa Kiarabu na Kiswahili).
- Desturi / Katiba ya Tabia Njema Katika Quran (Kwa Kifaransa – kimefasiriwa kwa Kiarabu).
- Dini.
- Habari Kubwa.
- Masomo ya Kiislamu Katika Mahusiano ya Kijamii na Kimataifa.
- Mitazamo Katika Uislamu.

- Asili ya Uislamu.
- Ibada: Swala – Zaka – Swaumu – Hija.
- Rai ya Uislamu Kuhusu Vita.
- Baina ya Udhanifu na Uhalisia.
- Al-Azhar ni Chuo Kikongwe Kipya.
- Mkusanyiko wa Hadithi za Redioni zinazohusu Dini na Tabia Njema.
- Mkusanyiko wa Mihadhara na Makala zenye Manufaa.

❋ ❋ ❋

## KATIKA KITABU HIKI

- Wanazuoni wa Kiislamu wa kizazi hadi kizazi wameifanyia kazi miujiza ya Quran. Wakapanua sana katika kubainisha sehemu za miujiza. Na wakazama katika aina za miujiza ambayo yenyewe inazidi uwezo wa kuidhibiti idadi yake… Isipokuwa miujiza hiyo ya Quran inasalia kuwa ni maalum na kutokana na miujiza hiyo huchimbuliwa mambo mapya katika kila zama. Na hivyo hivyo Quran inaendelea kuwa ni muujiza wa kila zama. Yenyewe inajisasisha daima. Jambo ambalo linathibitisha na kuonesha ushahidi ya kuwa Quran hii haitokani na mwanadamu… Bali yenyewe ni ﴿**Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye hikima na Mwenye ujuzi wa kila kitu.** ﴾ Hud 1. Pia chenyewe ni ﴿**… Mawaidha kutoka kwa Mola wenu na pozo (dawa ya) yale yaliyomo vifuani, na uwongofu (mkubwa) na rehemu kwa wanaoamini. (Nayo ni Qurani ambayo ikifuatwa humtengezea mtu dunia yake na Akhera** ﴾**.** Yunus 57. Ama kuhusu athari zake, hebu sikiliza kauli ya Allah Mtukufu: ﴿**Lau kama tungeiteremsha hii Quran juu ya mlima, ungeliuona ukinyenyekea (na) kupasuka kwa sababu ya hofu ya Mwenyezi Mungu...** ﴾ Al-Hasr 21.
- Na kitabu hiki cha **Habari Kubwa** – kipo tofauti na vitabu vingine vya miujiza ya Quran – kwani chenyewe kinajipambanua kwa mambo mengi:

- Mtindo wake wa kielimu ulio madhubuti. Na mfumo ambao fikra zake zimepangwa kwa hatua taratibu zenye kupanda juu.
- Ubainifu safi, ibara nyepesi, na dibaju yenye kung`aa.
- Kitabu kipo katika umbo la kati na kati, hivyo msomi hachoshwi wala hatakiona kuwa ni kirefu sana. Licha ya fikra zake za kina alizozichakata. Na hatua mbalimbali zilipitiwa na kitabu hiki.
- Kinawaongelesha watoto wa kizazi hiki. Kizazi ambacho kipo mbali mno na wema waliotangulia na wanazuoni waliopita, kwa kutumia mtindo wa kizazi hiki unaojulikana. Kwa hiyo kitabu hiki kimekuja kikiwa kimekusanya baina ya yale yaliyowanufaisha waliopita na baina ya yale yanayowafahamisha na kuwatikisa waliopo na watu wa kisasa. Kwa hakika Mwandishi – Allah amrehemu – amedhihirisha maarifa ya kina kwa kutumia Quran. Na uwezo mzuri sana wa kubainisha Miujiza kwa kutumia ibara nyepesi na kwa njia fupi.

- Kuzingatia umoja wa maudhui kwa sura za Quran. Na kuthibitisha kwa hoja na ushahidi ya kwamba, kwa hakika sura moja katika sura za Quran yenyewe ni kama jengo lililoshikamana haiwezekani kuondoa hata tofali moja bila ya kuliharibu na kulifisidi mfumo wake.

- Nitosheka kukipongeza kitabu hiki. Inamtosha mtunzi wake – Allah amrehemu – kwa kule kuacha kwake elimu yenye manufaa. Thawabu zake zinamwendea, na msomi anamrehemu hadi pale atakapopenda Allah.
- Na hiki kilicho mbele ya mikono yako, ewe ndugu mpendwa msomaji kinazunguka kuizunguka Quran Tukufu. Na sasa pokea mpangilio wake:

- **Utafiti wa kwanza:**
  Maana ya Quran na tofauti iliyopo baina yake na hadithi Qudusia na hadithi Nabawiya.
- **Utafiti wa pili:**
- **Hatua ya kwanza**: Chanzo cha Quran. Je inawezekana chanzo chake kiwe ni maneno ya Muhammad rehema na amani ziwe juu yake? Na kulipinga wazo hili kwa kutumia historia ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na kutokana na uhalisia wa utabiri wa Quran.
- **Hatua ya pili:** Kakana uwepo wa mwalimu yeyote wa kibinadamu kwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake.
- **Hatua ya Tatu**: Tukio la Ufunuo na namna linavyojulisha kuhusu chanzo cha Quran.
- **Hatua ya nne:** Kiini cha Quran kinafunua hakika ya chanzo chake.
  Miujiza ya kilugha – Miujiza ya kisayansi – Miujiza ya Utungaji sheria[1].
- Mfano wa tafiti za Miujiza katika mpangilio wa Quran, umoja wa Maudhui katika sura za Quran, Kutekeleza suala hili la umoja wa maudhui katika sura ndefu zaidi ya Quran nayo ni suratu Al-Baqarah. Na utafiti huu ni miongoni mwa ncha za utafiti wa kitabu hiki kizuri.

❋ ❋ ❋

[1] Mtunzi – Allah amrehemu – hajaitaja miujiza hii miwili ya mwisho katika kitabu hiki, lakini ameitaja katika miswada yake ya juzuu ya pili.

## KAZI YANGU KATIKA KUKITOA KITABU CHA (HABARI KUBWA)

- Kuzitoa – yaani kueleza sanadi za wapokezi wake – hadithi zote za kitabu hiki. Na kueleza sehemu zake katika vitabu vikuu vya hadithi za Mtume.
- Kubainisha sababu za kuteremka kwa aya pale muktadha unapokuwa na haja ya kubainisha hilo. Na kutoa maelezo katika baadhi ya maeneo.
- Kufafanua maneno mageni, kupambanua baadhi ya ibara muhimu na maswali ya mwongozo.
- Kuweka vichwa vya habari vya vifungu vya kitabu katika mabano kama hivi […] na mara nyingi vichwa hivi vya habari vinatokana na yaliyomo katika kitabu hiki. Na hili ni jambo muhimu kwa kuziunganisha fikra za kitabu hiki na kuzipanga katika ubongo wa msomaji.
- Kuzipambanua aya za Quran Tukufu, na vile vile hadithi tukufu za Mtume.
- Kuweka jina la sura na nambari ya aya baada ya kila aya mubashara katika mabano kama hivi […] ili iwe wepesi kuzirejea.
- Kusahihisha makosa ya kiuchapaji yaliyokuwepo katika chapa zilizopita.
- Kuitunza matini asilia ya kitabu. Sijaingiza ziada wala sijapunguza. Isipokuwa yale yaliyokuwa katika kukamilisha upungufu katika aya katika uk 47, 149 wa matini chanzi.
- Kupambanua maelezo ya Dkt. Muhammad Abdullah Daraazu Allah amrehemu, pambizoni mwa maelezo yangu kwa kuweka tamko [Daraazu] mwishoni mwa yale maelezo ya asili. Licha ya kwamba yenyewe nayo ni ya asili. Na hivyo ni kutokana na wingi wa maelezo au ufafanuzi wangu wa maneno mageni.
- **Uzinduzi:**

- Nimeweka nukta tatu zinazofuatana kama hivi … wakati nilipofuta baadhi ya maneno katika maelezo au unukuzi.
- Nimefupisha pale nilipozifanyia takhriji (kueleza wapokezi wake) hadithi kutoka swahihi mbili, kama itakuwa inatoka kwa zote mbili au katika kimoja wapo, nikiogopea kurefusha.

- Na wakati wa kuigemeza hadithi kwa Bukhariyy: nataja kitabu kisha namba ya kiujumla ya hadithi katika Swahihi Al-Bukhaariyyi.
- Na wakati wa kuigemeza hadithi kwa Muslim: nataja kitabu kisha namba maalum ya hadithi katika kitabu hiki.

Na ndugu mpendwa msomaji ukumbuke ya kuwa hakuna shaka katika juhudi hii kutoka kwangu ndani ya kitabu hiki, utapata baadhi ya upungufu, makosa au kuteleza kwa kalamu. Basi hayo ni katika hali ya ubinadamu.. na kama Rabiu bin Sulaiman mwanafunzi wa Shaafiiyyu alivyosema: (Nimesoma kitabu cha Al-Risala Al-Masriyyat Alaa Asshaafiiyyu zaidi ya mara thelathini na nusu. Hakuna hata mara moja katika hizo ila alikuwa akikisahihisha. Kisha Shaafiiyyu alisema mwishoni mwa kitabu hicho: Allah amekataa kuwepo kwa kitabu kilicho sahihi kabisa, zaidi ya kitabu chake… Na linalojulisha hivyo ni kauli ya Allah Mtukufu Aliyetukuka**: ﴿… na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi.** ﴾ An-Nisaa: 82[1].

Natarajia kutoka kwa ndugu mwema, awanasihi ndugu zake wasifanye ubahili wa kuwanasihi, kuwapa mwongozo au kuwaita wafanye yaliyo ya sawa sawa. Na Allah amrehemu ndugu yeyote atakayeniongoza kuzirekebisha aibu za nafsi yangu au za kazi yangu.

Namuomba Allah Mtukufu Aliyetukuka aniruzuku moyo safi katika nia yangu na kutenda ya sawa sawa katika kazi yangu hii. Na aninufaishe pamoja na mtunzi na ndugu zangu Waislamu kwa kitabu hiki. Na atufanyie ihsani kwa kutupatia ujira wake katika siku ambayo, mali hayatamfaa mtu wala watoto hawatamfaa. Isipokuwa atakayemwendea Allah akiwa na moyo uliosalimika.. Hakika yake ni Mwenye kusikia na ni Mwenye kujibu.

Na mwisho wa maombi yetu tunatoa shukrani na sifa njema zote kwa Allah Mola mlezi wa viumbe wote. Na rehema na Amani zimwendee Muhammad mja wa Allah na ni Mtume wake. Ewe Allah tukubalie.

*Imeandikwa na: Abdulhamid Ahmad Ad-dakhaakhiniyyu*

*Alexandria mnamo: 21 / 5 / 1417 HD.*
*3 / 10 / 1996 AD.*

[1] Sifa za Shaafiiyyu, na Al-Baihaqiyyu 2 / 36.

## *KWA JINA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU*

**Sehemu ya kwanza ya kitabu cha (Habari Kubwa) mzaliwa mpya … wa kale … mpya katika kipande chake na mwisho wake. Wa kale katika machomozo yake na mwanzoni mwake …**

Kitabu hiki kimezaliwa katika kampasi ya Chuo Kikuu. Tangu miaka ishirini na nusu, lakini kwa wakati huo kilikuwa hakijadhihiri isipokuwa shingo na kifua chake tu… ama ncha zake zilikuwa hazijazaliwa. Na umbo lake lilikuwa halijakamilika, isipokuwa leo hii.

Wanafunzi wa jana walishuhudia mwanzo wa jambo lake. Pale walipokuwa wakisomewa vipande vipande vilivyo tawanyika. Kwa vipindi vinavyofuatana au visivyofuatana. Na kila wanapokusanyika walikuwa wakipitia kurasa chache zisizozidi kumi na baadhi sehemu ya kumi tu. Waliharakisha kuzichapisha na wakawa wakimuhimiza mtunzi aweke kipande chake kinachofuatia…

Kisha baada ya hayo yalikuja mambo[1] yaliyozuia kukikamilisha. Hivyo akashindwa kukikamilisha… Kwa hiyo, kile kiasi kilichochapwa kilibakia kimezuiliwa katika shirika la uchapaji. Au kikiwa kwa wanafunzi wa utafiti huu wa wakati huo tu… hadi pale leo hii Mtukufu Mweye cheo – na kila kitu kwake yeye kina makadirio yake – alipomuidhinisha mtunzi kuongeza chembechembe nyingine. Kwazo, ndipo nguzo za kitabu hiki zilipokamilika.

---

[1] Mtunzi aliishi nje ya nchi kwa miaka kumi na miwili: kuanzia mwanzoni mwa mfunguo sita 1355 hadi ulipodhihiri Mfungo saba 1367 (Mei 1936 – Machi 1948) akipelekwa na Chuo Kikuu cha Al-Azhar kwenda katika vyuo vikuu vya Ulaya. Huko akajifunza lugha kadhaa miongoni mwa lugha za watu wa Magharibi. Na alizijua njia za kitafiti – za wataalamu wa Ulaya. Kisha akaandika tafiti mbili za Chuo Kikuu kwa lugha ya Kifaransa nazo ni: Kuhusu Quran na Kuhusu Dasturi ya Tabia njema katika Quran… Kisha baada ya kurudi kwake nchini Misri akapitisha miaka tisa mingine akishughulika katika mambo ya kielimu. Hebu na tutoe maalezo kwa haraka, kuhusiana na miongoni mwa mambo yake ya muhimu ni:

1- Mihadhara katika elimu ya Historia ya Dini katika kitengo cha Sanaa cha Chuo Kikuu cha Cairo.
2- Mihadhara katika falsafa ya Tabia njema katika kitengo cha Attakhaswuswi katika Chuo Kikuu cha Al-Azhar.
3- Kuiandika mihadhara yake hii na ile mingine kisha kuitoa katika risala mbili kwa lugha ya Kiarabu.. Ya kwamba mtunzi, wakati wa shughuli zote hizi, mapenzi yake yalikuwa yanamjia na kumtaka akamilishe Juzuu hii. Na hakuacha kuendelea katika kipindi hicho akipokea barua baada ya barua kutoka kwa watoto wake na wenzake, zikimtaka aendeleze utafiti huu. Na lakini yeye hakupata wepesi wa kufanikisha baadhi ya haya matamanio isipokuwa kwa sasa hivi tu. Na utukufu ni wa Yule Allah ambaye hashughulishwi na jambo na kuacha jambo lingine [Daraazu].

Na kwazo ndipo kikawa tayari kutolewa nje ya wigo wa usomi wa chuo kikuu. Na kwenda katika anga za usomi za kimataifa. Ili kiongee na akili zote zilizomacho na zenye uhakiki wa mambo. Zisizochukua kila inachokichukua ila kwa uelewa na hoja madhubuti. Na hazikiachi kile inachokiacha ila kwa uelewa na hoja madhubuti. Na kuelekea kwa kila hisia za kimajaribio zenye vionjo vizuri. Zisizotosheka na habari tu zikaacha cha kushuhudia. Na hazitosheki na uzito zikaacha kupima.

Kwa hakika yenyewe ni simulizi inayoanzia katika nukta ya kuanzia…

Haimhitajii msomaji ajiunge chini ya bendera fulani; wala kuingia katika madhehebu maalum. Wala haimlazimikii awe mbobezi katika fani fulani; wala kupata daraja fulani ya kielimu, bali anatakiwa airejeshe nafsi yake katika ule ukurasa mweupee usio na kitu. Isipokuwa tu abakishe maumbile yaliyosalimika. Na hisia zenye hamu ya kujua, na matakwa ya kweli ya kufikia katika haki kuhusiana na hii Quran…

Na hakika mambo yalivyo, Allah akipenda, kitakuwa ni chenye kufika tu.

Mwezi Shaabani mwaka 1376 (Machi 1957).

***Muhammad Abdullah Daraazu***

**Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwenye Kuneemesha Neema Kubwa Kubwa Na Mwenye Kuneemesha Neema Ndogo Ndogo.**

(Sifa njema ni za Allah) aliyetufanya wabora juu ya nyumati zote kwa kupitia Quran. Na kwayo ametupatia kile ambacho hajawapatia watu wowote ulimwenguni: amekiteremsha kikiwa ni mwongozo wa daima wa ulimwengu wote. Na akakifanya ndio mwisho wa sheria zote za kutoka mbinguni. Kisha akakifanya kuwa chenyewe ndio hoja iliyosimama kwa zama zote. Na rehema na amani ziwe kwa yule ambaye tabia yake ilikuwa ni Quran.[1] Na usia wake ni Quran.[2] Na urithi wake ni Quran.[3] Aliyesema: ‘‘Mbora wenu ni yule aliyejifunza Quran na kuifundisha’’[4]

Ewe Mola wetu, kama ulivyotupatia hadhi ya kuwa warithi wa utajo huu wa hekima, tufanyie wepesi kuuhifadhi na kuukumbuka. Na tufanye wenye kupenda kuisoma na kuizingatia. Tunakuomba utujaalie tuwe miongoni mwa watu bora kabisa wanaoirithi, ambao wao kwa mwongozo wa Quran ni wenye kushikamana nao. Na ambao wao ndio wenye kusimamia kuilinda. Na ambao siku ya kiama watafufuliwa chini ya bendera ya Quran. Wakiwa katika jeshi la kiongozi wetu mkuu na Mtume wetu mkarimu sana ambaye ni Muhammad Ibnu Abdullah rehema na amani ziwe juu yake. Na juu ya aali zake, maswahaba wake, wafuasi wake na vipenzi vyake.

۞ ۞ ۞

(Ama baada ya hayo) hizi ni tafiti kuhusu Quran Tukufu. Nimeziwasilisha katika darasa za tafsiri kwa wanafunzi wa kitengo cha Misingi ya dini katika chuo kikuu cha Al-Azhar iliyojengeka.

---

[1] Hii ni ishara ya hadithi ya Mama wa waumini, Aisha Allah amuwie radhi pale alipoulizwa na Saadu bin Hishaam kwa kusema: **‘‘Ewe Mama wa waumini, nieleze kuhusu tabia za Mtume rehema na amnani ziwe juu yake. Bibi Aisha akasema: Je hausomi Quran? Akamwambia: hapana (ninasoma). Akamwambia: Kwa hakika tabia za Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake zilikuwa ni Quran. Akasema Saadu: Nikakusudia kusimama na sitomuuliza yeyote kitu chochote mpaka nakufa….’’** Imepokewa na Muslimu katika mlango wa swala ya wasafiri 139. Na imepokewa na Ahmad 6 / 91, 163 kwa tamko: ‘‘Tabia zake zilikuwa ni Quran’’.

[2] Hii ni ishara ya hadithi ya Abdallah Bin Abii Aufii: **‘‘Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake, ameusia Kitabu cha Allah’’**. Imepokewa na Bukhariyyu na Muslimu. Bukhariyyu ameipokea katika Almaghaazii 4460. Na Muslimu katika Alwasiyyati 16.

[3] Ibnu Abbasi Allah amuwie radhi na baba yake, aliulizwa: **‘‘Je, Nabii rehema na amani ziwe juu yake aliacha kitu? Akajibu: Hajaacha ila kile kilichopo baina ya majalada mawili [yaani Quran]’’**. Imepokewa na Bukhariyyu katika Fadhaailu Alquran 5019.

[4] Imepokewa na Bukhariyyu miongoni mwa hadithi ya Othman Bin Affaan Allah amuwie radhi katika mlango wa Fadhaailu Alquran 5027.

***Nimetaka kwa tafiti hizi kukisifu kitabu cha Allah kwa undani wake na mambo yake maalum. Na kunyanyua niqabu (pazia) kuhusu upande fulani wa mambo ya hakika yanayoshikamana nayo. Na niweke mpango unaotakikana kuupitia katika kuisoma Quran***.

Kwa hakika katika tafiti nyingi miongoni mwa hizi nimechunga aina fulani ya kutolea maelezo na uchambuzi. Na kiasi fulani cha kuyafanyiakazi na kutolea mifano. Sijatosheka na kuashiria tu pale ibara inapowezekana kufanya hivyo, wala kwa kutoa hoja tu, pale inapowezekana kuweka kitu halisi. Kwa kufanya hivyo natarajia yafunguke macho ya walioghafilika. Na kwa hiyo waipate nuru yao ikiwa inatembea mbele yao na kuliani kwao. Na vifurahie vifua vya waumini. Hivyo wazidi kuamini juu ya Imani yao.

Ewe Mola wetu! Tutimizie nuru yetu. Tusamehe, kwa hakika wewe ni muweza juu ya kila kitu. Na kuhusu kupokea maombi yetu, wewe ndiye unayestahiki zaidi.

1352 HD. – 1933 AD.

Muhammad Abdullah Daraazu

۞ ۞ ۞

## TAFITI YA KWANZA

## KUHUSU KUAINISHA MAANA YA QURAN

### Na tofauti baina yake na hadithi Qudsiyyu na hadithi Nabawiyyu

### [Maana ya kilugha na kiminyumbuliko ya maneno mawili: (Quran) na (Kitabu)]

Neno Quran kiasili ni mzizi wa neno ulio katika uzani wa fu-`ulaan kwa ‘u’ mwanzoni. Kama ghuf-raan, shuk-raan na tak-laan. Kwa mfano unasema: Nimekisoma kwa qar`an, qiraa-atan, na quran zote tatu kwa maana moja nayo ni nimeisoma kisomo hasa. Kwa hakika matumizi ya neno Quran yamekuja kwa maana hii ya kimzizi katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha). Wakati tunapokusomea, basi fuata (Qar`anahu) kusomwa kwake.** ﴾ Al-Qiyama 17 – 18. Kwa maana ya kusomwa kwake.

Kisha neno hili likawa nomino ya pekee[1] la hiki kitabu kitukufu. Na matumizi haya ya neno hili ndio yanayotumika sana. Na miongoni mwayo ni kauli Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Hakika hii Qurani inaongoza katika njia iliyonyooka kabisa…** ﴾**.** Bani Israil 9.

Katika kuiita jina hili la Quran imezingatiwa kuwa yenyewe inasomwa[2] katika ndimi. Kama ilivyozingatiwa katika kuiita kwa jina la Kitabu, kuwa

---

[1] Jina hili huitwa kwa kumaanisha mjumuisho ya matamko ya mkusanyiko wa hiki kitabu. Na kwa kila kipande cha kitabu hiki. Kwa hiyo, ukimsikia anayesoma aya ya Quran, ni sahihi kwako kusema kuwa mtu huyo anasoma Quran: ﴿**Na isomwapo Quran isikilizeni na nyamazeni ...** ﴾ Al-Aaraf 204 [Daraazu].

[2],3 Huu ni ubainifu wa namna zilivyounganishwa baina ya maana mbili, maana iliyonukuliwa na maana iliyohamishiwa. Nayo imejengewa kwa kile kilichokuwa mashuhuri katika matumizi ya kusoma katika upekee wa kuisoma. Na kusoma ni kuyaunganisha matamko baadhi kwa baadhi nyingine katika kuyatamka. Na kutukia neno Al-Kitaabu kwa maana maalum mwandiko. Na mwandiko ni kuyaunganisha maneno baadhi yake kwa mengine katika hati. Tukirejea katika mizizi asili wa maneno mawili haya, katika lugha ya (Kiarabu). Tunakuta matamko mawili (ka ta ba = ameandika) na (qa ra a = amesoma). Yote mawili yanazunguka juu ya maana ya kukusanya na kujumuisha bila kizuizi. Na asili hii ya mwanzo inaangaza kuwa kila moja katika majina mawili haya linaonesha kuwa lina sifa ya kujumuisha. Ama kwa maana ya nomino ya mtenda au nomino ya mtendwa. Kwa hiyo maana yake inakuwa (Mjumlishaji) au (kinachojumlishwa). Na nomino hii sio tu inajulisha kuwa hichi kinachoitwa hivyo ni chenye kukusanya sura na aya, au ya kwamba chenyewe ni mjumuiko wa hizo sura na aya. Kwa kuzingatia kuwa hayo ni maandiko yaliyoandikwa katika kurasa za moyoni. Au

chenyewe kimeandikwa[1] kwa kalamu. Majina yote mawili, ni katika ile kukuita kitu kwa kuzingatia maana halisi ya kinachotokea katika kitu hicho.

### [Siri Ya Kuitwa Majina Yote Mawili]

Na katika kuiita Quran kwa majina haya mawili kuna ishara inayoonesha kuwa miongoni mwa haki zake ni kutiliwa umuhimu kwa kukihifadhi katika sehemu mbili na sio sehemu moja. Namaanisha ya kwamba, ni wajibu kukihifadhi vifuani na katika maandiko vyote kwa pamoja. Kama kitapotea kimoja basi kingine kitamkumbusha. Hakuna kuamini hifadhi ya aliyekihifadhi mpaka iwe imeafikiana na maandishi yaliyokubaliwa na Maswahaba. Iliyonukuliwa kizazi kwa kizazi hadi kutufikia ikiwa katika umbo lilelile la mara ya kwanza. Na hakuna kuamini maandishi mpaka yaafikiane na yale yaliyo kwa mwenye kuihifadhi kwa mapokezi sahihi iliyopokewa kwa njia ya almutawaatiru[2].

---

kwa kuzingatia kuwa yenyewe ni michoro ilichorwa katika kurasa na mbao. Au kwa kuzingatia kuwa zenyewe ni sauti zisomwazo zilizopangiliwa ulimini. Bali ni kwa maana ya kina zaidi kuliko hizi zote. Nayo ni kuwa maneno haya kwa hakika yamekusanya fani za kimaana na hakika mbalimbali. Na kwamba chenyewe kimekusanya ndani yake vijitabu vya hekima na hukumu. Na pale unaposema Alkitaabu au Alquran, utakuwa kama vile umesema (Maneno yanayojumlisha elimu) au (elimu zilizojumlishwa katika kitabu). Na hivyohivyo Allah Mtukufu amikielezea pale alipotoa habari ya kwamba amekiteremsha ﴿**… Na tumekuteremshia Kitabu hiki kielezacho kila kitu…** ﴾ An-Nahl 89. Hivyohivyo Mtume rehema na amani ziwe juu yake amekielezea, pale aliposema: **‘‘Ndani yake kuna habari za mambo ya kabla yenu, na habari za baada yenu. Na hukumu zenu.’’** Imepokewa na Attirmiziyyu [Daraazu].

- Nikasema: hadithi hii kwa Attirmiziyyu ipo katika Fadhaailu Alquran 2906. Na hadithi kama hii ipo kwa Ahmad 1 / 91 zote ni katika mapokezi ya Alhaarithu kutoka kwa Ali bin Abii Twaalib. Na Attirmiziyyu alisema kuhusu hadithi hii: Hadithi hii hatuijui kutoka kwa mwingine isipokuwa tunaijua kwa njia hii tu, na katika sanadi yake kuna asiyejulikana, na kuhusu huyu Alhaarithu kuna maneno (maqalu). أ – هـ. Na Alhaafidhu ibn Kathiiri amemuelezea katika Fadhaailu Alquran uk 11: na ufupisho wa hadithi hii ni kuwa haya ni maneno ya Amiri Muuminiina Ali Allah amuwie radhi. Na baadhi wamefahamu vibaya na kuiegemeza kwa Mtume. Na haya ni maneno mazuri na yapo sahihi. أ – هـ. Kisha akatiririsha ushahidi wa hadithi hii kutoka katika hadithi ya Ibnu Masuudi katika Fadhaailu Alquran cha Abuu Ubaid. Na hadithi hii ya ushahidi imepewa hukumu ya udhaifu sana na Sheikh Ahmad Shaakir katika Almusnad 704. Pia na Sheikh Albaaniyyu katika Adhwaiifatu 1776.

[1] Maelezo yale yale ya maelezo ya kifungu cha pambizo kilichopita. Kuweka mbili kwa pamoja!

[2] Almutawaatiru: nayo ni ile iliyopokelewa na wapokezi wengi katika kila tabaka miongoni mwa matabaka ya wapokezi wake kiasi ambacho haiwezekani kwa wingi wao huo wawe wameafikiana kuzua na kudanganya.

**[Siri ya Quran kuhusika yenyewe peke yake kuwa ya milele bila ya kupotoshwa, kinyume na vitabu vilivyopita]**

Na kwa uangalizi huu wa pande mbili, ulioletwa na Allah katika nafsi za umma wa Muhammad kwa kumuiga nabii wake, ndipo Quran imebakia ikiwa imehifadhiwa katika hifadhi imara sana. Na hilo ni kutekeleza ahadi ya Allah ya kusimamia mchakato wa kuilinda pale aliposema: ﴿**Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Quran); na hakika sisi ndio tutakayoyalinda.** ﴾ Al-Hijr 9. Na Quran haikupatwa na yale yaliyovipata vitabu vitabu vilivyopita, miongoni mwa kupotoshwa[1] kubadilishwa[2] na kukatika kwa wapokezi wake[3]. Ni vitabu ambavyo Allah hakuweka ahadi ya kuvilinda. Bali ameviacha katika hifadhi ya watu. Na kwa hiyo Allah amesema: ﴿**… na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; …** ﴾ Al-Maidah 44. Yaani walitakiwa wakilinde[4] - Na

---

[1] Kupotoshwa: Kubadilishwa na kupindisha kitu kwa kukitoa kutoka katika maeneo yake kwa kukitanguliza au kukicheleweshaa au kukifuta au kukizidisha au kukipunguza.

[2] Kubadilishwa: ni kukiweka kitu sehemu ya kitu kingine.

[3] Kukatika kwa wapokezi: ni kutowepo au kutokujulikana wapokezi au wasimulizi walioinukuu habari katika muda fulani.

[4] Allah Mtukufu Aliyetukuka amesema kuhusiana na Wayahudi na wanzuoni wao**:** ﴿**… na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; …** ﴾ Al-Maidah 44. Aliwataka wakihifadhi na kutekeleza hukumu zake. Wakakipoteza na kukipuuzia na kutengua ahadi yao na Mola wao. Kama Allah Mtukufu Aliyetukuka alivyowaelezea, pale aliposema: ﴿**Na Mwenyezi Mungu alifunga ahadi na wana wa Israili (Mayahudi). Na tukawawekea miongoni mwao wakubwa kumi na mbili. Na Mwenyezi Mungu akasema: ‘’Kwa yakini mimi ni pamoja nanyi. Kama mkisali na kutoa zaka na mkiwaamini Mitume wangu na kuwasidia na kumpa Mwenyezi Mungu karadha iliyo nzuri (kwa kutoa katika njia ya kheri na kusaidia masikini), bila shaka nitakufutieni maovu yenu na kukuingizeni katika Mabustani ipitayo mito mbele yake. Lakini atakayekataa miongoni mwenu baada ya (ahadi) hii, bila shaka amepotea njia iliyo sawa. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, tuliwalaani na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu (hazisikii kheri) wamekuwa wanayabadilisha maneno ya (Mwenyezi Mungu yaliyo katika Taurati na Injili) na mahali pake. Na wameacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa…** ﴾ Al-Maidah 12 – 13. Na kusahau ni binadamu kuacha kudhibiti kile kilichohifadhiwa ima kwa udhaifu wa moyo wake, au kwa kughafilika au kwa kukusudia hadi hicho kitu kinafutika kukumbukwa moyoni (Ameyaeleza haya Raaghibu katika Mufradaatu Alquran uk 803). Na mwenye Attahriiru Wattanwiiru amesema (6 / 144): na kusahau makusudio yake ni kupuuzia/kuzembea kunakopelekea kusahau mara nyingi. Kwa hakika aya hii imejumuisha ushahidi wa uchache wa kuifuata kwao dini. Na udhaifu wao wa kufuata misingi mitatu nayo ni: Kufanya makusudi kutengua waliyoahidiana kuyatekeleza. Na kudanganyika na tafsiri potofu wazitoazo. Na kusahau kulikotokana na uchache wa

kushikamana na dini na uchache wa kuitilia umuhimu dini. أ – هـ … Kisha Allah Mtukufu Aliyetukuka akawataja Wakristo na hali yao pamoja na kitabu chao pale Allah Mtukufu Aliyetukuka aliposema: ﴿**Na kwa wale waliosema: ''Sisi ni Wakristo,'' tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa, kwa hivyo tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka siku ya Kiama. Na Mwenyezi Mungu atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.** ﴾ Al-Maidah 14. Sheikh Rushdu Ridhwaa amesema katika Almanaari 6 / 287: Pale Allah Mtukufu alipobainisha mafunzo ya Wayahudi kutengua ahadi yao, na kile kilichowatokea, alifuatisha kwa kubainisha hali ya Wakristo katika suala hilo kwa kusema: ﴿**Na kwa wale waliosema: ''Sisi ni Wakristo,'' tulichukua ahadi kwao, lakini wakaacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa…** ﴾ Al-Maidah 14. Yaani na hivyo hivyo tulichukua ahadi kwa wale ambao wao wenyewe wamejiita Wakristo miongoni mwa wale waliopewa Kitabu cha Kwanza. Nao ndio wale ambao walisema kwa hakika wao ni wafuasi wa Masihi Issa na wao ndio watetezi wake … nao wakatengua ahadi yao na wakasahau hadhi na sehemu ya kile walichokumbushwa kupitia kwa ulimi wa Masihi Issa mwana wa Maryamu. Kama walivyofanya wale waliokuwa kabla yao. ﴿**… kwa hivyo tukaweka baina yao (wenyewe kwa wenyewe) uadui na bughudha mpaka siku ya Kiama…** ﴾ Al-Maidah 14. Kwa hiyo kusahau sehemu kubwa ya kitabu chao ndio ikawa sababu ya kutumbukia kwao katika matamanio ya nafsi zao na kufarikiana katika dini. أ – هـ [kwa ufupisho kidogo].

Na jambo la kuchekesha katika yanayohusiana na aya hii ni kile kilichopokelewa na Alqurtubiyyu katika Tafsiri yake 10 / 5 kwa mapokezi yake mpaka kwa Yahya Bin Akthamu amesema: Maamuni alikuwa na kikao cha kutazama mambo. Katika jumla ya watu walioingia, aliingia myahudi mmoja aliyevaa nguo nzuri, ana sura nzuri na harufu nzuri akaongea maneno na vifungu vizuri. Na kikao kilipoisha, Maamuni alimwita huyo myahudi na kumwambia: Wewe ni muisraili? Akajibu: ndio. Akamwambia: Tafadhali silimu ili nikufanyie hili na hili, na akamuahidi mambo kadhaa. Myahudi akasema: Nabaki na dini yangu dini ya baba zangu! Kisha akaondoka. Na baada ya mwaka mmoja alitujia akiwa muislamu. Na akazungumzia sheria za Kiislamu kwa uzuri sana. Na kikao kilipoisha, Maamuuni alimwita na kumwambia: Je, wewe sio yule swahiba wetu myahudi wa mwaka jana? Akajibu: hapana, kwa kweli ndio mimi. Akamuuliza: sababu ya kusilimu kwako ni ipi? Akasema: nilipoondoka kutoka mbele yako nilipenda kuzijaribu dini. Nami kama unavyoniona nina mwandiko mzuri. Nikaikusudia Taurati na nikaiandika nakala tatu nikizidisha ndani yake na kupunguza, na kuiingiza katika sinagogi, nao wakainunua bila kung`amua. Na nikaikusudia Injili, na nikaiandika nakala tatu nikizidisha ndani yake na kupunguza, na kuiingiza kanisani, nao wakainunua bila kung`amua. Na nikaikusudia Quran na nikaiandika nakala tatu nikizidisha ndani yake na kupunguza, na kuiingiza wanapouza vitabu vya Kiislamu, nao wakaipekua kurasa zake. Na walipoiona kuwa imeongezwa na sehemu nyingine imepunguzwa waliitupa na hawakuinunua. Nikajua kuwa Kitabu hiki (Quran) kimehifadhiwa na hii ndio ikawa sababu ya kusilimu kwangu.

Na kisa hiki kiliposimuliwa kwa Sufiani bin Uyaina Allah amrehemu alisema: hili limesadikishwa katika Kitabu cha Allah Mtukufu Aliyetukuka katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka kuhusu Taurati na Injili: ﴿**… kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu;…** ﴾ Al-Maidah 44. Akaweka jukumu la kukihifadhi liwe juu yao, kikapotea. [Na inaonekana kuwa Allah amewasifu kuwa wao walitakiwa wakihifadhi na hakuwaambia wao kuwa wamekihifadhi] na Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka amesema: ﴿**Hakika Sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Quran); na hakika Sisi ndio tutakayoyalinda.** ﴾ Al-

siri ya huku kutofautisha ni kuwa vitabu vingine vya mbinguni vimeletwa kwa muda maalum[1] na si kwa muda wote[2]. Kwa hakika Quran imeletwa ikiwa ni msadikishaji wa vitabu vilivyopita na yale yaliyomo ndani yake. Kwa hiyo chenyewe kinakusanya yaliyomo katika vitabu hivyo miongoni mwa mambo ya hakika yaliyothibiti. Pia kikizidisha yale ambayo Mwenyezi Mungu aliyapenda kuyazidisha. Kwa hiyo kimekuwa kikamilishi kilichokamilisha vitabu vilivyopita, kwani hakukuwa na kitu kingine cha kuvikamilisha. Kwa hivyo Allah ameamua kuwa kitabu hiki kiwe hoja mpaka kiama kitakaposimama. Na Allah anapoamua jambo analirahisishia visababishi vyake. Na yeye ndiye Mwingi wa hekima na Mwingi wa Ujuzi.

### [Je, inawezekana kueleza fasili (maana) ya Quran kimantiki?]

Kwa kuwa Quran kwa sehemu na uhakika wake ina maana hii tukufu, haiwezekani kueleza sifa zake bainifu kwa fasili ya kimantiki yenye jinsi (genus), aina na namna yake ya kipekee. Na hali hii hii ndio hali ya kila visehemu vya hakika, kwani vyenyewe haviendani na ufahamu wa visehemu. Kwa kuwa yenyewe inakubali kuendana na kila kile kinachochukuliwa kuwa kinafanana nacho katika sifa zake akilini, hata kama kitu hicho hakipo katika uhalisia. Kwa hiyo sifa hizo haziwi sifa bainifu kwa kitu hicho pekee na kuvitoa vitu vingine. Kwa hiyo fasili hiyo haitakuwa fasili sahihi ya kitu hicho peke yake.

Kwa hiyo sehemu hupewa fasili kwa kuiashiria kwa ishara iliyopo katika hisia, au iliyozoeleka akilini. Ukitaka kutoa fasili ya Quran kwa fasili yenye sifa bainifu, huna njia ya kufanya hivyo ila kwa kuiashiria (kuionesha) kwa kueleza yaliyoandikwa katika msahafu au yanayosomwa ulimini, kwa

---

Hijr 9. Hivyo Allah Mtukufu Aliyetukuka akatuhifadhia Kitabu chetu na hakikupotea. أ
هـ – kwa ufupi kidogo.

Hayo, na atakayeitafakari vizuri aya hii ya suratul Al-Hijri kisha akaitafakari kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Suratul Al-**Qiyamah ﴿Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha﴾**. Al-Qiyama 17. Kisha atafakari tena kauli ya Mtukufu Aliyetukuka katika suratul Al-Aalaa ﴿**Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau** ﴾ Al-Aalaa 6. Atakuta kuwa jukumu la kuilinda, kuikusanya na kuisomesha analisimamia mwenyewe Allah Mtukufu Aliyetukuka. Mamia kisha maelfu kisha mamilioni ya watu, wote hao wameihifadhi Quran vifuani. Pia Allah Mtukufu ameuhifadhia umma huu baadhi ya nakala za Misahafu iliyoandikwa zama za Maswahaba wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. kwa hiyo jamani, hivi kuna kuhifadhiwa gani kulikotimilifu zaidi na bora zaidi kuliko kuhifadhiwa huku na Mola Mlezi, kukihifadhi kitabu hiki bora na cha mwisho.

[1] Kwa muda: ni wakati maalum uliowekewa kitu fulani.

[2] Kwa muda wote: Kuwa milele daima dumu.

hiyo utasema: Quran ni jumla ya yale yaliyomo baina ya haya majalada mawili. Au useme Quran ni: ﴿**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu. Shukran zote anastahiki Mwenyezi Mungu... Mpaka: … (Ambaye ni) katika majini na watu** ﴾.

Ama fasili zilizotajwa na wanazuoni zinazoeleza kwa jinsi, namna na sifa bainifu, kama vinavyofasiliwa vitu kamili vya hakika. Kwa hakika wanazuoni hao walikusudia kukaribisha maana ya Quran na kuipambanua na vitu vingine vinavyoshirikiana nayo kwa jina hata kama kwa dhana tu. Na hilo ni kwa vile vitabu vingine vyote vilivyotoka kwa Allah na hadithi Qudusi na baadhi ya hadithi za Mtume zinashirikiana na Quran kwa kuwa zenyewe nazo ni ufunuo kutoka kwa Allah. Na huenda mwenye kudhani akadhani kuwa vitu hivyo pia vinashirikiana na Quran katika jina la visomwa. Kwa hiyo hao wanazuoni wakataka kubainisha kuwa jina hilo linahusika na Quran tu kwa kubainisha sifa zake bainifu zilizojipambanua nazo kinyume na aina hizo nyingine. Wakasema:

***(Quran ni maneno ya Allah Mtukufu, yaliyoteremshwa kwa Muhammad rehema na Amani ziwe juu yake, na kuisoma ni kufanya ibada).***

**[Vipengele muhimu katika fasili hii mashuhuri ya Quran]**

**(*Maneno)*** ni jinsi (genus) inajumuisha kila aina ya maneno. Na kule kuunganishwa kwake na (Allah) huko ni kuyapambanua na maneno mengine ya asiyekuwa Allah. Sawa sawa yawe ya mwanadamu, jinni au malaika.

Na (***yaliyoteremshwa)*** neno hili linaondoa yale maneno ya Mungu aliyobaki nayo Mwenyewe, au aliyowaambia malaika wakayafundisha bila ya kuyateremsha kwa yeyote miongoni mwa wanadamu; kwa kuwa sio maneno yote ya Allah Mtukufu yameteremshwa. Bali aliyoyateremsha ni machache tu katika maneno yake mengi. ﴿**Sema: ‘‘Hata bahari ingalikuwa ndio wino kwa (kuyaandika) maneno ya Mola wangu, basi bahari ingalikwisha kabla ya kwisha maneno ya Mola wangu, hata kama Tungalileta (bahari) kama hiyo kuongezea.’’** ﴾ Al-Kahf 109. ﴿**Na lau kama miti yote iliyomo katika ardhi ingalikuwa kalamu, na bahari hii (ikafanywa wino), na ikasaidiwa na (kuongezewa maji) na bahari nyingine saba, maneno ya Mwenyezi Mungu yasingelikwisha. Bila**

**shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.** ﴿ Luqman 27.

Na neno iliyoteremshwa ***(kwa Muhammadi)*** linamaanisha kuyaondoa yale yaliyoteremshwa kwa manabii wa kabla yake, kama Torati iliyoteremshwa kwa Musa. Na Injili iliyoteremshwa kwa Issa, na Zaburi iliyoteremshwa kwa Daudi, na Kurasa zilizoteremshwa kwa Ibrahimu Amani iwe juu yao wote.

Na kizuizi cha (***na kuisoma ni kufanya ibada****)* – kinamaanisha kuwa imeamrishwa kuisoma Quran katika swala na sehemu nyingine za kiibada – kizuizi hiki kinatoa yale maneno ambayo hatujaamrishwa kuyasoma katika ibada hizo. Kama visomo vilivyonukuliwa kwa njia ya mtu mmoja mmoja. Na hadithi Qudusi; nazo ni zile zilizoegemezwa kwa Allah Mtukufu, hata kama tutazisema kuwa zenyewe ni zile zilizoteremshwa kutoka kwa Allah kwa matamshi yake.

[**Kutofautisha baina ya Quran,**

**Hadithi Nabawiyyu na Hadithi Qudusiyyu**]

Ama hadithi Nabawiyyu, kwa hakika zenyewe kwa kigezo cha kuzingatia maana zake, zinagawanyika vigawo viwili:

- (Kigawo cha kuwafikishwa) hadithi hizi ni ung`amuzi wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kwa ufahamu wake wa maneno ya Allah au tafakuri zake juu ya uhakika wa ulimwengu. Na kigawo hiki si maneno ya Allah kabisa kabisa.
- Na (kigawo cha kupokea) Mtume rehema na amani ziwe juu yake, ameyapokea madhumuni yake kutoka katika ufunuo kisha yeye akawabainishia watu kwa kutumia maneno yake. Na kigawo hiki, hata kama ndani yake kuna elimu iliyoegemezwa kwa mwalimu wa wake na mfunuliaji wake ambaye ni Allah Mtukufu. Lakini yenyewe – kwa upande wa kuwa ni maneno – yanahusika zaidi yakiegemezwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Kwa sababu maneno hunasibishwa na yule aliyeyaweka na kuyasema. Aliyoyapangilia kwa mpango maalum hata kama ndani yake kuna maana zilizopokelewa na hisia, na huyo msemaji wa mwisho amezipata maana hizo kutoka kwa wa kwanza. Kwa hiyo hadithi Nabawiyyu kwa

vigawo vyake vyote viwili, zipo nje na zimetolewa na hiki kizuizi cha kwanza[1] katika fasili hii ya Quran.

Na hivyo hivyo, hadithi Qudusiyyu, hata kama tutasema kuwa zenyewe zimeteremshwa kwa maana yake tu. Na hii, kwa upande wetu, ndio kauli dhahiri/yenye nguvu kabisa kati ya kauli mbili juu ya hadithi hizi. Kwa sababu lau kama zenyewe nazo zingeliteremshwa kwa matamko yake, basi zingekuwa zina utukufu na kulindwa, kwa mtazamo wa kisheria sawa sawa na mfumo wa Quran. Kwa kuwa hakuna namna ya kutofautisha baina ya matamko mawili yaliyoteremshwa kutoka kwa Allah. Kwa hiyo lingelazimisha uwajibu wa kuyahifadhi maandiko yake, na isiruhusiwe kuipokea kwa maana kwa makubaliano ya wanazuoni. Na iwe haramu kwa mwenye hadathi kugusa kurasa zake. Na hakuna aliyesema hayo yote. Na vile vile, kwa hakika Quran, ilivyokuwa makusudio yake, pamoja na kuyafanyia kazi madhumuni yake, ni kitu kingine nacho ni kutoa changamoto kwa muundo/mtindo wake, na kuabudu kwa kuisoma. Ikahitaji iteremshwe kwa tamko lake. Na hadithi Qudusiyyu haikuteremshwa kwa lengo la kutoa changamoto wala kuabudu kwa kuisoma bali yenyewe imeteremshwa kwa lengo la kuifanyia kazi tu yale yaliyomo ndani yake.

Na faida hii inapatikana kwa kuteremsha maana yake tu. Kwa hiyo kauli ya kusema kuwa hadithi Qudusiyyu imeteremshwa kwa tamko lake ni kauli ambayo ndani yake kuna kitu fulani kisicho na haja katika kuiangalia kwa uchunguzi. Na hakuna ushahidi wa kisheria juu ya hilo. Zaidi ya kile kinachoweza kuonekana kuwa ni kiashiria tu. Nacho ni kule kuiegemeza hadithi Qudusiyyu kwa Allah kwa muundo huu (Allah Mtukufu Aliyetukuka anasema kadha kadha). Lakini vithibitisho tulivyovitaja hivi punde vinatosha kuweka wazi uwanja huu na kuyafasili maneno hayo kwa kueleza kuwa makusudio yake ni kuegemeza madhumuni tu na sio matamko yake. Na fasili hii imeenea sana katika Kiarabu. Kwa mfano unaweza kusema pale unapoelezea beti ya kishairi kwa lugha ya mjazo (mshairi anasema kadha kadhaa). Na unasema pale unapotafsiri aya kutoka katika Kitabu cha Allah kwa maneno kutoka kwako: (Allah Mtukufu anasema kadha kadha). Na kwa kanuni hii hii, Allah Mtukufu amesimulia kuhusu Musa na Firauni na wengineo kwa kueleza madhumuni ya maneno yao kwa matamko yasiyo matamko yao. Na mitindo/miundo usiyo mitindo/miundo yao na hayo yamenasibishwa kwao.

---

[1] Nayo ni maneno kuwa ni maneno ya Allah [Daraazu].

Kama utadai eti kama katika hadithi Qudusiyyu kusingekuwa na kitu kingine kitukufu zaidi ya maana. Ingekuwa sahihi kwetu kuziita baadhi ya hadithi Nabawiyyu kuwa nazo pia ni hadithi Qudusiyyu. Kwa kuwa nazo zina maana hiyo hiyo. Basi jibu la kauli hii ni kuwa sisi tulipokata kauli kuwa hadithi Qudusiyyu kuwa zimeteremka kwa maana yake kwa kuwa kuna andiko la kisheria inayozinasibisha kwa Allah. Kwa kauli yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake: (**Allah Mtukufu amesema kuwa**) kwa ajili hiyo ndio tumeiita hadithi Qudusiyyu, na hii ni kinyume na hadithi Nabawiyyu, kwani zenyewe hazina andiko kama hili. Ndio inajuzu kwa kila moja kati ya hizo kuwa maana yake yamefundishwa kwa ufunuo na kung`amuliwa kwa jitihada na rai. Na kwa hiyo zote zikaitwa hadithi Nabawiyyu kwa ajili ya kusimamia katika jina kwa mujibu ya mipaka ya fasili iliyokatwa. Na lau kama tungalikuwa na alama zinazotutofautishia baina ya kigawo cha ufunuo na kingine; basi nazo pia tungeziita hadithi Qudusiyyu.

Upambanuzi huu hauleti matokeo yoyote ya kiutendaji. Kwa hiyo ni sawa sawa kwetu tutakapoifanyia kazi hadithi yoyote iwe ya kigawo hiki au kile. Kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake katika ufikishaji wake, yeye ni mkweli mwaminifu. Na katika jitihada zake yeye ni mwerevu mwenye kuwafikishwa. Na Roho Mtakatifu anampa nguvu kwa hiyo hamkubalii makosa kama atakosea katika jambo miongoni mwa mambo ya kisheria. Kwa hiyo, marejeo ya mambo yote, kwa hakika ni kwa ufunuo katika hali zote mbili. Ima kwa kuanza na kufundishwa au ima kwa kukubaliwa au kwa kufutwa mwishoni. Na kwa ajili hiyo, ni wajibu kwetu kuzipokea sunna zake zote kwa kuzikubali ﴿**… Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho…** ﴾ Al-Hashr 7.

﴿**Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao…** ﴾ Al-Ahzab 36.

۞ ۞ ۞

## UTAFITI WA PILI

## KATIKA KUBAINISHA CHANZO CHA QURAN

## NA KUTHIBITISHA KUWA YENYEWE INATOKA KWA ALLAH KWA TAMKO LAKE NA MAANA YAKE.

[**Kuanisha Madai Haya Kwa Kuchukua Maandiko Ya Quran**]

Kwa ujuzi usiochanganyika na shaka, watu wote wameshajua kuwa kitabu hiki kitukufu, kimekuja kupitia ulimi wa Mwarabu asiyejua kusoma na kuandika, aliyezaliwa Makka katika karne ya sita AD. Jina lake ni Muhammad bin Abdullah bin Abdulmuttwalibi. Rehema na amani ziwe juu yake na aali zake... Kwa kiasi hiki, kwa hakika hakuna kuhitilafiana baina ya muumini na asiyeamini. Kwa sababu ushahidi wa kihistoria uliotufikia kutoka kwa wasimulizi wengi haufanani wala haukaribibiwi na ushahidi wa kitabu kingine wala tukio lingine lililodhihiri katika mgongo wa ardhi.

Ama baada ya hayo. Hivi Muhammad bin Abdullah rehema na amani ziwe juu yake na aali zake amekitoa wapi kitabu hiki? Je, kutoka nafsini mwake na ufunuo wa dhamira yake, au kutoka kwa mwalimu? Ni nani huyo mwalimu?

Tukisome katika kitabu hiki hiki, kwa hakika chenyewe sio kutokana na matendo ya swahiba wake. Bali chenyewe ni kauli ya mjumbe mtukufu, mwneye nguvu, mwenye cheo cha heshima kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi. Anayetiiwa, tena ni mwaminifu: huyo kwenu nyinyi, ndio Jibrilu amani iwe juu yake. Ameipokea kutoka kwa Mwenye hikima na Mjuzi. Kisha akaiteremsha kwa lugha ya Kiarabu iliyo wazi, katika moyo wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na aali zake. Naye Muhammad rehema na amani ziwe juu yake akasomewa kutoka kwake kama anavyosomewa mwanafunzi na mwalimu wake, andiko kwa andiko kutika maandiko hayo. Naye hakuwa na kazi yoyote katika hiyo Quran, baada ya kusomewa isipokuwa:

(1) Kuizingatia na kuihifadhi, kisha
(2) Kuisimulia na kuifikisha, kisha
(3) Kuibainisha na kuifasiri, kisha
(4) Kuifanyiakazi na kuitekeleza.

Ama kubuni maana zake na kuunda jengo lake, kwa hayo, yeye hakuwa na njia ya kuyafanya. Na kwa mambo mawili hayo, Mtume hakuwa na lolote. Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi (ufunuo), uliofunuliwa (kwake).

Na hivyo hivyo ndivyo Quran ilivyojiita, pale inaposema: ﴿**Na usipowaletea Aya (wazitakazo) husema: ‘‘Kwa nini huzizui (mwenyewe)?’’ Sema: ‘‘Nayafuata yaliyofunuliwa kwangu (nilioletewa wahyi) kutoka kwa Mola wangu (sizui mwenyewe)…** ﴾ Al-Aaraf 203. Na inasema: ﴿**… Sema: ‘‘Siwezi kuibadilisha kwa khiari ya nafsi yangu; sifuati ila yanayofunuliwa kwangu (ninayoletewa wahyi)…** ﴾ Yunus 15. Na mifano ya maandiko kama haya ni mingi katika jambo la kuashiria maana yake. Kisha inasema kuhusiana na jambo la kuashiria matamko yake: ﴿**Hakika sisi tumeiteremsha Quran kwa Kiarabu ili mpate kufahamu** ﴾**.** Yusuf 2. ﴿**Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau** ﴾**.** A`laa 6. ﴿**Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka. Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu). Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha). Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha (kukubainishia** ﴾**.**[1] Al-Qiyama 16 – 19. ﴿**Soma…** ﴾ Alaq 1. ﴿**Na usome…** ﴾

---

[1] Kutoka kwa Ibnu Abbas, kuhusiana na kauli hii ya Allah Mtukufu: ﴿**Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka** ﴾**.** Amesema: ‘‘Jibrilu alipoteremsha ufunuo kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, Mtume alikuwa ni mwenye kuutikisa ulimi wake na midomo yake, na jambo hili likimuwia vigumu. Na alikuwa akijulikana na hali hiyo. Ndipo Allah akateremsha aya iliyopo katika ﴿**Naapa kwa siku ya Kiama** ﴾**:** ﴿**Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka. Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu). Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha** ﴾**.** Akasema: Ni juu yetu kuukusanya kifuani kwako na kukusomea. ﴿**Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake** ﴾**.** Na tunapoiteremsha isikilize. ﴿**Kisha ni juu yetu kuubainisha (kukubainishia** ﴾**.** Ni juu yetu kuibainisha kwa ulimi wako. Akasema: ikawa pindi anapojiwa na Jibrilu anakaa kimya, na akiondoka anaisoma kama alivyoahidiwa na Allah’’. Muttafaqu Alaihi: Albukhariyu ameipokea katika Attafsiiri 4929 na tamko hili ni lake. Na kwa Muslimu katika Aswalaati 147. Na Al-Haafidhu Ibnu Kathiiri amesema katika tafsiri yake 8/303:

Haya ni mafunzo kutoka kwa Allah Mtukufu Aliyetukuka kwenda Mtume wake rehema na Amani ziwe juu yake, juu ya namna ya kuupokea ufunuo kutoka kwa Malaika. Kwa hakika Mtume alikuwa anaharakisha kuuchukua na kushindana na Malaika katika kuusoma. Ndipo Allah Mtukufu Aliyetukuka akamwamrisha kuwa pindi unapojiwa na Malaika na ufunuo anatakiwa amsikilize. Na Allah amedhamini kuwa ataukusanya katuka kifua chake, na atamfanyia wepesi kuutekeleza kwa namna aliyompa. Na atambainishia na kumfasiria na kuuweka wazi:

Kwa hali ya kwanza: kuukusanya katika kifua chake.
Na ya pili: kumsomea/kumsomesha/

Al-Kahf 27. ﴿**… na soma Quran …** ﴾ Muzzammil 4. Tazama uzuri namna ilivyoelezwa kwa kutumia maneno: soma, wasomee, isome vizuri, tikisa ulimi wako, na kwamba maneno haya ni ya Kiarabu. Yote hayo ni matukio ya matamshi na si matukio ya kimaana tupu.

Kwa hiyo, Quran ipo wazi kuwa yenyewe ***(haihusiani na ufundi wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. wala ufundi wa yeyote katika viumbe. Kwa hakika yenyewe imeteremshwa kutoka kwa Allah kwa matamko yake na maana yake).***

Cha kushangaza ni kuwa baadhi ya watu wamesalia bado wanahitaji ushahidi juu ya nusu ya kwanza ya maswala haya. Nayo ni kuwa Quran haitoki kwa Muhammad.

[**Kujiepusha kwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na kujinasibisha na Quran. Haya si madai yanayohitaji ushahidi bali yenyewe ni kukiri kunakomtia hatiani mwenye kufanya hivyo**]

Kwa haki kabisa, kwa hakika suala hili, kama kungalikuwapo na jaji anayehukumu kwa uadilifu, asiyetosheka na kusikia ushuhuda huu uliokuja

---

Na ya tatu: kumfasiria, na kumwekea wazi maana yake.

Na kwa ajili hii amesema: ﴿**Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka** ﴾**.** Yaani Quran… Kisha akasema ﴿**Ni juu yetu kuukusanya** ﴾ yaani kifuani mwako. Na ﴿**Kukusomea** ﴾ yaani kukusomesha. ﴿**Na tukikusomesha** ﴾ Yaani Malaika kutoka kwa Allah Mtukufu Aliyetukuka atakapokusomea ﴿**Basi ifuate Quran** ﴾ Yaani isikilize kisha isome kama alivyokusomea. ﴿**Kisha ni juu yetu kuibainisha** ﴾ Yaani baada ya kuihifadhi na kuisoma tutakubainishia na kukuwekea wazi. Na tutakupa ilhamu ya kujua maana yake kwa kile tulichokitaka na kile tunachokiweka kuwa cha kisheria. أهـ.

Na mwanazuoni bobezi Twahiru Ibnu Aashuri katika Tafsiri yake ya aya hii 29 / 350 amesema:

Na kile ambacho kinapita akilini mwangu kuhusiana na kuwepo kwa aya hii sehemu hii, bila ya kuwepo sehemu nyingine zilizotangulia kuteremka kabla ya kuteremka sura hii miongoni mwa sura za Quran ni kwamba: Sura za Quran zilipokuwa chache, Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa haogopi kuponyokwa na baadhi ya aya. Lakini sura zilipokuwa nyinyi na kufikia takribani thelethini – kulingana na alivyozihesabu Said Bin Jubair katika mpangilio wa kuteremka kwa sura – Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawa anaogopea kusahau baadhi ya aya. Huenda Mtume rehema na amani ziwe juu yake akaanza kuutikisa ulimi wake kwa matamko ya Quran ilipokuwa ikiteremka kwa ajili ya kuchukua tahadhari na aweze kuihifadhi vizuri. Na hayo yanatokana na pupa yake ya kufikisha kile alichokiteremsha Allah kama kilivyo. Na pale Allah alipompa dhamana ya kuihifadhi Quran, alimwamrisha asijikalifishe kwa kutikisa ulimi. Hivyo hili katazo la kutotikisa ulimi wake ni katazo la kumuhurumia na kumfanyia upole kwa kile alichokuwa akikipata katika suala hilo miongoni mwa taabu, أهـ .

kwa ulimi wa mwenye kuutoa dhidi ya nafsi yake. Na baada ya ushuhuda huu hakutaka kuwepo kwa ushahidi wa shahidi mwingine, wa kiakili au wa kunukuu. Na hilo kwa kuwa wenyewe si ushahidi wa namna ya (kimadai) kwa hiyo ukahitaji vithibitisho. Kwa hakika wenyewe ni ushahidi wa aina ya (kukiri). Ushuhuda ambao kwa sababu yake anaadhibiwa nao mwenye kuutoa. Wala hautegemei rafiki wala adui katika kuukubali. Hivi kuna maslahi gani kwa mwenye akili anayejidai kwa nafasi yake kuwa yeye ni mkuu na kutoa changamoto kwa watu kwa kuonesha mambo ya ajabu na miujiza ili kukazia hayo madai yake ya ukuu. Tunasema, hivi ana maslahi gani pale anapoinasibisha bidhaa yake kwa mwingine? Na anajivua nayo kabisa kabisa? Wakati ambapo anaweza kujinasibisha nayo na kujiongezea utukufu na ukubwa? Na lau kama angejinasibisha nayo kusingekuwa na mtu yeyote anayempinga na kisha huyo mtu akadai kuwa bidhaa hiyo ni yake yeye mwenyewe.

Kile tunachokijua ni kuwa wanafasihi wengi wanapitia athari za wengine na kuziiba au wanaiba kile kinachokuwa chepesi kukibeba na thamani yake ni ghali, na kimesalimika na kutuhumiwa. Imefika mpaka, miongoni mwao yupo anayefukua makaburi ya maiti na kuvaa sanda zao na kujitokeza kwa watu wake akiwa amevaa nguo hizo za kuazima. Ama atokee mmoja wao na kunasibisha athari bora zaidi ya akili yake au kitu ghali kabisa kilichotolewa na uwezo wake kwa mtu mwingine, kwa hakika hili bado halijawahi kuzaliwa kwa zama zote.

### [Muhammad kuiegemeza Quran kwa Allah haiwezekani kuwa ni hila zake ili akunjue makucha yake. Na kama si hivyo, kwa nini hakuzinasibisha kauli zake zote kwa Allah]

Lau sisi tukichukulia kwamba, pale tulipojua kuwa Muhammad ana sababu za msingi, wala sio za kufananafanana na za msingi, ila kwa kweli kuna kitu kimoja ambacho kinaleta ukakasi katika moyo wa asiyejua. Nacho ni kuwa kiongozi huyu mkuu ameonelea kuwa (kuiegemeza Quran kwa ufunuo wa Mungu) atapata kitakachomsaidia katika kuwarekebisha watu, kwa kuwa watu watamwitika na kumtii na hivyo yeye atatekeleza jambo lake kwao wao. Kwa sababu unasibishaji huo utaifanya kauli yake iwe takatifu na tukufu, jambo ambalo hatolipata endapo atainasibisha kwa nafsi yake.

Mlinganisho huu wenyewe ni batili. Umeharibika katika msingi wake.

Ama, kuwa wenyewe ni batili katika dhati yake, hilo ni kwa sababu mwenye Quran hii ameshatoa maneno ya kuyanasibisha katika nafsi yake na maneno yanayonasibishwa kwa Allah Mtukufu. Kwa hiyo kile alichokinasibisha kwa nafsi yake hakina upungufu hata kidogo kwa upande wa kulazimika kumtii. Na wala kule kunasibisha kwa Mola wake, kwa kile alichokinasibisha kuwa eti kinamuongezea chochote. Bali ni lazima kwa watu kumtii katika yote hayo mawili kwa sawa sawa.[1] Kwa hiyo mawili hayo yakawa ni matukufu katika nafsi za watu kwa sawa sawa. Na kumtii kukawa ndio kumtii Allah. Na kumuasi ndio kumuasi Allah. Sasa iweje azifanye kauli zake zote ziwe ni miongoni mwa maneno ya Allah Mtukufu. Lau ingekuwa kama yanavyotokota katika ufahamu wao mbaya.

Ama uharibikaji wa mlinganyo huu katika msingi wake. Ni kwa kuwa wenyewe umejengewa kwa dhana batili. Nayo ni kuruhusu kwa kiongozi huyu mkuu kuwa miongoni mwa wale ambao wakiwa katika kufikia lengo la kutengeneza, hawaogopi kueleza mipango yao kwa njia za uongo na kupotosha. Na jambo hilo linakataliwa kabisa kabisa na uhalisia wa

---

[1] Imamu Shafii katika kitabu chake (Alrisala) uk 82:

Mlango: Yale aliyoamrisha Allah miongoni mwa kumtii Mtume wa Allah: Allah Aliyetukuka kwa sifa zake amesema ﴿**Bila shaka wale wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi (hizi) anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa** ﴾. Al-Fath 10. Na amesema ﴿**Mwenye kumtii Mtume amemtii Mwenyezi Mungu….** ﴾ An-Nisaa 80. Amewajulissha kuwa kufungamana kwao na Mtume wake ndio kufungamana naye. Na hivyo hivyo amewajulisha kuwa kumtii Mtume ndio kumtii Yeye. أ هـ

- Nikasema: Na hivyo hivyo katika mapito ya Quran yote, utakuta aya za wazi wazi zinazowajibisha kumtii Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kwa mfano:

﴿**…. Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho…** ﴾ Al-Hashri 7. ﴿**Sema: ‘‘Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni; (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu…** ﴾ Aali Imran 31. ﴿**Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa** ﴾. Al-Ahzab 36. ﴿**Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa** ﴾**.** Aali Imran 132. Pia Allah Mtukufu amewawajibisha waumini wazifuate hukumu za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, katika kila kuhitilafiana. Na katika vifua vyao kusiwe na kukereka kwa aina yoyote ile, wala wasikipinge kile atakachokihukumu Mtume. Na hili ni katika mambo ya lazima ya imani. Allah Mtukufu amesema ﴿**Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa**﴾. An-Nisaa 65.

kihistoria. Kwani atakayefuatilia historia yake tukufu, katika harakati zake, utulivu wake, ibara zake, ishara zake, kuridhia kwake, ghadhabu zake, akiwa mpweke na akiwa na watu[1] hatokuwa na shaka yoyote ya kwamba yeye alikuwa ni mtu asiye na unafiki wala kuwapaka watu mafuta kwa mgongo wa chupa na kuficha uadui[2].

Na kwamba usiri wake na uwazi wake vilikuwa ni sawa sawa katika ukweli kabisa na uwazi wa haki, katika mambo matukufu na mambo ya kubezwa. Na kwamba, hayo yalikuwa katika mambo yake ya kipekee na sifa zake za dhahiri kabla ya kupewa utume na baada ya kupewa.[3] Kama

---

[1] Akiwa na watu: Akiwa mbele za watu wazi wazi.

[2] Kupaka watu mafuta kwa mgongo wa chupa: unafiki na kuficha uadui.

[3] Na lau Muhammad bin Abdullah angalikuwa anajulikana kuwa ameongopa walau mara moja katika maisha yake, basi maadui zake wasingemshuhudilia kwa yafuatayo:

(a) Annadhru bin Al-Haarith (alikuwa miongoni mwa mashetani wa Kikuraishi na mkali wao dhidi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake) alisema: ''Enyi makongamano ya Makuraishi. Hakika mambo yalivyo, nakuapieni kwa Mungu, limekujieni jambo ambalo mimi mwenyewe bado sijakujieni na ujanja wowote ule. Muhamad alikuwa kijana mdogo kwenu: mwenye kuridhiwa sana kwenu. Na mwenye kuongea ukweli zaidi kulko ninyi na mwaminika mkubwa kati yenu. Hadi mnapomuona mvi katika masharafa yake [masharafa: nywele za baina ya sikio na jicho]. Na amekujieni na kile alichokujieni nacho mkasema yeye ni mchawi .. Kuhani .. Mshairi .. Chizi .. Naapa kwa Mungu hayo sio … Enyi makongamano ya Mauraishi. Hebu tazameni mambo yenu, kwa hakika limekujieni jambo kubwa''. Historia ya Mtume: ya Ibnu Hishamu 1 / 327.

(b) Utubah bin Rabiah (alipowahutubia Makuraishi baada ya kutuhumiwa kuwa anaegemea upande wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake) alisema: ''Nilimwendea [yaani Mtume] ... naapa kwa Mungu, alinijibu kwa majibu ambayo kwa hakika si ya uchawi wala shairi wala ukuhani. Alisoma ﴾ **Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Haa Mym. Uteremsho (huu) umetoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu… ﴿.** Hadi akafikia ﴾**Basi kama wakipuuza sema ''Nakuhadharisheni adhabu mfano wa adhabu, (inayoshabihi adhabu) ya Adi na Thamudi.''** ﴿ nikauzuia mdomo wake [yaani mdomo wa Nabii rehema na amani ziwe juu yake] na nikamsihi kwa udugu wetu aache habari hizo. Na kwa hakika mmeshajua kuwa Muhammad anaposema kitu haongopi. Nikaogopea isikuteremkieni adhabu''. Mtiririko huu, Suyutwi katika Adduraru Almanthuuru 5 / 673, ameuegemeza kwa Al-Baihaqiyu katika Addalaailu na kwa Ibnu Asaakiru.

(c) Abuu Jahli Amru Bin Hishamu:

Kutoka kwa Abuu Maysarati amesema: ''Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipita kwa Abuu Jahli naye akasema: Naapa kwa Mungu, ewe Muhammad, sisi hatukuoni kuwa ni muongo, kwa hakika wewe kwetu sisi ni mkweli. Lakini sisi, tunakuona muongo kwa yale uliokuja nayo. Ndipo Allah akateremsha ﴾**… Basi wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu hao wanakanusha hoja za Mwenyezi Mungu**﴿**.** Al-An-am 33. Tamko hili, Suyutwi katika Adduraru Almanthuuru 3 / 18, ameliegemeza kwa Abdu Ibnu Hamid, Ibnu Almundhiru na Ibnu Mardawayhi Asaakiru. Na limepokelewa na Tirmidhiyu kutoka kwa Aliyu 3064 kwa mfano wake.

(d) Abuu Jahli Amru Bin Hishamu:

alivyoshuhudiwa na marafiki zake na maadui zake[1] mpaka leo hii ﴿**Sema: ''Kama Mwenyezi Mungu angalitaka nisingalikusomeeni hii (Quran),**

---

**''Ilipokuwa siku ya vita vya Badri, Al-Akhnasu na Abuu Jahli walikutana. Al-Akhnasu alimwambia Abuu Jahli: Ewe Baba wa hekima, nielezee kuhusu Muhammad, je, yeye ni mkweli au muongo? Kwani hapa tulipo hakuna yoyote miongoni mwa Makuraishi anayesikia maneno yetu zaidi ya mimi na wewe. Abuu Jahli akamjibu: Ole wako, naapa kwa Mungu, kwa hakika Muhammad ni mkweli. Na Muhammad hajawahi kuongopa katu. Lakini ukoo wa Quswayyu wakienda na bendera ya uongozi, pazia, kunywesha watu na Utume. Sasa makuraushi wengine watakuwa na nini?''**. Imepokewa na Attwabriyyu kwa sanadi yake kwa Assuddiyu 7 / 181, 182.

(e) Na lau kama Muhammad Ibnu Abdullah angekuwa ameshawahi kujulikana kwa uongo hata mara moja katika uhai wake, asingethubutu kutangaza katika kilima cha Swafaa: **''Enyi ukoo wa Fihru, enyi ukoo wa Adiyyu – kwa vizazi vya Makurayshi – hadi wakakusanyika. Na mtu akawa, pindi anaposhindwa kwenda yeye mwenyewe anatuma mjumbe akamtazamie kuna nini. Mtume akasema: Je, mnajionaje lau kama nitakuelezeni kuwa, farasi yupo jangwani, anataka kukushambulieni. Je, mtanisadikisha? Wakasema: ndio tutakusadikisha, kwa kuwa hatujapato kukusikia ila kwa ukweli…''.** Imepokewa na Bukhariyyu katika Attafsiiru 4770.

[1] Kwa mfano, soma kile kilichoandikwa na Mwingereza Thomas Carlyle katika kitabu chake cha (Heroes – Mashujaa). Na kile kilichoandikwa na Mfaransa Kent Henry De-Castry katika (Idies – Fikra) na (Opportunities – Fursa) zake kuhusu Uislamu. Kisha soma ushuhuda wa Makurayshi uliosajiliwa na Abuu Sufiayani wakati akiwa katika mila ya kijahiliya, mbele ya Hercules kiongozi wa Warumi pale Hercules alipowauliza: **''Je, mlikuwa mnamtuhumu kuwa yeye ni muongo kabla ya kusema kile alichokisema? Akasema: hapana. Akawauliza: je anavunja ahadi? Akasema: hapana''** Imepokewa na Bukhari na Muslimu. [Daraazu].

- Nikasema: Hadithi ya Hercules imepokewa na Bukhari katika Mwanzo wa Ufunuo 6, 7, na imepokewa na Muslimu katika Jihadi na Assayru 74. Na kwa umuhimu wa hadithi ya Hercules, nimeonelea niitaje kwa urefu wake hapa, kwa kuwa inaendana na maneno haya. Bukhari amepokea kwa mapokezi yake kutoka kwa Abdullahi bin Abbasi: **''Kwa hakika Abuu Sufiyani bin Harbu amemweleza kuwa Hercules alimpelekea mjumbe katika msafara wa Makureyshi. Nao walikuwa wafanyabiashara wanaoelekea Shamu katika muda ulee [yaani muda wa suluhu ya Hudaibiya] muda ambao, Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliwapa akina Abuu Sufiyani na makafiri wa Kikurayshi. Huo msafara ukamfikia Hercules, hali ya kuwa yupo Iliyaa [yaani Jerusalemu]. Naye akawaalika katika kikao chake na kandoni mwake kuna wakuu wa Kirumi. Kisha akawaita na kumwita mkalimani wake. Akasema: ni yupi kati yenu aliyekaribu zaidi kinasaba na huyo mtu anayedai kuwa yeye ni nabii? Abuu Sufiyani akasema: nikamwambia: mimi ndio wa karibu zaidi kwake kwa nasaba. [Yaani, kwa kuwa yeye ni wa ukoo wa Banii Abdi Manaafi; babu wa nne wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake]. Akamwambia: msogezeni karibu yangu na jamaa zake wawekeni karibu kwa nyuma yake. Kisha akamwambia mkalimani wake: waeleze kuwa mimi nitamuuliza mtu huyu, na kama ataniongopea elezeni uongo wake [Hercules alifanya hivyo ili watu wa Abuu Sufiyani wasione haya kumtuhumu uongo kama ataongopa. Na baada ya hapo Abuu Sufiyani alikuwa akisema: Naapa kwa Allah, lau ningeongopa wasingenikosoa. Lakini nilikuwa mtu wa kuheshimika na najiheshimu hivyo siongopi. Na nilijuwa fika kuwa jambo lepesi kabisa katika hilo ni kuwa, kama ningemuongopea, wangeyahifadhi maneno yangu kisha**

**wangenisimulia kwa sifa hiyo. Hivyo sikumuongopea]. Naapa kwa Allah lau kama si kuona haya kwamba wataniona mimi ni muongo ningemuongopea. Kisha swali la kwanza kuniuliza lilikuwa ni kusema:**

**Nasaba yake ipoje miongoni mwenu?**

**Nikasema: yeye ni mwenye nasaba nzuri miongoni mwetu.**

**Akasema: Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliyewahi kusema kauli hii hapo kabla?**

**Nikasema: Hapana.**

**Akasema: Je, miongoni mwa mababa zake alikuwepo mfalme?**

**Nikasema: Hapana.**

**Akasema: Je, anafuatwa na watu watukufu au anafuatwa na wanyonge wao?**

**Nikasema: Bali wanyonge wao/**

**Akasema: Je, wanaongezeka au wanapungua?**

**Nikasema: Bali wanaongezeka.**

**Akasema: Je, kuna yeyote miongoni mwao anayeritadi – anayetoka Usilamu – kwa kuichukia [Yaani anauchukia na kuubughudhi] dini yake baada ya kuiingia?**

**Nikasema: Hapana.**

**Akasema: Je, mlikuwa mnamtuhumu kwa uongo kabla ya kusema kile alichokisema?**

**Nikasema: Hapana.**

**Akasema: Je, anavunja ahadi zake?**

**Nikasema: Hapana. Na sisi tukiwa katika muda huu [yaani kipindi cha amani cha mpito] hatujui atafanya nini. Akasema: [yaani Abuu Sufiyan]: sikuweza kuingiza neno zaidi ya neno hili [Kwa kuwa linahusika na wakati ujao uliofichikana].**

**Akasema: je, mlipigana naye vita?**

**Nikasema: ndio.**

**Akasema: Vita vya baina yenu vilikuwaje?**

**Nikasema: Vita vya baina yetu na yake vilikuwa nasibu. Anatushinda na tunamshinda.**

**Akasema: Anakuamrisheni nini?**

**Nikasema: Anatwambia mwabuduni Allah peke yake wala msimshirikishe na chochote. Na acheni kile wakisemacho baba zenu. Na anatuamrisha kuswali, kusema ukweli, kujizuia na machafu na kuunga udugu.**

**Akasema: [Yaani Hercules] kumwambia mkalimani: Mwambie [yaani Abuu Sufiyani]:**

- **Nilikuuliza kuhusu nasaba yake ukasema kuwa yeye kwenu nyinyi ni mwenye nasaba nzuri. Na hivyo hivyo mitume huwa inapelekwa kwa watu wao ikiwa na nasaba nzuri.**
- **Nikakuuliza ikiwa kuna yeyote miongoni mwenu aliyewahi kuyasema maneno haya? Ukasema hapana. Nikasema: lau kungekuwa na mtu yeyote aliyesema kauli hii kabla yake ningesema huyu mtu anafuata [yaani anaiga] kauli ya mtu aliyekuwa kabla yake.**
- **Na nikakuuliza je, miongoni mwa mababa zake alikuwepo mfalme? Ukasema hapakuwepo. Nikasema: lau kama miongoni mwa mababa zake angelikuwepo mfalme ningesema: huyu mtu anataka ufalme wa baba yake.**

- **Nikakuuliza je, mlikuwa mnamtuhumu kwa uongo kabla ya kuisema hiyo kauli yake? Ukasema hapana. Nikajua kuwa huyu mtu hakuwa mwenye kuacha uongo wa kuwaongopea watu na amuongopee Allah.**
- **Na nilikuuliza wanaomfuata ni watukufu au wanyonge? Ukasema ni wanyonge ndio waliomfuata. Nao hao hasa ndio wafuasi wa mitume.**
- **Na nimekuuliza je, wanazidi au wanapungua? Ukasema kwa hakika wanazidi. Na hivyo hivyo huwa suala la Imani mpaka litimie.**
- **Nimekuuliza je, kuna mmoja wao anayeritadi kwa kuichukia dini yake baada ya kuiingia? Ukasema hapana. Na hivyo hivyo Imani ilivyo. Mpaka bashasha yake ichangamane na mioyo [yaani mioyo ifunguke kwa imani].**
- **Nimekuuliza je, anavunja ahadi? Ukasema hapana. Na hivyo hivyo Mitume huwa hawavunji ahadi.**
- **Nimekuuliza juu ya kile anachokuamrisheni. Ukasema kuwa, anakuamrisheni mumwabudu Allah bila ya kumshirikisha na chochote. Na anakukatazeni kuabudu masanamu. Anakuamrisheni kuswali, kusema ukweli na kujizuia na machafu. Ikiwa unayoyasema ni kweli basi mtu huyo atakuja kumiliki eneo la miguu yangu hii miwili. Nilikuwa najua kuwa mwenyewe atatokeza. Ila sikuwa nikidhani kuwa atakuwa miongoni mwenu [yaani miongoni mwa Warabu]. Na lau ningekuwa najua kuwa nitamfikia, ningejikalifisha nikutane naye. Na lau ningelikuwa kwake ningeuosha mguu wake [yaani kutia chumvi mno katika kuonesha unyenyekevu na utumishi wake kwake].**

**Kisha [Hercules] akataka apewe barua ya Mtume aliyoletewa na tarishi wa Mtume [huyu ni swahaba mtukufu aliyetumwa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, aipeleke barua kwa Hercules] gavana mkuu wa Basra. Hiyo barua ikapelekwa kwa Hercules. Naye akaisoma na kutahamaki akakuta ndani yake:**

**Kwa jina la Allah Mwingi a rehema Mwenye kurehemu**

**Kutoka kwa Muhammad mja wa Allah na Mtume wake. Kwenda kwa Hercules Mkuu wa Warumi. Amani iwe kwa wanaoufuata mwongozo. Ama baada ya hayo, mimi ninakuita katika wito wa Uislamu. Silimu utasalimika. Silimu Allah atakupa malipo yako mara mbili. Na kama utakengeuka, basi kwa hakika madhambi ya Waarian (Arianism) yatakuwa juu yako. Na (Sema: ‘‘Enyi watu mliopewa Kitabu (cha Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara)! Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu: ya kwamba tusimwabudu yo yote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe (Mwenyezi Mungu) na cho chote; wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu (au pamoja na Mwenyezi Mungu). Wakikengeuka, semeni: ‘‘Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu, tumenyenyekea amri za Mwenyezi Mungu’’﴿. Aali Imran 64. [Waariani]: hao ni wafuasi na wanyonge]**

**Abuu Sufiyani akasema: na aliposema kile alichokisema, na kumaliza kuisoma ile barua. Kukawa na kelele nyingi na sauti zikawa za juu. Na sisi tukatoka. Kisha tulipotoka nikasema kuwaambia maswahiba wangu: kwa hakika amepewa amri ya mwana kondoo [yaani suala la Muhammad rehema na amani ziwe juu yake limeshadhihiri]. Kwa hakika anaogopwa na mfalme wa wana wa manjano [yaani Warumi]. Na kisha nikaendelea kuamini kuwa Muhammad atashinda hadi pale Allah aliponiingiza katika Uislamu’’.**

**wala asingalikujulisheni (hiyo Quran). Nalikaa baina yenu umri (mwingi) kabla ya haya; (hamkunisikia kusema kitu). Basi hamfahamu (kuwa haya si yangu mwenyewe kwa nafsi yangu ﴾.** Yunus 16.

۞ ۞ ۞

[**Miongoni Mwa Mifano Ya Historia Ya Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake Ndani Ya Quran**]

Kana kwamba mimi nipo hapa mbele yako na wewe unapenda nikupatie historia yake safi, ikiwa ni mfano wa kuigwa wenye maana iliyowazi juu ya upeo wa ukweli wake na uaminifu wake katika madai yake ya ufunuo. Madai ambayo sisi tunayaelekea. Na kwamba yeye hakuwa na uwezo wa kuleta chochote katika Quran kutoka katika nafsi yake. Basi pokea sehemu miongoni mwa hayo:

1 – [**Kipindi cha Ufunuo katika tukio la uzushi]:**

Alikuwa akipatwa na majanga yanayomchochea aseme neno. Na alikuwa na haja kubwa mno inayomlazimisha aseme kitu. Kiasi kwamba, lau kama suala la ufunuo ni la kwake, angepata la kusema na nafasi ya kusema. Lakini mambo yalivyo, mchana na usiku vilikuwa vikifuatiwa na mchana na usiku mwingine bila ya kupata Quran ya kuwasomea watu juu ya jambo hilo.

Je, wanafiki hawakutetemeka kwa tukio la uzushi juu ya mkewe, Bi. Aisha, Allah amuwie radhi, huku ufunuo ukiwa umechelewa. Jambo hili likarefuka huku watu wakitumbukia katika jambo hili. Mpaka nyoyo zikafikia kooni na hali ya kuwa Mtume hawezi kufanya kitu isipokuwa kusema kwa kujichunga na kujizuia: ‘‘Kwa hakika mimi sijui kwake kitu kingine zaidi ya kwamba yeye ni mtu wa heri’’. Kisha Mtume, baada ya kutoa juhudi zake za kuchunguza, kuuliza na kuwaomba ushauri maswahaba wake, ulipita mwezi mzima. Na wote wanasema hutujui kwa Bi Aisha kuwa ana uovu. Mwisho wa siku Mtume hakuzidisha chochote zaidi ya kumwambia Bi. Aisha: ‘‘Ewe Aisha, hakika mambo yalivyo, imenifikia kadha kadha. Na kaama hukufanya Allah atakusafisha. Na kama umefanya hii dhambi, basi omba msamaha kwa Allah’’.

Maneno yake haya yanaonesha dhamira yake. Nayo kama unavyoyaona ni maneno ya mtu ambaye hajui yaliyofichikana. Na ni maneno

ya mkweli mwenye kuthibitisha mambo asiyefuata dhana wala hasemi kile asichokuwa na elimu nacho. Pia yeye hajaondoka sehemu yake baada ya kusema maneno hayo mpaka ukateremka mwanzo wa suratul Nuuri ukitangaza kumtakasa bibi Aisha. Na ukitoa hukumu inayothibitisha utukufu na utakasifu wake. Hadithi imetolewa na Mashekhe wawili[1] na wapokezi wengine.

Sasa kipi kilikuwa kinamzuia – lau kama suala la Quran ni lake – asitunge haya maneno ya kukata kabisa hapo mwanzoni, ili ailinde heshima yake na kuondosha kero hiyo katika nyumba yake na kuyapachika maneno yake katika ufunuo wa mbinguni, ili zikatike ndimi za waongo? Lakini hakuwa mwenye kuacha uongo wa kusingizia watu na aende kumsingizia Allah ﴿**Na kama (Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno tu. Bila shaka tungalimshika kwa mkono wa kuume, (wakulia). Kisha kwa hakika tungalimkata mshipa mkubwa wa moyo (tukamtoa roho yake). Na hapana yoyote katika nyie angeweza kutuzuia naye** –Haqqah 44 -. Al[2] ﴾ 47.

[1] Hadithi ya tukio la uzushi imepokewa na Bukharu na Muslimu: Bukharu amelipokea katika Attasfsiiru 4750 na sehemu nyingine. Na Muslimu katika Attawbati 57.

[2] Zamakhshariyu katika Alkasshafu 4 / 607 amesema: Attaqawwulu ni kuzua kauli, kama vile ndani yake kuna kujikalifisha kwa mwenye kuzua. Na kauli za kuzuliwa zimeitwa ﴿**Aqaawilu = vijizuliwa** ﴾ ni kuvidogesha na kuvibeza. Kama ukisema vijiajabu na vijichekesho… Na maana yake: na lau angedai juu yetu kitu chochote ambacho hatujakisema, basi tungemuua kwa swabran [Asswabru ni kumsimika mtu auliwe]. Kama wafanyavyo wafalme kwa wale wanaowazulia uongo ili kuwashughulikia kwa machukizo na kuwalipizia kisasi. Kwa hiyo akaleta taswira ya kumuua kiswabra kwa taswira yake ili iwe inatisha zaidi: nayo ni kumkamata mtu na kumkata shingo yake. Na umehusishwa mkono wa kulia na sio wa kushoto kwa sababu muuaji anapotaka kukata upande wa nyuma wa shingo ya muuliwa huwa anamshika kwa mkono wa kushoto. Na anapotaka kumkata upande wa mbele wa shingo na apambane naye kwa upanga [yaani amkate akiwa wanatazamana uso kwa uso] – na hali hii ni mbaya zaidi kuliko ile ya mswabirishwa, kwa kuwa mchinjwa anautazama upanga – anamkamata kwa kulia. Na maana ya ﴿**tungalimshika kwa mkono wa kuume** ﴾**:** tungalimshika kuliani kwake. Kama vile ilivyo kauli yake Allah ﴿**tungalimkata mshipa mkubwa wa moyo** ﴾**:** tungalimkata mshipa wa mkubwa wa moyo wake. Na hili lipo wazi. Na ﴿**Watini** ﴾ ni mshipa wa moyo nao ni mshipa mkuu wa kwenda katika moyo na unapokatwa, mtu aliyekatwa anakufa. أ هـ .

Na mwenye Attahriiru Wattanwiiru amesema katika 29 / 144 na yaliyo baada yake:

Sentesi hii ni ushahidi wa kuwa Quran imeteremka kutoka kwa Allah Mtukufu. Nao ni ushahidi uliotulizana akilini, ya kwamba Allah ana uwezo mpana. Na kwamba yeye ni mjuzi na hakubali kwa mtu yeyote kumsemea maneno ambayo hajayasema. Yaani lau Quran isingekuwa imeteremka kutoka kwetu, na huku Muhammad anadai eti

2. **[Quran kupishana na tabia za Mtume. Na lawama kali za Quran kumlaumu katika mambo ya halali]:** na wakati mwingine alikuwa akijiwa na kauli yenye mambo yaliyo kinyume na vile anavyopenda na kutamani. Yenyewe inamkosoa katika maoni anayoyaona. Na kumpa idhini ya kufanya jambo ambalo hukupenda kulifanya. Na akichelewa hata kidogo katika kulifanya jambo hilo. Quran inamsema kweli kweli, inamlaumu vikali, na kukosoa kwa uchungu. Hata katika maswala yenye hatari ndogo mno: ﴿**Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! Unatafuta radhi za wake zako…**[1] ﴾ At-tahrym 1. ﴿**… Na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa (nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitikadiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kuzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea…**Ahzab -Al [2] ﴾

---

imeteremka kutoka kwetu, tusingemkubalia hilo na tungejaalia kuangamia kwake. Na kule kutoangamia kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kunajulisha kuwa hakumzulia Allah uongo. Na maana ya ﴿**tungalimshika kwa mkono wa kuume** ﴾**:** tungelimkamata kwa nguvu yaani bila kuzembea. Na maana yake ni: tungemkamata mkamato wa haraka na papo hapo tungemkata mshipa wa moyo wake. Na katika hili kuna kuogopesha katika hiyo taswira ya ukamataji. Na mshipa wa moyo ni mshipa ambao moyo unaning`ia juu yake, nao ndio ambao unaunywesha damu mwili wote. Na kwa ajili hiyo mshipa huo huitwa mto wa mwili. Nao ndio unaokatwa wakati wa kuchinja vichinjwa. Kwa hiyo adhabu ya mwenye kumzulia uongo Allah imeshabihishwa na kuchinjwa kinachochinjwa na kukatwa mshipa wa moyo. أ هـ [kwa ufupi].

[1] Sababu ya kuteremka aya hii ni matukio mawili:

a- Kutoka kwa Aisha Allah amuwie radhi amesema: **''Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa anakunywa asali kwa Zainabu binti Jahshi na anakaa kwake. Kwa hiyo mimi na Hafswa tukapanga ya kwamba Mtume atakapoingia kwa yeyote miongoni mwetu, basi tumwambie: Umekula maghaafiru? Mimi nasikia kutoka kwako harufu ya maghaafiru [ute wenye ladha tamu, na harufu mbaya]. Mtume akasema: Hapana, lakini nilikuwa nakunywa asali kwa Zainabu binti Jahshi, na kwa hiyo sitorudia tena kuinywa. Nimeshaapa, na hili usimueleze yeyote''.** Imepokewa na Bukhariyu katika Kitabu Tafsiiri 4912 na wenginewe.

b- Kutoka kwa Anasi Allah amuwie radhi: **''Hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa na mjakazi anayelala naye. Bi. Hafswa na Bi. Aisha walimganda Mtume hadi Mtume akamuharamisha [yaani kwa nafsi yake]. Ndipo Allah Mtukufu akateremsha aya hii''.** Imepokewa na Annasaaiyu katika Sunani yake 7 / 71 na Haafidhi bin Hajari akaisahihisha kwa isinadi yake [Fat-hu Albaarii 9 / 288]. Na Haafidhu Ibnu Kathiru amezitaja njia nyingi za hadithi hii. Baadhi yake amezikatia shauri kuwa ni sahihi katika tafsiri yake 8 / 185 – 186.

[2] Assuddiyyu amesema: **''Imetufikia kuwa aya hii imeteremka kuhusiana na Zainabu binti Jahshi. Na mama yake alikuwa ni Umaima binti Abdulmuttwalibi shangazi ya Mtume rehema na mani ziwe juu yake. na Mtume rehema na mani ziwe juu yake**

37. ﴿**Mwenyezi Mungu amekuwia radhi (amekusamehe). Kwa nini umewapa ruhusa? (Ungengoja) mpaka wanaosema kweli wakupambanukie, na uwajue waongo**[1] ﴾. At-tawba 43. ﴿**Haimpasi Mtume na wale walioamini kuwatakia samahani washirikina ijapokuwa ni jamaa (zao); baada ya kuwabainikia kuwa wao ni watu wa (moto wa) Jahanamu**[2] ﴾. At-tawba 113. ﴿**Haimpasi Nabii kuwa na mateka mpaka**

---

**alikuwa anataka kumuoza kwa Zaidi bin Haarith ambaye alikuwa mtumwa wake aliyemwacha huru. Bi Zainabu hakupenda suala hilo. Kisha akaridhia kile kilichofanywa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akaolewa naye. Kisha Allah Mtukufu Aliyetukuka akamjuza Nabii wake rehema na amani ziwe juu yake kuwa huyo bibi baadaye atakuwa miongoni mwa wakeze yeye Mtume. Hivyo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawa anajisikia vibaya kumuamrisha Zaidi ampe talaka mkewe. Na baina ya Zaidi na Mkewe kulikuwa kunaendelea sintofahamu kama zinavyokuwa baina ya watu wengine [yaani migogoro na magomvi]. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akimwamrisha Zaidi aendelee na mkewe na amche Allah. Na [Mtume rehema na amani ziwe juu yake] alikuwa anachelea watu wasimuabishe na wasiseme juu yake kuwa amemuoa mke wa mwanawe. Kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa ameshamuasili Zaidi''.** Imepokewa na Ibnu Abii Haatimu: Fat-hu Albaari 8/384. Adduraru Almanthuuru 5/384. Tafsiiri ya Ibni Kathiiri 6/420.

[1] Aya hii imeteremka pale kundi la wanafiki lilipomuomba ruhusa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, wasiende vitani. [vita vya Tabuki] … na wakatoa udhuru kwa nyudhuru za uongo. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawaruhusu akiwachukulia kuwa ni wakweli. Kwani hali yao ya dhahiri ni Iamani. Na akijua kuwa hata kama wale waliomba udhuru watalazimishwa kwenda vitani, basi hawatosaidia chochote … Ndipo Allah alipomlaumu Nabii wake rehema na amani ziwe juu yake kwa sababu ya kuwaruhusu. Kwa kuwa hata kama asingewaruhusu wangekaa tu. Na kwa hiyo hilo linakuwa ni ushahidi kwa Nabii rehema na amani ziwe juu yake wa kujua unafiki wao na uongo wao katika madai yao ya kuwa wameamini. Ni kama Allah mtukufu alivyosema: ﴿**Na kama tungependa tungekuonyesha? (watu hao wenye bughudha na Uislamu) na ungewatambua kwa alama zao; lakini utaweza kuwafahamu kwa namna ya msemo (wao)…** ﴾ Muhammad 30. … Na Allah amefungua mazungumzo kwa kumjuza msamaha wake. Na hilo ni takrima kubwa na nukta nzuri. Akamweleza msamaha kabla ya kuanza kumlaumu. Na katika ufunguzi huu kuna fumbo juu ya tahfifu katika lawama, kwani zenyewe ni kama vile inaposemwa: haukutakiwa…

(Tafsiru ya Attahriiru Wattanwiiru 10/210 kwa ufupisho kidogo).

[2] Sababu ya kuteremka aya hii ni ile aliyoipokea Said bin Almusayyibu kutoka kwa Baba yake amemweleza: **''Hakika mambo yalivyo, kifo kilipomjia Abuu Twalibi. Mtume rehema na amani ziwe juu yake alimwendea na kumkuta akiwa na Abuu Jahli bin Hishaamu na Abdullah bin Abuu Ummayya bin Mughiira. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamwambia Abuu Twaalibi. Amii, sema hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah. Neno moja tu! Nitakalolitolea ushahidi kwa upande wako mbele ya Allah. Abuu Jahli na Abdullah bin Abuu Umayya wakasema: ewe Abuu Twaalibi, je, unaikataa mila ya Abdul Mutwalibi? Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuacha kuendelea kumuwasilishia suala hilo huku na hao wawili nao wanarudia kauli yao hadi hatimaye Abuu Twaalibi akasema kwa neno lake la mwisho alilowaambia: Yenyewe (yaani nafsi yake) ipo katika mila ya Abdul**

**apigane (sana) na kushinda (barabara) katika nchi (ndipo achukue mateka). Mnataka vitu vya dunia, hali Mwenyezi Mungu anataka (mpate thawabu za) Akhera! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima. Isingalikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu (kuwa mwenye kujitahidi mwisho wa jitihada yake hateswi), bila shaka ingalikupateni adhabu kubwa kwa yale mliyoyachuma[1] ﴾.** Al-Anfal 67 – 68. ﴿**Ama ajionaye hana haja (ya dini). Wewe ndiye unayemshughulikia. Lakini anayekukimbilia. Naye anaogopa. Wewe unampuuza (Usifanye hivyo)** 10. –. Abasa 5 [2]﴾

---

**Muttwalibi. Na akakataa kusema hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Ama mimi naapa kwa Allah, nitakuombea msamaha muda wa kuwa sijakatazwa kufanya hivyo. Ndipo Allah Mtukufu akateremsha kuhusu tukio hilo: ﴿Haimpasi Mtume ﴾ Aya hiyo**. Muttafaqun Alaihi: imepokewa na Bukhariyu katika Aljanaaizi 1360, na Muslimu katika Al-Iimani 39.

[1] Kutoka kwa Anasi Allah amuwie radhi: **''Mtume rehema na amani ziwe juu yake, alishauriana na watu wake kuhusu mateka wa vita vya Badri. Akasema: Hakika Allah Mtukufu Aliyetukuka amekuwezesheni dhidi yao. Omar bin Alkhattwaabi alisimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah wakate shingo zao. Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akamkatalia. Kisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akarudia kusema: Enyi watu! Hakika Allah Mtukufu Aliyetukuka amekuwezesheni dhidi yao. Na kwa hakika hawa ni ndugu zenu wa jana. Omar akasimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah wakate shingo zao. Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akamkatalia. Kisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akarudia na kuwaambia maneno kama hayo. Abuu Bakri akasimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah tunaonelea tuwasamehe na ukubali kuchukua fidia zao. Na akawasamehe na kukubali fidia zao. Na Allah Mtukufu Aliyetukuka akateremsha ﴿Isingalikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Mwenyezi ﴾ Hiyo aya.''**

Imepokewa na Ahmad 3/243.

Na kutoka kwa Ibnu Abbas Allah amuwie radhi na baba yake. Katika kuhusiana na aya ﴿**Isingalikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu…** ﴾ Maana yake ni ngawira za vita vya Badri kabla hazijahalalishwa kwa Waislamu. Anasema [yaani Allah Mtukufu Aliyetukuka] lau kama isingekuwa mimi simwadhibu aliyeniasi mpaka nimtangulizie [yaani nimtahadharishe] basi ingekupateni adhabu kubwa. Adduraru Almanthuuru ya Assuyutwiyu 3/367 na akaiegemeza kwa Attwabari na Ibni Almundhiru na Ibni Abii Haatimu na Attwabaraaniyu na wengineo.

[2] Kutoka kwa Aisha Allah amuwie radhi: imeteremshwa ﴿**Amekunja (Mtume) paji na akageuza uso** ﴾ **kwa ajili ya Ibnu Maktuum ambaye alikuwa kipofu. Alimwendea Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, na kuanza kusema: Ewe Mtume wa Allah nipe mwongozo. Na kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, kulikuwa na mtu miongoni mwa wakuu wa washirikina. Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, akawa akimpotezea [yaani Ibnu Ummi Maktuum] na kumwelekea yule mwingine na kusema: je, unaona kuna ubaya kwa kile ninachokisema? Na yule mtu anasema: Hapana. Basi katika tukio hili ikateremshwa**

Je, unaona lau kama hizi lawama za kuumiza moyo zingetoka katika hisia zake, zikieleza dhamira yake pale ilipomdhihirihikia kinyume na kile alichokikosea katika rai zake. Je, angezitangaza dhidi ya nafsi yake kwa mtindo huu wa kuogofya na kukera mno? Je, katika kuyanyamazia haya, hakukuwa na kuistiri nafsi yake. Na kubakisha heshima ya rai zake? Hapana! Bila shaka Quran hii, lau kama ingelikuwa inabubujika kutoka katika hisia zake. Basi wakati wa haja, angeweza kuficha baadhi ya hizo hisia. Na kama angekuwa ameficha kitu fulani, basi angezificha aya kama hizi. Lakini yenyewe ni ufunuo. Na yeye hawezi kuuficha**. ﴿Wala yeye si bakhili wa (kukuelezeni) mambo ya ghaibu ﴾.** At-Takwyr 24.

### [**Kutolea Ushahidi kwa Elimu Ya Saikolojia Juu Ya Kutengana Baina ya Uhusika Wa Ufunuo Na Uhusika Wa Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake**]

Itafakari vizuri aya ya suratul Anfal iliyotajwa. Utakuta ndani yake kuna tukio la ajabu; kwa hakika aya hiyo haikuteremshwa isipokuwa baada ya kuwaachia huru mateka wa Badri na kukubali fidia kutoka kwao. Yenyewe imeanza kwa kuonesha makosa na kupinga kitendo hiki. Kisha haukupita muda ikamalizia kwa kukikubali na kuzipoza nafsi kuhusiana na kitendo hicho. Bali lenyewe likawa ni tukio lililopita, na ambalo limepewa makemeo na lenyewe likiwa ni kanuni ya yale yatakayokuja baada yake. Je, hali ya kisaikolojia iliyotokea kwa maneno haya kwa mara ya kwanza – lau chanzo chake kingekuwa ndicho chanzo hicho hicho – inawezekana kwa chanzo hicho hicho yangetokea maneno ya mwisho wake? Na bado baina ya hali mbili hizo haujapita angalau muda kidogo unaotengenisha baina ya ukereketwa wa ghadhabu na majuto na baina ya tabasamu na kuridhia na kuona jambo ni zuri? Sivyo hivyo!

Kwa hakika hali mbili hizi za kisaikolojia, lau kama tungelazimisha kuwa zenyewe zinatokana na nafsi moja ila zimefuatana papo kwa papo, basi ya pili yake ingekuwa ni yenye kuipiga chini na kuifuta ile ya kwanza. Na

---

**aya hii.** Imepokewa na Attirmidhiyyu katika Attafsiiru 3331. Na sanadi yake imesahihishwa na Al-Bani katika Swahihu Attirmidhiyyu 2651.

Na katika aya hii, Alhaafidhu Ibnu Kathiiru anasema katika tafsiri yake 8/342: na kutokana na hapa, Allah Mtukufu Aliyetukuka amemwamrisha Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake, asimfanye yeyote kuwa maalumu wa katika maonyo. Bali katika hilo, afanye usawa baina ya mtukufu na mdhaifu, fakiri na tajiri, bwana na mtumwa, wanaume na wanawake, watoto na wakubwa. Kisha Allah amuongoze amtakaye katika njia iliyonyooka. Naye ana hekima kubwa na hoja zenye nguvu.

hiyo nafsi ingerejea na kubaki na fikra ya mwisho, na hii ni kwa mujibu wa kile kinachotokea katika uhalisia wa matendo. Kwa hiyo kuna sababu gani iliyofanya kuwepo kwa taswira hiyo ya kisaikolojia ya kufuta na kusajili. Ikiwa ndani yake kuna lawama za wazi wazi na za kuumiza moyo zisizo za haki. Na kuyachafua mapato haya, wakati anataka kuyafanya yawe ya halali tena ni mazuri mno? Kwa hakika kile wanachokifahamu wataalamu wa saikolojia kutokana na kulisoma andiko hili ni kuwa, kwa hakika hapa kuna uhusika wa watu wawili waliotengana. Na kwa hakika hapa kuna sauti ya bwana anamwambia mtumwa wake: kwa hakika umekosea lakini mimi nimekusamehe na nimekuruhusu ulichokifanya.

### [**Msimamo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, juu ya andiko la Quran ni msimamo wa mfasiri anayetafuta maana mbalimbali na kuchukua zile chaguzi za huruma**]

Na wewe kama ungelizitazama uzuri dhambi alizolaumiwa kwazo Mtume ungelizikuta zenyewe zimefungwa katika kitu kimoja tu. Nacho ni kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, pindi kunapokuwa na chaguzi mbili na haoni katika mbili hizo kama mojawapo ina dhambi. Basi alikuwa anachagua ile iliyokaribu na huruma kwa watu wake, kuwaongoza watu wake na kuwajenga wapinzani wake, ile iliyo mbali na ukali na ugumu, ile isiyochochea sintofahamu katika dini ya Allah. Na mbele yake hakukuwa na andiko atakaloenda kinyume nalo kwa kupambana nalo. Au amelikosea kwa makosa na kusahau. Bali dhambi zake zote ni kuwa yeye ni mwenye kujitahidi na akakosea kwa kuchagua kinyume na kile kilicho bora zaidi. Je, yeye si mwenye udhuru na mwenye kulipwa? Kwa kuwa kile alichokichagua kilikuwa ndicho bora wanachokichagua wale wenye hekima ya kibinadamu.[1] Na kwa hakika Quran imemzindua juu ya kile kilichobora zaidi katika mizani ya hekima ya Allah. Je, kiakili unaona katika hilo kuna dhambi inayowajibisha kulaumiwa na kutiwa hatiani? Au kuwa lenyewe linaonesha nafasi ya Mola Mlezi na nafasi ya Mtumwa. Na mwendo wa kupanda kwa

[1] Na uchaguzi wa Omar Allah amuwie radhi katika maswala ya mateka na mfano wake, haukuwa vingine ila ni mtazamo miongoni mwa mitazamo ya ukali iliyokuwepo kwa wingi katika tabia yake. Na ukali huu ulikaribia kumfitinisha na amri ya Allah siku ya Alhudaibiya kama itakavyokuja. Kwa hiyo kuafikiana kwake na ufunuo katika maswala hayo ni sadfa tu, kwa hukumu bila ya kuwa na sababu ya hakika alizonazo Allah mjuzi wa vilivyofichikana yeye peke yake. [Daraazu].

Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika ngazi ya kufundishwa na kuadabishwa?

‘‘Abdullah Bin Ubayi ambaye ni mkuu wa wanafiki alifishwa. Nabii akamvika sanda kwa nguo yake na akataka kumuombea msamaha na kumswalia. Omar Allah amuwie radhi alimwambia: Je, unamswalia na Mola wako ameshakukataza? Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: hakika si vinginevyo nimepewa uchaguzi na Mola wangu na alisema ﴿**Ewe Mtume)! Waombee msamaha (hao wanafiki) au usiwaombee; (yote sawa sawa). Hata ukiwaombea msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu hatawasamehe…** ﴾ At-Tawba 80. Basi mimi nitawazidishia zaidi ya mara sabini. Akamswalia. Ndipo Allah Mtukufu akateremsha ﴿**Wala usimsalie kamwe mmoja wao yeyote yule akifa, wala usisimame kaburini kwake (kumuombea dua)…** ﴾ At-Tawba 84. Hapo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akaacha kuwaswalia’’. Soma kisa hiki kilichothibiti kwa mapokezi ya Swahihi mbili.[1] Na tazama, unaona nini? Kwa hakika inakuwakilishia nafsi ya huyu mja anayenyenyekea, na aliyeifanya Quran kuwa ndio katiba, anapokea hukumu zake kutoka katika maandiko neno kwa neno.

Na inakuwakilishia moyo wa mtu huyu mpole akiwa ameliwazwa kwa maelezo ya dhahiri[2] ya andiko la kwanza kumpa uchaguzi baina ya njia mbili. Na haraka haraka Mtume rehema na amani ziwe juu yake akapita njia iliyokaribu zaidi na ukarimu na rehema baina ya njia mbili hizo. Hakurejea katika ile njia nyingine ila baada ya kujiwa na andiko la wazi linalokataza. Na hivi hivi, kila utakaposoma msimamo wa Mtume juu ya Quran katika maeneo haya au mengineo. Itakupambanukia kuwa maana ya utumwa wenye kumyenyekea na maana ya ubinadamu mpole mwenye huruna; na mkabala wa hivyo itakupambanukia katika upande wa Quran, maana ya nguvu ambayo haihukumiwi na vichocheo na malengo. Bali imepasua kwa kubainisha kipambanuzi baina ya haki na batili. Na mizani ya kupima mabaya na mazuri. Sawa sawa watu wapende au wachukie. Waridhie au

---

[1] Muttafaqu alaihi: ameipokea Bukhariyu katika Attafsiiri 4670 na sehemu nyingine. Na Muslim katika Fadhaailu Swahaba 25.

[2] Tunasema: dhahiri ya andiko hili, kwa sababu kuunganisha kwa, au inakubali kuwa ni sawa sawa na sio kuchagulishwa (kupewa nafasi ya kuchagua). Kama ilivyo muundo wa kutaja idadi unakubali kuwa kwa ajili ya kukoleza mno na sio kuweka ukomo wa idadi kama ilivyokuja katika asili ya kuwekwa kwake. Na kwa muktadha wa ukarimu wa tabia yake, Mtume Mkarimu rehema na amani ziwe juu yake hakuiacha fursa ya uchaguzi ila kwa andiko lingine.

wachukie. Waamini au wakufuru. Kwani yenyewe haizidishwi na utiifu wa wenye kutii na wala haipungui kwa maasi ya wenye kuasi. Na utaona baina ya nafasi mbili hizo yale yaliyo baina yake. Na ni mbali mno yaliyo baina ya bwana na mfuasi wa bwana. Na mtumwa na mwabudiwa.

3- [**Wakati mwingine Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasimama na hafahamu makusudio ya andiko hadi aletewe ubainifu wake**]:

Wakati mwingine alikuwa akijiwa na amri ya kauli ya kiujumla au jambo tata. Jambo ambalo tafsiri yake haibainiki kwake wala kwa maswahaba wake mpaka hapo baadaye Allah awateremshie ubainifu wake. Naapa kwa Mola wako, hebu niambie: Ni akili gani inayotoa ufunuo wa maneno kwa nafsi yake kisha yeye mwenyewe haijui maana yake. Na inamwamrisha jambo ambalo yeye mwenyewe hailifahamu hekima yake? Je, hilo si miongoni mwa ushahidi wa wazi wa kuwa yeye ni mnukuuji tu na sio msemaji wake. Na kuwa yeye ameamrishwa na sio aliyeamrisha?

### [**Mfano wa kwanza: Msimamo wake katika tukio la kujitathmini kuhusu nia**]

Kauli ya Allah Mtukufu imeteremka ﴿**… Na kama mkidhihirisha yaliyomo katika nyoyo zenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu atakutakeni hisabu ya (yote) hayo;… **﴾ Al-Baqarah 284. Iliwachanganya maswahaba mchanganyo mkubwa. Na ndani ya mioyo yao kulikuwa na kitu juu ya aya hii. Na hicho kitu hakikuwaingia kutokana na kingine zaidi ya kuwa wao waliifahamu kuwa wao watahesabiwa kwa kila kitu hata mapigo ya moyo na fikra zake – ndipo wakasema: ‘‘**Ewe Mtume wa Allah, imeteremka kwetu aya hii na wala hatuiwezi. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawaambia: Je, mnataka mseme kama walivyosema wale waliopewa kitabu kabla yenu: waliosema tumesikia na tumeasi? Bali ninyi semeni: Tumesikia na tumetii, tunaomba, msamaha ni wako ewe Mola wetu na kwako wewe tu ndio marejeo’’.** Wakawa wanaomba na kusihi sana kwa dua hizi mapaka pale Allah alipoteremsha ubainifu wake kwa kusema: ﴿**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yo yote ila yaliyo sawa na uweza wake… **﴾ Al-Baqarah 286. Mpaka mwisho wa sura tajwa. Na kwa hapo wakajua kuwa wao watahisabiwa kwa kile wanachokiweza miongoni mwa mambo ya moyoni nayo ni yale yanayokuwa kwa kunuia na kuazimia

kulikotulizana moyoni. Na sio kutokana na mapito na fikra za moyoni bila mtu kuchagua kufanya hivyo. Hadithi hii ipo katika Muslimu na wengineo.

Na Bukhariyu ameiashiria katika Attasfsiiru ikiwa kwa ufupi[1]. Na eneo la kutolea ushahidi kwa hadithi hii ni kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, lau angekuwa anajua maana yake tangu mwanzoni mwake, basi angewabainishia makosa yao na angewaondoshea utata waliokuwa nao papo hapo. Kwa sababu yeye hakuwa mwenye kuwaficha ujuzi huu na hali ya kuwa wao wanauihitaji sana. Na hakuwa mwenye kuwaacha katika mfadhaiko huu uliokaribia kuzing`oa nyoyo zao na hali ya kuwa yeye kwao wao ni mpole mwenye huruma nao. Lakini yeye alikuwa kama wao anasubiri fasili yake. Na kwa ajili ya jambo fulani, ndio maana Allah aliwacheleweshea huu ubainifu. Na kwa ajili ya jambo fulani ndio Allah akaweka neno la kuonesha kuchelewa katika kauli yake Mtukufu ﴿***Kisha* ni juu yetu kukubainisha (kukubainishia ﴾.** Al-Qiyama 19.

[**Mfano wa pili ni: mapito yake katika suala la Hudaibiya**]

Na soma suala la Hudaibiya[2] katika Swahihi Bukhariyu na Sunani Abuu Daudi na wengineo wasiokuwa hawa. Kwani ndani yake kuna alama ya wazi wazi: Allah amewaruhusu waumini wapigane vita na wale wanaowafanyia uadui popote walipo. Isipokuwa wasipigane katika msikiti wa Makka maadamu wao nao hawajawapiga vita katika msikiti huo. Na Allah amesema ﴿**Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni…** ﴾ Al-Baqarah 190. Na pindi Waislamu wote walipokubaliana waende kuuzuru msikiti mtukufu wa Makka katika mwaka huo, nao ni mwaka wa sita wa Hijiriya, walichukua silaha zao kama tahadhari tu, ikitokea wakapigwa vita na yeyote basi wajilinde kwa mujibu wa sheria. Na walipokaribia mipaka ya msikiti wa Makka walijua kuwa Maqurayshi wamejikusanya makundi yao karibu na

---

[1] Ameipokea Muslimu katika Al-Iimanu 199 kwa ukamilifu wake.

Na vile vile katika Bukhariyyu katika Attafsiiru kwa ufupisho sana 4545 , 4546.

[2] Hadithi ya Hudaibiya ni ndefu na kwa ukamilifu wake imepokewa na Bukhariyu katika Asshuruutwu 2731, 2732 miongoni mwa riwaya za Almasuuru ibni Makhramah na Marwani bin Alhakami kwa pamoja. Na kwa Abuu Daudi ipo katika Aljihadi 2765 miongoni mwa riwaya za Almasuuru. Na kwa Ahmad 4/323 miongoni mwa riwaya za Almasuuru bin Makhramah na Marwani. Na Bukhariyu aliipokea baadhi yake kutoka kwa Al-barraau katika Asswulhu 2698, 2700. Na katika Almaghaazi 4251. Na kutoka kwa Ibnu Omari katika Asswulhu 27.1, Na katika Almaghaazi 4252. Na imepokewa na Muslimu kwa ufupi katika Aljihadi na Assayru miongoni mwa hadithi ya Al-barraau 90, 92, na miongoni mwa hadithi ya Anasi Bin Malik 93.

wao. Hilo halikuwazuia wao kutimiza azima yao; kwani wao walikuwa tayari, tayari kwa lolote. Bali suala hilo liliwazidishia ushujaa na kung`ang`ania kuendelea hadi wafike msikitini. Na atakayewazuia watapigana naye. Na Maqurayshi walikuwa washamalizwa nguvu zao na vita walivyopigana. Kwa hiyo vichocheo vyote vya kuanzisha vita vilikuwapo kwa Waislamu, pia fursa ya kuingia katika vita vya kuwamaliza imewajia, ili Haki iweze kuishinda batili na kuiangamiza kabisa.

Na wakiwa wanatembea eneo la Hudaibiya ghafla ngamia wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na watu wake akapiga magoti. Na maswahaba wake wakawa wanamchochea aende upande wa msikiti mtukufu lakini yule ngamia hakukubali. Ndipo wakasema: Alqasuwaa amegoma. Alqasuwaa amegoma – yaani ngamia wa Mtume – amegome. Ndipo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: ‘‘Alqasuwaa hajagoma. Na hiyo sio tabia yake. Lakini amezuiwa na yule aliyemzuia tembo’’ yaani kwa hakika Allah ambaye alimkamata tembo na kuzuia watu wake wasiingie Makka kuupiga vita msikiti huo. Ndiye aliyemkamata ngamia huyu na kuzuia jeshi la Waislamu lisiingie kwa nguvu sasa hivi. Na hivyo hivyo ndipo alipoyakinisha kuwa Allah Mtukufu kwa mwaka huu hajawaruhusu kuingia Makka wakiwa wanapigana vita. Sio kwa kuanzisha vita wala kujitetea.

Na alipomkemea ngamia, ndipo akacharuka na kuelekea upande mwingine. Na hapo ndipo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawapeleka watu wake upande wa mabali wa Hudaibiya. Na akawaondoa wasiendelee na mwendo, na huko ni kutii ishara hii ya Mwenyezi Mungu. Ishara ambayo haijui hekima yake. Akawa anafanya juhudi za kuingia Makka kwa njia ya suluhu na Maqurayshi huku akisema: **‘‘Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, hawatoniomba mpango wowote, na katika mpango huo wanaadhimisha utukufu wa Allah, isipokuwa nitawapa mpango huo’’.** Lakini Maqurayshi walikataa kata kata, waislmu wasiingie Makka kwa mwaka huo. Sio wakiwa kivita wala wakiwa kiamani. Wakampa masharti magumu ya kuwa mwaka huo arejee. Na awarejeshe watu wote wa kutoka Makka watakaomjia wakiwa wamesilimu. Na Maqurayshi wasimrejeshe yeyote atakayewajia akitokea Madinia akiwa ameacha dini yake.

Naye Mtume akakubali masharti hayo, ambayo kiuhalisia, Maqurayshi wakiwa na udhaifu wao hawakuwa na ubavu wa kuyatoa kwa

Waislamu wakiwa na nguvu zao. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliwaamrisha maswahaba wake watengue hija ndogo zao na warejee kule walipotoka. Usiulize juu ya kile walichokuwa nacho maswahaba juu ya suluhu hii, miongoni mwa vitu vinavyoumiza mioyo ya waumini. Ilifikia mpaka, kwa hakika baadhi yao walipokuwa wanawanyoa wengine walikaribia kuuwana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ya bumbuwazi na kihoro kilichowapata.

Na nyoyo za miongoni mwa kundi la maswahaba wakubwa zilikaribia kupotoka. Wakawa wanaulizana wao kwa wao, kisha wanamrejea Mtume mwenyewe huku wakisema: Mbona tunatoa ‘addaniyyata’[1] katika dini yetu? Na hivyo hivyo, jeshi lilikaribia kuasi amri ya kiongozi wake na kuponyoka na kukata kamba kutoka mikononi mwake. Je, kwa wakati huo, lau kama kiongozi huyu angekuwa yeye mwenyewe ndiye anayeweka mipango hii, au japo alishiriki katika kuiweka, au anajua siri zake, haikuwa jambo la kawaida kuwabainishia maswahaba wakubwa hekima ya matendo haya yaliyo juu ya akili ya kawaida. Ili azime moto wa fitina kabla cheche zake hazijaruka na kusambaa?

Lakini hebu tazama, namna jibu lake lilivyokuwa pale Omar alipomrejea kwa kusema: **‘‘Kwa hakika mimi ni Mtume wa Allah. Na simuasi. Na yeye ndiye mwokozi wangu’’**. Anasema: hakika si vinginevyo mimi ni mja ninayeamrishwa na si lolote katika jambo hili isipokuwa kutekeleza amri ya Mola wangu huku nikiwa na Imani thabiti kuwa ataninusuru hivi karibuni au hapo baadaye. Na hivi hivi wakatembea kurejea na hali ya kuwa hawatambui fasili ya mkanganyiko huu mpaka ilipowateremkia suratul Al-Fat-h. ikabainika kwao wao hekima kubwa na bishara njema za kweli. Na kutahamaki kile walichokidhania kibaya na kujiumiza mwanzoni mwa maoni yao kikawa ndicho ushindi mkubwa na ukombozi mkuu[2]. Wapi na wapi mipango ya wanadamu katika mipango ya Qadari.

---

[1] Addaniyyata: Udhalili, kijidogesha na unyonge.

[2] Ibnu Is-Haqa amesema, Azzuhuriyu amesema: Hapo kabla hapajawahi kuwa na ukombozi mkuu katika Uislamu kuushinda ukombozi wa Hudaibiya. Kwa hakika kulikuwa na vita pale watu walipokutana. Na pale ilipotokea makubaliano ya kusitisha vita kwa muda, na kusitisha vita na watu wao kwa wao kupata amani, walikutana na kuzungumza kwa maneno. Kwa hiyo katika kipindi hicho, hakuongeleshwa mtu yoyote juu ya Uislamu kwa akili isipokuwa mtu huyo aliingia katika Uislamu. Na mwenye Al-Fat-hi amelifasiri hilo kwa kusema: Kwa ajili ya amani iliyotokea baina yao, watu

﴾**Na yeye ndiye aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kukupeni (Mwenyezi Mungu) ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu anaona (yote) mnayoyatenda. Hao ndio waliokufuru na wakakuzuilieni kwenda katika Msikiti Mtukufu (wa Makka baada ya kukaribia hapo kwa kiasi cha meili 48), na wakawazuilia wale wanyama (mliowachukua kwa ajili ya kuchinjwa) wasifike mahala pake. Na lau kama si wanaume Waislamu na wanawake Waislamu (walioko Makka wanaficha Uislamu wao), msiowafahamu, msije mkawasaga bila kujua, na kwa hiyo mkapata masikitiko kwa ajili yao; (ingalikuwa si haya Mungu asingekuzuilieni kupigana nao. Amefanya haya) ili Mwenyezi Mungu amuingize amtakaye katika rehema yake. Kama (Waislamu na makafiri) wangelitengana, bila shaka tungaliwaadhibu wale waliokufuru miongoni mwao adhabu iumizayo. Pale wale waliokufuru waliopitia nyoyoni mwao mori, mori wa ujinga; basi hapo Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya Waislam; akawalazimisha neno la kumcha Mungu; nao walikuwa ndio wenye haki zaidi nalo na waliostahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ndoto yake ya haki: Bila shaka nyinyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu. In shaa – Allah kwa salama; mkinyoa vichwa vyenu na kipunguza nywele (kama ilivyo wajibu kufanya hivyo). Na Mwenyezi Mungu) anajua msiyoyajua. Basi kabla ya haya atakupeni kushinda (kwanza) kuliko karibu (kuwashinda Mayahudi** ﴿**.** Al-Fat-h 24 – 27.

### 4 – [**Njia Yake Katika Kupokea Andiko, Mwanzo Wake Wa Kupokea Ufunuo**]:

Kwa hakia Mtume alipokuwa anateremshiwa Quran katika nyakati zake za mwanzoni za kupokea ufunuo alikuwa anaupokea hali ya kuwa anaharakisha na kutikisa ulimi na midomo yake akitaka kuuhifadhi. Na kuchelea kuupoteza kutoka kifuani mwake. Suala hilo halikuwa maarufu katika ada zake za kuhudhurisha maneno yake. Si kabla wala baada ya wito

---

walichanganyika wao kwa wao bila ya kuchukizana. Na wakadhihiri wale waliokuwa wanaficha Uislamu wao. Na Waislamu wakawasikilizisha Quran Washirikina. Na wakapeana midahalo ya hoja kwa uwazi huku wakiwa na amani. Na kabla ya hapo walikuwa hawaongei mbele yao juu ya hayo ila kwa uficho. Kwa hiyo washirikina wakadhalilika pale walipokusudia kupata utukufu. Na wakashindwa pale walipotaka ushindi. [Daraazu].

wake wa Utume. Pia hilo halikuwa miongoni mwa ada za Warabu. Kwa hakika walikuwa wanapitisha maneno yao katika nafsi zao. Lau Quran ingekuwa inatoka katika chanzo hicho hicho, basi ingepita katika njia ile ile ya maneno ya Muhammad na maneno ya Warabu. Na ingekuwa ina tafakuri na uvumilivu wa kunyamaza. Kiasi cha kumtoshelezea haja yake ya kuiweka madhubutu rai yake na kuisafisha fikra yake.

Lakini yeye alikuwa anaiona nafsi yake ipo mbele ya mafundisho yanayomjia ghafla kwa nyakati tofauti, naye haraka haraka anayakusanya mafundisho hayo. Kiasi ambacho hapati nafasi ya kutafakuri[1] chochote cha kukileta hata kama atatakiwa kufanya hivyo. Na wala si katika uweza wake kuudiriki na kuukumbuka lau kama kitampotea chochote katika ufunuo huo. Alichokuwa anapaswa kukifanya ni kurudia kile alichopewa neno kwa neno. Kwa hiyo katika nyakati za mwanzo za kupata ufunuo alikuwa na hali hiyo mpya. Hali ambayo hakuizoea katika nafsi yake, hali ya kuwa na pupa sana ya kufuatilia neno kwa neno. Mpaka pale Allah alipompa dhamana ya kuuhifadhi na kuubainisha ufunuo kwa kauli yake ﴿**Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka. Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu** ﴾. Al-Qiyama 16. Na kauli yake ﴿**… Wala usiifanyie haraka (hii) Quran (kwa kusoma), kabla haujamalizika Wahyi (ufunuo) wake. Na (uombe) useme: ''Mola wangu, nizidishie ilimu.''** ﴾. Ta-Ha 114.

Hii ni sehemu ya historia yake kuielekea Quran. Na haya yote ni ushahidi unaoongea juu ya ukweli wake unaoonesha ya kwamba Quran haitokani na yeye bali imemjia. Na ya kuwa yeye hakuileta kutoka moyoni mwake bali alimiminiwa.

* * *

## [Sehemu Ya Historia Ya Jumla Ya Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake]

Kama utapandisha macho yako na kuangalia historia yake kwa ujumla utapata katika pande zake mkusanyiko mzuri mno wa tabia njema za hali ya juu. Na kwa sasa ikutoshe katika hilo, mifano michache. Ukitafakari vizuri itakupa taswira ya mwanadamu safi, nguo zimemkaa vizuri, mwenye bidii, haiba kubwa, ulimi wake unakataa kujitumbukiza katika asiyoyajua, na macho yake yanakataa kuficha yale yaliyo kinyume na kile anachokitangaza.

[1] Kutafakuri: ni kulitazama jambo kwa kina na si kulifanyia haraka.

Na masikio yake yanakataa kusikiliza misifa ya kupitiliza ya wenye kumsifu: Unyenyekevu ni pambo la watukufu. Na uwazi ni nadra kwa viongozi wakuu. Na anapenda kuthibitisha sana, kiasi ambacho hilo ni mara chache mno kulikuta kwa wanazuoni. Kwa hiyo, ni wapi na wapi kwa mtu aliye mfano wake kuhadaa na kughushi? Au kudanganyika au kudanganya? Hapana kabisa naapa kwa Allah!

1 – [**Anajitakasa Na Elimu Ya Vilivyofichikana**]:

**‘‘Wajakazi walikaa wanapiga dufu, asubuhi ya harusi ya Rabia binti Muadhi wa Kianswari. Wakawa wanataja sifa za baba zao miongoni mwa mashujaa wa vita vya Badri mapaka mjakazi mmoja miongoni mwao akasema: na sisi tuna Nabii anayejua mambo ya kesho. Mtume rehema na amani ziwe juu yake na watu wake akasema: Usiseme hivyo, na sema kile ulichokuwa ukikisema’’**. Imepokewa na Bukhariyu[1]. Na kusadikisha yale yaliyo katika Kitabu cha Allah Mtukufu. ﴿**Sema: ‘‘Mimi sikwambieni kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu (nikakupeni mnayoyataka;) wala (sikukwambieni kuwa) najua mambo ya siri (ya Mwenyezi Mungu)… ﴾.** Al-An-Am 50. ﴿**… na lau kama ningalijua ghaibu ningejizidishia mema mengi;… ﴾** Al-Aaraf 188.

2 – [**Haoneshi kinyume na vile anavyovificha**]:

Abdullah bin Abuu Assarahu alikuwa mmoja wa wale waliotolewa na Nabii katika kupata amani siku ya ukombozi wa Makka. Na hilo ni kutokana na kuchupa kwake mipaka katika kuwaudhi Waislamu na kuwazuilia wasiingie Uislamu. Na pale alipokuja kwa Nabii, Nabii hakumkubalia amuunge mkono ila baada ya kuombewa msamaha mara tatu na Othman Allah amuwie radhi. Kisha akawaelekea maswahaba wake na kusema: **‘‘Hivi hakukuwa miongoni mwenu na mtu mtambuzi akasimama na kumuua mtu huyu pale nilipozuia mkono wangu asiniunge mkono? Wakasema: hatujui yaliyo nafsini mwako. Mbona hujatuashiria kwa jicho lako! Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Hakika mambo yalivyo, haitakikani kwa Nabii kuwa na usaliti wa jicho’’.** Imepokewa na Abuu Daud na Annasaaiyu.[2]

[1] Imepokewa na Bukhariyu katika Almaghaazi 4001, na kwa mfano wake katika Annikaahu 5147.

[2] Imepokewa na Abuu Daud katika Aljihaadi 2683, na Annasaaiyu katika Tahriiimi ddami 7/106. Na imesahihishwa na Albani katika Asswahiihatu 1723.

3 – [**Hofu Yake Juu Ya Kumzulia Uongo Allah**]:

**‘‘Na aliletwa mtoto wa Kianswari ili amswalie. Aisha Allah amuwie radhi akasema: kufaulu ni kwa mtoto huyu, hajafanyapo shari. Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake akasema: Ewe Aisha hauna lingine. Kwa hakika Allah ameumba pepo na kuiumbia watu wake. Na amewaumbia hiyo pepo huku wenyewe wakiwa katika migongo ya baba zao. Na ameumba moto na kuiumbia watu wake. Na amewaumbia huo moto huku wenyewe wakiwa katika migongo ya baba zao[1]’’** Imepokewa na Muslimu na Asw-haabu Sunani[2]

4 – [**Hajui Hadhi Yake Itakuwaje Mbele Ya Allah**]:

**‘‘Na pale alipofishwa Othman bin Madhuuni Allah amuwie radhi, mama Alaa – mwanamke wa Kianswari – alisema: Rehema za Allah ziwe juu yako ewe baba Assaaibiu. Ushuhuda wangu ni kwako, kwa hakika Allah amekurehemu. Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake amesema: ni kipi kinakujulisha kuwa Allah amemkirimu? Akasema: kwa baba yangu, ewe Mtume Allah. Je, ni nani anayekirimiwa na Allah? Akasema: Ama yeye kwa hakika ameshajiwa na yakini. Naapa kwa Allah, mimi namtarajia heri. Na naapa kwa Allah, sijui nitakachofanyiwa licha ya kuwa mimi ni Mtume wa Allah. Akasema yule mwanamke: Na ninaapa kwa Allah, katu sitomtakasa yeyote baada yake’’.** Imepokewa na Bukhariyu na Annasaaiyu[3]. Na kusadikisha yale yaliyomo katika Kitabu cha Allah Mtukufu ﴿**Sema: ‘‘Mimi**

---

[1] Wazuoni wamesema huku kusimama na kutotaja hukumu ya watoto kulikuwa kabla ya kujua kuwa watoto wa Waislamu ni watu wa peponi. [Daraazu].

[2] Imepokewa na Muslimu kwa mfano wake katika Alqadaru 30, 31, na Abuu Daud katika Assunna 4713. Na Annasaaiyu katika Aljanaaizu 4/57 na Ibnu Maaja katika Almuqaddima 82.
Sijaikuta kwa Annasaaiyu. Na vile vile Assuyutwiyu ameiegemeza kwa Annasaaiyu katika Adduraru Almanthuuru 6/5

[3] Imepokewa na Bukhariyu katika Aljanaaizu 1243, na wengineo. Na imepokewa na Ahmad 6/436. Na sikuikuta kwa Annasaaiyu. Na vile vile Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 6/5 ameiegemeza kwa Annasaaiyu. Na huenda ipo katika Assunanu Alkubraa yake.

**si kiroja (mpya), katika Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa nyinyi…**Ahqaf 9.-. Al[1] ﴾

Je, unamuona, kuwa pale anapojihami dhidi ya uongo huwa anajihami, kwa hadaa na kufanya siasa. Akiogopa mambo ya ghaibu yasije kuwekawazi kinyume na vile anavyosema kwa karibu au kwa mbali. Ni kipi kingekuwa kinamzuia kujitungia akitakacho kuhusiana na mambo ya baada ya umauti na hali ya kuwa yeye haogopi mtu atakayemrejea katika hilo. Na wala haogopi hukumu ya kihistoria juu yake? bali kwa hakika alizuiwa na Muumba Mtukufu, na kule kuheshimu majukumu makubwa mbele ya mwamuzi mwingine aliyejuu zaidi ya historia na watu wake. ﴿**Na kwa yakini tutawauliza wale waliopelekewa (Mitume), na pia tutawauliza (Mitume) waliopelekwa. Tena tutawaambia kwa ujuzi (uliyo kamili kila walilolitenda). Wala hatukuwa mbali (nao walipokuwa wakiyafanya**﴾**.** Al-Araf 6 -7.

* * *

## [**Kutafiti Tabia Za Nafsi Katika Historia Za Watu Wake**]

Na jua kwamba wewe, kwa vyovyote vile utakapoistarehesha nafsi yako na kuipa raha ya kuwa na yakini. Na kuichalia isiwe na mashaka. Na kuiacha ichukulie kuwa kuna mambo mabaya katika jambo moja na tukio moja katika historia hii tukufu. Kwa hakika wewe, kwa muda wowote utakaposimama na kuitazama vizuri kwa mjumuisho mzuri hutoweza kuimiliki nafsi yako na kuuondoa uyakini huo nafsini mwako isipokuwa hilo litakuwa baada ya kuzituhumu hisia zako na kushuku juu ya usalama wa akili zako. Sisi huwaona watu wakijifunza maisha ya washairi kwa kupitia mashairi yao. Kwa hiyo kutoka katika maneno ya mshairi wanachukua taswira kamili inayowakilisha itikadi yake, ada zake, tabia zake, mapito ya fikra zake, muundo/mtindo wake, mtindo wa maisha yake. Mapambio na mapambo mbalimbali ya mashairi hayawazuii watafiti kung`amua khailatihi[2] – aliyoyaacha – mshairi. Na kufunua mapovu yake kutokana na

---

[1] Wanazuoni wamesema: haya yalikuwa kabla ya kupewa kwake ufunuo wa aya za mwanzoni mwa suratul Al-Fat-hi. ﴿**Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yanayokuja, …** ﴾ Al-Fat-hi 2. [Daraazu].

[2] Kung`amua khailati; kilugha ni kibri. Lakini mnyumbuliko wa kitenzi: khaala Yakhiilu unadhihirisha maana ya kuficha, kutatiza na kuchanganya. Kwa hapa huenda neno (Kung`amua khailati) likamaanisha kufahamu na kudhihirisha yale yanayokusudiwa kufichwa.

maneno yake ya uwazi[1]. Hayo ni kwa kuwa ukweli una nguvu ya kushinda na kupenya katika kizuizi cha kuficha. Unasoma baina ya mistari na kufahamu kutokana na toni za kauli. Na mwanadamu kwa vyovyote vile atakapojitahidi kuigiza na kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa, kamwe hatoepukana na vijikosa katika kauli zake na vitendo vyake, vinavyoashiria tabia yake asilia pale atakapohifadhiwa au kutolewa au atakapohitaji au atakapopatikana au atakapowakosa wale anaowatumainia.

Amesema mshairi:

*‘’Vyovyote itakavyokuwa kwa mtu, katika tabia **
*Hata kama atazificha kwa watu zitajulikana tu’’.*

Basi ni ipi dhana yako katika maisha haya ya Mtume. Maisha ambayo katika kila kipengele miongoni mwa vipengele vyake yanakupa kioo safi kinachoakisi uhusika wa mwenye maisha hayo. Yanakuonesha undani wake na udhahiri wake. Na yanakuonesha ukweli na nia safi vinavyowakilishwa katika kila kauli miongoni mwa kauli zake na katika kila kitendo miongo mwa vitendo vyake. Isipokuwa yule aitazamaye historia yake, kama werevu wake ni uimara, na akaboresha utambuzi wake. Ataziona tabia zake njema zikipepea katika maisha yake hata kama yeye mwenyewe hajaongea au hajatenda. Na kutokana na hili, watu wengi miongoni mwa wale ambao Allah aliwafungulia vifua vyao kwa ajili ya Uislamu. Wao hawamuulizi Mtume awape ushahidi juu ya kile alichokisema. Na miongoni mwao ni jamaa[2] ambao walimjua kwa historia yake tukufu. Na miongoni mwao ni mgeni ambaye alimtambau kwa alama zake za usoni kwake. Abdullah Bin Salaam Allah amuwie radhi amesema: **‘‘Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipofika Madina. Watu walimkimbilia na pakasemwa: Mtume wa Allah amekuja! Mtume wa Allah amekuja! Nikaenda kwa hao watu ili nimtazame. Nilipouthibitisha uso wa Mtume Allah rehema na amani ziwe juu yake na aali zake nikajua kuwa uso wake si uso wa muongo’’.** Imepokewa na Attirmidhiyu kwa sanadi swahihi[3].

---

[1] Kufunua mapovu yake kutokana na maneno yake ya wazi: Mapovu ni yale yanayokuwa juu ya maziwa yanapomiminwa chomboni [yaani maputoputo]. Na Swarihu ni maziwa freshi. Na uelezaji huu kwa ujumla unamaanisha: Kufunua upotoshaji kuuepusha na ukweli.

[2] Jamaa: ni mke au watu anaoishi nao, au rafiki au ndugu wa karibu.

[3] Imepokewa na Attirmidhiyu katika Swifatul Qiyaamati 2485, Na Ibnu Maajah katika Kusimamisha Swala 1334, na Albaniy ameisahihisha katika hadithi swahihi 569.

Na kwa sasa, tumeshatekeleza ahadi yetu kwako. Ahadi ya kuwasilishia huu mfano kutoka katika historia ya Nabii. Hebu turudi katika ripoti ya kile tulichokikusudia katika uwasilishaji huu, na tunasema: kwa hakika mwenye tabia hizi tukufu na mwenye misimamo hiyo ya kinyenyekevu mbele ya Quran. Haitakikani kwa yeyote kutilia shaka ukweli wake pale yeye mwenyewe alipotangaza kuwa yeye sio aliyekitunga kitabu hiki. Na kueleza kuwa nafasi yake kwa Kitabu hiki ni nafasi ya mwanafunzi anayepata faida. Bali ilikuwa inapasa tukusajili kukiri huku kulikotakasika kuwe ushahidi mwingine juu ya uwazi wake na unyenyekevu wake.

* * *

### [**HATUA YA KWANZA YA UTAFITI**: **Kubainisha Kuwa, Haiwezekani Kwa Quran Kuwa Ni Maelezo Yanayotoka Katika Nafsi Ya Muhammad Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake**]

Jambo lililo mbele yetu lipo wazi kabisa na halihitaji hadi kusikia muungamo wa maneno kutoka kwake. Au litegemee utafiti unaohusu upande wa kitabia unaotokana na historia yake.

Je, haitoshi kumuhukumu mtu kuwa hana kosa kwa tendo miongoni mwa matendo. Kwa kuzingatia kigezo cha mtu mwingine wa maumbile yake kushuhudia kuwa hana uwezo wa kimwili kufanya tendo hilo?

Na mwenye akili atazame: Je, Nabii huyu rehema na amani ziwe juu yake, asiyejua kusoma na kuandika, kwa muktadha wa njia za kisayansi alikuwa na vigezo vya kufikiri katika nafsi yake maana hizo za Quran?

Wajinga miongoni mwa makafiri watasema: ndio anavyo, kwa hakika alikuwa na uwerevu wa kimaumbile na maono yake ni makali, yanayomwezesha kutambua haki na batili miongoni mwa maoni. Na kutambua nzuri na mbaya katika tabia. Na kutambua heri na shari katika matendo. Mpaka, inafikia, kama vile kitu fulani cha mbinguni kinampatia utambuzi au kinamfahamisha kimaumbile, au kinamfunulia mawazo ili ayashughulikie kwa maumbile yake yaliyo salama. Na akili yake iliyokamilika, na tafakuri yake ya kweli.

Na sisi huenda tunaamini mengi miongoni mwa yale aliyoelezewa miongoni mwa tabia. Lakini sisi tunauliza: ***Je, kila kilichopo katika Quran ni katika vile vinavyong`amuliwa na akili na tafakuri. Na vile***

***vinavyotambulika na kifahamu na kihisia? Naapa kwa Allah, hilo hapana kabisa.***

### [**Maumbile Ya Maana Za Kiquran Si Miongoni Mwa Zile Zinazotambulika Kwa Uwerevu Na Ukweli Wa Ung`amuzi**:]

a- **Kwa Habari Za Yaliyopita, Hakuna Njia Ya Kuzifikia Ila Kwa Kuzipokea Na Kuzidurusu**]

Ndani ya Quran kuna upande mkubwa wa maana za kunukuu tu! Na ambazo uwerevu na ung`amuzi havina nafasi juu yake. Na kwa yule ambaye habari hizo zimejificha kwake, hana njia ya kuzijua isipokuwa kwa kuzichunguza, kuzipokea na kujifunza. Watasema nini kwa yale tuliyosimuliwa na Quran kuhusu habari za yale yaliyotangulia, na zile alizotueleza kwa ukamilifu miongoni mwa habari hizo, kwa njia sahihi kama zilivyotokea? Je, watasema kuwa historia nayo huenda ikawekwa kwa kutegemea matendo ya kifikra na umakini wa ung`amuzi? Au watatoka kuelekea katika kufanya kibri kikubwa na kusema kuwa, kwa hakika Muhammadi aliishi zama moja na hizo nyumati zilizopita. Na kunukuu kutoka kwa wale walio wa rika moja naye. Na alishuhudia matukio haya pamoja na watu wake, kushuhudia kwa kuona hasa.

Au ya kwamba yeye amerithi vitabu vya watu wa kale na akavikalia kitako kuvisoma mpaka akawa miongoni mwa wabobezi katika elimu ya kina juu yao? Kwa hakika wao hawawezi kusema hili wala lile. Kwa kuwa wao ni wenye kukiri pamoja na dunia yote kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuwa miongoni mwa hao wala hawa. ﴾**… nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao ndani ya maji (kwa kura, wajue) nani wao atamlea Maryamu…** ﴿ Aali Imran 44. ﴾**… na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao, hali wakifanya vitimbi vibaya** ﴿. Yusuf 102. ﴾**Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, (ingekuwa hivyo) wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki** ﴿. Al-Ankabuut 48. ﴾**Hizi ni katika khabari za siri tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Quaran kuteremshwa)…** ﴿ Hud 49. ﴾**Sisi**

**tunakusimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Quran hii. Na hakika ulikuwa kabla ya haya ni miongoni mwa wasio na khabari (hizi ﴾.** Yusuf 3.

Hatusemi eti elimu ya kujua majina ya baadhi ya Manabii na nyumati zilizopita, na ujumla wa yale yaliyopita miongoni mwa matukio ya kuangamiza miji ya Adi na Thamudi, Tufani ya Nuhu na yanayofanana na hayo kuwa katu hayajawafikia wale wasiojua kusoma na kuandika. Kwani haya mambo kiduchu mno, na ni mara chache mno kutojulikana na mtu yeyote miongoni mwa watu wa majangwani au wa mjini. Kwa kuwa hayo ni miongoni mwa yale waliyorithishana kizazi hata kizazi na yakaenda kuwa mifano. Kwa hakika jambo la kutazamwa ni hayo maelezo ya kina kwa ukamilifu, na hazina zilizozikwa katika matumbo ya vitabu. Hiyo ndio elimu ghali isiyoguswa na mikono ya wasiojua kusoma na kuandika. Na hawakuwa wakiijua isipokuwa wachache miongoni mwa wasomi. Na kwa hakika wewe utapata habari sahihi zenye faida kubwa miongoni mwa habari hizi zikiwa zimechambuliwa katika Quran. Mpaka nambari kwa nambari: kwa mfano utaona katika kisa cha Nuhu amani iwe juu yake, ndani ya Quran ikieleza kuwa aliishi kwa watu wake miaka elfu moja isipokuwa miaka hamsini.

Na katika kitabu cha Mwanzo katika Torati utaona ya kuwa aliishi miaka mia tisa na hamsini. Na utaona katika kisa cha watu wa pangoni kwa watu waliopewa kitabu, ya kuwa walikaa pangoni mwao miaka mia tatu ya kalenda ya kuzingatia jua. Na katika Quran ni kuwa wao walikaa pangoni mwao ﴿**Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu, na wakazidisha (miaka) tisa ﴾.** Al-Kahf 25. Na hii miaka tisa ndio tofauti baina ya idadi miaka ya kalenda ya jua na miaka ya kalenda ya mwezi. Azzajaaju amesema, yaani kwa kukamilisha sehemu. Hebu tazama hesabu za kina zitokazo kwa umma usiojua kusoma, kuandika wala kuhesabu.

Mshairi amesema

*Inakutosha muujiza, kwa asiyejua kusoma kuwa na elimu,.*

*Katika zama za ujinga na kwa yatima kuwa* muadabishaji.[1]

---

[1] Hii ni beti katika Shairi la Al-Burda la Al-Buusuriyyu – Tazama Diwani ya Al-Buusuriyyu uk 246.

Naaam, kwa hakika hilo ni ajabu kweli: mtu asiyejua kusoma na kuandika akiwa katikati ya watu wasiojua kusoma na kuandika. Anayehudhuria matukio yao – yasiyo ya batili au ya uovu – na anaishi maisha yao akiwa anajishughulisha na kutafuta riziki yake na mkewe na watoto wake. Akichunga wanyama kwa ujira. Au akifanya biashara kwa ujira. Hana muunganiko na mambo ya elimu na wanazuoni. Anapitisha katika hali hii zaidi ya miaka arobaini ya umri wake. Kisha anatutokea katika mida iliyo baina ya usiku na asubuhi na kutuambia mambo ambayo hakuwa nayo hapo kabla katika maisha yake, na kwa yale ambayo hajamuongelesha yeyote kwa herufi moja kabla ya hapo. Na anatudhihirihishia miongoni mwa habari za karne hizo za mwanzo.

Zile zilizofichwa na wenye elimu katika madaftari yao na rafu zao. Je, katika maswala kama haya wajinga watasema, eti yeye amefunuliwa na akili yake na kupewa il-hamu na dhamira yake? Ni mantiki ipi inayoweza kukubali kuwa muendelezo huu mpya wa kielimu ni matokeo ya maumbile ya maisha hayo yaliyopita ya wasiojua kusoma na kuandika? Kwa hakika hakuna pa kutokea katika suala la akili, bali akili inakubali kuwa muhamo huu wa kimaumbile ni siri nyingine inayotafutwa nje ya mipika ya nafsi na nje ya duara la maarifa ya kale. Na kwa hakika makafiri wa kijahilia, nao walikuwa ni mabedui mabwege wa majangwani.

Kwa ujumla walikuwa wakweli zaidi katika kutoa sababu ya tukio hili na walikuwa karibu zaidi na kufahamu vizuri siri hii kuliko makafiri wa zama hizi. Kwani wao hawakusema kama walivyosema hawa wa kisasa ya kuwa Mtume amezipata habari hizi kutokana na ufunuo wa nafsi yake. Bali walisema ya kuwa hapana budi mtume amesomewa elimu mpya tangu siku hiyo alipotangaza wito wake. Kwa hiyo Mtume amesoma toka katika chanzo hicho kile ambacho hakuwa amekisoma. Na amejifunza kile ambacho hakuwa anakijua**. ﴿Na namna hivi tunazikariri aya (wapate kufahamu. Lakini itokeavyo ni) kwamba wanasema: ''Umesoma (haya, hakukuletea Mungu''… ﴾** Al-An-Am 105. ﴿**Na wakasema: ''Ni visa vya (watu) wa zamani alivyoviandikisha (Muhammad, kwani mwenyewe hajui kuandika wala kusoma), anavyosomewa asubuhi na jioni, kisha yeye anawasimulia watu'' ﴾** Al-Furqan 5.

Kwa hakika wamesema kweli; kuwa yeye ameyasoma, lakini kwa mwalimu ambaye ni Jibrilu. Na ameandikiwa ndio, lakini kutoka katika kurasa zilizohishimiwa, zilizotukuzwa, zilizotakaswa. Zilizomo mikononi

mwa malaika waandishi wa Allah, watukufu na wacha Mungu. ﴿**Sema: ‘‘Kama Mwenyezi Mungu angalitaka nisingalikusomeeni hii (Quran), wala nisingalikujulisheni (hiyo Quran). Nalikaa baina yenu umri (mwingi) kabla ya haya; (hamkunisikia kusema kitu). Basi hamfahamu (kuwa haya si yangu mwenyewe kwa nafsi yangu? ﴾.** Yunus 16.

Hayo ni katika mambo yaliyomo katika Quran miongoni mwa habari za kihistoria. Hakuna ubishi ya kuwa yenyewe yanapatikana kwa mapokeo na si kwa kutumia akili. Na ya kuwa yenyewe yanakuja kutoka nje ya nafsi ya mtu na sio kutoka ndani yake.

Ama elimu nyingine za Quran huenda ikasemwa kuwa zenyewe ni miongoni mwa elimu zinazotambulika kwa akili. Mwerevu anaweza kuzipata kwa utambuzi wake au kwa kuchunguza. Mwanzoni maneno haya yanaweza kuonekana ni ya kweli, lakini baada ya muda kidogo, yanaporomoka mbele ya majaribio.

Na hilo, ni kwa sababu akili za wanadamu zina njia zake maalum za kutambua vitu. Na mipaka maalum ya kuishia na haivuki mipaka hiyo. Kwa hiyo, kila kitu kisichotokea moja kwa moja chini ya hisia ya nje au ya ndani. Na hakijatulizana katika utambuzi wa kisaikolojia. Kwa hakika kitu hicho kinatambulika na akili kwa njia ya kauli-gezi (premise – utangulizi wa kimantiki) inayofahamika inayokufikisha katika kile kisichojulikana. Ima kwa haraka mno kama katika Alhadsi[1] na ima kwa pole pole mno kama katika kutoa ushahidi, kung`amua na Qiyasi.[2] Na kila kile ambacho hakijafuata njia na kauli-gezi hizi, kamwe haiwezekani kutambulika na akili. Na kwa hakika njia ya kukitambua ni Ilhamu (kufunzwa na Mungu), au kunukuu kutoka kwa yule aliyepewa hiyo ilhamu.

***Je, yale yaliyomo katika Quran miongoni mwa maana zisizo za kihistoria, zilikuwa chini ya njia na kauli-gezi katika mtazamo wa kiakili?***

Hayo ndio yale ambayo habari zake zitakujia baadaye. Lakini sisi, kwa sasa tunakuharakishia mifano wiwili miongoni mwa maana hizo. Tukitosheka kwa kuitaja hapa na tutairudia hapo baadaye:

**Wa kwanza**: Kigawo cha itikadi za kidini.

---

[1] Alhadsi: Dhana na kufikiria kuwa ni kitu fulani.

[2] Qiyasi: vipimo, navyo ni kutoa ushahidi wa kitu kwa kutazama kinachofanana nacho au kushabihiana.

**Wa pili**: Kigawo cha utabiri wa mambo ya siri.

### [**B – Mambo Ya Kweli Ya Kidini Yaliyofichikana Ambayo Akili Haina Njia Ya Kuyafikia**]

Ama suala la dini, kwa hakika huu ni upeo wa juu kabisa unaovunwa na akili miongoni mwa matunda ya utafiti wake huru, baada ya kusaidiana na maumbile yake yaliyo salama. Nayo ni kujua kuwa juu ya ulimwengu huu kuna Mwenyezi Mungu mwenye uwezo juu yake na kwamba hajauumba kwa batili. Bali ameuweka kwa muktadha wa hekima na uadilifu. Na hapana budi kwa huyo Mungu ataurejesha mara nyingine ili kila mtendaji apate malipo ya tendo lake, kama la heri au la shari. Na haya ndio yatakayopatwa na akili iliyokamilika kuhusiana na jambo la dini.

Lakini Quran kwa upande wake haisimami katika kiwango hiki tu. Bali tunaiona yenyewe inatufafanulia mipaka ya imani kwa maelezo ya kina. Na inatuelezea mwanzo wa uumbaji na mwisho wake. Inaelezea Pepo na aina za neema zake, na moto na aina za adhabu zake. Kana kwamba viwili hivyo vinaonekana kwa macho. Mpaka imefikia upeo zinahesabiwa idadi ya milango kadhaa. Na hesabu ya Malaika waliokabidhiwa milango hiyo. Je, kwa nadharia ipi ya kiakili ilijengewa maarifa haya ya kihisabati, na maelezo hayo yenye muanisho?

Kwa hakika mambo hayo ni katika yale ambayo hayafunuliwi na akili kabisa kabisa. Bali mambo hayo ima yawe ya batili na yanakuwa miongoni mwa ufunuo wa mawazo na kubahatisha, au ima ni ya kweli, na kwa hiyo hayapatikani ila kwa kufundishwa na kusomewa. Kwa hakika yenyewe ni ukweli ulioshuhudiwa na vitabu na kufahamika kwa kina na watu wa vitabu ﴿**Na hatukuweka walinzi wa huo Moto ila Malaika, wala hatukuifanya idadi yao (hiyo ya kumi na tisa) ila kuwa mtihani kwa wale waliokufuru; ili wawe na yakini waliopewa Vitabu (kabla yenu), na walioamni wazidi katika Imani yao…**[1] ﴾ Al-Muddathir 31. ﴿**Na namna hivi tumekufunulia**

---

[1]Al-Haafidhi Ibnu Kathiiru amesema katika tafsiri yake juu ya aya ya 8/294:
Na hayo ni jibu kwa washirikina wa Kikuraishi pale ilipotajwa idadi ya walinzi [yaani walinzi wa Jahanama], Abuu Jahli alisema: Enyi makongamano ya Makuraishi. Je, kila watu kumi miongoni mwenu hawawezi kukabiliana na mmoja miongoni mwao na kumshinda? Allah akasema ﴿**Na hatukuweka walinzi wa huo Moto ila Malaika…** ﴾ Yaani wana maumbo makali hawazuiliki wala hawashindwi**…** ﴿**… wala hatukuifanya idadi yao (hiyo ya kumi na tisa) ila kuwa mtihani kwa wale waliokufuru…** ﴾ Yaani

**Wahyi kwa amri yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini wala Imani;…** ﴾ Ash-Shuura 52. ﴿**Sikuwa na ilimu ya mambo ya viumbe watukufu (Malaika) walipokuwa wakishindana, (ila amenijulisha Mwenyezi Mungu** ﴾.[1] Sad 69. ﴿**Na haiwezekani kuwa hii Quran imetungwa, haitokani na Mwenyezi Mungu (kama mnavyojidai). Bali (imetokana na Mwenyezi Mungu), inayosadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya vitabu (vilivyopita). Haina shaka kuwa imetoka kwa Mola wa walimwengu (wote** ﴾. Yunus 37.

[C – **Habari Za Mambo Ya Wakati Ujao Huenda Yakang`amuliwa Na Vipimo Vya Dhana. Lakini Mambo Hayo Hayana Njia Ya Kuyayakinisha Ila Kwa Ufunuo Wa Kweli**]

Ama utabiri wa mambo ya siri, je, unajua namna mwenye akili kamili anavyohukumu katika haya? Kwa hakika yeye, kutokana na uzoefu wake uliopita anajifanyia taa inayomwangazia hatua zinazopitia matukio ya wakati ujao. Huku akifanya kile kinachoshuhudiwa na kipimo hiki kuwa ndicho kipimo cha hayo yaliyofichikana. Kisha ndipo anapotoa hukumu yake katika suala hilo akijihadhari na kuchukua kila aina ya tahadhari, huku akisema: (Hayo ndio mambo yanayopelekewa na maumbile ya matukio lau kama mambo yataenda katika maumbile yake na hakutotokea kile kisicho katika hesabu zetu). Ama kutoa hukumu ya kukata kabisa, na kuianisha kwa muainisho hasa, hata katika mambo ambayo hayajulishwi na kauli gezi miongoni mwa kauli gezi za kielimu.

Na hazioneshwi na alama yoyote miongoni mwa alama za dhana ya kawaida. Na hayo ndio yale ambayo hayafanywi ila na mmoja wa watu wawili:

---

kwa hakika tumeitaja idadi yao ya kwamba wao ni kumi na tisa ni jaribio letu kwa watu. ﴿**…ili wawe na yakini waliopewa Vitabu (kabla yenu** ﴾ yaani wajue ya kwamba huyu Nabii ni wa kweli. Na kwa hakika ametamka kulingana na yale yaliyo mikononi mwao miongoni mwa vitabu vya mbinguni vilivyoteremshwa kabla yake. ﴿…na walioamni wazidi katika Imani yao… ﴾ Yaani katika imani yao. Anamaanisha kwa kile wanachokishuhudia miongoni mwa ukweli wa habari za Nabii wao Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. أ هـ .

[1] Al-Haafidhi Ibnu Kathiiru amesema katika tafsiri yake juu ya aya ya 7/70: yaani lau si ufunuo, tofauti za viumbe wa juu ningezijua kutoka wapi? Akimaanisha kuhusiana na Adam na kujizuia kwa Ibilisi na kuacha kumsujudia. Na hoja zake dhidi ya Mola wake juu ya kujiona kwake kuwa yeye ni mbora [kama ilivyo katika aya zinazofuata].

- Ima awe ni mtu mwenye hatari asiyejali kama watu watamsema kuwa yeye ni muongo au mkweli. Na huo ndio mwendo wa wajinga wanaopata utabiri kutoka kwa wapiga ramli na watazamia nyota.
- Na ima awe mtu aliyechukua ahadi kutoka kwa Allah ya kuwa hatovunja ahadi yake.  Na huo ndio mwenendo wa Manabii na Mitume. Na hakuna watatu wao isipokuwa mtu aliyepokea habari zake kutoka kwa mmoja wa watu wawili hao. Je, mwenye Quran hii unamuona yupo kati ya mtu gani katika watu wa aina mbili hizi, pale katika ulimi wake zinapokuja habari za kukata kabisa zikieleza kitakachotokea baada ya mwaka mmoja na kitakachotokea katika miaka kadhaa. Na kile kitakachotokea zama zote. Na kile ambacho hakitotokea milele? Hilo, na yeye hakujishughulisha na elimu ya kupiga ramli, wala kutazamia nyota. Na tabia zake hazikuwa kama tabia zao, zinazowakilisha madai na kuyavamia. Na wala habari zake hazikuwa kama habari zao zilizochanganyika baina ya ukweli na uongo, usahihi na makosa. Bali Mtume, licha kutakasika kwake na kutojua elimu ya mambo ya siri, na licha ya kukaa kwake bila ya kujikalifisha na kuisaka elimu ya mambo ya siri. Ila hiyo elimu ya mambo ya siri humjia bila ya yeye kupanga, ikimuelezea mambo ambayo mabadiliko ya nyakati katika vipindi virefu tofauti tofauti, yanashindwa kuyatengua hata herufi moja miongoni mwa yale yaliyotabiriwa naye. ﴿**… bila shaka hicho ni kitabu kihishimiwacho. Haitafikia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa; na Mwenye hikima, ahimidiwaye** ﴾. Haa Mym Sajdah 41 – 42.

[**Mifano Ya Utabiri Wa Quran**]

Haya hebu tukusimulie baadhi ya utabiri wa Quran pamoja na kubainisha matukio yake ya kihistoria; ili uone, je, tangulizi zake za karibu au za mbali zilikuwa hadhiri. Kwa hiyo tabiri hizo zinakuwa ni miongoni mwa yale yanayofunuliwa kwa utambuzi wa hali ya juu na utambuzi wa kuangalia dalili na viashiria? Na tutayafunga maneno katika aina tatu tu:

1- Yale yanayofungamana na mustakbali wa Uislamu wenyewe au kuhusu kitabu chake na Nabii wake.
2- 3- Yale yanayofungamana na mustakbali wa makundi mawili: kundi la Allah na kundi la shetani.

**Mfano wa aina ya kwanza [Mustakbali wa Uislamu, kitabu chake na Nabii wake]:**

1- Yale yaliyokuja katika kubainisha kuwa dini hii imeandikiwa na Allah ibakie na kudumu milele. Na kuwa Quran hii, imedhaminiwa na Allah kuwa ataihifadhi na kuilinda. ﴿**… Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyotoa mfano wa haki na batili. Basi lile povu linapita kama takataka tu basi; lakini vile vinavyowafaa watu vinakaa katika ardhi…** ﴾ Ar-Raad 17. ﴿**Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri (ambao) mizizi yake ni imara na matawi yake yamenyooka juu. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake;…** ﴾ Ibrahim 24 – 25. ﴿**Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Quran); na hakika sisi ndio tutakayoyalinda.** ﴾ Al-Hijr 9. Je, wajua? Lini na wapi bishara njema hizi zenye hakika zilitolewa. Bali hizi ni ahadi za uthibitisho?

Kwa hakika aya hizi ni za Makka, zimo katika sura za Makka. Na wewe unajua suala la ulinganiaji wa Muhammad huko Makka? … miaka kumi yote ni kupingwa na kaumu yake, hawakutaka kuisikia Quran yake. Na kuwazuia watu wengine wasiisikilize. Na kuvitenza nguvu na kuviadhibu vikundi vya wachache vilivyomwamini. Kisha kumwekea vikwazo vya kibiashara yeye na ukoo wake na kumzingira kwa muda ambao si mdogo. Katika eneo miongoni mwa maeneo ya Makka. Kisha kumfanyia njama za siri au za wazi za kutaka kumuua au kumpeleka uhamishoni. Je, ni haki kwa mwanadamu, katika njia yake hii ya kiza totoro kama usiku mzito, ya muda wa miaka kumi, kuona mwanga japo mdogo wa kuwa na matumaini ya kupata faraja kwa idhini ya hawa waliodhulumiwa wanyanyue sauti zao na kutangaza dini yao?

Na lau kama mrekebishaji wa jamii angeinusa hiyo nuru ya matumaini katika pande za nafsi yake kutokana na maumbile ya wito wake. Lakini si katika upeo wa matukio. Je, inaafikiana kwake katika mfano wa mazingira kama haya, yakue katika nafsi yake, matumaini hadi yawe ni hukumu iliyokwisha katwa? Yakiwa yamemjaa matumaini ya kushinda kwa wito wake maishani mwake muda wa kuwa anajipa ahadi hiyo katika nafsi yake. Sasa ni nani atakayemdhaminia yeye baada ya kufa kwake kuwa wito huu utabakia na kulindwa ukiwa katikati ya mawimbi mazito ya mustakbali? Vipi yakini inamjia katika hilo na hali ya kuwa yeye kupitia zama anayajua yale yatakayomvunja nguvu zake katika uyakini huu? Kwani ni wapo wengi miongoni mwa warekebishaji jamii waliopiga kelele za kurekebisha jamii lakini haukupita muda ila sauti zao zikaenda patupu katika tabaka za hewa!

Na kuna miji mingi miongoni mwa miji katika historia iliyosimama kidete, kisha ikaporomoshwa na kusagwa sagwa athari zake! Na Manabii wengi wameuawa! Na vitabu vingi vimepotea au vimepunguzwa au vimebadilishwa!

Je, Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na aali wake, alikuwa ni miongoni mwa wale ambao kwao wao matumaini yamejificha, na kwa hiyo wanakwenda mbio pamoja na maono yao? Kwa hakika yeye kabla ya kupewa utume wake hakuwa ana tamaa ya kuwa nabii anayefunuliwa. ﴿**Nawe hukuwa unatumai ya kwamba utaletewa Kitabu (upate Utume); lakini ni rehema ya Mola wako; …** ﴾ Al-Qasas 86. Na wala baada ya utume wake hakuwa na dhamana ya nafsi kuwa ufunuo huu aliopewa utasalia ukiwa umehifadhiwa. ﴿**Na kama tungelipenda bila shaka tungaliondoa yale tuliyokufunulia, kisha usingalipata kwa (jambo) hili wa kukupigania juu yetu. Ila kwa rehema itokayo kwa Mola wako (ndio yakadumia haya). Hakika fadhila yake (Mwenyezi Mungu) iliyo juu yako ni kubwa kabisa** ﴾**.** Bani Israil 86 – 87.

Kwa hiyo, hakuna budi kuwepo kwa mlinzi wa nje ya nafsi ya Muhammad wa kuihifadhi. Sasa ni nani huyo ambaye anamiliki uwezo wa kudhamini hili kwa miaka yote inayopishana na iliyojaa mambo ya kushtukiza? Zaidi ya Mola wa zama zote. Mola ambaye mikononi mwake kuna hatamu za matukio yote. Na ambaye amekadiria mwanzo wake na mwisho wake. Na anaufahamu vizuri mwendo wake na mafikio yake. Na lau kama si fadhila za Allah na rehema zake, alizoziahidi katika aya iliyopita hivi punde, basi Quran isingaliweza kupambana na hivyo vita vikali dhidi yake. Na bado inaendelea kupambana baina ya muda na muda mwingine.

Uliza historia: ni mara ngapi zama zinaleta balaa katika nchi za Kiislamu na kuzisalitisha kwa waovu kuwatesa Waislamu, kuwaua na kuwasagasaga. Na kuwalazimisha baadhi yao wakufuru. Kuchoma moto vitabu vyao. Kubomoa misikiti, na wakafanya yale ambayo machache yake yanatosha kuipoteza hii Quran yote au baadhi yake. Kama ilivyofanywa kwa vitabu vya kabla yake. Na lau si kuwepo kwa mkono wa uangalizi unaoilinda, basi Qurani isingebakia katikati ya vita hivi vikali ikiwa inanyanyua bendera yake. ikihifadhi aya zake na hukumu zake. Pia yaulize magazeti ya habari za kila siku: ni vibunda vingapi vya dhahabu na fedha vinavyotumika kila mwaka kwa ajili ya kuifuta hii Quran na kuwazuia watu wasiufuate Uisalamu, kwa kupotosha, kuzuaa uongo, kuhadaa na

kuwaghilibu. Kisha watu wanaofanya hayo hawapati lolote ila kile alichokisema Allah Mtukufu: ﴿**Hakika wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuilia (watu wasipate kuamini) njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watazitoa, kisha zitakuwa majuto juu yao, kisha watashindwa…** ﴾ Al-Anfal 36.

Yanatokea hayo kwa kuwa yule aliyeishika Quran isitoweke ndio ambaye amezishika mbingu na ardhi zisitoweke.

Hayo, ni kwa kuwa Allah: ﴿**Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili aijaalie kushinda (dini hii) dini zote; ijapokuwa watachukia hao washirikina** ﴾**.** Attawba 33 na As-saff 9. Na Allah ndio mwenye kulifikisha jambo lake na mwenye kutimiza nuru yake. Hivyo itashinda na itabakia ikiwa mshindi. Haidhuriwi na mwenye kuipinga hadi pale itakapokuja amri ya Allah.

2 – (Na mfano mwingine) ni yale yaliyokuja katika changamoto zilizotolewa na hii Quran zinazoonesha kushindwa kwa ulimwengu wote kuleta mfano wa Quran. ﴿**Sema: ''Hata wakijikusanya watu (wote) na majini ili kuleta mfano wa hii Quran basi hawangeliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao''** ﴾. Bani Israil 88. ﴿**Na msipofanya – na hakika hamtafanya kamwe…** ﴾ Al Baqarah 24.

Tazama ukanusho huu uliokaziwa, bali hiyo ni hukumu ya milele! Je, Mwarabu anayejitambua anasema nini, anaweza kutoa hukumu hii na hali ya kuwa anajua kuwa wigo wa vitu vilivyosajiliwa baina ya warabu milango yake ipo wazi. Na kuwa mhakiki wa mwisho pindi atakapofanya utulivu katika kufuatilia kauli ya msemaji aliyetangulia, si aibu kwake kupata ndani yake mambo yaliyompita na yeye kuyadiriki; au akakuta upungufu naye akaukamilisha, au akakuta ukamilifu na yeye akauzidisha? Je, hakuwa akiogopa changamoto hii kuwa itachochea mihemko yao ya kifasihi na kwa hiyo watasimama kidete, kushindana naye na hali ya kuwa wote wanachukua tahadhari? Na kipi ambacho huenda akakifanya lau kama makundi ya wajuzi wa lugha (wana umbuji) wakakubaliana na mmoja wao. Wakatengeneza umbo pinzani. Kisha wengine wakalishughulikia kwa kiliboresha na kuliweka sawa.

Kama walivyokua wakifanya katika uhakiki wa mashairi. Kwa hiyo wa pili wao anakamilisha upungufu wa wakwanza wao na kuendelea hivyo hivyo. Mpaka watoe maneno ambayo, kama hayatoishinda basi kwa uchache

hayatakosa kuwa sawa nayo lau katika baadhi ya sehemu? Kisha basi lau angeitii nafsi yake na kutoa hukumu hii kwa watu wa zama zake tu. Sasa inakuwaje anaitoa hukumu hii kwa vizazi vijavyo vya mpaka siku ya kiama, tena kwa watu na majini? Kwa hakika ujasiri huu haufanywi na mtu anayejua uwezo wa nafsi yake ila kama ataufanya basi atakuwa ameijaza mikono yake kwa matendo ya qudura za Mungu na heri za mbinguni. Na hivyo hivyo, amezitoa changamoto hizo kwa ulimwengu wote. Na hilo likawa ni hukumu iliyokwishatolewa, ikizilenga akili na midomo. Na hakuna aliyesimama kukabiliana na changamoto hiyo ila alishindwa waziwazi na kufeli kwa kufedhehesha. Katika zama zilizopita na nyakati zilizopita.

3 – (Na mfano wa tatu) ni ile aya ambayo kwayo, Allah anamdhaminia Nabii wake kuwa atamlinda na kumpa amani katika maisha yake mpaka aufikishe ujumbe wa Mola wake: ﴿**Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi haukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu…** ﴾ Al Maidah 67.

Kwa hakika wa haya, naapa kwa Allah, ni dhamana isiyomilikiwa na mtu. Na huyo mtu, hata kama angekuwa mfalme mwenye kujizuia huku walinzi wakitembea pembezoni mwake, mbele yake na nyuma yake. Hivi ni wafalme watukufu wangapi tumewaona au wameonekana na watu wakitekwa na mikono yenye nguvu huku wakiwa katika misafara yao inayozungukwa na majeshi na walinzi. Lakini hebu tazama upeo wa kujiamini wa Mtume kwa sababu ya ahadi hii ya haki: Attirmidhiyyu na Al-Haakimu wamepokea kutoka kwa Aisha. Na Attwabraaniyu amepokea kutoka kwa Abuu Said Alkhudiriyyu amesema: **‘‘Mtume alikuwa akilindwa nyakati za usiku na iliposhuka aya hii aliacha kulindwa. Na akasema: Enyi watu! Ondokeni, kwa hakika Allah ameshanilinda’’**[1]

Na kweli kabisa, Allah alimlinda dhidi yao katika maeneo mengi yaliyokuwa ya hatari sana, na katika maeneo hayo kifo kilikuwa karibu sana

---

[1] Hadithi ya Aisha Allah amuwie radhi, imepokewa na Attirmidhiyyu katika Attafsiiru 3046, na Alhaakimu 2 / 313 na Albaaniyyu ameipa daraja ya hasan. Katika Swahih Attirmidhiyyu 2440. Ama hadithi ya Abuu Said Alkhudiriyyu, tamko lake **‘‘Abbasu alikuwa ni Ami ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, naye ni miongoni mwa wanaomlinda, basi ilipoteremka ﴿Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu ﴾ Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akaacha kulindwa’’.** Na Al-Haythamiyyu katika Majmau Azzawaaidi 7 / 17: ameieleza kuwa Imepokewa na Attwabraaniyyu katika Asswaghiiru na Al-Auswatwu, na ndani yake yupo Atwiya Al-Aufiyyu naye ni dhaifu أ هـ. Na pia Assuyuutwiyyu katika Adduraru Almanthuuru 2 / 529 ameiegemeza kwa Ibnu Mardawayhi

na yeye kuliko kamba za viatu vyake. Na yeye katika matukio hayo hakuwa na mlinzi zaidi ya Allah peke yake.

Na miongoni mwa matukio hayo ni yale yaliyopokelewa na Ibnu Hibbaani katika Swahihi yake kutoka kwa Abuu Huraira. Na imepokewa na Muslimu katika Swahihi yake kutoka kwa Jabir amesema: **‘‘Tulipokuwa safarini na kufika katika mti wa kivuli, tulikuwa tunamwachia Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake na aali zake. Na pindi tulipokuwa katika eneo la Dhaatu Arriqaau, Mtume wa Allah alifikia chini ya mti na akatundika upanga wake mtini. Ghafla mtu mmoja miongoni mwa washirikina alimjia na kuuchukua upanga wake na kuutoa katika ala na kumwambia Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Je, waniogopa? Akasema: Hapana. Akasema: ni nani atakuzuia na mimi? Akasema: Allah atanizuia dhidi yako. Weka upanga. Naye akauweka’’**[1]. Na yakutosha kujua kuwa usalama huu ulikuwa katika vile vita vilivyoanzishwa ndani yake swala ya hofu.

Na miongoni mwa matukio makuu ya kusadikisha habari hii ya haki, tukio hilo la kushtusha lililomsimamisha Nabii katika vita Hunaini. Akiwa peke yake baina ya maadui. Waislamu wameondoka na kumpa mgongo. Mtume akaanza kumkimbiza nyumbu wake kuelekea upande wa adui. Na Abbas bin Abdulmutwalibi akishika hatamu zake akizuia matakwa yake asiharakishe. Washirikina wakaja kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake na aali zake. Na walipomzingira hakuwakimbia wala hakuinamisha macho bali aliteremka kutoka katika nyumbu wake kana kwamba anajipeleka mwenyewe kwao wao. Akaanza kusema: **‘‘Mimi ni Nabii si uongo. Mimi ni mtoto wa Ibnu Abdulmutwalibi’’.** Kana kwamba anawapa changamoto na kuwajulisha sehemu alipo. Na naapa kwa Allah hakupatwa na chochote kibaya. Bali alitiwa nguvu na Allah kwa kumpelekea jeshi lake. Na kwa mkono wake, akaizuia mikono yao isimfikie. Hadithi hii imepokewa na Bukhariyyu na Muslimu kutoka kwa Albarraau bin Aazibi.

---

[1] Hadithi ya Jabir ni Muttafaq alayhi: Imepokewa na Bukhaariyyu katika Almaghaazii 4136, na Muslimu katika Swalaatu Almusaafiriina 311. Ama hadithi ya Abuu Huraira, yenyewe ipo katika Mawaaridu Adhwamaaani 1739. Na sikuikuta katika Al-Ihsaanu ila hadithi ya Jabiri 2883.

Na imepokewa na Muslimu kutoka kwa Abbas na Salama bin Al-Akuwaai, na pia imepokewa na Ahmad na Watu wa Sunani kutoka kwa wengineo.[1]

Na hivi hivi, Allah ameustarehesha umma wake, kwa hiyo hakumchukua kwake mpaka pale alipofikisha na kutekeleza amana aliyopewa. Na hadi pale Allah alipomteremshia kauli yake ﴿**… Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu…** ﴾ Al-Maidah 3.

**Pokea mfano wa aina ya pili [Mustakbali wa Waislamu: Chama cha Mwingi wa Rehema]:**

1 – Huko Makka Quran ilikuwa ikiwasimulia waislamu habari za Mitume zinazothibitisha vifua vyao. Na kuwaahidi wao kuwa watapata amani na ushindi uliokuwa kwa wale wa kabla yao. ﴿**Na bila shaka neno letu limekwisha kutangulia kwa waja wetu waliopewa Utume. Ya kuwa wao ndio watakaonusuriwa. Na kuwa jeshi letu ndilo litakaloshinda** ﴾. As-Saaffat 171 – 173. ﴿**Bila shaka sisi tunawanusuru Mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi (kushuhudia amali za viumbe** ﴾. Al-Muumin 51. Na pindi walipohamia Madina wakikimbia kwa ajili ya dini yao kuepuka fitina, huku wakiwa wanadhani kuwa wamepata sehemu yao ya amani kule walipohamia.

Lakini wao, haukupita muda wakashambuliwa kivita kutoka kila upande. Kwa hiyo wakatoka katika hofu na kwenda katika hofu kubwa. Na matumaini yao yote yakawa: ije siku ambayo wataweka chini silaha zao. Na katika nyakati hizi ngumu, Quran inawazindua juu ya yale yatakayokuwa kwao wao kuhusu ukhalifa na ufalme. Zaidi ya amani na utulivu, ni nini hiki? Je, ni ndoto na matumaini? Hapana, bali ni ahadi iliyokaziwa na kiapo: ﴿**Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada hofu yao…** ﴾ An-Nur 55.

---

[1] Hadithi ya Albarraau bin Aazibu imepokewa na Bukhariyu na Muslimu: Bukhariyyu ameipokea katika Almaghaazi 4315, 4316 na 4317. Na Muslimu katika Al-jihadi Na Assayri 78, 79, na 80. Na vile vile Attirmidhiyyu ameipokea katika Aljihadi. Ama hadithi ya Abbas yenyewe ipo kwa Muslimu katika Aljihadi 76, na hadithi ya Salama bin Al-Akuwai ipo kwa Muslimu katika Aljihadi 81. Na Ahamad ameipokea kutoka kwa Abdullah bin Masuudi 1 / 453.

Alhaakimu amepokea hadithi na kuipa daraja ya usahihi, kutoka kwa Ubayyu bin Kaabi amesema: **‘‘Pale Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, aali wake na maswahaba wake, walipofika Madina walipokelewa na Maanswari. Basi warabu kwa pamoja wakawavurumishia mapigo. Wakawa hawalali ila na silaha zao, wala hawaamki ila na silaha zao. Wakasema: Je, mnaona kuwa sisi tutaishi mpaka ifike siku ambayo tutalala kwa amani na utulivu hatuogopi chochote isipokuwa Allah? Hapo hapo ikateremka haya hii’’**.[1] Na imepokewa na Ibnu Abuu Haatimu kutoka kwa Albarraau amesema: **‘‘Aya hii imeteremka na hali ya kuwa sisi tupo katika hofu kubwa’’**.[2]

Hebu tazama namna fasili yake ilivyokuja katika maana yake pana, katika zama za Maswahaba wenyewe, walioelezwa kwa mdomo juu ya kauli ya Allah ﴿**Miongoni mwenu** ﴾ akawabadilishia baada ya hofu yao wakapata amani isiyo na hofu. Na wakawa makahalifa (viongozi) katika nchi na ardhi na wakayarithi maeneo ya mashariki na magharibi.

Na itafakari uzuri kauli yake katika aya hii ﴿**Na kufanya vitendo vizuri** ﴾ na kauli yake katika aya nyingine ﴿**… Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda. Wale ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi husimamisha sala na wakatoa zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mambaya…** ﴾ Al-Hajj 40 – 41. Utakuta ndani yake kuna habari nyingine juu ya siri wanayojaribiwa nayo waumini nyakati nyingine, miongoni mwazo ni kunyakuliwa kwa ardhi zao na kusalitiwa na maadui zao. ﴿**Nyinyi – ulipokufikieni msiba ambao nyinyi mmekwisha watia (maadui) mara mbili ya huo – mnasema: ‘‘Umetoka wapi huu?’’ Sema: ‘‘Huo umetoka kwenu wenyewe.’’…** ﴾ Aali Imran 165. ﴿**Hayo (ya kuwafika balaa hizi) ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, mpaka wabadilishe wao yaliyomo nyoyoni mwao…** ﴾ Al-Anfal 53.

---

[1] Imepokewa na Alhaakimu 2/ 401. Na Alhaithamiyyu akasema katika Almajimau 7 / 83: Imepokewa na Attwabaraaniyyu katika Al-Auswatwi na wapokezi wake ni watu wa kuaminika أ هـ. Na Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 5 / 100 ameiegemeza kwa Ibnu Almundhiru na Attwabaraaniyu katika Al-Auswatwu. Na Alhaakimu na ameipa daraja ya sahihi. Na Ibnu Mardawayhii na Albayhaqiyu katika Addalaailu. Na Addhiyaau katika Almukhtaaratu.

[2] Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 5 / 100 ameiegemeza kwa Ibnu Abuu Haatimu na Ibnu Mardawayhi.

**2 – (Na mfano mwingine):**

Waislamu walizuiwa wasiingie Makka katika mwaka wa Hudaibiya. Na Makurayshi waliwawekea masharti ya kuwa watakapokuja katika mwaka ujao, basi waingie Makka wakiwa bila ya silaha yoyote ila mapanga tu yakiwa katika ala. Je, ilipaswa kwa Waislamu wawaamini washirikina kuwa watatekeleza ahadi yao, huku hao washirikina wakiwa wameshatengua ahadi kibao, wameshakata udugu na wameshavunja mambo ya Allah? Je, leo hii sio wao washirikina ndio wanaozuia vichinjwa vya waislamu visifike sehemu yake ya kuchinjwa? Ni lipi ambalo hao washirikina watalifanya hiyo kesho? Hata kama wao ni wakweli katika kuwawezesha Waislamu kuingia Makka, lakini vipi Waislamu wawe na amani kwa upande wao pale watakapoingia kwao, katika mji wao huku wakiwa bila ya ngao wala silaha zao.

Je, haya hayawi vitimbi vinavyokusudia kuwavuta kidogo kidogo na kuwatumbukiza mtegoni? Na alama ya hilo ni kuwa wao wamewawekea masharti ya kutokuwa na silaha ila mapanga yaliyo katika ala tu. Na hayo mapanga ni silaha ambayo huenda Waislamu wakapata utulivu kwa ajili yake, ya kwamba wao hawatopatwa na mikono ya washirikina wala mikuki yao. Lakini yenyewe ni silaha ambayo ukiwa nayo haitoi usalama wa kutopatwa na mishale yao na maguruneti yao! Katika mazingira haya yenye kutia shaka mno, inawajia ahadi ya kukata kabisa juu ya mambo matatu yaliyo kwa pamoja: Kuingia Makka, Amani na Kutekeleza mambo ya Ibada. ﴿**Kwa yakini Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ndoto yake ya haki: Bila shaka nyinyi mtaingia katika msikiti Mtukufu In shaa Allah kwa salama; mkinyoa vichwa vyenu na mkipunguza nywele (kama ilivyo wajibu kufanya hivyo wakati wa Hija). Hamtakuwa na hofu…** ﴾ Al-Fat-h 27. Naam, wakaingia Makka katika umra ya kulipia wakiwa na amani na wakakaa hapo siku tatu mpaka walipotimiza umra yao na ibada zao.. Hadithi hii imetolewa na Bukhariyyu na Muslimu.[1]

**3 – (Na mfano wa tatu):** Washirikina walikuwa wakifanya midahalo na Waislamu huko Makka kabla ya kuhama. Wakiwaambia Waislamu: Kwa hakika Warumi wanashuhudia ya kuwa wao ni watu waliopewa kitabu. Na wameshindwa na wamajusi (watu wa Iran ya zamani). Na nyinyi Waislamu mnadai eti nyinyi mtatushinda sisi kwa kitabu ambacho kimeteremshwa

---

[1] Maelezo ya wapokezi wa hadithi hii yameshatangulia katika Uk wa 31 wa matini chanzi!

kwenu. Tutakushindeni kama wafursi walivyowashinda warumi. Ndipo ikateremka aya ﴿**Alif Laam Mym. Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu. Nayo ni Shamu); nao baada ya kushindwa kwao, watashinda. Katika miaka michache;…** ﴾ Ar-Rum 1 – 4.

Kwa hakika habari za kutokea kwa ushindi huu kwa muda ulioainishwa zilikuwa ni habari za mambo mawili, kila moja katika hayo yapo nje ya uwezo wa dhana za watu. Hivyo ni kwa kuwa dola la warumi lilikuwa limeshafikia udhaifu wa kiwango kinachotosha kusema ni dalili ya kuwa imepigwa nyumbani kwake na kushindwa katika miji yake, kama alivyosema Allah Mtukufu**:** ﴿**Katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu. Nayo ni Shamu** ﴾**.** Hakukuwa na yeyote anayedhani kuwa warumi watasimama tena baada ya hapo. Na hatari zaidi, ni kuainisha muda ambao warumi watakuwa na ushindi. Na kwa ajili hiyo, washirikina waliona kuwa hilo ni uongo na *wakabeti* (wakaamini) juu ya kuona kuwa hilo ni uongo.

Lakini Quran haikutosheka na hizi ahadi mbili tu, bali ilikazia ahadi mbili hizo kwa ya tatu, pale inaposema**:** ﴿**… Na siku hiyo Waislamu watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu (atakayowapa wao. Nayo ni kuwashinda Makureyshi siku hiyo)…** ﴾ Ar-Rum 4 – 5. Hii ni ishara ya kuwa katika siku ambayo warumi watawashinda wafursi, siku hiyo hiyo Waislamu watapata ushindi dhidi ya washirikina. Ijapokuwa kila ushindi mmoja kati ya hiyo miushindi miwili, wenyewe ulikuwa unaonekana kwa watu wengi ni mgumu mno kutokea. Je, vipi iwepo dhana ya kutokea kwa ushindi huo tena ukiwa umeambatana katika siku moja? Kwa ajili hiyo, ahadi hiyo ilisisitizwa ukubwa wa kusisitizwa kwa kauli yake: ﴿**Hii ni) ahadi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake, lakini watu wengi hawajui** ﴾**.** Ar-Rum 6.

Na hakika Allah amesadikisha ahadi ahadi yake. Warumi wakatimiza ushindi wao dhidi ya wafursi ndani ya muda wa chini ya miaka tisa[1], na hii

[1] Huenda msemaji akasema: Mbona Quran haikuainisha idadi ya miaka kwa tamko la wazi kabisa kuliko tamko la Bidh'i lenye maana ya nambari zilizopo baina ya tatu na tisa. Je, huyo Allah hajui siku, saa na hata mwaka halisi wa ushindi? Tunasema: sivyo hivyo. Lakini watu katika istilahi zao za kihesabu hawaendi kwa njia moja. Wapo miongoni mwao wanaohesabu kwa kutumia jua, na wengine wanahesabu kwa mwezi, na wengine wanakamilisha sehemu na wengine wanaziacha. Kwa hiyo muktadha wa hekima ni kuelezea kwa tamko la kweli kwa kila makadirio ili liwe ni la kukata kwa kila utata. Na liwe mbali likiepukana na mijadala na ubishi wote. Kisha huenda jambo la kupeana

ni kwa makubaliano ya wanahistoria wote. Na siku ya ushindi wao ndio siku hiyo hiyo iliyotokea ushindi wa Waislamu dhidi ya washirikina katika vita vya Badri Kuu. Kama ilivyopokewa na Attirmidhiyyu kutoka kwa Abuu Said[1]. Na Attwabariy ameipokea kutoka kwa Ibnu Abbas na wengineo[2].

Na hii ni miongoni mwa mifano ya aina ya tatu: [**Mustakbali wa wenye inadi**]:

1 – **{{Watu wa Makka walimuasi Nabii rehema na amani ziwe juu yake na aali zake. Akawaombea ukame kama ukame wa Yusuf'}}.** Hebu tazama kilichosemwa na Quran katika kuitika dua hii ﴿**Basi ingoje siku ambapo mbingu zitakapoleta moshi ulio dhahiri. Utakapowafunika watu; (wawe wanasema): ''Hii ni adhabu iumizayo''** ﴾. Ad-Dukhan 10 – 11. Kilitokea nini? **{{walipatwa na ukame mkali mpaka wakala mifupa, na mtu miongoni mwao alikuwa akitazama mbinguni, na kutokana na mashaka aliyonayo anaona kuwa kilichopo baina yake na mbingu ni kitu chenye umbo kama vile moshi]].** Imepokewa na Bukhariyu kutoka kwa Ibnu Masuud[3]. Kisha tazama kauli yake baada ya hapo ﴿**Kwa yakini sisi**

---

bishara njema na ushindi wenyewe vikachelewa, na pakatokea tofauti za wenye kuhesabu katika kuainisha muda ambao utaegemezewa nusra na ushindi. Na kwa hiyo, imekuwa vizuri kuelezea kwa tamko (katika miaka michache kati ya mitatu na tisa) bila ya kusemwa ni baada ya hiyo miaka michache kati ya mitatu na tisa. [Daraazu].

[1] Hadithi ya Abuu Said imepokewa na Attirmidhiyyu katika Tafsirul Quran 3192. Na Albani akaipa daraja ya usahihi katika Swahihu Attirmidhiyyu 2550. Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 5 / 290 ameiegemeza kwa Attirmidhiyyu na Ibnu Jariri na Ibnu Almundhiri na Ibnu Abuu Haatimu na Ibnu Mardawayhi.

[2] Hadithi ya Ibnu Abbas vile vile imepokewa na Attirmidhiyyu katika Tafsirul Quran 3193. Na Albani akaipa daraja ya usahihi katika Swahihu Attirmidhiyyu 2551. Na imepokewa na Attwabariy katika 21 / 16. Na katika hadithi ya Abuu said iliyotangulia, na ibnu Abbas ametaja kuafikiana baina ya vita vya Badri na ushindi wa warumi. Vile vile ameipokea Ahmad katika Almusnadu 1/276 pasi na kutaja Badri. Na kupata upana wa habari hizi rejea Adduraru Almanthuuru 5 / 288.

[3] Hadithi ya Ibnu Masuud ipo katika sababu ya kuteremka suratul Ad-Dukhaan. Imepokewa na Bukhariyyu katika Attafsiiru 4821, 4822 na wengineo. Na imepokewa na Muslimu katika Swifatu Almunaafiqiina 39, 40.

Pia kuna kauli nyingine katika tafsiri ya suratul Ad-Dukhaan. Maswahaba na wanazuoni wengi wamepita mapito ya kuwa tukio la moshi ni alama miongoni mwa alama za Allah na lenyewe litatokea kabla ya siku ya kiama kwa muda mchache. Na huo moshi ni miongoni mwa alama za kiama. Na hili wakalitolea ushahidi kwa hadithi miongoni mwazo ni:

- Hadithi ya Abuu Maaliki Al-Ash-ariyu: Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: **{{Hakika Mola wenu amekuonyeni mara tatu: Moshi utakaompata muumini kama mafua. Na kumpata kafiri avimbe mpaka huo moshi umtoke katika usikivu wake [yaani masikioni]. Ya pili ni mnyama. Na ya tatu ni Dajjali}}.**

**tutaiondoa adhabu kidogo (lakini) nyinyi mtarudia (makosa yenu). Na (wakumbushe) siku tutakayoshambulia mshambulio mkubwa: bila shaka sisi ni wenye kutesa (kweli kweli)**. Ad-Dukhan 15 – 16. Utaona ndani yake kuna tabiri tatu nyingine:

- Kuwaondolea adhabu. UK 55
- Kisha wao wakarejea katika vitimbi vyao viovu.

---

Imepokewa na Attwabariy 25 / 114. Na Haafidhu ibnu Kathiiri amesema kuhusu hadithi hii katika Tafsiri 7 / 235: na imepokewa na Attwabaraniyyu… na wapokezi wana daraja ya jayyidi أهـ. Vile vile Assuyuutwiyyu ameielezea katika Adduraru Almanthuuru 5 / 745 ila Alhaafidhu Ibnu Hajari ameipa daraja ya udhaifu katika Alfat-hi 8 / 436.

- Hadithi ya Abdullah Ibnu Abuu Mulaykat amesema: **{{Siku moja mapema nilienda kwa Ibnu Abbas Allah amuwie radhi na baba yake akasema: Usiku sikulala kabisa hadi kumekucha. Nikamuuliza: Kwa nini? Akasema: walisema imechomoza sayari yenye mkia. Nikaogopea isije ikawa ndio ule moto ndio ushagonga hodi. Kwa hiyo sikulala hadi kunakucha}}.** Imepokewa na Attwabariy 25 / 113. Na Ibnu Kathiir katika tafsiri yake 7 / 235 ameiegemeza kwa Ibnu Abuu Haatimu kutoka kwa Ibnu Abbas kama hiyo kisha akasema: na isnadi hii hadi kwa Ibnu Abbas mtaalamu wa umma na mfasiri wa Quran ina daraja ya usahihi. أهـ. Na Assuyuutwiyyu katika Adduraru Almanthuuru 5 / 744 ameiegemeza kwa Abdullah bin Humaid na Ibnu Jariiri na Ibnu Almundhir na Ibnu Abuu Haatimu na Al-Haakimu kwa sanadi sahihi.
- Ibnu Abbas amesema: **‘‘Ibnu Masuud amesema: Adhabu kubwa ni siku ya Badri. Na mimi ninasema hiyo ni siku ya kiama’’**. Imepokewa na Attwabariy 25 / 117 na Ibnu Kathiir katika tafsiri yake 7 / 237 akasema kuhusu hadithi hii: Isnadi yake ni sahihi kutoka kwake أهـ. Na Assuyuutwiyyu katika Adduraru Almanthuuru 5 / 745 ameiegemeza kwa Abdu Ibnu Hamiid na Ibnu Jariir kwa sanadi sahihi.
  Na tamko lililowazi zaidi kuliko yote hayo juu ya kuthibitisha kuwa moshi ni alama ambayo bado haijakuja:
- Hadithi ya Abuu Surayhat Hudhaifatu Bin Usayd amesema: **{{Mtume rehema na amani ziwe juu yake alitutokea huku sisi tukiwa tukijikumbusha. Akatuuliza: mnajikumbusha nini? Wakasema: tunajikumbusha kiama. Akasema: kwa hakika chenyewe hakitosimama mpaka muone alama kumi kabla yake akazitaja: Moshi – Dajjalu – Mnyama – Kuchomoza kwa jua upande wa magharibi – kuteremka kwa Issa mwana wa Maryam – na Yaajuuju Wamaajuuju – na kupatwa kwa mwezi mara tatu: kupatwa maeneo ya mashariki na kupatwa maeneo ya magharibi na kupatwa maeneo ya peninsula ya Uarabuni – na alama ya mwisho wao ni moto utokao pande za Yemeni utakaokuwa unawafukuza watu hadi katika sehemu yao ya kukusanywa}}.** Imepokewa na Muslimu katika Alfitani wa Ashiraatwu Assaa-ati 39, 40.
- Na kutoka kwa Abuu Huraira, kwa hakika Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: **{{Harakisheni kufanya mambo (kabla ya mambo) sita: Kuchomoza kwa jua kutoka magharibi. Au Moshi, au Dajjalu, au Mnyama, au jambo maalum la mmoja wenu [umauti]. Au jambo la wote [Kiama] }}.** Imepokewa na Muslimu katika Alfitani wa Ashiraatwu Assaa-ati 128.

- Kisha kuwalipizia kwa kuwatesa baada ya hayo.

Na yote haya matatu yalitokea kama yalivyobainishwa na hadithi sahihi iliyotajwa. Kwani wao pale walipomjia Mtume wa Allah wakimuomba awaombee mvua huku wakinyenyekea kwa Allah**: ﴿‘‘Mola wetu! Tuondolee adhabu (hii) hakika tutaamini’’﴾.** Ad-Dukhan 12. Allah akawanywesha hadi ardhi ikatota. Lakini wao, kwa haraka mno walirejea katika uovu wao na kibri chao. Ndipo Allah akawapa adhabu kubwa siku ya Badri[1]. Ambapo watu wao sabini waliuawa, na wengine sabini walitekwa.

Kwa hakika habari za huku kulipiziwa kisasa katika Quran ya kipindi cha Makka zimejirudia kwa namna nyingi:

- Wakati mwingine zinakuja kwa ujumla kama katika kauli yake: ﴿**… Wala msiba hautaacha kuwapata wale waliokufuru kwa sababu ya yale waliyoyafanya, au utashuka karibu na nchi zao, mpaka ifike ahadi ya Mwenyezi Mungu…** ﴾ Arraad 31.

Na kauli yake ﴿**Basi waachie mbali kwa muda mdogo (tu hivi). Na watazame tu; nao sasa hivi wataona** ﴾**.** Assaaffat 174 – 175.

- Na wakati mwingine inaainisha aina ya adhabu; nayo ni kuwa watashindwa katika vita. Kama katika kauli yake ﴿**Waambie: ‘‘Wingi wao huo karibuni hivi utaendeshwa mbio na watageuza migongo (wanakimbizana** ﴾ Al-Qamar 45.[2] Na hili kama unavyoliona ni miongoni mwa habari za maajabu ya huko Makka. Kwani kulikuwa hakuna nafasi asilani, ya kufikiria vita na kukutana na makundi. Na zaidi, eti kutegemea hao maadui watakimbia na kushindwa. Mpaka ikafikia kwa **‘‘Omar Allah amuwie radhi, ilipoteremka aya hii alikuwa akisema: ni kundi lipi hili? Akasema, basi ilipokuwa siku ya vita vya Badri nilimuona Mtume rehema na amani ziwe juu yake akilisema hilo kundi’’**. Imepokewa na Ibnu Abuu Haatimu na Ibnu Mardawayhi. Na kipande chake cha mwisho kipo katika Swahihi mbili[3].

---

[1] Hurejewa Kauli ya Ibnu Abbas mfasiri wa Quran, hakika adhabu kubwa ni siku ya kiama katika pambizo uk 54.

[2] Na mfano wake ni ile habari iliyokuja katika suratul Al-Muzzammil nayo ni miongoni mwa aya zilizoteremka mwanzo Makka ﴿**Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa na wengine watasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila ya Mwenyezi Mungu, na wengine watapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu…** ﴾ Al-Muzzammil 20. [Daraazu].

[3] Imepokewa na Attwabariy 27 / 108, na Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 6/184 ameiegemeza kwa Abdulrazak na Ibnu Abuu Shaybat na Ibnu Raahawayhi na

- Na wakati mwingine inaeleza juu sehemu maalumu za matukio katika hilo – na hili ni ajabu mno na la kushangaza sana – kama ilivyo katika kauli yake kuhusiana na mtu Zaniimu[1] ambaye alikuwa akiisema Quran kuwa yenyewe ni ngano za watu wakale ﴿**Tutamtia kovu juu ya pua yake, (tutamdhalilisha** ﴾**.** Al-Qalam 16. Naam akakatwa na upanga puani kwake katika siku ya vita vya Badri. Na hiyo ikawa alama yake ya kuabishiwa kwa muda wote alioishi. Imepokewa na Attwabariy na wengineo kutoka kwa Ibnu Abbas[2].

**Na mfano wa habari hizi za makafiri wa Kikurayshi ni zile habari zilizokuja kuhusu makafiri wa kiyahudi**. Tazama namna Quran inavyosema kuhusu wao ﴿**Hawatakudhuruni (hao maadui zenu; khasa mayahudi) ila udhia (mdogo tu hivi) na kama watapigana nanyi basi watakupeni migongo (wakimbie); kisha hawatanusuriwa** ﴾**.** Aal Imran 111. Na hili lilifanyika. Kisha inasema: ﴿**Wamepigwa chapa ya dhila mahala popote wanapokuwako; ila (kwa kushika) kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu au kamba ya watu (wawasaidie; lakini wenyewe peke yao hawajitoshelezi)…**[3] ﴾ Aal Imran 112. Na inasema: ﴿**Na (wakumbushe)**

---

Abdullah Bin Humayd na Ibnu Jariir na Ibnu Almundhiri na Ibnu Abuu Haatim na Ibnu Mardawayhi kwa mfano wake. Ama kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika ngao baada ya dua yake ndefu katika Kubba imetolewa na Bukhariyyu katika Attafsiiri 4875, 4877, na Ahmad 1 / 329 nayo kwa Muslimu kwa ufupi ipo katika Aljihaad na Assayru 58.

[1] Lililo mashuhuri huyo ni Alwaliidu Bin Almughiira Almakhzuumiyu aliyeteremshiwa aya hii ﴿**Niache mimi na niliyemuumba peke yangu** ﴾ Al-Muddathir 11. [Daraazu].

- nimesema: Zaniimu: ni mtuhumiwa wa nasaba aliyeambatanishwa kwa kaumu naye si miongoni mwao. Na asili ya neno (Azzanamatu) ni kipande kilichozidi kinachoning`inia na kinachokuwa katika sikio la kondoo na chini ya koo lake. Na Ibnu Abbas amesema kuhusiana na Azzaniimu: **‘‘Huyo ni mtu miongoni mwa Makureyshi ana kipande kilichozidi kama kipande kilichozidi kwa kondoo’’**. Imepokewa na Bukhariyu katika Attafsiiru 4917.

[2] Imepokewa na Attwabariy 29 / 28 kwa sanadi dhaifu kutoka kwa Ibnu Abbas. Na Assuyuutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 6/394 ameiegemeza kwa Attwabariy na Ibnu Abuu Haatimu na Ibnu Mardawayhi. Na katika jambo maarufu ni kuwa Alwaliidu Ibnu Almughiira alikufa kabla ya vita vya Badri kwa kitambo kirefu.

[3] Al-Aluusi amesema katika Ruuhul Maan 4 / 29:

Yaani hawasalimiki na kudhalilika kwa hali yoyote ile ila wawe wanashikamana na dhima ya Allah Mtukufu au kitabu chake alichowaletea na dhima ya Waislamu. Kwa hakika wao, kwa kufanya hivyo, watasalimika na kuuawa, kutekwa wao, kutekwa wanawake wao na kumaliziwa mali أهـ [kwa ufupi].

Na mwenye Attahriiru Wattanwiiru amesema katika 4 / 55: na maana ya kupigwa chapa ya dhila ni kuwa dhila imeungana nao na kuwazunguka. Dhila imefananishwa na kuba au hema lililowafunika. Na neno ﴿**Popote wanapokuwako** ﴾ kwa asili maana yake wamechukuliwa katika vita. Na maana yake kwa hapa: popote watakapopatikana, yaani

**alipotangaza Mola wako (ya kwamba) atawaletea (Mayahudi) mpaka siku ya Kiama watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya…** ﴾ Al-Aaraf 167.

Ajabu ilioje kwa aya hizi! Je, zimetungwa kwa kufuatanisha herufi na maneno? Au zilikuwa ni minyororo iliyowekwa milele katika shingo zao. Na vyuma vya mishikaki iliyofungwa mikononi mwao na haina kufunguka? Je, huwaoni wao kuwa walikuwa wametawanyika maeneo ya mabonde mbalimbali wakati zilipotolewa hukumu hizi. Wakiwa madhalili katika kila makazi. Na hawajawahi kuwa na dola katika zama zozote miongoni mwa zama. Na katu hawajapatapo kukusanywa katika mji mmoja. Na wao leo hii, licha ya kuwa uchumi wao wa mali ni mkubwa mno kiasi cha kukaribia nusu ya uchumi wa dunia. Lakini bado wanaendelea kuwa wametawanyika, kupasuka pasuka na wameshindwa kujisimamishia kijidola kama vilivyo vijidola vidogo vidogo.[1] Bali utawaona wao katika miji ya kimagharibi ya kikristo wakipewa aina mbali mbali za kudogeshwa na kuadhibiwa. Kisha mwisho wao utakuwa kuhamishwa na kufukuzwa. Na huku miji ya Kiislamu – ni miji katika miji ya Allah iliyokunjua zaidi vifua vyake – kwa hakika inawakubali wao wawe kama raia wanaoongozwa na si viongozi wenye kutawala.

Na je, zimeshakujia habari zao za mwisho?

---

wao hawapatikani ila ni wahukumiwa kwa ukali wa dhila yao. Na kauli yake: ﴿**ila kwa kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu** ﴾**.** Ahadi ya Allah ni dhima yake, na ahadi ya watu ni washirika wao na wanaowanusuru. Na maana yake hawatosalimika na dhila ila pale watakaposhikamana na ahadi ya kutoka kwa Allah. Yaani dhima ya Kiislamu au pindi watakapotafuta kunusuriwa na makabila yenye nguvu kubwa. Ama wao kwa nafsi zao hawana kujinusuru. Na hili ni miongoni mwa dalili za utume. Kwani wayahudi walikuwa na nguvu (watukufu) huko Madina, Khaibari, Annadhiiru na Kuraydha kisha wakawa madhalili. Na udhalili ukawaenea katika maeneo mengine ya dunia. أ هـ. [kwa ufupi].

[1] Ustadhi Daraazu, Allah amrehemu, ameandika sehemu kubwa ya kitabu hiki kabla kidogo ya mwaka 1933 AD kama ilivyo katika utangulizi. Katika wakati huo hakukuwa na hata mwislamu mwenye kujihisi vibaya sana aliyediriki kuwaza kuwa ndani ya miaka kumi na mitano tu kutadhihiri dola ya kiyahudi, ambao ni ukweli wenye kuumiza miongoni mwa ukweli wa eneo hili. Na chini ya miongo miwili tangu watakapoipora Palestina, majeshi yote ya Kiarabu yatashindwa vibaya kusikokuwa na mfano katika historia ya kisasa. Na wayahudi wataitawala Jerusalemu, ukingo wa Magharibi, peninsula ya Sinai na milima ya Golani. Kisha wayahudi wataendelea kujitanua mashariki na magharibi. Yote hayo yatatimia kwa kamba ya watu… Ndio, lakini ni mbele ya vumbi kama vumbi la njiani. Nao si wengine bali ni waislamu wa siku hizi. Na hakuna mwenye hila wala mwenye nguvu isipokuwa ni Allah tu.

Ndoto zao zimewapambia eti katika (ardhi tukufu) wajifanyie dola ya jamii yao itakayohifadhi vizazi vyao vya kutoka maeneo mbalimbali ya dunia. Lengo ni kuwa, wakijiunga hapo na kuwa umma uliojaa nguvu na kuwa na muda mrefu hawatosumbuliwa na yeyote. Wanahangaika kunyanyua aibu hii ya kihistoria iliyo juu yao, kwa kurudisha ufalme wao wa kale katika miji hiyo. Na kwa mwanga wa matumaini haya, makundi kwa makundi miongoni mwao yameanza kuhamia maeneo hayo, wakiwa makundi makundi au mmoja mmoja. Na wakifika huko wakiwa wepesi au wazito… Je, wameweza kusonga mbele katika hatua yao hii ya kwanza – au huenda ikawa ya kwanza na ya mwisho – wakiwa wanategemea nguvu zao za ndani? Sivyo hivyo. Lakini wanategemea (kamba ya watu!!) Kwa hiyo unasema nini? Sema: Allah amesema kweli. Na ni nani aliyemkweli zaidi wa kuongea kuliko Allah. Na ama dhana yao wanayoidhani, nayo ni kuwa kwa kusongamana kwao na wakazi asilia katika ardhi zao na miji yao ndicho kinachowaandalia kuhakikisha kile wanachokiota juu ya ufalme wao na usultani wao, na hicho ndicho kilichoandikwa na *Khartwi Alqataad,* yaani hakiwezeni kuwa hivyo. Wanataka kubadilisha maneno ya Allah. Na hakuna wa kubadilisha maneno yake[1] ﴿**Au wanayo sehemu ya ufalme (wa**

---

[1] Hapa kuna kuwahi kuyadiriki maneno ya ustadhi Darazu, Allah amrehemu kuhusiana na maneno haya. Na kwa kutafakari vizuri katika Sura Bani Israili pale Allah anaposema ﴿**Na tukawafunulia Bani Israili katika (hicho) Kitabu (chao kuwa): ''Bila shaka nyinyi mtafanya uharibifu katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtatakabari kutakabari kukubwa.'' ''Basi itapofika ahadi ya (kulipwa kwa ajili ya uharibifu wa) kwanza wa hiyo miharibifu miwili, tutakuleteeni watu wetu wenye mapigano makali nao wataingia mijini mwenu kila upande. Na hii itakuwa ni ahadi itakayotimizwa.'' (Tatakuadhibuni tu maadamu mtafanya fisadi). ''Kisha tutakurudishieni nguvu zenu juu yao (hao waliokushindeni), na tutakuongezeeni mali na watoto na tutakufanyieni wenye kundi kubwa kuliko wao.'' ''Basi mkifanya wema, mnajifanyia nafsi zenu; na mkifanya ubaya, mnajifanyia nafsi zenu wenyewe. Na itakapofika ahadi ya (malipo ya uharibifu wa) mwisho tutakuleteeni watu wenye nguvu vilevile) ili wazidhalilishe nyuso zenu, na wauingie Msikiti kama walivyouingia mara ya kwanza. Na waharibu kuharibu kukubwa kabisa muda wa kukutawaleni.'' (lakini mkitengenea) huenda Mola wenu akakurehemuni; na kama mtarudia (mwendo wenu wa kuharibu, Sisi pia) tutarudia (kukuangamizeni).'' Na tumeifanya Jahanamu ni gereza kwa ajili ya makafiri** ﴾. Bani Israil 4 – 8. Na kwa kutazama vizuri katika Tafsiri na tofauti zake tunakuta yafuatayo:

- Mwenye Attahriiru Wattanwiiru (15 / 18 na kile kilicho baada yake) na majumuisho yake ni:
  Kitabu kilichotajwa katika aya hizi ni Isaya na Jeremia navyo vipo katika daraja ya pili katika Torati. Na hizo aya zinaashiria matukio makuu baina ya Wana wa Israeli na Maadui zao miongoni mwa nyumati mbili kuu, nazo ni: Wababeli na Warumi.
  - Mara ya kwanza: ni kutekwa na wababeli wakiwa chini ya Bukhusuntwari na wengineo 606 BC, 598 606 BC na tukio hilo kubwa kuliko lile la kabla yake. 588

606 BC 588 na katika tukio hilo walitekwa watu wote wa Yahudha na kuchomwa kwa hekalu la Suleimani na mji wa Jerusalemu (Mji wa Qudsi) ukaachwa ukiwa umeharibiwa vibaya mno.

- Mara ya pili: ni mfululizo wa vita vya Warumi baada ya kuwaonya kwa manabii wao: Malachi, Zakariya, Yahya, Issa. Kwa hakika ardhi iliwaendea vizuri kwao wao tangu 530 kabla ya kuzaliwa Kristo mpaka 330 BC. Kisha utawala wao ukadhoofika kidogo kidogo hadi wakaingia katika utawala wa Warumi mnamo mwaka 40 BC. Kisha wakajaribu kutoka lakini Mrumi Titus aliwaangamiza watu wengi na kuwatia utumwani na kuwateka wengi. Kisha likatokea pigo la nokauti kwa wayahudi kutoka kwa Mrumi Hadrianus mwaka 135 AD أهـ .

- Na wafasiri wengi wemepita mapito ya kuwa waharibifu wengi wa Kiyahudi waliotajwa katika aya hizo zilizotangulia walishapita tangu zama za kabla ya kupewa utume kwa Mtume Muhammad rehema na amani ziwe juu yake (hii ni kinyume na yule aliyewamaliza kwa ajili ya ufisadi wao wa kwanza: Goliath Al-Jazari au Sennacherib mfalme wa Mosul au Nebokadreza mfalme wa Babeli. Na ni nani huyo mwenye kumaliza ufisadi wa pili: ni Nebokadreza wa Babeli au Alexander wa Macedont au mfalme Khardushi au Warumi).
- Lakini baadhi ya wanazuoni wa tafsiri (mfano Attwabariy 15 / 44, Ibnu Ajauziyu 5 / 11. Al-Aluusiyu 15 / 21) wamepita mapito ya kuwa wayahudi waliporudia ufisadi katika zama za Mtume Muhammada rehema na amani ziwe juu yake, hilo lilikuwa linaingia katika kauli yake Allah Mtukufu: ﴿**Mkirudia tutarudia**﴾ yaani katika ufisadi basi yatajirudia kwao wao wala hayatoishia katika zile mara mbili tu zinazojulikana. Na miongoni mwa kauli hizo ni ile aliyoipita Qatada pale aliposema: Umma umerudia – yaani wayahudi – kufanya shari ya kile kinachowahudhuria. Allah akawapelekea adhabu na mateso. Kisha hatima ya hivyo ikawa ni Allah kuwapeleka kati eneo hili la warabu. Basi wayahudi wapo katika adhabu kutoka kwa warabu hadi siku ya kiama. Mwenyezi Mtukufu Aliyetukuka amesema katika aya nyingine ﴿**Na (wakumbushe) alipotangaza Mola wako (ya kwamba) atawaletea (Mayahudi) mpaka siku ya Kiama watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya….** ﴾ Al-Aaraf 167. Hivyo Allah akawapelekea katika eneo hili la warabu. Pia Qatada amesema ﴿'' (lakini mkitengenea) huenda Mola wenu akakurehemuni; na kama mtarudia (mwendo wenu wa kuharibu, Sisi pia) tutarudia (kukuangamizeni)...'' Wakarejea, na Allah akawapelekea Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. Kwa hiyo wao wanatoa kodi kwa mikono yao huku wakiwa wanyonge. Na Ibnu Abbas amepita mapito haya haya katika moja ya mapokezi yake. na vile vile Abdulrahmaan Bin Zaid Bin Aslama pia.
- Nilisema: na miongoni mwa yanayotia nguvu rai hii ni kile kilichotajwa na Attwabary na Ibnu Aljawziy ya kuwa neno ﴿Huenda ﴾ likitumiwa na Allah lina maana ya lazima kutokea. Assuyutwiyu amenukuu katika kitabu Al-Itiqaanu 2 / 241 kutoka kwa Abuu Haatimu na Albayhaqiyu na wengineo kutoka katika hadithi ya Ibnu Abbas amesema: (Kila neno ﴿**Huenda** ﴾ katika Quran maana yake ni wajibu). Pia Assuyutwiyu amenukuu kutoka kwa Shaafi kauli yake: (Husemwa ﴿**Huenda** ﴾ kwa Allah ni wajibu).
- Na Al-Aluusi amesema katika Ruuhu Almaaniy 15 / 21 : kwa hakika walirudia – yaani wayahudi – kumkadhibisha Nabii rehema na amani ziwe juu yake na walikusudia kumuua. Na Allah akarejea kuwasalitisha kwa kupitia Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Akawauwa wayahudi wa Quraydhwa na kuwahamisha wa Banii Annadhiiru na akawalipisha kodi waliobaki.
- Na katika mambo ya ajabu ni kukubaliana kwa wafasiri juu ya kuwa huko kufisidiwa mara mbili kwa wayahudi kumeshapita kabla ya kupewa utume kwa Muhammad

rehema na amani ziwe juu yake kama ubainifu wake ulivyotangulia. Licha ya kutokuwepo kwa andiko la kukata lililo la wazi kuhusu hilo katika aya za sura ya Bani Israil au nyingine au katika hadithi za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, zinazoainisha huku kufisidiwa kuwili, na kwa hiyo iwezekane kukata shauri juu ya kupita kwake. Bali andiko la Quran linaonesha uwezekano wa kuwa hayo yalipita hapo kabla, na pia kuna uwezekano wa kuwa moja wapo limeshapita na lingine bado halijakuja. Na pia yanawezekana yote mawili bado hayajafika [wakati wa kuteremka Quran kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake wakati wa Makka. Kwa sababu sura ya Bani Israili ni ya Makka].

- Pia kuna rai nyingine ambayo watu wake wanapita mapito ya kuwa ufisadi mmoja katika hayo mafisadi mawili kwa wayahudi umeshapita na mwingine bado haujakuja. Ama kitabu cha kwanza kinachoeleza rai hii ni kitabu: Aljama-aatu Al-Islamiya cha Sulaymu Al-Hilaaliyu na Ziyad Addabiiju chapa ya pili ya mwaka 1981 (uk 56 na kurasa za baada yake) na ufupisho wa rai hii ni kuwa:

- Aya zinathibitisha kuwa hayo maufisadi mawili kwa wayahudi. Wakati ambapo historia inatubainishia kuwa wayahudi wamefisidiwa mara nyingi wala haijathibiti kwao wao kurudiwa kwa wale waliowaonjesha wao adhabu.
- Tamko ﴿**Pindi** ﴾ linamaanisha maana ya kielezi cha wakati na ushariti kwa wakati ujao na sio uliopita.
- Na wakati ujao katika ﴿**Latufsidunna – Mtafanya uharibifu** ﴾. Hiyo **‘LA** na **NNA’** ni kwa ajili ya kukazia kwa wakati ujao.
- ﴿**Na hii itakuwa ni ahadi itakayotimizwa** ﴾: ni ahadi ya wakati ujao.
- Wale waliowapatia adhabu Wayahudi, hapo kabla hawakuwa wenye kuamini. Na hili ni kinyume na tamko ﴿**waja wetu** ﴾.
- Je, watu waliowadhalilisha wayahudi hapo kale je, wapo hadi sasa na wanaweza kurudia kufanya hivyo kwa wayahudi)
- Mwishoni mwa uharibifu wa kwanza kutakuwa na kuangamizwa kwa wazi kwa hali ya juu kwa ushahidi ﴿**Na waharibu kuharibu kukubwa kabisa muda wa kukutawaleni** ﴾**.**
- ﴿**Na tukakufanyeni wenye kundi kubwa kuliko wao** ﴾**:** Jambo la kutamani kuwa kundi kwa sasa ni kubwa kwa wayahudi.
- Vijineno FA na THUMMA katika hizo aya: vinamaanisha kuwa kurejea kwa hilo kutakuwa baada ya muda mrefu. Na kuwa huo uharibifu hautaendelea muda mrefu (hili linajulishwa na kineno FA ﴾.
- Uwepo kwa uharibifu mkubwa kwa wayahudi kila uga kwa sasa.
- Maelezo ya Quran juu ya kuingia kwa uharibifu wa pili: ni kuingia katika msikiti Mtukufu. Na katika mara ya kwanza ilikuwa bila ya hivyo. Kwa kuwa kuingia kwa mara ya kwanza kumeshakatika kwa wayahudi kuitawala Jerusalemu.
- Ushahidi wa neno ﴿**Kwa pamoja** ﴾ na katika ﴿**Tutakuleteni kwetu (kwetu tukuhisabuni) nyote pamoja** ﴾. Bani Israili 104. Na atakayetafakari vizuri tukio la kuhama kwa wayahudi kwenda ardhi ya palestina kwa sasa atapata ya kuwa uthibitisho wa maneno ya Allah Mtukufu. Huu ni ufupisho wa mtazamo wa kwanza na ataona kuwa baadhi ya matamko yanabebeshwa maana isiyostahiki kubebeshwa katika lugha ya Kiarabu. Isipokuwa wenyewe ni mtazamo wenye kima chake kwa kutazama yafuatayo:
  - a- kutokuwepo kwa andiko la kukata kabisa la Quran na kufichikana kwa andiko la hadithi za Mtume rehema na amani ziwe juu yake.
  - b- Ubabe wa wazi na uharibifu mkubwa kutoka kwa wayahudi kwa sasa ni mara mbili zaidi ya uharibifu uliotangulia.

c- Baadhi ya ushahidi mpya unaopatikana kutoka katika hizi aya: Kwa pamoja – kundi – vijineno vya kuunganisha…
d- Kutokutangulia kuwepo kwa rai hii, jambo ambalo linaifanya rai hii iwe inahitaji kufanyiwa utafiti na kuitazama upya.

Na mwishoni, mwenye mtazamo huu anazunguka baina ya malipo ya msasishaji aliyepatia au msasishaji aliyekosea. Na wote wawili hao wanapata thawabu kwa mapenzi ya Allah).

- Ama kitabu cha pili ambacho mwenye nacho anaonelea rai inayokaribiana na hiyo iliyotangulia, ni kitabu Al-Asaasu fii Attafsiiri cha Said Hawiy (juzu 6, uk 3036 na yaliyo baada yake, chapa ya kwanza mwaka 1985) na ufupisho wake ni:

- Uharibifu kutoka kwa wayahudi ni mwingi lakini ufisadi ulioambatana na ubabe mkubwa na dola ni mchache. Huenda kwao wao ubabe na dola bila ya uharibifu kama ilivyo katika zama za Daudi na Suleimani amani iwe juu yao.
- Yale yaliyomo sasa hivi kwa wayahudi miongoni mwa ubabe pamoja na uharibifu. Wao wana dola yenye kusimama na kuharibu.
- Inawezekana kuwa Nebokadreza ni mtu mwenye kumwamini Allah Mmoja aliyetiishwa na Allah kuwaadhibu wayahudi [Hili na lile la kuhusiana na wale wanaoibebesha na wale walioingia kwa mara ya kwanza ndio watakaoingia mara ya pili...
- Neno ﴿**akhera** ﴾ katika kauli yake ﴿**na itakapokuja ahadi ya akhera** ﴾ inawezekana likawa siku ya kiama, na inawezekana likawa katika ubabe wa pili wa kabla ya kuangamia.
- Uharibifu wa kwanza ndio uliosalitishwa kwao kwa kumtumia Nebokadreza pale jambo hilo lilipoambatana na kufanya uovu na kuchupa mipaka. Na haijapatapo kwa wayahudi kutangulia kupata maangamivu ya wazi na uharibifu mkubwa wa mfano wake.
- Pia kuna uwezekano wa huo uharibifu wa pili ndio huu tunaouishi sisi sasa hivi pamoja na kuchukua kidogo katika tamko ﴿**Akhera** ﴾ na tamko ﴿**kwa pamoja** ﴾ pamoja na kutazama kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Na tuliwafarikisha (Mayahudi) katika ulimwengu makundi mbalimbali** ﴾. Al-Aaraf 168. Kama ni hivyo, maana ya aya itakuwa: ya kuwa katika uharibifu wa pili tutakupelekeni Palestina ﴿**kwa pamoja** ﴾. Na wakati huo wao watasalitishiwa wale wa kabla nao ni Waislamu (tukichukulia kuwa Nebokadreza alikuwa Muislamu).
- ﴿**Na tukakufanyeni wenye kundi kubwa kuliko wao** ﴾**:** kiasi ambacho kinachoonekana sasa hivi ni uwezo wa Wayahudi wa kukusanya jeshi kubwa na kuusumbua ulimwengu wote kwa ajili hiyo.
- Pia kuna ufahamu mwingine wa aya hii.
  Kwa kuzingatia kwamba uharibifu wa mwanzo ni kule kujaribu kwao kupambana na Uislamu kisha ndipo kukatokea kuharibika kwa mwanzo nako ni Allah kuwafanya Waislamu wawaadhibu na kuharibu miji yao huko Madina, Khaibaru, Fadaku, Taymaau na miji mingineyo. Kisha kukatokea kujikweza kwao kwa pili na uharibifu baada ya mamia ya miaka, wakawa matajiri wanaoweza kuusumbua ulimwengu wote. Kisha ndipo Waislamu wawapatie, waziadhibu nyuso zao na kuurejesha msikiti wa Jerusalemu kama walivyouingia mara ya kwanza katika zama za Omar.
- Na kinaoneka kuwa kauli yake Mtukufu ﴿**Na tulisema baada yake** ﴾ Yaani baada ya Musa ﴿**Kuwaambia Wayahudi kaeni katika ardhi** ﴾ ardhi yote mkiwa mmetawanyika ﴿**na itakapokuja ahadi ya akhera, tutakuleteni nyote kwa pamoja** ﴾ Yaani kwa pamoja kuelekea Palestina. Kwani katika swala linalojulikana ni kuwa kutawanyika kunakowahusu Wayahudi wote kulikuwa baada ya kurudi kwao kutoka

**Mwenyezi Mungu; basi wanahamaki kwa nini kupewa mtu kitu pasina amri yao)? Basi hapo wasingaliwapa watu hata tundu ya kokwa ya tende ﴿.** An-Nisaa 53. Na Allah anawafahamu vizuri sana.

Tazama ajabu ya mambo ya utabiri wa Quran, namna unavyopasua pazia la wakati ujao wa karibu na wa mbali. Na inahukumu tabia za matukio kwa kuyaelezea nyakati zake na kuyadumisha. Na namna zama zinavyokuwa ni uthibitisho wa utabiri huo kwa uchache au zaidi. Na yale ya karibu na ya mbali?

Lakini pia tazama jumla ya yale yaliyomo katika Quran kwa upande wa kutoa kwake habari na namna Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na aali wake anavyoshughulikia yale yaliyo nyuma ya hisia zake na akili zake katika habari zilizokuwa na zitakazokuwa na zile zilizopo. Namna ambavyo Quran, kila inavyotusimulia kuhusiana na mambo yaliyopita. Basi yanasadikishwa na ushahidi wa kihistoria. Kila inapotusimulia kuhusu wakati ujao, basi inasadikishwa na usiku na mchana. Na kila inapotusimulia

---

Babeli. Kwa hiyo kuadhibiwa kwa kwanza ni kwa kupitia Nebokadreza. Na kwa pili ndiko kunakotarajiwa sasa hivi. أهـ kwa muhtasari.

- Na ndani ya hayo yaliyopita inatakikana kwetu sisi tuwaadhike na kuzingatia yale yaliyotokea kwa Wayahudi:
  Pale Allah alipoteremsha ufunuo kwa Wayahudi waliukubali. Na kwa hilo wakawa na kutengenekewa na kufaulu. Kisha zama zikawa ndefu kwao, wakakufuru na kuchupa mipaka. Kwa hiyo wakastahiki adhabu ya Allah ambayo huenda ikawajiwa kutoka mikononi mwa watu wasio na huruma nao. Kisha wakatubia na kujirekebisha na Allah akawaondolea balaa. Basi wote na tuikumbuke kauli ya Allah Mtukufu ﴾**mkirejea tutarejea** ﴿
- Kwa hakika Allah ameuteremshia umma huu wa Kiislamu na kuuridhia uwe dini kwa wanadamu wote mpaka kusimama kwa Kiama, na kuwaamrisha waingie katika dini kikamilifu ﴾**Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuate nyayo za Shetani** ﴿ Albaqarah 208. Wakaitukuza amri ya Mola wao na Allah akawatoa katika kiza kwenda katika nuru, na akawafanya kuwa umma bora uliotolewa kwa ajili ya watu. Na akawafanya ni watu watukufu. Kisha wakatulizana duniani na kufuata hatua za shetani na kujiweka mbali na ufunuo wa Allah katika matendo yao, habari zao, siasa zao, uchumi wao, tabia zao na malezi yao. Allah akawasalitishia ndugu wa manyani na nguruwe wakawa wanachukua ardhi zao na kuwaonesha udhalili. Na nyumati zote za duniani zikaja zikijipatia chochote katika dhifa hiyo. Na wakasalitishiwa udhalili na unyonge. Na katika hili kuna onyo la Allah hadi yule anayefanya mchezo arejee katika mstari, na mwasi atubu, na aliyeghafilika azinduke na kwa hiyo umma uamke kwa mara ya pili na kuhakikisha ujumbe wake unawafikia ﴾**Wale ambao ukiwamakinisha, (tukiwaweka vizuri) katika ardhi husimamisha swala na wakatoa zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu** ﴿**.** Al-Hajj 41.

kuhusu Allah na Malaika wake na mambo yaliyofichikana, basi yanasadikishwa na Manabii na Vitabu.

Kisha iulize nafsi yako baada ya hapo. ***Je, unamuona mtu huyu asiyejua kusoma na kuandika amekuja na hadithi hii yote kutoka katika nafsi yake?***

Utaisikia ikikupa jibu la kimaumbile lisilo na shaka ndani yake likisema (Kwa hakika hapana budi kuwa yeye amezinywa habari hizi kutoka katika chanzo cha kielimu kilichothibitishwa na kutegemewa kwa kupitia kwa upana na utafiti wa kina. Na haiwezekani habari hizo zote ziwe zimezaliwa na akili zake na zao la uerevu wake na uhodari wake). Na kama si hivyo, uerevu huo u wapi, au uhodari huo u wapi. Aliopewa katika zama zake, awe amekingwa na makosa katika dhana zake zote katika kuyafunua matukio yaliyopita, vyovyote yatakavyokuwa yametangulia muda mrefu, na habari za wakati ujao vyovyote zitakavyokuwa za mbali?

[D – **Nabii bila ya ufunuo**

**wakati mwingine huenda akakosea dhana yake licha ya uerevu na utambuzi wake**]

Kwa hakika Manabii wenyewe – na wao ni wa tabaka la juu kwa uerevu na utambuzi kwa ushuhuda wa watu wote – hawakupata katika zama zao ahadi hii kwa matukio ya karibu yao. Kwa hakika wao, ukitoa ufikishaji wa ufunuo, wakati wanapojitahidi kwa rai zao kuhusiana na mambo yaliyofichikana katika vikao vyao, wakati mwingine utambuzi wao unapatia na wakati mwingine unakosea. Na huyu hapa ni Yakubu amani iwe juu yake tunamuona akiwatuhumu watoto wake pale walipomjia na damu ya uongo katika kanzu yake. Kisha anarudia na kuwatuhumu tena pale alipoambiwa kuwa mtoto wake ameiba. Anawaambia katika mara zote hizo ﴿**Bali nafsi zenu zimekuzainishieni jambo (kumfanyia mwenzenu) basi langu mimi ni subra njema** ﴾ Yusuf 18 na 83. Kwa mara ya kwanza amepatia. Lakini kwa mara ya pili amewatuhumu na hali wao hawana kosa. Na huyu hapa ni Musa amani iwe juu yake. tunamuona akimwambia mja mwema ﴿**Akasema: ''akipenda Mwenyezi Mungu utaniona mvumilivu, wala sitaasi amri yako''** ﴾**.** Al-Kahf 69. Kisha anasahau na hawezi kuwa na subra pamoja naye wala hatii jambo lake.

Na huyu hapa ni Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na aali zake, huenda watu walikusudia kumpotosha katika hukumu. Kwa hiyo anamlinda muovu kwa kumdhania kuwa hana kosa. Mpaka anapojulishwa na Mjuzi Mwingi wa habari.

Kama ukiwa na shaka na hilo hebu isome kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Wala usiwe mwenye kuwatetea wale wafanyao khiyana. Na mwombe Mwenyezi Mungu maghufira. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu ﴾.** An-Nisaa 105 – 106. Kwa hakika kuna hadithi sahihi ya sababu ya kuteremka aya hii: **{Usiku mmoja mwizi alipita katika mashriba[1] (chumba) cha mtu mmoja miongoni mwa Maanswari (watu wa Madina) aitwaye Rifaa. Akavunja chumba chake na kuiba yaliyomo ndani yake miongoni mwa  chakula na silaha. Na ilipofika asubuhi, yule Muanswari hakuviona vitu vyake mpaka akayakinisha kuwa hivyo vitu vipo katika nyumba ya ukoo wa Abriiqu. Na minngoni mwao kulikuwa na wanafiki. Basi akamtuma mtoto wa ndugu yake aende kwa Mtume kuwashtaki. Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake akasema: nitalitazama. Ukoo wa Abriiqu uliposikia hilo walienda kwa Nabii na kumwambia: Ewe Mtume wa Allah. Kwa hakika Qatada bin Nuumani na ami yake Rifaa wamewakusudia watu wa nyumba yetu. sisi ambao ni watu wa Waislamu na tuliotengenekea, wanatuvurumishia kuwa sisi ni wezi bila ya kuwa na kidhibiti wala uthibitisho. Kisha Qatada naye akaja, na Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake akamwambia: Ewe Qatada umeikusudia nyumba ya watu wanaotajwa kuwa ni Waislamu wazuri waliotengenekea na kuwavurumishia kuwa wameiba bila ya uthibitisho wala kidhibiti! Qatada akarejea kwa ami yake na kumweleza kilichojiri. Ami yake akasema: Allah ndio wa kumuomba msaada. Kisha haukupita muda ikateremka aya inayombainishia Mtume juu ya khiyana ya ukoo wa Abriiqu, huku ikimwamrisha aombe msamaha kwa kile alichomwambia Qatada}.** Hadithi hii imepokewa na Attirmidhiyu. Na Alhaakimu akaipa daraja ya sahihi kwa masharti ya Muslimu[2].

---

[1]Mashriba: Chumba.

[2] Imepokewa na Attirmidhiyu katika Attafsiiru 3036. Na Alhaakimu katika Almustadraku 4 / 385. Na Attwabary 5 / 265. Na Albaniy ameipa daraja ya Hassan katika Swahihu Attirmidhiy 2432.

Bali, isikilize kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake, akiisema nafsi yake, katika hadithi iliyopokewa na Ahmad na Ibnu Maajah: **{Kwa hakika mimi ni binadamu kama nyinyi. Na dhana yangu hukosea na hupatia. Isipokuwa kile nilichokwambieni kuwa Allah amesema. Kamwe sitomsingizia Allah}[1].** Na kauli yake **{Kwa hakika mimi ni binadamu. Na nyinyi mnagombana na mnakuja kwangu. Na huenda baadhi yenu mkawa mna hoja za maneno matamu kuliko wengine. Nami namdhania kuwa ni mkweli, na kuhukumu kwa kumpa haki kwa mujibu wa ninachokisikia. Basi yule nitakayempa haki ya Muislamu, kwa hakika hicho ni kipande cha moto. Basi na akichukue au na akiache}.** Imepokewa na Maaliku na Sheikhani na watu wa Sunani[2] Hivi yule ambaye nafsi yake haiwezi kutambua uhakika wa yale yaliyotokea baina ya wanaogombana wawili katika zama zake na katika mji wake, na ameshawaona hao wanaogombana na ameshasikia kauli zao. Bila ya shaka huyo hawezi zaidi kutambua yale yaliyopita na yale yanayokuja.

Huo ndio upande wa yale yaliyofichikana, huku taa za utambuzi na uwerevu zikiwa zimetoweka kwake. Na akili haiyasogelei mambo hayo ila zikiwa kama muokota kuni usiku[3] au Khabitwu Ashuwai[4]: Kama atapatia haki kwa mara moja anakosea mara nyingi. Na kama atapatia mara nyingi anakosea mara makumi kwa makumi. Ya kwamba yule ambaye anasadifiana na kupatia haiwezekani kumtegemea kuwa ataendelea kubakia akiwa amekingwa bila kupatwa na mabadiliko. Huenda akaondoshwa na upepo wa sadifa kama vile ulivyomjia. ﴿**Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi** ﴾. An-Nisaa 82.

* * *

[1] Imepokewa na Ahmad 1 / 162, 163 kutoka kwa Twalha, na Ibnu Maajah katika Arruhuuni 2470. Nikasema: na hadithi hii ipo katika Muslimu katika Alfadhaailu 139, katika hadithi ya Twalha na Raafiu Bin Khadiju.

[2] Muttafaqu alayhi: imepokewa na Albukhariyu katika Alhiyalu 6967 na katika Al-Ahkaam 7169, 7181, 7185 na imepokewa na Muslimu katika Al-Aqdhwiyatu 5, na Maaliku katika Al-Aqdhwiyatu 1.

[3] Mchanja kuni usiku: ni yule anayekusanya kuni wakati wa usiku na hivyo haoni kile anachokikusanya. Huenda akamkusanya na nyoka bila ya kumuona. Na mara nyingi hutumika msemo huu kumaanisha yule ambaye anachanganya katika maneno yake.

[4] Na Khabitwu ashuwai: ni mjinga. Na ashuai ni ngamia jike mwenye uoni dhaifu. Anajigonga pale anapotembea na hajichungi na chochote. UK 66.

## [HATUA YA PILI YA UTAFITI HUU:

## Kubainisha Kuwa Muhammad Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake, Lazima Atakuwa Amechukua Quran Kutoka Kwa Mwalimu. Na Kutafiti Katika Vyanzo Vya Kibinadamu Kuhusiana Na Huyo Mwalimu]

Kwa mtafiti hana pa kukimbilia na kuacha kupanua wigo wa utafiti wake kuhusu chanzo cha Quran. Na kama hatopata anachokitafuta kwa mwenye hiyo Quran kwa upande wa akili zake na utambuzi wake, atawajibika akitafute – na kukipata hasa – na kwa upande wa ujuzi na usomaji wake. Kwa sababu mwenye kuongea maneno. Basi maneno hayo hayavuki ima yatakuwa yeye ndiye msemaji wake au ameyanukuu. Na hakuna upande wa tatu zaidi ya hizo mbili.

Ndio, kwa hakika mwenye Quran hii hakuwa miongoni mwa wanaojirejeshea kitabu cha elimu na diwani zake. Kwa sababu mambo yalivyo, kwa kuungama kwa wapinzani wake kuwa amezaliwa akiwa hajui kusoma na kuandika pia amekulia akiwa hajui kusoma na kuandika na aliishi akiwa hajui kusoma na kuandika. Na haijapotokea hata siku moja miongoni mwa masiku kuwa anasoma kitabu cha karatasi[1] wala haandiki kwa mkono wake wa kuume. Hana budi, lazima ana mwalimu aliyemfunza maana hizi kwa njia ya maandishi na kusajili. Bali kwa njia ya kumtajia na kumsomea. Hii ndio hukumu ya kimantiki.

Utasema: ni nani huyo mwalimu?

Tunasema: huu ndio upande wa pili wa masuala ya Quran.

Na wewe ukitafakari vizuri hayo tuliyokutiririshia miongoni mwa hoja katika upande wa kwanza utapata kujua kuwa kandoni mwa kila moja katika hayo kuna hoja nyingine itakayobainishwa katika upande wa pili na utamjua ni nani huyo mwalimu? Isipokuwa sisi tunapenda kukuzidishia maarifa ili useme pamoja nasi katika hayo: Huyu si mwanadamu. Huyu si mwingine ila ni malaika mtukufu. Mwenye kufikisha kutoka kwa Mola wa ulimwengu wote.

* * *

[1] Karatasi: Kurasa.

[**Kumtafuta Mwalimu Wake Baina Ya Wajinga Wasiojua Kusoma Na Kuandika:**

**Ujinga Hauwezi Kuwa Chanzo Cha Elimu**]

Ama eti Muhammad rehema na amani ziwe juu yake hakuwa na mwalimu wa jamii yake ya wasiojua kusoma na kuandika. Hilo halina utata kwa yeyote. Na hutamdhania mtu yeyote kuwa anahitaji kupewa ushahidi wa hili zaidi ya jina (Ummiyya = asiejua kusoma na kuandika) jina ambalo wanalishuhudia kuwa umma wao walikuwa wametoka katika matumbo ya mama zao wakiwa hawajui lolote kuhusu jambo la dini. Na hivyo hivyo jina la ( Aljaahiliya) jina ambalo ndilo jina maalumu waliopewa Warabu wa zama za kabla ya Uislamu. Hawa ndio ambao walipoteza msingi huu wa elimu kwa nafsi zao mpaka ujinga ukanyambuliwa kuwa jina lao.

Sasa inakuwaje wao wabebe nishani ya kufundisha wengine. Vipi wamfundishe mwalimu wao ambaye amewaita wajinga si chini ya mara moja katika kitabu chake. Na ametiririsha ujinga wao katika sura zaidi ya moja katika kitabu hiki, mpaka ikasemwa (Kama utapendezwa na kujua ujinga wa Warabu basi soma yale yaliyo baada ya aya ya mia katika surat Al-An-aam).

[**Kumtafuta Mwalimu Huyo Baina Ya Wenye Elimu**]

Ama ya kuwa yeye hakuwa na mwalimu asiyekuwa wao. Basi yamtosha mtafiti wa hilo tumpeleke katika historia na kumtaka apekue kurasa za kale na za kisasa, za Kiislamu na za kimataifa. Kisha tunamuuliza. Je, amesoma hata mstari mmoja unaosema kuwa Muhammad Bin Abdullah Bun Abdulmutwalibi, kabla ya kutangaza Utume wake alikutana na fulani miongoni mwa wasomi na kukaa naye na kusikiliza maneno yake juu ya elimu ya dini, na visa vyake juu ya watu wa mwanzo na wa mwisho?

Sisi hatuna la kuliweka kuwa ni hoja kubwa ya kuthibitisha kuwa hilo la kuwa na mwalimu halikuwepo kuliko hii changamoto kubwa. Na hakika si vinginevyo, ni juu ya wale wanaodai kinyume na hivyo, wathibitishe kuwa hilo lilikuwepo. Na kama watakuwa na ujuzi basi na watutolee ikiwa wanasema ukweli.

Hatusemi ya kuwa Mtume amani iwe juu yake hajakutana na hajamuona kwa jicho lake yeyote miongo mwa wanazuoni wa maswala haya. Si kabla ya kupewa Utume wala baada yake. Sisi huenda tunajua ya kuwa yeye katika

utoto wake alimuona mchungaji jina lake Bahira katika soko la Busra huko Shamu[1]. Na huko Makka kwenyewe yeye alikutana na msomi aitwaye Waraqa Bin Naufal.[2] Na tukio hili lilikuwa ni kabla ya kuja kwa ufunuo wa wazi kwa Mtume na kabla ya kutangaza utume wake kwa miezi thelathini, kama tunavyojua kuwa yeye baada ya kutangaza utume wake alikutana na

---

[1]Kutoka kwa Abuu Musa Al-Ash-ariyu Allah amuwie radhi: **{Abuu Twalibu alitoka kwenda Shamu. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake alitoka pamoja naye akiwa na wazee wa Kikurayshi. Na pale walipomuona mchungaji waliteremka na wakawafungua wanyama wao. Basi yule mchungaji akawatokea, na kabla ya hapo walikuwa wakipita kwake na yeye hawatokei wala hawageukii. Amesema: huku wao wakifungua vipando vyao. Yule mchungaji akawa anapenyapenya baina yao mpaka akafika kwa Mtume na kumshika mkono Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kusema: Huyu ni Bwana wa ulimwengu. Huyu ni Mtume wa Mola wa ulimwengu. Allah amemtuma akiwa ni rehema kwa ulimwengu. Wazee wa kikureishi wakamwambia mchungaji: Kipi kilichokujulisha? Akasema: kwa hakika nyinyi pale mlipokaribia eneo la Akaba haukubaki mti wala jiwe ila liliporomoka kwa kusujudu. Na viwili hivyo havisujudu ila kwa Nabii. Na hakika mimi namjua kwa muhuri wa Utume ulio chini ya mfupa laini wa chini ya bega lake ulio kama tufaha (apple).**

**Kisha akarejea alipotoka na kuwaandalia chakula. Na pale alipowapelekea chakula, na yeye [yaani Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake] akiwa anamlisha ngamia, mchungaji akasema: mpelekeeni. Na Mtume akaja huku mawingu yakiwa yanamfunika asipigwe na jua. Na pale alipowasogelea wale watu aliwakuta washamtangulia kwenda katika kivuli cha mti. Na pale alipokaa chini; kile kivuli kiliinamia upande wake. Na akasema: Kitazameni kivuli cha mti kimeinama upande wake …}** Imepokewa na Attirmidhiyu katika Almanaaqibu 3620. Na Albaniy ameipa daraja ya usahihi katika Fiqihu Assiira uk 70. Na Swahihu Attiridhiyu 2862. Na Assuyuutwiyu amekusanya riwaya nane kuhusiana na tukio hili katika kitabu Alkhaswaaiswu Alkubraa 1 / 141 – 146.

Na katika kila riwaya kinaonekana kisa hiki {kisa cha mchungaji Behira] ya kuwa yeye ndiye alikuwa akimuuliza Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake juu ya hali yake, sifa zake, kulala kwake, umbile lake na mambo yake. Na yule mchungaji alikuwa akithibitisha kutokana na alama maalumu zilizokuwepo kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake. Na katika riwaya zote hakuna maelezo ya kuwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake ndiye aliyemuuliza au amejifunza toka kwake hata herufi moja ukiachilia mbali hiyo elimu kubwa.

[2] Yeye ni Waraqa Bin Naufal Bin Asad bin Abdul Ghuzza bin Qusway bin Kilab. Naye ni mmoja wa watu wanne miongoni mwa makureyshi waliokataa kuabudu masanamu ya kijahiliya. Na wakawa wanatembea ardhini wakitafuta dini ya Ibrahimu. Nao ni Zaidu bin Amru bin Nufailu, Waraqa bin Naufalu, Othman bin Alhuwayrithu na Ubeidu bin Jahshi. Waraqa alijifunza Ukristo na kukielekea kitabu chao mpaka alipoijua elimu ya Ahlu Kitabu. Naye ni mtoto wa Ami wa mama wa waumini Khadija binti Khuwaylidi Allah amuwie radhi. Na Alhaafidhu Ibnu Hajari amesema katika Fat-hu Albaary 1 / 34 : Na ama Waraqa alipendezwa na dini ya Kikristo na akauingia. Na alikutana na wale waliobakia miongoni mwa viongozi walio katika dini ya Issa na hawajabadilika. Na kwa ajili hiyo walimweleza habari za Nabii Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na namna alivyotabiriwa. Na yasiyokuwa hayo miongoni mwa mambo yaliyowaharibu watu na kubadili maandiko. أ هـ .

wanazuoni wengi wa Kiyahudi na Kikristo huko Madina. Lakini sisi tunadai madai maalumu, tunasema: ya kwamba yeye hajapatapo kuchukua kutoka kwa yeyote yule miongoni mwa hawa wanazuoni. Si kabla wala baada ya Utume. Na kuwa, kabla ya utume wake hakuwahi kuwasikiliza chochote miongoi mwa hadithi hizi katu.

Ama wale waliokutana nao baada ya utume, kwa hakika walikuwa akiwasikiliza na wao walimsikiliza. Lakini wao walikuwa wakimuuliza yeye na kuchukua kutoka kwake. Na yeye kwao wao alikuwa mwalimu, mtoa mawaidha, mwonyaji na mtoa habari njema.

Ama wale waliokutana naye hapo kabla, kwa hakika jambo la kukutana nao halikuwa la siri au lenye kufichwa. Bali mara zote Mtume alikuwa pamoja na shahidi: Ami yake Abuu Twaalibu alikuwa ameambatana naye pale alipomuona mchungaji wa Shamu. Na mkewe bi Khadija alikuwa ameambatana naye pale alipokutana na Waraqa. Ni kipi walichokisikia waambata wawili hawa miongoni mwa elimu za hao walimu wawili? Mbona historia haijatuhadithia juu ya habari ya yale yaliyotokea?

Kwa nini hiyo historia haitusimulii juu ya tukio hili la ajabu. Tukio ambalo katika muda huo mfupi lililkusanya elimu ya Quran na maelezo kwa urefu juu ya habari zake zilizo baina ya mwanzo wa ulimwengu na mwisho wake!! Kwa nini wanaompinga hawajachukua hoja hii ya wazi kabisa na kuifanya silaha yao kali ya kuzikata hoja zake. Pamoja na ukali wa harakati zao za kuuangamiza ujumbe wake. Na kukimbilia kwao katika utata dhaifu ili kumkadhibisha. Na silaha hii ilikuwa karibu mno na wao. Na yenyewe peke yake ilikuwa ina uwezo wa kutumika katika kubatwilisha jambo lake kwa kila walilolikimbila miongoni mwa vitimbi na viburi.

Kwa hakika kunyamaza kwa historia kuhusiana na hayo yote ni hoja tosha juu ya kutokuwepo kwa swala hilo. Kwa kuwa lenyewe si miongoni mwa mambo mepesi ya kuchukuliwa kiwepesi wepesi na watu wanaoyasimamia na kuyachunga kisha kuyafumbia macho.

Lakini historia haijanyamaza, bali imetuhabarisha kile kilichokuwa katika mambo ya wawili hao: historia imetusimulia kuhusu padre wa Shamu ya kuwa, pale alipomuona kijana huyu, alimuona ana alama za Mtume wa mwisho na sifa zake katika vitabu vilivyopita, jambo ambalo lilimtamkisha maneno ya kumbashiria ami yake kwa kusema: kwa hakika kijana huyu atakuwa na jambo kubwa. Na imetuelezea kuhusu Waraka ya kuwa, pale

aliposikia yale aliyosimuliwa na Mtume miongoni mwa sifa za ufunuo alikuta ndani yake kuna mambo maalum ya Namusi[1] aliyemteremkia Musa. Jambo lililomfanya aungame na kuukiri Utume wake na kutamani aishi mpaka aje kuwa miongoni mwa watu wake.[2]

---

[1] Namusi: ni mwenye siri. Na kwa hapa makusudio yake ni: Jibrilu amani iwe juu yake (Fat-hu Albaary 1 / 35). Na asili ya neno Namusi ni siri, na mwenye siri ya heri, mwenye busara nyingi, na yule ambaye kuingia kwake ni kwa upole. Na husemwa mtu amejinamusi kwa maana kuwa amijistiri na kujificha (Kamusi ya Almuhiitwu).

[2] Kisa cha Waraqa bin Naufal pamoja na Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake kimekuja katika Swahihi mbili kutoka katika hadithi ya Aisha mama wa Waislamu amesema: **{Jambo la kwanza aliloanza nalo Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika ufunuo ni ndoto nzuri akiwa usingizini. Alikuwa haoti ndoto ila inatokea kama mapambazuko ya asubuhi. Kisha akafanywa apende kujitenga na kuwa peke yake. Kwa hiyo akawa anajitenga katika pango la Hiraa na kunyenyekea hapo – yaani kuabudu – usiku wenye idadi maalum kabla ya kurejea kwa watu wake na kufanya maandalizi tena kwa ajili hiyo. Kisha anarejea kwa Khadija na kujiandaa tena kama hivyo.**

**Mpaka akajiwa na haki naye akiwa katika pango la Hiraa. Akajiwa na malaika na kumwambia: Soma. Akasema: Mimi si msomaji. Akasema, akanishika na kunibana mpaka kibano kakanibana sana kisha akaniachia na kusema: Soma. Nikasema: Mimi si msomaji. Akasema, akanishika na kunibana kwa mara ya pili mpaka kibano kakanibana sana kisha akaniachia na kusema: Soma. Nikasema: Mimi si msomaji. Akasema, akanishika na kunibana kwa mara ya tatu, kisha akaniachia na kusema: ﴿Soma, kwa jina la Mola wako aliyeumba. Amemuumba mwanadamu kwa pande la damu. Soma, na Mola wako ni Karimu sana ﴾. Alaq 1 – 3.**

**Kisha Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akarejea kwa Khadija huku kifua chake kikitetemeka. Akaingia kwa Khadija binti Khuwaylidi Allah amuwie radhi na kusema: Nifunike nguo! Nifunike nguo! Wakamfunika hadi hofu ikamuondoka. Akamwambia Khadija na kumhabarisha hiyo habari: kwa hakika nimehofia nafsi yangu. Khadija akasema: Sivyo hivyo! Nakuapia kwa Allah, Allah Hatokudhalilisha kamwe! Kwa hakika wewe utaunga udugu, na kuwabeba wote, na kumpa aliyenyimwa, na kuwapa chakula madhaifu, kuwasidia wenye shida kwa haki.**

**Kisha Khadija akampeleka hadi kwa Waraqa bin Naufal bin Asad bin Abdul Ghuzza – mtoto wa ami wa Khadija – na alikuwa ni mtu aliyeingia katika Ukristo katika zama za Jahiliya. Na alikuwa anaandika maandishi ya Kiebrania. Kwa hiyo akiandika Injili kwa Kiebrania kile Allah alichotaka akiandike. Na alikuwa mzee mkongwe sana na ameshapofuka. Khadija akamwambia: Ewe mtoto wa ami yangu, msikilize mtoto wa ndugu yako. Waraqa akasema: Ewe mtoto wa ndugu yangu waona nini? Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akamweleza habari za kile alichokiona.**

**Waraqa akamwambia: Huyo ni Namusi ambaye Allah alimteremsha kwa Musa. Laiti katika suala hili ningekuwa Jidhia [kijana]. Laiti niwe hai pale watu wako watakapokutoa. Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akasema: Je, wao watanitoa? Akasema: Ndio. Katu hakuna mtu aliyekuja na jambo kama hilo ulilokuja nalo isipokuwa atafanyiwa uadui. Na kama hiyo siku yako nitaidiriki basi**

Mwenye kuujua utukufu wa historia na kuamini matukio yake kama yalivyo. Matukio haya yalikuwa ni hoja yetu sisi dhidi yake. Na asiyeogopa kuzidisha kitu katika historia hata kama ni herufi moja kutoka katika nafsi yake. Basi huyo atasema kwa hakika Muhammad amekusanya kusikiliza katika kukutana na kisha atunge ayatakayo. Na ajue kuwa, kwa huku kuzidisha kwake kihistoria atakuja kutuletea historia kinzani ambayo mwanzo wake unapingana na mwisho wake. Na mwisho wake unakinzana na mwanzo wake. Kwani, vipi iingie akilini eti mtu mmoja ameona alama za Utume kwa mtu mwingine na kumbashiria hilo kabla ya kutokea. Au ameuamini huo utume kabla ya kutokea kwake. Na kujitoa kwake kwa nafsi yake asimame kwa mwenye huu utume msimamo wa mwalimu mwongozaji! Hivi wanaelekea wapi?!

**1- Sisi tunauliza: Je, kwa wasomi wa wakati huo kulikuwa na mtu anayefaa kuwa na mkono wa kielimu kwa Muhammad na Quran yake?**

Makafiri wenyewe wanasema: (Kwa hakika Quran ndio athari pekee ya kihistoria inayowakilisha roho ya zama zake ukweli wa kuwakilisha). Na hili ni neno la haki katika mipaka ya maana yake sahihi[1] sisi tunawachukulia wao kwa kukiri kwao, na kuwaita waivute taswira hiyo iliyohifadhiwa na Quran katika kioo chake kinachong`aa kuwa ndio mfano wa wazi wa wataalamu wa zama zake. Na wazisome Zahrawayiin Albaqara na Aali Imran na yale yaliyomo ndani ya sura mbili hizo, miongoni mwa mazungumzo ya wasomi wa Kiyahudi na Kikristo katika masuala ya kiitikadi, kihistoria na kihukumu za kisheria. Au na wasome watakazo miongoni mwa sura za Madina au za Makka na ambazo ndani yake kuna kuwataja Waliopewa Kitabu. Na watazame Quran inawaongelea kwa lugha gani. Na namna gani elimu zao zinavyotupatia taswira ya kwamba wao ni wajinga, na itikadi zao ni za upotovu na ni mambo ya hovyo hovyo, na matendo yao ni uovu na machukizo.

---

**nitakunusuru kwa nguvu zote. Kisha haukupita muda Waraqa akafa, na ufunuo ukasita}**. Imepokewa na Bukhariyu katika Mwanzo wa Ufunuo 3. Na Muslimu katika Al-Iimani 252.

[1] Nayo ni kuwa inaiwakilisha na wala haifanani naye. Na kama ukipenda sema kwa hakika inawakilisha ukweli wa kuwakilisha. Kisha linawakilisha uwakilishi mzuri zaidi. [Daraazu].

**[Msimamo Wa Muhammad Rehema Na Amani**

**Ziwe Juu Yake Kwa Wasomi: Ni Msimamo Wa Msahihishaji Wa Kile Walichokipotosha. Mfunua Wa Yale Waliyoyaficha]**

Kama utapenda ziada ya ubainifu pokea mifano ya wasifu wake na namna alivyovunja upotoshaji na uvurugugaji wao wa historia:

- ﴿**Enyi watu mliopewa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahimu, na hali Taurati na Injili havikuteremshwa ila baada yake? Basi je, hamfahamu?** ﴾ Aali Imran 65.
- ﴿**Mnasema (nyinyi Mayahudi na Manasara) kuwa Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa na Yaqubu na kizazi (chake) walikuwa Mayahudi (kama nyinyi) au Wakristo (kama nyinyi)?** ﴾ Al-Baqarah 140.
- ﴿**Kwa yakini nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu, kwa ajili ya watu (kufanya ibada) ni ile iliyoko Makka**Aali Imran 96. **.**[1] ﴾
- ﴿**Kila chakula kilikuwa halali kwa kizazi cha Israili (Mayahudi) isipokuwa kile alichojiharamishia Israili mwenyewe**Aali Imran 93. [2] ﴾
  Na hizi ni sehemu za sifa zake na namna ilivyovunja mambo yao ya hovyo hovyo ya kidini:
- ﴿**Wala hayakutugusa machofu**[3]Qaf 38. [4] ﴾
- ﴿**na Suleiman hakukufuru**Baqarah 102.-Al [5] ﴾
- ﴿**Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya wale (Mayahudi) waliosema: ‘‘Mwenyezi Mungu ni fakiri, na sisi ni matajiri**Aali [6] ﴾ Imran 181.

---

[1] Aya hii ni jibu la kauli yao: kibla chetu kilikuwa kabla ya kibla chenu [Daraazu].

[2] Aya hii ni jibu la madai yao, ya kwamba ngamia ni haramu kwa Ibrahimu [Daraazu].

[3] Machofu: ni kuchoka na kutaabika.

[4] Aya hii inakadhibisha kauli yao isemayo kuwa Allah baada ya kuwaumba viumbe kwa siku sita alipunzika katika siku ya saba. [Daraazu].

[5] Nayo ni kumtakasa Suleiman na madai yao ya kuwa yeye hakuwa Nabii bali alikuwa mchawi anayepanda upepo [Daraazu].

[6] Kutoka kwa Ibnu Abbas Allah amuwie radhi na baba yake amesema: **‘‘Pale ilipoteremka kauli ya Allah ﴿Ni nani atakayemkatia Mwenyezi Mungu sehemu bora (ya mali yake kwa kuwapa masikini na kwa kutoa katika mambo mengine ya kheri) ili Mwenyezi Mungu amzidishie mzidisho mwingi ﴾ Albaqarah 245. Wayahudi walisema: Ewe Muhammad, hivi Mola wako ni fakiri hadi anafikia kuwaomba mkopo waja wake? Ndipo Allah akateremsha ﴿﴿Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya wale (Mayahudi) waliosema: ‘‘Mwenyezi Mungu ni fakiri, na sisi ni matajiri ﴾.** Ibnu Kathiru katika Attafsiiru 2 / 153 ameiegemeza kwa Ibnu Mardawayhi na Ibnu Abuu Haatimu.

- ﴿**Na Mayahudi walisema: ‘‘Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba**Maidah 64.-Al [1] ﴾
- ﴿**Na Mayahudi wanasema: ‘‘Uzeri ni mwana wa Mwenyezi Mungu;’’ na Wakristo wanasema: ‘‘Masihi ni mwana wa Mwenyezi Mungu’’** ﴾ 30.Attawba [2]
- ﴿**Na Mayahudi na Wakristo wanasema: ‘‘Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake.’’** ﴾ Al-Maidah 18.
- ﴿**Bila shaka wamekufuru wale waliosema: ‘‘Mwenyezi Mungu ni Masihi (Isa) bin Maryamu.’’… Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: ‘‘Mwenyezi Mungu ni mmoja katika (wale waungu) watatu; (yeye ndiye wa tatu wao** ﴾**.** Al-Maidah 72 - 73.
- ﴿**Sema: ‘‘Enyi watu mliopewa Kitabu (cha Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara)! Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu: ya kwamba tusimwabudu yo yote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe (Mwenyezi Mungu) na cho chote; wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu** ﴾**.** Aali Imran 64.

Tazama namna Quran ilivyoleta taswira ya itikadi ya wasomi wa kidini katika zama zake na hasa hasa wasomi wa Kikristo. Kwa hakika tabia ya kishirikina ilikuwa katika dini yao na haifichiki kwa yeyote. Hadi wale wasiojua kusoma na kuandika wamelitambua hilo na kulifanya hilo ni suala la kuwapa pole wao katika shirki yao ﴿**Na alipopigiwa mfano mwana wa Maryamu, (Nabii Isa) mara watu wako wakaupigia kelele. Wakasema:**

---

[1] Kutoka kwa Ibnu Abbas Allah amuwie radhi na baba yake amesema: **‘‘Mtu mmoja miongoni mwa Wayahudi aitwaye Annabaashu Bin Qaysi alisema: Kwa hakika Mola wako ni bahili haitoi. Basi Allah Mtukufu Aliyetukuka akateremsha ﴿Na Mayahudi walisema: ‘‘Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba, (hatuoni kupata mali kama zamani).’’ (Siyo, bali) mikono yao ndiyo iliyofumba (haifanyi kheri ila kudhulumu na kupokonya); na wamelaaniwa kwa sababu ya yale waliyosema. Lakini mikono yake (Mwenyezi Mungu) iwazi hutoa apendavyo ﴾.** Alhaythamiyu amesema katika Majmau Azzawaaidi 7 / 17: imepokewa na Attwabaraniyu na wapokezi wake ni watu wa kutegemewa. أ هـ. Na Assuyutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 2 / 525 ameiegemeza kwa Ibnu Is-haqa na Attwabaraaniyu na Ibnu Mardawayhi.

[2] Ufupisho wa hadithi zilizotajwa katika tafsiri ya aya hizi ni kuwa Mayahudi walimwita Uzeri – naye ni mmoja wa watu wema wao – ya kuwa yeye ni mwana wa Mungu kwa sababu aliihifadhi Taurati na kuisoma kwa kichwa bila kuangalia. Ama kwa Wakristo kumwita Masihi jina la Mtoto wa Mungu hilo lipo wazi kwa kuwa yeye Masihi amani iwe juu yake alizaliwa bila baba, na hawakuujua uwezo wa Allah katika kuumba kwake mwanamke bila mwanamme. Na wamesahau kuumbwa kwa Adam bila ya mwanamme wala mwanamke bali ametokana na mchanga na maji.

**‘‘Je! Miungu yetu ni bora au yeye?’’**pia hilo Bali58. –57 Zukhruf -Az [1] ❵ walilifanya ni hoja yao dhidi ya Upweke waliolinganiwa na Quran ya

---

[1] Ibnu Is-Haqa amesema: **{Katika mambo yaliyonifikia ni kuwa Mtume rehema na amani iwe juu yake siku moja alikaa msikitini akiwa pamoja na Alwaliid. Akajiwa na Annadhwaru bin Alhaarithi akakaa pamoja nao katika kikao hicho. Na katika kikao hicho kulikuwa na watu zaidi ya mmoja katika Makurayshi. Basi mtume rehema na amani ziwe juu yake akaongea na kumuwasilishia Annadhwaru bin Alhaarithi. Mtume wa Allah akaendelea kuongea naye mpaka akamshinda kwa hoja. Kisha akamsomea na kuwasomea wengine aya hizi: ❴Hakika nyinyi na wale mnaowaabudu, mkamwacha Mwenyezi Mungu, ni kuni za Jahanamu; nanyi mtaifikia hiyo Jahanamu mkae humo ❵**. Al-Anbiyaa 99. Kisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasimama, na Abdullah bin Azzubaariyu Assuhamiyu akaja na kukaa. Papo hapo Alwaliidi bin Almughiira akamwambia: Naapa kwa Mungu, ya kuwa Annadhwaru bin Alhaarithi hajasimama wala hajakaa kwa ajili ya mtoto wa Abdul Muttwalibi. Kwa hakika Muhammad amedai kuwa sisi na kile tunachokiabudu miongoni mwa hii miungu yetu ni kuni za Jahanam. Abdullah bin Azzubaariyu akasema: ama naapa kwa Allah, lau kama nitamkuta nitagombana naye [yaani nitamshinda]. Muulizeni Muhammad: je, kila kinachoabudiwa kinyume na Allah ni cha Motoni pamoja na wanachokiabudu. Mbona sisi tunaabudu Malaika, Wayahudi wanaabudu Uzeri na Wakristo wanamwabudu Issa bin Maryam? Alwaliidu na wale waliokuwa pamoja naye kikaoni wakapendezwa na kauli ya Abdullah bin Azzubayriyu, na wakaiona kuwa ameshatoa hoja nzito ya ushindi. Hilo likatajwa kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, naye akasema: Kila aliyependa kuabudiwa kinyume na Allah basi huyo ndio yupo pamoja na wanaomwabudu. Kwa hakika wao wanamwabudi shetani na yule aliyewaamrisha wamwabudu. Ndipo Allah Mtukufu Aliyetukuka akateremsha **❴Hakika hao ambao wema wetu umewafikia, hao watakuwa mbali nayo (hiyo Jahanamu ❵.** Al-Anbiyaa 101. Yaani Issa na Uzeiru na wale walioabuduiwa pamoja nao miongoni mwa viongozi wa dini wa Kiyahudi na Kikristo ambao wametumia muda wao katika kumtii Allah Mtukufu Aliyetukuka. Kisha wale wanaowaabudu ambao ni miongoni mwa watu waliopotea wakawafanya miungu kinyume na Allah.} Imepokewa na Attwabariy katika tafsiri yake 17 / 96. Na hivyo hivyo imepokewa na Ibnu Hishaamu katika Assiira 2 / 106 (Arraudhwu Al-Unfu).

- **Faida**: katika Arraudhwu Al-Unfu 2 / 116, Assuhailiyu ametaja mambo ambayo ufupisho wake ni: Kwa hakika hoja ya Ibnu Azzubairiyu kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake haina mashiko kwa sababu mbili nazo ni:

a- Waongeleshwa katika aya hii ni makafiri wa kikuraishi na masanamu yao ya Allaata na Uzzaa na Hubalu.

b- Kwa hakika tamko la aya: ❴**na kile mnachokiabudu** ❵ na neno ❴**Maa = kile** ❵ katika lugha ya Kiarabu inajulisha visivyo na akili nayo ni masanamu. Ama kwa wale wenye akili kwa mfano Manabii na wengineo wao wametolewa na aya hiyo.

Nimesema: na kauli hii inashuhudiwa na hadithi nyingi nyingine katika Adduraru Almanthuuru cha Assuyuutwiyu 4 / 607, 5 / 728. Na miongoni mwazo ni hadithi ya Ibnu Abbas Allah awawie radhi yeye na baba yake, amesema: **{Kwa hakika Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amewaambia Makuraishi: Enyi makongamano ya Makureishi. Kwa hakika hakuna anayeabudiwa kinyume na Allah akawa ndani yake kuna heri. Na Makuraishi mmseshajua kuwa Wakristo wanamwabudu Issa Ibnu Maryamu. Hivi mnasema nini kumhusu Muhammad. Wakasema: Ewe Muhammad, je, hivi wewe hudai kuwa Issa alikuwa Nabii na mja mwema wa Allah? Kama ulikuwa ni mkweli, basi kwa hakika miungu yao**

kwamba, Quran yenyewe ni uzushi na haijawahi kutokea hapo kabla wakasema: ﴿**Sisi hatukusikia haya (ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja hata) hata katika hii mila ya mwisho. Hayakuwa haya (ya kusema kuwa Mungu ni mmoja tu ) ila uzushi (tu** ﴾**.** Sad 7. Wakikusudia dini ya Kikristo.

Na huu ni mlolongo mwingine wa madhambi yao unaoletwa na Quran pingili zake zikiwa zimeungana: ﴿**Basi (tuliwaadhibu) kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na kuzikataa kwao hoja za Mwenyezi Mungu, na kuua kwao Manabii bila ya haki, na kwa kusema kwao (kumwambia Nabii Muhammad): ''Nyoyo zetu zimefumbwa (haziwezi kuingia kitu katika hayo unayoyasema''** ﴾**.** Mpaka aliposema ﴿ **Na kwa sababu ya kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa (kuwa kamzaa Nabii Isa kwa kuzini). Na kwa (ajili ya) kusema kwao: ''Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu Mtume wa Mungu,''** ﴾**.** Mpaka aliposema ﴿**na vilevile) kwa sababu ya kuzuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu. Na kwa (sababu ya) kula kwao riba, na hali wamekatazwa wasiile, na (kadhalika) kwa kula kwao mali za watu kwa batili** ﴾**.** An-Nisaa 155 – 161.

***Je, unaona haya yote ni taswira ya walimu ambao kwao wao mwenye Quran anapata elimu yake? Au ni kinyume chake, na unaona kuwa yeye ndiye mwalimu anayewasahihishia makosa yao na kusafisha hali yao mbaya?***

Usipinge ya kuwa katika watu wa Kitabu kulikuwa na wasomi wabobezi wachache. Lakini wale wabobezi wa elimu miongoni mwao waliiamini Quran na wakajengea kwa Quran ﴿**Sema: ''Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na baina yenu (kuwa mimi ni Mtume) na (pia) yule mwenye ilimu ya Kitabu** ﴾**.**[1] Ar-Raad 43. Na lau wao ndio

---

**itakuwa kama mnavyosema. Akasema: Basi Allah Mtukufu Aliyetukuka akateremsha** ﴿**Na alipopigiwa mfano mwana wa Maryamu, (Nabii Isa) mara watu wako wakaupigia kelele.** ﴾**.** Imepokewa na Ahmad 1 / 317 na mwanazuoni Ahmad Shaakir amewapa wapokezi wake daraja ya Sahihi 2921.

[1] Aya ya kwanza ﴿**Na wanasema waliokufuru: ''Wewe si Mtume. ''Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu…''**﴾ Hiyo aya. Mwanazuoni Attwahiru bin Aashuuri katika tafsiri yake 13 / 175 amesema: Aya hii imetaja kuwa wao [yaani washirikina] wameshaweka wazi mara nyingi yale waliyokuwa wameyaficha. Wakatamka wazi wazi neno la kumkadhibisha na wakatoka katika hatua ya vitimbwi na kwenda katika hatua kudhihirisha ukafiri na wakasema ﴿**Wewe si Mtume** ﴾ na kauli yao imesimuliwa kwa umbo la wakati uliopo unaoendelea ﴿**na wanasema** ﴾ ili kujulisha kujirejea rejea kwa jambo hilo kwao wao, na kuzihudhurusha hali zao za ajabu kuanzia

wangekuwa walimu wake, basi wao ndio wangeamini badala ya kumwamini yeye.

2 – Hebu turudi kwa mara nyingine na kuuliza: Je, elimu ya wasomi wa zama hizo ilikuwa ikitolewa kwa anayeitaka, na ni halali kwa kila mwenye kuitafuta? Au pupa yao kwa elimu hiyo ilikuwa kali mno kuliko wanavyopupia maisha yao. Na walikuwa wakiificha hata kwa watoto wao ili walinde vyeo vyao au kwa sababu ya tamaa ya vyeo vya utume waliokuwa wakiuongaja katika zama hizo?

Hebu natuitamkishe Quran ambayo wapinzani wameiridhia iwe mwamuzi baina yetu na wao. Na kwa hakika yenyewe yatutosha tusitaabike kutafuta jibu la swali hili. Nayo ni hii hapa inatwambia: kwa hakika wao walikuwa katika njia ya kuficha vitabu vyao na elimu zao hawaogopi kutenda machafu. Na wakati mwingine walikuwa ﴿**Wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: ‘‘Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu.’’ Ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu** ﴾**.** Albaqarah 79. Na wakati mwingine ﴿**Wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); wala si ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu), na wanasema: ‘‘Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu; na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu…** ﴾ Aali Imran 78. Na wakati mwingine

---

kuendelea katika kumkadhibisha baada ya kuwa wameona alama za ukweli wake. Na pale maneno yao yaliyosimuliwa hapa yapo wazi hayana shaka. Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliamrishwa kujibu na sio mjadala. Na haya ni maamuzi ya Allah baina yake na wao.

Na kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliamrishwa kuwajibu kwa jibu la mwenye kujiamini kuwa jibu lake ni la kweli huku akilitolea ushahidi kwa ushahidi wa kweli kutokana na ushahidi wa Allah Mtukufu, na ushahidi wa wasomi wanaokijua Kitabu na sharia. ﴿**na (pia) yule mwenye ilimu ya Kitabu** ﴾**.** Yaani kila wale ambao wana ilimu ya Kitabu… na inawezekana ikawa makusuduio yake ni yule ambaye ni mtu maalum mwenye elimu ya Kitabu. Naye ni Waraqa bin Naufal, kwani yeye alikuwa ni mjuzi zaidi kuliko watu wote wa Makka na kwamba yeye ameshuhudia kuwa kilichofunuliwa kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake ni Namusi – siri iliyoteremshwa kwa Musa amani iwe juu yake. Na Waraqa alikuwa ni mtu wa pekee mwenye maarifa zaidi ya Taurati na Injili. Na kwa hakika habari ya kauli yake kwa Nabii rehema na mani ziwe juu yake ilikuwa maarufu kwa Makuraishi.

Na maelezo katika aya hii yalikuwa ﴿na **(pia) yule mwenye ilimu ya Kitabu** ﴾ na sio Ahlu Kitabu / watu wa Kitabu kwa sababu utekelezaji wa hilo la [kutabiriwa kuwa Nabii wa Mwisho, na kuafikiana kwa Quran na mwenendo wa sharia za Mungu. Na kufasiri misimbo iliyokuja katika Taurati na Injili kwa sifa za Nabii anayesubiriwa na aliyeahidiwa] hayajulikana ila na wataalamu wao. أ هـ [kwa ufupi na mabadiliko madogo].

﴾**Wanayabadilisha maneno ﴾ya Mwenyezi Mungu yaliyo katika Taurati na Injili) na mahali pake ﴿.** Almaidah 13. Na wakati mwingine wanakikata Kitabu na kwa hiyo wanaonesha baadhi yake na kuficha sehemu nyingine. ﴾**Sema: ''Ni nani aliyekiteremsha Kitabu alichokileta Musa? Chenye nuru na uwongofu kwa watu, mlichokifanya juzuu juzuu [karatwisu],[1] (zenye vile mnavyotaka vidhihiri) mkadhihirisha. Na yaliyo mengi mkayaficha…** ﴿ Al-An-am 91. Na wakati mwingine inawapa hoja watu wao waliohifadhi hivyo vitabu, na pindi wanapoambiwa ﴾**Sema: ''Leteni hiyo Taurati muisome ikiwa mnasema kweli.''**﴿ Aali Imran 93. Walipigwa butwaa na hawakujibu. Na huenda walikuja nayo na kuisoma kipengele kilicho kabla ya ushahidi[2] na kile kilicho baada yake na kuficha kile kipengele husika kwa kukifunika kwa viganja vyao, yale maeneo yenye andiko linalojadiliwa. Kama ilivyotukia katika kisa cha Kupiga mawe. Tazama Swahihi Albukhaariyu katika Tafsiiri ya aya iliyopita hivi punde.[3]

---

[1] Na mwanazuoni Attwahiru bin Aashuri amesema katika tafsiri yake 7 / 365:
Na neno karatwisu ni wingi wa neno kirtwasu nalo ni ukurasa wa kitu chochote kile… na kauli yake ﴾**mkadhihirisha. Na yaliyo mengi mkayaficha** ﴿ ni kivumishi cha nomino Karatwisu – juzuu juzuu – kwa maana mnavidhihirisha baadhi yake na kuvificha vingi katika hivyo. Kwa hiyo, maana ikafahamika ni kuwa: mnakifanya hicho Kitabu kuwa vijuzuu juzuu kwa lengo la kudhihirisha baadhi na kuficha baadhi nyingine. Na kivumishi hiki kipo katika eneo la kuonyesha makosa. Kwa hakika Allah ameteremsha vitabu vyake ili kuongoza watu. Na mwongozo wa vitabu vyake unasimama juu ya kudhihirishwa na kutangazwa kwa vitabu hivyo. Basi yule atakayekimegamega kwa lengo la kudhihirisha baadhi yake na kuficha baadhi nyingine, kwa hakika huyo ameenda kinyume na makusudio ya Allah katika hilo. أ هـ .

[2] Ushahidi ni: eneo lenye hoja au uthibitisho.

[3] Kutoka kwa Ibnu Omar Allah awawie radhi yeye na baba yake: **{Kwa hakika Wayahudi walimleta mtu mmoja na mwanamke mmoja waliozini miongoni mwao, na kuwapeleka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Mtume akawaambia: Mnamfanya nini yule aliyezini miongoni mwenu? Wakasema: Tunawaunguza na kuwapiga [kuwaunguza: ni kuwachoma nyuso kwa mkaa]. Akasema: Je, katika Taurati hamna kupiga mawe? Wakasema: hakuna ndani yake chochote. Abdulllah Bin Salaam akawaambia: mnaongopa, hebu leteni Taurati na muisome kama mnasema kweli. Akaweka kiganja chake juu ya aya ya kupiga mawe katika eneo la kusomea Tauratu, ni eneo ambalo analisoma katika vitabu vyao. Na akawa anasoma sehemu ambazo zipo nyuma ya mkono wake na zile za baada yake, na hasomi aya ya kupiga mawe. Abdullah akautoa ule mkono wake katika ile aya ya kupiga mawe. Akasema [Yaani Abdullah]: Nini hii? Na walipoona hilo wakasema: hii ndio aya ya kupiga mawe. Basi Mtume akaamrisha wale wazinifu wawili wapigwe mawe na wakapigwa eneo la karibu na eneo la majeneza msikitini''.**
Imepokewa na Bukhari na Muslimu: Bukhari ameipokea katika Attafsiiri 4556, na Muslimu katika Alhuduudi 26, 27.

Na Quran ikaja kuwatupia lawama za waziwazi za kuwa wao wanachanganya na kuficha ﴿**Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na mnaficha haki, hali mnajua?**﴾ Aali Imran 71. Pia imekuja ikiweka wazi kile walichokificha, huku ikibainisha walichokifisha, na kutoa maamuzi kwa waliyohitilafiana. ﴿**Enyi watu wa Kitabu! Amekwisha kufikieni Mtume wetu, anayekudhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu.** ﴾ Al-Maidah 15. ﴿**Bila shaka Quran hii inawaeleza wana wa Israili mengi ambayo kwayo wanakhitilafiana** ﴾. An-Naml 76. ﴿**Wallahi! Sisi tulituma (Mitume) kwa uma zilizokuwa kabla yako; lakini shetani aliwapambia vitendo vyao (vile vibaya wakaviona vizuri wakendelea navyo). Kwa hiyo leo, yeye (shetani) ni rafiki yao; (lakini watachukiana naye kweli kweli Akhera), nao watapata adhabu iumizayo. Na hatukukuteremshia Kitabu (hiki) isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalafiana, na (pia kiwe) uwongozi na rehema kwa watu wanaoamini** ﴾. An-Nahl 63 – 64.

Tazama aya hizi zilizo katika sura mbili za An-Nahl na An-Naml za Makka namna zilivyojaalia kuwa miongoni mwa makusudio ya msingi ya Quran ni kubainisha yale ambayo watu wa Kitabu wamekhitilafiana kwazo. Pia zenyewe zimelifanya jambo hilo ndilo kusudio kuu la kwanza[1] pale

[1] Na namna ya kutolea ushahidi aya mbili hizi zilizotangulia juu mada hii halipo wazi: Na aya ya suratul An-Namli haifahimiki kuwa yenyewe inatoa kipaumbele. Na ama aya ya suratul An-Nahl maneno yake hayazungumzii kuhusiana na watu wa Kitabu tu. Bali yenyewe ni ya nyumati zote zilizopita. Nyumati ambazo zilipotoshwa na shetani na zikaacha kumwabudu Allah. Kwa hiyo, inawajumuisha washirikina wa Kiarabu, Maswaibati, Majusi, Wayahudi, Wakristo na wengineo. Na jambo ambalo kwa ujumla watu wamehitilafiana kwalo ni kumpwekesha Allah, kuabudu, utume, kiama na hukumu za kisheria. Na hii ni mifano ya maneno ya wafasiri wa Quran kuhusu aya hii:

- Alhaafidhu Ibn Kathiiri katika tafsiri yake, amesema kuhusu aya hii:

Alla Mtukufu anataja kuwa yeye amepeleka Mitume kwa nyumati zilizopita, na hiyo Mitume ikakadhibishwa. Na ewe Muhammad, wewe una kiigizo kutoka kwa ndugu zako Mitume. Ukadhibishaji wa watu wako usikukere (usikusononeshe). Na ama Washirikina waliowakadhibisha Mitume. Kwa hakika kilichowafanya wao wafanye hivyo ni kule kupambiwa na shetani kile wanachokifanya. ﴿**na yeye ndiye mlinzi wao leo hii** ﴾ Yaani wao wapo katika adhabu na mateso. Na shetani ndio msimamizi wao na hamiliki uwezo wa kuwaokoa. Wala hawana wa kumpigia kelele. Na wana wao hao adhabu chungu. Kisha Allah Mtukufu akamwambia Mtume wake: Kwa hakika yeye, amemteremshia Kitabu ili awabainishie watu mambo ambayo wanatofautiana kwayo. Na Quran ndio kipambanuzi baina ya watu katika kila jambo wanalotofautiana. Na mwongozo kwa nyoyo. Na rehema kwa mwenye kushikamana nayo miongoni mwa kaumu za walioamini. أ هـ.

- Na Arraaziyu katika tafsiri yake 20 / 51 amesema:

Maana yake: Kwa hakika sisi hatujateremsha juu yako Quran ila, ili tuwabainishie wao mambo wanayohitilafiana kwayo kwa kupitia ubainishaji wa Quran hii. Na wanaotofautiana hao ni watu wa mila na matamanio ya nafsi. Na kile walichohitilafiana kwacho ni dini. Kwa mfano: Kumpwekesha Allah, Ushirikina, kulazimishwa, Kadari, kuthibitisha kiama na kukikanusha. Na mfano wa hukumu, kwa mfano wao waliharamisha vitu vya halali kama mnyama Bahira, Saiba na wengineo. Na walihalalisha vitu vya haramu kama mizoga أ هـ.

- Na mwenye Attahriiru Wattanwiiru katika 14/193 na zile kurasa za baada yake:

Imekusudiwa kufananisha [kushabihisha] hali ya washirikina inayosimuliwa kuwahusu wao na ukafiri wao katika ubaya wa matendo yao na hukumu zao, imefananishwa na hali ya nyumati zilizopotea kabla yao. Na amabao shetani aliwapumbaza miongoni mwa nyumati zilizoangamizwa, mfano uma wa Adi na Thamudi na nyumati za sasa kama vile Wayahudi na Wakristo… Na shetani alivyowapambia matendo yao hii ni kinaya (lugha fumbo) maana yake ni maasi. Na miongoni mwayo ni kutokuwa na Imani na Mitume, na huo ndio ukamilifu wa kufananisha. Na miongoni mwake kuna bidaa (uzushi katika dini) unaokataana na kile walichokuja nacho Mitume – amani ziwe juu yao – kwa mfano bidaa ya washirikina katika mnyama Bahira na Saiba. Na makusudio ni kuwa washirikina walienenda mwenendo wa wale walio kabla yao miongoni mwa nyumati ambazo matendo yao yalipambiwa na shetani... ﴿**Na hatukukuteremshia Kitabu (hiki) isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na (pia kiwe) uwongozi na rehema kwa watu wanaoamini** ﴾**.** An-Nahl 64. Imeunganishwa na sentensi ya kiapo [Wallahi! Sisi tulituma…].

Na uhusiano wake ni kuwa Quran imeteremshwa ili kutimiliza mwongozo na kufunua utata uliotokeza kwa nyumati zilizopita na za sasa. Na utata huo ukaacha athari zake kwa Warabu na wenginie. Na pale ilipotajwa upotevu wao na utata wanaouleta. Hilo limefuatiwa na kubainisha hekima ya kumpeleka Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na kuteremshiwa Quran. Kwa hiyo Quran imekuja ikiwa ni yenye kuwabainishia washirikina upotevu wao, ubainifu ambao hautoi njia ya kuingia katika nafsi. Na imeeleza kwa ufasaha ambao hauachi nafasi ya kutahayari katika akili. Na ni rehema kwa waumini kwa kile ilichowajaza wao kutokana na imani yao miongoni mwa heri za dunia na akhera.

Na imeeleza kuhusu upotofu kwa kutumia neno ﴿**yale ambayo wanakhitalifiana** ﴾ ili kuashiria kuwa sababu ya kupotea kwao ni kule kutofautiana kwao na manabii wao. Kwani upotofu wa Warabu ulitofautiana katika kuyaabudu masanamu. Kila kabila miongoni mwao liliabudu sanamu lake. Na baadhi yao waliabudu jua na nyota. Na kila kabila lilijifanyia matendo fulani na kudai kuwa matendo hayo ndio dini sahihi. Na wakakhitilafiana na Waislamu katika yote hayo kwa upande wa dini.

Na kuletwa kwa muundo wa kufunga katika kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Na hatukukuteremshia Kitabu (hiki) isipokuwa uwabainishie** ﴾ inakusudia kujumuisha yote miongoni mwa mambo muhimu katika lengo la Quran na faida yake ambayo kwa hiyo ndio imeteremshwa…. Ili wasikilizaji miongoni mwa waumini na makafiri wapende kuipokea na kuizingatia. Kila mmoja kwa kile kinachoendana na hali yake, ili wawe sawa sawa katika kuongoka.

Kisha kwa hakika muundo huu wa kufunga unazivunja kauli za washirikina walioidhania kuwa Quran imeteremshwa ili kutaja visa vya kufurahisha nyoyo nyakati za usiku na mfano wake. Hadi ilifikia, mpotoshaji wao alisema: Mimi nitakuleteeni visa bora kuliko alivyokuja navyo Muhammad. Nitakuleteeni kisa cha Rostom na Isfandiyaaru. Makusudio muhimu kabisa ya Quran ni hizi faida zenye kukusanya misingi yote ya heri. أهـ .

ambapo hizo aya zilianza na hilo. Na akafuatisha la pili kuwa ni mwongozo na rehema kwa waumini.

### [**Atakayedai Kuwa Muhammad Ana Mwalimu Wa Kibinadamu, Na Amtaje**]

***3 – Hebu turudi kwa mara ya tatu, na tuwaambie wale wanaodai kuwa Muhammad alikuwa anafundishwa na mtu: ‘‘Tuambieni, huyo mwalimu wake jina lake nani? Na ni nani huyo aliyemuona na kumsikia? Na alimsikia akisema nini? Na hilo lilikuwa lini? Lilikuwa wapi?*** Kwani neno mtu linawaelezea viumbe vitembeavyo ardhini vikiwa vimetulizana; vinaonekana na watu wengine vikienda na kurudi. Kwa hiyo usisikilize madai yao bila ya kuainisha na kufafanua. Bali madai yao yanakuwa kama vile wale wanaomzushia Allah kuwa ana washirika wakati washirika hao hawapo ila katika fikra zao na ufahamu wao mbaya. Basi mtu huyo ataambiwa kama walivyoambiwa hao ﴿**Sema: ‘‘Watajeni (washirika hao). Au je, mnamwambia asiyoyajua katika ardhi; au ni maneno matupu (tu hayo mnayoyasema, yamo midomoni mwenu tu, hayamo katika itikadi yenu)?’’** ﴾ Ar Raad 33.

Bali tunasema: ‘‘Je, huyu Nabii alizaliwa katika Mars, au alikulia katika eneo la mbali mno na dunia, na kwa hiyo hajafika kwa watu wake ila baada ya kufikia utu uzima na kukamilika. Kisha baada ya hapo hawakuwa wakimuona ila mara chache mno? Je, hakuzaliwa katika maeneo yao? Je, hakuwa akitembea katikati yao huku akiwa ameambatana nao na kugusana nao? Je, hawakuwa wakimwona kwa macho yao akiwa na mavazi yake na kipando chake? ﴿**Au hawakumjua Mtume wao, (tabia zake na mwendo wake), ndiyo maana wanamkanusha?** ﴾ Al-Muninun 69.

Naam, nafsi zao ziliwapambia kusema neno hili ﴿**Yuko mtu anayemfundisha** ﴾ An-Nahl 103. Lakini, hivi unawaona wao walikuwa wanamaanisha hasa waliposema neno hili, na walikuwa wakiashiria mtu kweli waliyemjua na mwenye cheo hicho cha kielimu? Sivyo hivyo, kwa hakika haikuwa muhimu kwao kama walikuwa wanamaanisha kwa haki. Na kwa hakika jambo walilolitilia umuhimu ni kuziondoa nafsi zao na aibu ya kunyamaza na kushindwa kihoja. Kwa kutumia taswira ya aina yoyote ile inayoafikiana nao katika miundo ya maneno: kwa ukweli au uongo, kwa kumaanisha au kwa mzaha.

***Na Ni Kipi Kitakachokujulisha Ni Nani Huyo Mtu Aliyekuwa Anamfundisha?***

Hivi unadhani kuwa wao walikuwa na uthubutu wa kuunasibisha ufundishaji huo kwa mmoja wao? Sivyo hivyo, kwa hakika wao wenyewe walijiona wazi wazi kuwa ni ujinga kudai kuwa wanamfundisha mtu aliyewajia na kile wasichokijua wao wala baba zao.

Au unadhani kuwa wao pale walipojua kuwa ardhi ya Makka haina wataalamu wa dini na historia katika zama za kupewa utume kwa Mtume Muhammad, kwa hiyo wakamkusudia mtu fulani miongo mwa wataalamu wa Madina au Shamu au wale wasio wa miji miwili hiyo kisha wakawanasibishia jambo la kumfundisha? Sivyo hivyo, kwa hakika ndimi zao hazikuwakubalia kutamka neno hili pia!

Basi ni nani huyo au hayupo …?

Kwa hakika walijikuta wanalazimika kumtafuta mtu mwenye kuwa na masharti mawili: la kwanza: awe ni miongoni mwa wakazi wa Makka yenyewe ili kuyapigia debe madai yao ya kuwa anakutana naye na kumsomea asubuhi na jioni. Na la pili: awe si wa miongoni mwao na mila zao ili iwezekane kusema kuwa mtu huyo ana elimu ya kile wasichokijua. Kwa hakika walitafuta sifa hizi na wakazipata. Je, wajua walizipata wapi?.. Kwa muhunzi wa Kirumi[1]!!

---

[1] Kutoka kwa Ibnu Abbas Allah amuwie radhi yeye na baba yake amesema: **Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akifundishwa na Qaynan [muhunzi] wa Makka. Alikuwa anaongea lugha ya kigeni – si Kiarabu, na jina lake lilikuwa Bal-aamu. Na washirikina walikuwa wakimwona Mtume rehema na amani ziwe juu yake pale alipokuwa akiingia na kutoka kwake, wakasema: Kwa hakika anafundishwa na Bal-aamu. Ndipo Allah Mtukufu akateremsha utajo wake ﴿Na bila shaka tunajua kwamba wanasema: ''Yuko mtu anayemfundisha.'' (Lakini) lugha ya yule wanayemwelekezea (kuwa anamfundisha Mtume) ni ya kigeni, na hii (lugha inayotumika katika Quran) ni lugha ya Kiarabu bulbul).** An-Nahl 103. Imepokewa na Attwabary 14 / 177. Na Suyutwi katika Adduraru Almanthuuru 4 / 247, amesema: Imetolewa na Ibnu Jariri na Ibnu Abuu Haatimu na Ibnu Mardawayhi kwa sanadi dhaifu أهـ .

Pia zipo riwaya nyingi zinazohusu sababu ya kuteremka kwa aya hii. Zinajumuika kwa kusema kuwa sababu ya kushuka kwake ni madai ya washirikina ya kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake anajifunza kwa mtu – na sio kwa malaika aliyetumwa kutoka kwa Allah – na aghlabu ya riwaya hizi zinazunguka juu ya mhunzi Mkristo aliyekuwa mtumwa kwa ukoo wa Alhadhwaramiyu. Kwa maelezo zaidi rejea: Sababu za kuteremka aya cha Alwaahidiyyu 281. Attwabary 14 / 177, 178. Adduraru

Naam, huko Makka walimpata kijana anayejulikana vilabuni na masokoni. Lakini hajulikani kuwa na elimu hizo iwe kidogo wala wingi. Ila yeye hakuwa asiyejua kusoma wala mwabudu masanamu kama wao. Bali alikuwa Mkristo anayejua kusoma na kuandika. Kwa ajili hiyo, kwa madai yao, yeye alikuwa anafaa zaidi kuwa mwalimu wa Muhammad. Na kwa hiyo, yeye ndiye mwalimu wa wataalamu wa Kiyahudi, Kikristo na dunia yote. Na kama utawauliza, je, kijana huyo alijishughulisha na kujifunza vitabu na kuchambua maswala ya asili na yale ya kupachikwa, kurudisha yale yenye utata na kuyaweka katika yasiyo na utata. Je, mwalimu huyo alikuwa amewekewa nyenzo ya kufahamu na kufahamisha katika akili yake na ulimi wake …

Ungejua kuwa mwenyewe alikuwa ni muhunzi aliyejitumbukiza katika shoka na vyuma vyake vya kugongea. Na kuwa yeye alikuwa mtu wa kawaida hana anachojua katika hicho Kitabu isipokuwa matamanio tu. Mgeni wa lugha, kusoma kwake hakuvuki zaidi ya kuwa ni lahaja ya mtaani ambayo Muhammad haijui na pia hakuna yeyote anayoijua miongo mwa watu wake. Lakini yote hayo hayakuwa kizuizi cha baina yake na kupewa jina la mwalimu, jina ambalo walimpa kinguvu licha ya kukataa kwa wapinzani wao!

[**Yule Ambaye Kwake Yeye Wigo Wa Kufanya Kitu Kikweli Kweli Ni Mfinyu, Basi Mtu Huyo Hana Nafasi Isipokuwa Ombwe La Mizaha**]

Hivyo hivyo, wigo wa kufanya kitu kikweli kweli umekuwa finyu kwao wao. Basi hawana nafasi isipokuwa ombwe la mizaha. Na hivi hivi wamebobea katika mizaha yao hadi wakatoka nje ya utulivu wa kiakili. Mfano wao ukawa kama mfano wa yule asemaye: Kwa hakika elimu inapatikana kwa mjinga. Na kwamba mwanadamu anajifunza kuongea maneno yake kutoka kwa kasuku! Na hili linatosha kuwa kushindwa na fedheha kwa mwenye kusema hayo. ﴿**Na bila shaka tunajua kwamba wanasema: ‘‘Yuko mtu anayemfundisha.’’ (Lakini) lugha ya yule wanayemwelekezea (kuwa anamfundisha Mtume) ni ya kigeni, na hii (lugha inayotumika katika Quran) ni lugha ya Kiarabu bulbul** ﴾**.** An-Nahl 103.

---

Almanthuuru 4 / 247. Asswahiihu Almusnadu cha sababu za kuteremka aya cha Muqbilu bin Haadiy 90. Al-Iswaaba 738, 1065, 9216, 9369.

Ndio, wao wameonelea katika mtindo huu kuna utamu na chumvi ya vichekesho, kitu ambacho kinasaidia kuondo uchungu wa uongo na batili. Na wameonelea kuwa katika taswira hii ya kifikra na uropokaji na kejeli zinazoweza kuponya vifua vyao na kuwafanya wao wanajichekesha kwa kuijaza midomo yao. Lakini wao, hawakutambua kuwa katika kejeli hii kuna kejeli dhidi yao. Na kwamba wao wenyewe wameshashuhudia katika hilo kwamba wao ni umma mjinga kuliko nyumati nyingine. Na kwamba kila mgeni kwao wao – hata kama atakuwa ni kijana mtumwa wa kuzurura masokoni – basi anafaa kuitwa kuwa ana elimu wasiyo nayo wao. Ee! Ajabu ilioje ya tamko ambalo kama wangeliacha kulitamka ingekuwa bora kwao na kuwastiri wao! Na ee! Silaha ilioje, waliyoitaka kumjeruhi nayo adui yao lakini ikawajeruhi wao wenyewe bila ya kutambua.

Ama ile haki waliyokuwa wakiipinga, kwa hakika, naapa kwa Allah, kwa tuhuma zao hizi, wameizidishia nguvu juu ya nguvu. Na hilo ni kwa kuwa wao, pale walipotoka kutafuta mtu miongoni mwa wanadamu anayewezekana kumpachika elimu hii ya ki-Muhammad, hawakuweza kumwekea chanzo cha elimu yake kilicho nje ya mipaka ya mji wake. Bali juhudi yao ya mwisho kuitoa ilikuwa hila zao. Na mshale wao wa mwisho waliourusha kutoka katika pinde zao ni kule kuja na kijana huyu ambaye habari zake zilikuwa zikijulikana.

Nywele zangu zilisisimuka, lau kama kijana huyu angekuwa ndio rejea ya kielimu kama walivyotaka kumsifu, basi ni kipi kilichowazuia wasichukue kutoka kwake kama walivyochukua kutoka kwa swahiba wao? Na kwa kufanya hivyo wangekuwa wanapumzika na tabu zake, na wanatibu kwa namna ya kuendea katika ugonjwa ulipo. Bali kizuizi ni kipi kwa kijana huyo kuonesha ulimwenguni kurasa zake na akajipatia utukufu wa kuwa mwalimu katika historia. Au yeye mwenyewe atawale huo uongozi wa dunia?

Nywele zangu zimesisimuka, kwa nini elimu hiyo ngeni hawajainasibisha kwa watu wake wanaosifika nayo miongoni mwa wasomi na wabobezi wa Kiyahudi wa Madina au kwa makasisi na mapadri wa Shamu. Kwa kuwa hao ndio ambao wamemaliza umri wao katika kujifunza na kuifundisha elimu hiyo? Je, hilo si – lau kama lingewezekana au linafanana na kuwezekana – lingekuwa bora kuliambatanisha, na lingependeza zaidi kuliunganisha, na lipo karibu zaidi katika kulipigia debe na lipo mbali zaidi na kule kulipachika kwa muhunzi wa Makka? Au ardhi

ilikuwa finyu kwao wao, na kwa hiyo hawakumpata yeyote mwenye kufaa kuliko yeye, wala mjuzi wa dini na historia?

Naapa kwa Allah, lau kana kwamba wao wengelipata mlango wa kujulisha kuwa ana mwalimu wa nje, uliomadhubuti zaidi kuliko milango mingine basi wangeungia kwa maana ya kibri cha hali ya juu. Kibri ambacho kingewatoa katika kile kilichowabania wigo wa kutuhumu hadi wakajitumbukiza katika jambo hili lisilowezekana na ambalo lipo wazi kabisa na linafedhehesha kwa kauli zao zilizopotoka.

Hawa ni watu wa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake. Na wao walikuwa wanapupa zaidi kuliko watu wote dhidi ya mgomvi wao. Na wanajua zaidi kuliko watu wote kuhusu safari na misafara yake. Na wamedhibiti harakati zake na utulivu wake. Wameshindwa, kama unavyoona, kuweka uhusiano wa kielimu baina yake na baina ya watu wenye elimu katika zama zake. Ni wapi na wapi kwa wapinzani wa leo, huku zikiwa zimeshapita zaidi ya karne kumi na tatu na nusu katika matukio hayo, kalamu zimeshakauka, na kurasa zimeshakunjwa, eti wao wanaendelea kuutafuta huo muunganiko wa kielimu katika malundo ya taka za kihistoria. Na kwa upande ambao watu wake walishindwa kuufukua?

Zinduka, hebu na wazipumzishe nafsi zao ziachane na tabu za kutafiti. Kwa hakika Makuraishi wamewatosha katika tabu hiyo. Na washughulike na upande mwingine usiokuwa huu ambao, historia na mantiki zimeshahukumu kuwa kila jaribio la kufanya hivyo linashindwa. Na kama watakataa, basi na wajue kuwa kila utata wanaouibua dhidi ya haki ya wazi, basi hiyo haki itasimama na kuutumia huo utata kuwa hoja yake miongoni mwa hoja zake.

## [T**ahayari Kwa Wabishi Na Kutikisika Kwao Katika Mjadala Hapo Kale Na Sasa**]

**4- Na turudi mara ya nne na ya mwisho, na tunasema: *Lau ingekuwa (kuinasibisha elimu hii ya KiQuran kwa mafundisho ya wanadamu) hilo lingekuwa ni miongoni mwa madai ambayo yanaeleza kuhusu fikra au utata uliosimama kwa dhati ya mwenye nao, basi ingesimama hapo hapo kwa wanaomkosoa na wasingevuka.*** Hilo ni kwa kuwa akili ingeepushwa na nafsi yake, katika kueleza sababu ya tofauti kuu baina ya maisha ya Muhammad ya wakati uliopita na maisha yake ya sasa – yaani maisha yake ya kabla ya kupewa utume na yale ya baada ya kupewa

utume – basi hiyo akili isingekubali zaidi ya kutoa hukumu ya kusema kuwa elimu hii ni mpya imezaliwa na mafundisho mapya.

Kwani watu hawajapatapo kuwa na walimu duniani zaidi ya wa kibinadamu. Kwa hiyo jambo la kwanza kuingia akilini lingekuwa kuna mtu aliyesimamia mafundisho haya. Na lau kama mkosoaji angepata chembe ndogo ya kuiegemea katika kukosoa miongoni mwa sababu halisi au zinazowezekana kumfanya awe na kitu fulani cha kumtosheleza kwa sababu hiyo iliyo baina yake na baina ya nafsi yake, basi asingeiridhia awe na kitu mbadala cha sababu hiyo. Na asingeiacha na kwenda katika kutoa sababu nyingine zozote zitakavyokuwa.

Lakini hawa wakosoaji, tangu ilipoteremka Quran mpaka siku yetu ya leo hawajaacha kuendelea kuwa wanatahayari katika kuinasibisha Quaran hii. Hawatambui, je, wainasibishe kwa mafundisho ya wanadamu kama mlivyosikia hivi punde, au wairejeshe kwa nafsi ya Muhammad mwenyewe kama mlivyosikia hapo kabla. Au waijumuishe baina ya kuinasabisha kuwili na hivyo wamwambie mwenyewe ya kuwa yeye ni ﴿**Amefunzwa (na watu haya, hakuletewa Wahyi; na) ni mwendawazimu** ﴾**.** Ad-Dukhan 14.

### [**Nadharia Ya Ufunuo Wa Nafsini Sio Mpya**]

Na mwenye kufuatilia aina za mijadala iliyoelezwa na Quran, ile inayohusiana na wakosoaji wake, ataona kuwa, kuinasibisha kwao Quran na mafundisho ya kibinadamu ndio maneno yaliyokuwa ya asilimia chache mno kutokea katika ndimi zao. Na kuwa maneno yaliyotokea sana katika mijadala yao ni kule kuinasibisha na nafsi[1] ya mwenye kuileta. Licha ya tofauti zao

[1]Na rai hii ndio inapigiwa debe na wapinzani wa kisasa, kwa kutumia jina la (Ufunuo wa maono ya kinafsi) huku wakidai kuwa wao kwa kutumia jina hili, ndio wametuletea na rai mpya ya kisayansi. Na kwa hakika yenyewe si mpya. Kiuhalisia hiyo ni rai ya zama za kale za Jahiliya. Haitofautiani nao kiujumla wake kwa maelezo yake mapana. Kwa hakika wao wamemswawiri Nabii rehema na amani ziwe juu yake na aali wake kuwa yeye ni mtu mwenye kuwa na taswira pana na hisia ya kina, kwa hiyo yeye ni mshairi. Kisha wakazidisaha na kuifanya hali yake ya kiakili inachupa mipaka sana kuzidi hisia zake hadi inampitikia katika mawazo yake ya kuwa anamwona na kumsikia mtu anamuongelesha. Na hicho anachokiona na kukisikia si kingine ila picha ya taswira ya hisia zake. Kwa hiyo yeye ni mwendawazimu au ana ndoto za mchana. Lakini wao hawakuweza kuvumilia na kudumu sana na sababu zao hizi. Wakalazimika kulihama neno la (ufunuo wa kinafsia) pale ilipodhihiri kwao, ndani ya Quran, upande wa habari za yaliyopita na yajayo, wakasema: Huenda amaezichukua kutoka katika midomo ya wataalamu katika misafara yake ya kibiashara, kwa hiyo yeye amefundishwa na wanadamu. Je, katika haya yote unaona jipya lipi? Je, yote sio maneno yanayorudiwa na kuigiza kauli za wajinga wa kikurayshi? Na hivi hivi, upingaji katika nguo yake mpya

katika kuainisha hali hiyo ya kinafsi, na kwa yenyewe ndipo Quran imechimbuka: Je, ni ushairi, au uwendawazimu, au ndoto zilizoparaganyika …

Hebu tazama: wamegeuza mangapi miongoni mwa taswira za rai katika maswala haya? Imefikia mpaka, wao wenyewe hawajasimama katika mpaka wanaoweza kuuweka katika maneno madhubuti kama Quran. Na katika akili madhubuti kama akili ya mwenye Quran. Bali walienda mbali zaidi katika hali za kinafsia, hali ambazo inawezekana kwazo, yakatoka maneno ya wenye akili na wendawazimu .. Kwa hakika hilo ni miongoni mwa ushahidi wa wazi juu ya kuwa wao hawakuwa katika njia hii au ile wakiashiria tuhuma zilizothibiti na zenye kuamka katika uhalisia wa nje au katika itikadi zao.

Na kwa hakika si vinginevyo, walitaka kutoa kila uwezekano na makadirio, huku wakifumbia macho yale yaliyomo miongoni mwa mambo ambayo hayawezi kutokea na yapo ng`ambo[1] mno na ya kutengana sana. Ili kwayo, wathibitishe kwa kupitia vumbi na ufahamu mbaya katika macho ya wenye kutazama katika mwangaza wa ukweli. Na kwa hayo watoe miba ya shaka katika njia ya wanaokwenda katika viwanja vya yakini.

---

umekuwa kopi iliyokopiwa, bali imebadilishwa na kuwa kopi mbaya kuliko ile nguo yake ya kale. Na chakula cha fikra hizi zinazojifanya za kisasa katika zama za sasa kimekuwa ni kuchukua kutoka mtawanyiko wa meza za chakula zilizoachwa na zile nyoyo zilizokuwa ngumu kama mawe katika zama za mwanzo za Jahiliya. ﴿**Vivyo hivyo walisema wale waliokuwa kabla yao, mfano wa kauli yao hii; nyoyo zao zimefanana.** ﴾ Al-Baqarah 118.

Kama unashangaa, licha ya hayo yote basi utashangaa zaidi, na kauli yao isemayo kuwa yeye alikuwa ni mkweli mwaminifu. Na kuwa yeye alikuwa na udhuru katika kuzinasibisha ndoto zake na ufunuo wa Mungu. Kwa sababu ndoto zake za nguvu zinamuonesha yeye ya kuwa huo ni ufunuo wa Mungu. Kwa hiyo, yeye hakutoa ushahidi isipokuwa ule alioujua. Na hili pia, Allah Mtukufu ameshatusimulia kuhusiana na watangulizi wao pale anaposema: ﴿**… Basi wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu hao wanakanusha hoja za Mwenyezi Mungu** ﴾. Al-An-am 33. Basi kama huu ndio udhuru wake katika kutaswawari ndoto zake na kusikia kwake, basi udhuru wake upo wapi katika wito wake wa kuwa yeye hakuwa akijua habari hizo. Si yeye wala watu wake wa hapo kabla ya hayo. Wakati ambapo yeye ameshayasikia hapo kabla, kwa mujibu wa madai yao? Kwa hiyo na waseme, ya kuwa yeye ameizusha, ili kwa hilo itimie kwao wao kule kufuatisha kila kauli za uzushi. Lakini wao hawataki kusema maneno haya kwa kuwa wao wanajifanya ni waadilifu na wanatumia akili. Zinduka, kwa hakika hilo wameshalisema bila ya wao wenyewe kutambua. [Daraazu].

[1] Ng`ambo: yapo mbali na yametengana sana.

Kwa hakika tunajua kuwa wao walikuwa na maazimio ya nafsi zao hawana utulivu juu ya rai nzuri wanayoiridhia miongoni mwa rai hizo. Na kwamba wao walikuwa kila wanapoweka mikono yao katika rai miongoni mwa rai hizo. Na kwa rai hiyo walitaka kuifumia Quran nguo. Na wakaipata ikiwa ya mbali mno katika vionjo vyao, haifai kuwa nguo yake. Na kwa hiyo, haraka haraka wakakimbilia jaribio la rai ya pili. Na yenyewe ikiwa si yenye kufaa kuishinda ile waliyoikataa, wanaikusudia ya tatu… na hivyo hivyo ni mizunguko na hawatulii katika hali moja kutokana na wasi wasi.

Kama utapenda kuzipitia taswira hizi zinazochekesha miongoni mwa blaa blaa za kimijadala, hebu soma namna zilivyoelezwa katika Quran: ﴿**Lakini makafiri walisema: ‘‘(Hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika, (zilizokorogeka)’’. Na pengine wanasema); ‘‘Bali ameyabuni mwenyewe)’’. (Na mara nyingine tena husema): ‘‘Bali huyu ni mtunga mashairi tu.** ﴾ Al-Anbiyaa 5. Huu ndio mjumuisho mfupi unaokuwakilishia yale yaliyomo katika mfululizo wa herufi za mitetereko na viwango vya kile kilichowapata miongoni mwa kutahayari na kuyumbayumba katika rai zao.

Na kupitia hizo zinakuonesha picha ya shahidi wa uongo pale anapohisi vibaya kwa msimamo wake: namna anavyobadilika badilika kulia na kushoto. Na namna njia zote zinapokuwa ni njia panda kwake yeye, hajui aende wapi, katika kusahihisha yale anayojaribu kuyarekebisha miongoni mwa mambo yasiyowezekana kurekebishwa. ﴿**Tazama jinsi wanavyokupigia mifano (ya uwongo; mara umerogwa, mara muongo, mara…). Basi wakapotea; kwa hivyo hawawezi kupata njia (ya kuwapeleka katika haki** ﴾**.** Bani Israil 48. Al-Furqan 9.

۞ ۞ ۞

## [**HAATUA YA TATU YA UTAFITI**:

## **Utafiti Katika Mazingira Ya Ufunuo Na Yale Maalum Yaliyoambatana Nayo Katika Chanzo Cha Quran**]

Na kwa sasa – tumeshakupitisha katika hatua mbili hizi za utafiti. Na tumeshakuonesha kuwa: Katika Quran hakuna chanzo cha kibinadamu, si katika nafsi ya mwenyewe wala kwa yoyote katika wanadamu. Na kuwa kila aliyejaribu kuifanya hii Quran kuwa (kazi ya kibinadamu) jambo lake hilo litamtaabisha. Na hoja zitasimama kueleza juu ya kushindwa kwake,

kuyumbayumba kwake na kubwabwaja kwake. Na kuzuiwa kwake na kibri chake – kwa hakika ni wajibu kwetu twende hatua ya tatu ili tukitafute hicho chanzo katika mawanda ya nje ya huu uwanda wa kibinadamu kwa ujumla; na tusisimame katika Quran pale waliposimamia wapingaji wa kale na wa sasa, wakiwa vizabizabina katika hilo, baina ya hizi njia mbili wakati mwingine wakichukuwa kwa moja wapo, na wakati mwingine wanachukua katika vyote viwili kwa pamoja. Wakijibadilisha badilisha hivi na hivi kwa fasidi kwenda kwa fasidi. Na kwenda katika ufisadi uliounganishwa hayo mawili na kuwa mkubwa zaidi kuliko hiyo mifisadi miwili yote. Sivyo hivyo, kwa hakika akili inatutaka tubatilishe yale yaliyobatilishwa na hoja bila ya kuleta kibri, na tumfuate katika mwendo wake hadi tufikie haki ya wazi.

Ama hawa wapingaji, kwa hakika hakuna kilichowakalisha kitako kufanya utafiti na kuufatilia – kama wanavyodai – isipokuwa ni kule kuchunga kwao utukufu wa maumbile ya ulimwengu. Na ili kuhifadhi sababu za kawaida zinazofanya kutokea sauti za wanadamu katika mambo yao ya kiakili na ya kunukuu. Kwa hakika uaminifu wao wa elimu ya maumbile umewakatalia wasichupe mipaka yake na kutoka kwenda katika kutafuta kitu kisichopatwa na macho yao.

Na hawajajaribu mfano wake katika nafsi zao. Na wewe umeshajua kuwa hiki walichokidhania ni uaminifu juu ya tabia za vitu kimewabadilikia na kuwa dhidi yao. Kwani katika njia yake wameshautoboa ukuta wa maumbile wa akili ya mwanadamu, na uhalisia wa kihistoria. Kwa hiyo wakakusanya baina ya vinyume viwili na kubadilisha mambo ya kihistoria. Wakazitenza nguvu tabia za vitu na kuzibebesha mambo visivyoweza kuvibeba. Ni akili gani inayoridhia kusimama msimamo kama huu, wa kuitetea ada yake na kuingamiza akili yake!!

Bali lililo la haki ni kuwa, kuna kizuizi kingine kinachowazuia wasifuate mwendo wa kwenda nasi. Lakini wao wanatuficha hicho kitu: ni kibri katika vifua vyao, eti wampe uongozi mtu aliyewapanda juu ya vichwa vyao na kudai kuwa yeye ni Mtume wa Allah kwao wao. Na kuwaamrisha na kuwakataza, anawawajibisha kumtii. Kisha yeye akiwa hivyo awaelekeze wao mambo ya kweli yaliyo machungu. Na kwa hiyo hicho kinazuia baina yao na baina ya kulichopita na ambacho wao wanashikamana nacho. Na matamanio ya nafsi ambayo wao wanayaabudu ﴿**Bali amewajia kwa haki, na wengi katika wao wanaichukia haki.** ﴾. Al – Muminun 70.

Tuwaache wakae pale wao wenyewe waliporidhia kukaa. Nasi tuendelee kuufuatilia utafiti juu ya haki hii huku tukitarajia kwa Allah atuongoze kuifikia hiyo haki. Na hakika sisi, Allah akipenda, ni wenye kuongoka.

۞ ۞ ۞

## [**Tukio La Ufunuo Na Uchambuzi Wa Matokeo Yake**]

Usije ukadhani kuwa, katika hatua hii ya tatu sisi tutahangaika jangwani tukitangatanga, au mwendo utatutupa katika eneo la mbali na kutuweka katika safari tusioikusudia. Sivyo hivyo, kamwe katika utafiti huu hatutotoka nje ya duara lenye mipaka maalum tunaloliona kuwa lenyewe ndio kusudio la siri tunayoitafuta. Na hayo ni kutokana na kutafiti hali mubashara, ambazo ndani yake Quran ilikuwa ikidhihiri kwa ulimi wa Muhammad bin Abdullah rehema na amani za Allah ziwe juu yake yeye na aali wake.

Sote tunayajua matukio hayo ya ajabu yaliyokuwa yakionekana katika uso wake mtukufu kila mara, pale anapoteremshiwa Quran. Na jambo hilo lilikuwa halijifichi kwa yeyote kwa wale ambao walikuwa wakimwangalia, na walikuwa wakimwona[1]:

- Kwa hakika uso wake[2] ulikuwa mwekundu ghafla[3].

---

[1] Sifa zote hizi ni zenye kuthibitishwa katika hadithi sahihi zilizo katika Bukhari, Muslimu na kwa Abuu Daudi, Attirmidhiyu na wengineo. [Daraazu].

Nikasema: na hizi ndizo hadithi zenyewe kwa urefu, kwa kuwa zenyewe zina faida nyingi:

[2] Katika hadithi ya Yaalii bin Ummayya kwa hakika alikuwa anamwambia Omar Allah amuwie radhi: ‘‘**Nilioneshwa Nabii rehema na amani ziwe juu yake pale alipoteremshiwa ufunuo. Akasema: Pale Nabii rehema na amani ziwe juu alipokuwa Jaaranah – akiwa pamoja na maswahaba wake – alijiwa na mtu na kumwambia: Ewe Mtume wa Allah, waonaje kwa mtu aliyenuia kufanya Umra huku akiwa amejipaka uturi mwingi? Mtume rehema na amani ziwe juu yake akanyamaza kwa muda. Akajiwa na ufunuo. Omari Allah amuwie radhi alimuashiria Yaaliyu, na Yaaliyu akaja – huku Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akiwa na nguo aliyofunikwa nayo – akaingiza kichwa chake, na kutahamaki akamkuta Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akiwa na uso mwekundu huku akipumua kwa sauti katika pua zake. Kisha akaachwa …’’** Hadithi imepokewa na Bukhari na Muslimu: Bukhari ameisimulia katika Alhaji 1536, na Muslimu katika Alhaji 8.

[3] Katika hadithi ya zaidi bin Thaabiti: **‘‘Mtume rehema na amani ziwe juu yake alimsomea ﴿Laa yastawiii…’’ papo hapo akajiwa na Ibnu Ummu Maktuum akasema huku Mtume akiwa ananisomea mimi: Ewe Mtume wa Allah, naapa kwa Allah, lau ningeweza kupigana jihadi ningepigana – na alikuwa kipofu – hapo Allah**

- Alipatwa na tabu sana[1].
- Mpaka paji lake la uso linakuwa linatiririka jasho jingi[2].
- Mwili wake ulikuwa mzito mno mpaka paja lake likakaribia kuvunja paja la yule aliyekaa kandoni mwake[3].
- Na hata kama alikuwa amepanda kipando basi hicho kipando kingepiga magoti[4].
- Na pamoja na hayo walikuwa wakisikia kutoka katika uso wake sauti zilizochanganyika, zinazofanana na mvumo wa nyuki[5]… kisha haupiti

---

**akateremsha kwa Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake huku paja lake likiwa katika paja langu. Basi ikawa uzito sana kwangu hadi nikaogopea paja langu *lisiturdhu* [yaani lisivunjike]. Kisha akaachwa na hapo ndipo Allah aliteremsha ﴿…isipokuwa wenye madhara… ﴾''**. Imepokewa na Bukhari katika Attafsiiri 4592.

[1] Katika hadithi ya Ubaadatu Bin Swaamitu: **''Nabii wa Allah rehema na amani ziwe juu yake pindi anapoteremshiwa ufunuo, alikuwa anataabika kwa ajili hiyo huku uso wake ukiwa mwekundu wenye weusi…''** Hiyo hadithi. Imepokewa na Muslimu katika Alhuduudi 13. Na maana ya Abarhaau ni: ukali wa tabu. Na katika hadithi Abdullah bin Abbas Allah amuwie radhi yeye na baba yake: **''Mtume rehema na amani ziwe juu yake akishughulikia uteremsho wa ufunuo kwa tabu…''** Hiyo hadithi. Imepokewa na Bukhari na Muslimu: Bukhari ameipokea katika mwanzo wa ufunuo 4. Na Muslimu katika Aswalaati 148.

[2] Katika hadithi ya Aisha Allah amuwie radhi amesema: **''… kwa hakika nilimuona [yaani Nabii rehema na amani ziwe juu yake] akiteremshiwa ufunuo katika siku yenye baridi kali na yeye akiwa anahisi joto, na paji la uso wake likichuruzika jasho''**. Imepokewa na Bukhari na Muslimu: Imepokewa na Bukhari katika Mwanzo wa Ufunuo 2, na Muslimu katika Alfadhwaaili 86.

[3] Katika hadithi ya Zaidu bin Thaabiti iliyopita ndani kuna: **''… hapo Allah akateremsha kwa Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake huku paja lake likiwa katika paja langu. Basi ikawa uzito sana kwangu hadi nikaogopea paja langu lisiturdhu [yaani lisivunjike]…''** Hadithi hiyo. Imetangulia katika maelezo ya chini ya hapo nyuma kidogo.

[4]Katika hadithi ya Aisha Allah amuwie radhi: **''Kama ufunuo utamjia Mtume rehema na amani ziwe juu yake na yeye akiwa juu ya kipando chake, basi hicho kipando kitakaa chini [yaani kitapiga magoti na shingo yake atailaza chini]''**. Imepokewa na Ahamad 6 / 118 na Alhaithamiyu akaisemea hadithi hii katika Almajmaa 8 / 257: na wapokezi wake wana daraja ya usahihi. أ هـ .

[5] Katika hadithi ya Omar bin Alkhatwabi Allah amuwie radhi: **''Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa, pindi anapoteremshiwa ufunuo, zikisikiwa kutoka katika uso wake kama mvumo [muungurumo] wa nyuki. Siku moja aliteremshiwa ufunuo, basi tulikaa saa nzima kisha akaachiwa naye akaelekea kibla …''** Hiyo hadithi. Imepokewa na Ahmadi 1 / 34. Na Attirmidhiyu katika tafsiiri ya Quran 3173. Na mwanazuoni nguli Ahmad Shaakir ameipa daraja ya usahihi 223. Na Al-Arnaawutwi ameipa daraja ya hasani katika Jaamiu Al-Usuuli 11 / 283.

muda anaachiwa na hizo tabu na kutahamaki yeye anasoma Quran mpya na utajo mpya[1].

Na atakayetaka kufanya tafiti juu ya chanzo cha Quran, basi haya hapa matirio (vyanzo) yake ya karibu zaidi. Na ambayo ndani yake watafiti wanatakiwa wafungike katika tafiti zao. Na tuwaongoze wale wanaotafuta haki wakipate wanachokitafuta. Hivi ni wapi tutapata sababu sahihi za athari ya kitu fulani kama hatujazitafuta pale ambapo ndipo palipodhihiri hiyo athari. Na sehemu ambapo uwepo wake unazungukia pia na kutokuwepo kwake?

Kwa sasa hebu na tutazame katika tukio hili: Je, lenyewe lilikuwa ni jambo la kujikalifisha sana na la kutengenezwa, na njia ya maandalizi na ambayo kwake yeye, fikra na maono yanajikusanya? Au limekuwa jambo lisilo na uchaguzi? Na kama litakuwa ni jambo lisilo na uchaguzi, je, lilikuwa na chanzo chake ndani ya nafsi kinachoanzisha sababu za kimaumbile na za kawaida. Kama vile vichocheo vya usingizi, au miongoni mwa sababu za kimaumbile zilizo nje ya utaratibu, kama vile kuwa na dosari katika nguvu ya mishipa ya fahamu? Au kilikuwa kitendo rejeshi kwa sababu za nje zilizojitenga na nguvu za nafsi?

Kwa hakika mtazamo mmoja tunaoweka katika dondoo za tukio hili ili zituongoze katika kujua kuwa lenyewe haliwezekani kuwa la kutengeneza na kujikalifisha. Na hasa hasa lau kama utatafakari vizuri sauti hizo mchanganyiko na ambazo zilikuwa zikisikika kutoka katika uso wa Mtume Mtukufu. Na vile vile, lau kama lingekuwa la kutengenezwa na kujikalifisha, basi lingekuwa linatii mamlaka yake na kwa hiyo lingekuwa hakuna hata siku moja akilitaka limjie nalo lisimjie, bali lingemjia Quran mpya kwa njia hii ambayo ameizoea katika kuliandaa. Na umeshajua[2] kuwa, ni mara nyingi ameitaka Quran katika nyakati akiwa na haja nayo, na alikuwa haipati isipokuwa pale tu anapotaka Allah.

- ***Kwa hiyo, hiyo ni hali isiyo ya uchaguzi.***

Kisha turejeshe jicho kwa mara nyingine ili tuone umbali mkubwa baina yake na baina ya hali ya tukio la usingizi wa kawaida unaomtokea

---

[1] Katika hadithi zote zilizopita tunapata kuwa, kusoma Quran kunafuatishwa mubashara mara tu baada ya kuachiwa kwa Nabii rehema na amani ziwe juu yake. Na hasa hasa hadithi ya Yaali, Zaidu na Omari Allah awawie radhi wote.

[2] Rejea uk 20 wa kitabu cha matini chanzi.

mwanadamu katika uhitaji wa kulala. Kwa hakika tukio hilo lilikuwa likimtokea akiwa amesimama au amekaa, anatembea au amepanda kipando, asubuhi au jioni, wakati akiongea na maswahaba zake au maadui zake. Na alikuwa akitokewa ghafla na kumwondoka ghafla, na linaisha katika vipindi vidogo[1]. Na si kidogo kidogo kunakotokea kwa mwenye usingizi. Na lilikuwa likiambatana na hizo sauti za ajabu zilizokuwa hazisikiki kutoka kwake wala kwa mwingine wakati wa kulala. Na kwa ujumla yenyewe ilikuwa ni hali kinzani na hali ya mwenye kulala katika maweko yake, nyakati zake, namna yake na jumla ya matukio yake.

- ***Kwa hiyo, hilo ni tukio lisilo la kawaida.***

Kisha tunaona utofauti uliokamilika na wenye kupingana kikamilifu baina yake na baina ya matukio ya mgonjwa wa kupandisha mashetani yanayosababisha nyuso kuwa za umanjano, na maeneo ya nchani yanakuwa ya baridi. Na meno yanakuwa yameumana, tupu zinafunuka, nuru ya akili inazuiliwa, na kiza cha ujinga kinaweka kambi. Kwa sababu tukio la kuteremshiwa Quran lilikuwa, kama ulivyojua, ni kichocheo cha kukua kwa nguvu ya mwili, kung`aa kwa rangi, kupanda kwa joto. Na zaidi ya hayo lilikuwa kichocheo cha nuru na si kiza, chanzo cha elimu na si ujinga, bali lilikuwa likija pamoja na elimu na nuru vitu ambavyo hukumu yake havijulikani na akili ya kibinadamu. Na wakati wa kutokea kwake nuru nyingine zinafifia.

Haya sisi ambao tunakaribia kufika .. Hebu simama na sisi kisimamo kidogo ili tuone kisababishi cha mwanga huu uliokuwa ukidhihiri kwa muda na kufifia kwa muda mwingine, kwa kiasi ambacho hakuna mkono wa Muhammad katika kudhihiri kwake wala katika kufifia kwake: Je, huenda lenyewe limetokana na tabia hii ya nafsi ya Muhammad? .. Kwa hiyo, Wallahi naapa, lingekuwa lafaa zaidi kama lingetoka kwake milele. Lakini lililo la haki zaidi lingetoka katika hali ya kuwa macho ya kawaida na maono ya kifikra kuliko kutokea katika hizo nyakati chache, pale anapofunikwa na haya mawingu mepesi na ambayo huenda yakafanana na kusinzia[2] au kuzimia.

Kwa hiyo, hapana budi nyuma ya mawingu haya kuwe na chanzo cha nuru, kinachoipa nuru nafsi hii ya Muhammad baina ya muda na muda. Na

---

[1] Kama ilivyo katika hadithi zilizopita zinazohusu wasifu wa ufunuo.
[2] Kusinzia: ni kufumba macho kidogo.

kwa hiyo impandishe na kumtoa katika anga la hisia zake zenye mipaka maalumu, na kumwongezea kila kinachotakiwa na Allah miongoni mwa elimu. Kisha ampeleke kwetu akiwa ametubebea shehena hiyo ya elimu hadi pale atakapokutana naye kwa mara nyingine. Kama vile watu walivyoamini kuwa nuru ya mwezi si yenye kutokana na mwezi wenyewe, bali inatokana na mwanga wa jua. Kwa kuwa hao watu wameona tofauti ya nuru yake ni kuwa yenyewe milele ni yenye kufuata tofauti za maeneo yake kutoka katika jua, iwe karibu au mbali.

Na hivyo hivyo, na waamini kuwa nuru ya huu mwezi wa Mtume, imekuwa ikiangaza kwa kuakisi mwanga wa hilo jua ambalo athari zake wanaziona ijapokuwa lenyewe hawalioni. Ndio, kwa hakika wao hawajaliona kwa macho yao likichomoza katikati ya mchana. Wala hawajasikia sauti yake kwa masikio yao, sauti inayofahamika na maneno yanatambulika na watu. Lakini wao walikuwa wanaona athari yake katika paji la uso. Na walikuwa wanasikia michakato yake kandoni mwa uso mtukufu. Na kwa hakika katika hilo kuna uwongofu kwa wenye kuongoka.

- ***Kwa hiyo, hiyo ni nguvu ya nje,*** kwa kuwa yenyewe haiungani na nafsi hii ya Muhammad isipokuwa kwa muda baada ya muda.
- ***Hiyo, hakuna kingine, ila ni nguvu yenye kujua;*** kwa kuwa inamfunulia elimu.
- ***Hiyo ni nguvu ya juu mno kuliko nguvu zake;*** kwa kuwa yenyewe inatoa katika nafsi yake na mwili wake hizo athari kubwa ﴿**Amemfundisha (Malaika) Mwenye nguvu sana. Mwenye uweza** ﴾ 6. –Najm 5 -An .[1]
- ***Hiyo ni nguvu ya heri iliyokingwa na maasi***; kwa kuwa yenyewe haifunui isipokuwa kile cha haki, wala haiamrishi isipokuwa kile cha wema. Hapana shaka yenyewe haiwezi kuwa nguvu ovu yenye shari kama zilivyo nguvu za majini na mashetani. Kwani majini hawana elimu ya vilivofichikana, na kwa hakika ﴿**… majini walitambua kama wangalijua siri wasingalikaa katika adhabu hiyo idhalilishayo** ﴾.[2] Saba 14. Shetani

---

[1] Mwenye uweza: ni mwenye nguvu, na asiili ya neno Almirrat ni kitendo: yaani kufutuka.

[2] Mwanzoni mwa aya hiyo ni ﴿**Na tulipomkidhia mauti (alipokufa), hakuna aliyewajulisha mauti yake ila mdudu wa ardhi, (mchwa) aliyekula fimbo yake. Basi ilipoanguka, majini walitambua kama wangalijua siri wasingalikaa katika adhabu hiyo idhalilishayo** ﴾.

hana kitu juu ya habari za mbinguni, kwani zenyewe zimehifadhiwa dhidi ya kila shetani aliyelaaniwa ﴿**Wala mashetani hawakuteremka nayo (hii Quran kama wanavyodai kusema hao makafiri katika kuitukana). Wala haiwi kwao (kuiteremsha Quran inayovunja hayo mambo yao), na hawawezi. Bila shaka wao wamezuiliwa kusikia (yanayosemwa na Malaika huko mbinguni ﴾.** As-Shuaraa 110 – 112.

Bali tunasema: Je si kweli kuwa **‘‘Roho ni majeshi yaliyoandaliwa kijeshi? Hivyo zile zinazojuana zinaungana. Na zile zisizojuana zainatofautiana’’**.[1] Hivi mtu hajulikani kwa wale wenza wake, na wafananao ndio hukaa pamoja? (Je, si kweli kuwa ndege wafananao huruka pamoja?). Inakuwaje hizo roho chafu ziungane na huo moyo safi uliotakasika? Au inakuwaje, kwa hizo nguvu ovu zinaungana na hii akili iliyokamilika na iliyo madhubuti? ﴿**Je, nikuambieni ambao mashetani wanawateremkia? Wanateremka juu ya kila mzushi mkubwa, mwenye madhambi; (shetani hawawateremkii watu wazuri). Wanawapelekea (hao wanaowafuga) yale wanayoyasikia; (na wakaongeza yao ya uwongo mtupu); na wengi katika wao ni waongo ﴾.** Ash-Shuaraa 221 – 223.

- ***Sasa nguvu hii inaweza kuwa nguvu ya kitu gani kama haitokuwa nguvu ya Malaika Mkarimu?***

Huo ndio upeo wa elimu, katika kuielezea nguvu hii ya siri, kwa vile ambavyo utafiti wa kiakili ulionyooka unavyoongozwa kufikia. Na muumini mwenye kuwa na uwekevu / iktisadi hana haja ya ziada kuliko kiasi hiki katika kuridhisha matamanio yake ya kielimu. Wala katika kuithibitisha

---

Imepokewa na Attwabriy katika tafsiri yake 22 / 76 kutoka kwa Atwaa amesema: Suleiman bin Daudi alikuwa anaswali, akafa huku akiwa amesimama katika swala, na majini walikuwa wanafanyakazi na hawakujua umauti wake. Mpaka pale mchwa alipokula [na kutoboa ule mti] fimbo yake. naye akaanguka. Na akasema katika 22 / 74: Mtukufu aliyetukuka anasema: pale Suleimani alipoporomoka na kuanguka kwa sababu ya kuvunjika kwa fimbo yake aliyokuwa akiegemea [yaani fimbo yake aliyokuwa akiegemea katika swala yake] ilibainika kwa majini ya kuwa, kama wangalikuwa wanajua mambo yaliyofichikana na wanayojidai kuwa wanayajua, basi wasingalikaa katika adhabu hiyo idhalilishayo na kufedhehesha, kwa mwaka mzima, baada ya kufa kwa Suleiman na huku wao wakidhania kuwa Suleiman yu hai. أ هـ .

Na ibnu Kathiri amesema katika tafsiri yake 6 / 489 maneno kama haya. Na vile vile wafasiri wote. Tazama tafsiri ya Adduru Almanthuuru ya Assuyuutwiyyu 5 / 431, 432, 433.

[1] Hili ni andiko la hadithi iliyopokewa na Bukhari na Muslimu: Bukhari ameipokea katika hadithi za Manabii 3336 kutoka kwa Aisha. Na Muslimu ameipokea katika Albiri Wasswilati Wal-Aadaabi 105, 160 kutoka kwa Abuu Hurayrah.

itikadi yake ya kidini. Basi atakayetaka ziada ya maelezo yake na sifa zake basi huyo, njia yake si kurejea katika ushahidi wa kiakili. Bali njia yake ni kurejea katika nukuu sahihi kutoka katika uteremko wa siri zake na muonekano wa nuru yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali wake. Yeye peke yake ndiye ambaye amemwona huyo muhusika na kuisikia sauti yake. Pia hizo ndizo simulizi za mwanafunzi aliyekaa kwa mwalimu wake si mara moja.

Ama yule anayeamini yaliyofichikana, basi huyo ataamini habari hizi kutoka kwake hata kama hajamwona. Kwa kuwa yeye ameona athari zake. Na kwa kuwa yeye anamwamini yule aliyempa habari. Ama wajinga, wale ambao wamepewa kiasi kidogo mno cha elimu dhahiri juu ya uhai, basi wanadhani kuwa wao wanajua kila kitu kwa undani na kwamba wao watakikadhibisha kila kile wasichokijua.

Na watakwambia: huenda hayo ni mivurugiko wa mishipa ya macho, iliyokuwa ikimuonesha kuwa anaona kitu kusikokuwa na kitu! Na wewe jikinge kwa Allah dhidi ya upofu wa nyoyo na macho, na sema: Sivyo hivyo! ﴿**Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka (uliowekewa** ﴾**.** An-Najm 17. Au wanasema: huenda ni mivurugiko katika nguvu za kufikiri iliyompatia picha ya maana ya vivuli vinavyofanana. Na ndoto za kweli zilizojitengeneza kiwiliwili! Jitakase kwa Allah dhidi ya uwendawazimu huo, na sema: Sivyo hivyo! ﴿**Moyo haukusema uwongo uliyoyaona. (Moyo wake ulisadikisha haya yaliyotokea** ﴾**.** An-Najm 11.

Ndio, kwa hakika wameshangazwa na juu ya kuwa mwanadamu anawaona Malaika kwa dhati yao kuongea nao kwa sauti. Bali wameshangazwa kuwepo katika dunia hii viumbe wasiowaona kwa macho yao. Na kuwepo kwa sauti wasiyoisikia kwa masikio yao. Basi wakasema, iweje Muhammad aone yale tusiyoyaona, na asikie yale tusioyasikia!

### [**Kujiliwaza Na Kile Kilichovumbuliwa Na Sayansi Ya Zama Za Sasa**]

Naapa, kwa hakika sisi tuna haki zaidi ya kushangazwa na maajabu haya. Kwa hakika sisi tunafahamu kuwa mambo hayo kama yangekuwa yanakubalika katika zama za kale za ujinga, basi yasingekuwa yanakubalika leo hii, huku ardhi ikiwa imejaa ushahidi wa kisayansi zinazotufasiria akili zetu, hayo maelezo ya kweli yaliyofichikana.

Kwa hakika ushahidi uliokaribu zaidi na matumizi ya watu wengi katika ushahidi huo ni ushahidi wa simu (Telephone). Watu wawili, ambao

mmoja wao anakuwa yupo mashariki ya mbali na mwingine yupo magharibi ya mbali wamekuwa wanaweza kuzungumza na kuonana. Kiasi ambacho wale waliokaa katika makazi hayo wanayozungumza hao wawili hawaoni kitu. Wala hawasikii ila miungurumo kama mvumo wa nyuki ambayo ilikuwa katika wasifu wa ufunuo.

Kama walikuwa wakitaka ushahidi wa kisayansi ulio wazi zaidi kuliko huu, na ambao unawakilisha kwao wao, tukio la ufunuo kwa uwakilishi mzuri, na kuwaonesha kwa njia ya majaribio – njia ambayo hawaamini nyingine ila hiyo tu – ya kuwa kuwasiliana kwa nafsi ya mwanadamu na nguvu za juu kuliko yeye huenda kukatoa tukio lililo kama tukio hilo, na kisha kuchonga katika hiyo nafsi maarifa ambayo hayakuwa yamehifadhiwa katika akili wala katika hisia hapo kabla.

Basi ushahidi huo ndio huu hapa Allah amewaonesha, ukiwa ni ushahidi wa ajabu kabisa katika (Ajabu ya kulalishwa kisumaku) kwa hakika, kwa sasa mtu mwenye nguvu ya kutaka amekuwa anaweza kutiishwa na nguvu ya kutaka kwake yule aliye mdhaifu zaidi kuliko yeye, mpaka anamfanya yeye alale usingizi mzito kwa amri zake, na wala hahisi katika usingizi huo hata akichomwa na sindano. Na kwa hapo anakuwa mateka wa ishara za huyo mwingine.

Na matakwa yake yanafutika kwa matakwa ya yule mwingine: Kama atataka kufuta katika nafsi yake maoni au itikadi, angeifuta kwa neno moja. Bali lau kama atataka kufuta kilichomo kifuani kwake hata jina lake angelifuta[1] na kumtamkisha jina lingine na kumkinaisha kuwa hilo ndilo jina lake, na kusingepatikana kwake ila kuamini na kukubali. Na jina lake halisi ligekuwa limesahaulika kabisa kabisa. Na hilo jina la kutengezwa ndilo lingebakia limeandikwa katika moyo wake na ulimi wake baada ya kuamka kwake hadi pale Allah atakapotaka. Na kama ikiwa hili ni tendo la mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake, unadhani nini kwa yule ambaye yeye ni mkuu zaidi kuliko nguvu za mwanadamu?

Na hilo ni kama mfano wa[2] mbeba ufunuo na mwenye kuupokea, amani iwe juu yao. Huyu ni mwanadamu, mtiifu na mwenye roho safi inayokubali

---

[1] Matukio ya kulazwa kisumaku na athari zake kimwili na kiroho yapo mengi kuliko vile yanavyoweza kudhibitiwa hesabu zake. Lakini sisi tumeashiria mfano huu juu ya tukio lililokuwa likishuhudiwa mubashara na wanazuoni wa Azhar (Profesa Muhammad Abdul Adhiimu Azzurqaaniy) naye ndiye ambaye aliyeerevuka na tukio hilo na kung`amua juu ya haya mazingatio ya kidini na kusambaza habari hizo katika jarida la Alhidaya Al-Islaamiya katika mwezi wa Mfunguo sita wa mwaka huu wa (1352 H) [Daraazu].

[2] Tafakari vizuri ukaribiano huu, utakuta ndani yake kuna ushahidi mwingine unaobatilisha madai ya kuwa (ufunuo ni habari za kinafsia). Madai yanayopigiwa debe

kuwekwa elimu ndani yake. na huyo ni Malaika mwenye nguvu kubwa na mwenye uweza, huyu Malaika anampelekea ujumbe wake na kumsomea. Na hasahau ila kile alichotaka Allah.

Licha ya kwamba kuna umbali mkubwa baina ya ufunuo wa Mtume na ufunuo wa watu baadhi yao kwa wao. Kwani watu, kama ulivyojua, huenda wakafunuliana maneno ya kudanganyana. Na mara nyingi wanaachia ufunuo wao katika nafsi inayobadilika hali zake za kiakili au kimwili zilizo ngumu kuzitibu. Sasa hili ni wapi na wapi na ufunuo ulio baina ya wajumbe wawili wanaotiwa nguvu kwa kuchaguliwa na Allah kupeleka ujumbe wake: Mjumbe wa Kimalaika, na mjumbe wa kibinadamu? Ama mjumbe wa kimalaika kwa hakika yeye kama ulivyojua, hafunui isipokuwa ya haki. Wala haamrishi ila la heri.

Ama mjumbe wa kibinadamu kwa hakika yeye ataendelea kuwa kama aliyokuwa hapo kabla. Ni mwenye uthabiti wa kifua, mkamilifu wa akili, mwenye nafsi na mwili wenye nguvu. ﴿**Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye mahala anapoweka ujumbe wake** ﴾ Al-An-Am 124.

* * *

---

na wapingaji. Kwani mambo yalivyo, ni katika nguzo za msingi zilizokubaliwa na wataalamu wa kulaza kisumaku, kuwa, kwa hakika suala hilo linakuwa baina ya nafsia mbili zilizotofautiana kitabia. Moja wapo ina nguvu ya utashi kubwa zaidi kuliko nyingine. Kwa hiyo mwanadamu hawezi kuendesha jaribio hili kwa nafsi yake mwenyewe, ila kama tukichukulia kuwa kuna kuungana kwa vinyume viwili, au moja iwe mbili. [Daraazu].

## [**HATUA YA NNE YA UTAFITI HUU**: **Kutafiti Kuhusu Kiini Cha Quran Yenyewe Na Uhakika Wa Chanzo Chake**]

Ama baada ya hayo, kwa hakika sisi katika njia hii tunayoipita, kuanzia mwanzo wa utafiti huu mpaka hapa tulipo, hatujapata kuiwasilisha Quran katika kiini chake. Bali upeo wa yale tuliyoyafanya ni sisi kuisoma njia iliyokujia hiyo Quran: na hatukupata, tena kwa kukiri kwa mwenye Quran, wala katika maisha yake ya kitabia, wala katika njia zake na miunganiko yake ya kielimu, wala katika mazingira mengine ya kiujumla au ya kiupekee na ambayo katika hayo Quran ilidhihiri, hatukupata ila ushahidi unaoongea kuwa; ardhini, Quran hii haina baba wa kujinasibisha naye kinyume na Allah.

Yote hayo ni tafiti za nje. Kwa hakika anazifanya mtu aliyesimama na sisi kwa upande wa wema katika haya maisha ya Mtume na yanayohusiana nayo. Na mtu huyo, pamoja na hayo, amekuwa ni mwenye kusalimika na maumbile yake, anafahamu vitu kwa kutumia vilivyo mfano wake. Na anaongoka kuvielekea hivyo vitu kwa alama zake za karibu. mtu kama huyu, ataturidhia walau kwa kiasi hiki na kuongoka nacho.

Na ama wale ambao hawayajui maisha hayo ya Mtume ila kidogo tu – na hao ndio wengi – na wale ambao wanataka kuchukua hoja za Quran kwa kutumia Quran yenyewe. Basi kwa hawa, hatuwezi kutosheka na kuwapuuza, bali tutawapigia hatua nyingine, na katika hatua hiyo tutawabainishia kuwa Kitabu hiki Kitukufu kwa tabia yake kinakataa kuwa kimetengenezwa na mwanadamu. Na kinatangaza kwa ulimi wa hali yake ya kuwa chenyewe ni ujumbe wa hukumu na makadirio ya Allah. Hata kama kitapatikana kimetupwa jangwani, basi atakayekitazama vizuri atayakinisha kuwa katika ardhi hii hakuna chanzo chake wala maoteo yake. Na kwa hakika, chenyewe kilikuwa kimetokana, kuchomoza na kuteremshwa na upeo wa mbinguni.

### [**Mipaka Ya Uwezo Wa Kibinadamu Na Mpaka Wa Kimuujiza**]

Hayo, ni kwa kuwa uwezo wa watu, hata kama watatofautiana, unaishia katika mipaka maalum na hauwezi kuvuka hapo. Na uwezo wa muumba kwa vitu vinavyowezekana hauna mipaka. Kila kiumbe anayevuka mipaka ya uwezo wa kibinadamu kwa hakika kiumbe huyo, moja kwa moja atakuwa katika uweza wa Mungu, na hakuna la tatu.

Mfano wake: Mtu anaweza kumpiga mtu mmoja, au wawili, au watatu au makumi. Lakini, je, kuna mtu miongoni mwa watu anayeweza kusimama na kukabiliana na dunia nzima na kuyashinda mataifa, moja moja au kwa pamoja?

Na Allah analileta jua kutokea mashariki, basi ni nani huyo atakayeweza kulileta kutokea magharibi?

Na wewe unaweza kuzima taa na kuiwasha pale utakapo. Lakini watu wote hawatoweza kulitoa jua kabla ya wakati wake. Au kulichelewesha kutoka nje ya muda wake. Au kuizima nuru yake. Au kuleta mfano wake hata kama watasaidiana wao kwa wao?

Kwa hakika wao hawatoweza kuumba inzi hata kama watakusanyika wote. Na kama inzi atawapora kitu, basi hawawezi kukikomboa kutoka kwake. Sasa wapi na wapi kwao wao wajilinganishe na hivyo viumbe vya juu na ambavyo mikono yao wala makombora yao hayawapati. Na mambo ambayo wao hawayamiliki kwayo ila kuyatazama, kuyashangaa, kufaidika nayo na kuyanyenyekea tu.

Na huko ndiko kushindwa kikamilifu katika kujilinganisha nayo na kujifananisha kuumba. Huo ni ushahidi wa kuwa hayo si katika ufundi wa kibinadamu. Na hiyo ndio tabia ya kiuungu na mandhari ya kimbinguni. Mandhari ambayo kwayo, ufundi wa Muumba unajipambanua katika uumbaji wa viumbe. Na huu ndio mfano ambao tunataka kuutekeleza katika Quran Tukufu.

Isipokuwa wapo miongoni mwa watu waliozama katika tope zito[1] la ubishi, wanaosema: ﴿**Na wakasema (kumwambia Musa): ''Ishara yo yote utakayotuletea ili uturoge kwayo (hutafanikiwa, kwani) hatukuamini** ﴾. Al-Aaraf 132. ﴿**Na lau kama tungewateremshia Malaika (kuwashuhudilia Ujumbe wa Nabii Muhammad kama wanavyotaka), na wafu wakazungumza nao (kuwa haya ni kweli), na tukawakusanyia kia kitu mbele yao (kikawaambia haya pia), wasingaliamini isipokuwa atake Mwenyezi Mungu**Am 111. -An-. Al[2] ﴾

---

[1] Tope zito: ni udongo mweusi wa mfinyanzi madhubuti.

[2] Al-Imaan Ibnu Aljawziy amesema katika Zaadi Almasiiri 3 / 106:

Sababu ya kuteremka aya hii ni kuwa wafanyastihizai walimwendea Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akiwa na kikundi cha watu wa Makka, wakamwambia: tufufulie baadhi ya maiti zetu ili tuwaulize: je, ni kweli kile unachokisema au ni batili? Au tuoneshe malaika wanaokushuhudia kuwa wewe ni Mtume wa Allah? Au tuletee huyo Allah na Malaika mbele yao. Ndipo ikateremka aya hii. Imepokewa na Abuu Swalihi kutoka kwa Ibnu Abbas. Na maana ya aya hii ni: lau sisi tungeteremsha kwa wao Malaika kama walivyotaka, na maiti zingeongea nao na kutoa

Na wenginewe hawapati utulivu wao ila katika mitikisiko ya shaka, na husema: ﴿**Hatudhani ila dhana tupu wala hatuna yakini''** ﴾**.** Al-Jathiyah 32. ﴿**Na lau tungaliwafungulia (hao makafiri) mlango wa mbingu, na wakawa wanapanda (na kushuka kama walivyotaka, ili uwe ndio muujiza wa Mtume). Basi wangalisema: ''Macho yetu yamerogwa tu, bali sisi (nafsi zetu) ni watu tuliorogwa (tunaona kinyume cha mambo''** ﴾ **.** Al-Hijr 14 – 15. ﴿**Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi (kama walivyotaka) na wakayagusa (maandishi hayo) kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangalisema: ''Haya si cho chote ila ni uchawi dhahiri (kiini macho tu hiki; si maandishi''** ﴾**.** Al-An-Am 7.

Kwa hawa na hao, kwa kweli sisi hatuna namna juu yao, wala hazitowasidia nasaha zetu, ikiwa Allah ameshawaacha kupotea. Kwani si katika mambo yetu kuwasikilizisha viziwi au kuwaonesha njia vipofu wala wale wanaoweka vidole vyao masikioni mwao, kwani wao hawatosikia. Au wanaweka viganja vyao machoni mwao. Basi jua kama limechomoza kwao linakuwa halijachomoza ﴿**Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumtia mtihanini[1], huwezi kumpatia mbele ya Mwenyezi Mungu cho chote** ﴾**.** Al-Maidah 41. Hakika si vinginevyo, njia yetu ni kusimamisha hoja juu ya wale wasiyoijua miongoni mwa wale wanaotafuta ukweli. Na kuiweka wazi njia kwa watakaoipita miongoni mwa wapendao vitu vya yakini.

Haya sisi hapa tunamwita kila mwenye kutafuta haki kwa uadilifu. Tunamwita atazame kwa uchunguzi pamoja nasi katika Quran, tena kwa upande wowote aupendao: Kwa upande wa muundo na mtindo wake. Au kwa upande wa elimu yake. Au kwa upande wa athari zake ilizozitoa duniani na kubadilisha uso wa historia. Au kwa ule upande wa kijamii – kwa sharti, awe na uzoefu baada ya hapo wa kuitazama katika mipaka ya mazingira na zama zake zilizodhihiri. Au achukulie kuwa chenyewe kimedhihiri katikati ya zama zilizoendelea sana kihistoria.

Pia ni sawa sawa juu yetu, kutazama utu wa mlinganiaji ambaye amekuja na Quran au atafute mtu asiye na kitu na ambaye kwake yeye mambo ya kifasihi yamejikusanya. Na utawala wa watawala wakuu. Na tafiti

---

ushahidi wa Utume wako. Na tungewakusanyia kila kitu duniani kiwe mbele yao. Wasingekuwa watu wa kuamini ila Allah akipenda. Kwa hiyo akaelezea kuwa tukio la kuwa na Imani linaendana na matakwa yake na sio kama wanavyodhania. Ya kuwa wao muda wowote wakitaka wanaamini. Na muda wowote wasipotaka basi hawaamini. أ هـ.

[1] Attwabry amesema katika tafsiri yake 6 / 238:

Maana ya kumtia mtihani kwa hapa ni: kupotea na kuiacha njia.

za wasomi wa elimu zote za kibinadamu – kisha tumuulize: je, anakuta ndani ya Quran kingine zaidi ya nguvu isiyo ya kawaida inayomshinda kila mwenye kushindana nayo. Na zinadondoka chini yake kila nguvu za mjuzi, na kila kiongozi mkuu. Na kila mshairi na mwandishi. Kisha vizazi hata vizazi, miongo na miongo vinaisha, na wala yale yaliyomo ndani yake miongoni mwa maajabu hayaishi. Bali huenda dunia yote ikatoweka, hali ya kuwa watu bado hawajajua tafsiri ya kila kilichomo ndani yake. ﴿**Siku yatakapotokea matokeo[1] yake hayo watasema wale waliopuuza hapo zamani: ''Kweli Mitume wa Mola wetu walileta haki''** ﴾**.** Al-Aaraf 53.

### [Pande Tatu Za Miujiza]

Kwa sasa – kwa msaada wa Allah na kuwafikishwa kwake – na tuanze kutafiti pande tatu miongoni mwa miujiza ya Quran. Namaanisha:

- Upande wa muujiza wa kilugha.
- Na upande wa muujiza wa kisayansi.
- Na upande wa muujiza wa kuitengeneza na kuirekebisha jamii.

Na mazingatio yetu yawe mengi katika upande wa kilugha, kwa kuwa wenyewe ndio upande ambao, kwa upande wake kumetukia tukio la kutolewa changamoto na Quran kiujumla na kwa maelezo ya kina katika sura iliyopo katika Quran. Na kwa ajili hiyo tunaanza nao.

⁕ ⁕ ⁕

[1] Matokeo yake: uhakika wake na maelezo yake. na siku ambayo matokeo yake yatakuja: hiyo ni siku ya Kiama.

## QURAN NI MUUJIZA KILUGHA

### [Kuzipitia Kauli Tata Zote Zinazoweza Kuonekana Kuwa Hivyo, Zile Zinazohusiana Na Suala Hili, Kwa Ajili Ya Kujiandaa Kuzifutilia Mbali Moja Moja]

Mwenye kitu cha shaka kinachohusiana na suala hili, basi na aturuhusu tumuombe atuweke wazi ni shaka ipi hiyo?

(1) Je, nafsi yake inamuongelesha kuwa yeye anaweza kuleta maneno yaliyo daraja ya umbuji ya Quran?
(2) Au yeye alijua mwenyewe kuwa na upungufu ulio chini ya daraja hiyo, lakini hakujua kuhusu watu juu ya kile alichokijua mwenyewe?
(3) Au alijua kuwa watu wote wamenyamaza hawaipingi Quran, lakini yeye hakujua kuwa kunyamaza kwao katika hilo ilikuwa ni muujiza. Na si kuwa kushindwa kwao kumekuja kutoka upande wa Quran yenyewe?
(4) Au alijua kuwa wao wameshaishindwa Quran, na kuwa yenyewe ndio ambayo imewashinda wao. Lakini yeye hakujua kuwa muundo na mtindo wake ulikuwa ndio miongoni mwa sababu ya muujiza wake?
(5) Au yeye ana yakini kuwa Quran Tukufu ilikuwa na inaendelea kuwa muujiza wa mbinu za ufikishaji kwa watu wengine wote. Lakini yeye hana yakini ya kuwa Quran ilikuwa muujiza pia kwa yule aliyeileta?
(6) Au yeye anaamini haya yote; lakini yeye hajui: siri zake ni zipi na sababu zake ni zipi?

Hizi ni namna sita. Kila namna katika hizi ina ushughulikiaji unaouhusu. Na tutazishughulikia kwa mpangilio huu.

### [**Utata Wa Kwanza: Chipukizi Mmoja Adanganyike Na Kujidai Kuwa Anaweza Kuleta Maneno Yaliyosawa Na Quran**]

1- Ama ikiwa kile kilichochochea utata kwa chipukizi huyo ni kuwa yeye amepitia kitu fulani katika ufundi wa mashairi au nathari. Na nafsi yake imezoea kuwa na uwezo mkubwa wa bayani[1]. Kwa hiyo shetani akamtia wasiwasi na kujiona kuwa yeye yu mbora sana na kule kutoijua kwake Quran, akajiona anaweza kuleta maneno kama Quran kwa muundo na mtindo wake. Dhana kama hiyo, huwa haidhaniwi na wataalamu wakubwa

[1] Bayani ni: kuwasilisha maana moja kwa njia tofauti tofauti za kilugha zenye vionjo mbali mbali, kama kuleta tashbiha, sitiari, methali, mbinu, nahau, tanakali sauti nk.

wa Bayani. Kwani dhana hiyo – kama itatokea – basi hutokea kwa chipukizi waliodanganyika. Na utata kama huu dawa yake kwetu sisi ni kumpa nasaha kuwa anapaswa atazame sana katika miundo na mitindo ya warabu. Na ajikaririshe kile alichofahamu katika hayo, kwa kujifunza elimu ya fasihi ya Kiarabu. Hadi awe na uwezo mkubwa na kuhakiki Kibayani. Na iwe wazi kwake yeye njia ya kuhukumu katika viwango vya maneno na matabaka yake. Kisha baada ya hapo ndipo aitazame Quran.

Na mimi kwake yeye ni kiongozi, kwa kila hatua atakayoichukua katika njia hii. Basi hatua hiyo itamzidishia maarifa ya uwezo wake. Na itakuwa kikwazo kwake miongoni mwa vikwazo vya shaka kinachomzuia kulitekeleza jambo lake. Kwani huko ataona kuwa, kila anapozidi kuwa na utambuzi juu ya siri za kilugha, na kuwa mzuri katika kuchambua kauli, na kumiliki kwake kiini cha Bayani, basi kwa kiasi hicho hicho atazidi kuitafuna nafsi yake na kuzipinga nguvu zake. Na atanyenyekea kikamilifu mbele ya muundo na mtindo wa Quran. Hili kwako wewe linaweza kuonekana ni la kushangaza, eti mtu azidi kuhisi kuwa anashindwa kuitengeneza. Kwa kadri nguvu zake zinavyokamilika katika ujuzi huo, na elimu yake kadiri inavyoendelea kupanuka.

Lakini hakuna la ajabu. Huo ndio mwendo wa Allah katika aya zake anazozitengeneza kwa mikono yake miwili: Kuujua mwendo huo na kutambua siri zake hakukuzidishii ila kunyenyekea ukubwa wake na kuamini kuzishindwa. Lakini ufundi wa viumbe hauko kama hivyo. Kwani ujuzi wa kujua ufundi wake unakuwezesha na kukufungulia njia ya kutengeneza kama hivyo na bora zaidi ya hivyo. Na kwa hapa, wachawi wa Firauni, wao ndio waliokuwa wa mwanzo kumwamini Mola wa Musa na Haruna.

Na kama huyo aliyedanganyika atakataa na kung`ang`ania kujidanganya kwake, na anaona kitu kikubwa sana kwake kukubali kushindwa na kuwa na upungufu. Tunamuita uwanjani ili yeye mwenyewe ajaribu nguvu zake. Na tunamwambia: hebu tutolee kile kilichobora zaidi kwako wewe ili tuone, unasema kweli au umekuwa miongoni mwa waongo… Isipokuwa sisi tutampa mawaidha ya jambo moja lingine: Asije akaitoa bidhaa yake kwa watu hadi pale atakapojiridhisha kuwa ameitengeneza kwa utulivu na kwa muda wa kutosha na kudhibiti mizania zake. Na pia ahakikishe kuwa ameifanya vizuri haina makosa. Kwa hakika yeye kama atafanya hivyo,

atakuwa amekaribia kutambua kosa lake na kuficha mwili. Na kama si hivyo, huyu maskini ameshaiharibu nafsi yake, pale alipotaka kulifanya vizuri.

Kwa hakika katika historia kuna mazingatio yanayowaathiri watu waliojaribu jambo kama hili: Wakaleta upinzani dhidi ya Quran kwa maneno yasiyofanana na Quran na wala hayafanani na maneno ya nafsi zao. Bali waliyashusha hadi daraja la upuuzi na kuchekesha na kuonesha utupu wake. Aibu yake na ubaya wake imesalia: miongoni mwao wapo wenye akili wameona haya kutimiza jaribio lao. Wakavunja kalamu zao na kuchana kurasa zao.[1] Na yupo miongoni mwao mfanya vitimbi na akawakuta watu wa zama zake wana akili sana na haiwezekani kuupigia debe upuuzi wake. Basi akakunja kurasa zake na kuzificha hadi muda fulani[2]. Na miongoni mwao wapo wafanya upuuzi, mmoja wapo alijidhihirisha kwa watu. Akawa ni dharau kwa wanaodharau, na mfano kwa wengine[3].

---

[1] Baadhi ya hayo yanaegemezwa kwa ibnu Almuqufau. Abuu Attwayyibu na Almaarriy. Na dhana kwa watu hawa ilikuwa kwamba wao kwa akili zao na vionjo vyao hawakuwa na haja ya kujiingiza katika jaribio hili. Ila kama itakuwa katika ile ya ﴿**Ili moyo wangu utulie** ﴾. AL-Baqarah 260. [Daraazu].

[2]Miongoni mwa hayo ni yale yaliyokuwa mashuhuri katika vile vitabu vilivyowekwa na viongozi wa mapote ya (Kikadiyani) na (Kibahaaiya) ili viwe katiba yao ya kidini kama ilivyo Quran. Kwa hakika ndani yake walipachika mpachiko dhaifu wa aya za Quran na maneno ya mtaani. Na ndani yake walibadilisha misingi ya Uislamu na matawi yake. Na ndani yake walijidai kuwa wao wenyewe ndio mitume au miungu. Na lakini wafuasi wao hawakuwa na ujasiri wa kuvisambaza vitabu hivyo huku jua la elimu likiwa linaangaza. Kwa hiyo wakavificha – kama paka anavyoficha kucha zake – hadi pale utakapokuja wakati ambao ujinga wa kutojua elimu na fasihi utakapoenea. Na nyoyo zitakuwa tayari kukubali mfano wa vitabu hivyo. Basi na wangoje katika zama za mwisho. [Daraazu].

[3] Na katika hao , mfano ni Musailama Muongo. Alidai kuwa yeye anafunuliwa maneno kama ya Quran. Na hakutengeneza kitu zaidi ya kuwa yeye anazikusudia aya miongoni mwa aya za Quran na kuiba maneno yake mengi na kuyabadilisha baadhi yake. Kama katika kauli yake: (Kwa hakika sisi tumekupa wewe jamhuri. Basi swali kwa Mola wako na udhihiri ﴾. Au kwa kupitia mizani ya maneno ya Quran anakuja na maneno na maana ya masokoni, kama katika kauli yake: (Na watwangaji kwa kutwanga. Na wakandaji kwa kukanda. Na waokoji kwa kuoka). Na hivyo hivyo, hakuweza kuulinda muundo na mtindo wake mwenyewe na hali yakuwa yeye ni Mwarabu halisi. Bali alishuka hadi kufikia upeo wa kusikitisha na akaleta upuuzi ambao huwa unaletwa na watoto katika michezo yao na kuichambua kwao kwa kugeuza mashairi na nyimbo kutoka katika sura yake asilia. Na haijifichi kuwa haya yote si chochote katika kuipinga Quran.

Bali yenyewe ni kuiiga na kuifisidi. Na hakuna mfano wake ila kama mfano wa yule anayebadilisha mtu kwa kuweka sanamu lisilo na roho. Na huku yeye katika sanamu hilo halina chochote cha uzuri wa kifani. Kwa hakika upinzani ni kutegemea maana miongoni mwa maana na kuyaeleza yeye mwenyewe kwa muundo na mtindo wake mwingine uliosanjari na ule wa asili kiumbuji au aupite uwe zaidi yake. Na atakayejaribu hilo katika maana za Quran, kwa hakika anajaribu jambo la muhali (lisilowezekana). Na

Basi yule ambaye nafsi yake inamuongelesha arudie kufanya jaribio hili kwa mara nyingine, basi na atazame uzuri katika mazingatio hayo na achukue yale mazuri. Na yule ambaye hajaona haya, basi na afanye atakalo.

[**Utata Wa Pili: Mwanafasihi Mnyenyekevu Anafahamu Vibaya Kuwa Uwezo Huu Upo Kwa Mwingine Miongoni Mwa Mafahali**]

2- Ama ikiwa lango la utata, kwake yeye, ni kuwa ameshaona kwa watu wengine, wana uwezo mkubwa kuipita Quran katika ufundi huu. Hivyo anajisemea nafsini mwake: (hata kama mimi sitokuwa miongoni mwa mashujaa wa uwanja huu. Na mimi sina mikono (uwezo) ya kushindana na Quran. Na huenda suala hili likawa lepesi kwa yule mwenye ulimi fasaha zaidi yangu na mwenye uchawi mkubwa wa kibayani). Basi kwa mtu wa

---

uzoefu ni shahidi mkweli sana. Bali anayejaribu kuleta mfano wa muundo na mtindo wa Quran kwa maana nyingine, huku akiwa hajipambi na ukweli na hekima katika hilo, basi mtu huyo kwa hakika amekuwa na tamaa ya kisichotakiwa kuwa na tamaa nacho. Na kwa ajili hiyo, miongoni mwa njia za kuwapa changamoto Warabu ni kutakiwa ﴿**Basi leteni sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii** ﴾ Hud 13.

Hili tunalolifahamu katika suala la Musaylama ndilo alilolifahamu mwanafasihi Arraafiiyyu: kwa hakika haijapokewa kuwa yeye aliipinga Quran kwa upande wa ufundi wa Kibayani. Kwani upande huo ulikuwa u wazi zaidi na suala lake halina shaka kwake yeye. Au aweze kumchanganya yeyote miongoni mwa warabu katika upande huo. Kwa hakika alitaka kuchukua njia yake ya kuipumbaza kaumu yake kwa upande wa mwingine huku akidhani kuwa upande huo ni dhaifu kwake na upo karibu zaidi katika kuziathiri nafsi zao. Hilo ni kwa kuwa yeye aliwaona warabu wanayaadhimisha na kuyatukuza maneno ya makuhani wa kijahiliya. Kwa ujumla mitindo na miundo ya makuhani ilikuwa miongoni mwake ni vina (sauti sawa mwishoni) vyenye kuchukiza na ambavyo wanadai kuwa vyenyewe vinatokana na maneno ya majini. Kama kauli yao: ‘‘Yaa Jaliihu. Amru Najiihu. Rajulun Fasiihu. Yaqulu laa ilaaha Illa Allahu’’ tafsir isiyo rasmi ya maneno haya inasema: ‘’Ewe mwenye kipara. Jambo la mafanikio. Mtu fasaha. Anasema hakuna Mola ila Allahu’’. Imepokewa na Bukhari katika sifa za kusilimu Omari. Na hivyo hivyo akajaalia kutumia vina hivyo katika kuiiga Quran ili kuwafahamisha vibaya kuwa yeye anapewa ufunuo kama anavyofunuliwa Muhammad.

Kana kwamba utume na ukuhani ni kitu kimoja. Lakini vile vile hakufaulu katika hila hii. Kwa hakika wengi katika wafuasi wake wanamjua ni muongo na mpumbavu. Na wanasema kuwa yeye katika kuyaendea kwake hayo, hakuwa kuhani mahiri wala katika madai yake ya utume hakuwa mkweli. Na kwa hakika wafuasi wake kwake yeye walikuwa kama vile alivyosema msemaji wao: (Muongo wa Kirabia anapendwa zaidi kwetu kuliko mkweli wa Kimudhwari). [Daraazu].

- Nimesema: hiyo hadithi ya vina iliyotajwa, imepokewa na Bukhari katika Sifa za Maanswari 3866. Ama yule aliyesema (Muongo wa Kirabia …) yeye ni Twalha Annimiriy pale alipoenda kwa Musaylama Mwongo na kumsikia, kisha akasema: (nashuhudia kuwa wewe ni mwongo. Na kuwa Muhammad ni mkweli. Lakini (Muongo wa Kirabia anapendwa zaidi kwetu kuliko mkweli wa Kimudhwari). Historia ya Attwabary 3 / 286.

mfano wa huyo tunamwambia: rejea kwa wenye ujuzi miongoni mwa wanafasihi wa zama zako na uwaulize, je wanaweza kuleta kilicho mfano wake? Na kama wakikwambia (Lau tungalitaka tungalisema maneno kama hayo). Basi waambie (Leteni hoja zenu!) Na kama wakisema (hatuna nguvu ya kufanya hilo). Basi waambie: Ni kitu gani kikubwa zaidi kuliko kushindwa kushuhudia kushindwa?

Kisha rejea katika historia na uiulize: watu wa mwanzo wana nini? Yenyewe itakueleza kuwa hakuna hata mtu mmoja aliyenyanyua kichwa chake mbele ya Quran katika zama yoyote katika zama zake. Na kwa hakika baadhi ya watu wachache wasiozidi kumi ambao walizamisha vichwa vyao katika suala hilo walirejea na fedheha na udhalili. Na ulimwengu uliondoa athari zao na kuzivutia katika mkia wa sahau.

Naam, historia imesajili huko kushindwa kwa watu wenye lugha yao katika zama za kuteremka Quran. Na ni kipi kitanakujulisha ni zipi hizo zama za kushuka Quran? Hiyo ndio zama ambayo Bayani ya Kiarabu ilistawi zaidi, na nafasi za umahiri wa lugha ulifikia upeo wa juu mno. Je, taasisi za lugha katika jamii yoyote miongoni mwa jamii dunia zimewahi kufikia kile kilichofikiwa na taasisi za Kiarabu katika zama hizo miongoni mwa kuithamini na kuifuatilia lugha yake. Hadi lugha ya Kiarabu ikafikia kilele chake, na kwao wao kwa kiasi cha nguvu ya kibinadamu ikatimia kuyaweka sawa maneno yake, miundo na mitindo yake? … Ee ajabu ilioje kwa haya makundi yaliyokusanyika jangwani. Na ajabu gani kwa haya majukwaa yaliyonyanyuliwa huku na huko? .. Kwa hakika yenyewe ni masoko ya Warabu na ambayo ndani yake kunawasilishwa bidhaa zao za thamani kubwa pamoja na bidhaa zao bora walizozitengeneza. na bidhaa hizo si nyingine ila ni ufundi wa maneno na ufundi wa mashairi na hotuba. Wanashindana kuwasilisha na kuzihakiki. Na kisha kuchagua bora yao na kujifaharisha nayo. Wanachuana vikali katika hilo. Na katika hilo wapo sawa wanaume na wanawake wao. Na suala la Hassaani na Khansaa na wasiokuwa wao kuwa si lenye kufichikana kwa mwanafasihi yeyote wa Kiarabu.

Na punde si punde tu ilipokuja Quran … kutahamaki masoko yameishiwa bidhaa ila bidhaa yake. na kutahamaki klabu zimepauka... ila kwake yeye. Hakuna yeyote aliyeweza kushindana naye wala kukimbizana naye, au aliyependekeza kuwa katika Quran kubadilishwe angalau neno moja kwa lingine, au kufutwa neno, au kuongezwa neno, au kulitanguliza moja na kulichelewesha lingine. Yote hayo ni kwa kuwa yenyewe

haijawazuia tu na mlango kushindana nayo bali pia iliwafungulia na kuwataka waupite wakiwa mmoja mmoja au makundi makundi. Bali iliwapa changamoto kwa namna kadhaa. Ikiwabeza na kuwapunguzia uzito, ikiwataka wawe wanachukua lile jepesi au jepesi zaidi:

- Kwa mara ya kwanza ikawataka walete mfano wake[1].
- Kisha ikawataka walete sura kumi[2] mfano wake.
- Kisha ikawataka walete sura moja[3] mfano wake.
- Kisha walete sura moja[4] mfano wa mfano wake[5].
- Na kwa mara zote imewahalalishia kupata msaada kutoka kwa wamtakaye na wanayeweza kumwomba.
- Kisha ikawavurumishia wao na dunia nzima kuwa imeshindwa bila ya shaka yoyote kwa kusema: ﴿**Sema ''Hata wakijikusanya watu (wote) na majinni ili kuleta mfano wa hii Quran basi hawangaliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao.''** Bani Israil 88. Na akasema: **''Na msipofanya – na hakika hamtafanya kamwe – basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, uliowekewa makafiri** ﴾. Al-Baqarah 24.

Hebu tazama, ni utishaji wa aina gani huu, na uchokozi gani huu!

Kwa hakika amewaandalia hukumu ya kukata na ya maisha katika kauli yake ﴿**na hakika hamtafanya kamwe** ﴾ kisha akawatisha kwa moto. Kisha akawalinganisha na mawe. Naapa lau kama katika wao kungekuwa na ulimi unaotikisika basi usingenyamaza na kuacha kushindana naye na hali ya kuwa wao ni maadui wakuu, na ni watu wanaochukia kudhalilishwa, wao ni

---

[1] Kama katika aya 88 ya suratul Bani Israili. Na aya ya 24 ya suratul Attwuuri.
[2] Kama katika aya ya 13 ya suratul Hud.
[3] Kama katika aya ya 38 ya suratul Yunus.
[4] Kama katika aya ya 23 ya suratul Al-Baqarah.
[5] Tazama namna ilivyowashusha katika madaraja haya kwa kuanzia na kuleta mfano wake hadi kufikia kuwataka walete chochote kinachofanana nayo. Kana kwamba anasema: Sikukalifisheni mlete maneno yaliyosawa na Quran yote. Bali inatosha mkileta kitu chenye kufanana nayo bila kukuwekeeni mipaka. Tena kiwe kinafanana kwa makadirio tu na sio kufanana kisawasawa. Na huu ndio upeo wa kujishusha. Na kwa ajili hiyo, hili ndilo likawa neno la mwisho kuteremka katika kuwapa changamoto. Kwa hakika katika Quran hakukuja neno la kutoa changamoto la kusema (Min mith-lihi) aliye mfano wa mfano wake ila katika suratul Al-Baqarah ya Madina. Na madaraja mengine yaliyobaki yamekuja kwa tamko (Mith-lihi) mfano wake katika sura zilizoteremka hapo kabla huko Makka: Tuitafakuri tofauti hii, kwa hakika yenyewe ni ya kufurahisha. Namuomba Allah atuwafikishe sisi na wewe kufahamu siri za kitabu chake. Na kunufaika na mwongozo wake na adabu zake. [Daraazu].

wajivunao. Naye amewapiga sehemu iwaumizayo hasa na ile ya utukufu wao na wanayojivuna nayo. Lakini wao hawakupata upenyo wa kujiokolea hata ule wa kumpinga. Wala hawakupata ngazi ya kupandia kwenda kusongamana naye. Bali walijikuta mbele yake wakiwa mbele ya mlima mrefu. Na hawakuweza kuutoboa[1].. Mpaka walipokata tamaa na uweza wao na kuyakinisha kushindwa kwao. Jibu lao halikuwa vingine ila kupanda ndani ya chombo cha kifo na kuyasemesha mapanga badala ya herufi. Na hiyo ndio mbinu inayokimbiliwa na kila aliyeshindwa kwa hoja na ushahidi. Na kila asiyeweza kujilinda kwa kalamu na ulimi.

Na zimeshapita zama za Quran, na hiyo changamoto bado ipo ili kutoa nafasi kwa kila mtu na nafsi yake. Na zimekuja zama za baada yake, na huko majangwani na viungani mwa mji kuna watu ambao nasaba zao hazijachanganyika. Na ndimi zao hazijapinda. Na ujuzi wao wa lugha haujabadilika. Na wapo miongoni mwao wale ambao wapo tayari lau wengeweza kuiendea[2] dini hii katika misingi yake na kuthibitisha kuwa wao katika suala la Quran wanaweza kukifanya kile walichokifanya wale wa mwanzo wao basi wangekifanya. Lakini wao shingo zao zimedhalilika kwa Quran na kunyenyekea kwake. Na pakazuiwa baina yao na baina ya kile wanachokitamani. Kama ilivyofanyika kwa wenzao wa hapo kabla.

Kisha na karne hizo nazo zikapita. Na lugha hii ikarithiwa na watu wake walioirithi. Isipokuwa hawa ambao wamekuja baadaye, walikuwa wameshindwa sana na ni wenye tamaa ndogo sana ya kufikia matakwa haya matukufu. Kwa hiyo ushuhuda wao kwa nafsi zao ukawa umeongezwa katika ushuhuda wa kihistoria wa wenzao waliotangulia. Na ukawa ni hoja ya kimuujiza inayosimama mbele yao kwa njia mbili: Kisaikolojia na kihoja.. na huu unaendelea kuwa ndio mwenendo wa watu na Quran mpaka siku ambayo Allah atairithi hii ardhi na waliomo juu yake.

---

[1] Tobo: tundu. Hapa mtunzi ametumia sitiari kwa aya hii ambayo ndani yake Allah Mtukufu Aliyetukuka anaelezea kizuizi kilichojengwa na Dhulqarnaini ili kuwazuia Yaajuju Wamaajuju waache kufanya ufisadi ardhini. Na Allah Mtukufu Aliyetukuka ameuelezea kwa sifa mbili:

a – Ya kwamba wenyewe haupandiki kwa urefu wake kwenda juu na kuteleza kwake.

b – Ya kwamba wenyewe haupenyeki kwa ugumu wake na unene wake.

[2] Kuiendea: ili kuiangamiza na kung`oa misingi yake.

**[Utata Wa Tatu: Ni Wa Warabu Kutoupinga Muundo Na Mtindo Wa Quran Huenda Hilo Lilikuwa Kwa Sababu Ya Kuondoka Kwa Hima Yao Na Sio Kwa Sababu Ya Kushindwa Kwao]**

3 – Na kama atatwambia: ndio, nimeshajua kuwa hakuna mtu hata mmoja aliyeleta kitu kinachochuana na Quran. Na lakini sio kila kinachofanywa na watu kinakuwa kipo nje ya mipaka ya uwezo wao. Huenda mwanadamu akaacha kufanya kitu kilicho miongoni mwa jinsi ya matendo yake ya kihiyari kwa sababu hakuna sababu zinazomchochea kufanya hivyo. Au kwa kuwa kuna kiondoshi cha Mungu kilichoondoa hima yake na kuondoa matakwa yake ya kufanya kitu hicho licha ya kuwepo kwa sababu zinazomfanya afanye hivyo. Au kwa sababu kuna kilichotokea ghafla na kuzuia utendaji na kukwamisha uwezo wake wa kukifanya kitendo hicho baada ya matakwa yake kuelekea upande wake.

Kwa mitazamo miwili ya kwanza, tukio la kutoipinga Quran linatokana na uchache wa kuwekeza nguvu kuhusu Quran na sio kutokana na kushindwa kuleta mfano wake. Na kwa mtazamo wa mwisho, kuacha kupambana na Quran kunatokana na kushindwa kufanya hivyo kikweli kweli. Lakini kizuizi sio kile kinachotoka upande wenye tabaka la juu kuliko usawa wa uweza wa kibinadamu. Bali kinachozuia ni kitu cha nje nacho ni himaya[1] ya uweza wa juu kwake yeye na kutoa ulinzi wake kwa jambo hilo dhidi ya upinzani wa wanayoyapinga. Na lau kama hiki kizuizi kingeondolewa, basi watu wangeweza kuleta kitu kinachofanana na Quran.

Tumemwambia: mitazamo hii yote haiendani na mada yetu kwa hali yoyote ile.

Ama la kwanza: Kwa hakika sababu zinazopelekea kushindana zilikuwa zipo tele. Je, ni kitu gani kina nguvu zaidi katika kuchochea mzuka wa adui yako kuliko maneno ya kiumbuji yenye kujirejea rejea na ambayo yanaelekezwa kwake huku yakitangaza kuwa ameshindwa kufanana na kazi zako? Kwa hakika changamoto hii peke yake yatosha kuamsha hamasa ya

[1] Hii ndio kauli ya kusema kuwa kuna Aswirfa, kauli iliyokuwa mashuhuri kuhusu mfumo (serikali) ya pote la Muutazila. Jambo ambalo japokuwa kwa ujumla ni kukiri kuwa kuna muujiza ila kwa hakika hawalikubali isipokuwa asiyekuwa mwarabu au anayefanana nao miongoni mwa wale wasioonja ladha ya umbuji wa lugha. Na kwa ajili hiyo, hakufuatwa na mwanafunzi wake ambaye ni Ajaahidhu wala mtu yeyote miongoni mwa wanazuoni wa Kiarabu. Na hilo linachukuliwa ni kinyume na kile kilichojulikana na warabu wenyewe kama tutakavyobainisha. [Daraazu].

mwoga na kuwasha hima yake ya kujilinda kwa vile uwezo wake utakavyofikia. Sasa inakuwaje, lau kama pamoja na hayo, utakuwa unamvurumishia kuwa ana rai za kipumbavu na amepotea njia? Na itakuwaje, lau kama nyuma ya vita hiyo ya kimijadala kuna kuvunja itikadi yake, na kufuta ada zake, na kukata muunganiko baina yake na historia yake na mustakbali wake?

Ama la pili: Kwa hakika sababu hizi, tumeshaziona kuwa zimeleta matunda yake katika uhalisia. Na kuamsha hima za wapinzani kwenda katika hatua zake za mipaka ya mbali zaidi. Mpaka jambo la Muhammad na Quran likawa ndilo shughuli yao inayowashughulisha. Na kihoro chao kinachowakera, kwa hiyo hawakuacha njia yoyote miongoni mwa njia za kupambana naye kwa upole au kwa ukali isipokuwa waliipita na kuifanya kigezo chao:

- Wamuhadae katika dini yake ili awe laini kwao na kijiegemeza kidogo katika dini yao[1].
- Au wanapatana naye kwa mali na ufalme ili aache madai yake[2].

---

[1] Wanaume wa kikuraishi walikwenda kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake wakamwambia: Ewe Muhammad, njoo ujikombe kwa miungu yetu, au jiunge kwa miungu yetu nasi tuingie pamoja nawe katika dini yako. Ndipo kauli ya Allah ilipoteremka**: ﴿ Na hakika walikuwa karibu kukukengeusha na yale tuliyofunulia (tuliyokuletea Wahyi) ili upate kutuzulia badala ya haya (ya haki tuliyokuteremshia ﴾.** Bani Israil 73. Imepokewa na Ibnu Mardawayhi kwa sanadi yenye daraja ya nzuri. [Daraazu].

Nimesema: Assuyuutwi katika Adduraru Almanthuuru 4/352 na katika Asbaabu Annuzuuli 123 ameiegemeza kwa Ibnu Is-Haqa na Ibnu Abuu Haatim na Ibnu Mardawayh. Kisha akasema katika sababu za kuteremka aya hii: hii ndio sahihi zaidi kuliko riwaya zote zilizokuja juu ya sababu za kuteremka aya hii, nayo ni sanadi nzuri. أ هـ .

[2] Hii ni kuashiria kisa kirefu ambacho kwacho kauli ya Allah Mtukufu imeteremka ﴿**Na walisema (makafiri wa Kiqureshi kumwambia Mtume): ‘‘Hatuwezi kukuamini mpaka utububujishie (utupitishie) chemchemu katika ardhi (hii yetu ya Makka ﴾.** Bani Israil 90 na aya za mbele yake. Imepokewa na Ibnu Jariiru kwa sanadi iliyoungana na yenye utata. Na hadithi hii ina ushahidi wa hadithi Mursal ambayo ni sahihi. [Daraazu].

Nimesema: Majumuisho ya kisa hiki ni kuwa wakuu wa Kikurayshi walikwenda kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kumuwasilishia mali kama ikiwa anataka mali. Au ubwana na utukufu, au awe mfalme wao. Au matibabu kama ana tatizo la kupatwa na jinni. Kwa sharti aache dini yake. Naye akawajibu kwa kukataa yale waliyomdhania kuwa atayakubali. Na akawafikishia kuwa yeye hahitaji kutoka kwao kingine zaidi ya Uislamu. Wakamtaka amuombe Mola wao aiweke mbali nao milima yote iliyokuwa karibu nao. Na ardhi yao aifanye tambarare na apitishe mito ndani yake. Na awafufulie wazee wao waliopita. Na Allah awapelekee Malaika. Au Nabii rehema na amani ziwe juu yake au na kasri lenye hazina na mabustani. Kisha mmoja wao akamtaka

- Au wanahusiana juu ya kumwekea vikwazo. Na kumzuia yeye na watu wake wa karibu wasipate bidhaa muhimu, mpaka wafe njaa au wamsalimishe Mtume[1].
- Au wazuie sauti ya Quran isitoke nje ya majumba ya waislamu kwa kuogopea isije ikasikika na yeyote miongoni mwa watoto wao[2].
- Au wamvurumishie kauli za kichochezi na kumchafua.
- Au wamtuhumu mwenye Quran kuwa ni mchawi na mwendawazimu ili wawazuie watu wa makabila wasiomjua, na ambao wanakuja Makka katika misimu maalumu.

---

Mtume rehema na amani ziwe juu yake ajitwalie ngazi ya kupandia mbinu kisha awaletee nakala ya Quran na ikiwa na malaika wanne wanaomshuhudia Utume wake… na yote hayo, kiuhalisia yamekuja kwa njia ya kubeza na kufanya istihizai, na ubishi na sio kutafuta haki.

Ime pokewa: Attwabary 15/164. Na Assuyutwi katika Adduraru Almanthuri 4/367 kwa Twabary na Ibnu Is-Haqa na Ibnu Almundhiri na Ibnu Abuu Haatimu. Na akaitia nguvu katika Sababu za kuteremka 126 kwa ushahidi ulio na daraja ya Mursalu katika sunani Abuu Said bun Munsuuri.

[1] Hii ni kuashiria habari za **‘‘Kurasa ovu ambazo Makureishi waliungana na kuziandika dhidi ya ukoo wa Haashimu na ukoo Almutwalib eti wasiwaolee, wala wasiwauzie, hadi wamsalimishe kwao, Mtume rehema na amani ziwe juu yake’’**. imepokewa na Bukhari na Muslimu kutoka kwa Azzuhuriyu. Na kuhusiana na muungano huu, Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasema: akiwa katika vita vya ukombozi wa Makka na vita vya Hija ya kuaga: **‘‘Nafasi yetu ni kesho Allah akipenda katika eneo la ukoo wa Kinana pale walipogawanyika kuhusiana na kukufuru’’.** Imepokewa na Bukharin a Muslimu [Daraazu].

- Nilisema: Hadithi ya kwanza: imepokewa na bukhari na Muslimu: Bukhari ameipokea katika Alhajji 1590 na Muslamu katika Alhajji 344.

Na hadithi ya pili: imepokewa na bukhari na Muslimu: Bukhari ameipokea katika Alhajji 1589 na Muslamu katika Alhajji 343.

[2] Watukufu wa kikuraishi hawakuweza kumvumilia Abuu Bakar akiitangaza Quran kwa kuisoma kwa sauti katika kiwanja cha nyumba yake. Kwani nyoyo nyingi za watoto wao wa kiume na wa kike na watumwa wao zilikuwa zikiporomoka kwake kusikiliza kisomo chake. Na washirikina wakaogopea wasije wakafitinika. Na Ibnu Addaghinah alikuwa amemkodisha eneo Abuu Bakri, na akamwamrisha Abuu Bakri amrejeshee eneo hilo kama Abuu Bakri atang`ang`ania kuendelea kutangaza kisomo chake. Na kwa hakika hili alilifanya. Hadithi hii imepokewa na Bukhari. [Daraazu].

Nimesema: imepokewa na Bukhari katika Alkafaalati 2297. Na mtiririko ulio timamu katika Manaaqibu Al-Answaari 3905.

- Au wanamfanyia vitimbi[1] au wamfunge[2] au wamuue au wamtoe[3].
- Au wazitie hatarini nafasi zao, mali zao na watu wao katika kumpiga vita.

Je, haya yote yalikuwa ndio kushughulika na kuipuuza Quran na uchache wa kuzingatia suala lake?!

Kisha kwa nini yote haya, hali ya kuwa yeye ameshawajulisha kuwa njia ya pekee ya kumnyamazisha ni kwa wao kuleta maneno yaliyo mfano wa yale aliyowaletea yeye? Je, hilo halikuwa ndilo jambo la karibu zaidi kwao na lenye kubakia na lau jambo lake lingekuwa mkononi mwao? Lakini wao walipita milango yote ila mlango huu. Kwa hiyo mauaji, utekajinyara, ufakirishaji na udhalilishaji, yote haya yakawa mepesi kwao kuliko kuipita njia hii yenye makorongo na ambayo wamejulishwa naye. Basi ni kitu gani kinakuwa ndio kushindwa kama ikiwa huku sio kushindwa kwenyewe?

Hapana shaka ya kuwa, kampeni hizi zote hazikuwa ni kupambana na utu wa Mtume na Maswahaba wake. Kwa hakika hapo kabla, walikuwa wakiwahurumia kwa huruma zao, na wakiwapenda kwa tabia zao njema. Kama zilivyo kampeni hizi kuwa zenyewe hazikuwa zikielekezwa dhidi ya Quran iliyoko vifuani wala iliyoko ndani ya majumba. Kwa hakika wao walishakubali kwa mtu yeyote aabudu Mola wake nyumbani kwake vyovyote atakavyo. Hakika si vinginevyo, kampeni hizo zilikuwa

---

[1] Hapo inaashiria kauli ya Allah Mtukufu Aliyetukuka ﴿**Na (kumbuka Ee Nabii Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakutoe (kwa hali mbaya katika Makka); na wakafanya hila (zao barabara); Na Mwenyezi Mungu akazipindua hila hizo. Na Mwenyezi Mungu ni mbora wa kupindua hila (za watu wabaya** ﴾**.** Al-Anfal 30.

[2] Wakufunge: wakuweke jela au wamjeruhi jeraha ambalo hatoweza kusimama nalo.

[3] Wamtoe: yaani kutoka Makka.

Alhaafidhu Ibnu Hajari katika Fatihu Albaari 7/278 amesema: Ahmad katika hadithi ya Ibnu Abbas kwa sanad yenye daraja ya Hassan ametaja: ‘‘**Kuhusu kauli ya Allah Mtukufu** ﴿**Na (kumbuka Ee Nabii Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru …** ﴾ **hiyo aya, amesema: Makuraish walishauriana usiku huko Makka, baadhi yao wakasema: kutakapokucha asubuhi, mfungeni kwa kamba – wakimkusudia Mtume rehema na amani ziwe juu yake – na wengine wakasema: bali muueni. Na wengine wakasema: bali mtoeni. Basi Allah akamweleza Nabii wake rehema na amani ziwe juu yake suala hilo. Basi Ali akalala katika kitanda cha Nabii rehema na amani ziwe juu yake katika usiku huo. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akatoka hadi akafika pangoni…**’’ Hiyo hadithi. أ هـ .

- Nimesema: Imepokea na Ahmad 1/348. Na wafasiri wengi wanaona kuwa aya hii imeteremka Madina ikiwa ni ukumbusho kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake juu ya neema za Allah kwake, pale alipomwokoa na vitimbi vya washirikina.

zikielekezwa katika lengo moja tu, na kupambana na hatari moja tu nayo ni kuitangaza[1] hii Quran na kuisambaza baina ya warabu.

Wala usiingiwe na hofu moyoni mwako eti wao hawajaona baya lolote katika kuitangaza Quran ila ni kwamba yenyewe ni mlinganio mpya wa kuiendea dini mpya tu. Sivyo hivyo! Miongoni mwa warabu walikuwepo mahunafaa (watu wanaoabudu kisawasawa) miongoni mwa wahutubu na washairi mafahali. Kama Qussu bin Saaidah, na Ummayya bin Abuu Aswilti na wasiokuwa wawili hao. Na hotuba zao na mashairi yao yalikuwa yamesheheni malinganio ya yale yaliyolinganiwa na Quran kuhusu dini ya kimaumbile. Sasa hebu jiulizeni, hivi kwa nini wao watilie umuhimu sana jambo la Muhammad na Quran yake tofauti na vile walivyotilia umuhimu jambo la wengine? Halikuwa hilo ila kwa kuwa wao walikuta kwake kuna jambo lingine halifanani na jambo la watu wengine. Na kwamba wao walihisi kuwa katika Quran yake kuna nguvu ya kushinda na mkondo kumbakumba. Anataka kupanua utawala wake pale itakapofikia mwangwi wa sauti yake. Na kwamba wao hawakuwa na njia ya kupambana naye miongoni mwa njia za kumpinga kimaneno, njia ambayo ni hijiiraahum[2]. Na ambayo yenyewe ndio njia mubashara aliyowapa nayo changamoto. Hakuna shaka ilikuwa njia ya pekee kwao wao kupambana naye na kuzuia kwa njia mbalimbali baina ya hii Quran na watu kwa vyovyote itakavyowagharimu, miongoni mwazo ni kujitoa muhanga. Na hivyo hivyo walifanya[3]. Na hivyo hivyo ukapita mwenendo wa wale ambao walikuja baada yao miongoni mwa maadui wa Quran mpaka siku yetu hii.

Ama la Tatu: Hakika mambo yalivyo, lau kushindwa kwao kufanana na Quran kungekuwa kwa tukio lililowapata, lililozuia baina yao na baina ya kitu katika uwezo wao, basi isingebainikia kwao wao kushindwa huko ila baada ya kukunjua ndimi zao kwake. Na kujaribu kwa uwezo wao dhidi

---

[1] Na katika hilo Nabii rehema na amani ziwe juu yake na aali zake, pale alipokuwa anajiwasilisha kwa watu katika visimamo alikuwa anasema: **‘‘Je, kuna mtu atanichukua na kunipeleka kwa watu wake? Kwa hakika Makuraishi wamenizuia nisifikishe maneno ya Mola wangu’’**. Imepokewa na Abuu Daud na Attirmidhiyu. Tazama kauli yake: **wamenizuia ‘‘kufikisha’’** na hakusema: wamenizuia ‘‘kusoma’’. [Daraazu].

Nimesema: Hadithi hii imepokewa na Abuu Daud katika Assunnatu 4734. Na Attirmidhiyu katika Fadhaailu ALquraan 2925. Na Ibnu Maajah katika Almuqaddima 201. Na Ahmad 3/322, 339 na 390. Na Albaniyu ameipa daraja ya sahihi 1947.

[2] Hajiiraahum: Mwendo wao na jambo lao.

[3] Rejea athari za Suluhu ya Hudaibiya na kuchanganyika kwa waislamu na washirikina na kusikia kwao Quran katika pambizo ya ukurasa wa matini chanzi 33.

yake. Kwa kuwa suala lenyewe, haiwi kwa mtu kuhisi kuondoka kwa uwezo wake wa kufanya kitu alichokuwa anakiweza. Kama uwezo wake wa kusimama na kukaa ila baada ya kukijaribu. Na sisi tumekwishajua kuwa wao wamekaa na kuacha jaribio hili, na hakujatokea kwao wao kulianza jaribio hili ila idadi chache miongoni mwao na wale wenye maono mabaya. Hilo likawa ni alama juu ya tabu yao ya kimaumbile kutoka kwao wenyewe. Na juu ya kuhisi kwao kuwa kushindwa kwao katika jambo hilo ni jambo la kimaumbile gumu mno. Kama vile kushindwa kwao katika kuuondosha mlima, na kuzifikia nyota za mbinguni. Na kwamba wao walikuwa hawana haja ya kutafuta ushahidi wa elimu hii ya lazima kwa kujaribu majaribio mengi.

Lau kama wao wangekuwa hawakujua kushindwa kwao na Quran tangu mwanzo wake, kwa hakika kushindwa kuliwakuta baada ya kuhisi kwao kuwa Quran yenyewe ipo katika kiwango cha maneno yao, basi ajabu yao ingekuwa inatokana na nafsi zao: Sasa iweje wataabike nayo hali kwao wao, hiyo Quran ipo katika ncha ya Mthumaami[1]? Wakakimbilia kuulizana wao kwa wao, ni ugonjwa gani uliotukumba na kuzilemaza ndimi zetu na zikashindwa kupambana na maneno haya yaliyo kama maneno mengine yote? Au lau wangerejea katika bayani yao ya kale kabla ya wao kupatwa na kushindwa, basi wakaja na kitu katika maneno yanayoenda sanjari na Quran. Lakini wao katika swala hilo hawajaleta jambo la kale wala jipya. Na Quran yenyewe imekuwa ndio inayochochea ajabu yao na kushangazwa kwao mpaka wakawa wakiporomoka kusujudu pale wanapoisikia kabla ya kupita muda wa kupima baina yake na maneno yao[2]. Bali kwa hakika miongoni mwao kulikuwa na yule anayeshindwa na hisia hii na kwa hiyo katika ulimi

---

[1] Ncha ya mthumaami: ni kitu ambacho si kigumu kukipata. Na Mthumaami ni mmea wa jangwani usiorefuka sana hadi kuleta tabu kuuchuma.

[2] Kutoka kwa ibnu Abbas Allah amuwie radhi yeye na baba yake amesema: ‘‘**Mtume rehema na amani ziwe juu yake alisujudu katika Najmi [yaani suuratul Najmi] waislamu, majini na watu wengine pia washirikina wakasujudu pamoja naye’’.** Imepokewa na Bukhari katik Attafsiiri 4862.

Na kutoka kwa Abdallah bin Masuudi Allah amuwie radhi amesema: ‘‘**Sura ya kwanza iliyoteremshwa ndani ikiwa na kusujudu {(Annajim ﴾. Akasema, basi Mtume rehema na amanai ziwe juu yake akasujudu, na wakasujudu walio nyuma yake ila mtu mmoja tulimuona akichukua gao la mchanga akausujudia. Na baada ya hapo nilimuona ameuliwa akiwa kafiri. Naye ni Ummaya bin Khalafi’’.** Muttafaqun alayhi: Imepokewa na Bukhari katika Attafsiiri 4863, na Muslimu katika Almasaajidu Wamawaadhiu Swalaati 105.

wake kunabubujika maneno ya kukiri kisawasawa: (haya si maneno ya mwanadamu)[1].

**[Utata wa nne: ni kwa yule anayedhani kuwa muujiza wa Quran sio kwa upande wa kilugha kwa kuwa yenyewe haijatokapo nje ya lugha ya Kiarabu katika msamiati wake wala sarufi yake]**

4 – Ikiwa atasema: Kwa sasa imeshabainika kuwa kunyamaza kwa watu kushindana na Quran ilikuwa ni kushindwa. Na kwamba wao walikuta katika tabia ya Quran siri miongoni mwa siri za kimuujiza unaotukuka na kuupita uwezo wao. Lakini mimi sifahamu kwamba upande wake wa kilugha ndio unaowezekana kuwa kiini cha siri hii. Kwa sababu mimi nasoma Quran na wala siikuti ikitoka katika kile kilichozoeleka na Warabu katika lugha yao ya Kiarabu: Kwani yenyewe maneno yake yameundwa kutokana na herufi zao. Na kutokana na maneno yao ziliundwa sentensi na aya zake. Na katika mtindo wao wa kutunga ndimo ulipokuja utungo wa Quran. Sasa kipya ni kipi katika msamiati wa Quran na ambacho warabu hawajakijua miongoni mwa maudhui yake na miundo yake? Na kipya ni kipi katika muundo wa Quran na ambacho warabu hawajakijua katika njia zao ambazo hazijachukuliwa kutoka katika mapito yao. Mpaka tuseme eti yenyewe imewaletea kitu kilicho juu ya uwezo wao wa kilugha?

Tunamwambia: Ama kuwa Quran Tukufu haijatoka nje ya lugha yake kwa kufuata mwendo wa Warabu katika msamiati wao wa neno moja moja na sentensi. Kwa ujumla wake hilo ni kweli halina shaka ndani yake. na kwa hivyo ndio limeingia katika muujiza. Na lipowazi zaidi katika kukata udhuru na visingizio ﴿**Na lau kama tungaliifanya Quran kwa lugha isiyo ya Kiarabu wanaglisema: ‘‘Kwa nini aya zake hazikupambanuliwa? Lo! Lugha isiyokuwa ya Kiarabu na (Mtume) Mwarabu! (mambo gani haya)!’’** ﴾. Haa Mym Sajdah 44.

Ama baada ya maneno hayo, je, imekutoka ukakosa kujua kuwa ujenzi wa ufundi wa lugha ni kama mfano wa ujenzi wa jengo: Mainjinia wajenzi hawaumbi vifaa vya ujenzi ambavyo havipo ardhini. Wala katika ufundi wao hawatoki nje ya misingi ya kiujumla ya kiujenzi. Wala hawavuki katika ujenzi wao nje ya kuwa wenyewe ni kuta zilizonyanyuliwa, vipaa vilivyoezekwa, na milango iliyosimikwa. Lakini wao wanatofautiana kwa ubora katika ufundi wao nyuma ya mambo hayo, katika kuchagua vifaa

[1] Hadithi kwa ukamilifu wake itakuja katika ukurasa wa 116 wa matini chanzi.

imara na vyenye kudumu muda mrefu. Majengo yenye kuwakinga watu wasipate joto kali na baridi kali. Na katika kusimika kwa kina kirefu nguzo zake na kurefusha jengo. Na kuweka malighafi mepesi katika kinachobebwa na majengo hayo, kunufaika na eneo dogo na kuweka maeneo muhimu mengi. Na kupangilia vyumba na maeneo ya mwanga, kiasi ambacho mwanga na hewa vinapenya kuingia ndani. Na wapo miongoni mwao wale wanaotekeleza hayo yote au mengi yao. Na wapo miongoni mwao wanaopunguza kitu katika hayo au vitu vingi… Mpaka fani za mapambo na urembo pia wanatofautiana kwa vionjo vya kiunjinia katika hilo kwa tofauti za mbali mno.

Hivyo hivyo unaona kwa watu wa lugha moja, huwa wanafikisha lengo moja kwa njia mbalimbali zinazotofautiana katika uzuri na kukubalika. Na hakuna neno katika maneno yao wala maweko katika maweko yao ulio nje ya vijenzi vya lugha na kanuni zake katika sentensi. Lakini suala la uzuri wa kuchagua vijenzi hivyo na maweko yake ndio yanayoyanyanyua maneno hadi yanazingatiwa na usikivu wako. Na kupoza kifua chako, na kuumiliki moyo wako. Ni sawa sawa na uchaguzi wa kitu chochote katika hayo huenda ukakiteremsha hicho kitu hadi kufikia kukera usikivu wako, na kuichefua[1] nafsi yako. Na tabia yako inayakataa maneno hayo.

Hayo yote ni kwa kuwa katika lugha kuna lugha ya watu wote na ya watu maalum, iliyoachiliwa na iliyofungwa, ya kiujumla na iliyochambuliwa, ya ndani ya ibara, ishara, yaliyomo, viashiria, maelezo na maombi, kuna sentensi za kuanzia na nomino na za vitenzi. Na ndani yake kuna ukanushi na kuthibitisha. Na ndani yake kuna hakika na majazi. Na ndani yake kuna kurefusha na kufupisha. Na ndani yake kuna kutaja na kuacha kutaja. Na ndani yake kuna kuanza upya na kuunganisha. Na ndani yake kuna kuanishwa na kisichoainishwa. Na ndani yake kuna kutanguliza na kucheleweshа na kadhalika…. Na kutokana na mapito haya yote watu wanayaendea malengo yao. Bila ya kuvuruga maweko katika hayo na kuyapuuza maweko ya lugha ya kiujumla. Bali wao wapo katika matawi yake wakitofautiana. Na katika mipaka yake wanakutana.

Lakini si kila kitu katika haya kinachokuwa kizuri katika kila sehemu. Na si kila kitu katika hayo kinakuwa kibaya katika kila sehemu. Kwa hiyo, dhamana ya jambo hilo ipo kwa mwenye kulitaka. Kama si hivyo, basi

[1] Kuchefua: Kukoroga, kama inavyotokea kabla ya kutapika.

umbuji wa maneno ungekuwa katika ulimi wa watu kwa ladha moja. Na katika masikio yao ni mrindimo mmoja. Sivyo hivyo! Kwa hakika njia moja inaweza kukufikisha sehemu yako ya amani kwa muda fulani. Na ikakuzuia kufikia haja yako wakati mwingine. Na huenda neno unaloliona katika sehemu fulani lipo kama hirizi iliyopotea. Kisha neno hilo hilo ukaliona katika eneo lingine ni kama kito cha thamani kinachong`aa. Kwa hiyo mambo yalivyo katika kuchagua njia hizi ni ipi yenye haki zaidi ya kupitwa katika lengo fulani, na ipi ndio ya karibu zaidi kufikisha katika kusudio:

- Katika mjadala ni njia ipi madhubuti kutolea hoja. Na yenye kusagasaga utata.
- Na katika wasifu ni njia ipi ni ya kina zaidi inayowakilisha matukio.
- Na katika maeneo ya ulaini ni njia ipi ni nyepesi zaidi kuisikiliza na ina upole zaidi katika maumbile.
- Na katika maeneo ya ukali ni njia ipi yenye ukali na yenye kupasua vifua kwa moto huo uwakao.
- Na kwa ujumla ni njia ipi inayotosheleza haja za kibayani na kwa uhondo wake inayobakia zama na zama.

Katika uchaguzi huu suala ni gumu na si jepesi. Kwa sababu Nyanja za kuchagua zina mawanda mengi yaliyo na rangi tofauti tofauti katika maumbo ya msamiati na tungo. Na watu hawapo sawa sawa katika kuwasilisha rangi hizi. Zaidi ya hapo hawapo sawa katika kuweka mizani baina yake. Na zaidi hawapo sawa katika uzuri wa kuchagua hizo rangi. Kwani huenda watu wawili, mmojawapo akaongoka kuchagua kile kilichosahaulika na mwenzake. Na huenda kila mmoja wao akaghafilika kukichagua kile kilichochaguliwa na mwenzake. Na huenda namna moja iliyosawa na namna mbili ikakupita hapa na kisha ukazipata namna zote mbili huko sehemu nyingine au kinyume chake.

Na kwa ujumla ya mitazamo yote inayotazamwa na msemaji kuhusiana na kauli yake, basi inazalika picha maalumu, mfano wake ni kama mfano uliopo katika tungo za kimaana zenye (hali ya mtu) katika tungo hizo. Kama hali ya mipandano ya vitu vya kimaada. Na hii (hali ya mtu) ndio tunayoiita muundo mtindo au njia. Na kwa kupitia hiyo hali ndipo kunapotokea tofauti katika viwango vya maneno. Katika hadhi yake ya uzuri na kukubalika.

Kipya katika lugha ya Quran ni kuwa, katika kila jambo linaloshughulikiwa na Quran miongoni mwa maswala ya kiakili, basi

yenyewe inalichagulia jambo hilo vifaa (maneno) vizuri. Na vinavyoshikama vizuri na maana lengwa. Na vyenye kukusanya vyote vilivyotawanyika. Na vifaa vilivyo karibu zaidi kuchanganyika vizuri. Kisha inakiweka kila kifaa hata kile kidogo kama punje ya nyuklia (Atom) katika sehemu yake ambayo ndio chenyewe kinastahiki kukaa hapo: Kiasi ambacho hapati maana katika tamko lake ila yenyewe ni kioo chake safi, na picha yake iliyokamili. Na wala hapati tamko katika maana yake ila lipo sehemu yake ya salama, na makao yake madhubuti. Si siku au baadhi ya siku. Bali hata kama zitapita zama na kuja zama nyingine. Hakuna sehemu mbadala ya neno (kifaa) inayotakiwa kukaliwa na mkazi (neno) mwingine. Wala hakuna mkazi anayetaka nyumba yake ipewe mbadala... na kwa ujumla Quran inakujia na muundo mtindo huu kwa kile kilicho bora kabisa katika ufundi wa bayani.

Matakwa haya yana kitu inachokionesha, na ujumla wake una maelezo yake. Na si kusudio letu kwa sasa kukuharakisha katika kutafuta ushahidi wake na maelezo yake. Kwa hakika tumetaka kukuondoshea huu utata ili ujue kuwa si kila maneno ya Mwarabu ni kama maneno yote ya Mwarabu mwingine. Na kwamba, katika upande huu wa kilugha, inastahiki zaidi tukitofautiana kinguvu huku tukishuka hadi upeo wa kushindwa. Au tukipanda hadi kufikia upeo wa muujiza.

Kama utapenda kujua yale ya Quran Tukufu, mtiririko wake na kufikia kwake upeo wa juu katika dhamira hizi. Na wewe bado hujaruzukiwa nguvu ya kutengeanisha baina ya madaraja ya maneno, basi jua kuwa huna njia ya kukomesha jambo hili kwa kutumia hisia na uzoefu. Kwa hakika njia yako ni kuchukua hukumu yake kwa kuipokea kutoka kwa watu wake na utosheke katika hilo kwa kupewa ushahidi wa wanaolijua. Na kwa hiyo, itakuwa ni miongoni mwa haki yako juu yetu kukupatia mfano wa ushuhuda wao. Hebu kwa sasa chukua mfano huu:

**‘‘Walidi Ibnu Almughiira alienda kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na aali zake. Aliposomewa Quran alikuwa kana kwamba moyo wake umelainika kwa Quran. Hilo likamfikia Abuu Jahli, naye akamwendea na kumwambia: Ewe ami, kwa hakika watu wako wanaonelea kuwa, wakukusanyie mali na wakupatie. Kwani wewe umemwendea Muhammad ili ukione kile kilicho kwake. Walidi akasema: Kwa hakika Maqurayshi wameshajua kuwa mimi nina mali nyingi miongoni mwao. Abuu Jahli akasema: Basi mseme Muhammad**

**kwa kauli ambayo itawafikia watu wako huku wakijua kuwa wewe unampinga na kumchukia. Akasema: niseme nini? Naapa kwa Allah, hakuna miongoni mwenu mtu mjuzi zaidi kuliko mimi kimashairi na kwa rajizi[1] zake wala kwa kaswida[2] zake, wala kwa mashairi ya majini. Naapa kwa Mungu yenyewe katika yale ayasemayo haifanani na chochote katika haya. Na ninaapa kwa Mungu, kwa hakika kauli yake ina utamu, na juu yake kuna uhondo[3] na kwa hakika yenyewe ni yenye kutoa nuru juu yake, na kuangaza chini yake, na yenyewe inakuwa juu wala haikaliwi juu. Kwa hakika yenyewe inavunja yale yaliyo chini yake..''** Hiyo hadithi [4] Imepokewa na Alhaakimu kutoka kwa Ibnu Abbas na akasema hadithi hiyo ina daraja ya sahihi kwa sharti za Bukhari[5].

---

[1] Rajizi: aina ya ushairi, na umeitwa rajizi kwa kutikisika kwake. Na mizani yake ni mepesi masikioni na inaingia moyoni.

[2] Kaswida: ni wingi wa neno kasida, nayo ni mashairi yale ambayo yamezidi beti kumi na tano za mashairi.

[3] Uhondo: uzuri, kupendeza na kukubalika.

[4] Hadithi hiyo ina vipande vilivyobakia, navyo ni: ''Kwa hakika Abuu Jahali alimsisitiza sana Walidi na kumwambia: Watu wako hawatakuridhia mpaka useme kitu katika hilo. Walidi akasema: niache nifikiri. Alipofikiri akasema: Huu ni uchawi unaoathiri kwa wengine''. Na katika hilo ikateremka kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Niache mimi na niliyemuumba peke yangu. Na nikamjaalia awe na mali nyingi. Na watoto waonekanao (kila mahala). Na nikamtengenezea mambo yake kumtengezea (kuzuri kabisa). Kisha anatumaini nimzidishie! Wapi! Hakika yeye alikuwa anazipinga Aya zetu. Basi nitamtesa kwa mateso makuu. Hakika yeye alifikiri na akapima (la kusema kuitukana Quran). Basi ameangamia. Namna gani alivyokadiri (katika kuitukana kwake Quran). Tena ameangamia. Namna gani alivyokadiri (katika kuitukana kwake). Kisha akatazama. Kisha akakunja kipaji (chake) na akafinya uso. Kisha akaipa mgongo (haki) na akatakabari (akajivuna). Na akasema ''Hayakuwa haya (aliyokuja nayo Muhammad) ila ni uchawi ulionukuliwa (kwa wachawi wakubwa kabisa wa zamani)''. ''Hayakuwa haya (anayoyasema) ila ni kauli ya binadamu** ﴾. Al-Muddathir 11 – 25.

Na kile kilicho baada yake. tazama taswira ya Quran namna inavyoonesha juhudi kubwa alizozitoa huyo mtu katika kutoa hukumu yake ya pili pale inaposema: Hakika yake alifikiri na akapima, kisha akatazama, kisha akafinya kipaji chake na kukunja uso, kisha akaipa mgongo na kujivuna. Na maana ya haya yote ni kuwa yeye alikuwa anapambana na maumbile yake, na kuilazimisha nafsi yake iende kinyume na hisia zake. Na kwa hakika yeye alikuwa katika kutahayari na kubanwa na kile anachosema…. Na hatimaye aliweza kusema yale aliyoyasema kwa kuteremka kwenda katika matakwa ya watu wake. Na tazama tofauti iliyopo baina ya hukumu hii ya kutengeneza na baina ya hukumu ile ya kimaumbile kwa warabu katika kauli yake ya mara ya kwanza: Hakika yenyewe yanakaa juu na hayatokaliwa juu, na hakika yake yanavunja yale yaliyo chini yake. [Daraazu].

[5] Imepokewa na Alhaakimu 2 / 506 katika hadithi ya Ibnu Abbas. Na Alwaahidiyi katika Asbaabi Annuzuuli 446. Na Assuyutwiy ameiegemeza kwa Alhaakim na Albayhaqiy katika Addalaaili. Na katika Asbaabu Annuzuli 209 aliongelea: ina daraja ya sahihi kwa

Ndio, ikiwa hutofautishi baina ya maneno na maneno basi huo ni ushahidi unaokutosha kuwa ushahidi. Achana na kuwa yenyewe ni ushahidi wa watu wa lugha wenyewe. Bali huo ni ushahidi wa maadui kwa adui wao.

Kama hukuona mwezi basi jisalimishe * Kwa watu waliouona kwa macho.

Ama ukiwa umepewa bahati ya kujua tofauti za maneno na kupambanua baina ya miundo mitindo yake, basi soma uzitakazo miongoni mwa hotuba za warabu, mashairi yao, hekima zao, methali zao, risala zao na mijadala yao. Na katika hilo ukifuatilia zama za kijahiliya (kijinga) na za Kiislamu kwa kuzingatia matabaka yao yaliyotofautiana. Kisha fungua ukurasa mmoja wa kitabu hiki Kitukufu (Quran) na utazame, je, unaona nini?

Mtindo muundo wa ajabu sana. Na njia ya mazungumzo ya hali ya juu yenye ubunifu. Kanakwamba yale maneno mengine miongoni mwa maneno yamenukuliwa, kama vile baina yake, kwa mujibu wa kauli ya baadhi ya wanafasihi (kuna maweko ya kuchechemea). Hutoona kitu kilichotangulia kilicholeta mfano wake, wala cha sasa kilichochapwa kama muundo wake. Lau kama aya moja katika Quran itakujia katika lundo la maneno ya wanaumbuji basi hiyo aya ingejijulisha sehemu yake iliopo. Na ingejipambanua baina ya maneno hayo. Kama inavyojipambanua sauti ya wimbo mzuri yenye kuvuta hisia baina ya aina nyingi za sauti za nyimbo. Au kama tunda jipya linavyojipambanua baina ya aina mbali mbali za vyakula.

### [**Utata Wa Tano:**

### **Anayedai Kuwa Kushindwa Kwa Watu Kuendana/Kushindana Na Muundo/Mtindo Wa Quran Sio Jambo La Pekee Kwa Quran Tu. Kwa Sababu Mtindo Muundo Wa Kila Msemaji Una Taswira Ya Mwenyewe Na Hali Yake Mwenyewe Kwa Hiyo Mtu Mwingine Hatoweza Kukaa Mahala Pake**]

5 – Muulizaji akiishia pamoja nasi katika eneo hili atasema: Kwa hakika nyinyi kwa kutumia bayani hii mmetufungia mlango wa shaka. Lakini nyinyi hamjakaa hata kidogo ila mmetufungulia mlango mpya. Je, hamjatwambia kuwa ufundi huu wa bayani kwa watu haupo daraja moja. Na kwamba nguvu

sharti za Bukhari. Na muqbil bin Haadiy Alwaddaaiy katika Asbaabi Annuzuli 168 ameipa daraja la sahihi. Na imepokewa na Attwabary katika Attafsiiri 29 / 156 ikiwa na daraja ya mursali kutoka kwa Ikrima.

katika hilo inaenda ikiwa tofauti tofauti kwa madaraja mbalimbali. Basi kwa hiyo kile tunachokiona kuwa ni kibaya kukihesabu kuwa ni muujiza na ambao mmetuelezea ni jambo lililoenea linatembea katika miundo mitindo ya watu kama inavyotembea katika Quran.

Hivi hamuoni kuwa kila msemaji au mwandishi kwa hakika anaweka bayani yake ikiwa ni kipande katika akili yake na hisia zake katika taswira ambayo maumbile yake na kipaji chake ndio yanamwongoza kuifikia? Na kwa hakika tofauti za watu katika njia hizi kwa kukata kabisa, zinafuatwa na tofauti za njia zao katika kujieleza kuhusu malengo yao? Kwa hakika nyinyi katika lugha ya Kiarabu mnaweza kudhibiti hesabu za taswira za kimaneno kwa hesabu ya wanayoiongea. Kiasi ambacho hamtompata mwandishi anayeandika kama anavyoandika mwandishi mwingine wakiwa sawa sawa. Wala msemaji ikiwa hivyo hivyo.

Bali bila shaka yoyote nyinyi mnapata kuwa, kwa kila mmoja ana njia yake mahususi kwake yeye tu katika utendaji wake: kwa hiyo mbedui (Mwarabu wa jangwani) si sawa na mwarabu wa mjini, wala mwerevu si kama mpumbavu. Na mcharuko si kama mwenye akili tulivu. Na wala mgonjwa si kama mzima. Na mtu wa chini sana katika mlango huu si mwenye kuweza kupanda hadi juu. Wala wa juu si mwenye kuweza kuteremka mpaka kuwa wa chini kabisa. Bali wawili wanaofanana kimaumbile na kihali za kinafsi, wenye kufanana kimalezi na kielimu. Huenda wakanywa katika kikombe kimoja kisha hawaongei maneno yaliyo na taswira moja.

Sasa iweje mnawaamrisha watu wakuleteeni mfano wa Quran na hali wao hawawezi kuleta maneno yaliyo mfano wa wao kwa wao? Na iweje hilo mlizingatie kuwa ni kushindwa kwao, na ni ushahidi wa utukufu wake. Na huku nyinyi humuhesabau kuwa ni kushindwa kwa kila mtu kuleta muundo mtindo wa mtu mwingine kuwa ni alama ya kuwa muundo mtindo huo ni ufundi wa Mungu tu. Wala sio chumo la yule ambaye imepita katika ulimi wake? Je, mlinganyo huu unakubalika kwetu kuulazimisha kuwa Quran ni maneno ya mtu kama yalivyo maneno mengine ya wanadamu? Isipokuwa yenyewe mtindo muundo umehusika na mwenyewe kama alivyohusika kila mtu na muundo mtindo wake?

Jibu letu kwa msemaji huyu ni kumwambia: sisi hatukubishii katika maneno ya muongeaji. Hakika si vinginevyo, yenyewe ni taswira tu

unayoijaza kwake kwa vipindi vyake na vipawa vyake. Na sio kuwa maumbile haya na kipaji hiki, licha ya kutofautiana kwake kwa watu wengi. Hapana budi vyenyewe vitaacha athari zake za kuonesha tofauti katika umbo la maneno yao. Na wala sio kuwa hayo maumbile na vipaji, hata kama vitashabihiana kwa kundi la watu fulani. Kwa hiyo wakawa na umbo linaloshabihiana katika kauli, kwa hakika hayo katika ujumla wa mambo hayamtoi katika umbo lake moja.

Yote haya tunayakubali na hatuyapingi. Lakini yenyewe hayo hayatudhuru wala hayadhoofishi chochote katika hoja zetu. Hivyo ni kwa kuwa sisi, pale tunapowapa changamoto watu kwa Quran hatuwataki wao watuletee umbo hilo hilo la Quran kimaneno. Sivyo hivyo, hilo ni jambo tusilokuwa na tamaa nalo. Wala hatuwaiti wapinzani walifanye. Kwa hakika tunataka maneno, vyovyote vile utakavyokuwa muundo wake na mtindo wake, yawe mfano ambao muongeaji anayaona kuwa ni mazuri, vyovyote vile yatavyokuwa maumbile yake na hali yake.

Kiasi ambacho, pindi yatakapopimwa na Quran kwa vipimo vya ubora wa kibayani wenye vionjo vitamu au uwe umekaribiana katika vipimo hivyo, hata kama vitakuwa havipo katika umbo lake la kipekee. Jambo tunalowaitia ni kutaka kufanana au kukaribiana katika kiwango hiki ambacho kwacho watu wa umbuji hushindania. Na kwacho wanafanana au wanakaribiana. Na hilo si kupingana na umbo ainishwa lisilo na kutofautiana baina ya muongeaji mmoja na mwingine.

Na kama itakuwa ni vigumu kwako kufahamu ni vipi utakuja na kufanana pamoja na tofauti hizi, basi tunakupigia mfano: Watu wanashinda kufikia lengo lenye mipaka maalum. Nao katika lengo hilo wamejiwekea uga mpana wala hawasongamani wao kwa wao katika hilo. Na mmoja wao haweki mguu wake katika mguu wa mwenzake. Bali kila mmoja amekuwa anaenda katika njia yake maalum, iliyo sambamba na wenzake mwanzoni na mwelekeo. Kisha atakuwa miongoni mwao mwenye kuwa kinara[1], wa pili[2], wa tatu[3] na anayefuata[4]. Na atakuwepo miongoni mwao yule asiye na bahati katika shindano.

[1]Kinara: Mshindi wa kwanza katika shindano la farasi. (Tazama Lisaanu: neno Swalaa. Na fiqihu llughati 202).
[2] Wa pili: mshindi wa pili.
[3] Wa tatu: mshindi wa tatu.
[4] Anayefuata: Mshindi wa nne.

Na watakuwepo miongoni mwao wale walio sawa waliodroo. Na hivyo hivyo, utawaona wao, huku wao wakiwa wametofautiana daraja. Na inatokea baina yao kushabihiana kama inavyotokea baina yao kupitana ubora. Kwa asilimia ya kile alichokikata kila mmoja wao katika njia yake ya kuelekea katika lengo la pamoja.

Na hivyo hivyo washindanao katika uga wa bayani, kila mmoja anakusudia kufikia lengo kwa njia anayoiridhia na kwa namna inayopendwa na nafsi yake. Kisha baina yao kunatokea kufanana au kutofautiana ubora kwa kadri ya kile wanachokitenda miongoni mwa haja za bayani au kile wanachokipunguza miongoni mwake. Hata kama njia zinazopitwa na kila mmoja wao zitatofautiana.

Amka, kwa hiyo wale wanaoitwa kuchuana na Quran, wapo miongoni mwao wenye uwezo sana na washindani wakuu walio magwiji kwa Nabii wa Quran kimaumbile na uwezo wa kukitumia Kiarabu. Au kuna wale ambao wamekamilika zaidi kuliko yeye katika suala hili. Au wao wote wapo chini yake katika nafasi hiyo. Ama wale walio juu yake wataleta kwa mujibu wa uwezo wao kwa kauli nzuri kuliko kauli yake. Na ama wale magwiji wataleta kitu mfano wake au zaidi. Ama wale wengine haitokuwa kubwa kwao kukaribia na kuleta kitu kilicho mfano wake[1] na kitu katika daraja hizi tatu[2] na lau kama hilo lingetimia basi lingekuwa latosha kuijibu hiyo hoja na kuibatilisha hiyo changamoto.

Utasema: bali nachagua uhalisia, nao ni kuwa Warabu licha ya tofauti ya daraja zao katika bayani. Hawajapatapo kupanda na kufikia tabaka la Muhammad kiumbuji. Na ninadai kuwa upungufu huu wa dhati yao ndio umewakalisha na wakaacha kupambana na Quran yake katika maneno yao yote. Na kwa hiyo, huku kushindwa hakuwezi kuwa hoja yenu dhidi ya utukufu wa muundo mtindo wa Quran kama vile ambavyo wenyewe haukuwa hoja kwenu nyinyi dhidi ya Utukufu wa muundo mtindo wa Mtume.

---

[1] Usisahau kile tulichokikubali cha kuwa kuna tofauti baina ya tabaka hili na lile la kabla yake uk 105 wa matini chanzi [Daraazu].

[2] Isipokuwa daraja la kwanza limenyamaziwa katika Quran Tukufu na halikutolewa maelezo yake, kwa sababu ya hima yao na kutosheka kwao na kushindwa kwao na kile kilicho baada yake. [Daraazu].

Tunajibu: Ama ya kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na aali wake alikuwa mfasaha zaidi kwa warabu[1]. Na yeye katika hili alikuwa na ubora sana wa kibayani kwa daraja ya kwanza baina ya Warabu bila ya kuwepo wa kumsonga. Kwa hiyo hatubishani – bali hatujadili – katika hilo. Sio sisi wala yeyote miongoni mwa wale wanaojua Kiarabu vilivyo. Isipokuwa sisi tunaomba ule upeo wa hii tofauti iliyokuwepo baina yao na yeye? Je, kulikuwa na mfano wake aliyekuwa anaafikiana naye katika kuyaendea mambo ya kiada baina ya baadhi ya watu na wengine ndani ya mipaka ya nguvu za kibinadamu. Au lenyewe lilikuwa ni jambo lililo nje ya kawaida lisilo la kimaumbile kwa ujumla wake?

Na ama likiwa kama tulivyozoea, kuwa lenyewe ni mshabaha wa kile kinachokuwa katika hali ya kawaida baina ya Mwenye umbuji na Mwenye

---

[1] Kutoka kwa Abuu Huraira Allah amuwie radhi: **‘‘Kwa hakika Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: nimetumwa nikiwa na maneno machache yenye kukusanya maana kubwa sana. Na nimenusuriwa kwa kuogopesha. Na wakati nilipokuwa nimelala, nilijiona nikipewa funguo za hazina za ardhi zikawekwa mkononi mwangu’’**. Imepokewa na Bukhariyu katika Attasfsiiri 7013. Na katika Al-Iitiswaamu Bikitaabi Wasunnat 7273.

Na Attirmidhiyu amesema, katika kile kilichonukuliwa toka kwake na Bukhariyu 12 / 418: imenifikia kuwa maneno machache yenye maana pana. Na kwamba Allah anakusanya mambo mengi yaliyokuwa yaandikwe katika vitabu vya kabla yake na katika jambo moja na mambo mawili au mfano wa hivyo. أ هـ .

Na Alhaafidhu katika Alfatihu amesema: Na maelezo ya maneno machache yenye maana pana yameshatangulia… na ndani kuna maelezo yake kutoka kwa Azzuhuriyu, na majumuisho yake ni: Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa anaongea kwa ibara fupi na iliyo na maneno machache na yenye maana nyingi. Na asiyekuwa Azzuhuriyu amekata kauli ya kuwa makusudio ya maneno machache yenye maana nyingi ni: Quran. Kwa ushahidi wa kauli yake ‘‘nimetumwa’’. Na Quran ndio upeo katika ufupisho wa matamko na upana wa maana… Na miongoni mwa mifano ya maneno machache yenye maana pana katika hadithi za Mtume:

- Hadithi ya Aisha **‘‘Kila amali/tendo lisilo la amri yetu basi hilo ni la kurejeshwa’’**.
- Na hadithi **‘‘Kila sharti lisilo katika Kitabu cha Allah basi sharti hilo ni batili’’**. Muttafaqun alayhimaa.
- Na hadithi ya Abuu Huraira **‘‘Nitakapokuamrisheni jambo basi liendee kwa kadiri muwezavyo’’.**
- Na hadithi ya Almiqdaamu **‘‘Hakuna chombo cha shari sana alichokijaza binaadamu zaidi ya tumbo lake’’** Imetolewa na wanne na Ibnu Hibbaani na Alhaakimu wameipa daraja la sahihi. أ هـ .

Mwenye kamusi ya Lisaanu Al-Arabi amesema katika 1/679: na katika sifa zake Mtume rehema na amani ziwe juu yake: ni kuwa yeye alikuwa akiongea kwa maneno machache yenye maana nyingi. Yaani alikuwa ni mwingi wa maana na mchache wa matamko. Na katika hadithi: Alikuwa anapenda maneno machache yenye maana pana katika dua. Na hayo ndio ambayo yanakusanya malengo mengi yanayofaa na makusudio sahahi. Au yenye kukusanya sifa za Allah Mtukufu na adabu za kuomba dua. أ هـ .

umbuji zaidi. Na baina ya zuri na zuri zaidi. Basi hakuna shaka kuwa mfano huu wa kuwa matawi ya juu, ndio unaozuia baina yao na baina ya kuleta maneno yaliyo mfano wa maneno yake yote. Basi usingekuwa unazuia baina yao na baina ya kipande kimoja cha maneno yake. Na kama kiasi hiki kidogo kitawashinda kukitekeleza kwa utimilifu basi haikuwa yenye kuwashinda wao kuteremsha katika hayo hadi eneo la karibu.

Zinduka, na hakika sisi tumewalegezea wasitaabike katika kupambana na Quran kwa hili au lile. Na tumewafumbia macho katika kile watakachotuletea kiwe chote au sehemu tu, kingi au kichache, kinacholingana au kinachokaribiana na kinacholingana. Kwa hiyo kushindwa kwako juu ya hayo yote kukawa ni sawa sawa.

Ama ikisemwa kuwa tofauti baina yake, rehema na amani ziwe juu yake na baina ya wanaumbuji wengine zilikuwa kwa upeo wa kukatika muunganiko wao na yeye kwa ujumla. Kwa kuwa yeye ni mahususi baina ya Warabu na baina ya watu wengine kwa maumbile yaliyo nje ya kawaida, hayanasibishwi na maumbile mengine kwa uchache wala kwa wingi kama unavyonasibishwa uwezo wao katika kushindwa au uwezekano katika kutowezekana. Basi hakuna shaka kuwa kauli hiyo ndio ndugu wa kauli ya kuwa miongoni mwa wanadamu wapo ambao si wanadamu. Au hiyo ndio kuungama kuwa yale anayoyaleta mwanadamu huyu si mengine ila ni matendo ya mwanadamu.

Hivyo ni kwa kuwa maumbile ya kiujumla ya mwanadamu ni mamoja. Na tabia za watu ndani yake kuna wanaofanana na kushabihiana katika kitu fulani baada ya kitu fulani, na kwa kimoja baada ya kimoja. Kama hilo halikuwa katika kila zama basi lipo katika zama zilizoendelea. Na kama halikuwa katika kila ujuzi wa maneno basi litakuwa katika baadhi ya ujuzi wake. Na umeshuhudia watu wengi nyoyo zao na akili zao zikifanana, na ndimi zao zikiafikiana na fikra zao na ibara zao kwa muda fulani, na zikikaribiana kwa muda mwingine. Hadi ikakuchanganya na kuona roho inayotembea katika kauli mbili ni roho moja. Na nafsi ya hapa ndio hiyo hiyo ya huko. Na hivyo hivyo tumeshawaona wanafasihi wa kisasa, kuna yule ambaye anaandika kwa muundo mtindo wa Ibnu Almuqaffau na Abdulhamiidi. Na yule yule ambaye anaandika kwa muundo mtindo wa Alhamadhaaniyu na Alkhuwaarizimiyyu na kuendelea.

Na lau kama muundo mtindo wa Quran unatokana na kazi ya mwenye Quran ambaye ni mwanadamu, basi kwa mtu mwingine anayefanana naye kihali, na aliye karibu naye kwa uongofu na utukufu, na aliyeungana naye kiundugu, na aliye zaidi yake kimapokeo na kielimu, kuweza kuleta kitu kilicho mfano wake ingekuwa inastahiki zaidi. Au maswahaba wake ambao Quran imewashukia na wakaisoma na kuihifadhi, wakaonja maana yake na kuitekeleza, na wakafuata hatua zake na kuchota katika vyanzo vyake, basi wao wangekuwa wanastahiki zaidi wawe na muundo unaokaribiana kiasi fulani na muundo wake kama inavyopaswa kuwa kwa hisia za kuigiza na hali ya kuhamisha tabia kutoka katika tabia nyingine. Lakini hakuna lolote katika hayo kilichotokea. Na kwa hakika upeo wa ubora wa kiumbuji kwao wao ulikuwa kama zilivyo juhudi za mwanaumbuji miongoni mwetu: ni kupata kitu atakachokichukua kutoka katika Quran ili kuyaongezea makala yake yapate kuwa ya juu na kuwa na umbo la kupendeza[1].

Bali tunasema, lau kama muundo mtindo wa Quran ungekuwa ni sura ya hayo maumbile ya Kimuhammad basi ingewajibika kwa kipimo cha kile kilichowekwa ndio asilia, miongo mwa tangulizi kiwe kinaafikiana na surah hii katika maneno mengine ya Muhammad, basi yangekuwa yanaafikiana na muundo mtindo wa Quran. Kwa sababu maumbile mamoja hayawi maumbile mawili. Na nafsi moja haiwi nafsi mbili[2] Nasi tunauona muundo

---

[1] Bali na miongoni mwao kulikuwa na washairi mafahali kama vile Labiidu. Yeye ni mmojawapo wa washairi wenye mashairi bora kabisa yaliyopendwa mno katika zama za Jahiliya. Alipoisikia Quran alisilimu na kubadilisha mashairi yake kwa Quran. Na katika habari zake kulikuwa na habari ya kwamba Omari bin Khattwaab alimwandikia gavana wake wa Kuufa: ‘‘Muulize Labiidu na Aghlabu [mshairi mwingine] ni kipi kilichoyatokea mashairi katika Uislmu? Labiidu akasema: Allah amenibadilishia mashairi kwa suratul Baqarah na Aali Imraan. Basi Omari akamzidishia posho yake [posho: ni haki na fungu lililokuwa wakipewa waislamu kutoka katika nyumba ya mali kwa mujibu wa vyeo vyao] hadi ikafikia elfu mbili. (Tabakaatu Fuhuuli Asshi’iri 135, Al-Iswaaba 6 / 4).

[2] Hapa kuna swali, kana kwamba sisi kuna msemaji anatwambia: kwa hakika sio kitu kipya kwa jambo hili la mwanaumbuji kuwa na aina mbili za maneno: ya kwanza anaileta katika hali ya kawaida na kuiachia kabisa kabisa bila ya kuzingatia kuiboresha na kuipamba. Na nyingine anaileta kwa utulivu, akiisheheni hasa hadi anaifanya baina yake na baina ya ile ya kwanza kuwa na umbali mkubwa ambao unaweza kuletewa taswira na msikiaji ya kuwa wenyewe ni kauli ya mtu mwingine licha ya kwamba kauli zote mbili zimetoka kwa msemaji mmoja. Mbona hamjaufanyia kazi mfano huu kwa maneno ya Muhammad na mkayafanya yenyewe ni ya aina ya kwanza na Quran ni ya aina ya pili?

Jibu: kwa hakika kugawanya hivi vigawanyo viwili katika hadithi na Quran ni mgawanyo usioafikiana na uhalisia hata kidogo. Kwani kwa hakika ufunuo mwingi wa Quran ulikuwa unamjia Mtume rehema ana amani ziwe juu yake, ukiwa unahusu mambo ambayo hayajapatapo kuyajua, wala hajawahi kuyafikiria. Bali ulikuwa ukimjia ghafla

papo kwa papo bila ya kutarajia wala kungojea, ikiwa ni jibu la swali la mwenye kuuliza, au fat-wa ya tukio lililotokea. Au kisa cha umma uliopita. Au yasiyokuwa hayo. Na ni mara chache mno ndipo ufunuo ulipokuwa ukimjia baada ya kuwa na shauku na kungoja jambo linalomuwezesha kufanya utulivu. Kama iliyo katika swala la tukio la uzushi na tukio la kubadilishwa kwa kibla. Na kwa hakika tumeona muundo mtindo wake katika hali zake zote mbili, na kutahamaki miundo yake yote ni miundo ya aina moja, na mfumo wake ni mfumo huo huo.

Na hivyo hivyo tunasema, kwa hakika maneno ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake yalikuwa yanatofautiana, kwake yeye na mazingira haya, lakini muundo mtindo wake ni mmoja. Kwa hakika wakati mwingine alikuwa anaongea baada ya kufikiri kwa muda mrefu na kutulia na kushauriana na maswahaba wake kama tulivyoona katika kauli yake katika tukio la uzushi (Uk 23 wa matini chanzi). Na kama tunavyoona katika maneno yake baada ya kushauriana katika maswala ya vita na usuluhishi na yaliyo mfano wake. Na wakati mwingine ni baada ya kusubiri kidogo akisubiri ufunuo kama ilivyo katika kisa cha **‘‘Mtu aliyemjia huko Aljaaraana mnamo mwaka wa nane. Huyo mtu akauliza kuhusu kufanya hija ndogo huku mtu akiwa amejipaka manukato na kuvaa juba. Mtume akamtazama mtu huyo kwa muda kidogo kisha akanyamaza mpaka alipojiwa na ufunuo. Alipomaliza kupokea ufunuo alisema: yu wapi yule muulizaji kuhusu hija ndogo? Basi akaletwa. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Ama manukato uliyoyapaka unapaswa uyaoshe mara tatu. Na ama juba, livue na fanya hija ndogo yako kama unavyofanya katika hija kubwa yako’’**. Imepokewa na Ashaikhaani.

Na tukio lingine alikuwa anaongea maongezi ya kawaida kuhusiana na mambo yasiyo na utata, miongoni mwa mambo yaliyotangulia juu ya maswala ya akili au dini. Na yeye katika yote hayo alikuwa akiyapitisha kwa namna moja kama unavyoona. Hutoweza kuyatofautisha katika muundo mtindo wake baina ya yale yaliyokuwa maana yake ni mazingatio ya rai na yale yaliyokuwa maana yake ni mafundisho ya ufunuo. Wala baina ya yale anayoyaachia kabisa kabisa katika simulizi zake na watu wake na maswahaba wake, na yale ambayo anashereheka nayo katika mijumuiko yenye mikusanyiko mikubwa na siku zenye kushuhudiwa. Basi kwa haya inabainika ubatili wa kile alichokitegemea muulizaji cha kutofautisha baina ya Quran na Hadithi kwa namna hii.

Bali sisi, lau kama tutaenda mbali zaidi ya hayo na kwa ajili ya mjadala tukachukulia kuwa mgawanyo huu ni sahihi, basi hata hivyo kwa msingi wenyewe usingefaa kusimama na kuwa msingi wa jengo la kuonesha utata. Kwa sababu kugawanyika kwa maneno kuwa yapo ya mjazo yaliyo ya kawaida na mengine yaliyopamba kwa utulivu. Basi kusingekuwa kuna kutofautiana kwa njia za maneno kwa Warabu halisia. Hii tofauti ya mbali na ambayo inadhaniwa kuwa yenyewe ni kauli wa wasemaji wawili. Na kwa hakika tofauti hii ilidhihiri tangu pale Warabu halisi wenye uwezo mkubwa wa Kiarabu walipoisha, na kuchipuka machipukizi watoto waliochanganya damu ya uwarabu na mataifa mengine na ambao waliichukua lugha hii kutoka kwa wasiokuwa mama zao. Ndipo lugha yao ikawa wanazungumza lugha isiyo ya lugha ya kile wanachokiandika.

Na hivyo hivyo ndipo wakaweza kwa kila mmoja miongoni mwao kuwa na muundo mitindo miwili inayoachana: mtindo mmojawapo unashuka hadi kufikia daraja la lugha ya mtaani, na mwingine unapanda hadi kufikia lugha ya Kiarabu fasaha inayosifika. Ama Kiarabu halisi kisichochanganyika kwa hakika muundo mtindo wake kwa ujumla haukuwa vingine ila ni ule wa kuzidisha kufikiria, kukadiria na kutulizana ili kufahamu ncha za mazungumzo na kukamilisha lengo. Na hayo hayakuwa yenye kumtoa nje ya muundo mtindo wake, njia yake na lugha yake ya pekee iliyozoeleka na tabia yake, na ambayo kwayo maneno yake yanabubujika. Nayo ni lugha ambayo watu wa fani

mtindo wa ki-Quran ukiwa ni wa namna ya peke yake. Na tunauona muundo mtindo wa ki- Nabii ukiwa ni wa namna ya peke yake, hauendani na Quran katika uga mmoja ila kama vile mbawa za ndege angani haziwezi kupanda kufika mbinguni. Kisha tunaona muundo mtindo wa watu wengine licha ya tofauti zake, wenyewe ukiwa ni wa aina moja ambayo haiwezi kupanda na kufikia paa la dunia. Kwani miongoni mwake kuna miundo inayotambaa

---

miongoni mwetu wanaikusudia na kushughulika nayo baada ya majaribio na kuichakata. Na kama kutakuwepo miongoni mwao kuna wachache, basi kuna yule ambaye anataka kusema maneno yasiyo ya tabia yake na kuyafanyia kazi na ambayo si miongoni mwa ada zake katika maneno yake.

Kwa hakika huku kujilazimisha kwake kutakuwa hakuwezi kumtoa nje ya mipaka ya mapito yake ya kiujumla. Bali atakuwa anaacha ndani ya mazungumzo yake vitu vinavyoashiria roho yake na mapito yake. Ya kwamba maneno yake baada ya huko kujilazimisha hayatokuwa yenye kuzidisha ufasaha na uzuri. Bali yatateremka katika huu mlango kwa kiasi kile kinachohesabiwa na muhesabuji ya kuwa yenyewe yanapanda. Na kutokana na hili Warabu walikuwa wanasifiana kwa jambo linalokuja kimaumbile na si kwa kujilazimisha. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakuwa na chochote miongoni mwa vitu vilivyoko kwa wanaojilazimisha. Bali alikuwa ni mtu anayechukia zaidi kujilazimisha katika maneno ya wengine. Na alikuwa akisema: **‘‘Wameangamia wanaojikalifisha’’**. Imepokewa na Muslimu na Abuu Daudi. Na kujikalifisha katika maneno: ni kuzama kwa kina na kusaka ufasaha wa kupitiliza.

Hebu tazama dhima ya mtu wa ukoo wa Alhadhaliyu pale alipogombana juu ya fidia ya ujauzito kwa kusema: **‘‘Ewe Mtume wa Allah. Vipi nigharamike fidia ya yule ambaye hana kinywaji wala chakula, wala hajatamka, wala hajalia kwa sauti? Basi mtu kama huyo anapuuzwa – yaani damu yake inaenda bure – Basi Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake akasema: Kwa hakika huyu ni miongoni mwa ndugu wa kuhani’’. Kwa ajili ya muundo mtindo wake aliouunda. Imepokewa na Ashaykhani na wengineo. Na katika riwaya nyingine: ‘‘Ameunda kama muundo wa mabedui?’’** na katika nyingine: **Je, ni muundo wa kijahiliya na makuhani wake?**’’ Basi Mtume aliushutumu mtindo huu wa muundo nao ni ule uliokuwa ni kama ule wa makuhani wa kutengeneza na usio wa kimaumbile. Na kwa hiyo maana yake ikawa ni ile ya kufuatana na tamko na sio tamko lifuate maana. [Daraazu].

- Nikasema: Hadithi ya yule mtu aliyemwendea Mtume rehema na amani ziwe juu yake huko Jaaraana: imeshatangulia kuelezwa katika ukurasa wa 88 namba ya pambizo ni mbili katika matini chanzi.

- Hadithi ‘‘Wameangamia wajikalifishao’’: Imepokewa na Muslimu katika Al-Ilimu 7, na Abuu Daudi katika Assunna 4608. Na Ahmad 1/386 wote wameipokea kutoka kwa Abdillahi bin Masuudi.

- Hadithi ya muundo ni Muttafaqun alayhi nayo inatokana na Abuu Huraira: Imepokewa na Bukhari katika Attwibi 5758. Na Muslimu katika Alqasaama 36, na tamko lake kwa wawili hawa ni: ‘‘… **Ndugu wa kuhani’’**. Na kwa Muslimu katika alqasaama 37, 38 kutokana na hadithi ya Almughiira bin Shuuba na tamko lake huko ni: **‘‘… je, ni muundo kama muundo wa Mabedui?’’** Na kwa Abuu Daudi katika Assunnah 7574 kutokana na hadithi ya Ibnu Abbas na tamko lake ni: **‘‘Je, ni muundo wa Kijahiliya na makuhani wake?’’** Nayo kwa Annasaai ipo hivyo hivyo kutoka katika hadithi ya Ibnu Abbas 8/51, 52 na tamko lake ni: **‘‘Je, ni muundo kama muundo wa kijahiliya na ukuhani wake?’’**.

kabisaa, na miongoni mwayo kuna inayokimbia sana. Na uwiano wa muundo mtindo wenye nguvu zaidi katika mitindo ya watu kwa Quran ni kama uwiano wa hivi (vyombo vya duniani[1]) na vile (vyombo vya angani[2]!).

Naam, huenda ukasoma kipande katika maneno ya Mtume na ukatamani kukinyakua na kwenda nacho kama ndege anavyotamani kunyakua na kwenda na kitu. Na huenda ukasoma neno miongoni mwa hekima kisha ukachanganyikiwa usijue: je lenyewe ni miongoni mwa maneno ya Mtume au ni maneno ya maswahaba au ya mataabiina? Hayo ni kwa kuwa kile kilichofanywa na muundo mtindo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake miongoni mwa ubora wake kwa ziada ya ufasaha na usafi wa dibaju na umadhubuti wa mtiririko. Lakini wenyewe ni ubora ambao huenda ukagonga kwa wale wasiobobea katika fani hii. Na huenda vionjo vya mtu vikawa na upungufu hata vikamzuia kuutambua huo ubora. Basi mtu huyo anakimbilia kunukuu kunakomsaidia kupambanua baadhi ya hadithi mar-fuu, hadithi mauquufu na maq-twuu[3].

Ama muundo mtindo wa Quran kwa hakika wenyewe unabeba tabia isiyochanganyika na kitu kingine. Wala haumfanyi mwenye tamaa atamani kuogelea katika himaya yake. Bali yenyewe inaziachia shingo zishoboke kwake kisha inazirejesha zikiwa zimeinamisha videvu vifuani.

Kila anayeona kwa macho mawili au anayesikia kwa masikio mawili, atakapoiweka Quran mbele ya kisichokuwa Quran katika vibakuli viwili vya mizani. Kisha akatazama katika kimojawapo kwa moja ya jicho lake au kwa moja ya sikio lake kwa muundo mtindo wa Quran, na lingine kutazama muundo mtindo wa hadithi za Mtume na miundo mitindo ya watu wengine. Na atakuwa amesharuzukiwa bahati fulani ya mlango wa fahamu wa bayani na uonjo wa kilugha. Kwa hakika, hakuna namna, ataamini pamoja nasi juu ya huu uhakika wa wazi. Nao ni kuwa muundo mtindo wa Quran hausogolewi na kingine chochote miongoni mwa hii miundo mitindo yote. Na tunamhesabu kuwa yeye baada ya kuamini ukweli huu kamwe hatokuwa na nafasi ya mengine ila kuamini kinachofuata … kwa kutolea ushahidi wa uumbaji (Hakuna chochote mfano wake) kwa muumba ﴿**Hakuna chochote**

[1]Vyombo vya usafiri: kilugha ni magari na misafara. Na inawezekana kwa hapa ikakusudiwa vyombo vinavyojulikana kwa sasa.

[2]Vyombo vya angani: nyota, sayari zinazotembea angani.

[3] Hizi ni istilahi za wanazuoni wa hadithi: wakimaanisha kuwa Marufuu ni hadithi iliyonasibishwa na Mtume, Mauqufu ni ile iliyonasibishwa na Swahaba na Maqutwuu ni ile iliyonasibishwa na Taabiina [Daraazu].

**mfano wake. Naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona''** ﴾ . Ash-shuura 11.

## [**Utata Wa Sita: Yule Anayeukubali Muujiza Wa Quran Lakini Hatambui Ni Zipi Siri Zake Na Sababu Zake**]

6 – Kama muulizaji ni miongoni mwa watafutaji wa haki kama tulivyoeleza, na kwa utafiti wake akafikia kujua yale tuliyoyaashiria, na akaona na akasikia, akapima na kuweka mizani, akaonja na kupata ladha basi huyo atatupeleka mbele kwa maneno yake ya mwisho akisema: Ndio, nimeshaachia upinde wa maneno yaliyo mbele yangu na mshale wake nikaurusha porini lakini sikupata chochote ambacho kipo kama Quran kwa kuwa nguzo madhubuti. Kwa hakika niliviendea vyanzo vya maneno na kuonja ladha zake, lakini sikupata ladha tamu mno kama ladha ya Quran. Na sasa nimeamini kuwa yenyewe ipo kama ilivyojielezea ikiwa ni mfumo wa peke yake. na kuwa yenyewe inakaa juu wala haikaliwi juu, na ya kuwa yenyewe inavunja vunja yaliyo chini yake.

Isipokuwa mimi, ingawa nimeshatambua nguvu ya muundo mtindo wa Quran na utamu wa kile nilichokitambua – lakini kile ambacho ninakihisi katika maana hiyo bado yanasitasita[1] kifuani mwangu na siijui vizuri tafsiri yake wala similiki ujuzi wa kujua sababu zake. Na baada ya haya na yale, nafsi yangu bado inaendelea kuwa na mgogoro wa kupata darsa ya vile vitu vya kipekee na ubora ambao umeipa Quran kipaumbele kuliko maneno mengine. Na katika hayo kukawa na siri za muujiza wa kilugha. Je, kuna njia ya kutuwasilishia kitu fulani miongoni mwa vitu hivyo ili nyoyo zetu zitulizane kwa vitu hivyo. Na kuzidi imani juu ya imani yetu?

Tunasema: Ama kwa sasa, tunaapa kwa Allah, kwa hakika wewe umetutaka kitu kikubwa mno. Na umetukalifisha malengo ya mbali mno. Kwa mfano wake wamepita wanazuoni na wanafasihi wa kabla yetu na wa zama zetu. Basi yameongezeka[2] na kuwa na maandiko mengi yaliyoandikwa na kalamu zao. Na hawajazidisha zaidi ya kupigia mifano tu. Na wamekiri kuwa mambo yaliyofichikana kwao katika hiyo Quran ni mengi zaidi kuliko yale waliyoyatambua. Na kwamba kile walichokieleza miongoni mwa

[1] Yanasitasita: yanarejea rejea kifuani. Na kusitasita ni kule maneno kutokuwa na ubainifu.

[2] Kuongezeka: ni kuwa na maandiko mengi.

walivyovitambua ni vichache mno kuliko vile vilivyobanwa na ibara zao. Wala ishara zao hazijayasimamia.

Na sisi tumeshafanya toba baada yao. Je, unadhani kuwa sisi tutapita njia iliyo kinyume na njia yao na kwa hiyo tutadai kuwa, eti sisi kwa haraka haraka tutakuonesha siri za muujiza wa Quran kwa ujumla wake? Sivyo hivyo, wala hatuwezi kudurusu yale yaliyogunduliwa na watu katika pande zake. Sivyo hivyo. Wala kuyang`amua yote yale tunayoyahisi kuwa yenyewe ni miongoni mwa pande hizo. Na hakika si vinginevyo, tunataka kukupa taswira ya baadhi ya hivyo vitu maalumu na ambavyo tumekutana navyo katika kitabu cha Allah kila tunapokisikiliza au tunapokisoma na kukizingatia. Huenda wewe ukawa ni mwenye kupata machache miongoni mwayo, yale ambayo hutoyapata katika vitabu vingi wanavyovizingatia watu. Hata kama watu watakuzidishia katika hivyo aina nyingi. Tunatarajia tutakuzidishia aina mojawapo ya kukutosheleza na kunufaisha.

❋ ❋ ❋

## [**MITAZAMO MIWILI KATIKA GAMBA LA JUU LA MATAMKO YA QURAN:** ]

### [**1- Uzuri Wa Mdundo Katika Mtawanyo Wa Irabu Na Konsonanti Zisizo Na Irabu, Kuvuta Sauti Na Ghuna Na Kuunganisha Na Kunyamaza**]

**Cha kwanza kinachokushtua:**

Cha kwanza kitakachokukuta na kuvutia utambuzi wako kutokana na muundo mtindo wa Quran Tukufu ni ile sifa ya utunzi wake wa sauti kimaumbo na kwa kiini chake.

Hebu mwache msomi wa Quran kwa tajwidi (usomi wa kiufundi na kuzingatia taratibu zake zote) aisome Quran kwa kuisoma vizuri haki ya kuisoma vizuri, akishusha pumzi zake katika maporomoko ya Quran. Na sio mwenye kuteremka na Quran katika miporomoko ya pumzi za msomaji. Kisha jitenge sehemu ya mbali ambako huko hutosikia kengere za herufi za eneo hilo, lakini utasikia irabu zake na konsonanti zake, kuvuta[1] kwake na

[1] Kuvuta: ni wingi wa neno madda nalo ni kurefusha sauti ya herufi inayovutwa. Na herufi za kuvutwa ni: alifu ikiwa na fatha herufi ya kabla yake, wawu ikiwa inadhwamma herufi ya kabla yake, na yaau ikiwa ina kasra herufi ya kabla yake.

ghuna[1] zake, na kuunganisha kwake na kunyamaza kwake. Kisha usikivu wako uweke katika mkusanyiko huu wa sauti huku ukiwa umeshajitoa kabisa kabisa katika mambo mengine, na mambo ya kipuuzi umeyaacha hewani. Kwa hakika utaipata nafsi yako ikiwa mbele ya kiburudisho kigeni na cha ajabu, na ambacho hutokipata katika maneno mengine hata kama utajitoa kama kujitoa huku, na huyo msomaji akasoma vizuri kama alivyosoma hapa.

Kwa hakika utakuta muunganiko na kukubaliana kunakoburudisha usikivu wako kama vile unavyoburudika na mziki na mashairi. Ya kwamba yenyewe si naghma za muziki wala si mizani ya kishairi. Na kwa hakika utapata kitu kingine usichokipata katika miziki wala mashairi. Hayo ni kwa kuwa wewe unasikiliza kasida ya ushairi na kutahamaki unaikuta yenyewe inaungana mizani yake beti kwa beti, mstari kwa mstari. Na unasikia kipande cha muziki[2] na kutahamaki chenyewe kinafanana na matamanio yake na

---

[1] Ghuna: ni wingi wa neno ghunnatu nalo ni kupitishwa kwa maneno katika tundu za pua na kutoka kwa sauti mororo.

[2] Ishara hii ya muziki huenda mtunzi Allah amrehemu ameitaja ili kuliweka karibu jambo hilo, na kuweka wazi makusudio ya kengele na naghama za sauti zenye kujisasisha katika Quran. Ama muziki, hukumu yake ya kisheria ni maarufu kikamilifu kwa watu wenye elimu bali na kwa wanafunzi bali na hata kwa watu wa kawaida wengi pia. Na tazama hukumu ya Uislamu kuhusu muziki:

- Abdulrahmaan bin Ghanam Al-Ashaariyu: Amenisimulia Abuu Aamiri au Abuu Maaliki Al-Ashaariyu – naapa kwa Allah hajaniongopea – alimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisema: ‘‘**Katika umma wangu kutakuwa na watu wanajihalalishia alhiri [tupu, na makusudio yake ni: uzinzi] na Hariri, pombe na maazifu (muziki).**’’ Imepokewa na Bukhari ikiwa Taaliqan katika Al-Ashribat 5590.
- Na Alhaafidhu Ibnu Hajari ameshereheshа katika Fatihu Albaariy 10/57 neno Maazifu ni wingi wa neno Maazafatu, nalo ni ala/vyombo za mapumbao, na katika Sahihu Aljawhariyu kwa hakika hizo ni ala za mapumbao. Na imesemwa hizo ni sauti za mapumbao أ هـ.
- Na Imamu Ibnu Alqayyimu katika Ighaathati Allahfaani 1/260 na yaliyo baada yake amesema: Na namna ya kutolea ushahidi hadithi hii ni kuwa: ala za mapumbao ni ala zote za kujipumbazia. Na hakuna kutofautiana baina ya wataalamu wa lugha katika hilo. Na kama zingekuwa ni halali basi zisingeshutumiwa kuzihalalisha. Na zisingeambatanishwa na kuhalisha pombe, Hariri na tupu za haramu أ هـ [kwa muhtasari na mabadiliko kidogo].

- Nimesema: na hadithi hii ndio yenye nguvu zaidi katika hadithi zilizokuja katika kuthibitisha hukumu ya kuharamisha muziki na ala zake kwa wazi wazi. Kwani Mtume rehema na amani ziwe juu yake pale anaposema ‘‘wanahalalisha’’ basi hii ni hukumu ya wazi ya kuwa jambo hili ni haramu kikamilifu. Kisha kuna ushahidi wa kuambatanishwa kwa ala za mapumbao pamoja na pombe, Hariri na uzinzi, hapo inabainika hukumu kikamilifu kwa yule ambaye hafanyi kibri wala hatakabari.

Na yule anayezitazama hadithi nyingine zilizokuja zilizo mfano wa ile hadithi ya Umraanu bin Huswayni, ya kwamba Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: ‘‘**Katika umma huu kutakuwa na kudidimizwa ardhini, kubadilishwa**

**kwa kufutwa na kusingiziana. Mtu mmoja akasema: Ewe Mtume wa Allah, ni lini yatatokea hayo? Akasema: Pale itakapodhihiri Alqiinaatu [waimabaji wa kike] na ala za muziki na unywaji wa mipombe''.** Imepokewa na Attirmidhiyu katika Alfitani 2212. Na Albani akaipa daraja ya sahihi 2203. Na Abdulqaadir Al-Arnaauutwi ameipa daraja ya Hassan katika Jaamii Al-Uswuuli 7933. UK 129

- Kwa hakika Allah Mtukufu Aliyetukuka, Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake, maswahaba, matabiina na maimamu wameuelezea huu muziki kwa sifa nyingi na zote ni mbaya zenye kuwakimbiza watu wenye Imani:

- Upuuzi na maneno ya upuuzi: ﴿ **Na katika watu wapo wanaokhitari maneno ya upuuzi ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu, pasipo wao kujua lolote, na wanaicheza shere hiyo njia ya Mwenyezi Mungu. Basi hao watapata adhabu ifedheheshayo** ﴾. Luqman 6. Ibnu Abbas, Ibnu Masuudi, Mujaahidu na Ikrimah wamesema: hizo ni nyimbo.
- Uongo na upuuzi: ﴿ **Na wale ambao hawashuhudii hasa hasa za uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima yao** ﴾. Al-Furqan 72.
- Batili: Fat-wa ya Ibnu Abbas na Alqaasimu Ibnu Muhammad.
- Miluzi na kupiga makofi: ﴿ **Na haikuwa ibada yao (hao makafiri) hapo kwenye hiyo nyumba tukufu ila kupiga miunzi (milunzi) na kupiga makofi...** ﴾ Ibnu Abbas, Ibnu Omar, Atwiya, Mujaahid, Dhwahaki, Alhassan na Qatada wamesema: (Miluzi: ni mbinja, na kupiga makofi: kukutanisha viganja ili kutoa sauti).
- Ruqiya ya uzinzi [yaani kichocho cha uzinzi]: kama alivyosema Yazidi bin Alwaliidi na wengine.
- Maoteo ya unafiki: kama alivyosema Ibnu Masuudi (Nyimbo zinaotesha unafiki moyoni kama maji yanavyootesha mimea). Na Ibnu Alqayyimu amesema: kamwe Quran na nyimbo havikai pamoja katika moyo. Kwa kuwa baina yao kuna kupingana. Kwa hakika Quran inakataza kufuata matamanio ya nafsi, na inaamrisha kujistiri, kujiepusha na. matamanio ya nafsi na visababishi vya upotofu. Na inakataza kufuata hatua za shetani. Na nyimbo zinaamrisha kinyume cha hayo yote. Zenyewe zinayaona hayo ni mazuri na kuzitia nafsi mihemko ya kufuata matamanio ya upotofu. Na kuamsha vilivyojificha katika nafsi na kumtaabisha mwenye kujizuia na hayo matamanio, na kumchagiza aliendee kila ovu… Na vile vile, miongoni mwa alama za unafiki: ni uchache wa kumtaja Allah, uvivu wakati wa kusimamisha swala, kuswali kwa kudonoa. Ni mara chache sana kukuta mtu aliyefitinishwa kwa nyimbo ila naye atakuwa na sifa hizi.
- Ni kisomo cha shetani: imepokewa kutoka kwa Abii Umaamah na Qatada.
- Sauti ya mpumbavu na sauti ya muovu: haya ni majina yaliyotolewa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika hadithi ya Attirmidhiy **''Kwa hakika nimekata sauti za aina mbili za wapumbavu na waovu: sauti ya wakati wa kuimba: ni upuuzi na mchezo na zumari za shetani. Na sauti ya wakati wa msiba ni: kunyofoa nyuso, na kupasua nguo na kupiga kelele''.** Imepokewa na Attirmidhiyyu katika Aljanaaizi 1005 kwa mfano wake. Na Albaaniyu ameipa daraja ya Hasani katika Swahiihu Attirmidhiyu 804.
- Sauti ya shetani: katika kauli ya Allah Mtukufu kwa shetani: ﴿ **Akasema: ''Ondoka! (Ondokelea mbali)! Atakayekufuata miongoni mwao, basi hakika Jahannam ndiyo malipo yenu, malipo kamili. Na wavute uwawezao miongoni mwao kwa sauti yako, na uwakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali yao na watoto wao, na waahidi (ahadi za uwongo).'' Lakini shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu (kwani ana lake jambo).** ﴾. Israa 63 – 64. Ibnu Abbas amesema: ﴿**Kwa sauti yako** ﴾**:** Kila mwenye

kinaenda mwendo wa kukaribiana. Na usikivu wako hautapitiwa na muda ila yatayabugia. Na kwa maumbile yako utayachoka endapo yatarudiwa rudiwa kwako kwa mirindimo ya aina moja. Wakati ambapo wewe kwa upande wa

---

kuwaita watu kwenye maasi. Na Ibnu Alqayyimu amesema: Na miongoni mwa mambo yanayojulikana ni kwamba, nyimbo ni miongoni mwa visababishi vikubwa vya maaswi. Na kutoka kwa Mujaahidi amesema: na sauti yake ni nyimbo na mambo ya batili na zumari.

- Zumari za shetani: Kutoka katika hadithi ya Abuu Bakar katika Swahihi mbili pale alipoingia kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kwa Bibi Aisha kuna wajakazi wawili wakiimba kwa nyimbo za Buaathi [yaani mashairi yaliyokuwa yakiimbwa katika vita vya Buaathi baina ya Ausi na Khazraji katika zama za Jahiliya] Abuu Bakar akasema: Zumari za shetani zipo kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake…
- Wimbo: Katika kauli yake Mtukufu ﴿**Je, Mnaistaajabu Hadithi hii? Na mnacheka; wala hamlii? Na nyinyi saamiduna – mmeghafilika tu!** ﴾**.** Ibnu Abbas amesema: (saamiduna – mmeghafilika: ni nyimbo kwa lugha ya Kihimiyari). Na kutoka kwa Abuu Ubaida na Ikrima kama hivyo.

- Na maneno ya wanazuoni wanne na wenzao kuhusiana na nyimbo na miziki zimetujia kwa njia ya kupokewa na wengi na zenyewe ni maarufu:
  - a- Madhehebu ya Hanafiyu: Nayo ndio madhehebu makali zaidi katika swala hili. Abuu Hanifa alikuwa anachukia nyimbo na kuzifanya zenyewe ni miongoni mwa madhambi. Na hivyo hivyo madhehebu ya watu wa Kuufa, kwa mfano: Sufiani, Hammaadu, Ibrahimu, Shaabiyu na wengineo, hakuna kutofautiana baina yao katika hilo. Na hivyo hivyo watu wa Basra nao hawana Khitilafu baina yao katika kukataza nyimbo. Na watu wa Abuu Hanifa wameeleza wazi wazi uharamu wa kusikiliza mapumbao yote… na wakaweka wazi kuwa hayo ni maaswi yanayompasa mtu kuwa fasiki na kukataliwa ushahidi wake.
  - b- Madhehebu ya Maalikiyu: Imamu Maaliki alikataza nyimbo na kuzisikiliza hadi ikafikia ya kuwa yeye ametoa fat-wa kuwa: Pindi atakaponunua – yaani mwanamume kumnunua – mjakazi na akamkuta ni mwimbaji basi mtu huyo ana haki ya kumrudisha kwa kasoro hiyo). Na pale alipoulizwa kuhusu nyimbo alisema: (kwa hakika hayo kwetu sisi wanayafanya mafasiki).
  - c- Madhehebu ya Kishaafiiyu: Shaafiiyu katika kitabu chake Adabu Alqadhwaai amesema: (Kwa hakika nyimbo ni upuuzi na chukizo. Zinafanana na batili na mambo ya muhali. Na atakayezifanya kwa wingi basi mtu huyo ni mpumbavu na ushahidi wake unakataliwa). Na watu wake walio wajuzi wa madhehebu yake wamesema wazi wazi kuwa nyimbo ni haramu, mfano wao ni Abuu Is-Haqa katika Attanbiihi: (Wala haiswihi – yaani kukodisha – kwa manufaa ya haramu, kama nyimbo, zumari na kubeba pombe) na katika hilo hakujatajwa tofauti yoyote. Na hivyo hivyo Annawawiyu katika Arrawdhwati: (Sehemu ya Pili: Kuimba kwa kutumia baadhi ya ala za mziki, miongoni mwazo ni nembo za wanywa pombe nazo zinaburudisha kama kigoma/tari/dufu, gita, matuazi, ala nyingine za muziki na kano: ni haramu kuvitumia na kuvisikiliza).
  - d- Madhehebu ya Hanbaliiy: Imamu Ahmad amesema: (Nyimbo zinaotesha unafiki moyoni. Na hazinipendezi). Na ameweka andiko la kuzivunja ala za mapumbao kama kigoma/tari na nyinginezo endapo ataziona zikifunuliwa wazi na akaweza kuzivunja.

Quran, milele utaikuta ikiwa na mirindimo ya aina tofauti tofauti inayojisasisha. Inahama kutoka katika Asbabu kwenda Autaadi hadi Fawaaswilu[1]. Katika maweko tofauti tofauti, kila moja linachukua mshipa miongoni mwa mishipa ya moyo wako kwa kiwango cha sawa sawa. Na licha ya wingi wa kurejea rejea kwake, hautopata uchungu wala kuchoka. Bali hutoacha kutaka upate ziada kutoka kwake.

Uzuri huu wa mirindimo katika lugha ya Quran haufichiki kwa yeyote yule anayeisikiliza Quran. Hata kwa wale ambao hawaijui lugha ya Kiarabu. Basi unafichikanaje kwa Warabu wenyewe?

Na utawaona watu wanajiuliza: ***Kwa nini Warabu walipokuwa wakigombana kuhusu Quran, basi waliilinganisha baina yake na mashairi kwa kukanusha au kuthibitisha, wala hawajaiwasilisha kwa maneno yao mengine miongoni mwa hotuba na mengineyo?***

Na wewe, je kwa hapa limeshakubainikia jibu. Na umeongoka kujua siri waliyoitambua Warabu na ambayo wanaojifanya warabu hawakuitambua?

Kwa hakika kitu cha kwanza kilichoonwa kuwa ni kizuri na hayo masikio ya Warabu katika mfumo wa Quran nacho ni huo mfumo wa sauti wenye ubunifu wa hali ya juu, mfumo ambao umegawanyika katika irabu na konsonati zisizo na irabu, katika migawanyo ya aina mbali mbali inayosasisha uchangamfu wa msikilizaji pale anapoisikiliza. Na imegawanywa kwa migawanyo ya herufi za kuvuta na za ghuna kwa mgawanyo wa vipimo vya uadilifu vinavyosaidia kuirejesha sauti katika vipimio hivyo na kuongoza nyoyo hatua baada ya hatua mpaka kufikia kitenganishi kingine na huko anapata raha yake kuu.

Na mfano huu wa mfumo wa sauti, Warabu walikuwa wanakusudia kuufanya katika mashairi yao, basi wakaenda ndani yake hadi wakafikia upeo wa kufanya fujo katika kupamba kisha wakafikia upeo wa kuboeka

---

[1] Je, wewe unahitaji kujua istilahi za vitu hivi? Hizi ni istilahi za ushairi wa Kiarabu nazo ni kuwa herufi yenye Irabu ikafuatiwa na isiyokuwa na irabu hizo mbili huitwa (sababu khafiifu). Na herufi mbili zenye irabu zikafuatiwa na isiyo na irabu ndio (watadu majumuu). Na herufi mbili zenye irabu na hazifuatwi na isiyo na irabu ndio (sababu thaqiilu) na herufi mbili zenye irabu na katikati yao kuna herufi isiyo na irabu ndio (watadu mafuruuqu) na herufi tatu zenye irabu na mwisho wake kuna herufi isiyo na irabu ndio (faaswila swaghiiratu). Na herufi nne zenye irabu na zikafuatiwa na herufi isiyo na irabu ndio (faaswila kabiiratu) [Daraazu].

(kuchoshwa) katika kukariri. Kwa hakika hilo lilikuwa kwa mashairi tu wala hilo halikuwa likiwezekana kwa wepesi katika lugha zao za mjazo. Hiyo ni sawa sawa kwa maneno yaliyoachiliwa na yenye vina. Bali katika maneno yao mazuri mno ya mjazo kulikuwa kunatokea dosari zinazozuia utiririkaji wa mipandano yake na wala haiwezekani pamoja nayo kuisoma vizuri ila kwa kuingiza kitu katika maneno hayo au kwa kufuta kitu.

Kwa hiyo, hakuna ajabu kuona kuwa majina ya chini kupewa Quran katika taswaira za Warabu ni kuwa yenyewe ni mashairi. Kwa sababu waliyakuta katika mirindimo yake kuna mitikisiko ambayo hutoikuta ila katika mashairi. Na si ajabu warabu wakazirejea nafsi zao na kusema: haya si mashairi; kwa kuwa yenyewe – kama alivyosema Alwaliid[1] – hayapo katika bahari[2] za kishairi wala katika mahsairi ya rajazi wala ya kasida. Kisha hakuna ajabu kama tahayari hii itarejeshwa katika aina fulani hivi ya uchawi; kwa kuwa yenyewe baina ya ncha zake mbili imekusanya kuachilia na kuzuia ikiwa katika mpaka wa ukati na kati: kwa hiyo wenyewe ukawa katika upande wa lugha ya mjazo ina utukufu wake na utamu wake, na kwa upande wa ushairi ina uzuri wake na starehe zake.

**[ 2 – Uzuri Wa Muunganiko Katika Kuziandalia Njia Herufi Zake Na Kuziunda Katika Mikusanyiko Yenye Muunganiko Mzuri Ulio Tofauti Tofauti]**

Kama utalisogeza sikio lako kidogo kidogo, na usikivu wako ukagongwa na kiini cha herufi zake zikitoka katika matokeo yake sahihi. Basi yatakushtua kwa ladha nyingine katika mfumo wa herufi hizo na njia zake na mpangilio wa maweko yake yaliyo baina yake: hii inagonga na ile inapiga filimbi, na ya tatu inanong`ona na ya nne inadhihirika, na nyingine inaterezekewa na pumzi. Na nyingine pumzi inazuiwa kwake, na kuendelea. Kwa hiyo utaona uzuri wa kilugha ukiwakilishwa mbele yako katika mikusanyiko mbalimbali yenye kuungana[3]: Si kukariri kariri[4] wala

---

[1] Neno la Alwaliid katika hilo limeshatangulia katika (Uk 116 wa matini chanzi) [Daraazu].
[2] Bahari: mizani.
[3] Anayezijua sifa bainifu za herufi na matokeo yake, kwa maana hii basi anazidi kuwa na elimu. Na kama ukipenda rejea katika kile kilichoandikwa na mwanafasihi Arrafiiyu kuhusiana na upande huu katika kitabu chake kilichopewa jina la (Muujiza wa Quran). Kwa hakika humo amerefusha na kufanya vizuri mno. [Daraazu].
[4] Kukariri kariri: ni kurudia kitu mara baada nyingine.

utharthara[1] wala rakhawatu[2] wala muuadhwalati[3]. Wala kutojuana wala kukimbiana[4].

Na hivyo hivyo utaona yenyewe ni maneno si ya watu wa mjini yaliyodhaifu wala si ya watu wa majangwani yanayokwaruza. Bali utayaona yakiwa yamechanganyika ndani yake na umadhubuti wa kuanzia na ukubwa wa umororo wake wa kimjini na kutiririka kwake. Kana kwamba yenyewe ni juisi ya lugha mbili na utamu wa mtiririko wao. Au yenyewe ni kana kwamba nukta ya kuunganika baina ya makabila. Kwake yeye vinakutana vionjo vyao. Na juu yake nyoyo zao zinaungana.

Na miongoni mwa haya mambo maalumu na ambayo mbele yake linaundwa gamba la juu la uzuri wa Quran. Na katika gamba hili hakuna jambo ila kama jambo la kome zinazohifadhi lulu zenye thamani ghali. Kwa hakika Yeye ambaye uwezo wake umetukuka amepitisha sunna yake katika mfumo wa ulimwengu huu, kufunika utukufu wa siri zake kwa pazia ambazo hazijaepukana na raha na uzuri. Ili hilo liwe ni miongoni mwa sababu za kuzilinda na kuzibakisha katika kushindana kwa wenye kushindana katika hizo, na kupupia kwao juu ya hilo. Hebu tazama namna alivyojaalia kichocheo cha kula na kiunganisho cha mapenzi kikiwa ndio nguzo ya kubakia mwanadamu mmoja na kundi lake.

Na hivyo hivyo, pale neno lake lilipotangulia kutulindia elimu bora kabisa iliyowekwa katika kitabu hiki kitukufu. Hekima yake imehukumu kukichagulia kinga, inayowafanya watu wakipende  kwa utamu wake, na kwa kuwavuta kwa uzuri wake, na chenyewe kiwe katika nafasi kama nafasi ya (kumwimbia ngamia ili aongeze kasi) inayohamasisha nyoyo kutembea juu yake. Na kurahisisha kwake tabu za safari katika kutafuta ukamilifu wake. Hakuna shaka kimechaguliwa kwa ulimi huu wa Kiarabu cha wazi, hiyo ndio kigezo kitamu na kizuri. Na kwa ajili hiyo sauti ya Quran itabakia milele, katika midomo ya watu na masikio yao, muda wa kuwa kwao wao upo mlango wa fahamu wa kuonja na mlango wa fahamu wa kusikia. Hata kama wengi wao hawatakuwa na nyoyo za kuifahamu kwa uhakika wa siri yake. Na kuondoka nazo katika kina chake cha mbali. ﴿**Hakika sisi ndio**

---

[1] Utharthara: ni maneno mengi katika kusitasita na kuchanganya.
[2] Rakhawa: ni kulegeza na kulainisha na kutamka herufi mbali mbali.
[3] Muadhwala: ni kuyatia mazonge maneno na kuyafuatanisha baadhi kwa baadhi.
[4] Kukimbiana: nako ni kukimbiana baina ya herufi. Kama katika herufi ambazo matokeo yake yanakaribiana kikamilifu. Mfano wa neno (الهُعْخُعُ) Alhu`khu`u.

**tulioteremsha mauidha haya (hii Quran); na hakika sisi ndio tutakayoyalinda ﴿.** Al-Hijr 9.

Je, ushajua kuwa Quran inakusanya uzuri wa utukufu na wa ajabu? Na je, umeshajua kuwa uzuri huu ndio ambao nguvu ya Allah imehifadhi Quran isipotee na kutoweka kwa kupitia uzuri huo?

Sasa tambua kuwa huu uajabu ulikuwa ni nguvu nyingine iliyosimamisha hoja ya Quran katika kutoa changamoto na muujiza. Na imejikinga kwake dhidi ya mikono ya wapinzani na wabadilishaji. Na kwamba uzuri huo peke yake usingetosha katika kuzuia mikono yao dhidi ya Quran. Bali wenyewe ulistahiki zaidi kuwavutia. Hilo ni kwa kuwa watu – kama anavyosema Albaaqilaaniy[1] - wanapokiona kitu ni kizuri hukifuata na kushindana kukiiga kwa sababu ya kichocheo cha maumbile[2]. Na hivyo hivyo tumewaona watu wa ufundi huu wakifuatana baadhi yao kwa wengine katika kile wanachokiona kuwa chenyewe ni kizuri miongoi mwa miundo mitindo.

Na huenda watu wanaofuata miongoni mwao wakatambua ushindi wa aliyetangulia au amemzidishia kwake. Kama vile Ibnu Al-Amiidi alivyofanya katika muundo mtindo wa Aljaahidhwi. Na kama wanavyofanya waadishi na watoa hotuba wa leo hii katika kuigana wao kwa wao. Na miundo mitindo ya watu, licha ya tofauti za njia zao katika lugha za mjazo na ushairi, isipokuwa yenyewe haikuwa vingine ila ni vyanzo vinavyoweza kufikiwa, mapito ya njia iliyoandaliwa, huchukuliwa kwa kujifunza. Na ndimi na kalamu huridhishwa katika hilo kwa kufanyiwa mazoezi, kama ulivyo ufundi mwingine.

Ni kipi hasa kilichowazuia watu wasitumbukie katika muundo mtindo wa Quran kwa ndimi zao na kalamu zao, hali ya kuwa wao ni watu wa shur`u[3] katika kuziona nzuri njia zake. Na wengi wao wanataka kuzibatilisha hoja zake?

Hilo halikuwa vingine isipokuwa ndani yake kuna kizuizi cha kimaumbile kilichozuia na kinaendelea kuzuia mikono yao isiifikie. Na hakuna shaka kuwa kizuizi cha kwanza utakachokutana nacho miongoni mwa vizuizi hivi vya kimaumbile katika vile tulivyokuletea taswira yake,

---

[1] Katika kitabu chake (Muujiza wa Quran) [Daraazu].
[2] Maumbile: walivyoumbwa na tabia zao.
[3] Shur`u: sawa sawa.

nayo ni miongoni mwa ajabu ya utunzi wake katika jengo lake na kile ilichokifanya katika kuzipangilia herufi zake, maneno yake, sentensi zake na aya zake. Miongoni mwa mfumo wenye sifa ya peke yake, na tabia maalumu kwake tu. Imetoka nje ya maumbo ya kila mfumo walioutumia watu au wanaoutumia. Hakuna shaka, hawajapata mfano wake wa kuulinganisha nayo, wala hawajapata njia ya kupitia kwenda kuitiisha njia yake.

Na alama ya hilo ni kuwa lau kama mtu mmoja angejaribu kuingiza kitu miongoni mwa maneno ya watu ndani ya Quran, awe miongoni mwa watu wa zamani au wa sasa, awe miongoni mwa wenye hekima au wanaumbuji, au manabii na mitume. Basi hilo lingeharibu namna ya Quran katika mdomo wa kila msomaji. Na hilo lingeufanya mfumo wake utikisike katika sikio la kila mwenye kusikia. Na kwa hiyo, chenye kuingia kingetangaza chenyewe kwamba yeye ni kitu kilichoingizwa si asili. Na Quran yenyewe ingekikataa kama mipulizo ya muhunzi inavyokataa mataka ya chuma ﴿**… bila shaka hicho ni kitabu kihishimiwacho. Haitafikia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa; na Mwenye hikima, ahimidiwaye** ﴾**.** Haa Mym Sadah 41 – 42.

* * *

### [**Mitazamo Juu Ya Bayani Ya Quran Na Sifa Zake Bainifu Ilizojipambanua Nazo Na Ambazo Hazipo Katika Maneno Mengine**]

Ikiwa wewe haujapumbazwa na uzuri wa gamba na kuacha kufikiria yale yaliyo chini yake miongoni mwa hazina zilizofichwa. Na hujazuiwa na uzuri wa pazia ukaacha kutazama yale yaliyo nyuma ya pazia miongoni mwa siri zenye kulindwa. Bali umepasua[1] gamba na kukipata kiini[2] chake. Na ukafunua kombe na kuweka wazi vito vyake, ukauvuka huu mfumo wa matamshi na kwenda katika mfumo ule wa kimaana. Wenyewe unakuonesha kile ambacho chenyewe ni kinapendeza na kuvutia sana. Na kutoka kwake ukapata kile ambacho ni kitamu mno na kina ubunifu mkubwa.

Hapa hatutaki kukusimulia kuhusu maana ya Quran na kile kilichomo miongoni mwa elimu zilizo nje ya uwezo wa mwanadamu. Kwa hakika habari hii, in shaa Allah Taala, itakuja katika sehemu yake inayohusu utafiti

[1] Hapa kupasua yaani: kufunua.
[2] Kiini: Moyo.

juu ya muujiza wa (kisayansi). Ama mazungumzo yetu kama unavyoyaona, yanaendelea kuhusu muujiza wa (kilugha), na hakika si vinginevyo lugha ni matamko.

Ingawa hayo matamko (wakati mwingine) huangaliwa kwa upande wa kuwa yenyewe ni majengo ya kisauti na vijenzi vyake ni herufi na sura yake ni irabu na konsonati zisizo na irabu bila ya kuangalia maana yake. Na upande huu tumeshapitisha kauli kuyahusu hivi punde. Na (wakati mwingine), tunayatazama matamko kama vile yenyewe ndio nyenzo ya kutuo taswira ya maana na kuihamisha kutoka kwa mzungumzaji hadi kwa mzungumziwa. Na upande huu ndio upande ambao tutauchakata sasa hivi. Na hapana shaka kuwa katika pande mbili hizi upande huu ndio mkuu zaidi kitaathira kuhusu muujiza wa kilugha tunaoushughulikia, kwani lugha zinatofautiana sana ubora katika viwango vya bayani, kuliko zinavyotofautiana ubora katika kuwa kwake yenyewe ni kengele na naghama.

Ama kutazama katika maana ya Quran kwa upande wa kile ambacho kipo ndani yake miongoni mwa elimu za ajabu. Basi hiyo ni hatua nyingine na mtazamo ulio nje ya utafiti wa kilugha kiujumla wake. Kwani ubora wa kibayani, kwa hakika wenyewe unategemea katika kuweka taswira za kina na kupatia kueleza maana kama ilivyo. Sawa sawa kwake, hiyo maana iwe ni miongoni mwa kile kinachojulikana na akili za watu au kisiwe hivyo. Bali ni sawa sawa hiyo maana iwe ya hakika au ya taswira. Na iwe uongofu au upotofu[1]. Hii ni kinyume na ubora wa kielimu, kwa hakika wenyewe unarejea katika maana katika dhati yake kwa sura yoyote itakayoitoa. Na kwa lugha yoyote itayoieleza.

Ndio, huenda lugha zikatofautiana katika kutekeleza haki ya maana. Kwa hiyo maelezo mazuri yanakuwa ni miongoni mwa yale yanayoongeza kima chake kielimu. Lakini kinachotazamwa hapa ni katika kima cha bayani na si kima cha kibainishwa. Kwa hiyo usituharakishe kwa mtazamo huo wa kielimu, subiri mpaka tumalize mtazamo huu wa kilugha.

Na sasa na tuanze kuelezea kwetu kuhusu baadhi ya sifa za kipekee za Quran kibayani. Na tuzipange kwa madaraja manne:

---

[1] Na kwa ajili hiyo simulizi za Quran kuwahusu watu wa batili zimekuwa ni kauli zisizo na upungufu katika balagha yake na kuwa kinyume na maneno yake mengine. Kwa sababu zenyewe zinaelezea yale yaliyo katika nafsi zao kwa njia ya utimilifu zaidi. [Daraazu].

## 1- Quran ikiwa katika vipande vipande[1] miongoni mwake.

[1] Kwa hilo tunakusudia yale yanayopelekea katika maana timilifu kama yale ambayo kikawaida yanapelekea katika baadhi ya aya. Huenda yakatekeleza katika aya ndefu au sura fupi. Nayo ndio upeo wa chini kabisa ulioteremshwa kama changamoto ya mwisho pale aliposema: ﴿**Basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake** ﴾**.** Al Baqarah 23. Na haikusema sura miongoni mwa sura zake zile ndefu au za kati na kati. Bali imeacha huru bila mipaka. Kwa hiyo hilo linajumuisha sura fupi ambazo nyingi zake ziliteremshwa Makka kabla ya kuteremka kwa changamoto hii ya mwisho. Yaani imo hata suratul Asr na Kawthar.

Na baadhi ya watu – hivyo hivyo Al-Aluusiyu katika utangulizi wa kitabu chake Ruuhul Maaniy amenukuu kutoka kwa msemaji aiyejulikana – anayepita mapito ya kuwa changamoto haikuweka kwa kuleta sura tu kwa kuachilia. Bali kwa sura (itakayofikia daraja ya umbuji katika vigezo vya bayani) kana kwamba yeye ameona kuwa daraja hii haibainiki katika kiwango cha aya tatu kwa mfano. Na hili, hata kama halitokuwa linatia dosari katika muujiza wa Quran, lakini halibatilishi hoja yake – kwani, inatosha kuthibiti kwa muujiza wake hata kama ingetakiwa kiasi cha suratul Al-Baqarah au suratul Yunus, au suratu Hud, au surat Israa. Au suratul Twuur. Na hizo ndizo sura ambazo kumekuja kutajwa hii changamoto – isipokuwa sisi tunachukulia kuwa, mwenye kauli hii pale alipopita mapito haya, kwa hakika alidhani dhana ambayo hakuwa na yakini nayo. Na aliweka mbali mno suala la kuwa hizi sura fupi nazo ni muujiza katika bayani yake. Kwa sababu yeye hakutambua mambo ya ajabu katika mfumo wake na hivyo hakufahamu vilivyo siri ya huu muujiza katika sura hizo. Lakini, hilo limefanywa hoja kwa uchache wa bidhaa zake katika ufundi huu. Na hakujaalia ujinga wake juu ya kima chake kuwa hoja ya Quran kutokuwa muujiza.

Na nyota zinaonwa na macho zipo ndogo * na vimondo nchani si kama nyota kiudogo.

Haya, hivi alifikiri kuwa Warabu ambao walisimamishiwa hoja ya kushindwa kwao, je uwezo wao mbele ya sura ndefu na fupi ulikuwa sawa sawa na kwa hiyo hawakushindana na hizi wala zile. Hili pekee linakata kabisa utata wake kama akiwa anatosheka na hoja. Na kama anataka ushahidi wa kidhibiti ataambiwa: hebu ikusudie mojawapo katika sura hizo kisha dhibiti maana yake moyoni mwako. Kisha lete hayo maana kwa maneno yako. Hapo utakuja ona kuwa wewe upo baina ya mambo mawili: Ima usiweze kuyatekeleza kwa namna yake ikiwa mfano wa kiwango hiki na mfano wa mfumo huu. Na ima urejeshe maneno yake yale yale, na hakuna la kuchagua la tatu. Na kwa wakati huo, inabainika kuwa siri ya muujiza katika sura fupi za Quran upo sawa sawa na ule wa sura ndefu. Kama vile siri ya muujiza wa kuumba sisimizi upo sawa na siri ya kuumba ndovu. Anaijua hilo aliyelijua. Na hakulijua hilo ambaye hakulijua.

Ibnu Atwiya Allah amrehemu amesema: (Na kwetu sisi tunabainikiwa na uhodari katika sehemu zake nyingi na hufichikana utamu wake kwetu sisi katika sehemu nyingi. Na hilo ni kutokana na udhaifu wetu kidaraja kuliko warabu wa wakati huo, kuhusiana na usalama wa vionjo na uzuri usio na makandokando. Kwa hakika hoja imeshasimama kwa ulimwengu wa warabu, kwa sababu kwao wao ndio mafasaha wa wanadamu imeishia) أهـ . Juu ya kufanya vizuri hasa. Tunasema: atakayeenda katika njia sahihi

2- **Quran ikiwa katika Sura miongoni mwake.**
3- **Quran ikiwa baina ya baadhi ya sura na baadhi nyingine.**
4- **Quran ikiwa katika ujumla wake.**

* * *

## Quran Ikiwa Katika Vipande Vipande Miongoni Mwake

Tunaapa kwa Allah, hatujui tukwambie nini kuhusu muundo mtindo wa kimuujiza katika kueleza wasifu wake. Kama ulivyo wenyewe ni muujiza katika dhati yake? isipokuwa sisi tunasema neno nalo ni kuwa kwa ujumla kauli kuihusu Qurani. Nayo ni kuwa (***Katika Quran, miisho ya mambo mema yote inakutana. Licha ya kuwa mbali na yale yote yaliyo katika ncha zake***).

Neno hilo linahitaji ufafanuzi mrefu, unaojaza kifua wala sio wa kutamkwa na ulimi. Kila kile ambacho tutakijaribu kukufafanulia, kwa mujibu wa uwezo wetu kitakuwa ni upande mmoja wapo miongoni mwa pande za Quran. Isipokuwa sisi, kabla ya kukusimulia upande huu kuhusu Quran, tutakusimulia kuhusu maneno ya watu. Simulizi inayofahamika na kila yule ambaye yeye mwenyewe amepitia ufundi wa bayani. Ili ujue sehemu za upungufu katika eneo hili na sehemu za ukamilifu katika eneo lile. Na miongoni mwa milango ya muujiza katika eneo hili na sababu za kuufanya kuwa ni muujiza katika eneo lile:

### A – B: (Makusudio Katika Kupamba Matamshi) Na (Kuitendea Haki Maana):

Kuna miisho miwili ya kila anayejaribu kukusanya baina ya mawili hayo. Atasimama kwa mawili hayo nafasi ya mume baina ya wake wawili. Hawezi kufanya uadilifu baina ya wawili hao bila ya kupendelea japo kwa kiasi fulani kwa mmoja wao:

Basi yule ambaye atakusudia kubania matamko na kutoyatumia ila kwa kiasi cha lazima tu. Basi mtu huyo hatoacha kuwa katika kudhoofisha maana kwa uchache au kwa wingi. Hivyo ni kwa kuwa ima yeye atakutekelezea makusudio yake kiujumla na si kwa maelezo mapana. Na kwa hiyo njia yake itakuwa ni njia ya yule anayesema, katika mlango wa

---

atafika. Na kama hajatambua kila kile anachotamani, basi kile alichokijua kitamjulisha kile asichokijua.. Na Allah ndio wa kuombwa msaada [Daraazu].

kutoleana hoja: (Kubalini au kataeni) na katika mlango wa kusifia: (nzuri au mbaya) na katika mlango wa kutoa habari: (Ilikuwa au haikuwa) na katika mlango wa matakwa: (fanya au usifanye) hana cha kuzidisha zaidi ya hapo.

Na ima aende mbele zaidi katika hilo na kuingia katika maelezo mapana. Lakini yeye atakuwa anachukua tahadhari ya kuzidisha na kutumia maneno kwa fujo. Atatoa juhudi zake katika kuunganisha ncha zake na kufuta yale anayoweza miongoni mwa maneno ya zana za utangulizi na kutia shauku, na za kuimarisha na kuthibitisha. Na yale yaliyo kama hayo miongoni mwa yale yanayogusa haja ya nafsi katika bayani. Mpaka aitoe ikiwa ni nguo iliyoruka, inakuwa fupi haitoshi lengo lake. Au iwe fuvu la mifupa isiyovikwa nyama wala mishipa. Na huenda herufi moja ikipungua katika maneno. Basi yenyewe inaondoa matamu yake mia moja. Na kukashifu jua la ufasaha wake. Na huenda kufupisha kukayakunja maneno mkunjo ambao unaisonga roho ya maneno hayo na kutia upofu njia yake, na huo ufupisho wake kuyarudisha hayo maneno katika kupotea na kuwa vitendawili tu.

Na yule anayekusudia kutekeleza haki ya maana na kuichambua nukta nukta. Na kudhihirisha kila kitu kwa kina (kwa kiasi kile kinachojulikana na elimu yake na kile kinachoelezwa na utambuzi wake) hatokuwa na budi aikunjue sana nafsi yake. Kwa sababu yeye katika maneno machache hatopata kile kinachoponya moyo wake, na kikamtekelezea ule ujumbe wake kwa ukamilifu. Na kama ataipa nafsi yake fungu lake katika hilo basi hatopitisha muda ila atatenganisha baina ya ncha za maneno yake. Na atakucheleweshа kufikia lengo lake. Basi nguvu za uchangamfu wako na kichocheo cha kuelekea kwako, utavihisi vinaanza kupungua na kunywea.

Wale wote tunaowajua miongoni mwa watu fasaha sana wa kale na wa kisasa mara nyingi huwa wanapatwa na upande huu. Namaanisha upande wa kuboa na kutumia maneno kwa fujo na sio upande wa upungufu na kupunja maana. Na wengi wao wanacharushwa na matamanio yao kibayani na kuelekea mbali zaidi ya mpaka huu:

- Wapo miongoni mwao wanaoenda hadi kufikia kujikalifisha na kupuyanga kwa kutumia msamiati na tungo za ajabu. Hivyo wanakukalifisha uoneshe, urudie, ukubali na utafakuri mpaka uongoke kupata uso wa makusudio yake. na hivyo hivyo, maneno yake kwa kuyarefusha hayazidishi ila kuufinya ufahamu wake.

• Na wapo miongoni mwao wale wanaotupia maana kwa kuzilundika na maneno yasiyohitajika, yalizidi kwa muundo wake na sentensi zake. Au wanayavalisha nguo pana sana la visawe na maneno yenye maana zilizokaribiana na yaliyo yenye kusumbua katika miisho yake. Huku mwenyewe akijiona kuwa anakutekelezea maana na kukuanishia. Na kwa haki kabisa, hakika anayatawanya na kuyaharibu. Na huenda mfano wa njia ya watu hawa ni kama vile yule aliyefuta nusu ya maneno yake ili nusu ya pili ikutosheleze kufahamu.

Hayo, jua kwamba wanaumbuji, vyovyote watakavyopambana kuwataabisha wanyama wao wanaowapanda na kuhangaika nao, na vyovyote watakavyowaleta farasi wao, na wakitembea kwa miguu, basi hata mmoja wao kwa kazi yake hiyo hatofikia lengo la matumaini yake. Na hakika si vinginevyo, atafikia, kama tulivyosema, katika ukamilifu wa kiasilimia (kwa kadiri ya kile kinachojulikana na elimu yake. Na kile kinachotekelezwa na utambuzi wake hapo hapo). Ama kuitekeleza maana kwa haki ya kuitekeleza, kwa kiasi ambacho hakosei hata nukta katika maneno yake wala pambo katika mapambo yake, wala isiongezeke kwake tukio la kigeni ambalo linahesabiwa kuwa ni kiraka katika nguo yake. Wala hali miongoni mwa hali hazitopinduka katika hilo na kufunika uzuri wa kusimama kwake. Kwa kiasi ambacho ndani yake kunakuwa hakuna njia ya kutengua au kupendekeza jipya. Basi hilo ni jambo ambalo mtu aliyenyooshwa kwa moto wa bayani hawezi kulifanya. Sembuse alifanye mtu asiye mwana bayani.

Na alama ya hilo ni kuwa wewe utaliona hilo pale maneno yale yale yanapofuatana muda[1] baada ya muda, katika hilo utakuta kuna cha ziada kinachofuta hayo maneno, pia kuna upungufu unaoyathibitisha. Na ndani ya hayo anapata kile kinachoyarekebisha na kubadilisha, na kile kinachotanguliza au kuchelewa. Mpaka yatapita njia yake kwenda moyoni yakiwa sawa sawa. Na huenda yeye, lau kama atayarejea mara sabini[2] basi mtu atapata katika kila mara mtazamo mwingine. Na kila anapotazama vizuri na kwa hisia ya kina, basi katika hilo anakuwa ni mchache wa kutosheka nalo na fikra zipo mbali. Kwani yeye ataona nyuma ya juhudi zake kuna upeo ambao ndio kiigizo chema anachokitamani kukifikia lakini hakiwezi,

---

[1] Muda: yaani kila saa, mara kwa mara.

[2] Kama inavyopokewa kutoka kwa Zuhairi kuhusiana na kuyaboresha mashairi yake aliyokuwa akiyaita (Al-Hawliyaati: yaani mwaka mpaka mwaka) [Daraazu].

na ukamilfu wa bayani unaohusiana na fikra zake lakini haupati ﴿ **… Kama yule anayenyoosha mikono yake miwili kwenye maji ili yafike kinywani mwake; lakini hayafiki...** ﴾ Raad 14.

Hii ndio nafasi ya maneno ya kiumbuji kwa mwenye kuyasema. Basi ni ipi dhana yako kwa yule anayemkosoa na kushindana naye?

Hili, na hali yeye kwa hakika anakusudia lengo moja. Sasa itakuwaje lau kama pamoja na lengo hilo akakusudia lengo lingine, na akajaribu kuweka huu utajiri wa kimaana katika tamko kusudiwa? Na hilo likatokea wapi, ikiwa yeye ni mfungwa wa haya maumbile ya kibinadamu ambayo hayawezi kumkurubisha hata katika ncha moja kati ya ncha mbili za njia ila kwa kiasi ambacho kinamuweka mbali na ncha nyingine?

Na kama utabahatika kumpata mtu mmoja ambaye atawafikishwa kuyaweka karibu malengo mawili hayo kwa kiasi fulani katika sentensi moja au sentensi mbili. Kisha baada ya hapo ngoja uone namna gani jambo lake litakavyokuwa. Na tazama, namna linavyopatwa na kuchosha, kuchuja na kudhoofu[1] kimaumbile ya kibinadamu, na kwa hiyo fundo la maneno yake lililokuwa limefungwa linafunguka, na ua lake lililokuwa imara na bichi linanyauka. Kisha hayarudi tena katika nguvu yake ila katika kitu kidogo baada ya kitu kidogo kingine. Kama vile unavyopata kipande cha dhahabu mchangani, kipande hapa na kipande kingine pale. Kisha useme: Hiki ni kipande chenye thamani na ni kizuri, na hiki kinathamani zaidi na ni kizuri zaidi. Na hiki ndicho kito (madini) kinachowekwa katikati ya mkufu[2] na ubeti wa kasida[3].

Uliza wasomi wa uhakiki wa mashairi na maneno: (je, mmeshawahi kuliona shairi au risala ambayo yote au sehemu kubwa yake ni maana kubwa, na tamko lenye kukusanya maana pana na mfumo mtamu?) – kwa hakika neno lao limekusanyika juu ya kuwa washairi mahodari hawajafikia kiwango cha kufanya vizuri ila katika beti chache tu, katika mashairi machache tu. Na wao hao, nyuma ya hayo walikuwa na maneno ya kiwango cha wastani na yale ya kiwango kibaya, na pumba na maneno ya kuchukiza. Na hivyo hivyo

[1] Kudhoofu: kwa kupauka na kupelea.
[2] Katikati ya mkufu; kito cha thamani kinachowekwa katikati ya mkufu au kidani. Nacho ndicho kipande kizuri zaidi na chenye thamani zaidi katika mkufu.
[3] Ubeti wa kasida: Ibnu Jinniy amesema: asili ya neno ni Ka-swa-da na maana yake katika maneno ya warabu ni kuazimia na kuelekea na kuamka kufanya kitu [Lisanu Al-Arabi 3643] na lenyewe kwa hapa lina maana ya lengo husika na kuu.

wamesema katika Alkitaabu wal-khutwabaau. Suala hili katika kitabu hicho, lipo wazi sana.

Kama utafurahia kuona namna malengo mawili haya yanavyojumuika pamoja yakiwa katika ukamilifu wake bila kuchosha wala kukatika. Tazama popote utakapo katika Quran Tukufu. Utakuta bayani iliyokadiriwa vizuri sana kwa mujibu wa haja na nafsi. Wala hutohisi katika hilo unene wa matumizi mabaya wala kukonda kwa kujibana. Kwa kila maana inakupatia picha safi toshelezi: (safi) isiyotiwa dosari na chochote miongoni mwa mambo ya kigeni kwake. (toshelezi) hakitoki katika picha hiyo kitu chochote miongoni mwa vitu vyake vya asili na vile viambata vyake vya kuikamilisha. Yote hayo yapo katika maneno mafupi yaliyo safi. Katika kila sentensi miongoni mwake, ni mtambo miongoni mwa mitambo ya maana. Na katika kila neno miongoni mwa maneno yake ni kiungo miongoni mwa viungo vyake. Na katika kila herufi miongoni mwake ni sehemu kwa makadirio yake. Na katika maweko ya maneno yake ndani ya sentensi, na maweko ya sentensi zake katika aya zake ni siri ya maisha inayopangilia maana katika utekelezaji wake. Na kwa ujumla utaona kama vile anavyosema Albaaqilaaniy: (mambo mazuri mutawaaliya[1] na umbuji wenye kufuatana).

Weka mkono wako popote utakapo katika msahafu. Na hesabu kile ambacho kiganja chako kitaweza kukidhibiti miongoni mwa maneno kwa kuyahesabu vizuri. Kisha dhibiti hesabu zake katika maneno ya umbuji sana utakayoyachagua na yaliyo nje[2] ya magamba mawili yake, na utazame uwiano wa kile kilichomo katika maneno haya miongoni mwa maana na kile kitakachokuwa huko kwingine. Kisha tazama: ni maneno mangapi utakayoweza kuyadondosha au kuyabadilisha katika maneno haya bila ya kuharibu lengo la msemaji wake? Na neno lipi utakaloweza kulidondosha au

[1] Asili ya neno hili ni (Tatawaalaa) hivi hivi lipo katika kitabu cah Muujiza wa Quran cha Albaqilaaniy, lakini sisi tumelinukuu kwa maana na wala hatujalinukuu kwa lengo la kurekebisha kosa mashuhuri kwa chipukizi. Kwa wao wanadhani kuwa neno (tat-raa) ni kitenzi cha wakati uliopo, wakati lenyewe ni nomino iliyonasibishwa na asili yake ni watiran yaani yenye kufuatana. Na wala haifichikani kuwa kwa kukifanya kiambata chake cha kwanza kuwa kitenzi cha wakati uliopo, kwamba hilo litafanya ufahamu huu mbaya uthibiti katika nafsi ya mwanafunzi. Na kwa hiyo tukatoa kipaumbele katika kulirekebisha liwe katika sura hii pamoja na kutoa angalizo juu ya hilo [Daraazu].

[2] Pia na maneno ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake ijapokuwa yenyewe – yamenyweshwa kitu fulani miongoni mwa roho ya ufunuo – ni mafupi na fasaha zaidi kuliko yote yalizungumzwa na watu. Lakini yenyewe katika ufupisho wake, hazina zake na kujaa kwake hayafiki hata moja ya kumi ya ule uchumi wa kimaana utakaoupata katika hilo ndani ya Quran Tukufu [Daraazu].

kulibadilisha huko katika maneno mengine? Basi kitabu cha Allah Mtukufu – kama asemavyo Ibnu Atwiya – (lau kama litaondolewa tamko moja tu kisha pangetafutwa katika lugha ya warabu tamko lingine lililobora kuliko hilo basi lisingepatikana)[1]. Bali kitabu hiki kipo kama vile kilivyoelezewa na Allah ﴿**Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye hikima na Mwenye ujuzi wa kila kitu** ﴾. Hud 1.

C – d: **(Kuwaongelesha Wote) Na (Kuwaongelesha Watu Maalum)**:

Malengo mengine mawili haya yapo mbali mno kwa watu. Na lau kama wewe utawaongelesha waerevu kwa uwazi uliounuliwa na ambao huongelewa kwao watu wenye ufahamu mdogo. Basi utakuwa umewashusha hao waerevu na kuwaweka katika kiwango wasichokiridhia katika nafsi zao katika hayo maongezi. Na lau kama wewe utawaongelesha watu wote kwa vidokezo na viashiria vinavyotumika kuwaongelesha waerevu, basi kwa kufanya hivyo utawapeleka katika jambo lisilowezekana na akili zao. Kwa hiyo wewe huna cha kukutosha – kama utataka kuyapa makundi mawili yote hayo haki yao kamili katika bayani yako – unapaswa uliongeleshe kila kundi katika makundi mawili hayo si kwa kile unachowaongelesha kundi lingine. Kama vile unavyowaongelesha watoto kwa kutumia maneno mengine yasiyo yale unayowaongeleshea wakubwa.

Ama uwepo wa sentensi moja inayotolewa kwa wasomi na wajinga, na kwa waerevu na wasiolewa haraka, na kwa watu wa masokoni[2] na wafalme, na kwa wote hao kila mmoja wao aione sentensi hiyo kuwa imekadiriwa kwa kiasi cha akili yake na kwa kuafikiana na haja yake. Basi hilo ni lile ambalo hutolikuta kw a ukamilifu wake ila katika Quran Tukufu. Yenyewe ni Quran moja, wanaumbuji wanaiona kuwa ni maneno yanayotosheleza kwa uzuri wa kujieleza. Na watu wa kawaida wanaiona kuwa yenyewe ni maneno mazuri na yaliyokaribu sana na akili zao. Hayapindi pindi katika fahamu zao, na wala hawahitaji kutafsiriwa nyuma ya maweko ya kilugha. Na yenyewe ni raha kwa watu wa kawaida na watu maalum kwa sawa sawa. Imerahisishwa kwa kila anayetaka ﴿**Na kwa yakini Tumeifanya Quran iwe nyepesi kufahamika (ili iwe kikumbusho). Lakini yuko anayekumbuka?** ﴾ Al-Qamar 17, 22, 32 na 40].

---

[1] Kutoka katika Al-Itiqaanu [Daraazu].
[2] Wa masokoni: ni raia wa kawaida, wa mtaani.

**E – F: (Kuitosheleza Akili) Na (Kuzistarehesha Hisia):**

Na katika nafsi ya mwanadamu kuna nguvu mbili: nguvu ya kufikiri na nguvu ya kihisia. Na haja ya kila moja katika nguvu mbili hizo sio haja ya mwenzake. Ama moja wapo inaichimbua haki ili kuijua. Na kuhusiana na habari ili kuifanyia kazi. Ama lingine linasajili hisia zake kwa kile kilicho katika vitu miongoni mwa ladha na maumivu. Na bayani kamilifu ndio ambayo inayokutoshelezea kwa hizi haja mbili na kuruka katika nafsi yako kwa hizi mbawa mbili. Na kuzipa fungu lake katika faida za kiakili na starehe za kihisia zote kwa pamoja.

Je, umeona ukamilifu huu katika maneno ya watu?

Kwa hakika tumeshayajua maneno ya wasomi na wenye hekima. Na tumeshajua maneno ya wanafasihi na washairi. Na hatukupata kutoka kwa hawa wala wale, ila kuchupa mipaka katika upande mmoja na upungufu katika upande mwingine:

- Na ama wenye hekima, kwa hakika si vinginevyo wanakutekelezea matunda ya akili yao kwa kukupatia chakula cha akili yako. Na nafsi zao hazielekei katika kupumbaza nafsi yako na kuzinyakua hisia zako. Kwa hiyo utawaona, pale wanapokupatia ukweli wa elimu, hawajali yale yaliyomo ndani yake miongoni mwa ukavu na utupu na kuboronga[1] katika tabia.
- Na ama kwa washairi, kwa hakika wao wanaenda mbio katika kuamsha hisia zako. Na kukutikisa mishipa ya hisia za nafsi yako. Na wala hawajali kile alichokuswawiria kama kitakuwa upotofu au uwongofu, na kama zenyewe ni hakika au ni dhahania. Kwa hiyo utawaona wakiwa kikweli kweli na hali wao wakifanya mzaha. Wanajiliza hata kama ikiwa hawalii. Wanaburudisha hata kama wenyewe hawaburudiki ﴿**Na watungaji mashairi (yasiyokuwa na faida) wanafuatwa na watu wapotofu (wapotevu). (Wenye akili zao hawawafuati watu hao. Je, huoni kwamba wao (wanazuzuka) katika kila upande (bure bure)? Na ya kwamba wao wanasema wasiyoyatenda?** ﴾ Ash-Shuaraa 224 – 226.

Na kila mtu pale anapofikiri, kwa hakika yeye ni mwanafalsafa mdogo. Na kila mtu pale anapohisi kwa hakika yeye ni mshairi mdogo, uliza wataalamu wa saikolojia: (Je, mshamuona mtu yeyote ambaye kwake zinalingana nguvu za kufikri, nguvu za kihisia na nguvu nyingine za

[1] kuboronga: mbali na mbaya.

kisaikolojia kwa sawa sawa? Na lau kama atapendelea katika nguvu hii na kusawazisha kidogo kwa watu. Je, utaiona inafanyakazi katika nafsi kwa mkupuo mmoja, na kwa uwiano mmoja?) Watakujibu kwa ulimi mmoja: (Sivyo hivyo, bali zenyewe hazifanyi kazi pamoja ila kwa kuwekea zamu katika hali baada ya hali. Na kila unapoitawalisha nguvu moja miongoni mwazo basi ile nyingine inakonda na athari yake kukaribia kufutika).

Basi yule anayezama katika kufikiri, basi nguvu ya hisia zake hupungua. Na yule ambaye anatumbukia chini ya kuathiriwa na ladha au maumivu, basi kufikiri kwake kunapungua. Na hivi hivi nafsi ya mwanadamu huwa haikusudii haya malengo mawili kwa mkusudio mmoja. Na kama si hivyo basi ingekuwa ni kwenda mbele na kurudi nyuma kwa pamoja. Na Allah amesema kweli: ﴿**Mwenye Mungu Hakumuekea mwanadamu nyoyo mbili kifuani mwake…**﴾**.** Ahzab 4.

Na vipi utakua na tamaa kwa mwanadamu akupatie haya matakwa mawili kwa sawa sawa. Na hali ya kuwa yeye hajayakusanya moyoni mwake kwa sawa sawa? Na maneno ya muongeaji hayakuwa vingine ila ni taswira ya hali iliyoshinda katika moyo wake baina ya hali hizo.

Hiki ni kipimo, unaweza kukitumia ili kubaini kila ulimi na kalamu yaani nguvu mbili ni ipi itakuwa ipo chini yake pale aliposema au alipoandika.

- Ukimuona anakusudia kuhamasisha nafsi au kuzifukuza, kuzikamata au kuziachia, kuchochea vilivyofichikana katika ladha zake au maumivu yake, utasema: haya ni matunda ya hisia.
- Na ukimuona amehama kutoka katika moja ya aina mbili hizi na kuelekea katika aina nyingine na akamaliza hilo baada ya kumaliza haja zake katika yale yaliyopita. Kama vile anavyohama kutoka katika lengo moja hadi lingine. Kwa hilo utajua kuwa kuna kupishana baina ya tafakuri na hisia katika nafsi yake.

Na ama kutakuwa na muundo mtindo mmoja unaoelekea mwelekeo mmoja na unaokusanya hizi ncha mbili kwa pamoja katika mikono yako, kama vile tawi moja la mti linavyobeba majani, maua na matunda kwa pamoja, au kama roho inavyotembea katika mwili na maji katika tawi bichi. Basi si katika yale yanayopatikana katika maneno ya mwanadamu. Na hilo si katika maumbile ya Allah katika nafsi ya mwanadamu.

Kwa hiyo utayapata wapi haya maneno ambayo yanakuja na uhakika wa hoja za kukata kabisa na ni zile ambazo zinawaridhisha hata wale wanafalsafa wabobezi. Na kuzipatia raha nafsi zilizo nzuri na ambazo zinawaridhisha hata wale washairi mamanju?

Huyo ni Allah Mola Mlezi wa viumbe wote. Kwani yeye ndiye ambaye hashughulishwi na jambo dhidi ya jambo lingine. Na yeye ndiye muweza wa kuzizungumzisha akili na moyo kwa pamoja kwa ulimi mmoja. Na kuchanganya haki na uzuri vyote kwa pamoja vikikutana na wala havibughudhiani. Na baina ya viwili hivyo anaweza kutoa kinywaji kitamu na chepesi kumezwa kwa wanywaji. Na hili ndilo utakalolikuta katika Kitabu chake Kitukufu popote utakapoelekea:

- Hivi huoni katika upana wa visa vyake na habari zake[1] hasahau haki ya akili kupata hekima na mazingatio?
- Hivi kweli hauoni katika sauti za hoja zake[2] na hukumu zake[3] hasahau fungu la moyo miongoni mwa kupewa shauku na kulainishwa, na kuonya na

---

[1] Kwa mfano soma suratul Qaswaswi na suratul Yusuf amani iwe juu yake [Daraazu].

[2] Kwa mfano soma kauli yake Mtukufu ﴿**Lau kama wangalikuwapo humo (mbinguni na ardhini) waungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu: bila shaka zingeharibika (hizo mbingu na ardhi). Na ametakasika Mwenyezi Mungu, Mola wa Arshi, yu mbali na yale wanayomsifu kwayo** ﴾**.** Al-Anbiyaa 22. Na tazama jinsi uthibitisho, kutisha na kukuza jambo kulivyokusanywa pamoja katika maneno haya machache. Bali uthibitisho wenyewe ni wenye kukusanya baina ya kina cha vitangulizi vya yakini na uwazi wa vitangulizi vya kukubalika visivyopingika. Na umakini wa kutoa taswira kwa kile kitakachofuata baada ya mgogoro miongoni mwa (uharibifu wa kutisha). Basi maelezo haya ni ya kujenga hoja na hapo hapo ni ya maelezo ya kihisia yote kwa pamoja. Je, utayakuta maneno kama haya katika kitabu miongoni mwa vitabu vya hekima za kinadharia? [Daraazu].

[3] Kwa mfano soma kauli yake Mtukufu ﴿**Enyi mlioamini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouawa – muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema; na yeye alipe (na kulipishwa) kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu na ni rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya hayo, basi yeye atapata adhabu iumizayo** ﴾**.** Albaqarah 178. Na tazama:

- Namna ya kuwavuta watu kidogo kidogo katika kumtii Allah katika ufunguzi wa aya kwa kauli yake: ﴿**Enyi mlioamini** ﴾**.**
- Kuzilainisha hisia baina ya walioua na waliouliwa mtu wao kwa kauli yake ﴿**ndugu yake** ﴾ na kauli yake: ﴿**kwa wema** ﴾ na kauli yake ﴿**kwa ihsani** ﴾.
- Na kuonesha neema zake katika kauli yake: ﴿**Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu na ni rehema** ﴾**.**
- Na vitisho mwishoni mwa aya…

Kisha tazama aya hiyo inaongelea jambo gani? Je, sio katika faradhi inayolezwa kwa upana na katika maswala ya damu? Na fuatilia maana hii katika aya nyingine za hukumu

kuepusha, kutisha na kushangaza, kuliza na kugombeza? Hayo yanatawanywa katika mapitio ya aya zake na vipande vyake na nyongeza zake. ﴿**Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa (kwa kuteremsha) kitabu chenye maneno yanayowafikiana, (yasiyopingana) (na) yanayokaririwa (bila kuchosha); husisimka kwayo ngozi, (miili) za wale wanaomwogopa Mola wao … kisha ngozi zao na nyuso zao huwa laini kwa kumkumbuka Mola wao…** ﴾**.** Azzumar 23. Na ﴿**Kuwa hii (Quran) ni kauli ipambanuayo haki. Wala si mzaha** ﴾ Tariq 13 – 14.

**G – H: (Ubainifu) Na (Ujumla):**

Na hii ni ajabu nyingine utakayoikuta katika Quran na wala hutoikuta katika vitabu vingine. Hivyo ni kwa kuwa watu pindi wanapokusudia kuainisha malengo yao hawana nafasi pana ya kufasili. Na pindi wanapoiweka katika ujumla wanaenda katika utata au kuchanganya. Au wanaenda katika upuuzi ambao hauleti faida. Na kwa wao, hizi ncha mbili hazikusanyiki pamoja katika maneno mamoja.

Na utasoma kipande cha Quran na utakuta matamshi yake yana uwazi na msawazisho na kudhibitiwa vizuri. Yameepukana na kila neno geni lisilofikisha katika lengo. Yale ambayo malengo yake yanashindana kwenda katika moyo wako bila ya kutaabika kwa kufikiri wala kurudia kusema. Kana kwamba husikii maneno na lugha, bali unaona picha na hakika zinazojiwakilisha. Na hili linakufanya wewe ufikirie kuwa wewe umeifahamu vizuri na umeshajua maana yake yenye mipaka maalum… hilo, na lau kama utairejea mara nyingine, basi ungeiona ukiielekea maana mpya sio ile iliyotangulia katika ufahamu wako kwa mara ya kwanza. Na kadhalika … mpaka unaiona sentensi moja au neno moja[1] lina njia nyingi. Na njia zote

---

hata katika hukumu ya viapo na dhihari (kumwita mkeo mama yako). Katika kitabu gani miongoni mwa vitabu vya sheria utakuta mfano wa roho kama hii? Bali katika lugha gani utakuta mchanganyiko huu wa ajabu? Naapa kwa Allah lau kama mtu mmoja akajaribu kukusanya katika bayani yake baina ya hizi ncha mbili. Hivyo basi akaitenganisha hima yake na kutawanya sehemu za nafsi yake, basi huyo angekuja na vinyume vinavyokataana, na angetokelezea na nguo ambayo bayani yake ipo baina ya hizi ncha mbili ikiwa na viraka iliyoraruka. [Durazu].

[1] Huu ni mfano mdogo: Soma kauli yake Mtukufu: ﴿**Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila hisabu** ﴾**.** Albaqarah 212. Na tazama, je unayaona maneno yenye bayani zaidi kuliko haya katika akili za watu. Kisha tazama maneno haya yana unyumbulifu wa kiasi gani. Kwa hakika lau kama utasema katika maana yake:

1- Hakika yeye Mtukufu anamruzuku amtakaye bila ya mhasibu wa kumhesabu, wala muulizaji anayemuuliza kwa nini anakunjua riziki kwa hawa na anawapa kidogo hawa, utakuwa umepatia.

hizo ni sahihi au zinauwezekano wa kuwa sahihi. Kanakwamba aya hiyo ni jiwe la alimasi ambalo kila upande wake unakupa miale. Na utakapotazama katika pande zake kwa ujumla zinakupendeza kwa rangi zake zote za upinde wa mvua. Wala jicho lako halitojua lichukue nini na liache nini. Na huenda wewe, lau kama ungemwakilisha mtu mwingine akutazamie katika hilo jiwe basi angeona mengi kuliko yale uliyoyaona. Na hivyo hivyo utakikuta chenyewe ni Kitabu kilichowazi kinaendana na wakati, na kila mtu anachukua kutoka katika Kitabu hicho kile ambacho ni chepesi kwake kukichukua. Bali utaona bahari kuu yenye pande zake za masafa marefu, kiasi ambacho akili za kila mtu haziwezi kuweka ukomo wake, wala vizazi kwa vizazi vya watu navyo haviwezi.

Hivi huoni namna makundi ya Kiislamu yalivyo mapana kwa tofauti za maoni yao katika misingi na matawi? Na namna rai za kielimu zilivyo pana licha ya tofauti ya njia zake katika zama za kale au za sasa? Na yenyewe licha ya ulaini wake akilini na katika ufahamu, kwa hakika ni ngumu na madhubuti. Haipingani na haibadiliki. Kila kundi linatolea hoja Quran kutetea msimamo wake, na linadai kuwa Quran ipo upande wao. Na hali hiyo Quran katika utukufu wake ipo juu ya wote inatazama mapambano yao

---

2- Na lau kama utasema: Kwa hakika yeye anaruzuku bila ya kubana wala kujihesabu yeye mwenyewe wakati wa kutoa kwa kuhofia yasiiishe utapatia.
3- Na ukisema: hakika yeye anamruzuku amtakaye bila ya kusubiri kitu wala kutarajia kitu. Umepatia.
4- Na lau kama utasema: Kwa hakika yeye anamruzuku bila ya kulaumu au kujadili tendo lake, umepatia.
5- Na lau kama utasema: anamruzuku riziki nyingi zisizoingia chini ya udhibiti na hesabu, umepatia.

Kwa kauli ya kwanza maneno yatakua ni kuikazia kanuni ya riziki duniani, na kwamba mfumo wake hauendi kwa mujibu wa kile kilichopo kwa mruzukiwa miongoni mwa kustahiki kwa elimu yake au kwa kazi yake. Bali riziki inapita kulingana na matakwa yake na hekima zake Mtukufu katika kutoa mitihani. Na katika hilo ndani yake kuna kuliwaza mafakiri walioamini. Na pia kuna kuzisaga nafsi za wanaodanganyika miongoni mwa watu wenye maisha mazuri. Na kwa hiyo ya pili inakuwa ni uzindushi juu ya upana usio na kikomo wa hazina zake na ukunjufu wa mkono wake yeye ambaye ni Mtukufu Aliyetukuka. Na kwa ya tatu inakuwa ni kuashiria kuwa waamini kwa kile ambacho Allah atawafungulia wao miongoni mwa milango ya ushindi na mafanikio mpaka atabadilisha magumu yao kuwa mepesi, na ufakiri wao utakuwa utajiri bila ya wao kudhania. Na kwa kauli ya nne na ya tano itakuwa ni ahadi kwa watu wema: Ima kwa kuingia kwao peponi bila ya hesabu. Na ima kwa kuwaongezea malipo yao nyongeza nyingi isiyodhibitiwa hesabu yake. Na yule anayejua elimu ya kufasili na kupitia eneo la mchuano wa fahamu za wanazuoni katika aya, ataona katika hayo ajabu ya maajabu [Daraazu].

kuihusu yeye. Kana kwamba ulimi wa hali yake unawaambia hawa na wale: ﴿**Sema: kila mmoja anafanya (amali zake) kwa njia yake. Na Mola wetu anajua aliyeongoka katika njia (wanazofuata)''**﴾ . Bani Israil 84.

* * *

Haya sisi ndio ambao tumeshakuwasilishia upande mmoja miongoni mwa hayo maajabu ya kibayani ambayo mfano wake haupatikani katika mikono ya watu. Na haya tumeshakupa mfano mdogo katika kifurushi cha kila moja katika hayo tunaokufungulia mlango wa kuufuata kuelekea katika sehemu nyingine za Quran. Je, unaona katika hili kuna kutekeleza kile tulichokuahidi, na kile tulichokuzoesha, miongoni mwa kukujulisha athari kwa maelezo marefu juu ya kitu fulani katika utumiaji na mifano? Au bado una haja ya ziada miongoni mwa mifano hii?

Tutakuzidishia na tutayaelekeza macho yako katika aina maalum juu ya kueleza kwa kina na umadhubuti wa mfumo wa ki-Quran. Na matendo yake ni ya ajabu mno hadi yanakuletea maana nyingi yenye utajiri katika matamshi yenye makusudio safi. Kwani, hii ni sifa ya pekee miongoni mwa sifa za pekee tulizozitaja – zinahitaji sana kusomeshwa na kuongozwa.

[**Matumizi Katika Aya Tukufu**]

Usije ukadhani kuwa sisi tutakupigia mifano ya zile aya tukufu ambazo zimetukia kuchaguliwa na watu na wakaelezea kupendezwa nazo. Kama kauli yake Mtukufu: ﴿**''Ewe ardhi! Meza maji yako…**Hud 44. Na [1] ﴾ kauli yake ﴿**Mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi enyi wenye akili, ili msalimike** ﴾.[2] Albaqarah 179. Na aya zinazoshabihiana na hizi. Bali tunataka kukuletea mfano wa ndani ya Quran kuhusu maana zisizopewa kipaumbele na watu wala kikawaida haitukii katika chaguzi zao juu ya mfano wake ili iwe uthibitisho wa kile kilicho nyuma yake.

Allah Mtukufu anasema katika kutaja hoja za Wayahudi: ﴿ **Na wanapoambiwa (hao Mayahudi): ''Yaaminini aliyoteremsha Mwenyezi Mungu,'' (kwa Nabii Muhammad) husema: ''Tunaamini yaliyoteremshwa juu yetu (kwa Nabii Musa)''; na huyakataa**

---

[1] Ukipenda soma yale yalioandikwa na Assakaakiyu kuhusu aya hii katika kitabu chake (Miftahu Al-Uluumi) baada ya kueleza fasili ya balagha na faswaha mwishoni mwa elimu ya bayani [Daraazu].

[2] Soma kile kilichoandikwa na wafasiri kuhusu aya hii na kile kilichoandikwa na mwenye (Al-Itiqaanu) katika utafiti wa ufupisho na urefushaji. (Daraazu].

**yasiyokuwa hayo. Na hali ya kuwa hii (Quran) ndiyo haki inayosadikisha yale yaliyo pamoja nao. Sema: ‘‘Mbona mliwaua Mitume wa Mwenyezi Mungu hapo zamani kama mlikuwa mkiamini? ‘‘Na alikufikieni Musa na hoja zilizo wazi wazi, kisha mkamfanya ndama (kuwa mungu) baada yake (baada ya kuondoka kwake), na mkawa madhalimu (wa nafsi zenu).’’ Na (kumbukeni) khabari hii kadhalika: Tulipochukua ahadi yenu (wazee wenu) na tukauinua mlima juu yenu? (tukakwambieni): ‘‘Kamateni kwa nguvu haya tuliyokupeni na sikilizeni.’’ Wakasema: ‘‘Tunasikia na tunakataa.’’ Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (mapenzi ya kuabudu) ndama kwa kufuru yao. Sema: ‘‘Ni kibaya kabisa (kitendo hicho) kilichokuamrishieni Imani yenu; mkiwa ni wenye kuamini’’** ﴾. Albaqarah 91 – 93.

Hiki ni kipande katika sura ya kisa cha Wana wa Israili. Na nukta asilia inazotudhihirihishia maneno haya machache, zenyewe zinafupika ifuatavyo:

(1) Makala inayowanasihi Wayahudi, kwani inawaita waiamini Quran.
(2) Majibu yao kwa mtoa nasaha huyu juu ya makala yake yenye kujumuisha makusudio mawili.
(3) Jibu kwa majibu yao kwa nguzo zake mbili, kwa njia nyingi.

Naapa lau kama mwanasheria (wakili) mwenye umbuji wa maneno amepewa kazi ya kutetea dhidi ya lugha ya Quran katika kesi hii. Kisha akaongozwa kung`amua maana hizi zinazoingia katika nafsi ya mfungua mashitaka na mfunguliwa mashitaka. Basi asingeweza kuitekeleza kazi yake kwa zaidi na zaidi ya maneno haya. Na huenda yeye, baada ya hayo, hatoweza kutosheleza kile ambacho kipo pembezeni mwa maneno hayo miongoni mwa ishara, tahadhari, heshima, adabu na tabia njema.

Huyo mnasihi amewaambia Wayahudi: Iaminini Quran kama mlivyoiamini Torati. Je, nyinyi sio wale ambao wameiamini Torati ambayo ililetwa na Musa kwa sababu yenyewe nayo imeteremshwa na Allah. Basi na Quran ambayo amekujanayo Muhammad nayo imeteremshwa na Allah. Hivyo iaminini kama mlivyoiamini hiyo.

Hebu tazama namna Quran ilivyokusanya maana hii nyingi katika haya matamko mafupi. ﴿ **Aminini yale aliyoyateremsha Allah** ﴾**.** Na siri ya hilo ni kuwa yeye ameyarekebisha maneno na kuacha kulitaja wazi wazi jina

la Quran na kufumba. Hivyo akafanya wito wa kuwaita wao kuiamini ndio huo huo wito wa kukiendea kitu kwa hoja zake. Na kwa hiyo ametoa ushahidi na wito kwa tamko moja.

Kisha tazama namna ilivyokujia kumtaja yule aliyeteremshiwa, ambapo haikusema: Aminini kile kilichoteremshwa na Allah (kwenda kwa Muhammad) licha ya kwamba sehemu hii ndio sehemu ya kukamilisha maelezo ya Quran yanayokusudiwa kuwa ndio wito wenyewe. Je, wajua kwa nini ikawa hivyo?... Kwa sababu yenyewe lau kama ingetajwa, basi ingekuwa katika mtazamo wa hekima za kibayani ni ziada isiyo na maana. Na katika matazamo wa hekima za mwongozo hilo lingekuwa ni kuharibu. Ama hilo la kwanza ni kwa sababu, jambo hili la kipekee haliingiliani katika kulazimisha. Hivyo jambo hilo likaendeshwa kwa kadiri ya ushirikishi[1] na kwa kiwango cha wastani zaidi na ambacho chenyewe ndio nguzo ya ushahidi. Na ama lile la pili, ni kwa sababu kuliweka jina hili katika masikio ya maadui, huwa linatoa mifundo yao na kuamsha chuki zao na hivyo litapelekea kutokea kinyume na makusudio ya mwitaji ambaye alikusudia kuweka karibu na kurekebisha.

Hayo, ukiongeza yale yaliyo katika ufutaji huo, miongoni mwa viashiria vya tabia ya Uislamu. Nayo ni kuwa Uislamu si dini ya kufarakanisha na kugombana. Bali wenyewe ni wenye kukusanya kile kilichofarakishwa na watu miongoni mwa dini mbalimbali. Unaita katika kuamini vitabu vyote kwa sawa sawa: kwa kile kilichoteremshwa kwa Ibrahimu, Ismaili, Is-Haqa, Yakubu na wajukuu. Na kile alichopewa Musa, Isa na Manabii kutoka kwa Mola wao. Hatutofautishi baina ya chochote miongoni mwa vitabu vyake. Kama vile sisi hatutofautishi baina ya yeyote miongoni mwa Mitume yake.

Majibu ya Wayahudi yalikuwa ni kusema: kwa hakika kile ulichotuitia cha kuiamini Torati sio eti kwa kuwa chenyewe kimeteremshwa na Allah tu! Bali tumekiamini kwa kuwa Allah amekitermsha kwetu, na Quran haijateremshwa kwetu. Kwa hiyo nyinyi mna Quran yenu na sisi tuna Torati yetu. Na kila umma una sheria zake na njia zake.

Hii ndio maana iliyofupishwa na Quran katika kauli yake: ﴿ **Tunaamini kile kilichoteremshwa kwetu** ﴾. Na haya ndio makusudio ya kwanza. Na kwa hakika amezidisha katika kuifupisha ibara hii kwa kumfuta

[1] Nayo ni yale aliyoyateremsha Allah.

mtenda wa kitenzi cha kuteremsha naye ni tamko Tukufu. Kwa sababu yeye ameshatangulia kutajwa katika sehemu kama hii.

Katika jambo lililowazi ni kuwa, kufungika kwao na kuamini kile kilichoteremshwa kwao kunaashiria kuwa wakufuru/wanapinga kile kilichoteremshwa kwa wengine. Na haya ndio makusudio ya pili. Lakini wao waliacha kutamka hilo kwa wazi wazi, kwa kuwa lenyewe lina ubaya mno wa kusajiliwa nafsi zao katika ukafiri. Hivyo Quran ikataka kuliweka wazi hilo. Tazama namna ilivyoliweka wazi? Hakika yake haikujaalia yale ya lazima katika madhehebu yao kuwa ndio madhehebu yao. Na wala haikuingiza madhumuni ya kauli yao katika ujumla wa kile ilichokinukuu kutoka katika maneno yao. Bali imeyatoa katika uwasilishaji wa kufafanua na kutolea maelezo juu ya kauli zao. Ikasema: ﴿ **Na kuyakufuru yasiyokuwa hayo** ﴾**.** Je, hilo sio upeo wa juu kabisa katika kunukuu!

Kisha tazama maelezo juu ya Quran kwa tamko ﴿ **yasiyokuwa hayo** ﴾**.** Kwa hakika neno hili lina upande unaojumuisha kile kisichokuwa Quran na kwa upande mwingine unaufanya huu mjumuiko kuwa unahusu vitabu maalumu. Hilo ni kwa kuwa wao kama walivyoikufuru Quran iliyoteremshwa kwa Muhammad, pia wameikufuru Injili iliyoteremshwa kwa Isa. Na vitabu vyote viwili ni vya nyuma ya Torati. Yaani vimekuja baada yake. Lakini wao hawajakufuru vile vitabu vya kabla ya Torati miongoni mwa suhufi za Ibrahimu, kwa mfano. Na hivi hivi unaiona imeshaainisha kosa kikamilifu wa kuliainisha kwa kutumia tamko hili lenye kukusanya wahusika wote na kuzuia wasiohusika wote. Na huu ndio upeo wa uadilifu na kujipamba na ukweli katika kutuhumu.

Nafasi ya kujibu ikaja, na mjadala kwa kile walichokitangaza na kile walichokifanya kuwa siri.

Utaiona yenyewe haianzi kujadiliana nao katika wito wa kuamini kwao kitabu chao. Bali hilo unaliacha kidogo, kana kwamba ni jambo linalokubalika ili kwa kutumia suala hilo ajenge hoja juu ya ulazima wa kuamini vingine miongoni mwa vitabu. Basi inasema: Vipi inakuwa imani yao kwa kitabu chao iwe kichocheo cha kupinga kile ambacho nacho ni haki mfano wa kitabu chao? – Hapana, bali ﴿ **chenyewe ni haki** ﴾**.** Yote[1] - Je,

[1] Kwa hakika kile kisichokuwa yeye kama kitapingana nacho basi kitakuwa na ushahidi dhidi yake mwenyewe kuwa chenyewe ni batili. Na kama si hivyo basi kitakuwa sahihi

chenyewe kinapingana na haki hadi iwe kukiamini kimojawapo ni kuwajibika kukipinga kingine?!

Kisha inapanda juu na kusema: na jambo lililopo baina ya hiki kitabu kipya na baina ya hicho kitabu kilichotangulia sio kama jambo lililopo baina ya kila haki na haki. Kwa hakika kitu kinaweza kuwa cha haki na kingine pia nacho ni haki na wala havikadhibishani/havisemani uongo. Lakini viwili hivyo vipo katika mambo mawili tofauti, kwa hiyo havitoleani ushahidi vyenyewe kwa vyenyewe. Ama kitabu hiki kwa hakika chenyewe kimekuja kikiwa ni ushahidi na ﴿ **chenye kusadikisha** ﴾**.** Vile vilivyopo ndani yake miongoni mwa vitabu. Inakuwaje kwa yule anayeamini vitabu hivyo akipinge kitabu hiki?!

Kisha inaendelea katika kukamilisha upande huu kwa kusema: Lau kama upotoshaji au kupotea kulikovipata vitabu hivi kungekuwa kumeondosha alama za haki zilizo katika vitabu hivyo kwa mpigo. Basi hilo kwao wao lingekuwa ni sehemu ya udhuru wa kuikadhibisha kwao Quran. Kwani wana haki wao waseme: (Kwa hakika kile kilichobaki bado kimehifadhiwa katika kitabu hiki katika zama zetu, baina yake na baina ya Quran hakuna kukubaliana wala kusadikishana. Kwa hiyo kuviamini sio kiwajibisho cha kuiamini Quran) .. Bali kwa hakika haya yaliyobakia hayapo kwao wao lakini wao walikuwa ni wenye kughafilika kuvisoma. Basi hilo kwao wao lingekuwa ni kama mfano wa udhuru ule. Ama na hii Quran kuwa ni yenye kusadikisha kile ambacho kipo miongoni mwa kitabu cha zama zao na kipo mikononi mwao na wanajisomesha wao kwa wao, sasa kwa nini wanatoa udhuru, hivi wanaenda wapi?! Maana hii yote inaletwa kwetu na Quran kwa neno ﴿ **kwa kile kilicho kwao**﴾**.**

Hebu tazama umadhubuti katika ufundi wa bayani: Kwa hakika si vinginevyo lenyewe ni neno lililoondoshwa na lingine likawekwa[1] katika

---

au kina uwezekano wa kuwa sahihi. Na kwa hivyo hicho ni kipimo kikuu cha haki na ni mzani wake [Daraazu].

[1] Hivyo kwa kuwa muktadha wa maneno ulikuwa unataka isemwe: (chenye kusadikisha kile kilichoteremshwa kwao) na lakini yenyewe kwa sababu ya jambo fulani hivi, ilifuta katika kitabu chao hilo jina la zamani. Na kuwavalisha anuani hii mpya. Na lau kama moja ya maneno haya mawili lingebadilishwa likawekwa sehemu ya mwenzake, basi isingefaa kwa moja lao kukaa sehemu ya swahiba wake. Bali, lau kama ungeleta jina lingine na ukasema (Chenye kusadikisha kwa kile ambacho bado kimebakia katika zama zao) au (chenye kusadikisha kwa kile kilichopo kwao) basi kulazimikiwa na hoja kusingetimia. Na hii ndio ajabu ya jambo la Quran: Hakuna kubadilishwa kwa maneno yake [Daraazu].

sehemu yake kwa kuwa kuna haja ya kufanya hivyo. Basi neno hili likawa ni lenye kukata kabisa kila udhuru, na lenyewe ni kizuizi cha kila mlango miongoni mwa milango ya kutorokea. Bali neno hili peke yake limekuwa kama vile harakati za kumdhibiti mpinzani zilizotimizwa katika hatua moja tu. Tena bila ya kelele wala minong`ono.

Na pale ilipomalizwa haja ya nafsi katika upande huu uliokunjwa na ambao umetiririshwa kwa mtiririsho wa kupinga na kutafuta. Imekaa sawa katika kujibu makusudio ya asili ambayo wamejifurahisha kwa kuyatangaza na kujifakharisha nayo. Nayo ni kuwaita waamini wa yale yaliyoteremshwa kwao. Na ikawakunjulia kwa kuwakadhibisha na kuzivunja hoja zao. Na ikabainisha kuwa ugonjwa wa kukanusha kwao wao ni wa kale. Kwa hakika umeshanyweshwa katika mioyo yao na umeshapitiwa na karne nyingi hadi ukawa ni maradhi ya kudumu. Na kwamba kile kilichowajia leo miongoni mwa kukufuru/kupinga kile kilichoteremshwa kwa Muhammad, si kingine ila ni duara lililoungana kwa mnyororo wa kufuru/kupinga kwao kile kilichoteremshwa kwao. Na juu ya hilo imetiririsha ushahidi wa kihistoria wenye kufedhehesha ambao hauna njia ya kuupinga. Kwa ujinga wao juu ya Allah, na kuvunja kwao utukufu wa Manabii wake, na kuzipiga vita kwao amri zake: ﴿ **Sema: ''Mbona mliwaua Mitume wa Mwenyezi Mungu hapo zamani kama mlikuwa mkiamini?.. ﴾.**

(1) Tafakari vizuri namna muhamo huu, ambapo nafsi zilivyokuwa zimeshajiandaa kwa ajili yake mwishoni mwa hatua iliyopita. Kwani yenyewe inamfahamisha msikilizaji kuwa miongo mwa ukadhibishaji wao wa kile kinachosadikishwa na kitabu chao ya kwamba wao wamekuwa ni wakadhibishaji wa kitabu chao chenyewe. Na je, yule anayemkadhibisha yule anayekusadikisha atabakia kuwa ni msadikishaji wako?!

Lakini maana hii, kwa hakika si vinginevyo, imechukuliwa kutokana na kung`amua katika kauli zao. Na kuwalazimisha wao kwa mujibu wa madhehebu yao. Na hayakuchukuliwa kwa njia ya moja kwa moja kutoka katika uhalisia wa hali zao. Kwa hiyo hili likawa ndilo jukumu la jibu jipya.

Na hivi hivi lilikuwa neno ﴿ **Na hali ya kuwa hii (Quran) ndiyo haki inayosadikisha yale yaliyo pamoja nao...﴾.** ni kifungo cha yale yaliyo kabla yake na funguo ya yale ya baada yake. Na likawa ngazi ya mwisho katika ngazi ya lengo la awali na lenyewe ni ngazi ya kwanza katika ngazi ya lengo la pili. Ni kipi kilichouthibitisha muungano huu wa baina ya aina za maneno!

Na kipi kilichoongoza uongozi huu wa nyoyo kwa hatamu za bayani, kidogo kidogo katika hatua zake. Na kuteremsha kwa kadiri ya haja yake. na katika wakati wa haja hiyo! Hicho hakikuwa kingine ila ni kiliwazo kilichoitokea nafsi na kuisimamia vizuri katika neno hilo na kuipeleka katika lengo. Kwa hiyo yenyewe imeshaiweka sawa hiyo nafsi kuelekea katika hilo lengo na kuijuza kwa ukamilifu uliotimia.

(2) Na tazama namna ilivyoacha kukiegemeza kiima[1] katika maweko yake ya asili na ikaacha kumtaja mchumaji wa kweli wa uovu huo. Basi haikusema: ﴿**Mbona baba zenu waliwaua Manabii wa Allah. Na wakajitwalia ndama kumwabudu, na wakasema tumesikia na tumeasi?**﴾. Kwani kauli katika maweko haya ilikuwa ni hoja inayovunjwa na ni rai mbaya. Mfano wake ni sawa na mfano wa kushindana hoja baina ya mbwa mwitu na mwana kondo  katika ngano ya kale iliyo mashuhuri[2]. Basi hapo wangekuwa na haki ya kujibu kwa kusema: (Sisi tunahusika vipi na baba zetu? Wao ni umma uliokwishapita. Na hatobeba mbebaji mzigo wa mwingine).

Na lau kama kwa mfano ingezidisha: (Na nyinyi ni kama wao. Kwa hakika nyoyo zenu zimeshabihiana na nyoyo zao). Basi baada ya kupitwa kwa wakati kungekuja huku kutambua, na hapo ingelegea kamba ya maneno na nguvu zake zingechoka.

Kwa hiyo ufupisho wa maneno ungekuwa kama unachokiona – kwa kuwasimamisha wao mwanzoni kabisa katika kisimamo cha mtuhumiwa – na huku ni kuharakisha kuuelekeza[3] sawa sawa mshale wa hoja kuelekea katika lengo lake. Na kwa wakati huo huo, huu ni uzindushi juu ya kuwa wao ni kizazi cha wao kwa wao. Na kwamba wao ni sawa sawa katika uovu.

---

[1] Kuegemeza kiima: hii katika elimu ya Maani ni kuunganisha neno kwa lingine kwa nia ambayo italeta maana ya kuhukumu moja lake ni (Kiarifu) na lingine ni (Kiima) kwa kuthibitisha au kukanusha. Mfano: Zaidu ni mwenye kusimama – hii imeleta maana ya kuhukumu kuwa kisimamo ni cha Zaidu. Na mfano: Muhammad si muongo – hii imemaanisha kukanusha uongo kwa Muhammad. Na hapa katika maudhui yetu Allah hajaliegemeza kosa la kuua Manabii kwa watu wake wa kweli waliolifanya, nao ni mababu wa hawa Wayahudi wanaozungumzishwa katika zama za Nabii Muhammad.

[2] Ngano inayodai kuwa mbwa mwitu alimfanyia uadui mwana kondoo mdogo kwa hoja kuwa ndugu yake au baba yake alimchafulia maji ya mto alipokuwa anakunywa tangu mwaka uliopita. Na ngano hii inawakilisha uadui mkubwa kwa wanyonge kwa kutegemea sababu dhaifu mno [Daraazu].

[3] Na hiki ndicho kinachoitwa katika malumbano ya hoja (Kukaribisha/kuleta karibu) baina ya ushahidi na kinachotakiwa [Daraazu].

Na kwa yoyote yule miongoni mwao, ukiweka mkono wako basi umeshauweka kwa muovu mwenye madhambi mengi. Kwa kuwa wao hawaachi kuepukana na kufuata mwenendo wa watangulizi wao. Au kuridhia matendo yao, au kujumuka katika mfano wa makusudio yao.

(3) Na tazama namna maana hii ilivyozidisha kukazia[1] kwa kulitoa kosa la kwanza nalo ni kosa ya mauaji kwa muundo wa kitenzi cha wakati uliopo kwa kuitolea taswira ya sura ya hali halisi kwa sasa. Kana kwamba, kwa kufanya hilo inatuwasilishia kaumu hii yenyewe na mikono yao imechafuka kwa damu hizo zilizo safi.

(4) Kwa hakika maelezo kwa muundo huu, pamoja na kuwataja manabii kwa tamko la kiujumla yalikuwa ni miongoni mwa yale ambayo yamefungua mlango katika kulitenga jina la Nabii Mkarimu wa Kiarabu. Na ni mlango wa kuwatamanisha maadui zake katika wepesi wa mipango yao na majaribio yao ya kumuua[2]. Na tazama namna ilivyotusaidia kwa kujihadhari na hayo

---

[1] Kukazia: kutia nguvu na kudhihirisha.

[2] Kwa hakika majaribio ya Wayahudi ya kumuua au kummaliza Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake yalikuwa mengi sana. Kwa mfano soma katika historia yake:

- Jaribio la ukoo wa Banii Nadhiiri la kurusha jiwe la kusagia juu ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake pale alipoegemea ukuta katika kuta zao. Na njama zao katika hilo na nyendo zao katika hilo bila ya yeyote miongoni mwa maswahaba kuhisi miongoni mwa wale walioongozana na Mtume wa Allah rehema na amani iwe juu yake katika hilo. Hapo unashuka ufunuo kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake ukimhabarisha. Na Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasimama kana kwamba anataka kwenda haja na kurejea Madina na kuwaeleza Waislamu juu ya hilo. Jambo ambalo linasababisha kuhamishwa kwa ukoo wote wa Banii Nadhiiri kuwatoa Madina baada ya kuombewa na Ibnu Saluuli katika hilo.
- Njama za Makuraydhwa pamoja na washirikina za kuwafungulia mji wa Madina ili waingie na kuwaangamiza Waislamu. Na kumpata Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake. Hili lilikuwa katika vita vya Khandaki. Lakini Allah aliwanusuru waumini dhidi ya makundi ya washirikina. Na akawaadhibu Wayahudi wa Quraydhwa kwa kuuawa na kutekwa wajakazi kama hilo lilivyo maarufu.
- Hata wanawake wa Kiyahudi walijaribu kumuua mtume rehema na amani ziwe juu yake. Katika vita vya Khaybari na baada ya kuukomboa kwa mapanga ya Waislamu. Mwanamke mmoja aitwaye Zainabu alitoa zawadi ya mbuzi aliyepikwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na akatia sumu, na hasa hasa katika mkono wa mbuzi. Kwa kuwa alisikia kuwa Mtume wa Allah anapenda sehemu hii ya mbuzi. Na pale Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipotaka kumla alisimama na akasema: Kwa hakika mkono huu unanieleza ya kuwa wenyewe umetiwa sumu. Na yule mwanamke akakiri suala hilo.

  Na matukio mengine yasiyokuwa haya yapo mengi. Nayo ni miongoni mwa yale yaliyoelezwa kwa wingi katika vitabu vya historia ya Mtume kuhusu msimamo wa Wayahudi dhidi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake na Waislamu kwa ujumla wao kama ilivyo katika:
- Vita vya Banii Qaynukaa, na maudhi yao kwa Waislamu kwa maneno na vitendo.

yote kwa kauli yake ﴿ **hapo kabla** ﴾. Kwa neno hili Quran imekata tamaa zao na kuuthibitisha moyo wa kipenzi chake. Kwani neno hili lilikuwa kama ahadi yake kwake kwamba atamlinda dhidi ya watu waovu. Hayo ukijumuisha na yale yaliyomo katika aya hizo miongoni mwa kuzindua juu ya asili ya maweko ya hayo maneno na juu ya kile kilichotengenezwa na asili hizo miongoni mwa huko kutoegemeza kiarifu kwa mtenda wake wa kweli kulikotajwa hivi punde katika ile sentensi na katika muundo.

(5) Na tazama namna matendo katika uovu unaofuata yalivyokuja kwa muundo wa kitenzi cha wakati uliopita baada ya kuwekewa neno hili: ﴿ **hapo kabla** ﴾**.** Basi historia ikasimama katika maweko yake ya kitabia pale ambapo hakukubaki haja ya maelezo kama yale ya mwanzo.

(6) Na tazama adabu za hali ya juu katika kuwasilisha uovu wa pili nao ni uovu wa ushirikina. Kwa hakika yake, pale uovu huu ulipokuwa mkubwa zaidi kuliko wa kabla yake, na ni wenye kukataliwa mno na akili. Basi hilo limetajwa kwa mtajo mzuri sana kwa kufuta moja ya nguzo zake. Kwa hiyo haikusema mmejitwalia ndama kuwa mungu. Bali huyu mtendwa wa pili amekunjwa kwa sababu ya kuona vibaya sana kulitaja wazi wazi katika mwambatano na wa mwanzo. Na kwa kubainisha kile kilichopo baina ya viwili hivyo miongoni mwa kutofautiana.. na katika kufuta huku kuna mengi mno miongoni mwa maelezo na kutisha!! Na huenda kunyamaza ndiko kunakotamka zaidi hukumu ya kitu, Na ni yenye ushindi mkubwa zaidi katika migogoro.

(7) Kisha tazama pande ambazo ndani yake zilitilia kipaumbele ujumla badala ya maelezo mapana. Zikikataa kila ziada isiyohitajika katika bayani kwa wakati huo. Kwa hakika yenyewe imesema kuwa Quran inasadikisha kile kilicho pamoja na wao. Lakini haijabainisha upeo wa huko kusadikisha: Je, ni katika misingi ya dini tu. Au katika misingi na matawi yote kwa

---

- Kuwachochea Makureyshi baada ya vita vya badri. Na Kaabu bin Ashraf kuwaombolezea wale waliouliwa miongoni mwa washirikina.
- Kunyanyasa kijinsia na kuwaongelea kimapenzi wanawake wa Waislamu katika mashairi.
- Shashu bin Qaysi na fitina zake baina ya Ausi na Khazraji. Mpaka wakakaribia kupigana vita.
- Salamu bin Mushkum ambaye ni Myahudi Kumpa makazi Abii Sufiyani. Na yeye kuwajulisha maadui udhaifu wa Waislamu katika vita vya Assuwayqu.
- Mchango wa ujumbe wa Wayahudi katika kupandikiza chuki kwa Makureyshi na makabila ya kinana, ghatwifani na mengineyo kwenda kuwapiga vita Waislamu katika tukio la khandaki.
- Maudhi kutoka kwa mashetani wa Kiyahudi: Kaabu bin Al-Ashraf – Salamu bin Abii Alhuqayqi – Abuu Afki na wngineo.

pamoja. Au katika misingi na baadhi ya matawi na mpaka ni wapi hasa? Hilo ni kuwa kwa hakika haya ni maneno ya wafalme hayateremki ila kwa kiasi maaluumu. Na mlinganiaji wa asili ya imani anamaanisha nini. Je, kukubaliana baina ya dini kupanuke hadi katika matawi au kusipanuke? Wataalamu wa sheria wafanye utafiti!

Na imesema, kwa hakika wao wanawaua Manabii wa Allah. Ni akina nani hao Manabii? … Wasomi wa kihistoria wafanye utafiti!

Na imesema kwa hakika Musa aliwaletea hoja zilizowaziwazi. Ni ngapi hizo hoja? Na ni zipi hizo?

Na imesema kuwa yenyewe imechukua ahadi nzito kwao wao. Je, hiyo ahadi nzito ilikuwa inahusu kitu gani?

Hakika hekima ya bayani ya Quran ni tukufu sana kuliko vile inavyoweza kuwasilishwa katika maelezo haya katika sehemu kama hii. Na lau kama ingetajwa hapa basi ingekuwa mfano wake ni mfano wa yule anayeulizwa: Kwa nini umempiga mtumwa wako? Naye aseme: Kwa sababu yeye amempiga kijana jina lake ni kadha na jina la baba yake ni kadha, na nguo zake ni kadha, na amezaliwa mwaka kadhaa. Hivi huoni kuwa hii ni ziada na nyingi sana[1]

(8) Na lau tungeenda na kufuatilia mambo mengine yaliyomo katika kipande hiki miongoni mwa maana nzuri basi tungetoka nje ya mipaka ya kuleta mfano na uzindushi tulioukusudia. Basi na tutosheke kwa kuyaelekeza macho yako katika siri ya kina ambayo hutoiona katika maneno ya watu. Hiyo ni kuwa mtu anapokuwa na umuhimu na jambo la kujilinda au kumtosheleza mwingine au mambo yasiyokuwa haya. Katika maneno yake kutadhihiri mguso fulani wa kuonesha hisia ya malengo yake. Kana kwamba

---

[1] Na kwa hili, maelezo marefu ya Imru`u Qaysi yalikosolewa kwa kuwa aliyaeleza katika sehemu isiyostahiki kutolea maelezo – na hayo yametokea katika kile kinachozingatiwa kuwa chenyewe ni miongoni mwa mashairi yake bora kabisa – na hiyo kauli yake ni:

*Simameni tulie kwa ajili ya kumkumbuka mpenzi na nyumba*
*katika eneo la Saqtwi Liwaa baina Dakhuuli na Fahaumili*
*Na kuweka wazi………………………………………………*
………………………………………………………………………

Hakutosheka katika kuielezea nyumba kwa kauli yake (eneo la Saqtwi Liwaa) mpaka akaiwekea mipaka minne. Albaaqalaaniyu amesema: (Kana kwamba yeye anataka kuuza nyumba, kwa hiyo anaogopa akikosea kuweka mipaka yake vizuri, kuuza kwake kusije kuwa batili na sharti lake nalo liwe batili!) [Daraazu].

athari yake kwa mambo hayo katika nafsi yako ipo kwa kiwango kile kile cha athari katika nafsi yake yeye mwenyewe. Kitabia au kujipamba na tabia hizo. Unakaribia kuhisi yale yanayopita moyoni mwake miongoni mwa furaha ya kupata kwake au miongoni mwa masikitiko ya kupoteza kwake. Bali utamuona anakaribia kufa kwa kusikitika lau kama watu watapuuza kumwongoza, endapo atakuwa anaamini jambo lake, na ana nia safi katika madai yake. Kama ilivyo kwa Manabii amani iwe juu yao. Ama hapa, kwa hakika wewe unapepesa macho, na nyuma ya maneno unaona nguvu ya juu isiyo na kuonesha hisia kwa matokeo haya. Nguvu inayoathiri na haiathiriki, inayokuelezea ukweli wa heri na wa shari kwa utukufu wa yule asiyenufaika na heri na kwa heshima kubwa ya yule asiyedhurika na shari.

Hii ni tabia ya kujivuna na kujitia ukubwa utaiona wazi wazi kupitia muundo mtindo huu wenye kutumia maneno machache katika hoja zake na wenye kuchukua na kurudisha, wenye kutumia maneno machache katika kueleza kwake kwa kusifu na kuponda.

Utazame pale unapojadili kuhusu Quran basi hauzidishi kuieleza kwa neno hili: ﴿**hiyo ni Haki** ﴾**.** Naam kwa hakika hilo ni neno linalojaza nafsi. Lakini, je neno hilo linakushibisha ewe mtu, pale unapotaka kueleza hakika miongoni mwa hakika ambazo wewe unazikubali na unapenda kuwakubalisha watu?

Na itazame Quran baada ya kusajili machafu ya machafu yote kwa Wana wa Israili. Nayo ni kule kumuweka kwao ng`ombe ambaye aliwakilishwa katika mji wao katika eneo la mtukufu mwabudiwa. Na baada ya kueleza ugumu wa roho zao katika kukataa kuziendea amri za Allah, pamoja na kwamba katika hilo wamebebeshwa aya za kutisha. Basi utayaona hayazidishi zaidi ya kusema katika sehemu ya kwanza: Kwa hakika hii ni ﴿ **dhulma** ﴾**.** Na katika ya pili: ﴿**ni mbaya zaidi** ﴾ mlichokifanya. Je, maneno hayo tu ndio kamaliza yote yaliyo mkabala wa maovu yao mengi? Naam, kwa hakika hayo ni maneno mawili yanayotosheleza kwa kiwango cha maovu hayo lau kama yangefahamika kwa njia zake. Lakini yapo wapi maumivu na machungu ya mihemko ya kulipiza kisasi? Bali ya wapi mapovu[1] na maneno ya kueleleza (kusimanga)? Na ya wapi matumizi ya fujo ya maneno na uovu unaouona katika maneno ya watu pale wanapochochewa kwa kuguswa heshima/nafasi zao?

[1] Povu: ni mineno michafu na mibaya.

Ni ya Allah tu! Kujizuia kulioje katika ugomvi huu! Na utukufu ulioje wa upande huu, na huu ndio upande wenye utajiri mwingi / uliotosheka, hauhitaji shukurani ya wanaoshukuru wala kufuru ya wanaokufuru!. Naapa kwa Allah kwa hakika maneno haya hayatokani na nafsi ya mwanadamu!

* * *

## [**Quran Yote Ni Ufupisho. Sawa Sawa Katika Sehemu Zake Za Ujumla Na Sehemu Zake Za Maelezo Ya Kina**]

Tumesema kuwa Quran Tukufu daima inawekeza kwa upole, kile kichache, kwa kadiri iwezekanavyo katika maneno ili kuzalisha maana pana kwa kadiri iwezekanavyo. Naam, Tukio hilo linadhihiri ndani ya Quran yote. Ni sawa sawa katika hilo kwenye sehemu za ujumla na ambazo watu huziita maeneo ya kufupisha. Na sehemu za maelezo mapana na ambazo watu huziita maeneo ya kurefusha. Na kwa ajili hiyo sisi tuniita ni ufupisho katika sehemu zote[1]. Kwa sababu sisi tunaiona katika sehemu zote mbili haivuki

[1] Pale Istilahi hii mpya ilipokuwa inaenda kinyume na istilahi ya kaumu yote, tumeona kuwa hatuna budi kuweka wazi sababu ya kwenda kinyume: Wataalamu wa Balagha (Umbuji wa maneno) wameyagawanya maneno kama ifuatavyo: (kusawazisha), (kufupisha) na (kurefusha). Na kufasili sawa ni kuleta maana kwa tamko la kiasi chake. na mafupi ni kuleta maana kubwa kwa matamko machache kuliko hiyo maana na yanayotosheleza. Na marefu ni kuleta maana kwa matamko mengi yaliyozidi maana kuu lakini kwa faida nyingine. Na wakajaalia kipimo cha kudhibiti mgawanyo huu ni swala la kimazoea au la kimaweko: Hivyo Assakaakiy amezingatia kipimo ambacho wanazungumza watu wa kati na kati katika mazungumzo yao na mazoea ya maongezi yao ndio kidhibiti cha kusawazisha. Nacho ni kiwango ambacho hakisifiwi wala hakishutumiwi katika mlango wa Balagha. Na yale yaliyopungua lakini yanatekeleza lengo basi hayo ndio kufupisha. Na yale yaliyozidi pamoja na kuleta faida basi hayo ndio kurefusha. Na maneno ya kibalagha/kiumbuji kwa hakika yanatukia katika ncha mbili hizi. Haya ndio majumuisho ya maneno ya Assakaakiy. Na kwa hakika amekubaliwa na wale ambao waliokuja baada yake katika kigawanyo hiki. Isipokuwa baadhi yao wameonelea kuwa, kujengea hili juu ya mazoea ndani yake kuna kurejea katika ujinga. Hivyo wakajaalia mpaka wa kusawazisha ni kiwango ambacho kinaleta maana ya mwanzo kwa maweko tena bila ya kuchunga matukio ya ziada juu ya asili ya maana.

Kwa hakika tumeshafahamu kutokana na maweko yao ya ugawaji juu ya msingi huu. Na kuzingatia kwao kusawazisha kwa moja ya hivi vipimo viwili vinavyoungana katika marejeo. Hakika wao wamedhani kuwa ibara ambayo inatekeleza maana ya mwanzo katika lugha za watu wa kawaida ndio daima inakaa baina ya kurefusha na kufupisha. Na hili halina ushahidi katika mazoea wala katika maweko. Ama la kwanza kwa hakika watu wa kawaida wanaongea kwa maana moja, wakati mwingine kwa kutumia matamko marefu, na wakati mwingine mafupi. Na kama hajapanga kupata kutosheleza katika kila moja katika hayo. Na ama la pili ni kwa sababu tamko ambalo limewekwa katika lugha ili kutoa maana ya mwanzo linatofautiana. Yapo miongoni mwayo yanayotekeleza kwa njia ya ujumla na mengine yanatekeleza kwa njia ya tamko

la kimaelezo. Na kila moja miongoni mwa ujumla na kimaelezo yanatofautiana yenyewe kwa tofauti nyingi. Kwa hiyo ikithibitiki katika mawili hayo kiwango maalum ambacho kitarejewa ili kujua ufupisho na urefusho. Kwani hakuna maneno mafupi ila inawezekana kutekeleza maana yake ya kiujumla kwa matamko machache kuliko matamko yake au kwa yale yanayokuwa sawa nayo hata kama hayatoshelezi kabisa wala kutekeleza kabisa. Hata mfano waliouchukulia kuwa ni kilele katika ufupisho. Nao ni kauli yake Mtukufu ﴿**Na mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi….** ﴾ Albaqarah 179. Inawezekana kuleta maana yake ya asili kwa kauli yako (lipa kisasa utasalimika) au (lipiza kisasa utakuwa hai) au kwa kutosheka na maneno mawili kati ya hayo (kisasi ni uhai). Bali kifunguzi cha Kitabu Kitukufu na ambacho kimekusanya makusudio yote ya Quran katika aya saba tu. Unaweza kuitekeleza maana yake ya asili kwa maneno matano tu 'ya Kiarabu': (Tunakushukuru Mola wetu na tunakuabudu na kukutaka msaada na kukuomba utuongoze) na kama ukitaka unaweza kwa maneno machache kuliko hayo.

Na hivyo hivyo husemwa: Hakuna maneno marefu ila unaweza kuyatekeleza maana yake ya kimaweko kwa njia maelezo katika matamko marefu kuliko hayo. Kwa kauli yake Mtukufu: ﴿**Na vitu vitakatifu viwekewe kisasi….** ﴾ Albaqarah 194. Huu ni ufupisho. Na ukunjufu wake umekuja katika kauli yake Mtukufu: ﴿**Na humo (katika Taurati) tuliwaandikia ya kwamba mtu (huuawa) kwa mtu, na jicho (hutofolewa) kwa jicho, na pua (hukatwa) kwa pua, na sikio (humeguliwa) kwa sikio, na jino (hung`olewa) kwa jino, na itakuwa kulipizwa kisasi katika kutiana majeraha…** ﴾ Almaida 45. Na maneno haya licha ya urefu wake yanazingatiwa kuwa ufupisho kama yatapimwa katika kauli yako katika mfano wa maana yake: (Atakayeiua nafsi naye atauawa kwa nafsi hiyo. Na atakayetofoa jicho atatobolewa jicho lake. Na atakayeimofoa pua atamofolewa pua yake. Na atakayekata sikio atakatwa sikio lake. Na atakayevunjwa jino naye atavunjwa jino lake... Na ukipenda zidisha: Mkono kwa mkono, kidole kwa kidole, na kupasuliwa kichwa kwa kupasuliwa kichwa, jeraha la kuonesha mfupa kwa jeraha la kuonesha mfupa .. na kuendelea). Na kauli yake Mtukufu ﴿**ila kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyotemshiwa na yale yaliyoteremshwa zamani…** ﴾. Maana imekuja ikiwa kwa upana katika kauli yake ﴿**Semeni: ''tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi chake, na pia yale waliyopewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao; …** ﴾ Albaqarah 136. Na maana hii kikawaida hutekelezwa kwa kauli yako: Tumemwani Allah na Quran aliyoiteremsha kwetu. Na taurati iliyoteremshwa na Allah kwa Musa, na Injili iliyoteremshwa na Allah kwa Isa, na Zaburi aliyoileta Allah kwa Daudi, na Suhufu zilizoletwa na Allah kwa Ibrahimu… Na lau ukitaka wahesabu hao vizazi kizazi kwa kizazi. Na taja wengine waliosimuliwa na Allah kwetu sisi miongoni mwa Manabii katika sehemu isiyokuwa hii. Bali Allah angetaka angetusimulia habari za Mitume wengine, zile ambazo hajatusimulia.

Na watu hawa kwa ndani wanakubali uwepo wa daraja mbili hizi katika maneno ya watu wa kawaida. Kwani walisema kwa hakika daraja la kufupisha kunakotia dosari na kurefusha kunakochosha kuwa hivyo sio katika Balagha hata kidogo. Kama mawili hayo hayawi katika maneno ya wanabalagha/wanaumbuji, basi yatakuwa ni maneno yasiyo ya kiumbuji bila shaka. Na kama si hivyo basi hayo yatakuwa ni maneno gani? Kwa hiyo maana za mwanzo na ibara za watu wa kawaida hazifai kuwa kipimo cha kudhibiti huo ukatikati wanaouweka.

Hili, kwa hakika kutokana na kipimo chao hiki cha ukati na kati kwa kipimo cha kile kinachotekelezwa na maana za mwanzo katika lugha za watu wa kawaida – baada ya kukubali kuwa hicho ndicho kipimo cha kati na kati – kimeanzisha kujaalia kuwa ubora

wa bayani katika mlango huu siku zote unaegemea katika ncha ya upungufu au ncha ya kuzidisha. Na hilo ni kinyume na kile kilichojengewa kanuni ya ubora miongoni mwa kushika kwake nafasi ya kati na kati baina ya ncha hizo (na kwa hakika tumeshangazwa! Pale ninapowaona wao wanarejea, na kuuingiza usawasawa katika maneno ya mtu mwenye umbuji kama hilo litahitajika na hitajio. Kama vile maneno yake yakiwa anaongea na watu wa kawaida. Kisha ajabu yako itazidi pale ukiwaona wanayaingiza hayo katika Quran yenyewe. Na hiyo Quran kama ulivyoijua ni kuwaeleza watu wa kawaida na watu wa kipekee kwa sawa sawa. Na wanaitolea mfano kwa kauli yake Mtukufu ﴿ **Na vitimbi vibaya havimteremkii ila yule aliyevifanya…** ﴾ Fatir 43. Ya kwamba katika neno hili kuna ufupisho kwa kufuta kwa mujibu wa istilahi yao yenyewe. Kwani maana ni kuwa madhara ya vitimbi vibaya na hatima yake haviteremki) .

Kwa ajili ya haya yote tumeona tuweke maweko mengine ya vigawanyo. Na katika hayo tunarejesha ubora katika fungu lake la upeo wa kati na kati. Na kurejesha shutuma kwa zile ncha mbili. Na hilo linajaalia kipimo ndio kiwango ambacho kinatekeleza maana kwa ukamilifu wake, kwa asili yake na mapambo yake juu ya hesabu ya yale yanayoitiwa na maqama (tukio) miongoni mwa kujumuisha au kueleza kwa upana. Bila ya kujikakamua wala kutumia maneno kwa fujo. Kiwango hiki – ndicho ambacho atakayekipunguza au kuzidisha, watu wa umbuji watamuhesabu kuwa amekengeuka na kiwango stahiki kwa kadiri ya vile alivyopunguza au kuongeza – chenyewe ndio mzani sahihi ambao wewe una haki ya kuzisema ncha zake mbili kwa haki kama zimepunguza au zimerefusha. Na kwamba kukiita hicho kuwa ni usawasawa au kusudio au kati na kati, au kadirio au kile unachopenda basi kiite. Na sisi pia tumeshakiita kwa jina la (Ufupisho) tukiwa tumetulizana juu ya usahihi wa jina hili. Pindi tutakapoona fasili ya ufupisho inaendana nayo.

Kwani ufupisho si vingine ila ni uharaka na kurahisisha katika kufikia haja kwa kiwango kinachowezekana. Yule anayeharakisha zaidi ya uwezo wake hakufikishi katika haja zako na kwa hiyo kutaabisha na kuwa yenye dosari. Na yule anayechelewa sehemu ya kuharakisha hatokuwa vingine ila ni mtumiaji wa fujo mwenye kuchosha. Na tumewaona watu wakiendelea kuhusiana kwa ufupisho huu katika bayani na kuyafanya maneno bora kuwa ni yale mafupi na kuleta maana. Mpaka ilipokewa kutoka kwa bwana wa umbuji rehema na amani ziwe juu yake na aali wake ya kwamba alimwambia Jariiri bin Abdullahi Albajaliy: **‘‘Ewe Jariiru pale utakaposema fupisha. Na utakapofikia haja yako usijikalifishe’’.** Na kwa sasa nimeihifadhi hadithi hii hivi hivi, na haunijii ufafanuzi wa wapokezi wake. Na hatujawahi kumsikia mtu yeyote anayeusia kufuatwa kwa huu urefushaji ambao, watunzi wameuzingatia kuwa ni ubora wa pili unaokabiliana na ufupisho. Na kwa hakika wenyewe ni moja ya matawi yake mawili: ufupisho wenye kufahamisha au urefushaji wenye kukuza. Na lau tungeuita ubora wa pili wenye kukabiliana nao. Basi tungechelea mkabala huo peke yake kuwa ni ruhusa katika uchambuzi miongoni mwa vizuizi vyake na kusameheana katika kufanya wingi ambako kumekuja katika kuushutumu kwa kila lugha. Mpaka Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: **‘‘…. Kwa hakika wenye kubughudhiwa zaidi kwangu mimi na waliombali zaidi na mimi kwa makao siku ya kiama ni wale wenye tabia mbaya zaidi kwenu, waongeaji sana waropokaji na waongeaji sana’’**. Imepokewa na Ahmad na Ibnu Hibbaani na wasiokuwa wawili hao kutoka kwa Abuu Thaalaba.

Sivyo hivyo! Nakuapia kwa Mola wako kwa hakika huo ni ubora mmoja unaomtaka muongeaji katika kila tukio. Na huchukuliwa kwa hilo katika upana wa maelezo, kama inavyochukuliwa katika ufinyu wa ujumla. Bali huenda wenyewe upo katika tukio la maelezo ya kina yanayohakikisha matakwa, na jambo la kupatwa kwa ugumu. Basi maneno marefu kama kila sehemu yake itakuwa na faida inayoguswa na

njia kusudiwa. Wala haiegemei katika kufanya matumizi ya fujo hata kidogo. Na tunaona kuwa malengo yake katika sehemu zote mbili, haiwezekani kuyafanya kwa ukamilifu wa nukta zake zote na kuyapamba kwa kutumia maneno mengine machache kuliko maneno yake, wala yale yanayokuwa

---

haja katika eneo hilo. Wala haiwi wepesi kuleta maana faida hiyo kwa maneno machache kuliko hayo basi itakuwa hayo yatakuwa ndio ufupisho wenyewe unaotakiwa. Na kama itawezekana kutekeleza malengo kwa ukamilifu kwa kufuta kitu fulani katika maneno hayo au kwa kubadilisha ibara fupi kuliko hiyo basi itakuwa hayo ndio ziada isiyo na maana au kurefusha kwenye kutia aibu. Na maneno mafupi kama yatatekeleza makusudio ya asili na ya kukamilisha yenye kunasibiana katika kila hali basi hayo yatakuwa ndio ukati na kati unaotakiwa. Na kama si hivyo basi yatakuwa ni kukatika au upungufu wenye kutia aibu.

Si ufupisho wenye upungufu katika upande wa ujumla kama walivyodai mpaka wakajengea juu yake yale waliyoyajengea. Na hata wakayatoa miongoni mwayo mfano wa kauli yake Mtukufu: ﴿**Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na (katika) kuandamizana usiku na mchana, na (katika mwendo wa) vyombo ambavyo hupita katika bahari…. ﴾.** Albaqarah 164. Wameijaliia aya hii kuwa ipo katika mlango wa kurefusha kwa hoja kuwa yenyewe inawezekana kuifupisha kwa ibara hii: (Hakika katika kutia nguvu kutokea kwa chochote kinachowezekana kimekuwa katika kutokutokea kwake kuna alama kwa wenye akili – Miftaahu Al-uluumi). Na wewe, je,umeshawahi kumsikia mwarabu mwenye umbuji au asiye na umbuji akiongea kwa namna hii ya kifalsafa iliyo kavu yenye kutia kihoro, ambayo imefikiriwa na Assakaakiyu na kuifanya ndio kipimo cha usawa katika maana ya aya… Sivyo hivyo, kwa hakika wewe lau kama utarejea katika kile kilichozungumzwa na watu katika aya za Allah za maumbile zilizo kwa maelezo mapana au kwa ujumla basi ungeona maneno sahihi ya warabu yakiwa marefu zaidi au mafupi zaidi kuliko haya. Na ungeiona hiyo aya tukufu yenyewe ndio maneno ya ufupisho zaidi na madhubuti zaidi kimfumo katika mlango wake katika maelezo. Kama vile kauli yake Mtukufu: ﴿**Sema: ''Tazameni nini yanayotokea katika mbingu na ardhi … ﴿** Yunus 101. Maneno haya ni maneno mafupi zaidi katika mlango wake kuliko kueleza kiujumla.

Tumesema kwa hakika ubora wa ufupisho kwa maana yake sahihi ni ukati na kati wa uadilifu. Nao ni ubora wa pekee ambao watu wa umbuji wanauusia katika kila tukio kwa mujibu wake. Isipokuwa mambo yalivyo mwanadamu hapati kile anachotamani. Kwani mfano kamili hata kama umenyanyuliwa shingo za watu na wakatofautiana katika kuitafuta kwa ukaribu na umbali, hakuna hata mmoja miongoni mwao anayeweza kuleta na kufikia lengo lake. Na hakika si vinginevyo hayo, ilipewa Quran Takatifu. Nayo ndio kiigizo chema cha hali ya juu katika uzuri wa ufupisho. Kivipi isiwe hivyo hali ya kuwa hiyo Quran ndio mpaka wa ufupisho [Daraazu].

- Nimesema: hadithi ya Jariiri : **''Ewe Jariiru utakaposema…''** Sijaikuta katika rejea zilizo mikononi mwangu. Ama hadithi **''Kwa hakika mwenyekubughudhiwa zaidi kwangu mimi …''** Imepokewa na Ahmad 4/193 – 194. Mawaaridu Adhwamaani 1917, Al-Ihsaanu 482. Na imepokewa na Attirmidhiyu katika Albirru na Asswilatu 2018 kutokana na hadithi ya Jaabiri. Na Albaaniyu ameipa daraja ya Hassan katika Asswahiiha 2/390 ya Shawaahidu zake. Na Al-Arnaauutwu ameipa daraja la sahihi katika Al-Ihsaanu 2/232.

sawa nayo. Ndani yake hakuna neno ila lenyewe ni ufunguo wa faida tukufu. Na ndani yake hakuna herufi ila imekuja kwa maana maalum.

### [Katika Quran hakuna Maneno Ya Kukurupuka, Wala Herufi Za Maana Zilizozidi]

Achana na kauli za yule ambaye anasema kuhusu baadhi ya maneno ya Quran kuwa yenyewe ni (ya kukurupuka) na katika baadhi ya herufi zake za maana kuwa zenyewe ni za (ziada), ziada ya kimaana. Na achana na kauli ya yule ambaye anabeza neno la (kukazia) na kuyavurumisha maneno hayo katika kila sehemu anayodhania kuwa ndani yake kuna ziada. Hajali kuwa ziada hiyo ndani yake kuna maana ya ziada inayofaa kukazia au haipo. Na hajali kuwa hiyo sehemu ina haja ya mkazo huo au haina haja nao.

Naam, achana na hili na hilo. Kwa hakika ya hukumu katika Quran kwa aina hii ya ziada au inayofanana naye, kwa hakika yenyewe ni aina ya ujinga – uliositiriwa au uliofunuliwa – kwa kina cha mizani iliyowekewa muundo mtindo wa Quran.

Hebu itumbukize nafsi yako katika kutafuta siri za kibayani katika mwangaza wa taa hii. Kama utapofuka na kutoona namna ya hekima ilivyo katika neno au herufi katika taa hii. Ole wako na kufanya pupa, kama walivyofanya pupa hawa wenye kudhani. Lakini sema kauli ya sawa sawa, nalo ndilo jambo dogo katika uaminifu na uadilifu. Sema: (Allah ndiye mjuzi wa siri za maneno yake. Na sisi hatuna elimu ila kwa yeye kutuelimisha). Kisha ole wake ubweteke na raha za kukata tamaa, na ukae na kuacha kutafuta siri hizo huku ukisema: Mimi ni wapi na wapi na fulani na fulani? .. Sivyo hivyo. Huenda mdogo aliyefadhilishwa akatambua kile ambacho hakijatambuliwa na mkubwa mwenye ubora. Hivi huoni katika kisa cha Ibnu Omar katika kitendawili[1] mashuhuri[2]? Jitahidi kutafuta na sema: Ewe Mola

---

[1] Kitendawili: swali au fumbo ambalo linahitaji werevu wa msikilizaji ili ajue jibu la sawa.

[2] Mtume rehema na amani ziwe juu yake alisoma kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri;…** ﴾ Ibrahim 24. **Akasema: hakika katika miti kuna mti usiopukutisha majani yake. na hakika mti huo ni kama mfano wa muislamu. Nielezeni ni mti upi huo? Elimu ya mti huo ikafichikana kwa watu hao, wakawa wanataja aina mbali mbali za miti ya jangwani. Na Ibnu Omar alifahamu kuwa mti huo ni mtende. Na alikuwa wa kumi kati ya watu kumi waliokuwepo. Naye ndiye mdogo wao kiumri. Na ndani yao kuna Abuu Bakri na Omar. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: huo ni**

wangu nizidishie elimu. Huenda Allah akakufungulia mlango wa fahamu utakaokuvumbulia kitu fulani miongoni mwa vile wenzako walitiwa upofu kwavyo. Na Allah ndio msimamizi wa wale walioamini, anawatoa kutoka katika kiza na kuwapeleka katika nuru.

### [Siri Ya Herufi Kafu Katika Kauli Yake Mtukufu: ﴿Hakuna Chochote Mfano Wake ﴾]

Na tunakupigia mfano. Kauli yake Mtukufu: ﴿**Hakuna chochote mfano wake''**﴾. Ash-shuura 11.

Wenye elimu wengi neno lao limefanana katika kueleza kuwa herufi kafu ni ziada. Bali wamekubaliana juu ya ulazima wa kuwa hiyo kafu imezidi katika sentensi hii. Na huko ni kukimbia muhali wa kiakili. Na kuona kuwa kubaki kwake kunapelekea kuondoka maana yake ya asili ile ya tashibiha. Kwani wao wameona kuwa hiyo kafu kwa wakati huo itakuwa inakanusha kinachofanana kilicho kama Allah. Na kwa hiyo itakuwa ni kukubali kuthibiti kwa mfano wake yeye Mtukufu aliyetukuka. Au kwa uchache inawezekana kuthibitika kwake na kutothibitika. Kwa sababu ukanushi (hasi) – kama wasemavyo wataalamu wa Mantiki (logic) – unasadikisha kutokuwpo kwa kiima. Au[1] kwa sababu ukanushi – kama wasemavyo wanazuoni wa sarufi (Nahau ya Kiarabu) – huenda ukaelekezwa kwa neno lenye kufungwa na kufungo chake kwa pamoja. Unaweza kusema: (Fulani hana mtoto anayemsaidia) kama hana mtoto kabisa au akiwa na mtoto lakini hamsaidii. Na unasema: (Muhammad si ndugu wa Ali) endapo huyo Muhammad ni ndugu wa mwingine asiyekuwa Ali au endapo huyo Muhammad hana ndugu hata mmoja.

(Na wachache miongoni mwao) waliopita mapito ya kuwa hakuna ubaya wa kubakia kwa hiyo kafu katika uasili wake. Kwani wameona ya

---

**mtende''**. Hiyo hadithi imepokewa na Asshaykhaani. Na katika Quran ﴿**Tukamfahamisha Suleimani….** ﴾ Al-Anbiyaa 79. [Daraazu].

- Nimesema: Imepokewa na Bukhariyu katika Al-Ilimu 61, 62 na katika Attafsiiri 4698. Na Muslimu katika Swifaati Almunaafiqiina wa Ahkamuhum 63, 64. Na katika Swahihi mbili hakujakuja kusomwa kwa aya hiyo mwanzoni mwa hii hadithi. Lakini Alhaafidhu ameitaja katika Alfat-hi 1/177 ya kwamba aya hiyo ipo kwa Albazzaari.

[1] Maelezo hayo yamejengwa kwa kuzingatia kuwa madhumuni ya sentensi au kilichotamkwa na hiyo sentensi. Kwa ya kwanza (madhumuni) hapo neno mfano linakaa sehemu ya kiima, kwa sababu lenyewe lina nguvu ya kauli yetu: (Mfano wake hauna mfano). Na kwa ya pili (kilichotamkwa) neno mfano linasalia kuwa kiarifu kwa kuwa lenyewe limekaa sehemu ya kiarifu ncha neno laisa (sio).

kwamba hiyo kafu haipelekei katika muhali huo, si kwa maandiko wala kwa uwezekano. Kwa sababu kukanusha mfano wa mfano kunafuatiwa katika akili na ukanushi wa mfano pia.

Na hilo ni kwamba, lau kama kungekuwa na mfano wa Allah basi kwa mfano huo kungekuwa kuna mfano wake bila ya kupepesa. Naye ni Allah mwenyewe wa haki. Kwa hakika kila wafananao wawili, basi kila mmoja wa wawili hao anazingatiwa kuwa ni mfano wa mwenzake. Na kwa hiyo, mfano wa mfano hautotimia kutoweka kwake ila kwa kutoweka mfano wa mfano na hilo ndilo jambo linalotakiwa.

Na ufupisho wa maelekezo haya – lau ukiyatafakari – ni kuwa yenyewe yanasahihisha na hayatii nguvu. Yaani yenyewe yanakanusha madhara ya herufi hii. Lakini yenyewe hayathibitishi faida yake wala hayabainishi haja kuu ya kuwa na herufi hiyo. Hivi huoni kuwa kinachotekelezwa na maneno yakiwa na hiyo kafu ni kama vile yanavyotekelezwa yakiwa bila ya kafu kwa sawa sawa. Na kwamba yeye hata kama imezidi kiasi fulani, kwa hakika imezidi kwa kiasi fulani cha kujikalifisha na kuzunguka. Na aina fulani ya kupofusha na kuleta utata. Na je hakuna njia yake ila njia ya yule ambaye alitaka kusema: (Huyu ni fulani), akasema: (Huyu ni mtoto wa dada wa halo (mama mdogo au mama mkubwa) wa fulani)? Kwa hiyo marejeo yake ni katika kauli ya kuzidi kwa kafu wanayojistiri nayo kwa jina la kukazia. Jina hilo ambalo huijulikani muitwa wake kwa hapa. Kwa hakika kukazia mfananishwa sio makusudio kabisa kabisa. Na kukazia ukanushi kwa herufi kunajulisha juu ya tashibiha nayo ni katika uwepo sehemu.

Na lau ukirejea kidogo katika nafsi yako utaona herufi hii ipo katika eneo lake ikiwa imehifadhi nguvu ya maana yake. Imesimama sehemu tukufu katika maana iliyokusudiwa katika sentensi yake. Na kuwa yenyewe lau kama hiyo herufi itaporomoka katika hiyo sentesi basi nguzo za kimaana nazo zengeporomoka pamoja naye au nguzo moja ingevunjika katika nguzo zake. Na sisi tunakubainishia hili katika njia mbili. Moja wapo ni ya mapito ya kina zaidi kuliko nyingine:

**(Njia ya kwanza):** nayo ni ya chini zaidi kati ya njia mbili hizo kwenda katika ufahamu wa wasomi wengi. Na kuwa yenyewe lau ingesemwa (Mfano wake hakuna chochote) hilo ingekuwa ni lenye kukanusha mfano wa sawa sawa. Nao ni mfano uliofanana kikamilifu tu.

Kwani maana hii ndio ambayo inaendana na ufahamu wa tamko mfano linapoachiliwa. Na kwa hiyo katika nafsi kungepita mpito wa shaka na kufahamu vibaya: huenda kuna daraja, lisilofanana na daraja la uungu lakini lenyewe linalifuata. Na huenda cheo hiki kikawa cha Malaika na Manabii. Au cha sayari na nguvu za kimaumbile. Au cha majini, masanamu na makuhani.

Kwa hiyo itakuwa kwa wao mbele ya Mungu wa kweli wana kushabihiana kwa kiasi fulani katika uweza wake au elimu yake. Na ushirika ndani ya yaliyomo katika uumbaji wake au amri zake. Kwa hiyo maweko ya herufi hii katika maneno haya ni kuuondoa ulimwengu wote na kufanana, kushabihiana na kufanana na kile kinachokaribia navyo. Kana kwamba anasema: hakuna kitu kinachofanana kuwa kama mfano wa Allah, zaidi ya kuwa na mfano wake kwa hakika. Na mlango huu wa kuzindua cha chini kabla ya cha juu, kupo katika mipaka ya kauli yake Mtukufu: ﴿**Basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee…** ﴾**.** Bani Israil 23. Ni kukataza maudhi madogo sana ya wazi wazi, na yale yaliyo juu ya hicho kichache yanaingia kwa njia ya kustahiki zaidi.

**(Njia ya pili)**: Nayo ni njia ya kina zaidi kimapito kati ya njia mbili hizi. Ya kwamba makusudio ya mwanzo katika sentensi hii ni kukanusha mshabaha. Hata kama unatosha kuileta maana hiyo kwa kusema: (hakuna kitu kilicho kama Allah) au (hakuna chochote mfano wake). Lakini kiasi hiki chenyewe sio kila kinachokusudiwa na hiyo aya tukufu. Bali hakika hiyo aya, kama inavyotaka kukupatia hukumu hii pia kwa wakati huo huo inataka kuelekeza katika sura ya hoja yake na njia ya hoja yake kiakili.

Hivi huoni ya kuwa wewe pindi unapotaka kumkanushia mtu upungufu katika tabia yake na ukasema: (Fulani haongopi wala hafanyi ubahili). Utakuwa umeyatoa maneno yako katika matokeo ya madai yasiyo na ushahidi wake. Na ukizidisha neno na kusema: (mfano wa fulani haongopi wala hafanyi ubahili) kwa hivyo hutokuwa umemwashiria kwa mtu mwingine anayefanana na ambaye ametakasika na upungufu huo. Bali huu utakuwa utakaso wake yeye kwa ushahidi wa yote. Nao ni kwamba yule anayekuwa na sifa kama zake na mwenendo wa ukarimu hawi hivyo. Kwa sababu ya kuwepo kukataana baina ya tabia za sifa hizi na baina ya huo upungufu unaodhaniwa.

Kwa njia hii ya kiumbuji umeiweka aya hiyo ya hekima kwa kusema: (mfano wake Mtukufu hauwi na mfano). Ukimaanisha kuwa mwenye kuwa ana sifa hizo nzuri na huo mfano wa kuigwa haiwezekani awe na mshabaha. Wala haiwezekani kuwepo wawili walio wa namna yake. Hakuna shaka katika hilo kumeletwa matamko mawili kila moja kati yao linatekeleza maana ya kufanana. Ili moja wapo lisimame kama nguzo ya madai na lingine ni kitia nguvu madai na hoja ya madai. Kwa hiyo tashibiha iliyojulishwa (na kafu) pale ilipolenga ukanushi umetekeleza asili ya upweke unaotakiwa. Na tamko (mfano) lililotajwa wazi katika tukio la tamko tukufu au kiwakilishi chake limezindua juu ya hoja ya takwa hilo.

Na jua kuwa hoja ambayo inaongozwa na hiyo aya kwa njia hii ni hoja tamu katika kuthibitisha upweke wa Muumba na hatumjui yeyote miongoni mwa wataalamu wa elimu ya maneno (wanafalsafa na wanamantiki) aliyeogelea katika hili. Kwani hoja zao zote zipo katika kuhusu upweke uliosimama kwa kubatilisha wingi kwa kubatilisha lazima zake na athari zake kiutendaji. Kwa mujibu wa ilivyoongoza kauli yake Mtukufu: ﴿**Lau kama wangalikuwapo humo (mbinguni na ardhini) waungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu: bila shaka zingeharibika (hizo mbingu na ardhi)[1]…** ﴾. Al-Anbiyaa 22.

---

[1] Na sisi hapa tunakufupishia njia za kutolea ushahidi wao katika mfumo mmoja. Ili ibainike kuwa njia zao zote ni zenye kusimama juu ya msingi wa maana uliochimbuliwa kutoka katika aya hii. Nao ni kuwa waungu wengi wenye kujumuisha masharti ya uungu hilo litapelekea:

- Ima kutokuwepo kwa kitu chochote miongoni mwa viumbe, na huo ndio uharibifu wake wakati wa uwepo.
- Na ima uwepo wa viumbe kwa njia ya kutofautiana na kuhitilafiana kunakopelekea kuharibika kwake mwishoni mwa uwepo.

Hilo ni kuwa lau matakwa ya waungu wawili yangeelekea katika kitu kimoja basi ingekuwa vigumu kwao kukizusha kwa sababu ni muhali/jambo lisilowezekana kuanza athari moja kutoka katika viathiri viwili. Na kauli ya kusema kuwa kitaanza kwa uwezo wa mmoja wao pamoja na kuwa wote ni sawa katika uweza na katika kuelekeza lengo basi huko ni kuupa nguvu upande mmoja bila kuwa na hoja ya kuupa nguvu. Na lau matakwa ya mmoja wao yakaelekea katika kitu na matakwa ya mwingine yakaelekea katika kinyume chake basi hao wawili hawatokitoa. Na kama si hivyo basi vingekutana vinyume viwili. Na kukitoa kimojawapo bila ya kingine inalazimisha huko kutia nguvu kulikotajwa. Na lau matakwa ya mmoja wapo yangeelekea katika baadhi ya kiumbe na nyingine kwa baadhi nyingine. Kwa hiyo kila mungu angeenda na kile alichokiumba. Na kungekuwa na ulimwengu wa aina mbili wenye kutofautiana kimifumo, na hautopita muda hiyo mifumo itashambuliana yenyewe kwa yenyewe ili kufutana. Na yote hayo ni batili kwa kushuhudiwa. Kwani tunaona ulimwengu umepatikana bila kuharibika na unaendelea bila kuharibika. Na tunauona unakusanya sehemu zake na juu ya tofauti ya

viungo vyake na maweko yake ya juu na ya chini, ya heri na ya shari. Yote yanatekeleza kazi ya mwili mmoja ambao viungo vyake vinaosaidiana kwa kila kimoja na kazi yake iliyo tofauti katika kulifikia lengo moja. Na umoja huu katika mfumo wa matendo ni ushahidi juu ya umoja wa mtenda mwenye kuupanga Mtukufu Aliyetukuka [Daraazu].

**Ufafanuzi usio na Budi Ili Kubainisha Uharibifu Wa Falsafa, Mantiki Na Elimu Ya Maneno Katika Usamehevu Wa Uislamu Na Wepesi Wake**

Katika jambo linaloumiza nafsi na kukibana kifua ni kuwa wanazuoni wengi wa umma huu – badala ya kuelekeza muda wao mwingi na juhudi zao kubwa katika Quran Tukufu na kuzizingatia aya zake na kuchimbua maana zake zilizojificha. Na kufahamu mifano yake iliyopigiwa wenye akili. Na kutoa kanuni za kiitikadi kutoka katika Quran Tukufu na Sunna za Mtume zilizo sahihi – wao wameenda katika falsafa na mantiki ya Kiyunani (Wagiriki wa kale). Na wamejaribu kuitiisha ili iitumikie Uislamu – kwa madai yao – na licha ya kwamba mara nyingi hili kwao wao lilikuwa kwa nia njema, ila kwa hakika kuingia kwa falsafa na mantiki ya Kiyunani katika elimu ya Tauhiidi (kumpwekesha Allah), na wasomi hawa kujenge hoja na kuulinda Uislamu kwa kutumia hoja hizi za kimantiki zilizojengwa juu ya mantiki ya Kiyunani, kwa hakika umeleta majanga katika umma kwa pande nyingi, na za muhimu zaidi ni:

1- Kuziondoa nafsi za watu katika kutilia umuhimu tauhiidi waliyotumwa nayo Manabii wote: nayo ni tauhiidi ya Allah katika ibada na kuacha kila kile ambacho kinaabudiwa kinyume naye. Na kuwakufuru matwaghuuti na miungu inayoabudiwa na makafiri na washirikina kinyume na Allah. Mwenye kufuatilia maneno ya wasomi wa elimu ya Kalamu (Maneno ya kimantiki) na wanafalsafa atapata kuwa wao wanatoa juhudi zao zote kuthibitisha uwepo wa Muumba. Wala hawatilii umuhimu juu ya kumpwekesha Mungu katika ibada. Hili linafanyika licha ya kuwa lenyewe ndilo ambalo Manabii wote wameletwa kwa ajili yake. Na kwa hakika Allah ameziangamiza nyumati zilizopita miongoni mwa wale waliofanya kibri na kuwakataa Mitume yao pale walipowaita kumwabudu Allah peke yake. Na ama kuthibitisha uwepo wa Muumba, hilo halikuwa na mgogoro hata kwa waabudu masanamu miongoni mwa Warabu ambao Allah aliwaelezea: ﴿**Na kama ukiwauliza ''Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalitilisha jua na mwezi?'' Bila shaka watasema, ''Mwenyezi Mungu''. Wapi basi wanakogeuziwa?** ﴾ Al-Ankabuuti 61. Na hakika si vinginevyo ushirikina wao ulikuwa katika kujitwalia vitu vya kati vya kuwakurubisha wao na Allah kwa madai yao. Na kwa jambo hili unakaribia kutoona athari yake katika vitabu vya wanakalamu.

2- Kuondoa mtazamo kutoka katika hoja za Quran zilizo nyepesi kuingia nafsini, na kuelekea katika takalifu (kujilazimisha) za kimantiki zenye ugumu kufahamika, jambo ambalo limeathiri sana katika kuleta utata katika itikadi ya Kiislamu. Allah amrehemu Ibnu Taymiya pale aliposema: (Kuingiza ufundi wa Mantiki katika elimu sahihi kunarefusha ibara na kuziweka mbali ishara zake, na kile cha karibu katika elimu kukifanya kuwa mbali. Na kile chepesi miongoni mwake kuwa kigumu. Na kwa ajili hii utamkuta mtu anaiingiza hiyo Mantiki katika fani tofauti; elimu ya maneno, misingi ya fiqihi na zisizokuwa hizo. Hiyo mantiki haijaleta faida isipokuwa wingi wa maneno (kalamu) na mipasuko pamoja na uchache wa elimu na uhakiki). Naqdhwi Almantwiqi (Yaani kutengua Mantiki) Uk 169. Majumuu Alfataawaa 9/24. Na vile vile, Allah amrehemu akasema: (Mantiki ya

Kiyunani haihitajiki na mtu mwerevu, wala haimnufaishi goigoi) Majumuu Alfataawaa 9/82.

3- Wanafunzi na wanazuoni wengi wamejiweka mbali na kuchukua moja kwa moja kutoka katika kitabu cha Allah na sunna za Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake, na kutafuta uongofu katika Mantiki ya wayunani ambao hawajateremshiwa ufunuo wa Mungu na wala hawajapata mwanga wa nuru ya utume.

4- Kuufarakanisha umma wa Kiislamu: ambapo bidaa nyingi, upotofu na matamanio ya nafsi vilivyodhihiri katika historia ya Uislamu vilikuwa kwa sababu ya falsafa na Mantiki ya Wayunani. Ima kwa kuzusha bidaa au ima kwa kuithibitisha na kuongeza utata. Na kwa sababu ya majaribio ya watu wa matamanio ya nafsi ya kukusanya baina ya Uislamu na huu upuuzi. Jambo ambalo limepelekea kuutenganisha umma na kumwaga damu na kuamsha fitina. Na huyu ni Abuu Haamidi Alghazaali anatoa ushuhuda wa kile kilichozaliwa kutokana na (kufungua mlango wa kuzama katika elimu ya maneno, miongoni mwa ubaguzi mbaya na magomvi yaliyotapakaa yanayopelekea katika kumwaga damu na kuharibu miji) أ هـ . Ihyaau Uluumi Diini 1/71.

5- Kuibadili dini ya Allah na hasa hasa itikadi ya makundi ya matalasimu na vitendawili visivyofahamika ila na yule aliyejitumbukiza katika hayo na kujifunza mantiki ya kiyunani. Jambo hilo lilipelekea wanazuoni wengi kutumbukia katika falsafa na mantiki ya kiyunani. Na hilo liliathiri vitabu vyao na maneno yao. Yakawa ugonjwa mzito wenye utata na kuchukiza. Na hili kwa nafasi yake limepelekea kwa wanazuoni kujitenga na waislamu wa kawaida miongoni mwa wale wasioshughulika na mantiki. Na hayo yametokea baada ya wote kuwa wanayafahamu maneno ya Allah na maneno ya Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake. Elimu ingefungika kwa wanazuoni waliobobea katika Mantiki. Na wanazuoni wakawa wanaandika na kujifunza kwa ajili ya nafsi zao. Na waislamu wa kawaida wapo katika bonde lengine hawajihusishi nao kabisa kabisa. Jambo lililozidisha ujinga katika umma.

6- Kuangamiza juhudi zao katika mambo yasiyokuwa na faida kiimani. Na kuacha kujitakasa na kutenda matendo mema na kueneza Kitabu na Sunna kama ulivyokuwa mwenendo wa salafi (wema waliotangulia) wa umma. Na kuvibadilisha kwa qiyaasi (vipimo vya kimantiki), tofauti, falsafa na kutembea ovyo ovyo katika kuzurura ndani ya upotofu unaoitwa falsafa. Bila ya mwongozo na kuacha nuru ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu.

7- Kuzihalifu nasaha za umma za kujiepusha na elimu ya kalamu na matamanio ya nafsi:

Imamu Shafii (Allah amrehemu) amesema:

- Kwa hakika nimepitia kwa watu wa elimu ya kalamu, Naapa kwa Allah katu sijaifahamu vibaya, na kwa mtu kujaribiwa kwa yale yote yaliyokatazwa na Allah isipokuwa kumshirikisha Allah, ni bora kwake kuliko kujaribiwa na Allah kwa kupewa elimu ya kalamu.
- Kila anayeongea kwa Kitabu na Sunna basi huyo ndiye yupo katika upeo unaotakiwa, na kila muongeaji bila ya asili ya Kitabu wala Sunna basi huyo yupo katika maruweruwe.
- Hukumu yangu kwa watu wa elimu ya kalaamu ni kwamba wapigwe kwa makuti ya mitende na waburuzwe na ngamia na kuzungushwa mitaani kwa koo na makabila, na watangaziwe: haya ni malipo ya mwenye kuacha Kitabu na Sunna

na kuelekea katika elimu ya kalamu. (Manaqibu Asshaafiiyi: Albayhaqiyu 1/452 – 470).

Na Imamu Ahmad amesema:

Atakayependa elimu ya kalamu hatofaulu. Kwa sababu elimu hiyo inayapeleka mambo yao katika kutahayari. Shikamaneni na sunna na hadithi na jiepusheni na kujitumbukiza katika mijadala na kujionesha. Tumewadiriki watu na hawakuwa wakijua hii elimu ya kalamu. Hatima ya elimu ya kalamu haipelekei katika heri. (Sayru Aalaamu Annubalaa 11/291).

Na Alghazaaliy katika Hukumu ya kujifunza mijadala na elimu ya kalaamu) amesema:

Shafii, Maliki, Ahmad bin Hanmbali, Sufian na watu wa hadithi wote miongoni mwa wema waliotangulia wamefuata madhehebu ya kuharamisha kusoma elimu ya mijadala (kalamu). Na kile kilichonukuliwa kutoka kwao cha kukazia hili hakidhibitiki kiidadi. [kisha akataja hoja ya wasemao kuwa elimu ya kalamu ni nzuri, na kisha akasema] Kwa hakika katika elimu hiyo kuna manufaa na madhara. Basi yenyewe kwa kuzingatia manufaa yake wakati wa kunufaika nayo basi ni halali au suna au wajibu kama inavyotakikana na tukio. Na elimu hiyo kwa kuzingatia madhara yake wakati na sehemu ya kudhurika nayo basi elimu hiyo ni haramu. Ama madhara yake ni kuchochoro cha shubuhaati (utata) na kutikisa itikadi na kuziondosha kutoka katika kuwa ya kukata na kushikiliwa. Na hilo ni miongoni mwa yale yanayopatikana mwanzo. [yaani mwanzoni mwa kujifunza elimu ya kalamu], na kurejesha kwake [yaani itikadi] kwa ushahidi ni jambo la kushukiwa. Na katika hilo watu wanatofautiana. Haya ndio madhara yake katika itikadi ya kweli. Na elimu hiyo ina madhara mengine katika kukazia itikadi ya wazushi juu ya uzushi na kuuthibitisha katika vifua vyao. Kiasi ambacho madai yao yanachimbuka na kupupia kwao kunashamiri katika kung`ang`ania hilo. Na ama manufaa yake huenda yakadhaniwa kuwa, faida yake ni kufunua ukweli na kuujua kama ulivyo. Hilo lipo mbali, katika elimu ya maneno hakuna kufikiwa kwa takwa hili tukufu. Na huenda kwenda ovyo na kupotea katika hilo ni kwingi zaidi kuliko kugundua na kujua… Sikiliza haya kutoka kwa wale ambao wameeleza elimu ya kalamu kisha wakajitoa baada ya kupata hakika ya uzoefu na baada ya kuzama katika elimu hiyo hadi kufikia ukomo wa daraja la wana elimu ya kalamu. (Ihyaau Uluuumi Diini 1/163 na ya baada yake).

- Nimesema: kwa hili inatosha kuwa nasaha kwa wale wenye kuhesabiwa kuwa ni wabobezi wa elimu ya kalamu na watu wenye uwerevu mkubwa duniani.

- Na mwanazuoni Ibnu Abii Al-Izzi [Baada ya kunukuu maneno ya Alghazaaliy yaliyopita]:

Na sababu ya kupotea: ni kukengeuka na kuacha kuzingatia maneno ya Allah na maneno ya Mtume wake. Na kushughulika na maneno ya wayunani na maoni tofauti tofauti. Na kwa hakika hawa wameitwa: watu wa kalamu (maneno), kwa sababu wao hawajafaidika na elimu yoyote ambayo haikuwa ikijulikana. Bali wameleta ziada ya maneno ambayo hayana faida. Nayo ni yale wanayoyapiga katika kiasi (kipimo) ili kuweka wazi yale yaliyojulikana kwa hisia (Attwahaawiyah 207).

Na mwisho, kwa hakika mwenye kutazama au kusoma madhehebu au kundi fulani, anapaswa atazame mwongozo wao katika nafsi zao. Na athari zao kwa wengine. Lau ukitafakari baadhi ya maneno ya hawa wana kalamu na wanafalsafa utaona ajabu, kwani miongoni mwa sifa zao, tena kwa kukiri kwao wenyewe kwa ndimi zao, ni:

a- Kutahayari, kutikisika, kujigongagonga, na kutokupata chochote chenye elimu yenye manufaa:
   - Abuu Abdallah Asshahrastaniy: Hakika yeye hajapata kwa wanafalsafa na wanakalamu ila tahayari na majuto, pale alipoimba:

Naapa kwa umri wangu, kwa hakika nimezunguka vyuo vyote,
Na jicho langu limetembea katika ulimwengu huo
Na sijaona ila mwenye kuweka kiganja chake kwa tahayari,
Juu ya kidevu au mng`oa jino mwenye kujuta
(Attwahaawiyah 209).

- Na Arraazi amesema:

Hatima ya kuitanguliza akili ni kufungwa,
na lengo la mwendo wa walimwengu ni kupotea
Na roho zetu zipo porini katika miili yetu,
na pato la dunia yetu ni maudhi na majanga
Na hatujapata faida ya utafiti wetu umri wetu woote,
isipokuwa kukusanya katika hilo: pamesemwa na wamesema.
(Attwahaawiyah 208).

- Na Shamsudini Alkhasrushaahii [na yeye ni miongoni mwa wanafunzi wakubwa wa Arrazai] amesema:

Na alimuuliza mmoja miongoni mwa baadhi ya wabora miongoni mwa wale walioingia kwake: Unaamini nini? Akasema: wanachokiamini Waislamu, na akasema: Je, na wewe umekunjua kifua chako kwa hilo huku unayakini nalo? Akasema: ndio. Akasema: Namshukuru Allah juu ya neema hii. Lakini mimi naapa kwa Allah sijui kile ninachokiitakidi. Naapa kwa Allah sijui kile ninachokiitakidi. Naapa kwa Allah sijui kile ninachokiitakidi. Na akalia mpaka ndevu zake zikalowa.

- Na Alkhufajiy wakati wa kufa kwake alisema:
  Katika nilichokipata sijui chochote isipokuwa: 'kile kinachowezekana kinahitaji wa kukitia nguvu kiwepo'. Kisha akasema: kuhitaji ni sifa hasi. Ninakufa na sijajua chochote (Attwahaawiyah 209).
- Na Ibnu Waaswili Alhumawiyu [na alikuwa hodari wao katika falsafa na elimu ya kalamu] amesema:
  Nalala chali juu ya kichogo changu na kuweka viambatisho vya maandiko katika nusu ya uso wangu kisha napitia makala na hoja za hawa na wale, upinzani wa hawa na wale mpaka alfajiri inachomoza hali ya kuwa hakuna kitu chochote katika hivyo kilichopata nguvu / kushinda kwa maoni yangu. (Naqdhi Almantiki 26).
  - Na Ibnu Abu Al-Izzi Alhanafiyu Allah amrehemu amesema kwa kuweka maelezo juu ya haya: Na anayefika hali kama hii, kama hajadirikiwa na Allah kwa rehema zake, vinginevyo anakuwa mzandiki. Kama alivyosema Abuu Yusuf: Atakayeitafuta dini kwa kalamu (mantiki na falsafa) atakuwa mzandiki (Attwahaawiyah 209).

b- Kuwa na yakini dhaifu, na unyonge wa itikadi, na shaka wakati wa kufa:

- Alghazaliyu amesema:
  - Watu wenye shaka sana wakati wa kufa ni : watu wa elimu ya kalamu. (Naqdhi Almantiki 25).
  - Imani inayopatikana kwa ushahidi wa elimu ya kalamu ni dhaifu sana. Inayokaribia kutoweka kwa sababu ya kila aina ya utata. (Alghazaaliy wattaswaufu 53).
  - Pima Imani ya watu wema na wacha Mungu miongoni mwa watu wa kawaida na imani ya watu wa kalamu na wanamijadala. Utaona Imani ya watu wa kawaida ni thabiti kama mlima mrefu haitikisiki kwa mabaya na vimbunga. Na imani ya mtu wa kalamu mwenye kuilinda itikadi yake kwa kuigawa vigawo vya mijadala ni

Ama aya ya Ash Shuura iliyotajwa, kwa hakika yenyewe ni yenye kutazama maana iliyo nyuma ya hilo. Kimsingi inatengua uwezekano wa kuwa wengi na inakubali kutowezekana kwake kwa dhati katika nafsi yake. Na inakata ule mtazamo kuhusu hiyo athari, kana kwamba sisi kwa hilo inatuambia:

---

kama uzi ulioachiliwa hewani ukipeperushwa [ukitikiswa] na upepo mara huku na mara kule. (Ihyaau Uluumidini 1/162).

c- Kujuta kwa kupoteza umri katika elimu ya kalamu na falsafa:
Na wakati mwingine Allah kwa rehema zake anawadiriki miongoni mwao kwa wale awatakao. Hivyo kabla ya kufa kwao wanarudi katika Uislamu wa msamaha, na wanachomoka kuwaonya wanafunzi wao na ndugu zao, wakiwapigia kelele, kwa mfano:

- Abuu Almaaliy Aljuwayniy [Mwalimu wa Alghazaaliy] amesema:

Enyi maswahiba wangu msishughulike na elimu ya maneno, lau ningejua kuwa elimu ya maneno itanifikisha katika kile nilichokifikia kwa muda wote nilioishughulikia. أ هـ. Na wakati wa kufa kwake alisema: Hakika nimezama katika bahari pana, na nikawaacha watu wa Uislamu na elimu zao. Na nikaingia katika kile walichonikataza, na sasa kama Mola wangu hata nidiriki kwa rehema zake, basi adhabu kali itamthubutukia Ibnu Aljawyniy. Nami nipo hapa nakufa katika Imani ya mama yangu – au amesema Imani ya wazee wa Naisapori. (Attwahaawiya 209, Swaunu Almantiqi walkalaami 236, 237).

- Na Arrazi [mwenye beti zilizotangulia] amesema:
  …. Kwa hakika nimetafakari njia za elimu ya maneno na mapito ya kifalsafa, na sikuiona ikiponya ugonjwa wala kupoza kiu. Na nimeona njia ya karibu zaidi ni njia ya Quran. Katika kuthibitisha nasoma: ﴾**Ndiye Mungu Mwenye rehema Aliyetawala juu ya Kiti chake cha Enzi** ﴿**.** Taha 5. ﴾**Kwake hupanda maneno mazuri** ﴿ Fatir 10. Nasoma katika ukanushi: ﴾**Hakuna chochote mfano wake** ﴿ Ash Shuura 11. ﴾**Wala wao hawawezi kumjua (Mungu) vilivyo** ﴿**.** Taha 110. Na atakayejaribu mfano wa majaribio yangu atajua mfano wa kile nilichokijua. (Attwahaawiyu 208, Sayri Aalaamu Annubalaa 21 / 501. Albidaya Wannihaaya 13 / 61.
- Na hivyo hivyo imenukuliwa kutoka kwa Alghazaaliy mwishoni mwa umri wake. Mwanafunzi wake ambaye ni Abdulghafaari Alfaarisiyu amesema: (Hatima yake ilikuwa: Kuzielekea hadithi za Mustafa na kukaa na watu wa hadithi, na kupitia Swahihi mbili – Albukhariy na Muslimu – ambazo zenyewe ni hoja ya Uislamu). (Alghazaaliyu Wattaswaufu uk 428).
  Na hivyo hivyo Ibnu Taymiya amesema kuhusu yeye. (… na akaegemea katika njia ya watu wa hadithi na akafa akiwa anashughulika na Bukhari na Muslimu). (Alghazaaliyu Wattaswaufu uk 430).
- Na kwa hakika maneno haya yanajitosheleza na hayahitaji maelezo. Maneno haya yanatokana na wale waliojitumbukiza katika jaribio gumu, na habari za elimu ya maneno na falsafa. Na kama wataiacha na kuihama basi hatokuwa mtuhumiwa katika nafsi yake wala katika elimu yake. Wala hilo asilidhanie ni kushindwa katika mantiki hii iliyopindwa. Wote ni wabobezi wa elimu ya maneno na ni wakuu wa watu wa elimu. Na maneno haya si kingine ila ni kelele kutoka kwao, isipokuwa nasaha za kiimani kwa ndugu zao na wanafunzi wao… na hayo yatosha, na yenyewe ni nasaha bora kabisa…. Laiti yangepata masikio yanayosikia na mioyo inayozingatia.

Hakika ya Mungu sio ile inayotokana na hakika ambazo zinakubali wingi na kushirikishwa na kufananishwa katika ufahamu wake. Sivyo hivyo, kwa hakika lile ambalo linakubali hivyo, ni ukamilifu wa nyongeza wenye upungufu. Ama ukamilifu uliotimia usio na mipaka – amabao wenyewe ni nguzo ya maana ya Mungu – kwani hakika yake inakataa akilini kukubali kushabihishwa na uwili kwa sababu vyovyote vile utakavyohakikisha maana ya Mungu basi umehakikisha kutangulia juu ya kila kitu na kuanzisha kila kitu: ﴾**Yeye ndiye Muumba wa mbingu na ardhi** ﴿**.** Ash Shuura 11. Na umehakikisha utawala juu ya kila kitu na kuwa juu ya kila kitu: ﴾**Funguo za mbinguni na ardhini ziko katika kabidhi yake** ﴿**.** Ash Shuura 12. Kama utaenda na kuamini kuwa kuna wawili wanaoshirikiana katika sifa hizi basi ungekuwa unapinga mwenyewe. Kwani unajaalia kila mmoja kati ya wawili hao ni mwenye kutangulia na mtanguliwa, mwanzilishi na mwanzilishwa, mkaa juu na mkaliwa juu. Au ungeuweka ukamilifu wa kuachilia katika ukamilifu uliofungwa katika hizo mbili. Kwani unajaalia kila mmoja kati ya wawili hao kwa kuiegemeza kwa mwenyewe sio mtangulia wala mkaa juu. Wapi na wapi kila moja kati ya hayo mawili kuwa mungu, wakati Mungu ndio mfano wa juu?!

Je, umeona kutokana na hii (kafu) tumejulisha njia ngapi za kimaana? Hifadhi mifano hii na kwa hiyo tambua undani wa mizani iliyowekewa huo mfumo madhubuti herufi herufi.

❋ ❋ ❋

[**Ufupisho Kwa Kufuta Ukiwa Pamoja Na Uwazi Na Utamu**]

Baada ya hayo, kwa hakika siri ya ufupisho katika Quran haisimami katika mpaka ambao tumeuashiria, miongoni mwa kujizuia na ziada isiyo na maana na porojo kabisa kabisa. Na kuteua matamko yenye kukusanya maana kubwa na yenye kuzuia ambayo nayo – kwa tabia yake ya kilugha – ni yenye kutimia zaidi katika kuainisha lengo, na yenye kupanuka kukubwa kwa maana zake zenye kunasibiana. Sivyo hivyo, bali hakika yake ni mara nyingi katika kufupisha inapita katika njia ya utukufu na ajabu.

Unaiona – baada ya kufuta maneno yasiyohitajika na ya ziada – inakusudia kufuta kitu katika mizizi na nguzo zake ambazo bila ya hizo, kikawaida maneno hayatimii. Na maana haiwi sawa ila kwa maneno hayo. Na kwa ufutaji huu huenda ukawa katika maneno na sentensi nyingi zenye kuambatanishwa na zilizofarakanishwa katika kipande kimoja. Kisha,

wakati huo huo unaioana ikifaidika na hayo matamko yaliyobakia katika kufikisha maana yote kwa uwazi kabisa, na kwa utamu usio na kifani, mpaka, kwa wepesi wa mapito[1], inakupitikia moyoni mwako kuwa, maana ya tamko lake ni pana kidogo kuliko hilo tamko lenyewe.

Kama ukitafuta siri ya hivyo, utaiona imewekwa katika maana ya hayo maneno au hizo sentensi zilizokunjwa, hapa katika neno na kule katika herufi. Kisha muundo ukaongozwa mwongozo wa ajabu, na ukapitishiwa katika mapito ya jandara[2] ya bayani kwa mkono wa fundi. Na akaidhibiti vizuri kuitengeneza na kuiweka sawa[3]. Kisha akaipulizia roho yake, na kutahamaki yapo vizuri, yamenawiri na kung`aa. Na nafsi haihisi kile kilichokuwepo mingoni mwa kufuta na kukunja, wala kwa kile kilichotokea miongoni mwa kutohitaji na kutosheka, ila baada ya kutafakari na kuchunguza kwa kina.

Hakuna kupinga, kuwa Waarabu walikuwa wanajua kitu fulani katika ufutaji katika maneno yao. Na hilo utaliona katika ubora wa kibayani wakati wowote ule, ushahidi wa hicho kilichofutwa utakapokuwepo, hata kama kitafutwa katika sehemu ya sentensi na nguzo zake. Pindi mbedui atakapoambiwa: Yu wapi nduguyo? Akasema: nyumbani. Na akiulizwa: nani yupo nyumbani? Akasema: ndugu yangu. Na lau kama atasema: ndugu yangu yupo nyumbani. Basi hilo lingehesabiwa kwa upande wake kuwa ni aina fulani ya upuuzi na ziada isiyofaa. Lakini dhumuni[4] lililofikiwa na Quran katika mlango huu – na milango mingine miongoni mwa milango ya kibalagha – haliwezi kufikiwa na ndimi na kalamu, wala matumaini na ndoto.

---

[1] Hili neno ni la kumithilisha, na kwalo tumekusudia kuleta taswira ya athari hii ya kibayani katika mfano wa ufundi wa kazi za mikono. Na hilo ni kwa kuwa wewe unamwona fundi cherehani mahiri akinufaika na vitambaa vichache na kutengeneza ua zuri lenye thamani kubwa mwilini. Bali lenyewe, kutokana na mapito ya viungo vyake yalivyo mepesi, unalidhania kuwa ni ua la rangi. Wakati ambapo fundi mwingine hawezi kunufaika navyo kwa kiasi hiki, wala zaidi ya hapo. Bali anaitoa nguo ya kubana. Huo ndio mfano wa ufupisho wa Quran ukiulinganisha na maneno ya watu [Daraazu].

[2] Jan`dara: kurudia, na jan`dara ya kitabu: ni kupitisha kalamu katika maneno yaliyofutwa.

[3] Ijapokuwa maneno haya yanafahamika vibaya kuwa eti Quran imeumbwa; ila maarifa ya kumjua Huyu Sheikh mtunzi na namna alivyowaraddi muutazila, kama ilivyotangulia katika kadhia ya Asswarfa, pale ambapo aliwatoa akili na kuwakosoa katika uelewa wao wa lugha ya Kiarabu. Yote haya yanatuwajibisha tumdhanie vizuri na tuseme kuwa maneno haya yamekuja katika mlango wa kuteleza kwa kalamu na kububujika kwa ubongo wa kibalagha ili kudhihirisha umadhubuti wa Quran na balagha yake tu.

[4] Dhumuni: lengo na upeo wa mwisho.

[**Utendaji Katika Aya Tukufu**]

Kwa hilo kwa mfano, chukua kauli ya Mtukufu: ﴿**Na kama Mwenyezi Mungu angaliwapa watu upesi upesi shari (wanayojihimizia iwafikie), kama wanavyojihimizia kuletewa kheri, bila shaka wanatimiziwa muda wao (mara moja wakajifilia mbali). Bila shaka wale wasioogopa kukutana na sisi tunawaacha katika upotofu (upotevu) wao wahangaike ovyo ﴾.** Yunus 11.

Aya hii imetiririshwa kuhusiana na wapinga kufufuliwa, wale ambao Mtume aliwaambia: Mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyinyi. Na mimi ni mwonyaji wenu mbele ya adhabu kali. Wakamwambia kwa kumbeza: ﴿**Ee Mwenyezi Mungu! Kama haya (aliyokuja nayo Muhammad) ni haki itokayo kwako, basi tupige kwa mvua ya mawe yanayotoka mbinguni au tuletee adhabu nyingine iumizayo (yoyote ile; lakini sisi hatufuati ﴾.** Al-Anfal 32. Basi pale ambapo Allah hakujibu pendekezo lao na kuwacheleweshea adhabu mpaka muda maalum. Amani ya muda mrefu, kuachwa bila shida na kuwa na afya kuliwazidishia upotevu mpaka wakasahau shaka ya ulimwengu na kuhisi amani dhidi ya adhabu za Allah. Wakawa wanaharakisha shari kama wanavyoharakisha heri huku wakisema: ni lini hiyo shari? Na hawakuwa wakidhania kuwa hiyo shari itakuja?

Katika kujibu uharakishaji huu, Quran imetaka kusema kuwa:

- Lau kama hukumu ya Allah imepita kuwa watu waharakishiwe shari pale watakapoiharakisha, kama anavyowaharakishia heri pale wanavyoiharakisha, basi angewaharakishia watu hao.
- Lakini mambo yalivyo, hukumu yake imeshapita, hukumu isiyobadilika ya kuwapa muda madhalimu na kuchelewesha hesabu yao mpaka muda uliotajwa.
- Na kulingana na nidhamu hii inayolindwa, Allah atawaacha watu hao mpaka uje wakati wao.

Haya ndio maweko ambayo, maneno huwekwa katika ndimi za watu na katika tabia ya lugha ili kuleta maana ya ujumla inayolengwa na hiyo aya. Tazama kimetokea nini…?

(1) Maneno katika maweko yake ya kawaida yalikuwa yameundwa na kadhia tatu: mbili katika hizo zikiwa ni vitangulizi, na ile ya tatu ndio matokeo. Hivyo Quran imefupika na ya kwanza na ya pili tu. Ama

ya kati nayo ni kutambua – au kuvua kama wanavyoiita wataalamu wa mantiki – imekunjwa mkunjo mkubwa.

(2) Utangulizi wa kwanza ulikuwa katika maweko ya kipuuzi ukiundwa na pande nne: Kuharakishwa mambo ya heri na shari kutoka kwa Allah na hivyo hivyo kuharakishwa kwa watu. Lakini hapa maneno hayana isipokuwa kitu cha kuharakishwa kimoja kutoka kwa Allah. Na kuharakishwa mara moja kutoka kwa watu.

(3) Na mkabala wake katika kushabihisha ukawa kwa kulingana na hali ya dhahiri. Nao si mwingine ila ni baina ya kuharakisha na kuharakisha. Au baina ya kutaka kuharakisha na kutaka kuharakisha. Katika hiyo aya, maneno yakaongozwa kwa sura ngeni, na mshabaha ukafanywa baina ya kuharakisha na kutaka kuharakisha.

Na baada ya utendaji huu wote, je, unaona kuwa hayo ni maneno yaliyokatika au njia yenye kona kona na kukwamisha ufahamu? Au unaona malengo ya hiyo aya yakipepea kwa watu wa kawaida na watu maalumu. Kama vile mwezi mpevu nyuma ya mawingu?

Rejea katika kutaka kitu katika siri za bayani, na sema: vipi huku kung`aa kumekuja licha ya huu ufupisho wa kibalagha?

Tunasema:

**(Ama la kwanza)**: Hakika yenyewe haikuwacha huo utangulizi uliokunjiwa ndani yake ila baada ya kuunyanyulia alama mbili zilizo kandoni mwake. Alama hizo zinajulisha nafasi yake na kuashiria kitu nyuma ya pazia. Kwa hakika kuliani kwake imesimika neno ﴿ **lau** ﴾ ya kujizuia na ambayo imeanzwa nayo huo utangulizi wa kwanza. Ikijulishwa kuwa hakutakuwa kutoka kwake huu uharakishaji. Na kushotoni kwake kuna herufi ya kuweka matawi na ambayo kwayo imeteremka na matokeo katika kauli yake ﴿**Na sisi tunawaacha** ﴾ ili kuonesha kuwa tawi hili lina mzizi utokanao na neno la aina yake. Kwani katika hilo husemwa: lakini jambo lake ni kuwaacha watu. Na kwa hiyo anawaacha hawa.

Na pale herufi faau ilipokuwa ipo peke yake, basi si nasu (andiko, hukumu) inayotakiwa; kwa kuwa yenyewe, kama inavyokuwa ya kuonesha matawi pia inakuwa ya kuunganisha tu – na huenda msomaji akaiunga na sehemu ya sharti la kabla yake. Na hilo ni kabla ya kumbainikia kuharibika kwa maana lau kama ataifanya hiyo faau ni ya kuunganisha – na haitotosheka na faau. Bali angeitia nguvu kwa nguvu mbili nyingine. Kwani angegeuza muundo wa matokeo kutoka katika wakati uliopita na kuwa wa sasa. Kisha kutoka katika nafsi ya tatu kuwa nafsi ya kwanza. Ili kukatika huku kwa

maneno baina yake na yale ya kabla yake kuwe ni tangazo la kukatika kwake na hilo kimaana na iwe ruhusa ya kusimama kabla yake. Ili nafsi isitumbukie katika kile kilicho chini ya mitikisiko au kukorogeka hata kidogo. Hayo, ukijumuisha na yale yaliyomo katika mabadiliko haya, miongoni mwa kutoa fani mbalimbali katika mtindo kwa kusasisha uchangamfu wa msikilizaji. Na miongoni mwao ni kutia hofu nyoyoni kwa kutoa matamko ya vitisho na kuwavuta kidogo kidogo kwa ulimi wa ukuu wa kifalme wenyewe.

**(Ama ya pili):** Hakika mambo yalivyo, pale alipofuta pande mbili katika hizo pande nne, hakuzifuta zikiwa za namna moja. Bali katika kila jozi mbili alibakisha kipande kimoja nacho kikiwa ni mkabala wa kile kilichofutwa kwa mwenzake. Ili kwa kile kilichotajwa kitanabaishe kile kilichofutwa. Kwa hiyo neno (kuharakisha) likawa kitanabaishi cha mkabala wake katika mshabihishwa kwake. Na neno (kutaka kuharakishwa) likawa kizindushi cha mkabala wake katika mshabihishwa.

**(Ama ya tatu):** Hakika yenyewe inatanabahisha juu ya maana ambayo yenyewe ni upeo wa uzuri. Nayo ni siri ya kutoa muda. Na hekima ya kutoharakisha kwa Allah. Hivyo ni kwa kuwa yeye ameweka taswira ya huku kuharakisha kunakotakiwa kwa taswira ya tashibiha ya mtakaji kutafuta na kupupia mno katika kuridhisha matamanio yake na kukidhi haja zake zinazomchagiza, na ambazo zinamchochea aharakishe. Na hasa hasa pale alipokuwa anataka heri kwa ajili ya nafsi yake. Kana kwamba imesemwa: Hakika yeye Mtukufu lau kama angewaharakishia hilo basi angekuwa kama wao katika hili la kuharakisha, katika kule kuwa na vichocheo vinavyomsumbua. Na Allah ameepukana na hilo.

Haya, ukijumuisha na uchambuzi mwingine wa ajabu mno:

- (Miongoni mwazo) ni kuwa neno (lau) kwa kutegemea maweko na tabia ya maana yake, linahitaji lifuatiwe na kitenzi cha wakati uliopita. Lakini hapa kinachotakiwa si kukanusha kilichopita tu, bali kubainisha kuwa kitenzi hiki ni kinyume na mwenendo wa Allah usio na mabadiliko. Na lau maana ingeletwa kwa maweko haya basi maneno yangekuwa marefu, na pangesemwa: (lau mwenendo wa Allah unaoendelea kwa viumbe wake ungekuwa kujaalia…… mpaka mwisho): Hebu tazama namna maneno yalivyofupishwa katika tamko moja kwa kukitoa kitenzi katika muundo wa wakati uliopo unaojulisha kujirudiarudia, kujikariri na kuendelea. Na ikatosheka kwa kuiweka (lau) ikiwa ni ushahidi wa kwamba kile kilicho

baada yake nacho ni chenye kupitiwa na maana yake. Na hivi hivi imetekeleza maana mbili zote kwa uzuri na ulaini kabisa.

- (Na miongoni mwazo) ni kuwa, muktadha wa upatanisho baina ya sharti na jibu ni jibu kuwekwa likilingana na sharti lake, hivyo husemwa: (angewaharakishia). Lakini yenyewe, imeacha hayo na kwenda katika kile kilicho kikubwa zaidi na kikubwa mno. Pindi ilipobainisha kuwa lau angewaharikishia watu shari angewaharakishia hawa katika hiyo shari kwa namna mahususi wanayostahiki nayo. Nayo ni adhabu asilia na ambayo inamaliza maisha yao.

- **(Na miongoni mwazo)** ni kuwa, muktadha wa dhahiri katika kuyathibitisha matokeo, isemwe: (Na sisi tunawaacha wao) au (Na sisi tunawaacha hawa) lakini yenyewe imesema: ﴿**Bila shaka wale wasioogopa kukutana na sisi, tunawaacha katika upotofu (upotevu) wao wahangaike ovyo** ﴾**.** Ili kukusanya malengo mawili muhimu. La kwanza: Kuzindua juu ya chanzo cha huku kutaka kuharakisha kwao wao nacho ni kule kutokuwa kwao na imani ya kukufuliwa. Na ya pili: Matokeo ya kuwa kanuni ya kuwapa muda itokayo kwa Allah ni kanuni ya wote kwao wao na wale walio wa mfano wao.

- **(Na miongoni mwazo ni yale yasiyokuwa hayo…)**

Ukiapa kwa Mola wako, tuambie: Lau kama utapata katika maneno ya kibinadamu japo mojawapo ya huu uchambuzi. Hivyo katika mtindo gani usiokuwa wa mtindo wa Quran unaweza kupata mkusanyiko huu au kile kinachosogeleana nacho kwa kiasi hiki au kile kilicho mara mbili yake katika matamko?

[**Mfano Mwingine**]

Pokea mfano mwingine wenye maana hiyo hiyo: - ﴿**Sema: ‘‘Mnaonaje kama ikikujieni hiyo adhabu yake usiku au mchana, (mtaweza kukimbia)? Basi kwa nini wale wenye makosa wanaitaka ije kwa haraka? Ikishatokea ndiyo mtaiamini? (Mtaambiwa wakati huo): ‘Je, sasa (ndio mnaamini?)’ Na mlikuwa mkiihimiza?’**’﴾ **.** Yunus 50 – 51.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: -

Nielezeni kuhusu hali zenu itakapowajia adhabu kwa ghafla usiku au mchana, siku hiyo nyinyi mtafanya nini? Kwa hakika nyinyi katika siku hiyo mtakuwa baina ya mambo mawili: ima kung`ang`ania kile mlicho nacho sasa cha kukadhibisha na kutaka kuharakisha; na ima kuamini. Ni kipi mtakachokichagua? (Je, mtaitaka iharakishwe) hiyo adhabu ya siku hiyo kama mnavyotaka iharakishwe leo hii? Sivyo hivyo! Kwa hakika nyinyi ni

waovu. Na inakuwaje mwovu awe na shauku ya kuiona adhabu ambayo kama itakuja, basi lazima imfike? Kisha nielezeni ni aina gani ya adhabu mnayotaka iharakishwe? Kwa hakika hiyo adhabu si ya aina moja bali ni za aina na nakshi mbalimbali. (Au) nyinyi leo hii mnaikadhibisha kisha itakapotokea baada ya muda mnaiamini? Zindukeni, hakika mambo yalivyo, siku hiyo, imani yenu haitowanufaisha baada ya kujicheleweshа mpaka mkapoteza nafasi na mkapitwa na wakati wa kuwahi. Bali huko mtaambiwa kwa kutiwa majuto na hasara: Je, sasa hivi ndio mnaamini, wakati mlikuwa mkiikadhibisha na kutaka kuiharakisha!!

Hii ndio maana ikiwa katika nguo ya kawaida.

Tazama, ni maneno mangapi mangapi na sentensi ngapi ngapi zimekunjiwa katika moyo wa maneno hayo na katika pande zake mbili? Na namna yenyewe, pale yalipokunjwa hayakuacha kitu ila kimejaaliwa katika hilo tamko kuna taa inayofunua hilo lililokunjwa, na kuna funguo inayokufikisha katika hilo neno? Kwani maweko ya maulizo mawili yanayokabiliana katika hayo maneno yanakujulisha kuwa huko kuna maulizo yanayojumuisha zote mbili na yenye shaka shaka baina ya mbili hizo. Katika hilo husemwa: Mtafanya nini, na njia ipi kati ya njia mbili hizo mtaipita? Na kuuliza kuhusu aina ya mwenye kutaka kuliharakisha miongoni mwa adhabu inajulisha kuwepo kwa maulizo ya utangulizi ya kabla yake juu ya kupatikana asili ya kutaka kuharakisha. Na neno ﴿**waovu**﴾ limejulisha kutowezekana kuwepo kwa upande huu wa shaka. Na neno ﴿**Kisha**﴾ la kuunganisha limejulisha kilichounganishwa kwake aliyekunjwa baina yake na baina ya herufi *hamza.* Na tamko la kielezi cha wakati ﴿**Sasa**﴾ limejulisha mtenda wake aliyekadiriwa. Na pimia kwa hayo kwa vile vyote vilivyofutwa… Hadi muda wa kuuliza wenye kuingia katika kielezi hiki nao umejulisha urefu wa muda wa kucheleweshа, muda ambao umezuiwa kukubaliwa kwa imani yao. Kwa sababu wao walirefushiwa umri wao na hakukumbuka katika umri mrefu huo mwenye kukumbuka.

Basi ni nani yule ambaye anaweza kupitia sehemu[1] fulani katika njia hizi au sehemu mbili. Kisha pumzi yake isitetereke. Na bila ya kukosolewa na magwiji na mabingwa wa bayani?

Ewe Mola wangu, kwa hakika, kinyume na hayo ni sehemu ya mbali mno, na ni safari isiyokusudiwa. Na kwa hakika, kinyume na hayo kuna mpaka wa muujiza.

* * *

---

[1] Sehemu: fungu.

## - 2 –

## Quran, Sura Kwa Sura Miongoni Mwake: (Wingi) Na (Umoja):

Hili tulilokusimulia la kuhusu ukwasi na wingi wa kimaana katika mtindo wa Quran na ufupi wa tamko lake. Huongezewa jambo jingine nalo ni mapambo ya ukwasi huo na uzuri wake. Huo ndio mshikamano wa maweko yake, na kuungana nukta zake, na mpangilio *hujzi*[1] mzuri baina yake, hadi ikafikia ya kuwa yenyewe imejipanga na kuwa kitu kimoja kilicho madhubuti kisichotengana.

Na wewe huenda ukajua kuwa maneno ya jambo moja, yakipangwa vibaya, umoja wa maana yake unaharibika na vifungu vyake vilivyokuwa pamoja hufarikiana, na kile kilichokuwa kimeungana hujitenga. Kama inavyoangamia taswira ya umoja katika kioo endapo usawa wa hicho kioo hauko sawa sawa. Je, maneno sio kioo cha maana? Kwa hiyo, hakuna budi kudhihirisha huo umoja wa kimaumbile (kimaana) katika kuudhibiti huu umoja wa kifani (kibayani). Na hivyo ni kwa kutimiliza kule kuweka karibu baina ya vifungu vya bayani na kupatanisha baina ya dondoo zake mpaka zinashikamana na kukumbatiana sana.

Hilo si jambo jepesi kama anavyolidhania mtu mjinga asiyejua ufundi huu. Bali jambo hilo ni takwa kubwa (linahitaji) umahiri, uhodari na hisia ya kupenda katika uteuzi wa maeneo bora ya vifungu hivyo: kipi kina haki zaidi ya kufanywa kuwa ndio asili au kikamilisho. Na kipi kina haki zaidi ya kuanza au kumalizia, au kiwekwe sehemu ya katikati? (Kisha linahitaji) mfano wa hivyo katika kuteua njia bora kabisa ya kuvichanganya: kwa kuviegemeza, au kuvining`iniza, au kwa vinginevyo. Yote haya ni baada ya kutulia katika uteuzi wa hivyo vifungu vyenyewe. Na kuwa na amani ya kuwa kuna muunganiko katika kila kimoja katika hayo kwa roho ya maana. Na kwamba vyenyewe vipo safi havina makando kando. Yana uchache wa kuhama kutoka mazungumzo kwenda mazungumzo mengine, na kwamba ncha zake na kati kati yake zipo sawa sawa katika kuliekea lengo. Na vipo sawa katika kulilenga hilo lengo. Kama zilivyosawa pande za nukta ya mduara kwa kupima kuelekea katikati ya kituo. Na iliyosawasawa kwa kipimo kuelekea kila kimoja katika hivyo.

[1] Mpangilio hujzi: wingi wa neno Hujzatu nalo ni sehemu ya kiunoni (sehemu ya kufungia msuli). Na maneno yaliyochukuana yenyewe kwa yenyewe hadi nyongani ni yale yaliyopangwa na kushikamana vizuri (Asaasu Albalaagha).

### [**Ufundi Wa Bayani Katika Kuhama Kutoka Katika Maana Hadi Maana Nyingine Iliyongumu Kuliko Hiyo Katika Kuhama Baina Ya Vifungu Vya Maana Moja**]

Hiyo ndio hali ya maana moja ambayo vifungu vyake vinaungana vyenyewe kwa vyenyewe kwa muungano wa kikawaida. Sasa unadhani nini katika maana tofauti tofauti katika kiini chake, zilizotengana kwa tabia yake? Ni umahiri na uhodari wa kiasi gani huo! Bali ni uwezo kiasi gani huo wa kiuchawi, unaohitaji kuzoesha baina ya michanganyiko yake ya ajabu, na mielekeo yake yenye matawi mengi? Hadi inafikia hakuna kukusanya baina yake katika habari moja kama kukusanya baina ya kalamu, kiatu, msumeno na maji. Bali hadi kufikia mkorogo mmoja na mwelekeo mmoja. Na hadi uwe katika umoja wake mdogo na umoja wa kukusanya mwingine.

Hakika yake, kwa ajili ya utukufu wa takwa hili, tunawaona wanaumbuji, hata kama watafanya vizuri na kuboresha hadi kufikia upeo wa juu kabisa katika kila lengo. Basi watakuwa na makosa na kuharibu katika mfumo wa malengo hayo yote au mengi yake. (Kwani washairi) pale wanapoleta shairi moja likiwa na maana nyingi, basi mengi ya yale wanayoyaleta ni maana mtawanyiko isiyokuwa pamoja yenyewe kwa yenyewe. Na ni mara chache mno wanapoweza kumaliza vizuri lengo moja na kwenda lengo lingine. Kama ilivyo katika kuhama kutoka katika *annasiibu*[1] kwenda katika kusifu. (Na waandishi) huenda wakataka msaada wa kuzuia mianya hiyo kwa kutumia nyenzo za kuzindua au simulizi za moyoni. Kama wasemavyo: Zinduka, kwa hakika… Hili, lakini … tumebakisha … na tuhamie… turudi… tulisema… tutasema….

Hii ndio hali ya malengo yaliyotofautitofauti pale yanaposhughulikiwa na maneno mamoja katika kikao kimoja. Basi inakuwaje lau kama hayo maneno yatakuja katika zama na mazingira mbalimbali kwa vipindi vya muda mrefu? Je, muunganiko katika maneno hayo hautakuwa wa kukatika sana, na ombwe la baina yake halitokuwa pana sana?

Ikiwa kama umeshangazwa na kuwa Quran katika mfumo wa kibayani wa kupangwa kwake upo katika kipande kimoja. Ambapo kuna maudhui moja kwa maumbile yake. Hebu njoo utazame sura katika Quran yenye

[1] Annasibu: ni shairi zuri la kimapenzi kuzungumzia wanawake.

maudhui kadhaa, na mazingira tofauti tofauti ili uone katika mfumo huu, kile ambacho kinaingiza zaidi katika kushangazwa na muujiza.

Hivi hujui kuwa kile ambacho muundo wa Quran unajipambanua nacho kwa ubora, miongoni mwa kujiepusha na njia ya kurefusha na kujilazimisha na upande wa kufupisha – kwa kiasi kinachotosheleza kwa uzuri wa lugha – hicho kimeifanya Quran kuwa ndio maneno yenye fani nyingi zaidi. Tunamaanisha ndio maneno yenye wingi kushughulikia mambo ya maneno na yenye haraka zaidi kuhama baina yake[1] kutoka katika maelezo

[1] Na la kushangaza zaidi ni kuwa, pamoja na kuwa kwake ni maneno yenye fani nyingi na kuwa na maudhui mbalimbali. Yenyewe ndio maneno yenye fani nyingi na kupamba mno katika muundo wa maudhui moja. Yenyewe haiendelei sana katika mtindo mmoja wa maelezo. Kama vile yenyewe haiendelei muda mrefu katika lengo moja la maana. Hivi huioni inavyohama katika sura moja kutoka katika maana moja kwenda maana nyingine. Inahama katika maana moja baina ya muundo wa kiinshaai (sentensi ambazo haziwezi kuhukumiwa kuwa ni kweli au si kweli mfano; Chota maji.) na kihabari (sentensi ambazo zinaweza kuhukumiwa kuwa ni za kweli au si zakweli mfano; Wewe unachota maji.), nomino dhahiri na kiwakilishi, Sentensi zinazoanza na nomino au zinazoanza na vitenzi, vitenzi vya wakati uliopita, uliopo na ujao, nafsi ya kwanza, ya tatu na ya pili, na yasiyokuwa hayo miongoni mwa njia za utendaji. Kwa namna ya haraka ambayo hujapatapo kuuona mfano wake, wala kile cha karibu yake miongoni mwa maneno ya wengine katu. Pamoja na mabadiliko haya ya haraka yanayoendelea na ambayo ndio chanzo hasa cha kukukoroga na kuleta mitikisiko. Bali pia ndio chanzo cha janga na kukwama, ndani ya maudhui au kutoka nje yake. Lakini yenyewe utaiona haitikisiki wala haikwami bali inadumisha tabaka hilo la juu kwa umadhubuti wa mfumo na uzuri wa mtiririko. Hadi kutokana na hizi fani nyingi inaunda mandhari iliyoungana. Ni mtu gani anayekiweza Kiarabu na kisha kuutazama mfumo huu wa Quran kwa mtazamo mmoja kisha asione ndani yake athari za uweza vyenye kushangaza ikiwa ni siri miongoni mwa siri za kutoa changamoto na muujiza?

Na wewe umeshawasikia baadhi ya wale wanaochipukia katika vionjo vya uzuri wa Quran na kutafiti juu ya vyanzo vya uzuri wake wakijiuliza: Hali hiyo ya kisaikolojia ina siri gani, na ambayo anaipata anayeisoma Quran na msikilizaji wake miongoni mwa uhondo na kusasisha uchangamfu pamoja na kila hatua yake. Mpaka hajui kupata uchovu vyovyote atakavyofanya kwa kina kutembea ndani yake? Wazindue wao kuwa tukio hilo la ajabu, lina vyanzo vingi ndani ya Quran. Baadhi yake vimeshaashiriwa hapo kabla na miongoni mwazo ni (ni yale masimulizi yaliyotangulia yanayohusu umahususi wa Quran kiupande wa sauti Uk 127 wa matini chanzi. Na umahususi huu tunaouashiria sasa ndani yake kuna chanzo kingine cha kina zaidi na chenye mengi zaidi. Isipokuwa chenyewe hakipewi heshima yake ukweli wa heshima yake. Isipokuwa kwa mwenye kutazama katika maneno ya wanaumbuji na kufahamu upeo wa fani zao katika mitindo yao, na upeo wa fani zao katika malengo yao. Kisha aje atafakari hizi pande mbili katika mfumo wa Quran. Huko atajiona yupo mbele ya mwisho ambao hata mwanzo wake haujapatapo kuvukwa na wanaumbuji. Kwani ataona kuwa yenyewe haihami kutoka hatua moja kwenda nyingine ila inaonesha na kuwasilisha katika hatua inayofua mapito na aina mbalimbali za maana na mitindo mipya baada ya mipya. Sasa itakuwaje uchovu upate njia ya kuingia katika moyo wake. Pamoja na kudumu kwa nadharia hii na kujisasisha? Kila mtu anaweza kuijaribu nafsi yake pale anaporefusha kusimama mbele ya mandhari

kwenda katika simulizi, kwenda katika kuweka sheria, kwenda katika mjadala, na kwenda katika aina nyingine mbali mbali. Bali hilo limefanya fani moja katika Quran kuwa na matawi ya fani nyingi. Na jambo moja ndani yake kuwa linajumuisha chini yake mambo na mambo mengi.

[**Kuteremka Quran Ikiwa Imetawanyika Kulingana Na Matukio Na Visababishi, Licha Ya Kuwa Kwa Vipindi Mbali Mbali, Jambo Ambalo Kikawaida, Haliruhusu Kuwepo Kwa Muunganiko Na Kushikamana**]

Je, hujui kuwa Quran – katika mambo yake mengi – haikuwa ikiteremka ikiwa na maana hizi zilizo tofautitofauti kwa mkupuo mmoja. Bali ilikuwa ikiteremka kipande kipande vikiwa tofauti tofauti kulingana na matukio na visababishi vinavyojisasisha. Na kuwa huku kuachana kwa wakati baina yake, na kutofautiana kwa dhati baina ya visababishi vyake, kwa tabia yake vilikuwa vikifuata kule kutengana kwa mazungumzo yake juu ya aina ya kuwa huru na kuanza upya ambako hakuachi baina yake tatizo la kuungana na kushikamana?

***Je, hizi sababu mbili hazikuwa nguvu mbili zenye kusaidiana katika kuusambaratisha umoja wa maneno na kukata mizizi yake. Pindi inapotakiwa kupanga kikundi cha mazungumzo hayo katika uzi mmoja chini ya jina moja?***

[**Kukusanya Mazungumzo Yenye Maana Tofauti Tofauti, Yaliyo Katika Nyakati Mbalimbali, Yaliyo Ya Nyanja Tofauti Tofauti Na Kuyaweka Katika Mazungumzo Mamoja Yaliyoachiliwa. Kwa Hakika Hilo Ndilo Kiini Cha Kumeguka Meguka Na Kukata Maneno Bila Kuyamaliza. Na Hilo Ndilo Kiini Cha Kufarikiana Na Kutofautiana**]

Chukua mkononi mwako matini kadhaa zilizokamilika za hadithi za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, zilizokuwa zimezungumzwa katika nyakati tofauti tofauti, na zilizoshughulikia malengo yanayopishana. Au chukua maneno kadhaa ya yeyote yule umtakaye miongoni mwa wanaumbuji. Na jaribu kuyaleta yakiwa katika mtiririko mmoja ili uyafanye

---

moja nzuri. Je, katika mandhari hiyo anapata mtikisiko wa kuiona nzuri katika huku kuendelea kwake, kama vile anaoupata lau kama ingemtokea safu za mandhari matamu, yaliyosheheni ndani yake aina mbali mbali za faida na starehe. Kisha zikafanywa zinampitia zikiwa za aina mbalimbali katika ubunifu na mfumo mzuri wa upangaji? Ee Mola wangu kwa kweli haiwezekani. Basi hivyo ndivyo hivyo hivyo [Daraazu].

yawe mazungumzo mamoja. Bila ya kuzidisha au kupunguza chochote baina yake. Kisha tazama: Namna maana zake zinavyokataana, na miundo yake inavyokimbiana katika masikivu na ufahamu! Na namna yanavyoonekana yakiwa na viraka na kupachikwa na kufarikiana kiasi ambacho hayaonekani kuwa ni ya kauli moja iliyoachiliwa!

* * *

### [**Wanadamu Wameshindwa Kufikia Upeo Wa Kuainisha Maweko Ya Kila Kifungu Katika Vifungu Vya Kitu Changamani Kabla Ya Kutimia Kwa Vifungu Vyake. Bali Kabla Ya Kujua Tabia Ya Vifungu Hivyo**]

**Na sababu ya tatu**, ilikuwa inastahiki zaidi kuufanya mfumo wa sura uparaganyike zaidi na zaidi na kuupasua pasua umoja wake. Hiyo ndio njia ambayo imefuatwa katika kuunganisha (nujuumu)[1], yaani vifungu vya Quran vyenyewe kwa vyenyewe. Na katika kuunda umoja wa sura kutokana na vifungu hivyo. Kwa hakika yenyewe ni njia ya kufurahisha, na katika njia hiyo tutakuonesha ajabu kubwa ya tatu na ambayo ndio imeutoa muundo wa Quran kutoka katika maumbile ya miundo ya kibinadamu. Hebu njoo na utazame!

Mtazame mwanadamu pale anapofanya ufundi fulani miongoni mwa ufundi wa kuchangamanisha vitu. Hivi daima humuoni akianza kazi yake kwanza kwa kuvijua vifungu na viungo vya mchangamano huo. Kisha anafahamu vifaa na vikamilisho vyake. Kabla ya kuamua maweko ya kila kifungu katika vifungu hivyo katika sehemu yake. Hizi ni hatua mbili ambazo hatua ya pili inateremka na kuwa katika nafasi ya taswira ya malighafi yake. Hakuna tabu kuwa kinyume cha kadhia katika mawili hayo haiwi ila ni kuipeleka akili ya mwanadamu katika njia isiyo yake, na kuikokota katika tope ambalo ndani yake mguu wa mwanadamu hauna

[1] Nujuumu: wingi wa najmu, nayo ni kifungu miongoni mwa Quran kinachoteremka kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake. Kwa hakika Quran imeteremka ikiwa vifungu vifungu vilivyo tofauti tofauti kwa muda wa miaka ishirini na mitatu kamili. Huenda kifungu kimoja kikateremka kikiwa ni sura kamili au aya kadhaa, au aya moja au sehemu ya aya kama vile katika hadithi ya Zaid bin Thaabiti Allah amuwie radhi, hadithi ambayo imeshatangulia kutajwa katika ukurasa wa 88 wa matini chanzi ikiwa na nambari 3 katika maelezo ya chini. Na husemwa kwa Kiarabu, amezinajimu mali. Ikimaanisha amezitoa vifungu vifungu (tofauti tofauti).

utulivu wala kuweza kutembea. Je, ushawahi kumuona yeyote aliyepita njia hii ya mashaka kisha mambo yake yakatulizana hadi akafika mwisho wake?[1]

Bali mtazame mwanadamu pale anapoanza kupanga vifungu vya kitu changamani baada ya kuvikusanya. Hivi humuoni akifuata mwenendo wa kutembea wa kimaumbile ambao kila mtembeaji anayeenda katika lengo fulani la kihisia au kiakili anautii? Kwani yeye kama katika njia yake atakata hatua kadhaa basi hatoweza kuvuka hatua inayofuata kabla ya kuivuka ya kwanza yake. Na kama atapanda ngazi au madaraja basi hatoweza kuzicheleweshа ngazi za chini kabla ya kufika za juu.

Hiyo ni mipaka iliyowekwa na kanuni za jumla za kimaumbile. Hivyo hakuna hata mtu mmoja anayeweza kuzigeuka. Ni sawa sawa katika ufundi wa kimaada au wa kidhahania. Kwani mjenzi, mfuma nguo, mwandishi na mshairi katika mipaka hii wapo sawa sawa.

[**Mifano Katika Ufundi Wa Fani Mbalimbali**]

Tunakupigia mfano:

Kadiria katika nafsi yako, mtu mmoja ameteremka katika bonde pana lisilo na jengo lililosimama, na hakuna kitu miongoni mwa vitu vya kujengea wala vifusi. Na haukupita muda akahisi tetemeko la ardhi au kimbunga cha

---

[1] Tunasema: Je, ushamuona mwenye akili akiharakisha kutoa maamuzi juu ya kuanisha eneo la kifungu fulani katika ufundi wake kabla ya kuvijua vifungu vingine? Na kama atafanya hivyo je, unaona kuwa, maamuzi yake katika utaratibu huo ni maamuzi sahihi? Kisha kama atang`ang`ania kuufuata mpangilio huo, je, unamuona atatimiza kile anachokitamani katika ufundi wake kwa mfumo ulio madhubuti?
- Sivyo hivyo! Kwa hakika mwenye akili lau kama atafanya zoezi hili katika baadhi ya vifungu akijishusha katika hali ya kawaida ya uwepo, kwa hakika hilo atalifanya kuwa ni egesho la muda tu. Na kidogo kidogo itamdhihirihikia yeye kiungo kingine chenye kustahiki zaidi kuwekwa katika nafasi hii au ile. Kisha hautopita muda mrefu, atarudi mwanzoni ili akiweke kila kitu sehemu yake kwa uchache au kwa wingi. Au akitenganishe na kundi hili na kukipeleka katika kundi lingine. Au kikijaalia chote kuwa ni chenye kusimama kichwani kwake... na hivi hivi hatoacha kuendelea kubadili sura ya mwonekano katika mfumo wa umbo hilo hadi atakapomaliza kulikusanya na kuliweka sawa. Na kisha likawa wazi kwake kiujumla na kimaelezo zaidi. Hapo tu, ndipo atakapoweza kukituliza kila kifungu katika eneo lake la mwisho. Na kuupa huo mchangamano taswira yake ya mwisho. Na kila mpangilio, unaofanywa na kitu kimoja kimoja kabla kujua ujumla wake basi kitu hicho hakiunganishwi ila kinarundikwa tu. Na hatokipa ila taswira mbaya. Na hivyo kila mfumo uliosimamishwa juu ya msingi usio wa kielimu ya kina juu ya vifungu vyake vinavyouunda mfumo huo, basi mfumo huo unastahiki zaidi kuwa mfano wa udhaifu na dosari. Na hata kama leo hii utabakia ukiwa umesimama, basi mfumo huo hautokaa muda mrefu kesho yake utaporomoka. [Daraazu].

angani. Na kutahamaki unaona lundo la mlima ukipasuka kidogo kidogo na kurusha mawe au baadhi ya mawe pembezeni mwake… Kisha unapita muda mrefu au mfupi, na kutahamaki tetemeko la pili au la tatu nalo likitupia mapande ya vyuma na majivu. Au vipande vya fedha na dhahabu.. Je, unaona mtu huyu au mtu yoyote mwingine mwenye akili, punde tu anaanzia hatua za mwanzo za kuandaa ramani ya jengo ili ajenge mji kwa kukusanya hizo malighafi zilizotawanyika. Na ni kipi hasa kile ambacho ataweza kukileta kutokana na mfano kama huo? Na aanze kazi katika jukumu la kuweka mipango na majengo? Ni kipi kitakachomjulisha kwamba huenda tukio hili halitojirudia tena mbele yake likijikariri mara nyingine. Kisha ni kipi kitakachomjulisha kuwa kama kitajirudia basi kitajirudia mara ngapi, na aina gani ya matirio ambayo itakayodondoshwa katika kila mara, na vipande vingapi vya matirio hayo vitakuwepo katika kila mara likijirudia, na majengo mangapi yanaweza kujengwa kutokana na matirio hayo, na mfumo gani mahususi wa kiinjinia utatumika kwa kila jengo: upana, mwinuko, uchongaji, mapambo, na ukubwa wa dheraa[1] ya eneo la wazi utakaotumika na majengo haya kwa ujumla wake?..

Katika mazingira kama haya yaliyojaa utata na kufahamu vibaya, hakuna mwenye akili atakayethubutu kuanza kuweka mipango yake ya ujenzi wa kibanda dhaifu, seuze kujenga mji mkubwa na kutoa haraka haraka katika kuitekeleza azima yake na kuendelea na jukumu la kujenga tangu muda uliomfikia hayo matofali ya mwanzo.

Na lau kama tukichukulia kuwa kuna mtu aliyethubutu kuingia katika hatari hii. Na kwa haraka haraka kudura zimekuwa katika upande wake na kumsaidia kwa kile anachokitaka miongoni mwa matirio ya ujenzi ambayo aliyafikiria na kuyatamani. Je, unamuona akikusudia kujitia hatari nyingine. Na kwa hiyo katika huo ujenzi anajifanyia mtindo wa ujenzi unaokinzana na kanuni za kimaumbile, kwa kujiapiza[2] moyoni mwake kamwe asiache tofali litakalofika mkononi mwake ila ataliteremsha – muda ule ule linapofika – eneo la kulijenga popote litakapokuwa? Hilo ni pale ambapo hayo matofali hayajamteremkia yakiwa ya namna moja na kupangwa kwa mpangilio wake katika maweko yake yanayosuburiwa. Bali yamejaaliwa yanatawanyika kuna mepesi na mazito, yana rangi, ukubwa, mali ghafi na nishati yake ni tofautitofauti. Na huenda ikamdondokea mapambo na roshani (kibaraza cha

[1] Dheraa: Dheraa ni ukunjufu wa mkono. Na hapa maana yake ni upana na umbo.
[2] Kujiapiza: kuapa yeye mwenyewe.

ghorofa) kabla ya kuteremkiwa na baadhi ya misingi na saafaati[1] (kozi). Na hueanda akateremshiwa vifungu vyenye upungufu kwa mfululizo ili viwekwe katika maeneo tofauti tofauti, katika majengo yaliyo mbali mbali. Je, humuoni kama ataenda kukiweka kila kifungu katika sehemu yake maalumu katika muda ule ule kilipoteremka, kuwa hatokuwa na namna ila kuharibu vifungu vya hilo jengo hapa na pale, kwa umbali umbali usiokuwa sawa sawa wala kunasibiana, na kwa hiyo ataviweka karibu baina yake kwa hatua na kuviweka mbali kwa hatua nyingine, atavipandisha wakati fulani na kuvishusha wakati mwingine, mpaka atafikia kujenga sehemu za juu za nyumba kabla ya kujenga sehemu za chini na kushikilia kitu kibebwacho kikiwa kimening`inia bila ya kile kinachokibeba.

Vipi kwa mwanadamu vyovyote vile atavyokuwa ataweza kulitekeleza jukumu hili? Kisha vipi atasonga mbele katika jambo hili mpaka afikie mwisho wake, bila ya kurudia katika kifungu fulani kwenda kukiondosha sehemu yake ambayo alikiweka sehemu hiyo pale mara ya kwanza, au akirudie ili kukivunja au kukichonga au kuujazia au kuupa nguvu? Kisha vipi mwisho wa jambo lake utakavyokuwa, hakika yake katika ule wakati anaweka tofali la mwisho kwa njia hii, basi atakuwa ananyanyua mkono wake kutoka katika huo mji uliofutika, usio na kasri wala chumba wala tofali wala hata sehemu ndogo wala kubwa ila itakuwa imeshaporomoka na kufikia sehemu yake madhubuti na ambayo inaridhiwa na vionjo vya kiufundi. Hata kama itabadilishwa moja katika hayo na kuwekwa sehemu ya mwingine basi hilo jengo lingetetereka au mfumo wake ungeharibika?

***Je, hilo kama litatokea, halitokuwa ni changamoto kwa uweza wa wanadamu wote?***

Zinduka hilo limeshatokea likiusadikisha mfano huu katika maswala yetu. Na pokea ubainifu wake:

- Ama huyo mtu basi huyo ni Nabii asiyeweza kusoma na kuandika rehema na amani ziwe juu yake.
- Na ama huo mji ambao ameanza kuujenga tangu ilipomteremkia matofali yake ya mwanzo, basi hicho ni Kitabu Kitukufu na ambacho yeye tangu alipofikiwa na mwanzo wa ujumbe wake, alianza kuvipanga vifungu vyake katika mpangilio wa mtu mwenye kujiamini na

[1] Saafaatu: ni wingi wa neno saafu, nalo ni kila kozi ya tofali au udongo ukutani.

kutulia juu ya kwamba yeye atakuwa na diwani kamili yenye kukusanya mengi.

- Na ama makasri, vyumba na matofali hivi ni vifungu vya diwani hii: miongoni mwa sura, vifungu na aya.

- Na ama hivyo visababishi (factors) za ghafla na ambazo zimejaaliwa zikiteremka zikiwa katika madini tofauti tofauti ya mlimani na ambayo yamechangamanishwa katika kujenga makasri haya, basi hivyo ndio yale matukio ya kiulimwengu na kijamii, na matatizo ya kidini na kidunia na ambayo yalikuwa yakiwatokea watu muda baada ya muda katika mambo ya watu wote na ya watu mahususi. Kwa hiyo ikawa muumini miongoni mwao anamjia katika matukio hayo akimtaka fat-wa (rai ya kisheria) na kumuomba mwongozo. Au mkadhibishaji mwenye kuwa na tatizo na kutaka mjadala. Na kulingana na hivyo, maneno ya Allah yalikuwa yakiteremka vifungu vifungu, kwa maana tofauti tofauti kwa tofauti za matukio hayo na vichocheo vyake. Na kwa kiwango cha tofauti zao kiuchache au kiwingi. Na kwa njia za kuwa na aina mbali mbali kiulaini na kiukali… Na miongoni mwa hivi vifungu vifungu vilivyo mbalimbali na kufarikiana ndipo yakaunda mikusanyiko itwayo sura. Na si kwa msingi wa kufanana baina ya vifungu vya kila mkusanyiko katika hayo. Bali ni kuyaweka katika zizi moja kwa kile utakacho miongoni mwa makundi ya namna moja na makundi ya namna tofauti tofauti.

- Ama njia ya ajabu iliyofuatwa katika ujenzi wa majengo hayo kutokana na vifungu vyake – hiyo ndio sababu ya tatu iliyoyanyanyua maswala haya kutoka katika mpaka wa ugumu hadi mpaka kutowezekana – nayo ni kuwa huyo ambaye ameteremshiwa hakungoja mpangilio wa vifungu vyake hadi vikamilike kuteremka. Bali hakusubiri kuijenga sura moja katika hiyo Quran mpaka vipengle vyake vitimie. Bali mwenyewe alikuwa kila anapopewa aya moja au aya nyingi, anaamrishwa kuiweka au kuziweka katika eneo lake papo kwa papo ikiwa imepangiliwa katika sura maalum[1]. Wakati ambapo, aya hizi na sura hizi zenyewe katika kuteremka

---

[1] Othman bin Affaan Allah amuwie radhi amesema: **‘‘Hakika Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake, miongoni mwa yale yaliyokuwa yanamjia katika wakati, anateremshiwa baadhi ya sura zenye idadi kubwa ya aya. Na alikuwa pindi anapoteremshiwa kitu, anawaita baadhi ya waandishi wake, na kuwaambia: hii iwekeni katika sura inayotaja kadha kadha. Na humtermkia aya na yeye husema: ziwekeni aya hizi katika sura inayotaja kadha kadha. Na humteremkia aya, naye husema: iwekeni aya hii katika sura inayotaja ndani yake kadha kadha…’’** Hadithi hiyo.

kwake hazikufuata njia yake ile iliyoifuata katika kuwekwa katika mpangilio. Sura nyingi zimeteremka kwa jumla moja au vipande vipande katika vipindi mbali mbali. Vipande vingine vikiwa baina ya sura nyingine. Na kuna aya nyingi katika sura moja zilizotangulia kuteremka na kucheleweshwa katika mpangilio. Na kuna aya nyingi zilizo kinyume na hivi.

Ndio, kwa hakika vipande vipande vya Quran katika kuteremka kwake na mpangilio wake vilikuwa ni matukio mawili yaliyotofauti. Na ni njia mbili ambazo ni mara chache mno kukutana. Na kwa hakika kutokana na kutofautiana kwake zimetupatia mazingatio makubwa katika mpangilio huu wa ki-Quran.

Na lau kama wewe ungetazama katika hivi vipande wakati vinapoteremka, na ukatazama kile kilichoandaliwa miongoni mwa sababu zake. Basi ungeona kila kipande ni mdhamana wa kuteremka kwa haja kubwa. Au kutokea sababu ya jumla au mahususi. Kwa hiyo, katika hilo ungeona kila moja katika hayo ni utajo uliotokea kwa wakati wake. Na ni kauli ya kuchechemea kwa kichocheo chake. Nafsi haijatanguliza kukihisi kabla ya kutokea kwake na sababu yake. Na katika hilo, pia ungeona kila

---

Imepokewa na Ahmad 1/57, na Abuu Daud katika Asswalaati 786/787, na Attirmidhiyu katika Attafsiiri 3086 na akaipa daraja ya hasani. Na Annasaaiyu katika Fadhaailul Qur`aan 32, na Ibnu Hibbaani katika Swahihi yake (Al-Ihsaani) 43, na Alhaakimu 2/330. Na sheikh Ahmad Shaakir katika Almusnad 1/399 ameipa hukumu ya udhaifu sana. Na vile vile katika Attwabariy 1/102.

- Na iliyosahihi kuliko hiyo ni hadithi ya Othman bin Abii Al-Aaswi pale alipoambiwa na Mtume rehema na amani ziwe juu yake: **‘‘Jibrilu amani iwe juu yake alinijia na kuniamrisha niiweke aya hii katika eneo hili la surah hii ﴿Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu, na kufanya hisani, na kuwapa jamaa (na wengineo) na anakataza uchafu na uovu, na dhulma. Anakunasihini ili mupate kufahamu (mfuate ﴾.** An-Nahli 90. Imepokewa na Ahmad katika Musnadi wake 4/218. Na Alhaithamiyu katika Majmau Azzawaaidu 7/49 amesema: Sanadi yake ina daraja la hasani. Na Ibnu Kathiri katika tafsiri yake 4/516 amesema: na isinadi hii haina ubaya أ هـ .

- Na Assuyutwiyu katika Al-Itikani 1/211 amesema: Makubaliano ya wanazuoni na maandiko yanayofanana yanajulisha kuwa mpangilio wa aya ni kutoka kwa Allah. Na hilo halina utata, ama kwa upande wa makubaliano ya wanazuoni, hayo yamenukuliwa na zaidi ya mmoja. Miongoni mwao ni Azzarkashiyu katika Alburhaani na Abuu Jaafar bin Azzubeir katika Munaasabaatihi, na kauli yake ni: mpangilio wa aya katika sura zake ni kwa mujibu wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na ni amri zake. Bila ya kuwepo na tofauti katika hili baina ya waislamu. UK 189.

moja limesimama lenyewe likiwa halina mfumo ulioainishwa na ambao unalikusanya na lingine katika mpangilio mmoja.

[**Kukusanyika Kwa Sababu Zote Hizi Katika Sura Zenye Vipande Mbalimbali Bila Ya Kutia Dosari Hukumu Za Umoja Wake, Wala Msimamo Wa Mizani Yake. Kwa Hakika Hili Ni Muujiza Wa Miujiza**]

Na lau kama wewe utalitazama hili kwa wakati huo huo, basi ungeliona kila kipande katika hivyo, tayari kimeshaandaliwa mfumo maalum wa kuteremkia, uliotangulia au wa sasa, katika saa ya kuteremka kwake. Na lishawekewa mipaka ya eneo maalum ndani ya huyo mfumo, ni sawa sawa ukiwa umecheleweshwa au kutangulizwa[1]. Kwa hiyo kupitia mgawanyo huu wa papo kwa papo wenye mipaka maalumu utaona kuwa, katika hilo kuna mpango wenye maelezo ya kina yaliyo jumuishi. Katika hayo kumeandikwa maeneo ya vipande vyote kabla ya kuteremka kwake. Bali kabla kuumbwa sababu zake. Bali kabla ya kuanza hatua zilizoandaliwa za kutokea sababu. Na kwamba mpango huu uliopangwa kwa mipaka na maelezo yenye umakini sana, ulipangwa kwa muundo na maazimio yenye mkazo mkubwa. Kwa hiyo, hakuna kipande kilichowekwa katika sura fulani, kisha kikavushwa na kuwekwa katika sura nyingine. Na hakuna kipande kilichojaaliwa katika sehemu fulani katika sura ya mwisho au ya kwanza, kisha milele, kikapata kitu cha kukigeuza wala cha kukibadili.

Na hapa unasimama kisimamo cha kutahayari juu ya jambo lako. Na unakaribia kupinga yale yaliyo chini ya usikivu wako na uoni wako. Kisha unarejea katika nafsi yako na kuiuliza kuhusu namna ya kuunganisha baina ya kile ulichokiona na unachokiona: - (Je, uteremsho huu sio ule niliousikia sasa hivi ukiwa mpya uliozaliwa siku hii, na ukiwa peke yake ukitegemea sababu yake. Sasa, nina nini mimi nauona sio mpya wala sio wa kipekee? Kana kwamba mimi juu ya uteremsho huo na juu ya Quran yote, lilikuwa ni tukio katika moyo wa mtu huyu kabla ya kudhihiri kwake katika ulimi wake. Na sura hii ilikuwa imeshatungwa katika kifua chake kabla ya kuitunga kwa bayani yake. Na kama si hivyo, iweje anatunga utungaji huu baina ya vipande kimoja kimoja ambavyo kwa tabia yake havielekei kukusanyika

[1] Kwa mfano, kipande hiki wakati wa kuteremka kwake utakiona kikiamrishwa kuwekwa mwishoni mwa sura kadhaa. Na kipande kilicho baada yake kinaamrishwa kuwekwa katikati ya sura hiyo hiyo, mwanzoni mwa idadi maalumu ya aya zake. Na hili linafanya mwanzo wa sura kuja baada ya muda fulani. Na kile kipande kinachofuata kinachukua upande katika sura iliyopita tangu muda fulani… na kuendelea [Daraazu].

pamoja? Kwa nini hakuviacha vikiwa kimoja kimoja kama vilivyokuja vikiwa vimetawanyika? Na je, mbona anapotaka kuvikusanya haviingizi vyote katika mkusanyo mmoja? Au je, mbona hajavigawa makundi yaliyo sawa sawa au yanayonasibiana? Je, unaona, ni kwa kanuni gani amejengea mgawanyo wake na uainishaji wa maweko yake ulio kama hivi kabla ya kutimia kwake yote au kabla ya kutimia fungu katika hayo?

- Je, huenda maweko haya yote yakawa ni yenye kupita katika nasibu na kuafiki tu? Sivyo hivyo, kwa hakika katika kila muweko katika hiyo, kumeshadhihiri kuwa kimekusudiwa chenyewe kwa dhati yake. Kama lilivyodhihiri kusudio katika kila kifungu kifume mfumo mmoja wenye mipaka maalumu na wenye mpangilio na vipimo vyake chenyewe.
- Au je, huenda maweko haya yakawa – hata kama yamekusudiwa – si zao la makadirio yaliyopita. Bali kwa hakika yenyewe ni tajriba ya kupima iliyokuwa ni tunda la fikra za wakati fulani tu?

- Sivyo hivyo, kwa hakika mwekaji wake pale alipoviweka mweko wa *dharba laazibi*[1] kisha hakurejea nyuma na kuubadili wala kuugeuza. Kwa hiyo, Je, ni juu ya nini wamejengea kusudio hilo na mfumo huu?).

Jibu halitokuwa lile ambalo unalisikia katika nafsi yako lau kama litapigwa kelele katika akili yake ya kawaida isipokuwa utasema:

(***Hakika mambo yalivyo hatojasiri katika kina cha yaliyofichikana, kuweka mpango huu wenye maelezo kamili na wenye kuundwa vyema ila mmoja wa watu wawili: mjinga tena mjinga katika kina cha ujinga, au mjuzi tena ni mjuzi aliyejuu ya maendeleo ya kiakili. Hakuna mtu wa tatu).***

- Ima kama alikuwa amemaliza katika kuweka mfumo wa kuitunga na kuweka taswira ya muunganiko wake kabla ya kupata elimu ya yakini juu ya sababu yake, makusudio yake, nyuma yake na hatima yake. Na hakika si vinginevyo, yeye amejengea jambo lake juu ya dhana, kuhisi hisi, kufikirika na kutamani. Na kwa hiyo, huyo ni mtu ambaye yeye mwenyewe alifikia ujasiri wa kutangaza kuwa yeye ni mmiliki wa kile asichokimiliki na kudai ujuzi wa kile ambacho masiku yajayo yatafichua ujinga wake. Na si juu yako wewe ila kumngojea kidogo tu ili uone jambo lake linavyobatilika na kuharibika kile alichokijenga. Na ni mbali mno, au haiwezekani kabisaa ujinga ukazaa mfumo unaoenda vizuri na umadhubuti wenye kubakia.

---

[1] Dharba laazibi ni: Mweko wa lazima uliothabiti. Na mtindo huu umeazimwa, umefanyiwa istiari kutoka katika dharba saifi, pigo ya upanga lililothabiti.

- Na ama kama atakuwa ameshatenganisha baina ya elimu na maono, na kila sehemu katika huo uteremsho, kuipa sehemu yake kwa mizani na viwango. Basi hakuna shaka mfumo wake utakuwa ni mfano wa kufanyika kwa ubora na alama ya uzuri. Lakini kwa hiyo, mwekaji wake haiwezekani awe ndiye mtu huyu. Ila atakuwa amelipata jambo hilo kutoka katika upeo wa juu zaidi kuliko upeo wa nafsi yake. Na mzingo/wigo mpana zaidi kuliko wigo wa elimu yake. kwani, ni kivipi kwa mwanadamu, huku akiwa yeye ndiye wa kuhukumiwa kwa tabia yake ya milele awe ndiye wa kuhukumu? Au iweje iandalike kwake na huku yeye yupo ujingani mwake wa kupitiliza juu vitangulizi vya kazi yake, na iweje awe mjuzi na mwekaji wa matokeo yake yenye maelezo mapana? Je, huyo mtu atakuwa katika jambo moja hilo hilo ni mjuzi na mjinga kwa pamoja? Au awe kwa upande mmoja ni mwamuzi na mwamuliwa kwa pamoja?

Na je, umeona au kusikia kuwa mtu mmoja miongoni mwa waandishi au washairi, ambaye mwanzoni mwa uhai wake wa kifasihi aliweza kudhibiti kila kile kitakachokuja katika ulimi wake miongoni mwa mashairi mazuri au nathari katika matukio mbalimbali mpaka mwisho wa uhai wake duniani. Na tangu siku yake ya kwanza ameweka mpango wa diwani yake inayosubiriwa. Mpango unaotoa maeleze ya kina. Na mpango huo hautosheki tu na makadirio ya milango yake na sura zake, bali kwa kila mlango inakadiria idadi ya yaliyomo miongoni mwa maelezo au kasida. Na inaainisha sehemu maalumu isiyotangulizwa wala kuchelewesha kwa kila kimoja katika viwili hivi. Mpaka itakapokuja katika sababu yake inairejesha katika sehemu bila kungoja wala kusita. Kisha anafanikiwa katika zoezi hili mafanikio yasio na dosari yanayotekelezeka katika hukumu zake zote na kuhakikisha ndoto zake. Na kwa hiyo mpangilio wake unasimama sawa sawa baina ya vipande vyote hivi, bila ya kutanguliza chochote au kuchelewesha chochote katika hivyo. Na bila ya kuzidisha baina yake au kupunguza chochote?

Naapa, kama suala hili lingekuwa sahihi kwa yoyote yule miongoni mwa wanadamu, basi lingekuwa sahihi kwa Nabii wa Quran. Lakini mwanadamu ni mwanadamu tu. Na yule asiyekijua kile kitakachomtokea katika maisha yake miongoni mwa vichocheo vya kauli na fani zake, basi huyo yupo mbali mno na kufahamu kila kitu kuhusu maandiko. Na huyo yu mbali mno sana na kufahamu kila kitu katika daraja za maandiko. Bali mwanadamu, pale kichocheo cha kusema kinapomchochea na kumpitikia kitu. Basi mtu huyo hatovuka moja ya hatua mbili katika hilo. Kwani yeye:

- Ima akiache kama kilivyo, kikiwa ni tukio lililojitenga. Na hivyo atafanya katika vile vilivyo mfano wa hicho. Mpaka atakapofikia lengo/upeo atarejea na kuchukua katika hilo kukusanya na kutenganisha, kuweka milango na mipangilio.
- Na ima afanye kuunganisha maandiko hayo, yakifuatana kulingana na kuja kwake, kwa hiyo la mwanzo ndilo litakalokuwa la kwanza.
- Na ima jambo la tatu, nalo ni kuvijaalia katika makundi mawili. Na aendelee kuvichanganya kwa ukaribu na umbali, kuliani kwake na kushotoni kwake na katikati yake. Kwa njia hii yenye mipaka yake, na kwa njia hii iliyoparaganyika na iliyotata. Aijaalie kila sehemu ya tukio katika hayo liwe na sehemu iliyosajiliwa haibadilishwi sehemu hiyo wala haitolewi. Kisha naye kwa ufundi huo, awe na tamaa ya kutoa diwani kamili yenye vigawanyo na milango. Yenye mfumo na mpangilio mzuri, imeungana, imeshikamana kwa ujumla wake na ufafanuzi wake neno kwa neno, herufi kwa herufi. Matamanio hayo mtu hawezi kuyapata isipokuwa atapata kinyume cha kile anachokitamani).

* * *

Ahaa haya, wewe umeshaijua njia ya utunzi wa mwanadamu katika ufundi wa kibayani na usiokuwa wa kibayani. Na umeshaona umbali wa kile kilicho baina yake na baina ya njia ya utunzi katika vipande vya Quran. Na umeshajua kipi kilikuwa kinapaswa kutokea katika mfumo wa ki-Quran kulingana na njia hii ya ajabu. Kwa sababu tatu[1] ambazo kutokana na sababu hizo, maneno hayawezi kunyooka hata kidogo, wala hayatoungana na kujumuika.

Na kwa sasa hebu tazama, je, sababu hizi, licha ya kupatikana zote, ziliweza kupata kitu chochote katika kunyooka kwa mfumo wa sura zilizotungwa kwa njia hii?

Ama warabu ambao walipewa changamoto na Quran kwa kuleta sura moja tu iliyo kama Quran. Na kwa hakika ulishajua kuwa lau kama katika mfumo wa sura moja katika hizo wangelipata upenyo wa kuingiwa na tamaa kwa mwenye kutamani, au upenyo wa kutumbukia kwa mwenye kutumbukia, basi wao wangekuwa na shauri lingine. Na wao ndio wao.

---

[1] Nukta tofautofauti za kimaana. Mazingira ya nyakati zilizotengana. Maweko ya utunzi ya haraka haraka na yaliyo tawanyika [Daraazu].

Na ama wanaumbuji wa baada yao, na bado tunaendelea kuwaita kuwa wao ni wenye kupigiwa mifano ya uzuri wa muundo na kudhibiti mtiririko kwa hii Quran pale inapohama kutoka fani moja kwenda fani nyingine.

Na ama wewe, hebu elekea wewe mwenyewe katika kuzingatia mfumo huu mtukufu ili ujue ni kwa mkono gani imewekwa bayani yake? Na kwa jicho gani umetengenezwa mfumo wake? Hadi ukawa kama alivyouelezea Allah ﴿**Quran iliyoteremshwa kwa lugha ya Kiarabu (ifafanuayo vizuri); isiyo na kombo (upotofu ﴾.** Az-Zumar 28.

Hebu ikusudie sura moja miongo mwa zile sura zinazogusia maana zaidi ya moja – na wingi ulioje wa sura hizo katika Quran, hakika sura hizo ndizo nyingi – na ihamishe fikra yako pamoja na sura hiyo kutoka hatua moja hadi nyingine. Kisha lirejeshe jicho lako mara ya pili: Vipi umeanza? Na vipi umemalizia? Na vipi umekutana na maweko yake na kuyasawazisha? Na vipi umezipokea nguzo zake na kuzikumbatia? Na vipi mitangulizi yake imekuwa miwili miwili kwa matokeo yake, na za mwanzoni mwake zimezikanyaga za mwisho wake? ..

Na mimi kwako wewe ninadai kuwa wewe kamwe hautopata katika mfumo wa maana zake au majengo yake kile kitakachokujulisha kuwa sura hizi zilikuwa zimeteremka zikiwa kipande kimoja au vipande kadhaa. Na utadhani kuwa zile sura saba[1] ndefu katika sura za Quran. Kila moja katika hizo imeteremka kwa mara moja. Hadi pale historia itakapokuelezea kuwa

[1] Na ikiwa sura hizi, licha ya urefu wake na wingi wa vipande vyake, kimfumo hazioneshi kutengana. Sasa dhana yako ipoje kwa zile sura za chini yake miongoni mwa sura fupi fupi. Pale ambapo, hata katika baadhi ya sura fupi zimepitikiwa na kuteremka vipande vipande. Kama Dhuhaa, Iqraa na Almaauuni. Sura ambazo kila moja iliteremka tofauti kwa vipande viwili [Daraazu].

- Nilisema: kwa Suratu Almaauun, Ibnu Abbas, Abdullah bin Az-Zubeir na Jamuhuri ya wanazuoni wamepita mapito ya kuwa yenyewe ni ya Makka. Na zipo riwaya nyingine zinaonesha kuwa yenyewe ni ya Madina, kutoka kwa Ibnu Abbas, Qatada na Addhwahaaki. Basi huenda huku kuwa na shaka juu ya sura hii katika hilo kunahusiana na kutajwa kwa swala ndani yake, na wale wanaoipuuzia, hao ni wanafiki. Na wanafiki hawakuwepo Makkah. Ama kuteremka vipande vipande kwa sura hizi hakujapokelewa kutoka kwa yoyote ila kwa mwanazuoni mkubwa aitwaye Hibatu llahi bin Salaama Almaqriyu (Aliyefishwa mwaka 410 H) pale alipopita (katika kitabu chake cha Annaasikhu Walmansuukhu uk 205) mapito ya kuwa nusu yake imeteremka Makkah kwa sababu ya Al-aaswi bin Waaili Assahamiyu. Na nusu yake nyingine imeshuka Madina kwa sababu ya Abdullah bin Ubayyi bin Saluuli ambaye ni mnafiki.

zenyewe zote au nyingi[1] zao zilitemka vipande vipande. Au utasema kwa hakika zenyewe baada ya kuteremshwa zikakusanywa kwa kutofautishwa. Kwa hakika katika kuteremka kwake zilikuwa zimetofautishwa na hazikukusanywa. Kama vile jengo lililokuwa limesimama juu ya misingi yake. Na pale lilipotakiwa kuondoshwa kama lilivyo kutoka sehemu lililokuwepo na kupelekwa sehemu nyingine likakadiriwa pande zake na kurekodiwa nambari za vipande vya matofali yake.Kisha likatawanywa vipande vipande na baada ya hapo kila kipande kikajulikana sehemu yake ya kuwekwa kwa nambari yake. Na kutahamaki jengo hilo likarudi likiwa madhubuti huku kuta zake zikishikamana vizuri zikiwa katika umbo kama lile umbo lake la mara ya kwanza[2].

Ndio, kwa hakika wewe utasoma sura ndefu iliyoteremka vipande vipande na ambayo mtu mjinga ataidhania kuwa ina maana zilizoparaganyika zilizowekwa hovyo hovyo. Na yenyewe ni kundi la majengo yaliyokusanywa kibahati bahati tu. Lakini ukitahamaki, na utazitafakari vizuri sura hizo utaziona kuwa zenyewe ni jengo lililoshikamana vizuri lililojengwa kwa makusudio yote tena juu ya misingi

---

[1] Shaka hii ni mkabala wa tofauti za wafasiri katika Surat Al-An`aam. Wanazuoni wengi wamepita mapito ya kuwa sura hii imeteremka yote kwa pamoja. Na hakika Attwabariyu na wengineo wamepokea kauli hii kutoka kwa Ibnu Abbasi ikiwa ni hadithi mauqufu kwake. Na imepokewa kutoka kwa Ubayyi bin Kaabi ikiwa hadithi mar-fuu kwa sanadi yenye udhaifu. Na lau kama yale mapito ya wanazuoni wengi yangekuwa sahihi katika surah hii basi mapito yao yangekuwa ni miongoni mwa jumla ya ushahidi wa kuwa moja ya njia ya mpangilio katika sura zilizoteremka vipande vipande na nyinginezo. Kwa sababu mfumo wa kuhama baina ya maana katika sura ya Al-An-aam unafanana na wa sura zilikubaliwa na wote kuwa zimeshuka vipande vipande [Daraazu].

- Nimesema: kuna hadithi nyingi zilizotaja kuteremka kwa Sura ya Al-An-aam kwa mara moja. Kutoka kwa Ibnu Abbas, Asmaau binti Yazid, Ibnu Omar, Ali bin Abii Twaalib, Ubayyi bin Kaab, Mujaahidi, Abii Juhahfah, Atwaa, Shahri bin Huushabi na wengineo. Tazama Majmau Azzawaaidi 7/19, 20. Tafsiri ya Ibnu Kathiri 3/233, 2334. Adduraru Almanthuuru cha Assuyutwiyi 3/3, 4. Al-Itqaani cha Assuyutwiyi 1/18.

[2] Miongoni mwa yanayothibitisha maana hii ni: Hadithi ya Ibnu Abbas: ‘‘Quran iliteremshwa yote kwa pamoja hadi katika mbingu ya dunia katika usiku wenye cheo (lailatul Qadiri), kisha baada ya hapo ikateremka kwa miaka ishirini. Kisha akasoma: ﴿**Na Quran tumeigawanya sehemu mbali mbali (kwa kuiteremsha kidogo kidogo) ili uwasomee watu kwa kituo; na tumeiteremsha kidogo kidogo (iwe wepesi kuhifadhika** ﴾**.** Bani Israil 106. Imetajwa na Alhaafidhu Ibnu Kathiri katika Fadhaailu Al-Quran uk 6 kutoka katika njia ya Abii Ubaid Alqaasim bin Salaam amesema: Isnadi hii ni sahihi أ هـ . Na kwa riwaya iliyo kama hiyo ipo katika Fadhaaili Al-Quran ya Annasaaiyi 14, 15. Na Assuyutwiyu katika Adduraru Almanthuuru 4/371 ameiegemeza kwa Annasaaiyi, Ibnu Jariir, Ibni Abii Haatim na Alhaakim na kuipa daraja la sahihi. Na Ibnu Mardawayhi na Albayhaqiyi.

na nguzo imara. Na juu ya kila msingi katika misingi hiyo kumesimamishwa pande na mitawanyo. Na katika kila pande katika pande zake kuna matawi mafupi au marefu. Na utaendelea kuhama baina ya vifungu vyake kama unavyohama baina ya vyumba na viwanja katika jengo moja lililowekewa ramani yake mara moja. Huhisi chochote miongoni mwa kukataana kwa maweko katika mikato yake na mshikamano wake, wala chochote cha kuachana katika kutoka njia moja kwenda nyingine; Bali utaona baina ya makundi tofauti tofauti kuna ukamilifu wa kuzoeana. Kama unavyoona baina ya vitu vya kundi moja kukiwa ni mwisho kupangika na kushikana. Yote hayo yametokea bila kujikalifisha wala kutaka msaada wa kulitekeleza jambo hilo kutoka nje ya maana yenyewe. Na kwa hakika yenyewe ni mtiririko mzuri, wenye tangulizi zenye kupendeza mwanzoni mwa kila lengo na kipande chake na wakati wake. Kinakuonesha kile kilichotengana kimeungana na kilichotofautiana kimezoeana.

Na kwa nini tunasema kuwa maana hizi zinashikamana katika sura moja kama vinavyoshikamana vyumba katika jengo? Laa hasha. Bali hakika yake inashikamana ndani yake kama vinavyoshikamana viungo katika mwili wa mwanadamu. Kwa hiyo baina ya kila kipande na jirani yake kuna mafungamano ya kimaudhui kwa sehemu mbili hizo. Kama vile mifupa miwili inavyokutana katika maungio na huku juu yake kukiwa na mtandao wa nyavu zenye kuungana na zinazoizunguka sana mifupa miwili hiyo. Kama vile viungo viwili vinavyoingiliana na mishipa midogo na mishipa mikuu. Na nyuma ya hayo yote yanatiririshwa katika ujumla wa sura kwa mwelekeo maalumu. Na kwa ujumla wake inatekeleza lengo mahususi, kama vile mwili unavyochukua kisimamo kimoja. Na kusaidiana kwa pamoja katika kutekeleza lengo moja licha ya kutofautiana kazi za kila kiungo.

Ee! Nywele zangu mimi!! Ikiwa viungo na sehemu zote zinazounda sura zinahusiana na sababu ambazo zote hazikuwa ni zenye kuwepo wala kutarajiwa kuwepo. Na ili kutimiza kifungu hiki, ikawa hapana budi kutokee kwa sababu zote hizo, tena katika zama za kuteremka kwa Quran na kushughulika katika kuibainisha Quran. Basi ni kipi kile ambacho kimeutiiisha mzunguko wa anga na kuuweka katika mfumo wa vifungu hivi vya Quran na kuyafanya matukio haya yote yawe yanakuja nyakati za kuteremka Quran? Kwa nini haijaafiki katika tukio hata moja katika matukio hayo kuwepo kwa kutofautiana na ulimwengu uliopo. Na siku hiyo, mfumo

huu wa anga utaharibika na kusababisha kuja kwa sura miongoni mwa sura za Quran ikiwa imevurugwa mwanzoni mwake au mwishoni mwake au baina ya hayo?

***Je, matukio hayo ya kimaumbile si yenye kutii, na kutoa ushirikiano wa kina kwa mfumo wa vifungu hivi vya ubainifu daima. Vikiwa vinatoa ushahidi wa wazi juu ya kuwa kauli hii na kitendo kile vilikuwa vinakuja kutoka katika njia moja. Na hakika yule aliyeyatoa maneno haya kwa elimu yake ndiye huyo huyo aliyevitoa viumbe hivyo kwa matakwa yake[1]?***

Bali ee nywele zangu! Lau huyu mwanadamu wa ajabu ambaye Quran imekuja kwa ulimi wake, angekuwa ameshayadhibiti yale ambayo yatazaliwa na nyakati miongoni mwa matukio ya baadaye na ya kushtukiza madogo kwa makubwa katika upeo wa maisha yake. Kisha akakadiria kile kitakachotakiwa na uteremkaji huo wa mafundisho ya Quran. Basi ni kipi kilichomjulisha huo mfumo wa kibayani ambao utawekewa muundo wa mafundisho hayo? Kisha ni kipi kilichomjulisha, ni mafundisho gani katika haya yatakuwa kiambata cha sehemu hii au ile? Ili ajiandae kwa ajili ya viambata hivyo kabla ya kuja kwake na hivyo kila sehemu aiwekee saa ya kuteremka kwake kipande kipande kikiwa kinaendana na kiambata chake kilichoainishiwa, hadi kitapokuja, basi kishikamane na kipande chake na kuchanganyika na kiambata chake na hivyo kuwa jozi madhubuti. Kwa nini, pale kila kiambata kilipokuja, kilipata katika kiambata chake jirani yake ambaye hawezi kuwa na jirani mwingine, na wala yeye kupatiwa jirani mwingine. Na pembezoni mwake kikapata sehemu ambayo inakisubiri, sehemu ambayo si finyu ikamletea msongamano na kumbana, wala si pana mno ikaondoa muunganiko baina yao. Bali kimeipata hiyo sehemu ikiwa imekadiriwa kwa vipimo vyake. Hadi inafikia kuwa, kwa mwenye kukipitia hana haja ya kutaka kudiriki kufuta hata herufi moja wala kuzidisha herufi moja, wala kubadilisha maweko, na pia hakuna nafasi ya kusema (laiti…) , wala (lau kama …). Bali, vipi kila sehemu katika sehemu hizi ilijua li wapi kundi lake, ni wapi makao yake ya baina yake katika kichwa au kifua au ncha. Hilo ni kabla ya kubainika vitu vingine vilivyo vimoja vimoja na vilivyo makundi makundi.. Mpaka ilipotimia kutawanya sehemu hizo zilizotofautiana, na vipande vilivyopasuka pasuka. Ghafla pazia linainuliwa

---

[1]Sema: Yote yatoka kwa Allah Mtukufu, hakuna wa kuhoji hukumu yake, wala kubadili maneno yake. [ Daraazu].

katika kila sura na mdoli mrembo wenye viungo vilivyokamilika na mapambo yaliyoshikamana vizuri sana!

Mipango madhubuti ilioje hii! Na makadirio mazuri yalioje haya! Na elimu kubwa isiyo poteza wala kusahau ilioje hii! Haisitisiti wala kukawia. Ilikuwa imeshaandaa mfumo kwa ajili ya matirio haya yaliyotawanyika, na katika kutawanyika kwake, umeyaongoza kwenda katika kile alichokikadiria kwa ajili yake. kutokana na vipande hivyo ikafikia akafuma mkufu uliofumika. Na baina yake ukapita mchanganyiko huu wa ajabu?

Utakatifu ni wa Allah! Je, mwenye akili anaona kuwa hii ni elimu ya kibinadamu, na kuwa hii ni rai ya unufu[1]. Mtu wa majangwani anayekisemea kitu: (Lau nikilielekea jambo langu, basi sitorudi nyuma na kusema, ningesema au ningefanya, wala ningetanguliza au ningechelewesha). Hakuwa mwenye vigezo vya kuzitangulia zama na kuyatangulia matukio kwa mazingatio haya ya ajabu? Je, hili peke yake halitoshi kuwa alama inayobainisha juu ya kuwa mfumo huu wa Quran sio maweko ya mwanadamu. Na kwa hakika yenyewe ni ufundi wa yule mjuzi mno na mwingi wa habari? Hapana, inatosha. ﴿**Hawaizingatii nini, hii Qurani? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi.** ﴾ Annisaa 82.

❋ ❋ ❋

Ama kama unataka ushahidi wa kuonekana juu ya usahihi wa kile tulichokieleza katika sura kuhusu mfumo wa vifungu katika sura, licha ya wingi wa sababu za kutofautiana kwake. Na kama utapenda tukuonshe vielelezo vya sura zilizoteremka vipande vipande na namna vilivyoshikamana na kuunda mlolongo mmoja wa kifikra, huku sura zake na vipengele vyake vikiambatana na kufuma kitu kimoja cha kibayani, kinachokumbatiana kwa sentesi na maneno. Je, ni kitu gani kikubwa kinachoweza kuwa ushahidi wa kweli zaidi kukitolea mfano kuliko sura tunayokuwasilishia nayo ni sura ndefu zaidi katika Quran yote. Nayo ndiyo sura iliyokusanya maana nyingi zilizo tofauti tofauti. Nayo ndiyo sura iliyoteremka kwa vipande vingi kuliko sura zote. Nayo ndio sura yenye umbali mkubwa wa kuchelewa baina ya kipande na kipande.

[1] Unufu: wa mwanzo usio na mfano wake uliotangulia.

***Hiyo ndio suratul Al-Baqarah iliyojumuisha aya mia mbili themanini na kitu. Na kwa habari zilizotufikia kuhusu sababu za kuteremka vipande vyake ni kuwa yenyewe imejumuisha sababu za vipande themanini na tisa. Na muda wa kutofautiana baina ya vipande vyake ulifikia miaka tisa kwa idadi[1].***

* * *

Na jua kuwa, kwa sasa lengo letu sio kukufunulia mkusanyiko wa muingiliano wa matamko na maana ambao vifungu vyake vinafungamana vyenyewe kwa vyenyewe na sura hii tukufu. Huu ni upembuzi wa kimaelezo ya kina una sehemu yake katika vitabu vya tafsiri. Hayo, na lau kama tungependa basi tungekuonesha katika kipande kimoja miongoni mwake chenye sababu nyingi zenye upana mno kuliani kwake na kushotoni kwake, vinaungana na jirani yake wa karibu na jirani wake wa pembeni. Katika mtandao wa mahusiano unaotahayarisha macho kwa nyuzi zake. Kiende upande upi? Wala haijulikani ni upi ndio upande ambao uliokusudiwa kwa kusudio la kwanza.

Kwa hakika, tunataka kukuwasilishia hiyo sura muwasilisho mmoja tukichora kwa mwasilisho huo mstari wa mwendo wake kuelekea katika lengo lake. Na kudhihirisha kwa mwasilisho huo, umoja wa mfumo wake wa kimaana katika sentensi zake. Ili katika mwangaza wa ubainifu huu uone namna kila kipengele kilivyotukia na kukaa sehemu yake katika huo mlolongo mkuu.

Isipokuwa sisi. Kabla ya kuchukua yale tuliyoyakusudia, tunapenda kusema (neno) lililoletwa na maongezi haya: Nalo ni kuwa siasa – utaratibu

---

[1] Ndani yake kuna kutajwa ubadilishwaji wa kibla. Kutajwa kwa funga ya Ramadhani. Kutajwa vita vya kwanza vilivyotokea katika Uislamu; kwa sababu yake imeteremka kauli ya Allah Mtukufu ﴿**Wanakuuliza (hukumu ya) ya kupigana vita katika miezi mitakatifu ….** ﴾ Al-Baqarah 217. Zote hizi kuteremka kwake kulikuwa mwanzoni mwa mwaka wa nane Hijiriya. Na ndani yake kuna ile aya ya mwisho iliyoteremka mwishoni mwa mwaka wa kumi wa Hijiriya nayo ndio aya ya mwisho hasa kuteremka katika Quran. ﴿**Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu….** ﴾ Al-Baqarah 281. Na ndani yake kuna sababu zilizo baina yake [Daraazu].

Nimesema: Attwabariy amepokea hadithi ya Ibnu Abbas amesema: **''Aya ya mwisho kuteremka kwa Nabii rehema na amani ziwe juu yake ni ﴿Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu….** ﴾ 6/40 [T Shaakiru] Na mwanazuoni mkubwa Ahmad Shaakir ameipa daraja la sahihi.

Ama kubadilishwa kwa kibla, funga ya Ramadhani na kikosi cha Nakhlati katika jambo mashuhuri linalojulikana ni kuwa haya yote yameteremka mwaka wa pili.

– bora wa kutafiti mfumo wa Quran unataka uwe unafuata hatua hii na kuifanya ya kwanza katika utafiti huo. Mtafiti wa kuchunguza muunganiko wa kimaudhui baina ya kifungu na kifungu asiutangulie. Na huo ndio ule muunganiko uliotawanywa katika marejeo ya aya, mwanzoni mwake na mikato yake – ila baada ya kudhibiti vizuri katika kuangalia sura yote kwa kuhesabu vifungu vyake na kudhibiti makusudio yake kwa namna ambayo inakuwa ni msaada kwake katika kutembea katika maelezo hayo ya kina juu ya ubainifu wake.

Zamani wanazuoni walisema[1]: (Kwa hakika hizi surah, vyovyote zitakavyokuwa kadhia zake, hayo ni maneno mamoja ambayo mwishoni mwake yanahusiana na mwanzoni mwake. Na mwanzoni mwake yanahusiana na mwishoni mwake. Na yote kwa ujumla wake yanalenga lengo moja. Kama sentensi zake zinavyohusiana zenyewe kwa zenyewe katika kadhia moja. Na hakika ya mambo, hakuna kujitosheleza kwa mwenye kutaka kufahamu mfumo wa sura, akawa haihitaji kuitaza sura yote. Kama vile ilivyo, hakuna kujitosheleza juu ya hilo katika vifungu vya kadhia fulani).

Na kwa hili tunajua upeo wa makosa unaowapata wanaotazama katika matukio yaliyo baina ya aya. Pale wanapokaa kitako kutafiti miunganiko hiyo ya visehemu vilivyo baina yake kwa kutazama karibu katika kadhia mbili au kadhia zilizojirani. Wakifumba macho yao hawaoni mfumo huu wa yote yote na ambao umewekwa na sura kwa ujumla wake. Ni mara nyingi kwa huu mtazamo finyu kumletea mwenye kuufuata kupotoka katika lengo. Na mara nyingi unamweka mbali na sehemu tamu tamu zenye uzuri mno katika huo mfumo.

Je, mfano wake katika hilo utakuwa vingine zaidi ya mfano wa yule mtu aliyewasilishiwa koja lililopambwa vizuri kwa vitu vidogo vidogo ili azitafakari nakshi zake, naye akawa analitazama nyuzi kwa nyuzi, na kipande kwa kipande. Huku macho yake hayavuki ukubwa wa eneo la kiganja chake. Na pale alipoliona lina uzi mweupe ukiwa jirani na na uzi mweusi na nyuzi nyingine zenye rangi tofauti tofauti kwa ukaribu au umbali.

---

[1] Kama Abubakar Annaysaporiyu, Fakhri Raziy, Abubakri bin Al-Arabiy, Burhanidini Albaqaaiy, Abu Is-haqa Asshaatwibiy na wasiokuwa wao. Ama andiko lililotajwa hapa, limetoholewa kutoka katika maneno ya Asshaatwibiy katika Almuwaafaqaati. Katika maswala ya kumi na tatu juu ya maneno kuhusiana na ushahidi wa maelezo ya kina. Humo amewasilisha suratul Almuuminuuna mwasilisho wa kiujumla [Daraazu]/

Na hakuona kupendeza kokote katika hizo nyuzi zikikaa jirani baina rangi na rangi. Hakuna kinachompendeza na kumfurahisha[1].

Lakini yeye, lau kama angekunjua macho yake yaende mbali zaidi ya ncha za nakshi, basi angeona uzuri wa kushikamana baina ya kifungu na kifungu. Ambao hajauona baina ya kimoja na kimoja. Na ingebainika kwake kutokana na eneo la kila rangi katika mkusanyiko mwingine, kile ambacho hakikumbainikia yeye hapo kabla. Mpaka alipotupia mtazamo katika koja lote kwa mtazamo wa kiujumla akaona ncha zake na katikati yake zimepangika mkono mmoja zikiwa na maumbo yenye mshikamano na ufundi wa kina jambo linaloleta kupendeza na kuvutia. Hivyo hivyo, mwenye kuitazama Quran anatakikana awe katika kuizingatia kwake namna ya mfumo wa sura na sura za Quran.

(Na neno lingine) linalogusa haja ya mtafiti katika mfumo huo, pale anapoelekea katika hayo matukio ya kimaudhui baina ya vifungu vya sura: nalo ni kuujua muunganiko baina ya kifungu na kifungu. Haimaanishi kuwa vyenyewe ni kitu kimoja au vinafanana au kuingiliana au yale yaliyo kama hayo miongoni mwa miunganiko ya kiaina tu. Kama walivyodhania baadhi ya wenye kutafiti matukio. Kundi miongoni mwao, mapito yake yakawa ni mapito ya kujaribu aina hii ya muunganiko pamoja na kujikalifisha na kulazimisha. Na kundi lingine, pale ambapo halikupata huo muunganiko kwa namna ya karibu, basi, linaharakisha kusema kuwa, katika maudhui haya[2] kuna ufupisho tu. Wakipita mapito ya ada za Warabu za kufanya ufupisho wa maneno.

---

[1] Kumfurahisha: kinachompatia furaha na kumpendeza.

[2] Bali baadhi yao walidai kuwa ufupisho ndio asili ya Quran yote. Assuyutwiyu – katika Al-Itiqaanu katika mada ya kutafuta mnasaba baina ya aya na sura – amenukuu kutoka kwa Abuu Al-Alaa Muhammad bin Ghaanimu ya kwamba Quran, kwa hakika si vinginevyo, imetukia katika ufupisho ambao ndio njia ya Warabu katika kuhama kuelekea katika kitu kisichohusiana. Na hivi hivi imenukuliwa kutoka kwa Izzudini ibnu Abdussalaam kuwa, mtazamo katika minasaba ya aya haipendezi ila katika swala lililoteremka kwa sababu moja. Ama zinapohitilafiana sababu, basi kiunganishi baina yake na aina fulani ya kujikalifisha. Kwa sababu Quran imeteremka kwa muda wa miaka ishirini na kitu ikieleza hukumu mbalimbali zenye sababu mbalimbali. Na kilicho kama hivyo hakiwi na muunganiko wa baadhi yake kwa baadhi. أ هـ Na katika hilo wamepingwa na wanazuoni wengine na wakaonwa kuwa wamefahamu vibaya. [Daraazu].

Ila rai hii na matawi yake ni yenye kupotea zaidi katika makosa kuliko ile rai iliyoitangulia[1]. Na kuichukua rai hii licha ya dosari zake na kuiweka katika Quran basi huko ni kughafilika na kupotoka kukubwa katika kiwango cha umbuji wa Quran, kiwango ambacho Quran inajipambanua nacho kuliko maneno mengine.

Lau kama mpitaji akapita huku akifuta hizo tofauti za kimaumbile baina ya maana tofauti tofauti zinazofumwa na Quran katika sura miongoni mwake. Kwa hiyo ingeiondoshea jambo mahususi mno kwake nalo ni kuwa yenyewe haitiririshi maongezi katika namna moja ya kuyatiririsha tu kunakopelekea kurefusha na kuchosha. Hilo linawezekanaje wakati yenyewe ni mazungumzo yasiyochosha?

Na lau kama yenyewe – kwa ajili ya kudumisha uhuru wa haya maana – ikapita mapito ya kuyafarakanisha na kukata muunganiko wake. Na kuondosha visababishi vya kimaana na kimfumo vilivyopo baina yake. Kwa hivyo, ingeiondoshea jambo lake mahususi lingine. Nalo ni kuwa yenyewe haihami katika habari zake muhamo wa kuruka unaoitoa hadi kuipeleka katika kiwango cha kufarakiana kitoto ambako kunakusanya baina ya habari mbali mbali bila ya mpangilio. Na mfarakano ambao haumpi nafasi msikilizaji kutaka kupata kujua hitimisho la maneno na ufunguzi wa maneno. Iweje iwe hivyo, hali ya kuwa yenyewe ni kauli madhubuti iliyopangwa vizuri?

Sivyo hivyo, bali kuiongelea ni kama vile ulivyojua, kwenyewe kuna pande nyingi. Lakini yenyewe pale inapokusanya pamoja makundi tofauti tofauti haiyaachii hadi itakapoyadhihirisha katika taswira ya kuungana pamoja. Na hadi itakapojaalia katika kutofautiana kwake kwenyewe ndio kuwe nguzo ya kuungana kwake. Na huku kuungana baina ya vilivyohitilafiana bado kunaendelea kuwa kwenyewe ni fundo linalohitaji kufunguliwa katika kila fani na ufundi mzuri. Na hilo ndilo kipimo makini ambacho kinapimia viwango vya uhodari na umakini wa vionjo katika fani na ufundi. Kwa hakika kutathmini mfumo na kurekebisha hali baina ya rangi

[1] Nayo inabana wigo wa kutafiti kuhusu mahusiano kwa kutafuta kwake baina ya maana zilizojirani kwa mahususi. Katika hilo litakapoongezwa kushikamana na njia maalumu katika mahusiano. Nayo ni kuwa katika upande wa uhusiano wa kimaana basi suala hilo linazidisha kujibana na kutaabisha. Na kwa ajili hiyo, rai hii imewapelekea watu wake waende katika moja ya ncha mbili zenye makosa, nazo ni: kujilazimisha au kutoka [Daraazu].

na dondoo nyingi ni jambo gumu zaidi kulifanya na lina tabu mno hasa katika sehemu za rangi moja na dondoo moja.

Na kwa kanuni hii wakati mwingine unaiona Quran ikikusudia vinyume viwili ikiviweka jirani na kwa kufanya hivyo inatoa mazuri yake na mabaya yake mandhari yake ya wazi kabisa. Na wakati mwingine inakusudia mambo yaliyohitilafiana yenyewe bila ya kuwa vinyume na kuyafanya yanashirikiana katika hukumu zake kwa kuyatiririsha baadhi yao kwa mengine katika mtiririko ambao kukabiliana au kuwekana matawi, au kutoleana ushahidi au kung`amua funzo, au kukamilisha au kujihadhari na yasiyokuwa hayo. Na huenda ikafanya kuambatana kwa maana mbili kutukia kihistoria au kuwa jirani kwa vitu viwili katika maweko ya kieneo, hivyo kuwa ndio nguzo ya kuambatana kwao katika mfumo.

Kwa hiyo mtu mjinga asiyejua sababu za kuteremka kwake na tabia ya maeneo yake atayadhania kuwa yenyewe ni kutoka nje ya mada, lakini huko si kutoka bali huko ni kujibu haja za nafsi ambazo zinadai maana hizo. Na kama hakutakuwa baina ya maana mbili mafungamano wala muunganiko kwa nanma fulani miongoni mwa namna hizi na mfano wake. Utaiona Quran inafanya upole katika kuhama kutoka maana moja kwenda nyingine, ima kwa umaliziaji mzuri na utangulizi bora. Na ima kwa kulilalisha umbo la muundo liwe katika muweko[1] ambao ndani yake vitu vilivyo mbali mbali vinakutana. Na vitu vinavyokataana kupeana mikono.

---

[1] Katika njia hii ya kilugha huenda ikawasilishwa siri za ndani mno. Lau kama mtu wa bayani ataulizwa juu ya njia ya uzuri katika hilo, basi angeshindwa kuielezea. Bali hata kama ataulizwa u wapi muweko wa kuunganisha katika hilo. Basi ingekuwa vigumu kwake kuliainisha kwa kanuni za kielimu. Juu ya kwamba yeye, lau angejisahaulisha hayo mavyeo ya kisomi na maswali ya kidadisi na kuiacha nafsi yake na muono wake kisha akaungana na maweko haya kwa kusoma au kusikiliza basi asingehisi kuwa baina yake kuna kitu cha kutoka nje ya mada au kuhama kunakokataliwa na vionjo au anapata tabu katika kusikiliza. Bali atahisi kuwa baina yake kuna roho ya kuungana na utamu wa kuhama kabla hata ya kuongoka na kujua upande wa uainisho wake au sababu maalum ya hilo.

Na yule mwenye kurefusha kushughulika na miundo ya maneno na vionjo vyake kwa ladha yake hadi akabobea katika hilo na kupata ufasaha wa kupambanua baina ya kizuri na kibaya atajipatia yeye mwenyewe vigezo vya kuhukumu hivi. Hata kama haitokuwa katika mfano wa kutolea ushahidi wa kimantiki, basi kwa namna ya kuona ni bora kitaalamu. Na hasa hasa kama atakuwa ni miongoni mwa wale katika mishipa yao kumebakia matone ya damu ya Kiarabu na katika nyoyo zao kuna athari za hisia za Kiarabu. Na yule ambaye maono yamemkosesha kuupata uzuri wa kiufundi katika eneo fulani la Quran basi asiilaumu ila nafsi yake mwenyewe. Na wala asiharakishe kutoa hukumu kabla ya kujiandaa. Na daima akumbuke kuwa kwa kupitia vipimo vya yale

Na haya yote ni njia nzuri lau kama yangetazamwa baina ya umoja wa maana. Yangejitosheleza baadhi yao kwa mengine katika kuusimika huo mfumo.

Ya kwamba utamu wa mfumo wa Quran, kama ulivyojua hausimamii daima katika uzuri wa kuwa jirani baina kimoja kimoja. Bali huenda ukauona umeshatimiza kikundi cha maana kisha unarudi katika kikundi kingine kilicho mkabala wake. Kwa hiyo kunakuwa na uzuri wa maweko katika kuwa jirani baina ya makundi mawili, kunakuwajibisha kuwepo kwa mkabala mzuri baina ya vifungu vya mwanzo vya kila kikundi katika vikundi viwili hivyo. Au vile vile baina ya miisho. Na si baina ya cha kwanza katika kundi hili na cha mwisho katika kundi lile.

Na mfalme wa mambo katika hilo ni kuwa, utazame katika mfumo wa mjumuiko uliowekewa hiyo sura yote kama tulivyokuhusia hapo kabla. Na sasa sisi ni wenye kukukumbusha kielelezo katika hilo lau kama utakiweka machoni pako na kukiangalia vizuri katika sura nyingine basi hilo litakuwa ni mwongozo mzuri katika utafiti wako. Na Allah tu ndio mwenye kuwafikisha.

* * *

---

anayoyapata upande wa muundo wa Quran miongoni mwa kuuona ni mzuri au umesimama. Kwa hakika huyo anajaribiwa kwa yale yaliyo katika hali yake ya kinafsia kwa upande wa kilugha, je, yapo sahihi au yana kasoro.

Na katika masomo yake ya kilugha kuna upungufu au yamekamilika. Na mambo yalivyo, si kwa vionjo vya wenye upungufu miongoni mwa vizalia wa mfano wake ndio hujaribiwa lugha ya Quran. Itakuwaje hivyo, wakati waliwekwa chini yake watu wake wale waliosujudu kwa umbuji wake huku miongoni mwao akiwemo mwamuzi ambaye wanamridhia hukumu zake. Hili kwa upande mmoja. Na kwa upande mwingine nyinyi mna nafasi ya kusimamia katika elimu ya upasuaji na kutambua siri za kuumba katika baadhi ya viungo vya ndani ambavyo wanasayansi bado hawajajua kazi zake. Je, kuna wanasayansi wowote miongoni mwa wataalamu wa upasuaji wanaomwamini Mungu na wanaoamini maumbile waliohukumu kuwa viungo hivyo havina hekima wala faida? Sivyo hivyo! Kwa hakika wao, pale yalipowashangaza wao maajabu ya uumbaji katika viungo vingine vya mwili. Kwa kile kidogo wasichokijua hawakuweza kusema vingine ila kukiri kwa ujumla ya kuwa kiungo wasichokijua kina hekima yake ila bado haijagunduliwa na sayansi. Kisha haupiti muda wanagundua hekima yake kutokana na kutaabishwa na hima za kufanya tafiti na kuungwa mkono na uwezeshaji wa Mungu. [Daraazu].

## MFUMO WA KUFUNGA MAANA KATIKA SURATUL BAQARAH

Jua ya kuwa surah hii licha ya urefu wake, umoja wake unaundwa kwa: Utangulizi, na makusudio manne na hitimisho. Kwa mpangilio huu:

(Utangulizi): unazungumzia kulitambulisha jambo la hii Quran[1]. Na kubainisha kuwa yale yaliyomo ndani yake miongoni mwa mwongozo umefikia upeo wa uwazi kiasi ambacho hakuna shaka ndani yake kwa mwenye moyo ulio salama. Na kwa hakika, anaukataa mwongozo huo yule asiye na moyo au yule ambaye katika moyo wake kuna ugonjwa.

(kusudio la kwanza): kuwaita watu wote kuingia katika Uislamu.

(Kusudio la pili): kuwaita ahlu kitabu (watu wa kitabu – Wayahudi na Wakristo) mwito wa kipekee waache batili zao na waingie katika dini hii ya haki (kweli).

(Kusudio la tatu): Kuwasilisha sheria za dini hii kwa maelezo mapana.

(Kusudio la nne): Kutaja hali na mwelekeo wa kidini ambao unasukuma katika kudumisha sheria hizo na kujikinga dhidi ya kwenda kinyume nazo.

(Hitimisho): Kuwatambulisha wale ambao wameitikia vizuri wito huu wenye kujumuisha makusudio hayo, na kubainisha yale yanayotarajiwa kwao kwa sasa na kwa baadaye.

* * *

[1] Juu ya utafiti wa kwanza umejua kuwa tamko Quran humaanisha likiwa lote lote na likiwa vipande vipande. Na mwashirio kwa hapa unafaa kuelekezwa kwa Quran ya kiujumla, na kuelekezwa kwa suratul Baqarah kwa sifa mahususi. Na kwa hakika tumetaka iendelee kubakia katika uwezekano huu ili kulifuata andiko la Quran Tukufu: ﴿ **Hiki ni Kitabu** ﴾ kwa sababu mwashirio hapa ni kwa katika uwezekano huo pia. [Daraazu].

Mapenzi yetu kwako ewe msomaji mwema, pale unapodurusu pamoja nasi maelezo ya kina juu ya mfumo huu ufunue msaafu uwe mbele yako ili uwe miongoni mwa wale wenye yakini na usahihi wa kile tunachokionesha katika kila hatua.

## Utangulizi

### [**Unazungumzia Kulitambulisha Jambo La Hii Quran Na Kubainisha Uwazi Wa Mwongozo Wake**]

Katika aya ishirini [1 – 20]

**(1)** Sura hii tukufu imeanza kwa herufi tatu zilizo moja moja na ambazo Warabu hawakuwa wamewahi kutoa kama hizo, katika lugha zao za mjazo wala katika nyimbo zao. Kwa hakika walichokizoea kutoka kwa wasomaji na waandishi katika kuanza mafundisho yao ya kutamka alfabeti kwa watoto ni: ﴿ **A - Alifu. L - Laam. M - Miim** ﴾ [1][1].

Na vyovyote itakavyokuwa, kuhusiana na suala la maana iliyokusudiwa na herufi hizi, na siri ambayo kwa ajili yake herufi hizi zimewekwa hapa. Kwa hakika, kuzitanguliza mbele katika mazungumzo pamoja na ugeni wa mfumo wake na maweko yake. Katika mambo yake, yenyewe inaamsha masikivu na kuzielekeza nyoyo ziende katika kile kinachofuata baada ya muundo huu mgeni.

**(2)** Na kuambatana na hizi herufi tatu zimeambatanishwa sentensi tatu:

Ama ya kwanza yao ni tangazo kwa msikilizaji ya kuwa kile utakachosomewa sasa hivi ni kitabu bora kabisa walichopewa watu. Na katika uwepo hakuna kinachofaa kuitwa kitabu bora ukilinganisha na hiki – ﴿**Hiki ni Kitabu** ﴾ [2].

Ama aya mbili zifuatazo zenyewe zinakazia hukumu hii kwa hoja na ushahidi wenye nguvu. Je, ubora wa kitabu hautokani na kile kilichomo ndani yake miongoni mwa mambo ya haki yasiyo na dosari za batili? Je, ukamilifu wa haki hii haufai kuwa nuru isiyotikiswa na utata? Au je, si ukamilifu wa ukamilifu baada ya hiki na kile, kuwa hiyo haki ni miongoni mwa mambo yanayogusa haja za watu za kutaka nuru ya njia na kusimikiwa ushahidi wa hilo pale wanapopata utata wa kutojua njia sahihi na panapokuwa na njia panda nyingi? Hiyo kwenu nyinyi, ndio Quran yenyewe inayokusanya haya mambo matatu yaliyobora kabisa: Yenyewe ni Haki safi

[1] Kuanzia hapa, wakati wa kutaja aya za suratul Baqarah: Hutajwa nambari yake tu.

isiyo na batili ndani yake. bali yenyewe ni haki yenye kudhihiri isiyo na utata wa batili ndani yake. Kisha baada ya hayo yenyewe ni mwongozo wa wazi unaowatoa watu kutoka katika viza na kuwapeleka katika nuru ﴿**Hakina shaka ndani yake, ni mwongozo** ﴾ [2].

Hivi hivi ndivyo yalivyo maweko ya sentensi tatu hizi baada ya herufi tatu hizo. Zikiwa katika maweko ya kuashiria makusudio baada ya kuzindua juu ya jambo hilo.

Na hivyo hivyo mlezi mwema (huanza) mazungumzo yake yaliyo matukufu kwa kuwanyamazisha watu na kuvuta usikivu wao. Na anafuatisha kwa kutumia njia zenye kuleta shauku na zinazowaamsha wayaelekee mazungumzo yake kwa kutaka kupata faida.

**(3)** Kitu cha kwanza kinachotazamiwa na nafsi baada ya kusikia wasifu huu mzito wa Quran na mwongozo wake, ni kutambua athari itakayoitoa kwa watu na kiwango cha mwitikio wao juu ya wito wake. Basi kukawa na haja kubwa kutiririsha mazungumzo ili kubainisha ukweli huu wa ajabu. Nao ni watu kugawanyika katika hilo na kuwa makundi matatu:

- Kundi linalokiamini.
- Kundi linalokipinga (linalokikufuru).
- Na la tatu lina shaka shaka limetahayari, halipo huku wala halipo kule.

Je, waionaje inavyohama kutoka kuzungumzia kuhusu kitabu hiki na kuhamia katika kuzungumzia watu? Je, kiyafanye mazungumzo kuhusu watu hao ni mazungumzo mapya kabisa? .. Au ayatiririshe katika mtiririko wa kuyadiriki yale yaliyo kabla yake? ..

Kitu chochote katika haya hakijatokea. Lakini hebu itazame ikiwa imechanganya hayo mazungumzo ya aina mbili kwa mchanganyo ambao ni wa ajabu sana unamuacha mtu mwenye uerevu wa kina juu ya mabadiliko ya mienendo ya kauli asielewe kilichotokea baina ya mazungumzo mawili hayo katika suala la muhamo. Hilo ni kuwa yenyewe, hapo mwanzoni haikuwasilisha mtajo wa hayo makundi mawili ya mwishoni, bali iliyaacha kana kwamba Quran haikuteremka kwa ajili yao. Kisha ikalikusudia kundi la kwanza na kuyafanya mazungumzo kulihusu kundi hilo kuwa ndio ukamilifu wenyewe wa mazungumzo ya mwongozo wa Quran kwa kusema, hakika chenyewe ni ﴿**uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini..** ﴾ [2-3]. Kwa hiyo hii (laam ya kujarish - Kihusishi 'kwa' –

Preposition) ndio daraja la siri ambalo maneno yameteleza juu yake na kumiminika mmiminiko mmoja kwenda katika mwisho wa mazungumzo yanayowahusu wamchao Mwenyezi Mungu.

**(4)** Kwa hakika upungufu wa kutonufaika na mwongozo wa Quran kwa kundi hili peke yake baada ya maelezo ya Quran kuwa yenyewe ni haki ya wazi isiyo na shaka ndani yake, umekuwa ndio unaostahiki hasa kuzingatiwa kuwa wenyewe ndio miongoni mwa tofauti za msingi zinazoamsha kustaajabu mno katika moyo wa msikilizaji. Kwani, ukweli wa Quran unawezaje kuwa na daraja hii ya uwazi kisha isiingie katika moyo wa kila anayeisikiliza?!

Na kwa upande mwingine Nabii huyu mwenye huruma katika umakini wake uliofikia upeo wa juu katika kuuita umma wake, na kupupia sana juu ya kuwaongoza, alikuwa na msimamo wa mwenye kuwa na taswira katika jicho la mwenye kumuona akiwa na taswira ya mwenye tamaa ya kutamani watu wote waamini, mwenye kudhani kuwa matumaini yake haya yatakuwa yenye kufikiwa na yeye pale tu atakapofuata sababu za kawaida za kufanikisha hilo. Kana kwamba yeye anaona kuwa, baina yao na mwongozo hakuna kitu ila sauti ya Quran ifike katika masikio yao na kutahamaki wao wanakuwa Waislamu. Hilo, licha ya kwamba kwa sasa Quran inakaribia kuanisha jukumu lake kwa kusema: (Kwa hakika atakayenufaika na mwongozo wake ni yule atakayekuwa miongoni mwa wamchao Mwenyezi Mungu). Kwa hiyo uainisho huu ukawa ndio dhana iliyomfanya Mtume amuombe sana Mola wake kwa kusema: Utakatifu ni wako ewe Mola wangu. Mbona watu wote hawaongoki nayo!

Kwa hiyo ikawa ni wajibu kwa Quran kuusimika ukweli kwa taswira ya kukata kabisa kwa kila mwenye tamaa na shaka, ikiituliza nafsi ya mwenye kutaka kile kisicho na njia ya kukifikia. Na pamoja na hayo, kubainisha vizuizi vya kimaumbile vya kuzuia ujumla wa mwaongozo wa Quran, kwa mtindo unaoitakasa Quran yenyewe na kuiepusha na makando kando ya kuwa na upungufu. Na kuurejesha huo upungufu katika kukubali kwa mwenye kukubali na sio kwa utendaji wa mwenye kuutengeneza huo uwongofu. Na je, inawezekana kufumbia macho uhodari wa tabibu, ikiwa mgonjwa atatumia dawa kijinga na hatimaye kufariki kwa ujinga wake? Na je, jua linadhurika endapo kipofu au anayejitia upofu atashindwa kunufaika na mwanga wa jua? – ﴿**Hakika wale waliokufuru (kwa ukaidi tu na inadi) ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye; hawataamini.** ﴾ 6.

Hivi hivi, mazungumzo kuhusu waumini waliotangulia kuwa na wema yanahama na kuelekea kwa makafiri ambao ni haki yao neno la kuadhibiwa. Na hivyo si kwa njia ya kuyaambatanisha hayo mazungumzo ya aina mbili katika lengo moja kwa mara ya kwanza. Kwani ingekuwa hivyo basi zungumzo moja lingeunganishwa kwa lingine kwa kiunganishi. Bali limekuja kwa njia iliyojengewa baadhi ya maneno kwa mengine, yakijibu swali hili ambalo limetamkwa na hali halisi ya mambo, na kuondoa huo mshangao ambao umeamshwa na kauli iliyotangulia. Na hiki ndicho kinachoitwa (istiinaafu Albayaaniy – kuanza upya kibayani) na wanazuoni wa balagha.

**(5)** Kisha mazungumzo yakaendelea kuwazungumzia hawa makafiri hadi mwisho wake. Wenye kufanana wakaunga na wafanana nao na kwa hiyo kundi la tatu likaunganishwa na kundi lenzake. Kwa sababu wao wote wanashirikiana katika kuwa kando na mwongozo wa Quran. Nyoyo zao zinafanana hata kama ndimi zao zinahitilafiana – ﴿**Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao: ''Tumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho''; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini.** ﴾ 8.

**(6)** Na kwa sasa rejea kidogo katika mfumo wa mazungumzo kuhusu haya makundi matatu. Ili uone namna maweko yao yalivyokabiliana kwa ukamilifu wa kukabiliana; kwa hakika mazungumzo ya kila kundi yamejumuisha mambo matatu zilizopangiliwa kwa mtindo huu: Kuelezea hakika ya uhalisia. Na kubainisha sababu yake. Na kutoa habari inayohusu matokeo yao yanayotazamiwa.

**(Basi hakika)** ya kundi la kwanza ni kwamba wao watu waliopata fadhila za ucha Mungu kwa nguzo zake zote mbili za kielimu na kivitendo. (na sababu ya hivyo) ni kushikamana kwao na mwongozo na kujazwa kukubaliwa kutoka kwa Mola wao. (Na matokeo ya jambo lao) ni kufuzu na kufanikiwa.

**(Na hakika)** ya kundi la pili ni kwamba wao wameepushwa na kumcha Mungu nako ndio kuamini. Na kwamba wao wamepewa taswira ya ubishi huo usio na manufaa hata kama wakionywa. (Na sababu) ni kule kutonufaika kwao na kile walichopewa na Allah miongoni mwa njia za kielimu. Wao wana nyoyo ila hawafahamu kwa nyoyo hizo. Na wana macho ila hawaoni kwa macho yao. Wana masikio ila hawasikii kwa masiko yao. (Na matokeo ya jambo lao) ni kuadhibiwa adhabu kubwa.

**(Na hakika)** ya kundi la tatu ni sifa zilizoambatana kwa nje ni za heri na kwa ndani ni mbaya. Wao wanasema kwa ndimi zao kuwa wao ni wenye kuamini. Lakini katika nyoyo zao hakuna chochote cha kiimani. Na kila moja katika sifa mbili zao hizi ina (sababu) na (malipo). Ama madai yao ya kuwa na imani, sababu yake ni kukusudia kuhadaa, na malipo ya hadaa yanawarejea wao wenyewe. Ama kuuficha kwao ukafiri, sababu yake ni maradhi ya nyoyo zao. Na malipo yake na kuzidi kuwa na maradhi na kupata adhabu chungu.

Na kama tulivyobainisha katika kundi la pili ya kwamba lenyewe limefikia upeo wa juu kabisa wa kung`ang`ania ujinga, upeo ambao hata maonyo hayatasaidia kitu. Hivyo akabainisha katika kundi la tatu kuwa lenyewe limefikia upeo wa juu kabisa wa kujidanganya na ujinga uliopandana. Kiasi ambacho nasaha za mwenye kuwanasihi hazifai kitu. Kwani wao ni wafanya ufisadi huku wakidai kuwa wao wanatengeneza mambo yawe mazuri. Wao ni wapumbavu huku wakidai kuwa wao ni waerevu. Na wapi na wapi kwako wewe uweze kumponya mgonjwa anayeamini kuwa yeye ni mzima?

Kisha kama mazungumzo kuhusiana na kundi la kwanza yalivyohitimisha kwa kuliandikia sifa ya uwongofu na mafanikio, vile vile mazungumzo ya makundi mawili ya mwisho yamehitimisha kwa kuwaandikia[1] sifa ya kupotea na kupata hasara kubwa.

---

[1] Imepita kwa wafasiri wengi kusema kuwa, kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ﴿**Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.** ﴾ 16. Inaashiria kundi la karibu zaidi kutajwa katika hayo makundi mawili nao ni wanafiki. Lakini kilichopokewa kutoka kwa Ibnu Abbas na Ibnu Masuud Allah awawie radhi ni kuwa aya hiyo inarejea kwa makafiri bila kuainisha. Na hii ndio kauli ambayo tunaikubali kwa kuwa inakaa vizuri kimaana na kimfumo. Ama kimaana na kwa sababu mambo yalivyo, hakuna kitu cha kati baina ya uongofu na upotofu (Kuna nini kingine baada ya kuitoa haki zaidi ya kuwepo na upotofu). Ikiwa wote wameukataa uwongofu, na wanashirikiana katika upotofu, kuihusisha ishara kwa baadhi yao licha ya kuwezekana kwake kwenda kwa wote kiwazi wazi. Huko ni kuhusisha bila ya kuwa na kiwajibishi cha kuhusisha. Ama katika mfumo ni kuwa, hiyo ishara ikirejea kwa makundi yote mawili ndipo kunapotimia ule mkabala mzuri baina ya ishara mbili katika kauli yake ﴿**Hao wako juu ya uwongofu** ﴾ [5]. Na kauli yake ﴿**Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.** ﴾ 16. Kisha kwa hili ndipo kunapotimia uzuri wa ufundi katika kuvitofautisha, hivyo vigawanyo kisha kuvikusanya. Kisha kuvitofautisha kisha kuvikusanya. Kwa hakika utaiona Quran ikiyatofautisha hayo makundi mawili katika sifa zao za kimahususi. Kisha inayaunganisha katika sifa hii wanayoshirikiana. Na utaiona hii Quran inarudi katika kuyatofautisha katika kuwapigia mifano. Kisha inayakusanya kwa

**(7)** Ya kwamba sifa hizi za uhakika kwa haya makundi mawili hazikuwa hizo tu zenye kuutosheleza moyo kuona ajabu katika jambo lao. Kilichozoeleka kwa watu ni kwamba wao, kwa hakika wanahitilafiana katika mambo tata na si katika mambo ya hakika yaliyo wazi kabisa. Kwa hiyo tofauti za watu hawa katika suala la Quran licha ya uwazi wake. Inazingatiwa kuwa ni jambo la kinyume na maumbile. Kwa hiyo jambo hilo linahitaji wasifu wa kushabihishwa unaolikurubisha na hali ya kushuhudiwa kihisia, mpaka moyo utulizane katika uwezekano wake.

Na kwa ajili hiyo, Allah ameyapigia mifano makundi mawili hayo yote[1] inayoendana nayo.

---

mara nyingine na kuwa pamoja katika majina mengine ya kipekee kwa kuwaita mwito ufuatao: ﴿**Enyi watu mwabuduni Mola wenu** ﴾ [21]. [Daraazu].

[1] Huenda wewe kwa hapa unaona kuna kitu tofauti na maneno ya wafasiri. Kwani wao wameijaalia hiyo mifano miwili yote inarejea kwa wanafiki kwa sifa ya kipekee. Na sisi tumeyajaalia hayo kuwa yamegawika kwa hayo makundi. Yakitawanywa kwa utaratibu wa kuzunguka. Lakini wewe. Utakaporejea wewe mwenyewe katika vifungu vya mifano miwili hiyo utaona maana ya kuwa mfano wa kwanza unaendana kikamilifu na sifa zilizotajwa na Allah kuwahusu makafiri. Na kwamba ule mfano ambao unaafikiana na sifa za wanafiki, kwa hakika huo ndio ule mfano wa pili peke yake. Kwani watu hawa ndio ambao ﴿**Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao hiyo na kuwaacha katika viza; hawaoni. Viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawatarejea.** ﴾ [17 – 18]. Je, hawa sio hao watu ambao ﴿**Kana kwamba) Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana kifuniko;** ﴾ [7]. Na hivi viza vilivyothibiti na kutulizana na ambavyo havina hata chembe ya mwanga, na ndani yake hakuna kubadilika wala kusitasita. Je, katika hili unaona kuna taswira ya aina za unafiki na njia zake tofautitofauti kwa kutofautiana hali zake? Kwa hakika wewe hutoikuta taswira hii ila katika mfano wa pili pale ambapo kuna kupishana baina ya kiza na nuru na kusimama na kutembea. Na hivyo hivyo katika mfano wa pili utawaona watu wenye masikio na macho, Allah hajawaondoshea vitu hivyo wala hakutaka viondoke. Na haya yanaendana na kauli kuwahusu wanafiki ﴿**Nyoyoni mwao mna maradhi** ﴾ [10]. Amewasifu kwa maradhi na hajawasifu kwa kuwaweka muhuri katika nyoyo na milango ya fahamu.

Naam, inawezekana kuyakubali maneno ya wafasiri kuwa yapo katika njia sahihi kama tutayaunganisha na kiunganishi fulani hivi. Nacho ni hiki, tuseme kuwa mfano wa kwanza inatoa taswira ya hali yao ya nje yao. Nalo ndilo jambo linalobadilika badilika kwao wao kwa kubadilika visababishi. Kwa sababu kubadilika kwao kwa hakika ni kubadilika kwa nje tu na si kwa ndani. Isipokuwa madai haya pia, nayo ni sehemu ya kutazamwa. Kwani ni kipi kinachotujulisha kuwa, huenda aina ya ukafiri anaouficha mnafiki ni aina mahususi. Katika aina hiyo moyo wake unabadilika na kuwa shaka na kusita sita. Na kwa hakika huu mtikisiko ambao tunaushuhudia katika harakati zake za dhahiri katika kauli zake na matendo yake. Kwa hakika hiyo ni taswira ya mtikisiko uliopo nafsini mwake na ambao yeye anauhisi upo ndani yake. Kinyume na aina ya kwanza nayo ni ukafiri wa wenye kudhihirisha, wenyewe ni wa tabia moja iliyojengwa, kama unavyoshuhudiwa na umoja wa athari zake. [Daraazu].

Kundi la ving`ang`anizi waliopigwa muhuri katika nyoyo zao amelipigia mfano wa watu wanaotembea kizani usiku. Kisha mtu mmoja miongoni mwao akasimama na kuwawashia taa ili iwaongoze kwa mwanga wake. Na pale ile taa ilipoangaza yale yaliyo pembezeni mwake, baadhi ya watu hao hawakufungua macho yao kuutazama mwanga huo ung`aao. Bali kwa jambo fulani hivi, wakapokonywa uoni wao na hisia zao nyingine zote zikashindwa kufanyakazi katika mshangao huu. Basi mfano huo ni mfano wa nuru ambayo imemchomozea Muhammad[1] rehema na amani ziwe juu

[1] Na hili vile vile sio lile walilolitaja wafasiri. Wao walijaalia mwenye kuwasha moto ni mfano wa (mnafiki ambaye amejikalifisha kutamka neno la kuingia katika Uislamu kwa hadaa. Kwa hiyo hajanufaika nalo ila kidogo sana katika dunia yake. Kisha muda wake ukiisha na kuoneshwa matendo yake, kutahamaki yupo katika kiza na hasara kubwa). Hivi hivi ndivyo walivyokichukulia kiwakilishi cha wingi katika kauli ya Mtukufu ﴿**Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao hiyo… mpaka mwisho** ﴾ kinarejea kwa ﴿**yule aliyekoka moto** ﴾ kwa kuzingatia maana yake. Baada ya kiwakilishi cha mmoja kurejea kwake kwa kuzingatia tamko.

Na sisi hatudai kuwa fasiri hiyo ni batili, wala hatupingi kukubalika kwake kilugha. Lakini njia tuliyoiwasilisha hapa katika kuufafanua huo mfano inakusanya baina ya kukubalika kwake kiakili na kilugha. Na kwamba wenyewe umeng`amuliwa kutokana na mfumo wa Quran yenyewe. Pamoja na hivyo tunaudhania kuwa upo karibu zaidi na muundo wa Quran na unaendana na umadhubuti wake. Na kama hautakuwa huu, basi na uwe ni mmojawapo wa njia zinazokubalika na Quran.

Ama kuhusu ni vipi tumeng`amua maana hii kutokana na mfumo. Pokea ubainifu wake:

Kwa hakika tumeitazama hiyo mifano miwili tukaona muundo katika mifano miwili hiyo inaelekea mwelekeo sambamba. Kwani mwanzoni mwa kila mmojawapo katika miwili hiyo ni mazungumzo yanayohusu kitu kimoja. Na mwishoni mwa kila mmoja wapo kuna mazungumzo kuhusu kundi fulani. Kisha tukautazama mfano wa pili na tukakiona kiwakilishi cha wingi ndani yake hakirejei katika mrejesho wa kiwakilishi cha umoja. Bali chenyewe kwa makubaliano ya wafasiri kinarejea katika jambo linalofahamika kutokana na muktadha wa mazungumzo nalo ni watu ambao wamenyeshewa na mvua. (Ni jambo linalojulikana kuwa tashibiha hizi ambatani na ambazo zinatazamwa katika mkabala wa kundi kwa kundi hazimaanishi mkabala wa tamko moja baina ya yale yaliyo kabla ya herufi ‘Kaafu – yenye maana ya ‘kama’ na kile kinachofuata kwa mpangilio: bali huenda kuhitilafiana baina ya mawili hayo kama ilivyo hapa ni jambo linalotakiwa na wanabalagha katika ufupisho wa maneno. Na kwa hilo anakusudia kuzindua tangu mwanzo wa jambo ya kwamba kile watakachokizungumzia katika kushabihisha ni miongoni mwa kukunja, kutanguliza na kuchelewesha, kuzindua juu ya kwamba kifananishwa kwake sio chenye kuingia katika hiyo herufi Kaafu peke yake. Kwa hakika chenyewe ni kisa chenye vitengo vingi. Na huku kuingia ni moja ya vitengo vyake. Limekuwa hilo ili msikilizaji abakie akiwa amehifadhi kuzinduka kwake na shauku yake ya kutimiza maneno ambayo kwa hilo ndio kukubaliana baina ya ncha mbili za tashibiha ndio kunadhihiri kwake. Na kwa hilo ndipo inapowezekana kukirejesha kila kitu katika kile kinachofanana nacho – mtindo huu katika muundo wa Quran upo mwingi sana. Miongoni mwao ni kauli yake Mtukufu ﴿**Na mfano wa wale (wanaowalingania) waliokufuru (kwa inadi tu, si ujinga) ni kama mfano wa yule anayemwita asiyesikia ila sauti ya kelele** ﴾ Al-Baqarah 171. Na kauli yake ﴿**Hakika**

**mfano wa maisha ya dunia (na starehe zake namna zinavyoondoka) ni kama maji ﴾** Yunus 24. Na kauli yake ﴿ **Au (mfano pia) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni ﴾ .** Al-Baqarah 19.

Kwa wakati huo tumerejea katika mfano wa kwanza na tukasema, je, haiwezekani ikawa, huenda mfano huu pia ni wenye kwenda katika mwendo wa mifano hii kama mlinganyo wa kimuundo unavyoongoza?.. Kwa hiyo kiwakilishi cha wingi katika mfano huo kinakuwa si chenye kurejea katika ﴿**yule mwenye kuwasha moto** ﴾ bali kinarejea kwa watu ambao moto umewashwa kwa ajili yao. Je, msikilizaji, pale anapomalizia neno ﴿**yaliyo pembezeni mwao** ﴾ anazidi kuhisi kuwa kuna watu wanaofananishwa kwao? Kwani ni haraka mno ubongo unahama kutoka sehemu kwenda sehemu nyingine.. Hatua hii ni ya kwanza, haukupita muda ikaambatishwa na hatua zifuatazo, nazo ni: Kwa hakika hiyo nuru ambayo Allah ameiondosha, kama ingekuwa ndio hiyo nuru ya watu hao, na yenyewe haukuwa ule mwanga wa moto uliowashwa na mwashaji. Basi huo moto haukuzimwa wala mwanga wake haukuondoshwa. Sasa ni kipi kitakuwa ndicho kilichopigiwa mfano wa huu mwanga ambao wenyewe umebakia na kilichoondoka ni kingine?.. Je, hauwezi kuwa wenyewe ndio mwanga wa mwongozo wa kweli na ambao, Allah amekataa kuufanya vingine ila kuutimiliza hata kama makafiri watachukia. Kisha nani atakuwa ndiye mpigiwa mfano wa muwasha moto? .. Je, huyo hawezi kuwa ndiye yule mwongozaji mkuu rehema za Allah ziwe juu yake.. Kwa hakika yeye aliwasha mwenge wa mwongozo wa Uislamu. Yaani ameshughulikia kuuwasha mbele ya vimbunga vya fitina, pepo kali za upinzani mkali. Na pale alipouwasha na kuangaza yale yaliyo pembezeni mwake bila kujali harakati za maadui wa haki, ambao ujinga na husda vimezila nyoyo zao. Basi uoni wao ukapofuka na wakawa, kila huo mwanga unapozidi kuangaza na kuchomoza basi na wao wanazidi kuwa kizani na kutaabika.

Hadi kufikia hapa, kwa hakika nguzo za tashibiha zimeshatimia. Na hii maana mpya imesimama madhubuti, ya kwamba yenyewe ni uwezekano unaweza kuchukuliwa katika kuifahamu hii aya kwa mujibu wa lugha na akili, pia kwa mujibu wa kile kilichozoeleka katika Quran. Katika kupiga kwake mfano wa nuru na mwanga kuwa mfano wa mwongozo na imani. Ama kiza na upofu ni mifano ya ujinga na ukafiri. Isipokuwa kule kuafikiana kwa ufafanuzi ambao tuko nao, ule wa kumjaalia muwasha moto kuwa mfano wa wanafiki. Hilo limetufanya tujiweke sawa na kutunza adabu tusije tukampigia mfano Mtume Mwaminifu bila ya kuwa na ushahidi unaothibitisha hilo kutoka katika Kitabu na Sunnah. . Na tofauti hii inayokereketa kifuani na kuondosha utulivu wa moyo wa kukubali maana hii, haikupita muda mrefu tukapata ushahidi wa wazi kabisa ulio na daraja ya sahihi katika hadithi ya Nabii akijizungumzia yeye mwenyewe, pale Mtume rehema na amani ziwe juu yake anaposema: **‘‘Kwa hakika mfano wangu na mfano wa watu kama mfano wa mtu aliyewasha moto. Na pale ule moto ulipoangaza kilicho kandoni mwake, basi vipepeo na viumbe ambao wanafuata moto wakawa wakitumbukia katika moto huo. Huyo mtu akawa anawatoa lakini wao wanamshinda na wanauuingia moto huo. Na mimi ndio mwenye kushika vifundo vya nguo zenu na kukuzuieni msiingie motoni na nyinyi mnapambania kuuingia.’’** Impokewa na Shaykhaani. Naam, kujifananisha kwake katika hadithi hii kupo katika njia isiyo ile njia ambayo ipo katika hii aya. Lakini hili halidhuru. Kwani mfano mmoja unaweza kupigwa kwa maana nyingi kwa mazingatio tofauti tofauti. Na kile kinachotuhusu, kwa hakika si kingine bali chenyewe ni kutukia kuwapo na mfano wa Nabii Mkarimu katika hilo. Nao upo wazi mwanzoni mwa hadithi kama tunavyoona. Na kwa hiyo, nafsi imezidisha kutulizana katika usahihi wa hilo.

Ama baada ya hayo, kwa hakika sisi – Allah anajua – hatupendi kuhitilafiana wala hatuna matamanio ya kuonekana tuna jambo geni. Lakini mambo yalivyo, hii ni amana

yake katika umma huo usiojua kusoma na kuandika katika kipindi cha utume. Kwa nuru hiyo macho yenye nuru yakafunguka hapa na pale. Lakini nuru hiyo haikuafikiana na matamanio ya wenye kibri ambao wamezoea maisha ya kiza cha ujinga. Hawakuiinulia kichwa hiyo nuru, bali waliinamisha vichwa vyao. Wala hawakuifungulia jicho bali waliporomoka chini na kuiacha wenyewe wakiwa viziwi na vipofu ﴿**Sema: ''Hii Quran ni uwongofu na poza kwa wale walioamini; na wale wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo (Quran) ni giza kwao.** ﴾. Haa Mym Sajdah 44.

Na kwa waasi waliohadaika aliwapigia mfano wa watu ambao mbingu iliwatendea wema kwa kuwapa mvua nyingi katika usiku wenye radi na mimeto ya umeme. Ama hiyo mvua hawakuijali wala hawajaipatia chochote cha manufaa. Hawakunywa maji yake hata tone moja, wala hawajaoteshea tunda hata moja, wala hawajamwagilia mimea wala kunywesha wanyama. Na ama hayo mabadiliko ya hali ya hewa ya mara kiza, mara radi na mmeto, yenyewe yalikuwa ndio yenye kuamsha hima zao, na ndio suala walilolifikiria hasa. Na kwa ajili hiyo, wakawa wanatazamia hali ya hewa, na wanayaendesha mambo yao kulingana na hayo mabadiliko. Na kila hali wakiivalisha nguo yake: wakati mwingine wanatembea, wakati mwingine wanasimama, na wakati mwingine wanajificha.

Huo ndio mfano wa Quran ambayo imeteremshwa na Allah ikiwa ni mvua inayouhisha nyoyo. Na kuotesha matunda ya tabia njema na matendo mema. Kisha waumini wakapewa mtihani utokanao na mvua hiyo. Kwa kupewa kupambana jihadi, kusubiri, na kuwafanyia siku zao kuwa ni

---

ya kielimu na nasaha kwa ajili ya Kitabu cha Allah Mtukufu, iliyotufanya tusema katika kitabu hiki kile kilicho bora katika kile tunachokijua? Kisha haya tuliyoyasema kwa mdomo yakatushajiisha kuyaandika kwa kalamu, ili kuyawasilisha katika kurasa mbele ya macho ya wasomaji. Kama tulivyoiwasilisha katika lile somo linahusu masikivu ya wanafunzi. Huenda hawa wakawa ni wenye kupata katika hilo maudhui ya uhakiki na kukichuja ili kuondoa makandokando, kile ambacho wale wengine hawakipati. Na mlango huu ni miongoni mwa milango ya utafiti na kung`amua kile ambacho hakigusi msingi miongoni mwa misingi ya dini. Wala hakihalalishi la haramu au kuharamisha cha halali. Jambo ambalo linaendelea kuwa wazi kwa kila Muislamu ambaye Allah amempa ufahamu katika Kitabu chake, kwa sharti la kuwa na kukusudia na unyenyekevu katika mwendo wa akili. Pamoja na kupata mwanga wa taa mbili katika mwendo huu, mwanga wa lugha na wa sharia. Kwa kiasi ambacho tumekielezea, na mapito ambayo tumeyaweka. Na kuafikishwa kunatoka kwa Allah [Daraazu].

Nimesema: Hadithi ''Kwa hakika mfano wangu na mfano wa watu kama mfano mtu...'' ni Muttafaqun Alayhi, inatokana na hadithi ya Abuu Huraira: Imepokewa na Bukhari katika Al-Riqaaqi 6482, na Muslimu katika Alfadhaailu 18.

mzunguko baina ya siku za amani na za vita, baina ya kushindwa na kushinda. Na nafasi ya baadhi ya watu katika Quran hiyo haikuwa vingine ila walivaa kaulimbiu yake katika ngozi zao, bila hata ya kunywa mapenzi yake moyoni mwao au kuonja kile kilichomo ndani yake miongoni mwa chakula cha roho na akili. Bali nafsi zao ziliwashughulisha na kuwatilia umuhimu nafsi zao za haraka (dunia). Wakazifunga fikra zao zote katika kile ambacho huenda kikawazunguka miongoni mwa ngawira wanazoziendea. Au gharama wanazoziogopa. Au majanga wanayosimama wakiyachelea na kuyangojea. Na hivi hivi wameenenda katika kufuata dini. Kwa hiyo Quran wakiienda mwendo wa kusuasua, kigeugeu uliojengewa juu ya msingi wa kupata faida na hasara na usalama wa duniani:

Pale wanapoona kitu kizuri cha karibu au safari yanye makusudio na matumaini yakawaangazia (mwangaza) wa matumaini wa kupata ngawira, basi wanaiendea pamoja na waumini ubavu kwa ubavu. Na pale kunapozuka moto wa vita na kulipuka (vimbunga vyake) vikionya juu ya uwepo wa kifo na kushindwa. Hapo wanachukua tahadhari zao na kutoroka mbele ya adui huku wakisema ﴿**Hakika nyumba zetu ni tupu** ﴾ Al-Ahzab 13. Au wanarejea njia huku wakisema: ﴿**Tungejua kuwa kuna kupigana bila shaka tungekufuateni** ﴾Aali Imran 167. Hadi likiwa jambo la tatu, na kwalo hawajaona tumaini lolote na mwangaza, wala hawakutarajia kupata maumivu ya kimbunga bali mambo yamewatatiza. Na anga haieleweki imetapakaa mawingu tu, hapo wanasimama wakingoja, hawasogei mbele wala hawarudi nyuma.

Lakini wanadumu na upande usiofungamana na popote, wakisubiria huenda mawingu ya shaka yakapambazuka. ﴿**Basi mkipata kushinda kunakotoka kwa Mwenyezi Mungu, husema (kukwambieni): ‘‘Je! Hatukuwa pamoja nanyi?’’ (Na kama makafiri wamepata sehemu (ya kushinda) husema: kuwaambia makafiri), ‘‘Je, hatukukurubia kukushindeni (tulipokuwa katika jeshi la Waislamu), tukakuzuilieni na (kudhuriwa na hao) Waislamu?’’** ﴾ An-Nisaa 141. ﴿**Na wako katika nyinyi wanaokaa nyuma (wasiende vitani, na huwakataza wenziwao wasiende vitani). Na kama unakupateni msiba (kila mmoja) husema: ‘‘Mwenyezi Mungu amenineemesha ilivyokuwa sikuhudhuria pamoja nao.’’ Na ikukufikieni fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu (kama kupata ngawira na kushinda), husema – kana kwamba haukuwa urafiki**

**baina yenu na baina yake – (husema): ‘‘Laiti ningalikuwa pamoja nao nikapata kufaulu kukubwa (huko).’’﴿** An-Nisaa 72 – 73.

Daima hiyo ndio hali ya wanafiki katika kila jambo lao: Wakitarajia faida ya haraka wanaitafuta kwa sifa yoyote ili waipate. Na kama wakitarajia madhara, wanalikataa lile kundi ambalo wanawapatisha madhara katika njia yake. Na pindi jambo linapokuwa kiza kwao wao, wanasimama mbali, si kwa hawa wala kwa wale. Ama yule ambaye anamwamini Allah na siku ya mwisho, kwa hakika yeye ana mwelekeo (kibla) mmoja anaouelekeza uso wake katika upande huo. Nao ndio mwelekeo (kibla) wa kweli, katika hilo haogopi lawama ya mwenye kulaumu. Mshairi amesema:

*Na hajali pale atakapouliwa akiwa Muislamu*

*Upande wowote atakaofia hiyo ni kwa ajili ya Allah.*

⁕ ⁕ ⁕

Hadi hapa utangulizi umekamilika baada ya Quran kueleza wasifu wa kile unachokistahiki, na kueleza wasifu wa wafuasi wake na wanaoipinga, kila mmoja kwa kile kinachomstahiki. Hakuna maringo kuyaelezea makundi haya yote, ukirejea katika marejeo ya kuisifu Quran. Kwa hakika kitu ambacho wafuasi wake wanakuwa ni watu waliongoka na kufanikiwa. Na wapinzani wake ni watu wa upotofu na hasara. Basi kitu hicho hakitakuwa vingine ila kitakuwa cha kweli (haki) iliyo wazi, hakina shaka ndani yake.

Ni ipi hiyo haki ambayo haifuatwi ila na yule aliyeongoka aliyefaulu. Na haipingi ila yule aliyepotea na kupata hasara? Bali ni ipi hiyo haki ambayo imepigiwa mfano wa mwanga ung`aao na mvua nyingi?

Hapana shaka kuwa haya yote yanampa shauku kubwa msikilizaji wa hakika zinazolinganiwa na Quran kuwalingania watu. Hebu tazama, kwa namna gani imetiririsha ubainifu wake.

Kwa hakika dhahiri ya muktadha unapelekea kusema: Kwa hakika haya mambo ya hakika, nayo ni wao kumwabudu Mola wao peke yake na wakiamini Kitabu chake na Nabii wake (… mpaka mwisho), yenyewe ni yenye kupita mapito ya mtindo wa nafsi ya tatu, mtindo ambao umepita katika kukielezea hicho Kitabu, na kuwaelezea watu. Lakini chenyewe kimebadilisha mapito ya mazungumzo kutoka katika hali ya kueleza kwa

kutumia nafsi ya tatu na kwenda katika kutumia miito na kutumia nafsi ya pili ikisema: ﴿**Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu…** ﴾ [21].

Je, wajua chochote kuhusu siri ya mabadiliko haya?

Kwa hakika wasifu huo wa kina ulioelezwa na Quran kuyaeleza hayo makundi matatu (wamchao Mungu, makafiri na wahadaika). Kwa hakika wasifu huo umemhamisha msikilizaji kutoka hali moja kwenda hali nyingine. Baada ya mambo hayo kuwa hayajulikani (yapo mbali – nafsi ya tatu) mwanzoni mwa mazungumzo yanayowahusu, baada ya wasifu huo wa kutosheleza kwa sasa wamekuwa ni wenye kuwepo karibu (nafsi ya pili) katika taswira ya msikilizaji kana kwamba wao wanaonekana kwa macho, na wapo katika sehemu unaweza kuwaita wakakusikia. Kwa hiyo wakastahiki kuelekezewa mazungumzo kama wanavyoelekezewa wale waliopo karibu kimilango ya fahamu na kuonekana. Hili kwa upande wa kiujumla. Ama kwa upande mwingine, kwa hakika mifano hii ya kibalagha na ambayo imepigwa kuhusiana na wapinzani kwa sifa ya kipekee. Kwa hakika imeshawekwa wazi mbele ya msikilizaji ikiwa katika umbo la kuhuzunisha linalochochea katika nafsi yake kichocheo cha nguvu cha kuwanasihi na kuwaonya. Hadi inafikia hakika ya msikilizaji huyo hawezi kuhisi vizuri kifuani kwake ila kwa kuwaita hao wapinzani au kumsikiliza yule anayewaita: Akiwaambia fungueni macho yenu enyi watu na njooni katika njia ya uokovu. Na hivi hivi, nafsi zimejiandaa ukamilifu wa kujiandaa kusikiliza wito huu: ﴿**Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu…** ﴾ [21]. Aya hizo mpaka mwisho wa kusudio la kwanza.

* * *

## KUSUDIO LA KWANZA MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII

### [Kuwaita Watu Wote Waingie Katika Uislamu]

### Katika Aya Tano [21 – 25]

Katika aya tano hizi, utasikia wito wa nguvu ukielekezwa kwa walimwengu wote kwa ajili ya matakwa matatu:

(1) Msimwabudu mwingine ila Allah wala msimshirikishe na chochote.
(2) Aminini Kitabu chake ambacho amekiteremsha kwa mja wake.
(3) Iogopeni adhabu chungu iumizayo, na tafuteni thawabu zake nyingi.

Haya ndio matakwa matatu, nayo ndio nguzo tatu za itikadi ya Kiislamu. Unayaona yamepanuliwa huku yakipangwa kwa mpangilio wa kawaida. Kuanzia wa kwanza kwenda wa kati hadi wa mwisho. Na unaiona kila nguzo moja katika hizo nguzo mbili za kwanza imesimamishwa juu ya nguzo msingi wa hoja za kiakili za kukata kabisa kila aina ya utata. Ama nguzo ya tatu, imeletwa ikiwa haina aina hii ya hoja. Lakini yenyewe imepuliziwa roho ya kutisha na kutikisha hisia kwa kutahadharisha na kubashiri, kwa kile kinachosimama katika maudhui yake msimamo wa hoja.

Kwa hakika wewe, utakapotazama uzuri katika nguzo hii utaikuta imetosheka haihitaji hoja mpya baada ya kuthibitishiwa hoja ya nguzo zilizoitangulia. Kwani yenyewe katika nguzo mbili hizo inasimama nafasi ya matokeo ya kimantiki yanayotokana na vitangulizi vyake.

Je, umeona, lau kama mfalme mwenye mamlaka makuu, ambaye hukumu zake zinapita akakuletea balozi anayebeba ujumbe wake. Na wewe ukayakinisha kuwa kile kilichopo mkononi mwa balozi huyo ni barua ya mfalme yenye muhuri wake. Je, nafsi yako itahitaji hoja mpya ili kuhakikisha kuwa yale yaliyomo ndani ya hiyo barua ni miongoni mwa habari na maonyo ya ajabu, baada ya kutulizana nafsini mwako na kujua kuwa hayo ni maneno ya yule ambaye akisema anasema ukweli na akiahidi anatekeleza?

Na hivyo hivyo, unayaona mazungumzo ya hapa yanayohusiana na vitu vya kusikika, yakiletwa yakiwa hayana vile vilivyothibitishwa katika suala la Utume. Na aina hii ya kuondoa hoja ni upeo wa juu sana katika uzuri na uhondo wa maneno: ﴿**Na msipofanya … basi uogopeni moto…** ﴾ [24].

* * *

**Zoea Kuanza:** katika aya kumi na nne [26 – 39]:

(1) Katika sura hii – kama ulivyojua – maneno yameanza kwa kuelezea wasifu wa Quran kwa kile kilichomo ndani yake miongoni mwa uwongofu wa jumla. Kwa hiyo imekuwa ni haki yake irudi katika kuelezea njia ya Quran katika uongofu huo. Ili iseme ya kuwa yenyewe ni mwongozo wenye ubainifu kamili, unaotosheleza na unaojumuisha kila kitu. Hebu tazama namna Quran ilivyoandaa maandalizi ya kuhama mazungumzo kwenda mengine, kwa maandalizi yanayoleta muunganiko tangu mwanzo wa sura mpaka eneo hili:

Ama katika utangulizi kumetajwa wasifu wa makundi matatu. Wasifu toshelevu ambapo watu wamepigiwa mifano yao. Na imethibitisha kuwa wale ambao wamekufuru wamefuata batili. Na kwa hakika wale ambao wameamini wamefuata haki kutoka kwa Mola wao.

Ama makusudio, kwa hakika, ndani yake kumebainishwa kuwa Allah peke yake ndio mtukufu ambaye hashirikishwi na chochote miongoni mwa miungu. Kisha akaweka ndani yake kipambanuzi cha baina ya Nabii na anayejifanya nabii kwa kuonesha ile miujiza ya kiulimwengu na ambayo hakuna mtu anayeiweza kuifanya kama hiyo bila kuwezeshwa na Allah. Kisha imetaja mfano wa moto ambao umeandaliwa kwa makafiri. Na mfano wa pepo ambayo imeandaliwa kwa wamchao Mungu.

Basi utaiona, kwa hakika katika mifano hii imegusia aina mbalimbali za hakika za Juu na za chini, za kimaada na kimaana … mpaka mwisho wa mazungumzo yake ukawa ni kuonesha yale yaliyomo peponi miongoni mwa aina za raha na ladha binafsi na za kimapenzi. Maana hizo ambazo, huenda mtu akaona haya kuzitaja. Na huenda ujinga ukamwingia huku ukimweka mbali na kufahamu mwenendo wa mazungumzo ya Mungu Mkuu, ukimghafilisha na asijue kuwa Allah ni Haki ambaye haoni aibu kubainisha haki. Na kwamba yeye ni mpole mno, na ambaye rehema zake anaziteremsha katika kiwango cha akili za wanadamu. akawabainishia kila kile wanachokihitaji kibainishwe miongoni mwa vile wanavyovipenda au wanavyovichukia. Na miongoni mwa vile wanavyovitarajia au wanajihadhari navyo.

Na hivi hivi, mazungumzo yametiririshwa kutoka katika kutaja mifano hii iliyo tofauti tofauti na kuelekea katika kung`amua kanuni ya kiujumla katika hizo. Kwa kubainisha kuwa njia hii ndio ya Quran katika

uwongozi wake. Yenyewe inapiga mifano yote. Na inabainisha hakika tamu na chungu. Ikiweka kila kitu katika eneo lake. Ikiita kwa jina lake. Haijali kukishughulikia katika kukibainisha kwake mambo matukufu au yanayodharauliwa: ﴿**Hakika Mwenyezi Mungu haoni haya kutoa mfano wowote wa mbu na ulio wa zaidi yake…** ﴾ [26].

Ni kweli, kuwa jambo la Kitabu hiki katika kueleza haki na batili, madhara na manufaa ina jambo kama lile la kitabu cha matendo katika kuelezea mema na mabaya. Yote mawili hayaachi suala dogo wala kubwa ila wanalidhibiti kwa kuliandika.

Na kama ulivyo wasifu wa Quran ya kuwa yenyewe ni mwongozo wa jumla. Kwa hakika imepita kutaja mgawanyiko katika kuukubali mwongozo wake. Na kutangaza kifo cha mwenye kuipuuza. Na hivyo hivyo imeelezea njia yake katika kuongoza, kwa hakika imepita hapa kwenda katika mfano wa mgawanyo huu: ﴿**Huwaachia wengi kupotea kwa mfano huo na huwaongoza wengi kwa mfano huo** ﴾ [26]. Na kwenda katika kutangaza kifo cha waliopotea kwa kutaja maovu yao na kutoa maelezo ya upungufu wao ﴿**Lakini hamwachii yo yote kupotea kwa mfano huo (na mwingine) isipokuwa wale wavunjao amri (zake** ﴾**.** [26].

Na kama vile ubainifu wa wasifu wao ulivyo huko, umewaweka wakiwa mbele ya msikilizaji, katika taswira ya kumtikisa anayewaita kusikiliza wito wao kwa nasaha na mafunzo. Na hivyo hivyo ubainifu wa wasifu wao ulivyo kwa hapa. Kwa hakika nafsi hizo zimechokoza masikivu ya yule anayewazungumzisha awazungumzishe kwa kustaajabu na kupinga: ﴿**Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu, …** ﴾**.** [28]. Hizo aya.

(2) Na hivyo hivyo mazungumzo yamerudi katika kusudio la kwanza kwa nguzo zake zote tatu. Lakini yakiwa katika nguo mpya:

- (Ama katika nguzo ya kwanza): Huku tuliyasikia yakiamrisha kumwabudu Allah. Na hapa utayasikia yakikataza kumkufuru Allah.

Na kule iliwakumbusha neema ya kuwepo kwao kwa ujumla. Na hapa inawakumbusha neema hiyo kwa maelezo mapana ya kutimiliza. Na kule iliwajulisha neema ya kutiishiwa kwao ardhi na mbingu. Na hapa inawajulisha neema hiyo ikiwa katika kitu fulani hivi cha maelezo marefu.

- (Na ama katika nguzo ya pili): Huko ilikumbusha Utume wa Nabii huyu wa mwisho. Na hapa inakumbusha Utume wa Nabii yule wa kwanza

ambaye ni Adam. Ili tujue kuwa Nabii wetu hakuwa kitu kipya katika maswala ya Mitume. Na kwamba jambo la kuwekwa sheria na Utume ni jambo la kale linaungana na mwanzo wa kuwepo kwa mwanadamu. Kwa hakika Quran imeuandalia ubainifu huu kwa kutaja historia ya huo mwanzo wa ajabu na kile kilichopita katika swala hilo miongoni mwa kuwepo kwa mazungumzo na malaika. Mazungumzo hayo yanajulisha ziada ya uangalizi wa Mungu kwa viumbe hawa wa kibinadamu. Kwani Allah alimchagua huyu mtu kuwa kiongozi ardhini na kumpa kipaumbele kuliko viumbe vingine vyote kwa fadhila ya elimu. Ili kuneemeshwa kwa jambo hilo kupite katika mapito ya pamoja na kuhisi neema ilikotajwa katika nguzo ya kwanza kwa namna bora kabisa ya ufumaji… Kisha ikaunganisha kutoka katika huku kuwafadhilisha kwenda katika kufafanua kile kilichotokezwa na mwanadamu huyo miongoni mwa husda za ibilisi na uadui wake wa kale dhidi ya mtu wa kwanza, na kumwadaa kwake kwa kumtia wasi wasi. Na kile kilichomalizikiwa katika jambo la mwenye kufanya hadaa na mwenye kuhadaiwa miongoni mwa kuwapa mitihani wao, na vizazi vyao kwa kuwakalifisha. Nayo – kama unavyoyaona – ni mazungumzo yanayotafutana yenyewe kwa yenyewe, na baadhi yake yanachukua shingo za mengine.

- (Na ama katika nguzo ya tatu): kwa hakika huko umeshaona inavyoelezea pepo na moto na kile kilichomo katika viwili hivyo miongoni mwa sifa nzuri na za kutisha. Na kwa hapa unaiona ikitosheka kwa kuvielezea viwili hivi kwa kutaja majina yao na kuainisha watu wa kila kimoja chao. Ikifuma muweko wa malipo yakiwa pamoja na makalifisho katika uzi mmoja. Na ikiachana na kila kimojawapo na kwenda kwa kingine kwa mwachano mzuri kabisa. Kwa kuthibitisha kuwa kufuata makalifisho au kutoyafuata ndio kiini cha kupata furaha au hali ngumu katika hatima.

Hapa imemaliza maneno – kama ilivyomaliza katika utangulizi – kwa kueleza suala la wanaoiendea kinyume. Ili kuandaa maandalizi ya kuhama kwa mara nyingine na kwenda katika kuita kundi moja miongoni mwao na kuwaita wao waje katika Uislamu na haya ndio makusudio ya pili.

* * *

## MAKUSUDIO YA PILI MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII

### [**Kuwaita Watu Wa Kitabu Wito Mahususi, Wa Kuacha Batili Zao Na Kuingia Dini Hii Ya Haki**]

### Katika aya mia ishirini na tatu [40 – 162]

Yakutosha wewe ujue kuwa sura hii ndio ya kwanza katika sura za Madina. Na kwamba Madina kulikuwa kunakaliwa na watu wenye uadui zaidi na wale walioamini. Na watu wenye mijadala zaidi katika dini yao kutokana na kile walichopewa miongoni mwa elimu ya kabla yao. Pia yakutosha ulijue hili na lile ili ujue siri ya uangalizi huo ulio mwingi katika upande huu katika wito (daawa – ulinganiaji). Tunamaanisha kuwaita wana wa Israeli kwa sifa mahususi baada ya kuwaita watu wote. Na ili ujue hekima ya huko kurefusha wakati mwingine katika mazungumzo pamoja nao, na wakati mwingine, kuwazungumzia wao. Kwa rangi zinazotofautiana, mara za kuwashambulia, kujilinda, kuwavutia na kuwarefushia, mpaka ikafika eneo lililo baada ya nusu ya sura hii.

Na pale unapohama hama katika mazungumzo haya, hatua kwa hatua, utaona yale yanayoumiliki moyo wako miongoni mwa uzuri wa mfumo wake na umakini wa vigawanyo vyake.

(Yameanza) Mazungumzo pamoja nao kwa aya ya kipekee aya [40] nayo licha ya uchache wa maneno yake imekusanya malengo yote ya mazungumzo. Ndani yake inawaita kwa majina yao wanayoyapenda, na nasaba zao tukufu kabisa, na inawakumbusha neema za Allah kwao wao zilizotangulia kwa ujumla. Na inajenga juu ya hilo, wito wa kuwaita wao watekeleze ahadi yao. Kuwapendezesha na kuwatisha.

(Kisha) ikarejea katika malengo haya na kuyaeleza kwa upana kidogo kidogo na kwa kiasi maalum. Basi ikafafanua ile ahadi ambayo iliwataka waitekeleze. Kwa aya sita [41 – 46]. Na ikabainisha kiwango cha neema ambazo walineemeshwa katika aya ya [47] na kiwango hofu ambayo aliyowahofisha katika aya ya [48].

(Kisha) ikayagawa mazungumzo katika makundi manne:

- (Kundi la kwanza): ndani yake kunatajwa kizazi cha kale cha Wayahudi tangu walipopelekewa Musa amani iwe juu yake.

- (Kundi la pili): ndani yake kunatajwa hali za Wayahudi kwa zama za Utume wa Muhammad.
- (Kundi la tatu): ndani yake kunatajwa kuwa Uislamu ndio wa mwanzo tangu kwa Ibarahimu amani iwe juu yake.
- (Kundi la nne): ndani yake kunatajwa namna ilivyo hali ya Waliosilimu wakati wa Utume.

### 1- **Kutaja Kizazi Cha Kale Cha Wayahudi** [49 – 74]:

Katika kundi hili mazungumzo yameanza kwa aya nane zinazowatambulisha wana wa Israeli kwa maelezo ya kuonesha neema ambazo walipewa mara kwa mara. Nazo zi zile neema za kihistoria za kale na ambazo athari yake imeungana na manufaa yake yakaendelea toka mizizi hadi katika matawi. Ikawa inawatajia siku za neema za Allah kwao wao:

- Siku alipowaokoa kwa watu wa Firauni.
- Siku alipowaokoa wasizame baharini na kuzamishwa maadui zao.
- Siku alipowaahidi kuwateremshia Kitabu.
- Na siku alipotimiza ahadi yake kwa kuwateremshia hicho Kitabu.
- Na siku alipokubali toba yao ya kuiasi dini na kufanya shirki kwa Allah.
- Na siku alipokubali toba yao ya kumfanyia uasi Nabii wao na kumpendekezea mambo makubwa makubwa.

Kwa hakika hizo ni neema tukufu (zenye kutangulia dhambi zilizofuata). Kuzitaja neema hizi kunalainisha nyoyo na kutikisa hima za shukurani kwa mnemeeshaji na kutii amri zake.

Na kabla haijahama katika kuwakumbusha neema hizo tukufu zenye kuwapa tamaa ya kupata ziada wale wenye kushukuru. Na kuhamia katika kuwakumbusha maovu yao na kile kilichowapata miongoni mwa aina mbalimbali za adhabu zenye kulazimisha kutii na kuzingatia. Quran imejaalia baina ya mazungumzo ya aina mbili hizi kuwepo na kizuizi kilichochanganya kukumbusha baadhi ya neema na kukumbusha kile walichokabiliana nacho kwa neena hiyo. Baada ya kuiandaa nafsi iende katika kizuizi hiki kwa kugeuka kidogo. Ndani yake kuna alama ya kukengeuka na kutoridhia. Ikabainisha ya kwamba Allah Mtukufu amewastarehesha wao zaidi ya hayo yote kwa starehe nzuri wasiyoihesabia. Na bila ya kuitabikia wala kuihangaikia. Lakini wakadhulumu nafsi zao na

wakafanya kibri kwa neema hiyo na kupotosha neno la shukurani na kulibadilisha kuwa ni upuuzi na mchezo. Wakapendekeza mbadala wa riziki hiyo laini wapate maisha kuhangaika na kutaabika. Na Allah akawalazimisha kile walichojilazimisha wao wenyewe na kuwapiga kwa udhalili na umasikini.

Na haya hapa ni mazungumzo tu ya kukumbusha makosa na adhabu. Imetaja kuwa wao wameingia katika adhabu zitokazo kwa Allah, kwa sababu walizikufuru aya za Allah na kuwauwa Manabii (isipokuwa yenyewe, imewatoa waumini miongoni mwao wasiingie katika adhabu hii). Pia waliasi amri za Torati kiujumla mpaka wakalazimishwa kuzifuata. Kisha wakakengeuka na kuiacha Torati baada ya hapo mpaka wakawa wanastahiki kuteremshiwa yale yaliyoteremshwa kwa watu wa waliyoiasi Sabato, lau si kama kuwepo kwa fadhila za Allah kwao, basi adhabu ingewateremkia. Na kwamba wao walijicheleweshа katika kutekeleza amri ya Nabii wao na kuwafikisha kutokujua nafasi ya utume wake wakadhani katika baadhi ya ufikishaji wake kutoka kwa Mola wake, kwamba anatania na hayupo makini na hilo...

### **Kiungo Cha Muunganiko Baina Ya Vile Vigawo Viwili Cha Kwanza Na Cha Pili** [74]:

Na Quran imetaka kuunganisha yale ya sasa yao na yale ya kale yao. Hebu tazama namna ilivyoweka baina ya mawili hayo kiungo cha kuunganisha katika aya hii ambayo imemalizia kikundi cha kwanza: ﴿**Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo (yote); hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi;** ﴾ [74]. Na kauli yake ﴿**baada ya hayo** ﴾ ni neno lililoainisha msingi wa historia ya roho ngumu na haikuainisha mwisho wake. Kana kwamba kwa kueleza hivyo, imeweka juu yake muhuri wa kuendelea. Na kuliachia likipiga hatua katika zama na vizazi katika taswira ya msikilizaji. Mpaka anadhani kuwa hayo mazungumzo yanaingia katika zama za sasa. Kisha haupiti muda kwa dhana hii, hadi inaongezeka nguvu kwa kuja umbo la sentensi ya kimajina katika kauli yake ﴿**zenyewe ni kama mawe** ﴾ bila ya kusema: (zikawa kama mawe).

Kisha tazama namna mwisho wake ulivyokuwa wa kuzielezea nyoyo zao kwa maelezo haya yanayodokeza kubadilika kwa mtindo wao. Kwa hakika yule ambaye moyo wake unafikia upeo huu wa ugumu na kutokuwa na ulaini hata kidogo. Basi kuendelea kuzungumza naye kunakuwa ni kukosa hekima.

Na mtu huyo anakuwa ni mwenye kustahiki kutomuelekezea mazungumzo na badala yake uyaelekeze kwa mwingine ambaye ana moyo salama. Na hivi hivi maneno yanahama kutoka katika mazungumzo na wao katika suala la watangulizi wao na kuelekea katika mazungumzo pamoja nasi kuhusiana na suala lao wao wenyewe.

2 – **Kutajwa Wayahudi Wa Zama Za Utume** [75 – 121]:

Katika kundi hili maneno yamefunguliwa kwa sentensi ya kufurahisha. Haipo katika mwenendo wa zile aya za kabla yake wala za baada yake katika ule mtindo wa utiririshaji wa kihabari. Bali yenyewe ni sentensi ya kuuliza yenye herufi mbili za ajabu. (Mojawapo): inarejesha katika kumbukumbu kila kilichopita miongoni mwa matukio ya kikundi cha kwanza. (Na nyingine): inafungua mlango kwa kila kinachokuja miongoni mwa matukio ya kundi hili. Herufi hii ipo baina ya historia mbili ya kale na ya sasa katika mkao wa mazingatio yaliyonga`amuliwa kutokana na matokeo yaliyothibitishwa, baina ya sababu zilizopita na sababu zinazokuja: ﴿**Mnatumaini (nyinyi Waislamu) ya kwamba watakuaminini (hao Mayahudi); na hali baadhi yao walikuwa wanasikia maneno ya Mwenyezi Mungu…?** ﴾.

Hii faau (herufi ya kiunganishi) inatuambia: Je, baada ya kila kile tulichokisimulia anatokea mtu mwenye tamaa akatamani kuamini kwa watu hawa. Huku wao ndio warithi wa historia hiyo chafu? Na hii wawu (kiunganishi) inasema: (haya. Na wana wao matendo yasiyokuwa hayo wanayoyatenda..).

Na inarudi kutiririsha sentensi za kimaelezo hadi katika mapito yake ya kimaelezo kamili. Na inatusimulia sifa za uovu za Wayahudi wa zama za Mtume miongoni mwao, vitendo vyao viovu na kauli zao za uzushi kiasi cha sababu ishirini hivi. Kiasi ambacho kwa mwenye tamaa hana tena tamaa nao ya kuwa wataamini. Ni sawa sawa katika haya yale yaliyokuwa mahususi kwao na kile kilichokuwa wakishirikiana na wengine katika hilo, miongoni mwa watangulizi au Wakristo au wapagani.

Kisha haikuacha dai lolote miongoni mwa madai yao ila imesimama kidete kulijibu kwa kile kinachostahiki miongoni mwa majibu na kulivunja dai hilo.

- (Kwa hakika maelezo haya yameanza) kwa kuwagawa katika makundi mawili: wanazuoni wanaopotosha maneno ya Allah huku wakihusiana kuyaficha yale waliyonayo miongoni mwa elimu ili isiwe hoja dhidi yao. Na wajinga wasiojua kusoma na kuandika, na hawa ndio mateka wa matamanio na ufahamu mbaya. Na ni wahanga wa kupotoshwa na kuvurugwa ambako kunaletwa na wanazuoni wao. Sasa ni nani yule ambaye ana tamaa kwa watu hawa kuwa watatengenekewa katika lindi la ujinga wao wa kupotoshwa na kuhadaiwa kulikochukuliwa kwa jina la dini, kumbe chenyewe si cha dini. Mjuzi wao ni mpotoshaji afanyaye hadaa. Anaandika kitabu kwa mkono wake kisha anasema chenyewe kimetoka kwa Allah.
- (Na ukafuatisha) kwa kubainisha chanzo cha kujitumbukiza kwao katika kila lenye kuangamiza. Nacho si kingine ila ni kudanganyika kwao kwa kudai kuwa eti moto hautowagusa isipokuwa kwa siku chache sana zinazohesabika. Na kwa hakika Mtume ameamrishwa ayaeleze kwa upana madai haya ili kuyatengua na kuyabatilisha. Na ameamrishwa aende nao hatua kwa hatua katika mjadala huu, kwa mujibu wa hatua za kimantiki (kiakili) zilizo salama na upembuzi yakinifu.
- Na akaanza kwa kuwataka walete hoja ya kile walichokidai.
- Kisha inakitengua kwa kubainisha namna kinavyoenda kinyume na kanuni za kiuadilifu wa Mwenyezi Mungu. Kanuni ambazo hazitambui dhulma yoyote wala upendeleo kwa yeyote. Bali mbele yake, viumbe vyote vipo sawa. Kila mtu yupo rehani kwa matendo yake. Na atakayefanya uovu au wema basi atalipwa kwa alichokifanya.
- Kisha inayapinga madai hayo kwa kuigeuza hiyo kesi kuwa dhidi yao. Kwa kuwabainishia kuwa wao ni miongoni mwa wale ambao wamechuma maovu na kuzingirwa na dhambi zao: Je, hamkuweka ahadi ya kumcha Allah na kuwafanyia wema watu kisha mkakengeuka? Je, hamkuweka ahadi ya kuacha dhambi na uadui kisha mkachupa mipaka? Kisha mkaamini baadhi ya mandiko na mkayakufuru baadhi nyingine. Na mkahukumu katika mambo ya kisheria kwa mujibu wa matamanio ya nafsi zenu. Hivyo walipokujieni Mitume wakiwa na kile kisichopendwa na nafsi zenu mkafanya kibri.
- (Kisha hilo lilifuatishwa na upuuzi wao) na ikataja:

1- Wao kujitia uziwi ya kutoisikiliza haki kwa madai ya kuwa nyoyo zao zimefungwa.
2- Kufuru yao kwa Kitabu Kipya eti kwa kuwa chenyewe kimetermshwa kwa asiyekuwa wao, baada ya kuwa shingo zao zikirefuka kungojea

kutokea kwa jambo hili likiwa mkononi mwa Nabii atakayewanusuru wao dhidi ya wapagani.

3- Madai yao eti wanatekeleza wajibu wao ambao ni kuyaamini yale yaliyoteremshwa kwao tu. Licha ya kwamba wao wameshakikufuru hata kile kilichoteremshwa kwao. Na hiyo ndio ada[1] yao tangu walipoabudu ndama na kunyweshwa mapenzi ya kumpenda huyo ndama mioyoni mwao.

4- Madai yao ya kuwa wao peke yao ndio watakaopata makazi mema huko ahera. Kisha kujipinga wao wenyewe katika hilo kwa kuchukia kwao kifo na kuwa na pupa sana katika kupenda kuishi.

5- Uadui wao dhidi ya Jibrilu eti kwa kuwa yeye amekiteremsha kitabu kwa asiyekuwa wao. Licha ya kwamba yeye amekiteremshwa kwa mujibu wa ujuzi wa Allah.

6- Kujirudia na kujikariri kwa kukataa na kuvunja ahadi.

7- Kujishughulisha kwao na vitabu vya uchawi na kukiacha kitabu cha Allah nyuma ya migongo yao.

8- Kupindisha kwao ndimi zao wanapomuongelesha Mtume kwa kutumia neno[2] lenye kumchezashere na kuichafua dini yake hata kama neno hilo kwa nje nje lina maana ya kumtukuza. Au kwa neno hilo wanakusudia kumkera na kumuuliza maswali mengi yasiyo na maana na kumpa mapendekezo kibao. Kama alivyoulizwa Musa hapo kabla (Kwa hakika haya yametiririshwa katika muktadha wa kuwahadharisha waumini wasiliseme neno hilo).

---

[1] Ada yao: Tabia yao na mwenendo wao.

[2] Nayo ni kauli (Raainaa) na neno hili kwa nje yake linaonesha heshima. Lakini lenyewe katika lugha ya Kiarabu lina maana nyingine ya kijinga. Na katika Kiebrania kuna neno la tusi lililokaribu kimatamshi na neno hili. Kwa hakika tamko (ra`a) kwa Wayahudi, maana yake ni muovu mshari. Na tamko (raa`a) maana yake ni shari na uovu. Na pindi linapoegemezwa katika kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi, katika lugha yao, linakuwa (raa-iinuu) na maana yake katika nafsi ya pili umoja ni: wewe muovu wetu na mshari wetu…. Huenda wao – Allah anajua – walikuwa wanapindisha ndimi zao katika kulitamka ili walikurubishe na muundo wa Kiarabu ili waifiche nia yao. Na ili watosheke na ile alama inayofahamika baina yao. Ndipo Allah akawaamrisha waumini wamuongeleshe Mtume kwa kuali yake **(Undhurnaa)** ili wanafiki wasipate uchochoro wa kuchezea matamko yenye pande mbili. Au vile vile, kwa hakika neno **(raa`inaa)** husemwa na muulizaji aliyeachwa akilitumia neno hilo ili asikilizwe na muulizwa mpaka amalize maswali yake. na hiyo ni desturi ya Wayahudi pale wanapozidisha kuuliza. Ndipo Allah akawaamrisha waumini wadumishe tabia ya kusikiliza vizuri ili wasije wakahitaji kuuliza. Na waseme **(undhurnaa)** na neno hili husemwa na mwanafunzi pale anapotaka kuthibitisha kile anachoambiwa na sio kuzidishiwa. [Daraazu].

9- Chuki zao, na kwa chuki hizo zikawaathiri wao wenyewe na wapinzani wengine miongoni mwa waliopewa Kitabu na washirikina, na kuchukia kwao kuteremka kwa ufunuo kwa wasiokuwa wao. Licha ya kwamba Allah anamuhusisha kwa utume wake, yule amtakaye. Na Allah ana haki ya kufuta sheria na kuleta sheria nyingine iliyokama ile ya kwanza au iliyobora kuliko ile ya kwanza.
10- Wengi wao wanapenda kuwarudisha waumini katika ukafiri.
11- Madai ya wote – Wayahudi na Wakristo – kuwa hatoingia peponi asiyekuwa wao. Matumaini wanayoyatamani bila ya hoja nzito.
12- Makundi yote hayo mawili yanachafuana yenyewe kwa yenyewe. Wayahudi wanasema: Wakristo hawana kitu. Na kauli ya Wakristo nao: Wayahudi hawana kitu. Na washirikina wanayachafua makundi yote hayo mawili.
13- Makundi matatu yote hayo yanashirikiana katika kuing`oa misikiti isiwe na wanaomtaja Allah.
14- Kushirikiana kwao katika ujinga wa kutomjua Allah na kumnasibisha kuwa ana mtoto.
15- Kushirikiana kwao katika kuafikiana juu ya sharti la kuamini Mitume, ambalo ni kuwa Allah awasemeshe bila ya mtu wa kati au awateremshie alama zenye kuonesha hilo.

- (Kisha ikahitimisha upuuzi huu) kwa madai ya kukatisha tamaa kuhusu imani yao. Nayo ni kuwa wao wanatamani Mtume mwenyewe abadilike na kufuata matamanio yao. Sasa inakuwaje kwa yeye Mtume awe na matumaini ya kuwa wao watafuata mwongozo wake? Hapana kabisa kabisa. Lakini atosheke tu kuwa wale wabobezi katika elimu miongoni mwao, nao ndio wale ambao wanakisoma Hiki Kitabu ukweli wa kukisoma, hao huamini mwongozo huu aliokuja nao. Na makafiri hao ndio wenye hasara.

### 3- **Kutajwa Kwa Waislamu Wa Kale, Kuanzia Kwa Ibrahimu [122 – 134]:**

Ni hali ya mrekebishaji mwenye busara katika wito wake kama hali ya mkulima anayeanza na ardhi kwa kung`oa magugu na kuitakasa ardhi isiwe na majani yenye madhara kabla ya kupanda mbegu bora au kupanda miti yenye manufaa. Na hivyo hivyo mlinganiaji mwenye busara huanza na kuzijenga nyoyo na kuziondosha katika batili na ufisadi kisha anazielekeza katika njia ya haki na mwongozo. Haya mawili ndio vilele. Kimojawapo

kinasimama katika kusafisha na kuandaa na cha pili kinakamilisha na kupambia. Na wewe umeshaona maneno yanayohusu kuwalingania Wana wa Israeli, yenyewe yamepita katika upeo huu wa kubainisha kupinda kwa njia wanayoipita. Na umeshayaona namna yalivyoeleza kwa upana wa bayani katika hilo hadi yakafika mwishoni mwa mzunguko wa kwanza. Je, kwa hiyo, si katika haki yaanze mzunguko wa pili na kubainisha njia ya sawa sawa na ambayo inapaswa waipite?

Kisha umeona bayani iliyopita namna ilivyomalizia kwa kutaja mwongozo wa Allah na elimu aliyomfundisha Nabii wake na kulitaja kundi ambalo linatarajiwa kuwa litamwamini miongoni mwa waliopewa Kitabu. Nao ndio ambao wanakisoma Kitabu ukweli wa kukisoma. Je, umaliziaji huu ni mzuri wenye kuzifanya nyoyo ziwe na shauku juu ya ufunguzi huu?

Kisha umeona masimulizi katika mzunguko wa kwanza yakiwa yamegawanyika sehemu mbili: sehemu moja inazumngumzia yale yaliyopita kwa Wayahudi. Na sehemu ya pili inazungumzia mambo yao ya sasa. Je, haiwi mlinganyo mzuri kama mazungumzo ya pili, nayo yakagawanywa sehemu mbili. Za kuhusu yaliyopita na yaliyopo kwa Waislamu?

Hayo ndio utakayoyaona katika yafuatayo:

Bali utaona yale yaliyo katika mlinganyo ulio timamu zaidi. Na hapa, katika sehemu ya kwanza, mazungumzo yatapita kwa mwendo wa kuwaongelesha (kwa nafsi ya pili) wana wa Isareli. Ama mazungumzo katika sehemu ya pili, yatapita kwa mwendo wa kuwaongelea (nafsi ya tatu) kama yalivyopita, kule katika vile vigawanyo viwili kwa sawa sawa kabisa.

Na kubwa zaidi ya haya yote ni kuwa, wewe utaziona zile aya mbili tukufu, zilizoanzwa na mazungumzo ya kule mwanzo, zikiwa zenyewe zimeanzwa kwa mazungumzo ya hapa. Ili kuwaita wao waingie katika haki kama vile ilivyowaita wajiepushe na batili. Ili ithibiti na kutulizana kwa msikilizaji huyo huyo tangu mwanzoni ya kuwa mazungumzo yatarudi kama yalivyoanza. Lakini ikiwa katika njia inayokabiliana na njia ile iliyotangulia. Na kwa maana mpya iliyosawa na maana ile ya zamani: ﴿**Enyi kizazi cha Israili (Mayahudi)! Kumbukeni neema Zangu nilizokuneemesheni, na (kumbukeni) nilivyokufadhilisheni juu ya viumbe wengine (wote waliokuwa zama hizo). Na iogopeni siku ambayo nafsi haitaifaa kitu nafsi nyingine, wala hakitakubaliwa kikomboleo kwake; wala maombezi hayataifaa, wala hawatanusuriwa. Na (kumbukeni khabari**

**hii:) Mola wake alipomfanyia mtihani (Nabii) Ibrahim kwa amri nyingi;…** ﴾ Al-Baqarah 122-124.

Na hivi hivi, imeanza kwa kuwaita wana wa Israeli waingie katika njia ya watangulizi wema. Na si kwa muundo wa kuwaamrisha na kuwachagiza, uliojaribiwa hapo kabla na haukufanikiwa kwao wao. Bali kwa muundo wa masimulizi wenye kuvutia na ndani yake unawasilisha historia tukufu ya Ibrahimu amani iwe juu yake, watoto wake na vijukuu vyake katika zama za dhahabu. Zama ambazo, hakuna yeyote miongoni mwa watu wa Kitabu wala Wapagani wa Kiarabu anayepinga utukufu wao na kupenda kujinasibisha nao. Muundo ambao unakariri yale yaliyo katika ndimi zao wao wote. Unakariri lile neno tamu lililoachwa na Ibrahimu likiwa limebakia baada yake na likarithiwa na watoto wake na vijukuu vyake. Kila mmoja miongoni mwao akilihusia neno hilo kwa kizazi chake. Neno la kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote).

Na katikati ya uwasilishaji wake wa historia na Uongozi wa Ibrahimu amani iwe juu yake kwa watu, utaiona Quran haisahau kusimulia maneno ya Ibrahimu aliyomuomba Mola wake awajaalie kizazi chake wawe viongozi kwa watu kama alivyojaaliwa yeye kuwa hivyo.

Kisha utaiona Quran, pale inaposimulia namna Ibrahimu na mwanawe Ismaili waliposimama kujenga nyumba inayotukuzwa. Nyumba ambayo Allah ameijaalia kuwa ni tukufu yenye amani na kimbilio la watu na kibla cha swala zao. Haisahau kusimulia unyenyekevu na kuomba kwa wawili hao kumuomba Allah awajaalie vizazi vyao viwe umma uliojisalimisha (wa Kiisalamu). Na apeleke Mtume kutoka miongoni mwao atakayewaelimisha na kuwatakasa.

Kwa hili na hilo, inaandaa kutulizana kwa muunganiko huo madhubuti wa kihistoria. Muunganiko ambao unawaunganisha Nabii huyu na umma wake na hao Manabii wawili watukufu. Na sio tu muungano wa damu wa mwana na baba. Bali pia ni muungano wa msingi na kiunganishi cha umoja wa kidini. Wao ni katika kizazi cha wawili hao. Na uwepo wa umma huo ni kithibitisho cha kukubaliwa kwa dua za wawili hao. Na mila yao ndio mila ya wawili hao. Na kibla chao ndio kibla cha wawili hao. Na sehemu yao ya kuhiji ndio sehemu ya kuhiji ya wawili hao.

Na kwa wakati huo huo inathibitisha moyoni kuwa kukatika kwa uhusiano mtukufu kama huu kwa upande wa Wayahudi wanaojinasibisha

kuwa wao ni watoto wa Ibrahimu na Yakubu. Na hali ya kuwa wao wamekengeuka na kuacha mila za wawili hao. Na usia wa wawili hao wameuhalifu. Sasa udugu wa kinasaba unasaidia nini panapokosekana adabu? Na aliyecheleweshwa na matendo yake hajawahishwapo na nasaba yake**. ﴿Hao ni watu waliokwishapita, hapana faida kujitapa nao). Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakavyochuma, wala hamtaulizwa nyinyi waliyokuwa wakiyafanya wao. (Kila mmoja ataulizwa alipwe kwa alilolifanya mwenyewe﴾.** Al-Baqarah 134.

### 4- **Kutajwa Kwa Mambo Ya Waislamu Wa Zama Za Kupewa Utume [135 – 162]:**

Na kutajwa kwa waliopo na waliopita kumeungana. Na mazungumzo yakatoka katika kuashiria na kuingia katika kutaja wazi wazi. Yakaanza kuthibitisha nyoyoni – wazi wazi – kuwa, muunganiko wa umma huu wa Kiislamu na umma ule uliokuwa mwema ni katika misingi ya mila yake na katika matawi yake yale ya muhimu sana. Na inatusimulia yale maswala yanayojaribiwa na wapumbavu miongoni mwa wana wa Israeli na wengineo, ili kuwanyima Waislamu muunganiko huo. Na hayo ni kwa kule kuwaita kwao Waislamu wafuate mila zao kwa wakati fulani. Na kwa wakati mwingine wanakisema vibaya kibla chao. Na katika majaribio mawili yote hayo wanataka kuuvunja na kuukomesha Uislamu.

Kwa hakika umeshaona mazungumzo yaliyopita hivi punde, namna yalivyochanganyika, ndani yake kukiwa na kutajwa kwa mila ya Ibrahimu na kutajwa kwa kibla chake. Hebu tazama namna ya jambo hilo lilivyokuwa ni msingi wenye nguvu mno wa kile kinachojengwa juu yake kwa hapa, miongoni mwa kutajwa kwa mila ya Waislamu na kutajwa kwa kibla chao.

Katika suala la mila imesema: Kwa hakika watu wa Kitabu wanakuiteni –baada ya ubainifu huu – muwe Wayahudi au Wakristo. Waambieni: bali tunafuata mila ya Ibrahim aliyeziacha mila za upotofu akashika dini ya haki. Na wajulisheni kiwazi wazi suala linalohusu mila hii ya haki, nayo ni kumwamini Allah kwa kila alichokiteremsha kwa Manabii. Hatumtengi yeyote miongoni mwao. Hii ndio itikadi yetu, nyeupee pee! Sasa ni kwa nguzo yake ipi mtatufanyia inda? Na kwa lipi hasa mnagombana nasi? Je, ni kwa Allah ambaye ni Mola wetu na ni Mola wenu? Au kwa Ibrahimu na

watoto wake na wao [hawa-][1] kuwa Wayahudi wala Wakristo ﴿**Hao ni watu waliokwishapita. Wao watapata waliyoyachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma, wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyokuwa wakiyafanya** ﴾**.** Al-Baqarah 141.

Maelezo haya peke yake yalikuwa yanatosha kuzivunjilia mbali hoja zao na kuwafungia mlango nyusoni mwao kwa upande huu. Kwani imeshabainika kuwa misingi ya mila hii ni imara sana kiasi ambacho haina mjadala wa chochote katika nguzo hizo.

Quran ikahama kutoka katika hilo huku ikiwa imekaribia sana kulibatilisha jaribio lao lingine, katika masuala ya (Kaaba tukufu). Masuala ambayo kwayo, kunapatikana mambo mawili makuu ya ibada za Kiislamu nayo ni: (Swala na Hija). Na hiyo kaaba imeshathibiti kuwa yenyewe ndio asili kuu katika dini, kwa vile Ibrahimu na Ismaili wameifanya sehemu hiyo kuwa mwelekeo na sehemu ya kuswaliwa. Lakini hili halikutosha kuwanyamazisha wanaojadili, wale waliolichukua suala la Waislamu kubadilisha kibla chao na kuelekea Kaaba kwa kukiacha kile kibla walichokuwa wakikielekea, kuwa ndilo jambo la kuusema vibaya utume. Na kwa hilo waliwafitinisha baadhi ya waumini madhaifu. Kwa hiyo kukawa na haja kubwa ya kuzidisha ufafanuzi katika suala hili ili kutuliza hoja na kuuvunja utata unaoibuliwa. Na kwa ajili hiyo unaiona Quran ikilielekea suala hilo kwa ncha mbili kuu kabisa miongoni mwa ncha za kulizingatia:

- Mwanzo kabisa inamwamrisha Mtume awajibu wanaohoji juu ya hekima ya huku kubadilika kwa kibla, kwa jibu la nguvu, utukufu na kukataa. Kwa hiyo katika suala hili inalirejesha kwa Yule asiyeulizwa kwa kile akifanyacho. Huku akiwaambia: Kwa hakika pande zote ni sawasawa. Allah anatuelekeza pande aitakayo katika pande hizo, na yeye ndiye anayeongoza katika njia iliyonyooka.
- Kisha wakati mwingine ikaanza kumwamrisha Mtume, na wakati mwingine kuwaamrisha waumini. Na wakati mwingine kuwaamrisha wote kwa pamoja. Kwa mtindo wa kukazia wenye maelezo ya kina ili wathibiti katika kibla hiki walichonacho. Sehemu yoyote watapokuwa wanaishi na katika sehemu yoyote watakapotoka na kuwa safarini.

[1] Yaliyo katika mabano hayakuwepo katika yaliyochapwa. Lakini mtiririko hauwezi kuwa sawa ila kwayo.

- Kisha Quran ikaanza kutawanya nyongeza za amri hizi zenye kutiliwa mkazo, kwa kile akitakacho miongoni mwa kuwafasilia siri za sheria za kale na mpya. Hivyo Quran inasema kwa hakika sheria za kibla kile cha kwanza zilikuwa za muda tu. Na hazikuwa vingine ila ni mtihani wa kupima imani za Wahamiaji ili miongoni mwao abainike yule anayemfuata Mtume na yule aliyekengeuka na kurudi nyuma. Na ama sheria ya kibla hiki cha sasa, ni yenye kubakia. Na sheria hii ina hekima kubwa na lengo tukufu. Kwani chenyewe ni kibla cha kati na kati. Kibla ambacho kinaendana na nyinyi enyi umma wa kati na kati. Hicho ni kibla unachokiridhia ewe Mtume, na ni mara nyingi uligeuza uso wako kuuelekeza mbinguni kwa kuomba na kusubiria ufunuo juu ya kibla hiki. Hiki ni kibla ambacho watu wa Kitabu wenyewe wanakijua kuwa chenyewe ndicho kibla cha haki kutoka kwa Mola wao licha ya kwamba wao wanaficha suala hilo kwa husuda na inadi. Hiki ni kibla ambacho Allah anakishuhudia kuwa chenyewe ndicho cha haki kutoka kwake. Na kwa kumalizia hiki ni kibla ambacho, hakuna yeyote miongoni mwa wasemao ukweli atakayekitolea hoja dhidi yenu. Ama wale madhalimu kamwe hawatoikatisha mijadala yao ya kuhusu suala la kibla hiki, muda wa kuwa bado wanaendeleza uadui wao kwenu. Lakini nyinyi msiwaogope bali jikiteni katika kujitoa kwa ajili ya njia ya Allah. Na vumilieni wala msiwahuzunikie wale watakaouawa miongoni mwenu wakiwa katika njia hii. Kwa hakika umauti katika njia hii ndio uhai utakaobakia milele.
- Kisha ikaashiria kuwa mijadala ya kuhusu kibla hiki sio tu kuzuia matukio ya kiibada yaliyomo ndani ya huo msikiti Mtukufu, bali pia yanazuia yale yaliyomo pembezeni mwake miongoni mwa matukio ya kiibada ﴿**Hakika Safaa na Marwa (Majabali mawili yanayofanyiwa ibada ya kusai (kutembea) huko Makka) ni katika alama za kuadhimisha dini ya Mwenyezi Mungu.** ﴾ Al-Baqarah 158.
- Kisha ikakazia suala la matendo mawili haya ya kiibada kwa namna ile ile ilivyokazia suala la kibla kwa kuwataja watu wa Kitabu waliokuwa wanajua asili ya matendo mawili haya ya kiibada katika historia ya Ibrahimu. Lakini wanaficha yale yaliyoteremshwa na Allah miongoni mwa mambo yaliyobayana kabisa, huku wao wenyewe wakijua.

* * *

Je, umeziona hizi hatua nne zilizotiririshwa na Quran katika kuwalingania wana wa Israeli. Namna zilivyopangiliwa hatua kwa hatua. Na namna kila hatua katika hatua hizo ilivyopita moja moja.

Hebu, kwa mara nyingine lirejeshe jicho lako katika hatua hii ya mwisho katika hatua hizo. Ili uone namna nafasi yake hii ilivyotumika kufikisha malengo mawili tofauti. Na kuifanya hatua hii kuwa kiungo cha kuunganisha baina ya makusudio mawili yaliyo mbali mbali. Hatua hii kwa ujumla wake ni uwokovu kutoka kwa Allah kwenda kwa Mtume na waumini katika suala lao mahususi, na kile kitakachowasaidia wao katika jambo la dini yao. Lakini Quran imejaalia uwokovu huu uwe wa ncha mbili. Na kila ncha imepakwa rangi maalum ya makusudio yanayofungamana nayo. Kwa hiyo makusudio mawili hayo yamekutana katika hatua hii kwa jambo lililokadiriwa.

Hivi hujaona namna ilivyoianza hatua hii kwa kuwasimulia waumini kisa cha kauli za maadui zao kuhusiana na baadhi ya mambo ya hakika ya Kiislamu. Na imekusudia haya mambo ya hakika waliyoyazozania sana. Na Quran ikawa inapangusa vumbi la utata katika uso wa hakika hizo mpaka ikautakasa na kuuweka ukiwa mweupee pee! Mbele ya watazamaji. Kwa hiyo mwanzo huu ukawa, kama unavyouona, ndio mwisho wa hivyo vita virefu, vita ambavyo ndani yake batili ilipigwa kila sehemu.

Kisha umeshaona namna Quran ilivyotiririsha mazungumzo hayo, na ikawa inazithibitisha nyao za waumini zithibiti katika mambo hayo ya hakika kinadharia na kiutendaji. Na ikiwahimiza washikamane nayo si chini ya aya moja.. Je, mwisho huu hautakuwa mwanzo wa kusudio jipya la baada yake linalolenga kuwaongoza waumini katika mafundisho ya Uislamu kwa maelezo kamili?

Hapana.. Kwa hakika mwisho huu ndio unaoashiriwa na mtiririko wa maelezo ya huo uwokovu unaoendelea. Uokovu ambao umekunjuliwa katika kuwaeleza waumini kwa kukunjuliwa sana. Na kwa hiyo, kidogo kidogo, ukabadilisha mwelekeo wa mazungumzo pamoja nao. Mpaka ikafika kuwa kila atakayeyasikiliza maongezi hayo kila mara, atasikia ndani yake kuna wito uliojificha ukisema: leo tumeshamaliza kupambana na maadui, na tumeelekea kuwafundisha na kuwaongoza wapendwa. Na tumeshakifunga kitabu cha waovu, na tumekuja kufungua kitabu cha wema. Na kuwa kurasa hizi za mwisho za kuwalingania wana wa Israeli, hazikuwa kitu kingine ila ni vikosi vya kwanza vya haki. Zikileta habari ya kuwa vyenyewe vitafuatwa na jeshi kumbakumba. Au miale ya alfajiri ya mwongozo itakayobadilisha zama kutoka katika kiza cha usiku kwenda katika weupe wa mchana. Hivi huoni kuwa uwanja umeshakuwa tupu, hauna tena hivyo viutata vya Kiisraili ambavyo katika kiza za batili vilikuwa vikionekana mbele yako kana

kwamba vikiyashambulia matendo hayo ya kiibada na kukushambulia wewe. Je, unahisi katika wao kuna yeyote aliyesalia. Au unawasikia walau kwa visauti vya chini chini?[1]

Je, huioni hii miale ya mwanzo ya jua la sharia ya Kiislamu ikiwa imeshachomoza na ikiongozana yenyewe kwa yenyewe: Misingi inayojumuisha nadharia, ikifuatwa na kikundi cha matawi yake makubwa makubwa ya kiutendaji.. Je, bado haujafika muda kwa matawi mwengine nayo yaje nyuma yake hadi hilo jua lifikie upeo wa mng`ao wake..

Hivi hivi masikio yanafunguka kusikiliza sharia za Uislamu kwa ukamilifu. Na lau kama yenyewe yangetujia sasa hivi kwa kuhesabu na kutiririshwa, basi mazungumzo ya masuala hayo tusingeyadhania kuwa yenyewe ni mazungumzo yaliyokatika.

Lakini Quran, kwa hakika yenyewe imeshawekwa katika mizani madhubuti ya kibayani. Na ikaambatanishwa na haja za nafsi. Haikupenda kuyashambulia hayo makusudio kwa kutosheka na utangulizi huu tu, bali imetaka kuleta mbele yake upande fulani ambao katika upande huo nafsi itaambatana vizuri katika safari hiyo ya mbali. Na itajiandaa kwa safari nyingine ya kuelekea katika kusudio jipya. Hebu taza haya yafuatayo:

### **Lango La Kusudio La Tatu: Aya Kumi Na Tano** [163 – 177]

Aya kumi na nusu aya miongoni mwa aya tukufu. Hizo ndio masafa ya maingilio yaliyopo baina ya mlango na nyumba. Na mtembeaji anayakata masafa haya kwa hatua tatu:

- (Hatua ya kwanza) kuthibitisha upweke wa Muumba anayeabudiwa.
- (Hatua ya pili) kuthibitisha upweke wa Mtoa amri Mwenye kutiiwa.
- (Hatua ya tatu) kuweka faharasa ya jumla ya maamrisho na utiifu utakiwao.

### (**Hatua Ya Kwanza) Kuthibitisha Upweke Wa Muumba Anayeabudiwa**.

Kwa hakika hatua hii imekuja katika wakati ambao inahitajika sana baina ya hatua zilizoitangulia na zinazoifuatia. Kwa hakika kile kilichopita, miongoni mwa kutukuza suala la Kaaba, Maqaam, Swafaa na Marwa. Kwa

[1] Visauti vya chini chini: visauti vya mbali au vidhaifu.

upande wake kilikuwa kinawapatia Waislamu wapya maana fulani hivi miongoni mwa maana za upagani wa mwanzo, ikionesha kuyatukuza mawe na maada. Na hasa hasa, kwa siku hizo, maeneo haya matakatifu yalikuwa ni makazi ya masanamu na kusimikwa matambiko pembezeni mwake na juu yake. Kwa hiyo ikawa lazima suala hilo la kuyatukuza lisiachwe hivyo hivyo bila ya kuwekewa mipaka na kufungiwa. Na hiyo mihemko ya kinafsi isiachwe bila ya kusukumwa na kutengwa mbali. Ili kusibakie na shaka yeyote juu ya kusimama kwa waswaliji katika Maqaam ya Ibrahimu na kuelekeza nyuso zao upande wa Kaaba, na kujipangusia kwa nguzo zake kwa wanaoizunguka, na kwa mahujaji na wafanyao hija ndogo/umra kuzunguka baina ya Swafaa na Marwa.

Kwa yote hayo, Uislamu haukusudii kuelekeza nyoyo za watu kwa mawe haya na athari hizi kwa kujikurubisha[1] na kuyaabudu au kutarajia rehema zake au kutaka uombezi wake. Hakika si vinginevyo, hayo yanakusudiwa kumuheshimisha Mungu wa haki na kutii amri yake ya kumwabudu yeye tu katika maeneo ya rehema zake na Baraka zake. Maeneo ambayo waja wake wema wa hapo mwanzo waliyaendea. Kisha kusasisha kumbukizi ya watu wema hao katika nafsi. Na kuyawezesha mahaba ya kuwapenda nyoyoni. Kwa kufuata athari zao, na kuigiza harakati zao na utulivu wao. Ili hali ya umma kwa sasa iwe na muunganiko na hali ya umma ya kipindi kilichopita. Na ili, kutokana na hilo, kuwe na mfumo wa umma mmoja unaozunguka katika mhimili mmoja. Na unaoelekea katika lengo moja, ambalo ni makusudio makuu na mataukufu zaidi. ﴿**Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye…** ﴾ Al-Baqarah 163.

Je, mnamjua ni nani huyo..? Yeye si Kaaba wala Swafaa na Marwa. Si Ibrahimu wala Maqamu Ibrahimu. Lakini Yeye ni ﴿**Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo** ﴾ Al-Baqarah 163. Ambaye rehema na neema zake zimekienea kila kitu. ﴿**Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi… bila shaka zimo ishara kwa watu wenye akili (kuwa yuko Mwenyezi Mungu na ni Mmoja tu** ﴾**.** Al-Baqarah 164. Ambaye mikononi mwake kuna nguvu zote na mamlaka zote: Hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu kwake na wala hatafunga yoyote jinsi ya kufunga kwake. ﴿**… Na laiti waliodhulumu nafsi zao wanaijua (balaa itakayowapata) watakapoiona adhabu (siku hiyo ya Kiyama), kwa kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu (siku hiyo – hakuna masanamu wa**

[1] Kijikurubisha: kutaka ukaribu wa kumnyenyekea na kumwabudu.

**kuwashufaia wala mengineyo) na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu ﴿.** Al-Baqarah 165.

Haya ni kwa upande wa kusudio lililotokewa na ombwe.

Na ama kwa upande wa kusudio tuliolielekea, kwa hakika hatua hii ilikuwa ni ya msingi. Na kutangulia kwake kulikuwa hapana budi. Kabla ya kuingia katika maelezo kamili ya hukumu ya kiutendaji. Ili hatua hii iwe ni kuyaelekeza macho yatazame upande ule unaotakiwa kupokea mazungumzo ya kuhusiana na suala la hukumu hizo. Na hayo ni kwa kuwa mwanadamu anapojua kuwa ana bwana mmoja na akausalimisha uso na mwelekeo wake kwa bwana huyo. Basi anapaswa asifanye chochote ila kwa amri za bwana huyo wala asichukue sheria zozote ila kutoka mkononi mwa bwana huyo. Na yule mwenye miungu tofauti tofauti, na kwa kwake yeye, hiyo miungu washirika inagombana na kuchuana, na kila mmoja wao anataka kutekelezewa hukumu zake na apate sehemu yake ya kutiiwa. Na kwa hiyo mtu huyo atakuwa na vyanzo vingi vya amri za kutiiwa. Amri ya mababa na ukoo, amri ya desturi na ada za kurithiwa zilizozushwa, amri za watawala na wakuu, amri za shetani na matamanio ya nafsi… kwa ajili ya hayo ikaikazia kwa ile hatua ya pili.

### (**Hatua Ya Pili) Kuthibitisha Upweke Wa Mtoa Amri Mwenye Kutiiwa)**.

Nayo ni nguzo miongoni mwa nguzo za itikadi ya upwekeshaji katika Uislamu. Na kama vile ilivyo katika asili ya upwekeshaji, katika ibada zetu tusijitwalie mungu mwingine kinyume na Mwingi wa rehema, ambaye mkononi mwake kuna uumbaji, riziki, madhara na manufaa. Na vile vile katika asili ya upwekeshaji, usikifanye kitu kingine chochote kiwe na maamuzi katika matendo yako yote. Bali uitakidi kuwa hakuna hukumu ila za kwake tu. Na kwamba mkononi mwake yeye peke yake ndio kuna maamrisho na makatazo. Na halali ni ile aliyoihalalisha Allah tu. Na haramu ni ile aliyoiharamisha Allah tu. Na mtu atakayehalalisha lile lililoharamishwa na Allah au kuharamisha lile lililohalalishwa na Allah, basi mtu huyo ameshakufuru. Na kama ilivyo kwamba haistahiki yeye awe Muumba kisha aabudiwe mwingine, na yeye ndiye mtoa riziki kisha

anashukuriwa mwingine. Vilevile haistahiki yeye kuwa mwamuzi na kutiiwa mwingine[1].

---

[1] Hapana shaka ya kwamba Sheikh Muhammad Abdullah Daraazu – Allah amrehemu – kwa maelezo yake makali na ubainifu wake wa wazi kwa hapa, katika suala la: Kuhukumu Kwa Mujibu Wa Kile Alichokiteremsha Allah. Hakika si vinginevyo anaungana na msafara wa wanazuoni wachamungu katika kujitoa kwao na nia zao safi na kutoa nasaha za dini ya Allah na sheria zake. Wanazuoni ambao wameieleza haki bila ya kuchelea. Hawana tamaa ya dhahabu ya mwenye kutukuzwa wala hawaogopi upanga wake. Kwa hakika hawaogopi ila Allah tu. Na tazama baadhi ya yale yanayoliweka wazi suala hili:

- Allah Mtukufu Aliyetukuka kuwaelezea wapingao hukumu na kuhukumiwa kwa sharia zake kwa sifa mbaya katika Quran Tukufu, miongoni mwazo ni:
- Ukafiri: ﴿**Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri** ﴾. Al-Maidah 44.
- Kumshirikisha Allah: ﴿**Oh! Wana washirika (wa Mwenyezi Mungu) waliowawekea dini asiyoitolea Mwenyezi Mungu ruhusa (yake** ﴾**?** Ash-Shuura 21.
  Na vile vile ﴿**Nao hawana mlinzi badala yake (Mwenyezi Mungu) wala yeye hamshirikishi yoyote katika hukumu zake** ﴾. Al-Kahf 26.
- Kuhukumiwa kitwaghuti = kwa njia isiyowafiki Sharia: ﴿**Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Nao wanataka wakahukumiwe kwa njia isiyowafiki Sharia; na hali wameamrishwa kukataa njia hiyo. Na shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki** ﴾**.** An-Nisaa 60.
- Unafiki: ﴿**Na wanapoambiwa: ''Njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na (njooni) kwa Mtume, '' utawaona wanafiki wanajiweka mbali nawe kabisa** ﴾**.** An-Nisaa 61.
- Kupotea na kufuata matamanio ya nafsi: ﴿**Ewe Daudi! Hakika tumekujaalia kuwa Khalifa katika ardhi, basi wahukumu watu kwa haki wala usifuate matamanio ya nafsi yasije yakakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa yakini wale wanaopotea, wakaacha njia ya Mwenyezi Mungu, wao watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau (kupuuza) kwao siku ya Hisabu** ﴾**.** Sad 26.
  Na vile vile ﴿**Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki** ﴾**.** Al-Maidah 48.
- Kufuata hukumu za kijahiliya: ﴿**Je, wao wanataka hukumu za Kijahili (ya zile siku za ujinga kabla ya kuletwa Mtume)? Na nani aliyemwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini** ﴾**.** Al-Maidah 50.
- Kukosa Imani: ﴿**Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa** ﴾**.** A-Nisaa 65.
- Dhulma: ﴿**Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu** ﴾**.** Al-Maidah 45.
- Ufaski/maasi: ﴿**Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio maasi** ﴾**.** Al-Maidah 45.
- Maradhi ya moyo, shaka mbaya na kumdhania vibaya Mwenyezi Mungu na Mtume wake: ﴿**Na wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili awahukumu**

**baina yao; baadhi yao wanayakataa hayo (wanapohisi kuwa wao ni madhalimu, hawatapata haki). Na kama ikiwa haki ni yao, wanamjia (upesi Mtume) kwa kutii. Je, wana maradhi katika nyoyo zao, au Mwenyezi Mungu na Mtume wake atawadhulumu! Bali hao ndio madhalimu** ﴾. An-Nur 48 – 50. Kinachojulishwa na aya hizi ni kuwa wao wanakataa kuhukumiwa kwa mujibu wa Allah na Mtume wake ila katika hali moja tu, nayo ni pale wanapokuwa na yakini kuwa hukumu itakuwa upande wao. Kwa hiyo wao, kwa hakika, ni waabudu wa tamaa zao za batili na matamanio yao.

- Kuwaiga makafiri na washirikina: ﴿**Na wanapoambiwa; ''Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu'' husema: ''Bali tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu.'' Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu chochote wala hawakuongoka (watawafuata tu** ﴾**?** Al-Baqarah 170.
- Kuizushia dini na kudanganyika na huo uzushi: ﴿**Hawaoni wale waliopewa (kufahamu) sehemu ya Kitabu cha (Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara) wanaitwa kukiendea Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili kiwahukumu (haki) baina yao; kisha taifa moja miongoni mwao hukengeuka? Nao (daima) ni wenye kukengeuka tu. Hayo (ya kutojali maamrisho ya Mwenyezi Mungu wala makatazo yake) ni kwa sababu walisema: ''Hautatugusa Moto isipokuwa kwa siku chache;'' na yakawadanganya katika dini yao yale waliyokuwa wakiyazua: (kuwa watasamehewa au watakaa siku chache tu Motoni** ﴾**.** Aal-Imran 23 – 24.
- Ujinga/kutokujua: ﴿**Kisha tumekuweka juu ya sharia ya amri yetu, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wale wasiojua kitu** ﴾**.** Al-Jathiyah 18.
- Na Sheikh Abdul Azizi Bin Baazi – Allah amuhifadhi – amesema katika risala yake (Ulazima wa kuhukumu kwa Sharia za Allah na kuziacha zile zilizokinyume nazo) Uk 6: Imani ya mja haitotimia ila pale atakapomwamini Allah na kuridhia hukumu zake kwa machache na mengi. Na kuhukumu kwa sheria zake yeye peke yake katika kila jambo miongoni mwa majambo yake: Katika nafsi, mali na heshima. Na kama si hivyo, basi atakuwa anamwabudu mwingine kama Allah Mtukufu alivyosema: ﴿**Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma ya kwamba ''Muabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni (Ibilisi) muovu.''** ﴾ An-Nahli 36. Basi atakayenyenyekea kwa Allah Mtukufu aliyetukuka, kumtii yeye na kuhukumu kwa ufunuo wake, basi huyo ndiye anayemwabudu yeye. Na atakayenyenyekea kwa mwingine na kuhukumu kwa sharia isiyokuwa sharia yake, basi mtu huyo atakuwa amemwabudu twaghuti na kumtii. Kama Mtukufu alivyosema: ﴿**Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Nao wanataka wakahukumiwe kwa njia isiyowafiki Sharia; na hali wameamrishwa kukataa njia hiyo. Na shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki** ﴾**.** An-Nisaa 60. أ هـ.
- Na Al-Haafidhu Ibnu Kathiiri katika tafsiri yake 13/122 amesema:
  Na kauli yake ﴿**Je, wao wanataka hukumu za Kijahili (ya zile siku za ujinga kabla ya kuletwa Mtume)? Na nani aliyemwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini** ﴾**.** Al-Maidah 50. Allah Mtukufu anawapinga wale waliotoka katika hukumu za Allah zilizo madhubuti zenye kujumuisha kila la heri. Zinazokataza kila la shari. Na kuziacha na kuzifuata nyinginezo miongoni mwa rai, matamanio na istilahi zilizowekwa na wanadamu bila mashiko kutoka katika sheria za Allah. Kama vile walivyokuwa watu wa kijahiliya wakihukumiana kwa upotevu na ujinga. Miongoni mwa yale wanayoyaweka kwa maoni yao na matamanio yao. Na kama wanavyohukumu Matataru wa Kimongoli miongoni mwa siasi za kifalme zilizochukuliwa kutoka kwa mfalme wao Jimkiizu

Khan aliyewawekea (Al-Yaasiqu) nayo ni kifungu cha kitabu kinachojumuisha hukumu alizozichukua kutoka katika sheria mbali mbali zikiwemo za Kiyahudi, Kikristo na Mila ya Kiislamu.

Na ndani yake kuna hukumu nyingi alizozichukua kutoka katika mtazamo wake na matamanio yake tu. Na kwa wanawe zikawa ni sheria zenye kufuatwa. Wanazitanguliza sheria hizo kuliko kuhukumu kwa Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake. na atakayefanya hivyo miongoni mwao basi huyo ni kafiri anapaswa kupambana naye. Hadi arejee katika hukumu za Allah na Mtume wake. Wala asikifanye hakimu kitu kingine kwa kichache wala kwa kingi… Na ni nani aliyemwadilifu zaidi kuliko Allah katika hukumu zake? Mwenye kutia akilini kumhusu Allah atamfanya kuwa ndio mwekaji wa sheria zake, atamwamini, na atayakinisha, na atajua kuwa Allah Mtukufu ndio mbora wa wenye kuhukumu. Na ni mwingi wa huruma kwa viumbe wake kuliko mama kwa mwanawe. Kwa hakika yeye Allah Mtukufu ndiye Mjuzi wa kila kitu. Muweza wa kila kitu. Mwadilifu katika kila kitu. أ هـ .

- Na vile vile Al-Haafidhu Ibnu Kathiiri katika Albidaayatu Wannihaayatu yake 13/128 amesema: (baada ya kutaja baadhi ya hukumu za Al-Yaasiq nacho ni kitabu cha sheria alichokiweka Jimkiizu Khan Mmongoli kuwawekea watu wake): Na katika hayo yote kuna kwenda kinyume na sharia za Allah zilizoteremshwa kwa waja wake ambao ni Manabii rehema na amani ziwe juu yao. Na mwenye kuacha sharia madhubuti iliyoteremshwa kwa Muhammad bin Abdillah Nabii wa mwisho, na akahukumu kwa sheria nyingine miongoni mwa sheria zilizofutwa huyo atakuwa ameshakufuru. Na inakuwaje kwa yule anayehukumu kwa Al-Yaasaa na kuitanguliza mbele na kuacha sharia ya Allah? Atakayefanya hivyo ameshakufuru kwa makakubaliano ya waislamu أ هـ .
- Na Sheikh Ahmad Shaakir, kadhi wa kisharia na mwanajopo wa mahakama ya juu ya kisharia na mwanachuoni wa hadithi aliye maarufu, Allah amrehemu…. Amesema katika Umdatu Attafsiiri 4/173:… baada ya kunukuu haya maneno yaliyopita ya Alhaafidhi Ibnu Kathiiri:

  Ninasema: – pamoja na haya – Je, katika sheria za Allah inafaa kwa Waislamu katika nchi yao watumie sheria walizozipata kutoka katika sheria za Ulaya ya Kipagani yenye kukufuru? Bali wafuate sheria zinazoingiliana na matamanio na rai za batili. Wanazibadili na kuzigeuza kama watakavyo. Mwekaji wake hajali kama zimeafikiana na sharia za Kiislamu au zinapingana?

  Kwa hakika Waislamu hawajapatapo kupatwa na mtihani huu katu – katika historia yao tunayoijua – ila katika zama hizo za Tatari. Na hizo zilikuwa ndizo zama mbaya kabisa zenye dhulma na kiza. Pamoja na haya, kwa hakika Waislamu hawakuwanyenyekea wao. Bali Uislamu uliwashinda Matatari. Kisha ukawachanganya hao Matatari na kuwaingiza katika sharia zake. Na ikaondoka ile athari ya kile walichokifanya. Kwa kuthibiti kwa Waislamu katika dini yao na sharia zao. Na kwa kuwa utawala huo mbaya muovu, chanzo chake kilikuwa ni kikundi cha watawala wa wakati huo. Haukuchanganyika na yeyote miongoni mwa raia wa Kiislamu wanaotawaliwa. Na raia hawakujifunza sheria hizo wala hawajawafundisha watoto wao. Kwa hiyo ni haraka ilioje kwa kuondoka kwa athari za sheria hiyo.

  Je, hamjayaona haya maelezo ya nguvu ya Alhaafidhu Ibnu Kathiiri – katika karne ya nane – dhidi ya hiyo kanuni ya kidunia. Kanuni ambayo imetengenezwa na adui wa Uislamu Jankiiz Khan? Je, nyinyi hamuoni kama anaelezea hali ya Waislamu wa zama hizi, za karne ya kumi na nne. Isipokuwa katika kundi moja tulililoliashiria hivi punde: Kwa hakika hilo lilikuwa kwa tabaka maalum miongoni mwa watawala. Nalo kwa

﴿**Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri, wala msifuate nyayo za shetani (yale anayokuamrisheni). Bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri** ﴾**.** Al-Baqarah 168.

Kwa hakika katika kukazia huu upweke wa kutunga sharia kama vile ilivyopita katika kukazia umoja wa uungu.

Quran ikaanza swala hili kwa kuwajulisha watu neema za Allah zenye kukusanya kila kitu, na rehema zake zilizokamilifu. Wepesi wa sharia na kuendana kwake na maumbile. Kwani zenyewe zina upana wa uhuru wa kuchagua, hazijawaharamishia chakula isipokuwa vitu vinne[1] tu na vyote ni uchafu mbaya. Na wamehalalishiwa wanufaike na yasiyokuwa hayo katika vile vyote vilivyomo ardhini vikiwa ni vya halali na vizuri. Na kunapokuwa na dhiki ya dharura, basi vyote vinabadilika na kuwa vya halali, na watakaokula hawatapata dhambi. ﴿**Lakini aliyefikwa na dharura (ya kula vitu hivi) bila kutamani wala kupita kiasi, yeye hana dhambi. Hakika**

---

haraka haraka likajiwa na muda wake likachanganyika katika umma wa Kiislamu. Na athari za kile kilichokifanya kikaondoka.

Kisha Waislamu wa sasa wamekuwa na hali mbaya zaidi na dhuluma na kiza zaidi kuliko wa zama hizo. Kwa sababu nyumati nyingi za Kiislamu, kwa sasa zinakaribia kuchanganyika katika kanuni zinazoenda kinyume na sharia. Hizi ni kanuni ambazo zinafanana na zile za (Alyaasiq) zilizotengenezwa na mtu kafiri ukafiri wa wazi. Ama hizi ni kanuni zinazotungwa na watu wanaojinasibu na Uislamu. Kisha wanawafundisha watoto wa Kiislamu. Na wanajifakharisha nazo mababa na watoto. Kisha wanafanya kuwa rejea za mambo yao ni kuzifuata hizi (Alyaasiq za sasa) na wanambeza yule anayepingana nao katika hilo. Na yule anayewaita washikamane na dini yao na sharia yao wanamwita (mrejesha nyuma) na (asiyebadilika)! Na matamko mengine mabaya kama hayo...

Kwa hakika jambo katika kanuni hizi za kisekyula lipo wazi sana kama uwazi wa jua. Zenyewe ni ukafiri wa wazi. Hauna kujificha wala kupindisha pindisha. Hakuna udhuru kwa yeyote miongoni mwa wale wanaojinasibisha na Uislamu – vyovyote atakavyokuwa – akizifanyia kazi au akizinyenyekea au akizikubali. Basi mwanadamu ajihadhari yeye mwenyewe. Na (kila mtu ni mwenye kuihesabu nafsi yake).

Zinduka, na wanazuoni waidhihirishe haki bila kuhofia. Wafikishe kile walichoamrishwa kukifikisha bila ya kuchoka, kudhoofu wala kufanya upungufu. أ هـ .

[1] Navyo ni:

- Mzoga: mnyama aliyekufa bila kuchinjwa kisheria miongoni mwa wanyama wanaoliwa.
- Damu: Yaani damu iliyotiririka kutoka kwa mnyama.
- Nyama ya nguruwe.
- Kilichochinjwa kwa ajili ya asiyekuwa Allah: yaani kile kilichochinjwa kwa ajili ya masanamu, makuhani, upagani, mizimu, mashetani na kilicho kama hivi miongoni mwa vile vilivyokuwa vikifanywa na watu wa zama za ujinga, wakichinja kwa ajili ya vitu hivyo.

**Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu ﴿** . Al-Baqarah 173. Na ukiachana na mtindo huu unaozilainisha nyoyo na kuzichukua zinyenyekee amri za Huyu Mola Mwingi wa huruma kwa waja zake. Je, yule anayekuhalalishieni vitu vizuri na kukuharamishieni vitu vibaya, ana haki ya kutiiwa, au yule: ﴾**Yeye (Shetani) anakuamrisheni (kufanya) mambo mabaya na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu msiyoyajua (yakini yake kuwa kweli kasema au hakusema ﴿.** Al-Baqarah 169. Je, yule anayewaongoza katika haki ndiye anayestahiki kufuatwa au yule: ﴾**hata kama baba zao walikuwa hawafahamu chochote wala hawakuongoka (watawafuata tu ﴿?** Al-Baqarah 170.

• (Kisha Quran ikahitimisha suala hili) kwa kuwajulisha upeo wa ghadhabu zake na ulipaji kisasi wake. Kwa wale ambao wanaficha jambo la amri zake na makatazo yake na kuyabadilisha mawili hayo na mengine asiyoyaamrisha wala kuyakataza, na kwa hayo wanachukua rushwa na machukivu. ﴾**Hao hawali matumboni mwao isipokuwa moto, wala Mwenyezi Mungu hatawasemeza siku ya Kiama (maneno ya Rehema), wala hatawatakasa; nao watapata adhabu iliyokali ﴿.** Al-Baqarah 174.

Na mtazamaji katika mapito ya maelezo haya, kama atatafakari vizuri namna yalivyochaguliwa, mazungumzo ya ulaji na mapato miongoni mwa aina za halali na haramu. Ataona uzuri wa nafasi yaliyopo maneno haya kwa hapa. Kitu kinachojulikana kuwa chenyewe ndio kamba imara iliyofungwa katika kamba ya bayani. Na kuzuia mianya iliyopo baina ya hatua zake zilizotangulia na za sasa.

Yenyewe, kwa upande wa kiutendaji ni mojawapo ya hayo matawi yatakayoendewa na mazungumzo hivi karibuni tu. Na kutajwa kwake hapa kunachukuliwa kuwa ni kiashirio cha kukaribia kuanza katika kusudio jipya. Kisha yenyewe kwa upande wa kiitikadi yanaungana muungano wa kihistoria ulio imara na itikadi ya upwekeshaji, itikadi inayoiendea. Hayo ni kwa kuwa watu wa Jahiliya miongoni mwa wapagani na waliopewa Kitabu, pale walipofuata hatua za shetani, naye akawapoteza wakaepukana na upwekeshaji uliozoeleka hadi wakajitwalia waungu kinyume na Allah, wakiwapenda kama anavyopendwa Allah. Hawakuwa na muda mrefu hadi wakafunguliwa milango ya ushirikina katika sharia, baada ya kushirikisha katika ibada. Wakawa wanaharamisha mimea, wanyama wa halali na kuhalalisha wa haramu. Bali wakati wa kuchinja wanyama wao wakawa wanawachinjia si kwa ajili ya Allah – wakipaza sauti kutaja majina ya

miungu yao – na wakihalalisha nyama yao kwa uchinjaji huo. Kwa hiyo katika hilo wakakusanya baina ya ufisadi wa aina tatu: maaswi, uzushi na shirki kubwa.

Kana kwamba mlango wa kuharamisha na kuhalalisha vyakula na mapato ulikuwa ndio mlango wa kwanza kufunguliwa katika zama za jahiliya ili kutunga sheria bila ya idhini ya Allah. Na kwa ajili hiyo, huo ndio ukawa mlango wa kwanza uliozibwa na Quran baada ya mlango wa shirki kubwa. Kwa hiyo unaona makatazo juu ya hilo. Na andiko limeelezea hivyo na kubainisha lile la haki katika hilo. Kisha ikafuatisha kutaja itikadi hadi katika sura zilizoteremka Makka kama vile Suratul Al-An`aam[1], Al-Aaraf, Yunus, Annahl na nyinginezo.

Na miongoni mwa vilivyozidisha uzuri wa eneo lake hili ni kule kuja kwake katika mtiririko uliotaja ndani yake upwekeshaji. Limekaa kiuadilifu kwa kuja kwa hukumu ya kibla katika mtiririko wa kutaja mila ya Ibrahimu. Yote mawili ni matawi makuu yanayoungana na asili kubwa. Hivi huoni namna mazungumzo yalivyomalizia katika suala hilo kama vile

---

[1] Soma katika Suratul Al-An`aam aya ishirini na saba ambazo mwanzo wake ni kauli yake: ﴿**Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu sehemu katika mimea aliyoiumba (Mwenyewe) na katika wanyama (aliowaumba Mwenyewe)…** ﴾. AL-An`aam 136 – 152. Na katika Suratul Al-Aaraf kauli yake: ﴿**Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila Sala; na kuleni (vizuri) na kunyweni? (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi (wapindukiao mipaka). Sema: ''Ni nani aliyeharamisha mapambo ya Mwenyezi Mungu ambayo amewatolea waja wake. Na (nani aliyeharamisha) vitu vizuri katika vyakula?'' Sema: ''Vitu hivyo vimewahalalikia Waislamu (hapa) katika maisha ya dunia; (na) vitakuwa vyao peke yao siku ya Kiyama''. Namna hivi tunazieleza Aya kwa watu wajuao** ﴾. Al-Aaraf aya mbili 31 na 32. Na kauli yake: ﴿**Basi wakawaandamia nyuma yao (yaani baada ya wale Mayahudi wazuri, Mitume na wengineo, kikaja) kizazi kibaya waliorithi Kitabu (cha Mwenyezi Mungu pasipo kukifuata wala kuzingatia yale ambayo yaliwafika wabaya wao) wanachukua vilivyokatazwa vya hapa ulimwenguni…** ﴾ Al-Aaraf 169. Na katika suratu Yuunus kuna kauli yake: ﴿**Sema: ''Je! Mnaonaje zile riziki alizokuteremshieni Mwenyezi Mungu kisha mkafanya – katika hizo – (nyingine kuwa za) haramu na (nyingine kuwa za) halali. '' Sema: ''Je! Mwenyezi Mungu amekuruhusuni (kufanya hivyo) au mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo tu?'' na ni nini dhana ya wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo, juu ya siku ya Kiama?** ﴾ Yunus 59 – 60. Na katika suratu An-Nahl kuna kauli yake: ﴿**Wala msiuze ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa thamani chache…** ﴾ An-Nahl 95. Na kauli yake: ﴿**Amekuharamishieni nyamafu tu (mzoga) na damu na nyama ya nguruwe na (mnyama) achinjwaye kwa jina lisilokuwa la Mwenyezi Mungu…** ﴾ An-Aam 115 – 116. [Daraazu].

ilivyomalizia huko kwa kutoa maonyo kwa wapingaji[1]. ﴿**Hakika wale wafichao aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika kitabu…** ﴾ Al-Baqarah 174? Au huoni namna Uislamu ulivyojaalia maswala mawili: Kibla na vichinjwa. Yote mawili ni miongoni mwa matendo ya kiibada ambayo kwayo, Muislamu anajipambanua na mtu mwingine. Kama anavyojipambanua kwa shahada na swala: **‘‘Atakaye swali swala zetu na kuelekea Kibla chetu, na akala vichinjwa vyetu basi huyo ni Muislamu ambaye ana dhima ya Allah na Mtume wake’’[2].**

Uzushi wa kuharamisha kwa kutumia rai katika mlango huu haujaishia katika lile kundi lililotoka katika mila ya Kiislamu tu. Bali, kwa hakika baadhi ya Waislamu wa zama za Nabii walikaribia kupatwa na maambukizi ya nyumati za kabla yao. Kwani walikusudia kufanya utawa, na kujiharamishia vitu vizuri miongoni mwa vyakula na vinginevyo[3]. Hakuna kuharamisha miongoni mwa vile alivyovihalalisha Allah? Bali kuvipa nyongo na kuichukua nafsi iwe na subira na vitu hivyo kwa kuweka nadhiri au viapo au kuazimia hasa hasa. Basi Quran ikawajibu suala hili la kizushi na kuufunga kabisa mlango wake. Ili usijekuwa ndio uchochoro[4] wa vile vilivyo nyuma yake. na ikawazindua kuwa, katika suala la kumpwekesha kwao Allah, wajishushe katika hukumu zake katika vile alivyowahalalishia. Katika hivyo wasimamie sharia na kushukuru. Kama ilivyoteremka katika hukumu yake juu ya kile alichowaharamishia kukisimamia kwa sharia ya

---

[1] Hii ni kuashiria kauli yake Allah Mtukufu huko: ﴿**Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule afichaye ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu?** ﴾**.** Al-Baqarah 140.

[2] Hiyo ni hadithi ya Anasi bin Maaliki iliyo marufuu. Na ukamilisho wake ni: **‘‘na wala msimuasi Allah katika dhima yake’’.** Imepokewa na Bukhari katika mlango wa Swala 391.

[3] Na miongoni mwa hayo ni hadithi ya Anasi iliyopokewa na Bukhari na Muslimu: **‘‘Watu watatu walikwenda katika nyumba za wake wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, wakiulizia ibada ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Na pale walipoelezwa, kana kwamba waliziona chache. Wakasema: sisi tu wapi na wapi kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake? Yeye ameshasamehewa na Allah madhambi yaliyotangulia na yajayo. Mmoja wao akasema: Ama mimi, nitaswali usiku milele. Na mwingine akasema: Mimi nitafunga zama zote wala sitofungua. Na mwingine akasema: Mimi nitajitenga na wanawake. Wala sitaoa kamwe. Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akaja na kusema: Nyinyi ndio wale ambao mlisema hivi na hivi? Ama naapa kwa Allah, kwa hakika mimi ndio namuogopa zaidi Allah kuliko nyinyi, na namcha Allah zaidi yenu. Lakini mimi nafunga na ninafungua, naswali na nalala, na naoa wanawake. Atakayejitenga na mwenendo wangu huyo si katika mimi’’.** Imepokewa na Bukhari katika mlango wa Ndoa 5063. Na Muslimu katika mlango wa ndoa 5.

[4] Uchochoro: mapito na njia.

kusubiri: ﴿**Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa mnamwabudu yeye peke yake** ﴾**.** Al-Baqarah 172.

Tazama namna mazungumzo kwa watu yalivyokuwa ya kiujumla kwa asili hii na viambata vyake. Vikiashiria kuwazungumzisha waumini kwa sifa ya pekee, na kile watakachokisoma miongoni mwa hukumu. Kama yalivyo mazungumzo kwa watu wote juu ya nguzo za Kiislamu mwanzoni mwa surah hii, yalikuwa yanaashiria yale yanafuatia miongoni mwa kuzungumzishwa wana wa Israeli kwa sifa ya kipekee. Kuwaita wao waingie katika hilo kwa moyo wote. Je, unaona kuna muundo mzuri kuliko mfumo huu wenye kukabiliana na kulingana?

Na sasa umeshavuta pumzi ya kujiandaa kupokea maamrisho na makatazo mengine. Tazama namna ilivyolipangia hilo hatua ya tatu na ya mwisho.

### (Hatua Ya Mwisho) Majumuisho Ya Sharia Za Kidini

Na ndani yake utaona maajabu ya ufundi wa mpangilio:

(1) Tazama uzuri wa kumalizia katika kuunganisha kwake baina ya kusudio la mwanzo na kusudio jipya, kwa namna ambayo makusudio hayo yanaungana kimatamko. Na kwa namana hiyo yanatengana kihukumu.. yenyewe katika kuyaunganisha kimatamshi, kana kwamba inaweka mmoja wa miguu yako mwishoni mwa kusudio la mwanzo na mguu pili inauweka mwanzoni mwa kusudio jipya. Lakini yenyewe katika kuyatenganisha makusudio hayo kihukumu, kwa kutumia maneno mawili: la ukanushi na la kudiriki. Kana kwamba inaigeuza miguu yako yote ielekee mbele. ﴿**Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali). Lakini yako na mema mengine…** ﴾**.** Al-Baqarah 177.

Anasema: suala la kuainisha maeneo na pande katika mionekano ya kiibada – suala hilo ndilo ambalo limeshughulisha akili za wenye kutofautiana na wenye kuungana katika kuhakiki, kukosoa na kujibu – Kwa hakika suala hili sio kila kitu kinachotakiwa kushughulika nacho katika maswala ya wema. Bali lenyewe ni sehemu mojawapo katika jumla ya mambo mengi yanayojumuisha suala moja miongoni mwa maswala yake. Kwa hakika wema ni neno linalokusanya mambo yote ya heri: kinadharia na

kivitendo, katika miamala na viumbe, katika kumwabudu Muumba na katika kuzitakasa tabia. Na kwa mambo haya yote, ndipo waumini wa kweli wanatakiwa wajishughulishe nayo.

(2) Kisha itazame pale ilipoelekea katika kutoa maelezo ya maswala hayo. Namna yenyewe haijayaelekea kwa mpigo mmoja. Bali imeanza kidogo kidogo kwa upole na ulaini. Ikatanguliza neno lililo juu ya ujumla na chini ya maelezo kamili. Neno hilo ni kama faharasa ya kanuni za imani na sheria za Kiislamu. ﴿**Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na wanawapa mali – juu ya kuwa wanayapenda – jamaa na mayatima na masikini… ﴾.** Al-Baqarah 177.

(3) Na hapa tazama utiririshaji wa misingi ya imani, namna ilivyoepa mpangilio wake uliozoeleka. Mpangilio uliozingatiwa mwanzoni mwa sura hii si chini ya mara moja. Utaiona, hapa imekusanya baina ya pande mbili (kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho) na ikamalizia na cha kati (Kuwaamini Malaika, Vitabu na Manabii). Hivyo ni kwa kuwa, kutokana na hivi vitu vya kati ndipo kunapojulikana hukumu za kisheria. Na kutoka mkononi mwake ndipo zinapochukuliwa. Ili hukumu hizo ziungane na hayo mpaka kusiwe na kizuizi chochote baina ya Asili na tawi. Na kwa ajili hiyo, imechunga mpangilio wa nguzo za haya ya kati vyenyewe kwa vyenyewe. Ikaanza na Malaika, na wao ndio wabeba ufunuo. Ikifuatisha na Kitabu nacho ndicho ufunuo unaobebwa. Na ikafuatiliza kwa Manabii, nao ndio wanaoshushiwa ufunuo. Na kwa hapa imeungana kwa kubainisha sharia hizo zilizotufikia kwa njia ya Utume.

⁕ ⁕ ⁕

## KUSUDIO LA TATU MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII

### [Kuwasilisha Sharia Za Dini Hii Kwa Maelezo Ya Kina]

Kwa aya mia moja na sita [178 – 283]

Baada ya kusimika msingi mkuu, ndipo kunapokuwa na usimamishaji wa jengo. Na baada ya kutulizana juu ya usalama wa nje. Ndipo zamu ya ujenzi wa ndani inapokuja..

Ndio, matengenezo (ujenzi wa imani) ambayo yenyewe ndio roho ya dini na kiini chake yameshatimia. Hivyo na yaanze (maelezo kamili ya sharia). sharia ambayo yenyewe ni mwonekano wa dini na umbo lake.. utata wa wapinzani umeshaondoshwa. Na wakapewa hoja nzito. Na hakuna kilichobaki zaidi ya kuwaangazia njia wasafiri. Na kuiweka wazi mbele yao njia iliyonyooka. Hapo mwanzo uangalizi ulikuwa ukielekezwa katika kubainisha (uhakika wa imani). Na kwa sasa hebu tuelekee katika kukunjua (sharia za Uislamu).

Na wewe umeshaona namna Sura hii ilivyoliandaa badiliko hili. Kwani imeweka kizuizi kinachounganisha ncha za mazungumzo. Mtiririko na muundo wa mazungumzo hayo yanakutana. Na kwa sasa lau kama ungegeuka mgeuko mdogo tu kuelekea upande wako. Ungeona sehemu ndogo kabisa ya kizuizi hiki kwako. Ile aya kusanyifu (aya ya wema). Aya ambayo imejumuisha misingi ya kulingania kwa pande mbili: kinadharia na kiutendaji. Na ungeliona ncha ndogo zaidi baina ya ncha mbili hii kwako. Nayo ni hii ncha ya kiutendaji.

Kwa sasa jua kuwa, upande huu wa kiutendaji. Upande ambao tumeshaugusia hapo kabla, umejumuishwa katika faharasa kwa ufupi. Na katika yafuatayo tutauona, ukiwa umekunjuliwa kibayani na kuelezwa kikamilifu.

Na katika aya mia moja na nusu, utaona kilele kipya cha maana. Umuhimu wake ni kuchora mfumo wa matendo kwa waumini. Na kuwaelezea maelezo kamili ya mambo ya wajibu, ya haramu na ya halali katika pande zote za maisha: kuhusu mambo ya mtu binafsi, mambo ya kifamilia, na mambo ya umma… wakati mwingine kwa bayani iliyoanza

upya[1]. Na wakati mwingine jibu la swali. Wakati mwingine kwa ujumla wake ikishughulikia makumi ya matawi ya hukumu mbali mbali…

Hii ndio hekima ya jumla: katika kuchelewesha kulisimamisha hilo jengo. Imesubiria ili kusimika misingi yake na kuchelewesha matawi hadi pale misingi hiyo ilipokuwa madhubuti. Nyuma yake kutadhihiri hukumu za vipande vipande na siri za kina kwa mwenye kuyaelekea matawi haya na kutazama mshikamano wa matofali yake katika kulijenga jengo hili. Na mshikamano wa pingili zake katika kidani chake. Kisha arejee na kutazama makubaliano yaliyopo baina ya ujumla huo uliopita na haya maelezo kamili yanayoungana nayo.

Katika kuwasilisha hebu na tuchukue ***onesho kuu*** la mlolongo huu mpya: aya ya wema imehitimishwa kama ulivyoona, ***kwa jambo miongoni mwa mambo ya wema.*** Katika muanisho wake wa maneno, umeanishwa kwa muanisho wa kipambanuzi[2]. Kwa hiyo, hilo likawa kiashirio kikubwa sana juu ya jambo hilo... ***Huo ndio utamu wa subira***. Utamu uliogawanywa na aya hiyo kwa sehemu tatu za Subira: Subira katika shida, Subira katika madhara na subira wakati wa matatizo na vita.. Je, wajua kuwa, kwa sasa, nafasi ya maelezo kamili imeshaanza. Na mambo haya na matawi yake matatu ndio yatakayokuwa ya mwanzo kutiliwa umuhimu kuenezwa na sura hii katika mambo hayo. Na kwamba yenyewe itayatangaza matangazo yaliyopangwa kwa mpangilio wa kupanda juu. Hii ni kinyume na mpangilio wa Atwayi: Subira wakati wa matatizo na vita, subira katika madhara na subira katika shida.. Je, wajua kuwa mfumo huu wa kupanda, wenyewe

---

[1] Kuanza upya: kuanzia tena.

[2] Nayo ni sentensi: ﴿**Na wavumiliao katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita** ﴾**.** Al-Baqarah 177. Katika uchambuzi wa maneno ya sentensi za Kiarabu utaona neno wavumiliao limenasibishwa kwa yee (mansuubu ) licha ya kwamba lenyewe limeunganishwa katika sentensi iliyopita ya kurufaishwa kwa wau ﴿**Na watekelezao ahadi zao wanapoahidi…** ﴾. Al-qaasimiyu katika Mahaasini Atta-awili 3/393 amesema: ﴿**wavumiliao** ﴾ limenasibishwa kwa sababu ya Al-ikhtwiswasu yaani mahususi. Na mtiririko wake umebadiliswa kinyume na wa kabla yake ili kuzindua juu ya ubora wa kuvumilia na uzuri wake. Nayo kwa hakika imeunganishwa na yale ya kabla yake. Abuu Ali amesema: zinapotajwa sifa za kusifu au kuponda, katika masuala ya irabu kukatokea kwenda kinyume kwa baadhi ya sifa. Basi hicho kilichoenda kinyume, kimeenda kinyume ili kuone fani fulani. Na fani hiyo huitwa (katian – kukata). Kwa sababu mabadiliko yaliyozoeleka yanajulisha kuongezeka kwa mvuto wa kusikiliza kile kinachotajwa na ziada ya kutilia muhimu jambo lake… Arraaghibu amesema: vile subiri kwa upande fulani hivi ilivyokuwa ndio chanzo cha fadhila. Na kwa upande mwingine, uvumilivu unakusanya fadhila. Kwani hakuna fadhila ila na uvumilivu utakuwa una athari kubwa ndani yake. kwa hiyo imebadilisha irabu yake ili kutoa habari ya makusudio haya.

utafuatwa katika mambo mengine: Kutekeleza ahadi na mikataba, kisha kusimamisha swala na kutoa zaka, na kutoa, kujitoa katika njia ya Allah?.. Pokea bayani kwa maelezo kamili:

### Subira Wakati Wa Matatizo Na Vita

Kwa hapa subira hiyo usiidhanie ni kuvumilia majeraha na maumivu ya vita. Kwani hiyo ni maana hasi ya kujisalimisha. Na wala usiidhanie ni uvumilivu juu ya mateso na kuraruliwa na maadui. Kwani hii ni juhudi chanya ya kiutendaji ya kweli. Lakini marejeo yake ni nguvu ya viungo na mishipa, sio nguvu ya kitabia na adabu **(Mwenye nguvu si kwa kupiga mieleka, lakini mwenye nguvu ni yule anayeimiliki nafsi yake wakati wa kughadhibika)**[1]… Hivi hivi Allah atatuchagulia mifano ya subira iliyo kama hii, na miongoni mwa mizani ya Allah ni mizani yake katika vipimo vya maadili: hilo ni kuidhibiti nafsi wakati wa shida na vita. Kujizuia na kukurupuka kwa kichocheo cha kulipiza kisasi. Na kukemea hilo dhidi ya kuua kwa fujo. Na kusimama kwa hilo katika mpaka wa kushabihiana na kulingana kwa uadilifu [Kisasi 178 – 179].. na ikiwa wito wa kimaana unatupeleka kutoka katika mazungumzo juu ya wauliwa hadi katika mazungumzo kuhusu wale wanaokaribia kufa. Ikinasibisha ukamilisho wa maneno kwa kubainisha yale yanayopaswa kufanyiwa mtu anayekaribia kufa miongoni mwa kutoa usia kwa ndugu wa karibu kwa kuwafanyia wema [Usia 180 – 182].

### Subira Katika Madhara

Na hivyo hivyo, Allah atatuchagulia mlango wa juu kabisa katika milango ya uvumilivu katika madhara: Sio uvumilivu wa kuvumilia magonjwa na maumivu bila kuanishwa. Lakini ni subira ya kuvumilia kiu na njaa kali katika kumtii Allah. [Funga 183 – 187].. na mazungumzo yanaendelea katika funga kujizuia ya muda maalum kuhusu baadhi ya mambo ya halali, hadi funga ya daima ya kujizuia na machukivu na mambo ya haramu. [188].

[1] Hili ni andiko la hadithi iliyopokewa na Bukhari na Muslimu: Imepokewa na Bukhari katika Al-Adabu 6114, na Muslim katika Albirri na Aswilatu na Al-Aadaabu 107, 108. Hadithi zote zimetoka kwa Abuu Huraira.

## Subira Katika Shida Ya Vita

Na kwa muundo huu huu, hapa tutauona uvumilivu katika shida, wenyewe ukiwa sio uvumilivu ule wa dharura, wa kuvumilia ufukara, matatizo ya mali na majanga yatokayo mbinguni na kuikumba mali. Lakini wenyewe ni uvumilivu wa hiari, wa kuzitoa muhanga mali na kuzitumia katika njia ya Allah. Na mfano uliochaguliwa na Quran Takatifu, kwa hapa, ni mfano wenye pande mbili[1]. Ndani yake kuna uvumilivu wakati wa vita na uvumilivu katika shida. Kwani wenyewe unakusanya baina ya jihadi ya nafsi na jihadi ya mali. [Kuhiji katika nyumba ya Allah 189 – 202]. Na kwa hapa, wala usisahau, kutazama maelezo matamu yanayohamisha mazungumzo kutoka katika funga na kuelekea hija. Hilo ni suala la miezi miandamo[2] iliyojaaliwa na Allah kuwa vipimo vya nyakati za funga na hija zote. [189].

Hebu na tukusimamishe hapa hapa, kisimamo kifupi. Ndani yake tunaashiria jambo la ajabu miongoni mwa mambo ya mfumo wa Quran katika mada hii:

Hilo ni kwa kuwa lenyewe pale lilipoanzwa kwa kutajwa hija, halikuunga na hukumu zake kwa kufuatanisha. Bali kulitengenishwa baina ya jina lake na hukumu zake kwa aya sita za hukumu ya jihadi ya nafsi na mali katika kuwapiga vita maadui [190 – 195].. Utenganisho ambao mjinga anaudhania kuwa wenyewe ni kiraka cha ajabu katika nguo ya maana mpya.. Lakini ambaye anajua historia ya Uislamu na sababu za kuteremka Quran. Anajua utukufu wa eneo kilichopo kitenganishi hiki, na kimepatia kuwa

[1] Bali ukipenda, sema: mfano huo una rangi tatu; kwa kuwa mfano wenyewe, katika mapito yake, utaingia uvumilivu wakati wa vita, kupambana na maadui wa Allah. [190 – 195] [Daraazu].

[2]Miezi miandamo: ni wingi wa neno mwezi mwandamo, nao ni mwezi wa angani uliozaliwa kwa siku mbili za mwanzo wa mwezi wa kuhesabu siku.

Na maswala ya miezi miandamo ni maswala yaliyopokewa na Qatada kwa daraja ya mursali. ‘’Walimuuliza Mtume rehema na amani ziwe juu yake juu ya hilo: kwa nini imewekwa miezi hii? Ndipo Allah alipoteremsha katika hilo hiki mnachokisikia: ﴾Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili (ya mambo) ya watu ﴿. Akaifanya kwa ajili ya funga na kufuturu kwa Waislamu, na kwa ajili ya matendo yao ya kiibada na hija zao. Na kwa ajili ya eda za wanawake wao. Na ni sehemu ya dini yao. Katika mambo ambayo Allah anayajua kuhusu kile kinachowafaa viumbe wake. Imepokewa na Attwabariyu katika Tafsiri yake 3067 (ط شاكر) . ina ushahidi wa hadithi yenye daraja ya marufuu na daraja ya mursali katika Duraru Al-Manthuuri cha Assuyuutwiy 1/367, 368. Na Attwabariyu ( 3/553, 554 ط شاكر).

katika eneo hili la kukata[1]. Sio kuambatana kwa muda tu baina ya sharia za Hija na Vita vya Hudaibiya katika mwaka wa sita wa Hijiriya. Lakini ni kwa sababu kutekeleza matendo ya ibada ya hija kwa mwaka huo yalikuwa ni maazimio yasiyotekelezwa, na matumaini yasiyotimia.

Kwani siku hiyo Waislamu walizingirwa wasiifikie hiyo nyumba Tukufu. Na walikusudia kuwapiga maadui wao waliowazuia wasiifikie. Lau kama sio Allah kuwakataza wasianzishe uadui, na kuwaamrisha wasipigane katika Msikiti Mtakatifu ila na yule atayewapiga vita katika msikiti huo. Wakaondoka wakirejea, huku wakiwa wamesalimu amri ya Allah. Wakisubiri kutimia kwa ahadi ya Allah.. Na hivyo msomaji au msikilizaji atoke hapa huku akiwa na kiu ya kutimiza mazungumzo ya Hija kwa sharti la kuyarudia baada ya kitenganishi. Kama vile Waislamu walivyoondoka kipindi kile na kuiacha Makka na huku wao wakiwa na kiu ya kuifika, wakiwa na sharti la kuirudia mwaka unaofuata..

Hivi hivi ndivyo zilivyokuwa aya hizi za kutenganisha zikiwa zenyewe ni ukumbusho wa milele wa matukio hayo ya mwanzo.. na hivi hivi ndivyo Quran Tukufu ilivyokuwa kioo safi, tunatazama kwa kioo hicho picha za hakika za kila rangi. Tunazipata hatua kwa hatua kutokana na maelezo yake ya wazi. Na kwa hatua ya mapito yake na mitindo yake katika kuharakisha ubainifu au kuuchelewesha. Kisha kwa wakati huo huo aya hizi za kutenganisha zimekuwa somo kivitendo juu ya uvumilivu wa mwanafunzi kwa mwalimu wake. Asimuharakishe kwa kumuuliza jambo wakati analiongelea. Lakini angojee kidogo hadi asimuliwe jambo hilo kwa kutajwa katika wakati wake uliowekewa.. Na hivi hivi kungoja kwetu hakujarefuka sana tunaziona hukumu za Hija na Umra zikija baada ya aya hizo za kutenganisha kwa shauku na kiu. Kwa hiyo utashiba na kukata kiu kwa bayani yenye kuponya yenye kutosheleza [197 – 203]. Na kwa kutimia kwa bayani hii, ndipo panapotimia mzunguko wa kwanza wa hukumu. Namaanisha ulazima wa kusubiri katika shida, madhara na wakati wa vita.

**Mapumziko** [204 – 214]

Hekima na upole wa Allah katika kuzilea nafsi zetu katika kutii amri zake vimetutakia, visitupandishe katika mzunguko wa pili punde tu baada ya huu. Lakini iwe baada ya mapumziko ndani yake yana kitu fulani miongoni

[1] Eneo la kukata: ni sehemu ya kutenganisha. Na kupatia eneo la kukata ni fumbo lenye maana ya kupatia.

mwa mawaidha ya jumla. Yanayothibitisha nyoyo katika yale yaliyopita. Na kuzipatia njia ya kuelekea katika yale yaliyobakia.. Na kutokana na uzuri wa eneo la mawaidha haya ya jumla. Ni kwamba yenyewe yameungana na mawaidha maalum ambayo yamemaliziwa na mazungumzo kuhusu Hija. Na ambayo yamewagawanya watu kwa kigezo cha matumaini yao na tamaa zao katika makundi mawili: kundi linatafuta heri za dunia na wala halifikirii jambo la ahera. Na kundi lingine halisahaulishwi na dunia yake kusahau ahera yake [200 – 202].

Yakaja mawaidha ya jumla yakiwagawanya watu makundi mawili kwa kuzingatia kigezo cha yale yaliyomo kwao miongoni mwa tabia za kutoa kipaumbele: kundi lisilojali kujitoa katika njia ya matamanio yake ya maisha ya watu na kuziendeleza nchi. Na kundi lingine likiwa kinyume na hayo, halina dhamana ya kujitoa nafsi yake katika njia ya kumridhisha Allah [204 – 207]. Na hizi aya tukufu zinajumuisha mgawanyo huu kwa kuelekeza nasaha kwa waumini wazitakase nafsi zao na makandokando ya matamanio ya nafsi. Wajisalimishe wazima wazima katika maamrisho ya Allah. Bila ya kutenganisha baina ya baadhi yake kwa zingine. Zikiwatahadharisha na kuteleza na kuacha hilo baada ya kuongozwa katika hilo na kulisimamia. Likiwaeleza kile ambacho huenda kikawapata miongoni mwa shida na madhara katika njia ya kuelekea kusimamisha jambo hilo. Katika hilo, ikiwapigia mfano wa mwenendo wa wale wema waliotangulia miongoni mwa nyumati zilizopita [208 – 214].

Kwa hapa mapumziko yamekamilika kwa mawaidha ya jumla.

Kutakuwa na ***mzunguko unaofuata*** kwa maelezo kamili ya kipengele cha pili miongoni mwa vipengele vya kiutendaji. Vipengele ambavyo vilielezwa kwa ujumla katika ile aya ya wema. Nacho ni: ***Kipengele Cha Pili Cha Kutekeleza Ahadi Na Mikataba***. Na miongoni mwa mikataba hii kipengele cha pili kitachagua mkataba wenye haki zaidi kuzingatiwa na kuchungwa: ***nao ni mkataba wa ndoa na kile kinachozunguka pembezeni mwa muhimili wake miongoni mwa mambo ya familia.*** Je, familia sio sekta ya kwanza ya kufanyia mazoezi ya kuishi vizuri, na kujiepusha na machafu ya ubinafsi na kujipendelea? Kisha, je, si kuwa mambo yanapotengemaa katika jamii hii ndogo, ndipo kidogo kidogo yanatengemaa katika jamii kubwa, kisha katika jamii kubwa zaidi?..

Unaona namna utakavyokuwa uhamaji wa kuelekea katika mzunguko huu wa pili? Je, Quran inatupandisha ghafla katika maelezo kamili ya mambo haya ya nyumbani yenye kuingiliana na matawi mengi? Sivyo hivyo, kwa hakika bayani hii ya kimalezi iliyo takatifu, haitotushambulia na kutupeleka huko kwa mpigo mmoja. Lakini yenyewe itatuonea huruma katika kutufikisha huko kwa ngazi za maswali na majibu. Ya mwanzo wake[1] yanaungana na hukumu zilizopita: Kutoa matumizi na jihadi [215 – 218]. Na za mwisho wake[2] zinaungana na hukumu zinazofuata: Kuchanganyika na mayatima, masharti ya kuoleana, na makatazo ya kuchangamana. [220 – 222].. Na hivi hivi tunafika kwa upole na ulaini. Bila ya kuikatisha[3] wala kuhitaji kitu kabla ya muda wake[4] katika kiini cha mzunguko wa pili [223 – 237] pale tunapokutana katika jambo la maisha ya ndoa na desturi madhubuti, zilizoundwa kwa ncha mbili:

- Ncha yake ya kwanza inashughulikia mambo ya familia wakati zinapoelewana. [223 – 232].
- Na ncha yake ya pili inashughulikia mambo yake katika hali kutoelewana na kutengana. [233 – 237].

Chukua huu mzunguko mpya wa sura hii Tukufu. Na ujue sababu za kuteremka kwake. Na utazame namna kila suala katika hayo lilivyokuwa ufafanuzi wa kisheria juu ya tukio maalum lililotengana na mengine. Kisha rudi uone sentensi katika mtindo wa bayani. Na jaribu kuliangalia kwa mguso wa kutengana au kuhama. Au uhisi katika hilo athari ya kiufundi

---

[1] Na 2 Rudisha macho mara mbili katika mfumo huu wa uhandisi katika bayani… kisha jiulize: je, ilikuwa inawezekana kifungo cha nidhamu yake kushikana lau kama kusingekuwa na matukio ambayo kwa matukio hayo ndipo palipochukuliwa mada ya kuongelea. Au lau baadhi yake yangetokea na mengine yasingetokea. Au yote yangetokea na kwa hiyo kaumu, kusingekuwa na moyo wa kuuliza juu ya hukumu zake…? Kwa hiyo, Qudra au uwezo wa Allah umekuwa ukienda katika mwendelezo wa mfumo huu. Qudra ikachochea mada ya matukio yake, na kuamsha haja za nafsi za kutaka ubainifu wake… na hakuna kilichobakia ila useme pamoja naye: Nimeamini hakika yule ambaye mkononi mwake kuna utendaji wote wa nyakati, yeye ndiye ambaye mkononi mwake imeteremka hii Quran… Zinduka uumbaji wote ni wake na amri zote ni zake. Ametakasika Allah Mola wa viumbe wote. [Daraazu].

[2] Maelezo ni sawa na ya namba 1 hapa juu.

[3] Kukatisha: ni muongeaji kukatisha maongezi anayoyaongea, kisha kuingia katika maneno mengine bila ya maneno ya pili kuwa na uhusiano na yale ya kwanza. Na bila ya maandalizi na kujiandaa baina ya maneno ya pili na ya kwanza. Na kukatisha ni kukatisha kauli ya mtu.

[4] Kuhitaji haja bila kufikia muda wake. Au katika muda usiowekewa haja hiyo. Au kuharakisha jambo kabla ya muda wake.

iliyogandana. Au kulazimisha kuungana… Na tangu sasa, jua kuwa wewe utajaribu bure. Kwa hakika wewe hutopata mbele yako ila kipande kimoja kinachoshughulikia mshipa mmoja. Na ndani yake kunapita maji ya aina moja. Licha ya kwamba chenyewe kimejumuisha madini mbali mbali..

Tafakari vizuri mwanzo wa kila kitu katika mstari wa mwendo wa maana:

Tazama namna mazungumzo yalivyoanza kwa kusimika msingi. Na hivyo, ni kwa kuripoti haki ya maisha na kuchangamana katika ndoa. [23]. Kisha tazama namna ilivyofuatishwa na makatazo ya kuingiza viapo katika mambo kama haya ya haki yenye kutukuzwa. Ni sawa kuapa ili kuzuia kumfanyia wema anayestahiki kufanyiwa. Au ili kukata yale aliyoyaamrisha Allah yaungwe. [224 – 225]. Na namna ilivyofuatishia kwa hukumu ya tawi miongoni mwa matawi ya msingi huu wenye kuungana kwa mahusiano ya ndoa. Nayo ni hukumu ya mwenye kuapa ajizuie asilale na mkewe. [226 – 227]. Na kwa kutokea hapa namna ilivyounga na hukumu za talaka miongoni mwa haki na wajibu. [228..].

Na kama huu mtiririko wa kimaana, na huku kueleza hatua kwa hatua kwa mantiki, katika mambo yaliyokuwa yametengana, matukio yaliyapeleka mambo hayo kwa kuchechemea kukubwa, kama yatakupendeza, njoo nami niuweke mkono wako katika kipande hiki kwa herufi moja. Katika hilo upapase upeo wa umadhubuti katika kuunganisha hivi vilivyotengana. Hadi vikawa jambo moja lenye mfumo mmoja:

Hiyo ndio nukta ya kuhama kutoka katika maelezo ya ufafanuzi wa sheria ya viapo kwenda katika maelezo ya ufafanuzi wa sheria ya talaka: ﴿**Na wakiazimia kuwaacha (basi); Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kujua. Na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka tahara tatu…** ﴾ [227 – 228]. Hivi huoni namna huu mtindo ulivyoongozwa katika hukumu ya viapo kwa namna maalum. Katika hilo, msomaji ananyanyuliwa angani ameganda huku akihadharisha juu ya uwezekano wa utengano. Na pale baada yake, yalipokuja mazungumzo yanayohusu hukumu za kutengana hazikuwa ngeni.

Bali zimepata nafasi yake ikiwa imeandaliwa kwa ajili yake hapo kabla. Kana kwamba hatima ya hukumu ya viapo ilikuwa kama vile kamba iliyofunguka. Ikisubiria kamba nyingine iungane nayo. Na pale ilipokuja fat`wa (maelezo ya ufafanuzi wa kisharia) ya talaka katika nyakati hizo. Basi

fat`wa hiyo ndio ikawa hiyo kamba inayongojwa. Na hilo si kitu kingine ila zimekutana kamba mbili hadi zikakumbatiana na kutokana na kamba mbili hizo kukapatikana mzunguko wenye ombwe usiojulikana ncha zake zi wapi. Na hivi hivi hayo mazungumzo mawili yakawa ni zungumzo moja.

Inashangaza, hivi ni nani aliyemfundisha Muhammad – lau kama Quran ingekuwa inatoka kwake – kwamba yeye ipo siku moja atakuja kuulizwa kuhusu hayo maelezo kamili na ya kina ya hukumu za talaka? Na ni nani aliyemfundisha kuwa yeye atalipatia jawabu hili. Na kwamba hilo jawabu litawekwa katika mafungamano na hukumu za viapo. Na kwamba yeye, ili asimamishe mafungamano yote anatakiwa atiririshe hukumu ya viapo. Hukumu ambayo imetokewa na kuulizwa juu ya ufafanuzi wake sasa hivi. Kwa namna ambayo inafanya upande wake wa mwisho katika pande mbili hizo kuwa ndio upande wa karibu zaidi na mazungumzo juu ya talaka. Talaka ambayo itakuja kuulizwa baada ya muda kidogo. Ili umbo hilo liungane na umbo lake pale litakapokuja wakati wa bayani yake?.. Ni mbali mno kwa elimu ya kibinaadamu kuongelea katika upeo huu wa juu mno. Kwa hakika hilo ni jambo la Mjuzi wa yaliyofichikana na yanayoonekana. Ambaye amekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza…

Na sura inaendelea katika huu mtindo mpya, ikieleza kwa ukamilifu athari za talaka na vile vyote vinavyofuatia baada yake: Eda, kurudiana, kujivua katika ndoa, kunyonyesha, kutaka kunyonyoshewa, uchumba, mahari, kitoka unyumba… mpaka utimilifu wa mzunguko huu wa pili. [237].

Na huko kunaanza ***mzunguko wa tatu*** ﴿**Angalieni sana sala (zote kuzisali, khasa jamaa) na (khasa) ile sala ya kati na kati…** ﴾ [238 – 274].

Hebu tutazame: Namna ulivyotimia muhamo baina ya hii mizunguko miwili?

Kwa hakika sisi kwa kiasi tulichokiona cha kusubiri na kungoja, kupumzika na kuvuta pumzi baina ya mzunguko wa kwanza na wa pili. Tutaona kinyume cha hivyo baina ya mzunguko wa pili na wa tatu. Kuna muhamo unaoshabihiana na mnyakuo, bali kitu cha ghafla. Huenda mtazamaji akakidhania kuwa ni kukatisha mazungumzo na kuingia katika mazungumzo mengine bila kuwa na mahusiano. Na kuhama huko si kukatisha maneno, isipokuwa kwa hukumu ya mtazamo wa juu juu.. Ama yule aliyefuatilia mwendo wa msafara wa maana tangu mwanzo wake, na akakata pamoja nasi theluthi mbili za njia hii ambayo imechorwa na aya ya

wema: miongoni mwa kutimiza ahadi, kuwa na subira katika shida, madhara na wakati wa vita. Kwa hakika hakuna shaka kuwa mtu huyo atakuwa pamoja nasi katika theluthi iliyobaki: Kusimamisha swala, kutoa zaka, na kutoa mali kwa kupenda katika njia ya Allah. Na ataona kuwa huu mzunguko wa tatu umekuja hapa kwa nafasi yake na katika eneo lake lililokadiriwa. Kulingana na utaratibu wake katika ile aya inayokusanya.

Msemaji atasema: Ndio, kwa hakika imekuja katika eneo lake na mpangilio wake. Lakini muhamo wa kwenda katika mzunguko huo umetimizwa bila ya kuwa na maandalizi ya kinafsi (kisaikolojia), wala maandalizi ya kibayani.

Tunasema: Haya maandalizi na utangulizi vilikuwa katika aya tukufu iliyomalizia mzunguko uliopita**: ﴿Na kuachiana ndiyo kunakomkurubisha mtu sana na kumcha Mungu. Wala msisahau kufanyiana ihsani baina yenu; hakika Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyafanya ﴾.** [237]. Aya hii kama utaitafakari, ni kivuko cha dhahabu kilichowekwa katika wakati kinapohitajika baada ya kurefusha mazungumzo katika kueleza kikamilifu haki na wajibu wa nyumbani. Kivuko kilicholetwa kituchukue kutoka katika kelele za kuhesabiana na kugombana, na kutupeleka katika utulivu wa kusameheana na kukirimiana.

Kwa hiyo kivuko hiki kikawa ndio ngazi ya kati na kati iliyotupandisha mpaka anga za juu. Kukiandaa kutupandisha katika yafuatayo hadi katika anga za juu.. Hivi huyasikii maneno haya: **﴿Wala msisahau kufanyiana ihsani baina yenu ﴾.** Msisahau .. kufanyiana ihsani … baina yenu. Kwa hakika kila herufi katika maneno haya inaita kuwa yenyewe ni maneno ya mpenzi mwenye kuaga. Alikuwa amekaa baina yetu kwa muda fulani. Ili apambanue katika mambo yetu. Kisha kwa sasa ameanza kukunja kurasa za hukumu zake. Ili atubadilishie mambo hayo na kutupatia lingine ambalo ni muhimu sana kuliko hiyo ya kwanza. Akatuambia, huku akizikunja: Acheni kugombana katika mambo haya madogo madogo, yasawazisheni miongoni mwenu kwa kutumia kanuni ya wema na kufanyiana ihsani.

Kanuni ambayo yenyewe ndio bora zaidi kuliko kanuni ya haki na uadilifu. Na geuzeni macho yenu pamoja nami na kuyaelekeza katika mambo makubwa na ya kiujumla. Mambo ambayo yanastahiki kuazimiwa na kukusudiwa. Na yanayofaa sana kushughulikiwa na akili pamoja na moyo… Ndio, ndio. Mazungumzo haya yanayohusu haki za mke na mtoto

yashakutosheni. Na sasa sikilizeni mazungumzo yanayohusu haki za Allah na nchi[1]:

---

[1] Hakuna shaka kuwa mtunzi – Allah amrehemu – anakusudia haki ya nchi kwa ufahamu wake wa Kiislamu sahihi. Nao si mwingine ila ni kuipenda nchi ya Kiislamu na wajibu wa kuilinda na kuwanasihi wananchi wake. Kile kilicho cha haki ni kuwa nchi ya Muislamu ni itikadi yake.. kwa hiyo kila sehemu kunakopandishwa bandera ya Uislamu hapo ndipo nchi ya Muislamu.

Lakini ufahamu huu mzuri wenye uzani umepotea kwa watu wengi miongoni mwa wale ambao hawajaongoka na mwongozo wa Uislamu. Na kwa wao kuipenda nchi kukawa ni itikadi mpya inayowakilisha kujitoa katika kuipenda nchi, kuutukuza udongo wake, uzalendo wa nchi, na kukipenda kitu kwa kuwa cha nchi hiyo, na kukichukia kwa ajili yake, ubaguzi kwa ajili yake, na kukitoa kitu kingine chochote chenye kusababisha kutengana miongoni mwa dini, utaifa, mifumo ya kisiasa endapo itapingana na umoja wa ardhi ya nchi. Kwa mfano kama itikadi za kiimani au misingi ya kitabia au mifumo ya kitabia itakuwa ndio sababu za kutengana… basi kwa wao wanapaswa kuacha yote haya yaliyotangulia miongoni mwa itikadi, misingi na mengineyo ili muungano wa nchi uwe safi bila ya vipingamizi na sababu za kufarakiana.

Lau kama mtu mwadilifu atautafakari vizuri wito huu wa uzalendo, ataona kuwa ndani yake umekusanya makabila mbali mbali yanayogombana au yenye uadui. Na huenda ukakusanya dini na madhehebu yanayoshindana. Na kujifunga na uzalendo tu hakutoshi kusimamisha muungano wa kweli wa daima na wenye ufanisi.. Kwa hakika muungano huo utatengana patakapotokea kukataana kiitikadi au kusigana kwa mifumo ya kisiasa au kimaslahi au kikabila au kiutaifa… Na haya ndio tunayoyaona katika uhalisia na katika habari za kila siku zinazotuzunguka. Na haiwezekani kwa watu wajitoe akili zao, fikra zao na ufahamu wao maishani, na itikadi zao kuhusu chanzo cha maisha, mambo ya wajibu na marejeo. Na waache haja zao za misingi na njia za mienendo ya kitabia. Eti wawafikiane katika njia moja (utaifa) na waepukane na matamanio yao, mapenzi yao na maslahi yao kisha eti wauweke mbele uzalendo wa kitaifa dhidi ya viunganishi vyote hivi… Hili kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine kuna ugumu wa kuainisha nchi na kuchora mipaka yake kwa picha thabiti.. kwani kile ambacho leo hii ni cha nchi jana hakikuwa hivyo... Na hiyo nchi siku zote ipo chini ya mabadiliko na kugeuka kwa sababu ya kubadilika kwa nguvu na matukio ya kisiasa na kijeshi, bali hata kwa mabadiliko kihisia na kisaikolojia.

Na kwa masikitiko makubwa, wito huu wa utaifa kwa maana yake hii ya batili umeshaleta matunda yake machungu. Katika utamaduni wa watu pekee na wa watu wote kumedhihiri athari nyingi na picha tofauti tofauti. Na athari ya hatari zaidi, bila ya shaka, ni nchi kuigeuza mungu anayeabudiwa pasi na Allah..

Hebu isikilize kauli ya Shauqiy (Katika Kuipenda Misri):

*Lau kama ningeitwa, basi ungekuwa dini yangu*
*kwayo nakabiliana na hatima inayojibiwa*
*Nakuelekezea wewe kabla ya kaaba, uso wangu*
*pindi nitakaposhindwa ni shahada na kutubia*

[Mielekeo ya kizalendo: 2 / 145]

Au pale anaposema:

*Uso wa kinana (Misri) sio wa kumkasirisha Mola wenu*
*mkiufanya kama uso wake unaoabudiwa*
*Elekezeni kwake nyuso zenu katika masomo yenu*

*na mtakapomaliza iabuduni tahajudi*

[Mielekeo ya kizalendo: 1 / 84]

Kisha mtazame Mustafa Kaamili akishangilia:

Nchi yangu! .. Nchi yangu!.. Ni yako wewe tu mapenzi yangu yote na moyo wangu wote… Ni wako wewe tu maisha yangu na uwepo wangu.. Ni yako wewe tu damu yangu na nafsi yangu.. Ni yako wewe tu akili yangu na ulimi wangu.. Ni zako wewe tu akili zangu na moyo wangu... kwani wewe, wewe ndio maisha, na hakuna maisha ila kwako, ewe Misri.

Kisha nyamaza umsikilize Muharram anaita:

*Kama watauliza, ni nini kuipenda Misri? Kwa hakika*
*Damu yangu, moyo wangu, mbavu zangu na kifua*
*Misri ndio maisha na kifo, bughudha na utajiri*
*Kwa wanawe, na ufakiri, na amani na kihoro*
*Hiyo ni heshima itembeayo, hiyo ni chuki na radhi*
*Hiyo ni dini na dunia, hiyo ni watu na zama*

[Mielekeo ya kizalendo: 1 / 89]

Ama yale yanayosikika usiku na mchana katika vyombo vya habari, kwa mfano: Tunaishi kwa ajili ya Misri na tunakufa kwa ajili ya Misri… Au: Ewe jina tamu zaidi katika uwepo.... Na yasiyokuwa haya miongoni mwa upuuzi na upumbavu ni mengi na hayadhibitiki kwa kuyahesabu… Na kwa hakika sio Misri tu! Isipokuwa Misri ni mfano wa kile kinachotokea katika ulimwengu wote wa Kiislamu. Hebu niambie, nakuapia kwa Mola wako, Kama hili halikuwa ndilo kujitwalia nchi kuwa ndio mungu anayeabudiwa pasi na Allah … Je, hili linaweza kuwa nini lingine?

Na kwa uadilifu, kwa hakika hisia za kuipenda nchi ni hisia za kibinadamu kwa ujumla, wanadamu wote wanashirikiana katika hisia hizi. Kwa hakika Mtume rehema na amani ziwe juu yake, pale alipotoka kwa ajili ya kuihama Makka amesema: **’’Uzuri wako ulioje! Kwa nchi! Nakupenda sana kwangu mimi. Na lau si watu wangu kunitoa kwako, nisengekaa nchi nyine zaidi yako’’.** Imepokewa na Attirmidhiyu, na Albaani ameipa daraja ya sahihi katika Sahihi Attirmidhiy 3083.

Uislamu hauondoshi msingi wa mafungamano wa kikabila, utaifa na yaliyo kama hayo – kwa hakika Uislamu umehimiza kuunga udugu, kuwahurumia watu wote na kuzilinda nchi za Waislamu … Lakini yote haya kwa sharti la kwamba mahusiano hayo yote yasigongane wala kupingana na itikadi ya Kiislamu, sharia zake, tabia zake na makusudio yake ya kijumla. Ama kama mafungamano haya yanapitikia katika chochote katika haya … Basi mafungamano hayo na yakatwe yote na kubakishwe mafungamano ya Kiislamu kwa nguvu zake na umadhubuti wake.

Sikiliza kauli ya Allah Mtukufu: ﴿**Sema: ‘‘Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizozichuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka** ﴾. At-tawba 24. Hapa aya inabainisha kwa uwazi kabisa na kwa kukata, kwamba Muislamu wa kweli, anapaswa kutanguliza kumpenda Allah na Mtume wake, na kupigana katika njia ya Allah kuliko vingine vyovyote vinavyopendwa. Kuanzia ndugu wa karibu, ukoo, biashara na nchi. Na kwa hakika baba wa Manabii Ibrahimu amani iwe juu yake aliyafanya haya. Kisha Musa amani iwe juu yake, naye aliyafanya. Kisha yalifanywa na Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake pale alipohama kutoka Makka kwenda Madina. Kwa hiyo nchi ya Muislamu ni itikadi yake. Ama ile hadithi maarufu ‘‘Kuipenda nchi ni katika imani’’ Hadithi hiyo haina asili

yeyote, yaani haijapokewa hata kwa mlolongo (sanadi) ya kusingiziwa kutoka kwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake.

Wito wa kupenda nchi kwa maana hii ya batili umedhihiri katika ulimwengu wa Kiislamu katika karne iliyopita, kwa sababu nyingi miongoni mwazo ni:

1- Kuiga wamagharibi kibubusa, waliobadilika na kuifuata fikra ya uwananchi baada ya kuraruliwa na vita vya kidini na kikabila kwa karne nyingi zilizopita. Na kile kilichoambatana na vita hivyo miongoni mwa kuchinjana na kumwaga damu sana.
2- Mshindwa kupenda kumuiga mshindi – kama asemavyo Ibnu Khaliduni – pale wamagharibi walipoishinda dola kubwa ya Kiislamu katika karne iliyopita. Waislamu wengi walidhani kuwa uwananchi ndio sababu ya kuendelea wamagharibi na kwa hiyo, uwananchi ndio utakuwa mwarobaini (dawa) yenye mafanikio kwa maradhi ya umma wa Kiislamu.
3- Kuhadaika kwa watu wengi wenye nia nzuri. Na kudhani kwao kuwa uwananchi ni fursa nzuri ya kuunganisha makundi ya umma yakiwemo Waislamu, Wakristo, Wayahudi, wapinga dini na wengineo, wawe kitu kimoja na kufanya juhudi ya kumwondosha mkoloni wa kimagharibi ili kujihakikishia uhuru.
4- Kuyahamasisha makundi yasiyo ya Kiislamu katika wito huu ya uwananchi. Hayo ni matokeo ya kujihisi kwao kuwa wao ni wanyonge na ugeni katikati ya mzunguko wa Kiislamu wa tabaka la juu. Na kwa kupenda kwao kuuyeyusha Uislamu katika nafsi za wana wa Kiislamu mpaka utu wa Kiislamu ufutike.
5- Misaada ya kimagharibi kwa huu ubaguzi wa kiuwananchi katika nchi za Kiislamu na kuunga mkono kwao kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia zisizo za moja kwa moja, miongoni mwazo ni:
    - Kuhamasisha tafiti za athari na kuanzisha zogo linalotiwa chumvi mno la kufufua ubaguzi wa mababu wa kale waliokuwa wapagani, na kusimika uzalendo kwa hao mababu. Kwa hiyo wamisri watajibagua kwa mafirauni, na wairaki kwa wababeli, washamu kwa wafiniki, na waturuki kwa koo zao za kipagani na hivi hivi udugu wa Kiislamu unaparaganyika na nafasi yake inakaliwa na mfarakano na ubaguzi. Na uma mmoja unakuwa na vijinchi mia moja … vijikundi vilivyopotea havina manufaa ila kwa wanaovila.
    - Kurudia kuandika historia: Wanaitukuza historia ya kipagani ya kale, na ufakhari na utukufu wanaujaza kwa mababu. Na kuipakazia historia ya Uislamu kwa kila upungufu. Na kuwachora Waislamu kama watu washenzi, wapenda vita, na wapori pori kwa picha mbaya sana.
    - Kuwaonesha baadhi ya viongozi wa kiuwanachi na kuwang`arisha ili watu wahadaike kwao na umma uwazunguke wao. Na hawaoni shida hata watawakandamiza hilo sio shida kwao. Au hata kuwapeleka uhamishoni ili kuleta athari zitakiwazo ikiwemo umma kushikamana na viongozi hao.

Kinachoonekana ni kuwa ubaguzi wa kiuwananchi mwanzoni mwake ulikuwa ni ubaguzi wa kuipenda nchi yote ya Kiislamu. Kisha ukapungua na kuwa nchi kubwa ya Kiarabu wakati wa utawala wa Ottoman. Kisha hatimaye ukaishia katika uwananchi wa vinchi finyu kwa mipaka ilichorwa na nchi za magharibi kwa eneo la Waislamu. Na mipaka hii inaendelea kubana kidogo kidogo. Tazama Lebanoni, Sudani. Iraki na nchi nyingine. Na hili ni miongoni mwa yale yasiyofichikana kwa yeyote yule.

Na matokeo ya mwisho ya wito huu ni yale tunayoyaona mbele yetu miongoni mwa kufarakiana – kudhalilika – kunyongea – uadui mkubwa baina ya nchi za Kiislamu. Mkabala wake ni amani, mshikamano uliopo baina yake na maadui zake wa kihistoria … Na hakuna mwenye nguvu wala ujanja ila Allah tu.

**Angalieni Sana Sala … Toeni katika njia ya Allah … Piganeni jihadi katika njia ya Allah …** (Na baada ya hayo). Je, mazungumzo ya swala kwa hapa yanachukuliwa kuwa ni kusudio asilia lililohuru au ni sehemu miongoni mwa kusudio lingine.

Ili tujibu vizuri swali hili. Ni vizuri turejeshe jicho mara nyingine. Ili tuone jumla ya mambo ambayo yamekusanywa katika aya ya wema. Na ambayo yameelezwa katika aya zilizo baada yake mpaka karibu na mwisho wa hii sura. Na ili tulinganishe baina ya hadhi zao za kupewa uangalizi wa Utajo Mtakatifu. Je, tunaona nini?

Tunaona kuashiriwa kwa fadhila mbili za kutoa na jihadi katika njia ya Allah. Hazitoacha kuendelea kurudiwa na kusomwa mwanzoni mwa mazungumzo na vipande vyake, kwa ujumla na kwa maelezo kamili. Kusomwa kunakotangaza kuwa yenyewe ndio makusudio muhimu zaidi, na ndilo lengo kuu la sharia katika sura hii.. Na lau kama sisi – katika mwangaza wa mtindo huu – tunapigiwa mfano wa mazingira yale na matukio yake, na tunapigiwa mfano wa kaumu inayosomewa sharia za sura hii na hukumu zake. Inatupigia mfano wa kambi imara ya jihadi yenye pande mbili, ya

---

Na yote haya, kwa hakika ni hila za hatua kwa hatua ili kuwachuna watu na kuwavua Uislamu wao, tabia zao na njia zao. Pale mtu atapovuliwa uzalendo wake kwa dini yake na akafungamana na nchi yake tu, hapo mafungamano ya kiimani na kijamii yanatawanyika… Kwa hiyo kusudio la mwisho kabisa la wito huu wa kiuwananchi katika nchi za Kiislamu ni: Kujitwalia msingi mwingine usiokuwa wa Kiislamu kuwa ndio mhimili wa maisha na injini ya hisia zote.

Na hakika ya uhamasishaji wa magharibi kwa harakati za uwananchi katika nchi za Kiislamu hautokani na mapenzi yao au huruma zao kwa harakati hizi. Bali unatokana na hofu yao juu ya mbadala mwingine unaotishia umagharibi. Zinduka, mbadala wenyewe ni Umoja wa Kiislamu na mafungamano ya hizi nchi za Kiislamu kuwa pamoja katika jengo moja kama nchi moja duniani. Inayotawala njia kuu za mawasiliano ya dunia. Na inakaribia kumiliki peke yake utajiri wa mafuta – na hayo mafuta ndio mishipa ya damu ya maisha ya sasa - nchi tajiri kwa kilimo chake, vyanzo vyake, malighafi zake na majengo yake. Na hii ni siasa ya ukoloni inayolenga kukata mizizi ya muungano baina ya nchi za Kiislamu hadi izimalize moja baada ya nyingine… Na wito huu unafupishwa na msingi mashuhuri wa Uingereza (wagawe uwatawale).

Na miongoni mwa tofauti za kushangaza – kwa mwenye kufahamu na kutafakari – ni kuwa, wakati ambapo wamagharibi wanahamasisha ubaguzi huu wa kiuananchi katika kila nchi miongoni mwa nchi za Waislamu zinazoshirikiana dini, historia, lugha na ustaarabu. Utawaona hao hao wamagharibi wenyewe wakiuzika ubaguzi huu wa kiuwananchi huko Ulaya kwenyewe… Tazama Soko la Pamoja la Ulaya, na kubadilika kwake kuwa Umoja wa Ulaya, kuunganisha kanuni zake, biashara zake na uchumi wake. Kuna bunge la pamoja la Ulaya. Kuna mkutano wa Kimataifa wa nchi zenye viwanda vikubwa .. Na kinyume chake .. Yote haya yanatokea licha ya tofauti za watu wa Ulaya kwa lugha, dini, historia, asili zao na utaifa .. lakini ni nani anayejali na nani anayeamka!!

kimali na kimwili. Na inatupigia mfano wa kuwa kiongozi wa kambi hii yu macho anatazama. Hapitwi na chohote miongoni mwa mambo ya majeshi yake, ya kimahususi na kiujumla. Haachi kuwapa amri zake na miongozo yake katika hayo mambo tofauti tofauti. Kila anapomaliza kuwafafanulia juu ya kero zao zinazowatokea kwa muda, anarejea kuwazungumzisha kuhusu mapito yake yaliyozoeleka. Yanayohusu mambo ya majukumu yao makuu ..

Hili bango la kijeshi liweke mbele ya macho yako… Kwako hakutokuwa na ajabu yoyote kuona mazungumzo ya jambo la jihadi yakitokea sasa hivi baada ya mambo hayo. Hilo ni kwa kuwa busati la kijeshi lilikuwa limekunjuliwa muda wote. Na kwamba, siku zote mtangazaji wake alikuwa kasimama tayari. Na pale utajo wake utakaporejea baada ya kuondoka kwa yale ya pembezoni mwake yanayoshughulisha kwa muda. Kwa hakika lenyewe linakuja katika asili yake na sifa yake. Kwa hiyo sababu ya kuwepo kwake haitaulizwa …

Tuseme nini?.. Jambo la jihadi!! Je, kwa sasa mazungumzo hayafunguliwi kuhusu swala, eda ya kufiwa na sio jambo la jihadi?

Bali tunasema, nasi tunamaanisha tuyasemayo: kwa hakika kwa sasa mazungumzo yanarudi katika jambo la jihadi. Na kwa hakika kwa hapa mazungumzo yanaelekezwa kwa swala na menginieyo kwa kuwaelekeza mujahidina kwa vile wao ni mujahidina. Ili kutatua matatizo yanayochochewa na mazingira ya jihadi yenyewe. Kabla ya kuwaelekezea maamrisho ya wazi juu ya vita ..

Tatizo la kwanza katika matatizo haya ni tatizo la swala katika vita: Je, jihadi haiwi ruhusa ya kuacha wajibu huu wa swala au haiwi ruhusa ya kuicheleweshа?

Kitabu Kitukufu kinatujibu: Hakuna ruhusa ya kuacha swala wala kuichelewesha. Si katika hali ya usalama wala vitani. Si katika amani wala katika hofu: ﴿**Angalieni sana swala** ﴾ [238].

Kwa hakika ruhusa ya wakati wa hofu inahusu kitu kimoja tu: sifa ya swala na namna ya kuiswali: ﴿**Na kama mkiwa na khofu (kusali kidesturi; mmo katika kupigana; basi salini) na hali ya kuwa mnakwenda kwa miguu au mmepanda (wanyama). Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu (salini) kama alivyokufunzeni yale mliyokuwa hamyajui**﴾**.** [239]. Na swala kama tunavyoijua ni nguvu ya

moyoni dhidi ya adui, na ni maandalizi miongoni mwa maandalizi ya ushindi[1]. Hakuna shida ilikuwa ni katika hekima kuongezea wajahidina moyo wa kupambana kwa kutumia swala. Kabla ya kuamrishwa kupigana kwa amri ya wazi.

Na wakati huo huo swala ni kitakaso cha nafsi na tabia mbaya. Swala inaisafisha nafsi na uchafu wa ubahili na kupupia mambo ya dunia[2]. Hakuna shida, vile vile ilikuwa ni katika hekima, kuifanya hiyo swala kuwa nguzo ya usia wa hivi punde. Ambao umetuamrisha kusameheana na kukirimiana katika miamala… Hivi hivi ndivyo yalivyokuwa maweko ya swala yakiwa yana faida zenye pande mbili: dawa na chakula kwa pamoja. Hutazamwa mbele na nyuma kwa pamoja. Bali sema, hakika hilo lina faida za pande tatu; kwa kuwa lenyewe katika mtazamo wake wa kuangalia nyuma haiangalii hiyo aya iliyopita hivi punde peke yake. bali pia inaitazama hiyo aya kama aya inayokusanya mengi. Ili kufafanua yale yaliyotajwa kwa ujumla katika upande huu[3]..

Na kwa uchache, mwanajeshi akiwa vitani unashughulishwa na vitisho viwili: kitisho kwa nafsi yake na kwa wajahidina walio pamoja naye. Dhidi ya hatari ya umauti na kushindwa. Na kitisho kwa watu wake wasipotee na

---

[1] Hivi hivi Allah amesema: ﴿**Na takeni msaada kwa kusubiri na kuswali** ﴾ [Daraazu].

[2] Na hivi hivi Allah amesema katika kumwelezea mwanadamu: ﴿**Na apatapo heri anaizuia isipokuwa wenye kuswali ..** ﴾ [Daraazu].

[3] Ukifahamu uzuri wa upole huu, katika kuhama kutoka katika maana ya zamani kwenda katika maana mpya. Na ukatambua uzuri wa maweko haya ya kiufundi yanayoendana na maana iliyotangulia na ya sasa. Utata wa kuona kuwa mazungumzo yamekatika utakuwa umeshakutoka kwa hapa, na kuhamia katika mazungumzo ya swala .. Isipokuwa sisi, tukiupima mhamo huu na ule mhamo uliopita baina ya ile mizunguko miwili wa mwanzo na wa pili. Je, hatuoni kuwa utangulizi huu ni mfupi, na mabadiliko haya ni ya haraka? Je, hapa nafsi katika kwenda kwake haitambui upande uliojificha wa mabadiliko haya ya haraka, mabadiliko ambayo yanalazimishwa na harakati za kiongozi wake?

Zinduka na fahamu – Allah akuelimishe – haraka hii imekusudiwa. Na ni katika heri kwetu tuhisi huu mtikisiko hafifu wa athari za mabadiliko hayo ya haraka. Kwa hakika hilo lina faida ya kina katika kuzilea nafsi zilizoamini… Kwa hakika kuhama huku kunatupatia picha ya kile kinachopaswa kuwa nacho muumini. Atakaposikia wito wa kutekeleza wajibu wa kiroho huku yeye akiwa ametumbukia katika vita vya maisha. Kana kwamba sisi katika mtindo huu mtakatifu unatuita: hakika mambo yalivyo, si katika hali ya muumini kuhitaji mchakato mkubwa ili kuitukuza roho yake juu ya shughuli za watu na watoto. Na kwa hakika hali yake ni kuwa anatakiwa aing`oe nafsi yake kutoka katika kile ilichokizamia haraka papo kwa papo. Ili aharakishe kuitikia huo wito mtakatifu. Huku akiiambia dunia yake yote: (niache nimwabudu Mola wangu!). Naam, hii ndio hali ya waumini**: ﴿Huinuka mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku ili kumwabudu kwa kuogopa Moto na kutaraji Pepo;… ﴾.** As-Sajdah 16. [Daraazu].

kupata ufukara[1] kama atauawa … Kwa hiyo, huu ubainifu Mtukufu umeendana na kuziondoa moyoni mwake hizi hofu mbili zote: Ama kuhusu watu wake kwa hakika Allah ameshahusia kuhusu mke, kama atafiwa na mumewe, basi aishi mwaka[2] mzima nyumbani kwa mumewe. Na hivyo hivyo, mke atakayepewa talaka naye atapata haki ya kitoka unyumba kisichosahauliwa. Kwa hiyo atulize jicho lake kwa upande huu. [240 – 242].

Ama hofu ya umauti, na ajue kuwa anayeyatafuta mauti huenda akapewa uhai: ﴿**Hukusikia habari za wale waliotoka katika majumba yao (wanawakimbia maadui zao), nao walikuwa maelfu-elfu wakiogopa mauti? Mwenyezi Mungu akawaambia: ''Kufeni''. (Wakafa bure bila sababu yoyote); kisha akawahuisha…** ﴾ [243]. Na ama hofu ya kushindwa, kwa hakika ushindi upo mkononi mwa Allah: ﴿**Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenyezi Mungu yu pamoja na wafanyao subira.''** ﴾**.** [249]. Hiyo ndio suna ya Allah kwa Mitume [246 – 253].

Hivi hivi imeweka mbali hofu zote katika mioyo ya mujahidina. Na baada ya kuziongezea roho zao kwa maandalizi ya uchamungu. Na hivi wamekuwa na maandalizi ya kisaikolojia yaliyokamilika. Ili kupokea maamrisho kutoka juu. Na amri ya wazi ya jihadi katika njia ya Allah kwa mali zao na nafsi zao kwao wao na itoke. [244 – 245][3]. Na ili uwafikie uzoefu

---

[1] Ufukara: umasikini.

[2] Wafasiri katika aya hii wana kauli mbili mashuhuri:

- Ya kwanza, huu ni usia wenye hukumu ya sunna na sio wajibu.
- Ya pili huu ulikuwa wajibu mwanzoni mwa Uislamu kisha ukafutwa na aya iliyopita [234] aya inayowajibisha kusubiria miezi minne na siku kumi na si zaidi … Na kilichowazi ni kuwa kauli zote mbili zimejengwa juu ya kuwa ile aya ya mwaka mmoja, hukumu yake inaenda kwa wake wote … Lakini mtiririko Mtakatifu umetufunulia maana hii mpya: Nayo ni kungoja mwaka kamili ilikuwa ni suala mahususi walilofadhilishwa nalo wake wa wajahidina kinyume na wake wa wale waliokaa nyumbani. Na Allah ndiye mjuzi zaidi [Daraazu].

[3] Na katika mambo ya kupendeza ya kibayani katika mtindo wa Quran kwa hapa ni kuwa matokeo katika hilo yanakaa katika vitangulizi eneo la katikati katika duara. Na sio eneo la nchani katika uzi kama lilivyo jambo la mtindo mashuhuri wa ufundishaji. Je, hulioni jambo hili katika kupigana vita katika njia ya Allah [244]. Kwa hakika jambo hili limezungukwa pande zake zote mbili kwa nguzo zake na vichocheo vyake: kwa ujumla hapo kabla, na kwa maelezo kamili hapo baadaye?.. Jua ya kwamba njia hii nzuri haihusu eneo hili katika Quran. Kwa hakika wewe utapata ushahidi wake umetawanywa katika maeneo mengi ndani ya Kitabu Kitakatifu .. Tafakari kauli ya Mtukufu katika sura ya Al-Maidah: ﴿**Leo nimekukamilishieni dini yenu** ﴾**.** Al-Maida 3. Kwa hakika kukamilika kwa dini ya Kiislamu kunajumuisha mambo ya kimaada na kiroho juu ya kila mfumo unaotosha kumtengeneza mtu, familia, kundi, nchi na ubinadamu kwa ujumla. Na hapo

wa kihistoria, unaozithibitisha nyayo zao wakati wa vita. Na ambao unawaongezea wao matumaini ya ushindi. [246 – 253].

Na jihadi, kama tulivyosema ni jihadi mbili: Jihadi ya nafsi na jihadi ya mali. Na jihadi ya mali sio wakfu kwa mambo ya vita, bali yenyewe ni kutoa katika kila kinachoboresha maisha ya umma na kutia nguvu hali ya dola. Na kuilinda mila ya Kiislamu.

Na kwa hakika jihadi imepata hadhi yake ile ile ya kulinganiwa katika aya fupi [244] kisha katika aya nyingi [246 – 253]. Na jihadi ya mali imechukua baadhi ya hadhi yake katika aya fupi [255]. Na katika uadilifu, na ichukue hadhi yake kamili katika aya nyingi vile vile. Na hivi hivi tunaona wito wa jihadi hiyo unachukua fungu lake kwa sasa. Wakati mwingine ikiwa na tabia ya ukali [254 – 260][1] Na kwa tabia ya ulaini kwa wakati mwingine [261]. Na kwa tabia ya kufundisha taratibu za kutoa kwa maelezo kamili wakati mwingine. [262 – 274].

Kisha mazungumzo yanatiririka kutoka katika kujitoa na kutoa kipaumbele kwa ajili ya wengine, jambo ambalo ni fadhila bora zaidi kijamii na kuelekea katika kueleza uovu wa uroho na kujipendelea. Mambo ambayo yenyewe yapo katika ncha inayokabiliana. Muamala mbaya kabisa wa kibinadamu (namaanisha uovu wa riba. Uovu ambao ndani yake shida za dhaifu zinatumiwa. Na katika hilo mfadhili anapokea thamani ya wema ulioutenda) [275 – 279]. Na muunganiko huu baina ya mawili hayo uliokuwa

---

kabla, dalili zake hazikutajwa ila kidogo. Ama hoja zilizobakia zimetawanywa mara tu baada ya hilo katika utimilifu wa aya ya kumi ya sura iliyotajwa…. Na itazame kauli ya Allah Mtukufu katika surat Annahli: ﴿**Na Mwenyezi Mungu amesema: ‘‘Msifanye waungu wawili; hakika Yeye ni Mola Mmoja tu: basi Niogopeni Mimi tu** ﴾**.** An-Nahl 51. Kwa hakika imekuja ikiwa ni ya kati na kati baina ya ushahidi wa upweke katika kupangilia. Na ushahidi wa upweke katika kuneemesha na ihsani… Na tafakari kauli yake katika sura hiyo hiyo ﴿**Na tumekuteremshia Kitabu hiki kielezacho kila kitu** ﴾**.** An-Nahl 89. Kwa hakika kauli hii imekuja baada ya kubainisha misingi ya itikadi. Na kabla ya kubainisha misingi ya fadhila za kiutendaji. Na katika jumla ya vilivyopita na vilivyopo kunatengenezeka hoja za ukweli wa suala hili. Nayo ni kuwa Kitabu hiki ni bayani ya kila kitu… [Daraazu].

[1] Na katika aya saba hizi kuna maonyo makali kwa mabahili juu ya siku isiyotolewa fidia, wala mwandani hata msaidia mwandani wake. Wala hayatofaa maombezi ya wenye kuombea. Kisha inakazia maana hii kwa kufuta kila aina ya utata unaofungamana na maombezi kwa wale wanaotegemea maombezi. Na kukanusha mamlaka yote na uwezo wa kutenda kwa asiyekuwa Allah. Na kuondosha kila shaka kuhusu ukweli wa siku ya malipo … Na hayo yote, ili kutoa kuwe kwa ajili ya imani na itikadi salama. Sio kujionesha wala kujikurubisha kwa yeyote. Lakini kuwe kwa ajili ya kutaka dhati ya Allah wa peke yake na ni mmoja tu. [Daraazu].

katika bayani ni kudhihirisha upeo wa muunganiko baina ya thamani ya mawili hayo katika hukumu ya dhamiri iliyo hai.

Na baina ya ncha mbili hizi zilizo mbalimbali, Quran inasimamisha mizani ya uadilifu katika mpaka wa kati na kati ukimjaalia mwenye haki kuwa na mamlaka ya kudai mtaji wote bila kupungua chochote ﴿**Msidhulumu wala msidhulumiwe**﴾ 279. Isipokuwa yenyewe inatutahadharisha juu ya ubaya wa kuitumia haki hii mbele ya wenye hali ngumu. Na inatuamrisha tuwafanyie moja ya wema wa aina mbili: Ima tuwasubirie hadi wawe na hali nzuri, na ima tuwasamehe kabisa hilo deni. Na huu ndio ukarimu na ni bora zaidi. ﴿Na kama nyinyi (mnaodai mkazisamehe deni zenu) mkazifanya sadaka, basi ni bora kwenu. Ikiwa mnajua haya (basi fanyeni ﴾. [280 – 2081].

Na kwa vile tabia inayodhihiri katika sharia hii ya Quran imekuwa ni ile tabia ya kutosheka na kusamehe. Huenda hilo likaashiria katika nafsi kitu fulani cha kuzembea katika jambo la mali. Na huenda hilo likapelekea kuchupa mipaka katika kuihifadhi na kuiwekeza. Hivyo zikaja aya mbili za deni na rehani[1]. [282 – 283]. Aya hizi zinatuondolea huu ufahamu mbaya katika nafsi zetu. Na zinawatengenezea waumini kanuni ambayo ndio kanuni makini katika kanuni za kiraia. Katika kuhifadhi haki, kuzidhibiti na kuzithibitisha kwa njia mbali mbali. Kwa ajili ya kuandaa kuzitoa katika njia nzuri zaidi .. Na yule ambaye hajapata njia ya kuweka vithibitisho kwa kithibitisho fulani. Na mbele yake hakujabaki chochote isipokuwa kumuegemeza yule anayemfanyia muamala katika dhima yake na uaminifu wake ﴿**aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake** ﴾ [283].

Na hivi hivi upande wa kiutendaji umehitimishwa katika sura hii kwa kanuni hii bora kabisa na ya kupigiwa mfano. Kanuni ambayo yenyewe ndio msingi wa kila muamala mzuri. Namaanisha kanuni ya ukweli na amana. Allah atujaalie tuwe miongoni mwa watu wa ukweli na uaminifu … aamiin.

❋ ❋ ❋

[1] Na aya ya deni ndio aya ndefu katika Quran [Daraazu].

## KUSUDIO LA NNE MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII

## [**Kutaja Msukumo Na Hisia Ya Kidini Inayochochea Kushikamana Na Sharia Hizo Na Kuzuia Kwenda Kinyume Nazo**].

### Katika aya moja [284]

Katika aya iliyopita, jukumu la hukumu za maelezo kamili limeisha. Katika mpaka ambao Allah alitaka kuubainisha katika sura hii. Na kwa aya hiyo umehitimishwa upande wa pili katika hakika za kidini. Nao ndio upande wake wa kiutendaji. Baada ya kusimika upande wake wa kiitikadi katika aya za [122 na zilizo baada yake].

Na hivi hivi, mpaka sasa bayani imeshashughulikia:

1 – Hakika za imani.

2 – Sharia za Uislamu.

Je, katika jengo la dini kumebakia kitu kilicho juu ya nguzo hizi?

- Naam, kwa hakika kumebakia kilele cha juu kabisa, na pambo lake kubwa ..

Baada ya imani .. na Uislamu .. kumebakia ihsani (wema). Nao ni kama vile ulivyofasiriwa na mwenye ujumbe rehema na amani ziwe juu yake. Ni kumchunga Allah katika kila jambo[1]. Na uuhisi muonekano wake kwako

---

[1] Kutoka kwa Omari bin Al-Khatwab Allah amuwie radhi amesema: **''Siku moja tulipokuwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Ghafla alitutokea mwanaume mmoja mwenye nguo nyeupe sana, nywele nyeusi sana. Haionekani kwake athari ya safari. Na hajulikani na yeyote miongoni mwetu. Akaja hadi akakaa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na kuegemeza magoti yake katika magoti yake. na akaweka viganja vyake katika mapaja yake. Na akasema: Ewe Muhammad! Nieleze kuhusu Uislamu. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Uislamu ni kushuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah. Na usimamishe swala. Na utoe zaka. Na ufunge Ramadhani. Na uhiji Makka kama utaweza kwenda njia hiyo. Akasema: umesema kweli … Akasema nieleze kuhusu imani. Akasema: Umwamini Allah na Malaika wake, na vitabu vyake, na mitume yake, na siku ya mwisho, na uamini qadar (uweza na makadirio) heri zake na shari zake. Akasema: umesema kweli.. Nieleze kuhusu ihsani (wema). Akasema: Kumwabudu Allah kana kwamba wamuona, na kama humuoni yeye anakuona .. ''. Na mwishoni mwa hadithi, Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Hakika yake ni Jibrilu. Amekujieni kukufundisheni dini yenu).**

Imepokewa na Muslim katika mlango wa Imani 1 . Na imepokewa na Bukhari kutoka kwa Abuu Huraira katika mlango wa Imani 50. Na katika mlango wa Attafsiiru 4777.

kwa siri na dhahiri. Na ujiandae kuwa yeye atakuhesabu wewe. Hata katika dhati ya kifua chako. Na ndani ya nafsi yako… Haya ni matakwa makubwa na hayawezi kutekelezwa na kila muumini, wala kila Muislamu. Kwa hakika wanaoogolea pembeni mwa himaya hiyo ni wale watakatifu wa watakatifu miongoni mwa wachamungu … Ni kama vile, kwa utukufu na thamani ya matakwa haya, Allah ameikinga lulu yake adhimu iliyo yatima kwa aya hii ya pekee. Aya ambayo imevikwa taji la sura hii. ﴿**Na kama mkidhihirisha yaliyomo katika nyoyo zenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu atakutakeni hisabu ya (yote) hayo** ﴾**.** [284].

* * *

# HITIMISHO

## [Katika Kutambulisha Wale Ambao Walioitikia Wito Huu Jumuishi Wa Makusudio Hayo. Na Kubainisha Yale Yanayotarajiwa Kwao Kwa Ya Baadaye Na Ya Sasa]

**Katika Aya Mbili** [285 – 286]

Na sasa, bayani imeshashughulikia nguzo zote za dini. Na imeshazizunguka dondoo zake zote: Imani, Uislamu na Ihsani. Hakuna kilichobaki, baada ya kutimia mazungumzo haya ila kukunja kurasa yake na kutangaza hitimisho lake?

Na je wajua ukurasa wa sura hii ulikunjwa vipi, na hitimisho lake lilitangazwa vipi?

Turudishe kumbukumbu yetu katika aya tano, ambazo sura Al-Baqarah ilifunguliwa nazo. Ili tuone namna utangulizi huo unavyoendana na hitimisho hili. Kisha namna ncha mbili hizi zinavyokumbatiana hivi hivi. Na hatimaye ziungane katika pinde zao na kuwa uzio madhubuti unaoizunguka sura hii. Na kutahamaki yenyewe ni sura ya kweli. Yaani jengo lililoimarika lenye uzio…

Je, mwanzo wa sura haukuwa ahadi ya ukarimu kwa atakayeiamini na kutii amri zake. Kwamba wao ni watu wenye kuongoka na ni watu wenye kufaulu?

Je, kwa sasa, hatungoji kusikilizwa kwa ahadi hii? Hapana, kwa hakika sisi kwa sasa tunaingoja hii sura itusimulie: Je, kuna mtu aliyeiamini, na je, kuna aliyefuata mwongozo wake. Kisha tunaingoja hiyo sura, kama hayo yameshatokea. Itueleze malipo ya mwenye kuisikiliza na kuifuata..

Na hivi hivi ndivyo kitakavyokuwa kipande cha sura hii:

(1) Kufikisha kuhusu kufaulu kwa wito wake: ﴿**Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu, (pia wameamini hayo): wote wamemwamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake; (nao hao Waislamu na Mtume wao husema), ‘‘Hatutofautishi baina ya yeyote katika Mitume wake (wote tunawaamini).’’ Na husema: ‘‘Tumesikia na tumetii. (Tunakuomba) msamaha, Mola wetu! Na marudio ni kwako.’’** ﴾. [285].

(2) Kutekeleza ahadi yake kwa kila nafsi iliyojitolea kwa uwezo wake katika kuufuata wito huu: ﴿**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yo**

**yote ila yaliyo sawa na uweza wake. (Faida ya) yale iliyoyachuma (hiyo nafsi) ni juu yake na hasara ya yale iliyoyachuma ni juu yake pia…** ﴾ [286].

(3) Kufungua mlango wa matumaini kwa vipande vyake viwili, mbele ya hawa walioongoka. Kwa hiyo, wakunjue viganja vyao kwa shangwe: ﴿**Mola wetu! .. Mola wetu! .. Mola wetu! .. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tusaidie juu ya watu makafiri.**﴾ **''** [286].

* * *

Hiyo ndio suratul Al-Baqarah .. Je, umeona umoja wake katika wingi wake: Je, umejua mwelekeo wa mistari yake katika ubao wake? Je, umeona namna matofali yake yalivyoshikamana bila ya udongo unaoyashika. Na mbingu yake imenyanyuka bila ya nguzo inayoiegemea? Je, umeona namna ilivyopangika kuanzia kichwani mwake, kifuani mwake, utumbo wake, na mikono yake. Sisemi ni mtoto wa sanamu mzuri zaidi … Bali ni sura hai nzuri sana. Kila punje katika seli zake, na kila seli katika viungo vyake, na kila kiungo katika upande wake, na kila upande katika mwili wake. Kinatangaza kuwa chenyewe kimechukua nafasi yake iliyogawiwa. Kulingana na mstari wa pamoja uliochorwa. Umechorwa na Mlezi wa nyoyo na mwenye kuzitakasa. Mwenye kuzinawirisha akili na kuziongoza. Mwongoza roho na mchungaji wake ..

Na naapa kwa Allah, lau kama sura hii ingepangwa baada ya kutimia kuteremka kwake, basi kuvikusanya vipande vyake vilivyotawanyika lingekuwa jambo la muujiza. Sasa itakuwaje ikiwa kila kipande katika vipande vyake – kama ilivyo vipande vingine katika sura nyingine – vingekuwa vinawekwa katika nafasi yake punde tu vinapoteremka. Na vingekuwa vinahifadhia nafasi vipande vingine kwa kungojea kufika kwake. Na hivi hivi kila kile ambacho hakijateremka katika vipande hivyo kingekuwa kinajulikana nafasi yake ikiwa na eneo lenye mipaka maalum kabla ya kuteremka? Kisha inakuwaje, wakati yenyewe ishakuwa jambo mahususi miongoni mwa sura zilizoteremka vipande vipande kuwa zenyewe zimeainishwa maeneo ya vipande vyake si kabla ya kuteremka kwake kwa mwaka mmoja au sehemu ya mwaka, bali kwa miaka tisa?

Jamani kwa umri wangu, lau kama kwa hakika Quran, kwa balagha ya maelezo yake, imekuwa muujiza. Na katika utabiri wake wa kweli imekuwa miujiza, na katika uwekaji sharia wake wa milele imekuwa miujiza, na katika

kila ilichokitumia miongoni mwa mambo ya hakika ya kisayansi ya kisaikolojia na kimaumbile ni miujiza na miujiza. Kwa umri wangu, hakika mambo yalivyo, katika mpangilio wa aya za Quran kwa namna hii ni muujiza wa miujiza!

❋ ❋ ❋

**Imetimia sehemu ya kwanza ya kitabu Habari Kubwa cha mtunzi wake, Sheikh Muhammad Abdullah Daraazu Allah amrehemu.**

**Na in shaa Allah, (Allah akipenda) inafuata sehemu ya pili ambayo yenyewe ni miswada inayokamilisha sehemu ya kwanza. Miswada ambayo imepatikana katika ofisi ya huyu sheikh Allah amrehemu.**

**Na mchakato wa kuiandaa ili kichapwe unaendelea kwa matakwa ya Allah na mwafaka wake.**

❋ ❋ ❋

## VYANZO NA REJEA

**Mosi: Quran Tukufu.**

⁕ ⁕ ⁕

**Pili: Tafsiri:**


- **Al-Asaasu Fii Attafsiri: Said Hawiy.**
  Daru ssalaam, chapa ya kwanza 1405 HD – 1985AD.
- **Adhuwaa Albayan Fii Iidhwahi Alquran Bilquran: Muhammad Al-amiinu Asshanqiitwiy.**
  Uchapaji wa Almadaniy – Misri, chapa ya 1386 HD – 1967 AD.
- **Attahariru Wattanwiiru Mina Attafsiiri: Muhammad Twahir bin Aashuur.**
  Daru Attunisiyat Linnashiri – Addaaru Aljamaahiriyah
- **Tafsiru Attwabariy (Jaamiu Albayani An Ta-awili Ayi Alquran): Attwabariy.**
  Maktaba na uchapaji wa Mustafa Al-Baabiy Al-Halabiy – Misri. Chapa ya tatu 1388 HD – 1968AD.
- **Tafsiru Attwabariy (Jaamiu Albayani An Ta-awili Ayi Alquran): Attwabariy.**
  Kuhakikiwa na kutolewa Hadithi zake: Mahmudu na Ahmad Muhammad Shaakir.
  Daru Almaarifa – Misri. Chapa ya pili 1969 AD.
- **Tafsiri Alquran Al-Adhiimi: Ibnu Kathiiri.**
  Uhakiki: Abdul Aziz Ghuneim – Muhammad Ahmad Aashuuri – Muhammad Ibrahim Albannaa.
  Daru Shaabi – Misri.
- **Tafsiri ya Al-Qurtubiy (Aljaamiu Liahkami Alquran): Al-Qurtubiy.**
  Masahihisho: Ahmadu Abdul Aliim Al-barduuniy.
  Daru Ihyaai Atturaathi Al-Arabiy – Beiruti – chapa ya pili.
- **Attafsiru Alkabiiru: Arraaziy.**
  Daru Alkutubu Al-ilimiyah – Beiruti. Chapa ya 1411 HD – 1990 AD.
- **Tafsiru Al-Manaari: Muhammad Rashid Ridhwaa.**
  Daru Almaarifah – Beiruti. Chapa ya pili.
- **Adduraru Almanthuru Fii Attafsiri Bilmathuri: Assuyuutwiyu.**
  Daru Alkutubu Al-ilmiyah – Beiruti. Chapa ya 1411 HD – 1990 AD.

- **Ruhu Almaaniy Watafsiru Assabai Almathaniy: Al-Aluusiyu.**
  Daru Ihyaai Atturathi Al-Arabiy – Beiruti.
- **Zadi Almusiru Fii Ilimu Attafsiri: Ibnu Al-Jawziyu.**
  Almaktab Al-Islamiy. Chapa ya tatu 1404 HD – 1984 AD.
- **Umdatu Attafsiri: Ahmad Muhammad Shaakir.**
  Daru Almaarifi – Misri. Chapa ya 1377 HD – 1957 AD.
- **Fii dhwilaali Alquran: Sayyidu Qutubi.**
  Daru Asshuruqi. Chapa ya Kisheria ya Tisa 1400 HD – 1980 AD.
- **Alkasshafu An Haqaiqi Attanziili: Azzamakhshariyu.**
  Mpangilio na udhibiti: Mustafa Hussein Ahmad.
  Daru Arrayyaani Linnashri – Cairo. Chapa ya tatu 1407 HD – 1987 AD.
- **Mahasinu Atta-awili: Al-Qaasimiyu.**
  Kuzitoa hadith zake na kuzisimamia: Muhammad Fuadi Abdul-Baaqaiy.
  Daru Ihyaai Alkutubi Al-Arabiyah (Issa Al-Baabiyu Al-Halabiyu) – Misri. Chapa ya kwanza 1376 HD – 1957 AD.
- **Mufradatu Alfaadhi Alquran: Ya Arraaghibu Al-Aswifahaaniyu.**
  Imehakikiwa na: Swafawani Adnani Daawudiyu.
  Daru Al-Qalam – Damaskasi. Maa Daru Asshaamiyati – Beiruti. Chapa ya Kwanza 1412 HD – 1992 AD.

**Tatu: Elimu / sayansi ya Quran:**

- **Al-Itiqaanu Fii Uluumi Alquran: Assuyutwiyu.**
  Kuhakikiwa: Muhammad Abu Al-Fadhili Ibrahimu.
  Alhaihatu Almisriya Al-aama Lilkitabi – Misri. Chapa ya 1974 HD.
- **Asbabu Annuzuli: Assuyutwiyu.**
  Daru Ihiyaai Alkutubi Al-arabiyah (Faisal Issa Al-Baabiyu Al-Halabiyu) – Misri. Chapa ya 1986 AD.
- **Asbabu Annuzuli: Al-Waahidiyu.**
  Kuzitoa hadith zake na kuzihakiki: Iswamu bin Abdul Muhsini Al-Humaydani.
  Muasasatu Arrayyaani – Beiruti. Chapa ya Kwanza 1411 HD – 1991 AD.
- **Iijazu Alquran: Al-Baaqilaaniyu.**
  Uhakiki: Bwana Ahmad Swaqaru.
  Daru Almaarifu – Misri. Chapa ya tano.

- **Asswahihu Almusnadu Min Asbabi Annuzuli: cha Muqbilu Bin Haadiy Al-Wadaaiy.**
  Usambazaji: (Almaktabu Assalafiy) Daru Ahlu Sunna – Misri.
- **Fadhailu Alquran: Ibnu Kathiiri.**
  Maktabatu asswahaba – Twantwa.
- **Fadhailu Alquran: Annasaaiyu.**
  Uhakiki: D. Faruqu Hamadah.
  Daru Atthaqafati. Addaru Albaidhwaai – Almagribu. Chapa ya Kwanza 1400 HD – 1980 AD.
- **Annaasikhu Wamansuukhu: Hibatul llahi Bin Salaamah Almuqriy.**
  Uhakiki: Zuhayri Asshaawishu na Muhammad Kanaani.
  Almaktabu Al-islamiy. Chapa ya Kwanza 1404 HD – 1984 AD.


**Nne: Hadithi:**


- **Al-ihsanu Fii Taqribi Swahihi Ibni Hibbaani: Ibnu Balbaani.**
  Kuzihakiki na Kuzitoa hadith zake: Shuaibu Al-Arnautwi.
  Muasasatu Arrisalah – Beiruti. Chapa ya kwanza 1408 HD – 1988 AD.
- **Jaamiu Al-usuli fii Ahadithi Arrasuli: Ibnu Al-Athiri (Abuu Assadati Almubaraku).**
  Uhakiki: Abdul Qadiri Al-Arnautwi.
  Daru Al-malaahi litwabaati Wannashri – Siria. Chapa ya Kwanza 1389 HD – 1969 AD.
- **Sunanu Attirmidhiyu.**
  Uhakiki na Ufafanuzi: Ahmad Muhammad Shaakir. Kisha wengineo wa baada yake.
  Daru Al-Hadithi – Misri.
- **Sunanu Abii Daudi.**
  Uhakiki: Izzatu Ubeid Addaasi ns Adil Assayyid.
  Daru Al-Hadithi – Himswi. Chapa ya Kwanza 1389 HD – 1969.
- **Sunanu Ibnu Maajah.**
  Uhakiki: Muhammad Fuadi Abdul Baaqiy.
  Almaktabat Al-ilmiyati – Beiruti.
- **Sunanu Annasaiy [Al-Mujtabaa] (Maa Sharhi Assuyutwiyu).**
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti.
- **Swahihi Bukhari (Maa Fat-hul Bariy li-Ibni Hajari).**
  Maandalizi: Muhammad Fuad Abdul Baaqiy. Na wengineo.

Almatwibau Salafiyati Wamaktabatihaa – Misri. Chapa ya pili 1401 HD.

- **Sahihi Muslimu.**
  Maandalizi na maelezo: Muhammad Fuadi Abdul Baaqiy.
  Daru Ihyaai Alkutubi Al-Arabiyati (Issa Albabiy Alhalabiy). Chapa ya Kwanza 1374 HD – 1955 AD.
- **Majimau Azzawaaidi Wamanbau Alfawaaidi: Al-Haithamiy.**
  Daru Arrayyaani litturathi – Cairo. Maa Daru Alkitabi Al-Arabiy – Beiruti.
  Chapa ya 1407 HD – 1987 AD.
- **Almustad-raku Alaa Swahihaini: Alhaakimu.**
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti. Chapa ya 1411 HD – 1990 AD.
- **Musnadu Ahmad.**
  Almaktabatu Al-Islamiy. Chapa ya Tano 1405 HD – 1985 AD.
- **Musnadu Ahmad.**
  Uhakiki na uandaaji: Ahmad Muhammad Shaakir.
  Daru Almaarifi – Misri, Chapa ya Tatu 1368 HD – 1949 AD.
- **Mawaaridu Addhwam-aani Ilaa Zawaaidu Ibni Hibbaani: Al-Haythamiy.**
  Uhakiki: Muhammad Abdul Razak Hamza.
  Almatiba-atu Salafiyati wamaktabatihaa – Misri.
- **Muwatwau Maaliki.**
  Uandaaji: Muhammad Fuadi Abdul Baaqiy.
  Daru Ihiyaau Alkutubi Al-Arabiyati (Issa Albaabiy Alhalabiy) – Misri.
- **Vitabu na Usahihishaji wa Albaaniyu – Allah amuhifadhi – na hasa hasa:**
- **Irwaai Alghaliili Fii Takhriiji Ahaadiithi Manaari Assabiili.**
  Almaktabu Al-Islamiy, Chapa ya Pili 1405 HD – 1985 AD.
- **Takhriiji Ahaadiithi Fiqihi Assiira Limuhammad Alghazaaliy.**
  Daru Alkutubi Al-Islamiyati – Cairo. Chapa ya nane 1402 HD – 1982 AD.
- **Assilsilatu Asswahiihatu:**
  Mjeledi wa kwanza na wa pili: Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya nne 1402 HD – 1985 AD.
  Mjeledi wa Tatu: Daru Assalafiy – Kuwait. Chapa ya kwanza 1399 HD – 1979 AD.

Mjeledi wa nne: Almaktabu Al-Islamiyati – Oman. Maa Addaaru Assalafiy – Kuwait. Chapa ya Pili 1404 HD.
Mjeledi wa tano: Daru Almaarifi – Riyadh. Chapa ya Kwanza 1412 HD – 1991 AD.

- **Assilsilatu Adhwaiifu:**
Mjeledi wa kwanza: Almaktabu Al-Islamiyi. Chapa ya Tano 1405 HD – 1985 AD.
Mjeledi wa Pili: Almaktabatu Al-Islamiyati – Jordan. Maa Maktabati Almaarifi – Riyadh. Chapa ya Tatu 1406 HD.
Mjeledi wa Tatu na wa Nne: Makatabatu Almaarifi – Riyadh. Chapa ya Kwanza 1408 HD.
- **Swahihu Al-Jaamiu Asswaghiiri.**
Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya pili 1406 HD – 1986 AD.
- **Swahihu Sunanu Attirmidhiy.**
Maktabu Attarbawiyyati Al-Arabiy Lidiwali Al-khaliiji. Chapa ya kwanza 1408 HD – 1988 AD.
- **Swahihu Sunanu Abii Daudi.**
Maktabu Attarbawiyyati Al-Arabiy Lidiwali Al-khaliiji. Chapa ya kwanza 1409 HD – 1989 AD.
- **Swahihu Sunanu Ibnu Maajah.**
Maktabu Attarbawiyyati Al-Arabiy Lidiwali Al-khaliiji. Chapa ya kwanza 1407 HD – 1986 AD.
- **Swahihu Sunanu Annasaaiy.**
Maktabu Attarbawiyyati Al-Arabiy Lidiwali Al-khaliiji. Chapa ya kwanza 1409 HD – 1989 AD.
- **Dhwaiifu Al-Jaamiu Asswaghiiri.**
Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya Pili 1408 HD – 1988 AD.
- **Dhwaiifu Sunanu Attirmidhiy.**
Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya Pili 1411 HD – 1991 AD.
- **Dhwaiifu Sunanu Ibnu Maajah.**
Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya Kwanza 1408 HD – 1988 AD.

❋ ❋ ❋

**Tano: Vitabu Vya Akida - Itikadi.**

- **Inil Hukumu Illaa Lillah: Muhammad Shaakir As-Sharifu.**
Daru Alwatwani – Riyadh. Chapa ya Kwanza 1413 HD.

- **Al-iimanu: Ibnu Taimiya.**
  Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya Tatu 1399 HD – 1979 AD.
- **Tahdhiiri Ahlil Iimaani Anil Hukumi Bighairi Maa An`zala Arrahmaanu: Ismaili Bin Ibrahimu Al-Hatwibu Al-As-ardiyu.**
  Maktabatu Tau`iyati Al-Islamiyati – Misri.
- **Tahkiimu Alqawaaniini: Muhammad Bin Ibrahimu Al-Sheikh.**
- **Sharhu Al-Akida Attwahawiyati: Ibnu Abii Al-Izzi Al-Hanafiy.**
  Almaktabu Al-Islamiy. Chapa ya nane 1404 HD – 1984 AD.
- **Asshariatu Al-Ilaahiyati laa Alqawaaniina Aljaahiliyati: Omar Suleiman Al-Ashqar.**
  Daru Annafaaisi – Jordan. Maa Maktabati Alfallaahi – Kuwait. Chapa ya Tatu 1412 HD – 1991 AD.
- **Fatihu Almajiidi sharhu Kitaabu Attauhidi: Abdul Rahman Bin Hassan Aalu As-Shaikh.**
  Muassasatu Qurtwubati – Misri.
- **Fadh`lu Alghinaa Alhamiidi: Yaasiru Barahaamiy.**
  Maktabatu Al-Iimani – Alexandria. Chapa ya Kwanza 1990 HD.
- **Kalimatu Haqi: Omar Abdul Rahman.**
  Daru Al-Iitwiswam – Misri.
- **Wujuubu Tahkiimi Sharia Allah wanabdhi maa khaalafau: Abdul Aziz Bin Baazi.**
  Riaasatu Idaaraati Albuhuuthi Al-Ilmiyati Wal-Iftaai Wadda`await Wal0Irshaadi – Riyadh.
  Chapa ya nne 1401 HD.

* * *

**Sita: Sira Na Historia Na Maelezo Ya Watu.**

- **Al-Iswaba Fii Tamiyiizi Asswahabati: Ibnu Hajar.**
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti.
- **Albidaayatu Wannihaayatu: Ibnu Kathiiri.**
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti. Chapa ya Kwanza 1405 HD – 1985 AD.
- **Taarikhu Attwabariy.**
  Uhakiki: Muhammad Abu Alfadhili Ibrahim.
  Daru Almaarifi – Misri. Chapa ya nne.
- **Abu Haamid Al-Ghazaliy Wattaswawufu: cha Abdul Rahman Damashqiyah.**
  Daru Twiibati – Riyaadh. Chapa ya kwanza 1406 HD – 1966 AD.

- **Alkhaswaaiswu Alkubraa: Assuyutwiy.**
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti. 1405 HD – 1985 AD.
- **Arrahiiqu Almakhtuumu: Swafiyu Rahman Almubar Kafuuriy.**
  Daru Walid Alkaabah. Chapa ya Kwanza 1400 HD – 1980 AD.
- **Arraudhul Unfu: Assuhailiy.**
  Uhakika: Twaha Abdul Raufu Saad.
  Maktabatu Alkulliyaati Al-Azhariyati. 1402 HD – 1973 AD.
- **Sairu A-alaamu Nubalaau: Addhahabiyu.**
  Uhakiki: Shuaibu Al-Arnawutwi, na wenginewe.
  Muassasatu Arrisaalah, Chapa ya nane 1412 HD – 1992 AD.
- **Assiiratu Annabawiyati: Ibnu Hishamu.**
  Uhakiki: Omar Abdi Salaam Tadmiriy.
  Daru Arrayyaani litturathi – Misri. Chapa ya Kwanza 1408 HD – 1987 AD.
- **Manaaqibu Asshaafi-iyu: Albaiyhaqiyu.**
  Uhakiki: Assayidu Ahmad Swaqar.
  Daru Atturathi –Alqahira. Chapa ya Mwanzo 1391 HD – 1971 AD.

⁕ ⁕ ⁕

**Ya Saba: Lugha, Fasihi Na Makamusi:**

- **Asaasu Albalaghati: Azzamakhshariy.**
  Daru Matwaabiu Assha`abi. 1961 AD.
- **Diiwaanu Albuuswiriyi.**
  Uhakiki: Muhammad Sayyid Kaylaaniy.
  Maktabatu Mustafaa Albaabiy Alhalabiy Wa`aulaadihi. Chapa ya pili 1393 HD – 1973 AD.
- **Twabaqaatu Fuhuuli Asshuaraai: Ibnu Salaamu.**
  Uhakiki na sherehe: Mahmudu Muhammad Shaakir.
  Matwiba`atu Almadaniyi – Misri.
- **Fiqihu Llughati: Attha`aalabiy.**
  Uhakiki: Mustafa Assiqaa – Ibrahimu Al-Abyaariy – Abdul Hafiidhi Shalabiy.
  Imenakiliwa kutoka katika chapa ya 1972 AD. Bila ya kutajwa msambazaji.
- **Alqaamusi Almuhitwu: Alfairuziaabadiy.**
  Uhakiki: Makataba ya uhakiki wa urithi katika taasisi ya Arrisaalah.
  Muassasatu Arrisaalah. Chapa ya nane 1407 HD – 1967 AD.
- **Lisaanu Al-Arabi: Ibnu Mandhuri.**

Uhakiki: Abdallah Ali Alkabiiru – Muhammad Ahmad Hassaballah – Haashim Muhammad Asshaadhiliyu.
Daru Almaarifi – Misri,

- **Mukhtaaru Asswihaahi: Muhammad bin Abii Bakri Arraaziyu.**
  Mpangilio: Mahmud Khaatwir Bekki.
  Almatwiba`atu Al-Aamiriya Bibuulaaqi – Misri. Chapa ya Tano 1358 HD – 1939 AD.
- **Miftaahu Al-uluumi: Assakaakiyu.**
  Udhibiti na maelezo: Naimu Zurzuuru.
  Daru Alkutubi Al-ilmiyati – Beiruti. Chapa ya nane 1407 HD – 1987 AD.

⁕ ⁕ ⁕

**Nane: Fiqihi Na Misingi Ya Fiqihi:**

- **Al-Ihkaamu Fii Uswuli Al-Ahkaami: Ibnu Hazimi.**
  Maktabatu Aatwifi – Misri. Chapa ya 1398 HD – 1978 AD.
- **I`Ilaamu Almuwaqiina An Rabbil Aalamiina: Ibnu Alqayyimu.**
  Uangalizi: Twaha Abdulrauf Saad.
  Maktabatu Alkuliyyaati Al-Azhariyati. Chapa ya 1388 HD – 1968 AD.
- **Arrisaalatu: Asshaafiiyu.**
  Uhakiki: Ahmad Muhammad Shaakir.
  Daru Atturathi – Misri. Chapa ya Pili 1399 HD – 1979 AD.
- **Al-Fiqihu Al-Islaamiyu Wa-adillatuhu: Wahabatu Azzahiiliy.**
  Daru Alfikri – Suuriya. Chapa ya Tatu 1409 HD – 1979 AD.
- **Al-Mustaswifaa: Al-Ghazaaliyu.**
- Maktabatu Aljundiyu – Misri.

⁕ ⁕ ⁕

**Tisa: Vitabu vya Aina Mbalimbali:**

- **Al-itijahaatu Alwatwaniyati Fii Al-adabi Almu`aaswiri: Muhammad Hussein.**
  Muassasatu Arrisala – Beiruti. Chapa ya sita 1403 HD – 1983 AD.
- **Ihyaau Uluumi Ddiini: Abuu Haamidi Alghazaaliyu.**
  Daru Assha`abu – Misri.

- **Attabshiiru Wal-isti`imaaru Fii Albilaadi Al-Arabiyati: Mustafa Khaalidiy na Omar Farukh.**
  Almaktabatu Al-Aswiiriya – Beiruti – Swaydaa. Chapa ya tano 1973 Ad.
- **Aljama`aatu Al-islamiyati: Sulaim Al-Hilaaliyu na Ziyad Addabiiji.**
  Chapa ya pili 1401 HD – 1981 AD. Bila kutaja msambazaji.
- **Alhukuumatu Al-islamiyati: Almauduudiyu.**
  Almukhataaru Al-Islamiyu – Misri.
- **Swaunu Almantwiqi Walkalaami An Fannayi Almantwiqi Walkalaami: Assuyutwiyu.**
  Uhakiki: Ali Saamiy Annashaaru. Suad Ali Abdul razaq.
  Majmau Albuhuuthi Al-Islaamiyati – Al-Azhar.
- **Qaadatu Algharbi yaquuluuna: Dammiruu Al-Islama, Abiiduu Ahlahu: Jalaalu Al-Aalimu.**
  Almukhataaru Al-Islamiyu. 1985 AD.
- **Kawaashifu Zuyuufi Fii Almadhaahibi Alfikriyati Almu`aaswirati: Abdul Rahman Hassan Habannakat Al-Maidaaniy.**
  Daru Al-qalami – Dimashqi. Chapa ya pili 1412 HD – 1991 AD.
- **Majumuu Fataawiy Ibnu Taymiyati.**
  Kuzikusanya na kuzipanga: Abdul Rahman bin Muhammad bin Qaasim. Na mwanawe Muhammad.
- **Madaariju Assaalikiina: Ibnu Alqayyimu.**
  Daru Alhadithi – Misri. 1983 AD.
- **Naqdhwu Almantiqi: Ibnu Taimiyati.**
  Uhakiki: Muhammad Abdulrazaq Hamza – Sulaiman Bin Abdul Rahman Asswanii – Muhammad Haamid Alfaqiy.
  Maktabatu Assunnati Almuhammadiyati – Misri.

❋ ❋ ❋

| YALIYOMO | |
|---|---|
| **Mada** | **Ukurasa** |
| **UTANGULIZI** | **4** |
| **WASIFU WA PROFESA / MUHAMMAD ABDULLAH DARAAZU – ALLAH AMREHEMU.** | 10 |
| **Kazi (Vitabu vya) Daktari Muhammad Abdullah Daraazu:** | **11** |
| **KATIKA KITABU HIKI** | **13** |
| **KAZI YANGU KATIKA KUKITOA KITABU CHA (HABARI KUBWA)** | **15** |
| ***KWA JINA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU*** | **17** |
| **Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwenye Kuneemesha Neema Kubwa Kubwa Na Mwenye Kuneemesha Neema Ndogo Ndogo.** | **19** |
| **TAFITI YA KWANZA KUHUSU KUAINISHA MAANA YA QURAN. Na tofauti baina yake na hadithi Qudsiyyu na hadithi Nabawiyyu. [Maana ya kilugha na kiminyumbuliko ya maneno mawili: (Quran) na (Kitabu)]** | **21** |
| **[Siri Ya Kuitwa Majina Yote Mawili]** | **22** |
| **[Siri ya Quran kuhusika yenyewe peke yake kuwa ya milele bila ya kupotoshwa, kinyume na vitabu vilivyopita]** | 23 |
| **[Je, inawezekana kueleza fasili (maana) ya Quran kimantiki?]** | **25** |
| **[Vipengele muhimu katika fasili hii mashuhuri ya Quran]** | 26 |
| [**Kutofautisha baina ya Quran, Hadithi Nabawiyyu na Hadithi Qudusiyyu**] | **27** |
| **UTAFITI WA PILI KATIKA KUBAINISHA CHANZO CHA QURAN NA KUTHIBITISHA KUWA YENYEWE INATOKA KWA ALLAH KWA TAMKO LAKE NA MAANA YAKE.** [**Kuanisha Madai Haya Kwa Kuchukua Maandiko Ya Quran**] | **30** |
| [**Kujiepusha kwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake na kujinasibisha na Quran. Haya si madai yanayohitaji ushahidi bali yenyewe ni kukiri kunakomtia hatiani mwenye kufanya hivyo**] | **32** |
| **[Muhammad kuiegemeza Quran kwa Allah haiwezekani kuwa ni hila zake ili akunjue makucha yake. Na kama si hivyo, kwa nini hakuzinasibisha kauli zake zote kwa Allah]** | **33** |
| [**Miongoni Mwa Mifano Ya Historia Ya Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake Ndani Ya Quran**] | **39** |
| 1 – [**Kipindi cha Ufunuo katika tukio la uzushi]:** | 39 |
| **2 - Quran kupishana na tabia za Mtume. Na lawama kali za Quran laumu katika mambo ya halali]:** | **41** |
| [**Kutolea Ushahidi kwa Elimu Ya Saikolojia Juu Ya Kutengana Baina ya Uhusika Wa Ufunuo Na Uhusika Wa Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake**] | 44 |

| | |
|---|---|
| [**Msimamo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, juu ya andiko la Quran ni msimamo wa mfasiri anayetafuta maana mbalimbali na kuchukua zile chaguzi za huruma**] | 45 |
| 3- [**Wakati mwingine Mtume rehema na amani ziwe juu yake anasimama na hafahamu makusudio ya andiko hadi aletewe ubainifu wake**]: | **47** |
| [**Mfano wa kwanza: Msimamo wake katika tukio la kujitathmini kuhusu nia**] | **47** |
| [**Mfano wa pili ni: mapito yake katika suala la Hudaibiya**] | **48** |
| 4 – [**Njia Yake Katika Kupokea Andiko, Mwanzo Wake Wa pokea Ufunuo**]: | **51** |
| [**Sehemu Ya Historia Ya Jumla Ya Mtume Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake**] | 52 |
| 1 – [**Anajitakasa Na Elimu Ya Vilivyofichikana**]: | **53** |
| 2 – [**Haoneshi kinyume na vile anavyovificha**]: | **53** |
| 3 – [**Hofu Yake Juu Ya Kumzulia Uongo Allah**]: | **54** |
| 4 – [**Hajui Hadhi Yake Itakuwaje Mbele Ya Allah**]: | 54 |
| [**Kutafiti Tabia Za Nafsi Katika Historia Za Watu Wake**] | **55** |
| [**HATUA YA KWANZA YA UTAFITI**: **Kubainisha Kuwa, Haiwezekani Kwa Quran Kuwa Ni Maelezo Yanayotoka Katika Nafsi Ya Muhammad Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake]** | 57 |
| [**Maumbile Ya Maana Za Kiquran Si Miongoni Mwa Zile Zinazotambulika Kwa Uwerevu Na Ukweli Wa Ung`amuzi**:] **a- Kwa Habari Za Yaliyopita, Hakuna Njia Ya Kuzifikia Ila Kwa Kuzipokea Na Kuzidurusu**] | **58** |
| [**B – Mambo Ya Kweli Ya Kidini Yaliyofichikana Ambayo Akili Haina Njia Ya Kuyafikia**] | **62** |
| [C – **Habari Za Mambo Ya Wakati Ujao Huenda Yakang`amuliwa Na Vipimo Vya Dhana. Lakini Mambo Hayo Hayana Njia Ya Kuyayakinisha Ila Kwa Ufunuo Wa Kweli**] | **63** |
| [**Mifano Ya Utabiri Wa Quran**] | **64** |
| **Mfano wa aina ya kwanza [Mustakbali wa Uislamu, kitabu chake na Nabii wake]:** | 64 |
| **Pokea mfano wa aina ya pili [Mustakbali wa Waislamu: Chama cha Mwingi wa Rehema]:** | 70 |
| [**Mustakbali wa wenye inadi**]: | **74** |
| **Na mfano wa habari hizi za makafiri wa Kikurayshi ni zile habari zilizokuja kuhusu makafiri wa kiyahudi**. | 77 |
| [D – **Nabii bila ya ufunuo wakati mwingine huenda akakosea dhana yake licha ya uerevu na utambuzi wake**] | 84 |
| [**HATUA YA PILI YA UTAFITI HUU: Kubainisha Kuwa Muhammad Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake, Lazima Atakuwa** | 87 |

| | |
|---|---|
| **Amechukua Quran Kutoka Kwa Mwalimu. Na Kutafiti Katika Vyanzo Vya Kibinadamu Kuhusiana Na Huyo Mwalimu**] | |
| [**Kumtafuta Mwalimu Wake Baina Ya Wajinga Wasiojua Kusoma Na Kuandika: Ujinga Hauwezi Kuwa Chanzo Cha Elimu**] | **88** |
| [**Kumtafuta Mwalimu Huyo Baina Ya Wenye Elimu**] | **88** |
| **1- Sisi tunauliza: Je, kwa wasomi wa wakati huo kulikuwa na mtu anayefaa kuwa na mkono wa kielimu kwa Muhammad na Quran yake?** | **92** |
| **[Msimamo Wa Muhammad Rehema Na Amani Ziwe Juu Yake Kwa Wasomi: Ni Msimamo Wa Msahihishaji Wa Kile Walichokipotosha. Mfunua Wa Yale Waliyoyaficha]** | **93** |
| [**Atakayedai Kuwa Muhammad Ana Mwalimu Wa Kibinadamu, Na Amtaje**] | 101 |
| ***Na Ni Kipi Kitakachokujulisha Ni Nani Huyo Mtu Aliyekuwa Anamfundisha?*** | 102 |
| [**Yule Ambaye Kwake Yeye Wigo Wa Kufanya Kitu Kikweli Kweli Ni Mfinyu, Basi Mtu Huyo Hana Nafasi Isipokuwa Ombwe La Mizaha**] | **103** |
| [T**ahayari Kwa Wabishi Na Kutikisika Kwao Katika Mjadala Hapo Kale Na Sasa**] | 105 |
| [**Nadharia Ya Ufunuo Wa Nafsini Sio Mpya**] | **106** |
| [**HAATUA YA TATU YA UTAFITI**: **Utafiti Katika Mazingira Ya Ufunuo Na Yale Maalum Yaliyoambatana Nayo Katika Chanzo Cha Quran**] | **108** |
| [**Tukio La Ufunuo Na Uchambuzi Wa Matokeo Yake**] | 110 |
| • ***Kwa hiyo, hiyo ni hali isiyo ya uchaguzi*** | 112 |
| • ***Kwa hiyo, hilo ni tukio lisilo la kawaida.*** | **113** |
| • ***Sasa nguvu hii inaweza kuwa nguvu ya kitu gani kama haitokuwa nguvu ya Malaika Mkarimu?*** | 115 |
| [**Kujiliwaza Na Kile Kilichovumbuliwa Na Sayansi Ya Zama Za Sasa**] | 116 |
| [**HATUA YA NNE YA UTAFITI HUU**: **Kutafiti Kuhusu Kiini Cha Quran Yenyewe Na Uhakika Wa Chanzo Chake**] | **119** |
| [**Mipaka Ya Uwezo Wa Kibinadamu Na Mpaka Wa Kimuujiza**] | 119 |
| **[Pande Tatu Za Miujiza]** | **122** |
| **QURAN NI MUUJIZA KILUGHA [Kuzipitia Kauli Tata Zote Zinazoweza Kuonekana Kuwa Hivyo, Zile Zinazohusiana Na Suala Hili, Kwa Ajili Ya Kujiandaa Kuzifutilia Mbali Moja Moja]** | **123** |
| [**Utata Wa Kwanza: Chipukizi Mmoja Adanganyike Na Kujidai Kuwa Anaweza Kuleta Maneno Yaliyosawa Na Quran**] | **123** |

| | |
|---|---|
| **[Utata Wa Pili: Mwanafasihi Mnyenyekevu Anafahamu Vibaya Kuwa Uwezo Huu Upo Kwa Mwingine Miongoni Mwa Mafahali]** | **126** |
| **[Utata Wa Tatu: Ni Wa Warabu Kutoupinga Muundo Na Mtindo Wa Quran Huenda Hilo Lilikuwa Kwa Sababu Ya Kuondoka Kwa Hima Yao Na Sio Kwa Sababu Ya Kushindwa Kwao]** | **130** |
| **[Utata wa nne: ni kwa yule anayedhani kuwa muujiza wa Quran sio kwa upande wa kilugha kwa kuwa yenyewe haijatokapo nje ya lugha ya Kiarabu katika msamiati wake wala sarufi yake]** | 136 |
| [**Utata Wa Tano: Anayedai Kuwa Kushindwa Kwa Watu Kuendana/Kushindana Na Muundo/Mtindo Wa Quran Sio Jambo La Pekee Kwa Quran Tu. Kwa Sababu Mtindo Muundo Wa Kila Msemaji Una Taswira Ya Mwenyewe Na Hali Yake Mwenyewe Kwa Hiyo Mtu Mwingine Hatoweza Kukaa Mahala Pake**] | 141 |
| [**Utata Wa Sita: Yule Anayeukubali Muujiza Wa Quran Lakini Hatambui Ni Zipi Siri Zake Na Sababu Zake**] | 151 |
| [**MITAZAMO MIWILI KATIKA GAMBA LA JUU LA MATAMKO YA QURAN:** ]<br>**1- Uzuri Wa Mdundo Katika Mtawanyo Wa Irabu Na Konsonanti Zisizo Na Irabu, Kuvuta Sauti Na Ghuna Na Kuunganisha Na Kunyamaza**] | **152** |
| **Cha kwanza kinachokushtua:** | **152** |
| **[ 2 – Uzuri Wa Muunganiko Katika Kuziandalia Njia Herufi Zake Na Kuziunda Katika Mikusanyiko Yenye Muunganiko Mzuri Ulio Tofauti Tofauti]** | **157** |
| [**Mitazamo Juu Ya Bayani Ya Quran Na Sifa Zake Bainifu Ilizojipambanua Nazo Na Ambazo Hazipo Katika Maneno Mengine**] | **160** |
| **Quran Ikiwa Katika Vipande Vipande Miongoni Mwake** | **162** |
| **A – B: (Makusudio Katika Kupamba Matamshi) Na (Kuitendea Haki Maana):** | **163** |
| C – d: **(Kuwaongelesha Wote) Na (Kuwaongelesha Watu Maalum)**: | 168 |
| **E – F: (Kuitosheleza Akili) Na (Kuzistarehesha Hisia):** | 169 |
| **G – H: (Ubainifu) Na (Ujumla):** | **172** |
| [**Matumizi Kwa Aya Tukufu**] | **174** |
| [**Quran Yote Ni Ufupisho. Sawa Sawa Katika Sehemu Zake Za Ujumla Na Sehemu Zake Za Maelezo Ya Kina**] | **185** |
| **[Katika Quran hakuna Maneno Ya Kukurupuka, Wala Herufi Za Maana Zilizozidi]** | **189** |
| **[Siri Ya Herufi Kafu Katika Kauli Yake Mtukufu: ﴿Hakuna Chochote Mfano Wake ﴾]** | **190** |

| | |
|---|---|
| **Ufafanuzi usio na Budi Ili Kubainisha Uharibifu Wa Falsafa, Mantiki Na Elimu Ya Maneno Katika Usamehevu Wa Uislamu Na Wepesi Wake** | **194** |
| [**Ufupisho Kwa Kufuta Ukiwa Pamoja Na Uwazi Na Utamu**] | **199** |
| [**Utendaji Katika Aya Tukufu**] | **201** |
| **Quran, Sura Kwa Sura Miongoni Mwake: (Wingi) Na (Umoja):** | **206** |
| [**Ufundi Wa Bayani Katika Kuhama Kutoka Katika Maana Hadi Maana Nyingine Iliyongumu Kuliko Hiyo Katika Kuhama Baina Ya Vifungu Vya Maana Moja**] | **207** |
| [**Kuteremka Quran Ikiwa Imetawanyika Kulingana Na Matukio Na Visababishi, Licha Ya Kuwa Kwa Vipindi Mbali Mbali, Jambo Ambalo Kikawaida, Haliruhusu Kuwepo Kwa Muunganiko Na Kushikamana**] | **209** |
| [**Kukusanya Mazungumzo Yenye Maana Tofauti Tofauti, Yaliyo Katika Nyakati Mbalimbali, Yaliyo Ya Nyanja Tofauti Tofauti Na Kuyaweka Katika Mazungumzo Mamoja Yaliyoachiliwa. Kwa Hakika Hilo Ndilo Kiini Cha Kumeguka Meguka Na Kukata Maneno Bila Kuyamaliza. Na Hilo Ndilo Kiini Cha Kufarikiana Na Kutofautiana**] | **209** |
| [**Wanadamu Wameshindwa Kufikia Upeo Wa Kuainisha Maweko Ya Kila Kifungu Katika Vifungu Vya Kitu Changamani Kabla Ya Kutimia Kwa Vifungu Vyake. Bali Kabla Ya Kujua Tabia Ya Vifungu Hivyo**] | 210 |
| [**Mifano Katika Ufundi Wa Fani Mbalimbali**] | **211** |
| [**Kukusanyika Kwa Sababu Zote Hizi Katika Sura Zenye Vipande Mbalimbali Bila Ya Kutia Dosari Hukumu Za Umoja Wake, Wala Msimamo Wa Mizani Yake. Kwa Hakika Hili Ni Muujiza Wa Miujiza**] | **216** |
| **MFUMO WA KUFUNGA MAANA KATIKA SURATUL BAQARAH** | 231 |
| **Utangulizi** [**Unazungumzia Kulitambulisha Jambo La Hii Quran Na Kubainisha Uwazi Wa Mwongozo Wake.** | 232 |
| **KUSUDIO LA KWANZA MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII** [**Kuwaita Watu Wote Waingie Katika Uislamu**] **Katika Aya Tano [21 – 25]** | 244 |
| **MAKUSUDIO YA PILI MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII** [**Kuwaita Watu Wa Kitabu Wito Mahususi, Wa Kuacha Batili Zao Na Kuingia Dini Hii Ya Haki**] **Katika aya mia ishirini na tatu [40 – 162]** | 248 |
| 1- **Kutaja Kizazi Cha Kale Cha Wayahudi** [49 – 74]: | **249** |
| **Kiungo Cha Muunganiko Baina Ya Vile Vigawo Viwili Cha Kwanza Na Cha Pili** [74]: | **250** |

| | |
|---|---|
| 2 – **Kutajwa Wayahudi Wa Zama Za Utume** [75 – 121]: | **251** |
| 3- **Kutajwa Kwa Waislamu Wa Kale, Kuanzia Kwa Ibrahimu [122 – 134]:** | 254 |
| 4- **Kutajwa Kwa Mambo Ya Waislamu Wa Zama Za Kupewa Utume [135 – 162]:** | 257 |
| **Lango La Kusudio La Tatu: Aya Kumi Na Tano** [163 – 177] | **261** |
| **(Hatua Ya Kwanza) Kuthibitisha Upweke Wa Muumba Anayeabudiwa**. | **261** |
| **(Hatua Ya Pili) Kuthibitisha Upweke Wa Mtoa Amri Mwenye Kutiiwa**. | 263 |
| **(Hatua Ya Mwisho) Majumuisho Ya Sharia Za Kidini** | **271** |
| **KUSUDIO LA TATU MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII [Kuwasilisha Sharia Za Dini Hii Kwa Maelezo Ya Kina]**<br>Kwa aya mia moja na sita [178 – 283] | 273 |
| **Subira Wakati Wa Matatizo Na Vita** | 275 |
| **Subira Katika Madhara** | **275** |
| **Subira Katika Shida Ya Vita** | **276** |
| **Mapumziko** [204 – 214] | **277** |
| **KUSUDIO LA NNE MIONGONI MWA MAKUSUDIO YA SURA HII** [**Kutaja Msukumo Na Hisia Ya Kidini Inayochochea Kushikamana Na Sharia Hizo Na Kuzuia Kwenda Kinyume** Nazo].<br>**Katika aya moja [284]** | 292 |
| **HITIMISHO** [**Katika Kutambulisha Wale Ambao Walioitikia Wito Huu Jumuishi Wa Makusudio Hayo. Na Kubainisha Yale Yanayotarajiwa Kwao Kwa Ya Baadaye Na Ya Sasa]**<br>**Katika Aya Mbili** [285 – 286] | 294 |
| **VYANZO NA REJEA** | 297 |
| **YALIYOMO** | 306 |